المستكشف ابو منال دانا
AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

تفسير سورة الكهف

تجميع وانتاج
المستكشف أبومنال دانا

TAFSIR YA SURAT AL KAHF

KIMETAYARISHWA NA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH
KIMECHAPISHWA NEW DELHI, INDIA.
MWAKA *1445 AL HIJRA – 2023 C.E*

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

§——————————§§——————————§

إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ ونَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضْلِلْ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Inna Al-hamda Lillaahi nahmaduhu wanasta'eenahu wa nastaghfiruhu, wa na'oodhu billaahi min shuroori anfusinaa wa min sayi'aati a'maalinaa. Man yahdih - Illaahu falaa mudhilla laahu wa man yudhlil falaa haadiya lahu. Wa ashhadu an laa ilaaha ill-Allaahu wahdahu laa shareekallahu, wa ashhadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasooluhu.

Tafsir: ***Kwa jina la Allah, ambae kwa hakika ndie anastahiki shukrani zote, tunaemuomba msaada na msamaha wake. Tunajilinda kwa ulinzi wa Allah na kila maovu ya Nafsi zetu na mambo mabaya yetu. Kwani kwa hakika mtu yeyote yule alieongozwa na Allah basi hakuna atakaempotoa, na aliepotoshwa na Allah basi hakuna atakaemuongoa. Nnashuhudia kua hakuna anaepaswa kuabudiwa isipokua Allah pekee asiekua na mshirika, na nnashuhudia kua Muhammad (Salallahu A'layhi wa Salam) ni Mja wake na ni Mtume wake.***

يَقُولُ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ

﴿يأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha haqqa tuqatihi wala tamootunna illa waantum muslimoona *(Surat Al Imran 3:102)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Muogopeni Allah (kwa kutekeleza maamrisho yake na kuachana na makatazo yake) kama anavyotahiki kuogopewa. (Mtiini, mshukuruni na daima mkumbukeni), na msife isipokua mkiwa katika hali ya kua ni Waislam.***

﴿يَأَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُواْ رَبَّكُمُ الَّذِى خَلَقَكُمْ مِنْ نَّفْسٍ وَحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالاً كَثِيراً وَنِسَآءً وَاتَّقُواْ اللَّهَ الَّذِى تَسَآءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيباً﴾

Ya ayyuha alnnasu ittaqoo rabbakumu alladhi khalaqakum min Nafsin wahidatin wakhalaqa minha zawjaha wabaththa minhuma rijalan kathiran wanisaan waittaqoo Allaha alladhii tasaaloona bihi waal-arhama inna Allaha kana AAalaykum raqeeban *(Surat An Nisaa 4:1)*

Tafsiri: ***Enyi Watu! Mcheni Mola wenu aliekuumbeni kutokana na Nafsi moja (Adam), na kutokana nae (Adam) akamuumba mke wake (Hawa), na kutokana nao (Adam na Hawa) akawaumba Wanaume na Wanawake wengi na muogopeni Allah ambae ana haki juu yenu, na msivunje udugu, kwani kwa Hakika Allah ni mwenye uangalifu mkubwa juu yenu.***

﴿يأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ وَقُولُواْ قَوْلاً سَدِيداً ۞ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَلَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزاً عَظِيماً﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha waqooloo qawlan sadeedan, Yuslih lakum aAAmalakum wayaghfir lakum dhunoobakum waman yutiAAi Allaha warasoolahu faqad faza fawzan AAadhiman *(Al Ahzab 33:70-71)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini! mcheni na muogopeni Allah, na (daima) semeni kauli za ukweli ulionyooka, atakuongozeni kufanya mema na kukusameheni dhambi zenu. Na kwa hakika yeyote yule ambae anaemtii Allah na Mtume wake (Salallahu A'layhi wa Salam) basi atakua ni miongoni mwa waliofuzu.***

Allahuma Ij'Aalna minna al faizin fawzan A'adhimah…Aamin

قَالَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللهُ:فَإِنَّ أَصْدَقَ الْحَدِيثِ كِتَابُ اللَّهِ، وَأَوْثَقَ الْعُرْيِ كَلِمَةُ التَّقْوَى، وَخَيْرَ الْمِلَلِ مِلَّةُ إِبْرَاهِيمَ، وَخَيْرَ السُّنَنِ سُنَنُ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَأَشْرَفَ الْحَدِيثِ ذِكْرُ اللَّهِ تَعَالَى، وَأَحْسَنَ الْقَصَصِ هَذَا الْقُرْآنُ

Qala Rasul Allahi Salallahu A'alayhi wa Salam: fa'inn 'asdaqa alhadith kitab allahi, wa'awthaq al'aAuryi kalimat alttaqwaa, wakhayr almilal millat 'Ibrahima, wakhayr alssunan sunan Muhammad Sala Allahu Alyhi wa Salam, wa'ashraf alhadith dhikr allah taalaa, wa'ahsan alqasas hadha al Quran.

Amesema Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam kua: **Kwa hakika hadith za kweli kabisa ni za Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na kauli zenye uzito ni kauli zenye Taqwa, na Mila bora ni *Milat Ibrahima,* Na Sunna bora ni Sunna za Muhammad (*Sala Allahu Alayhi wa Salam) na Maneno Matukufu ni Dhikr Allah Ta'ala na* Visa bora ni hii *Qur'an.***

وَيَقُولُ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ

﴿وَبِٱلْحَقِّ أَنْزَلْنَاهُ وَبِٱلْحَقِّ نَزَلَ وَمَآ أَرْسَلْنَاكَ إِلاَّ مُبَشِّراً وَنَذِيراً۞وَقُرْآناً فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى ٱلنَّاسِ عَلَىٰ مُكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنْزِيلاً۞قُلْ آمِنُواْ بِهِ أَوْ لاَ تُؤْمِنُوۤاْ إِنَّ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْعِلْمَ مِن قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلأَذْقَانِ سُجَّداً۞وَيَقُولُونَ سُبْحَانَ رَبِّنَآ إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولاً۞وَيَخِرُّونَ لِلأَذْقَانِ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعاً۞قُلِ ٱدْعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدْعُواْ ٱلرَّحْمَٰنَ أَيّاً مَّا تَدْعُواْ فَلَهُ ٱلأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ وَلاَ

تَجْهَرْ بِصَلاَتِكَ وَلاَ تُخَافِتْ بِهَا وَٱبْتَغِ بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيلاً۞وَقُلِ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى لَمْ يَتَّخِذْ وَلَداً وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ شَرِيكٌ فِى ٱلْمُلْكِ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ وَلِيٌّ مِّنَ ٱلذُّلِّ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيراً۞

Wabialhaqqi anzalnahu wabialhaqqi nazala wama arsalnaka illa mubashshiran wanadheeran, Waqur-anan faraqnahu litaqraahu AAala alnnasi AAala mukthin wanazzalnahu tanzeelan, Qul aminoo bihi aw la tu/minoo inna alladheena ootoo alAAilma min qablihi idha yutla AAalayhim yakhirroona lil-adhqani sujjadan; Wayaqooloona subhana rabbina in kana waAAdu rabbina lamafAAoolan; Wayakhirroona lil-athqani yabkoona wayazeeduhum khushooAAan; Quli odAAoo Allaha awi odAAoo alrrahmana ayyan ma tadAAoo falahu al-asmao alhusna wala tajhar bisalatika wala tukhafit biha waibtaghi bayna dhalika sabeelan, Waquli alhamdu lillahi alladhee lam yattakhidh waladan walam yakun lahu shareekun fee almulki walam yakun lahu waliyyun mina aldhdhulli wakabbirhu takbeeran *(Surat Al Isra 17:105-111)*

Tafsir: ***Na kwa haki tumeiteremsha chini (Hii Qur'an) na kwa haki imeshuka, na tumekutuma wewe (Muhammad) si kwa chochote isipokua kwa ajili ya kuweka wazi na kuonya. Na hii Qur'an ambayo tumeigawa (katika aya na sura tofauti) ili upate kuisoma kwa watu kwa makusudio. Na tumeishusha hii (Qur'an) kwa vituo (tofauti). Sema (Ewe Muhammad): 'Iaminini au msiiamaini. Kwani kwa hakika wale waliopewa Ilm kabla yake (Ilm ya Ahl Al Kitab kina Abd Allah Ibn Salam Radhi Allahu Anhu, Salman Al Farsi Radhi Allahu Anhu n.k)' waliposomewa, walianguka chini kwa nyuso zao kwa Unyenyekevu wa Kusjudu. Na wakasema: 'Utukufu ni Wa Allah Pekee. Ahadi ya Mola wetu ni lazime iwe ni yenye kutekelezwa'. Na wakaanguka kwa nyuso zao wakilia machozi na hii ilizidisha Unyenyekevu wao. Sema (Ewe Muhammad) Muombeni Allah, au muombeni Ar Rahmani, au kwa jina lolote (Katika Majina yake Matukufu), kwani kwake yeye ndio kwenye umiliki wa Majina Matukufu, na Salini bila ya kufanya kelele au kwa sauti ya chini, bali fuateni njia ya baina yake (hali hizo mbili). Na semeni shukrani zote anastahiki Allah ambae hana mtoto, na wala hana mshirika katika Ufalme wake, na ni asiekua (na uhitaji wa) Msaidizi wala Mlinzi. Na Mkuzeni kwa Takbir***

ALLAHU AKBAR!

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

YALIYOMO

VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH: *7*
MPANGILIO WA KUSHUSHWA KWA SURA ZA QUR'AN *8*
TAFSIR YA SURAT AL KAHF. *12*
AS-HAB AL KAHF *12*
AS-HAB AL KAHF WA KWANZA AMBAO NI WATU WATATU WENYE TAQWA *40*
FITYATUN - AS-HAB ALKAHF – VIJANA SHUPAVU WENYE TAQWA WA PANGONI *43*
FITYATUN - AS-HAB ALKAHF NI MITHILI YA UZAYR IBN SURAYAH. *92*
VIJANA WAWILI NA MASHAMBA MAWILI. *125*
KISA CHA AL KHIDR NA NABII MUSA ALAYHI SALAAM *167*
QISA AL MUSTAQILLA - NABII MUSA NA AL KHIDHR *186*
AL KHDHR NI NANI *212*
KISA CHA DHU AL QARNAYN *222*
AL MASIH AL DAJJAL *249*
YAJUJ WA MAJUJ *261*
KUFR - MAANA YAKE, AINA ZAKE NA HUKMU YAKE *278*
UTHIBITISHO WA UTUME WA RASUL ALLAH SALALLAHU ALAYHI WA SALAM *295*
SIKU YA KIAMA NA MIONGONI MWA DALILI KUU ZAKE. *315*
MARUDIO YA VITABU VILIVYOTUMIKA KATIKA KITABU HIKI: *375*
MARUDIO YA MITANDAO ILIVYOTUMIKA KATIKA KITABU HIKI *375*

VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH:

1-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA KWANZA - MWAKA - *1435 AL HIJRA* (2014).

2-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA PILI - MWAKA - *1437 AL HIJRA* (2016).

3-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAMU NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA TATU - MWAKA *1439 AL HIJRA* (2018).

4-TAFSIR SURAT YUSUF – AHSAN AL QASAS - MWAKA *1441 AL HIJRA* (2020).

5-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL AWWAL – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA KWANZA – MWAKA 1442 AL HIJRA (2021).

6-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL THANI – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA PILI – MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

7-TABAQAT WARATHAT AL ANBIYAI - AL JUZUU Al AWWAL - MATABAKA YA WARITHI WA MITUME-JUZUU YA KWANZA - MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

8- KANZ AL FAWAID WA AL MUJARRABAT FII QADHAI AL HAWAIJ (HAZINA YA FAIDA NA MUJARABATI KATIKA KUFANIKISHA MAMBO MBALI MBALI)- MWAKA 1445 AL HIJRA (2023).

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

MPANGILIO WA KUSHUSHWA KWA SURA ZA QUR'AN

Mpangilio wa Ushushwaji	Surah Nambari	Jina La Sura	Jina La Kiarabu	Idadi Ya Aya	Imeshushwa
1	96	Alaq	سُورَةُ العَلَقِ	19	Makkah
2	68	Qalam	سُورَةُ القَلَمِ	52	Makkah: Isipokua Aya ya 17-33 na 48-50 Zimeshushwa Madina
3	73	Muzammil	سُورَةُ المُزَّمِّلِ	20	Makkah: Isipokua Aya ya 10, 11 na 20 Zimeshushwa Madina
4	74	Mudathir	سُورَةُ المُدَّثِّرِ	56	Makkah
5	1	Fatehah	سُورَةُ الفَاتِحَةِ	7	Makkah
6	111	Lahab	سُورَةُ المَسَدِ	5	Makkah
7	81	Takwir	سُورَةُ التَّكْوِيرِ	29	Makkah
8	87	A'la	سُورَةُ الأَعْلَى	19	Makkah
9	92	Leyl	سُورَةُ اللَّيْلِ	21	Makkah
10	89	Fajr	سُورَةُ الفَجْرِ	30	Makkah
11	93	Duha	سُورَةُ الضُّحَى	11	Makkah
12	94	Inshira	سُورَةُ الشَّرْحِ	8	Makkah
13	103	Asr	سُورَةُ العَصْرِ	3	Makkah
14	100	Aadiyat	سُورَةُ العَادِيَاتِ	11	Makkah
15	108	Kauthar	سُورَةُ الكَوْثَرِ	3	Makkah
16	102	Takatur	سُورَةُ التَّكَاثُرِ	8	Makkah
17	107	Alma'un	سُورَةُ المَاعُونِ	7	Maakkah: Aya ya 1-3 Zimeshushwa Makkah zilobakia Madinah
18	109	Kafirun	سُورَةُ الكَافِرُونَ	6	Makkah
19	105	Fil	سُورَةُ الفِيلِ	5	Makkah
20	113	Falaq	سُورَةُ الفَلَقِ	5	Makkah
21	114	Nas	سُورَةُ النَّاسِ	6	Makkah
22	112	Iklas	سُورَةُ الإِخْلَاصِ	4	Makkah
23	53	Najm	سُورَةُ النَّجْمِ	62	Makkah: Isipokua Aya ya 32 imeshushwa Madina
24	80	Abasa	سُورَةُ عَبَسَ	42	Makkah
25	97	Qadr	سُورَةُ القَدْرِ	5	Makkah
26	91	Shams	سُورَةُ الشَّمْسِ	15	Makkah
27	85	Buruj	سُورَةُ البُرُوجِ	22	Makkah
28	95	T'in	سُورَةُ البُرُوجِ	8	Makkah
29	106	Qureysh	سُورَةُ قُرَيْشٍ	4	Makkah
30	101	Qariah	سُورَةُ القَارِعَةِ	11	Makkah
31	75	Qiyamah	سُورَةُ القِيَامَةِ	40	Makkah
32	104	Humazah	سُورَةُ الهُمَزَةِ	9	Makkah
33	77	Mursalat	سُورَةُ المُرْسَلَاتِ	50	Makkah: Isipokua Aya ya 48 Imeshushwa Madina

34	50	Q'af	سُورَةُ قٓ	45	Makkah: Isipokua Aya ya 38 imeshushwa Madina
35	90	Balad	سُورَةُ الْبَلَدِ	20	Makkah
36	86	Tariq	سُورَةُ الطَّارِقِ	17	Makkah
37	54	Qamar	سُورَةُ الْقَمَرِ	55	Makkah: Isipokua Aya ya 44-46 Zimeshushwa Madina
38	38	Sad	سُورَةُ صٓ	88	Makkah
39	7	A'araf	سُورَةُ الْأَعْرَافِ	206	Makkah: Isipokua Aya ya 163-170 Zimeshushwa Madina
40	72	Jinn	سُورَةُ الْجِنِّ	28	Makkah
41	36	Ya'sin	سُورَةُ يٰسٓ	83	Makkah: Isipokua Aya ya 45 imeshushwa Madina
42	25	Furqan	سُورَةُ الْفُرْقَانِ	77	Makkah: Isipokua Aya ya 68-70 Zimeshushwa Madina
43	35	Fatir	سُورَةُ فَاطِرٍ	45	Makkah
44	19	Maryam	سُورَةُ مَرْيَمَ	98	Makkah: Isipokua Aya ya 58 na 71 Zimeshushwa Madina
45	20	Ta Ha	سُورَةُ طٰهٰ	135	Makkah: Isipokua Aya ya 130-131 Zimeshushwa Madina
46	56	Waqiah	سُورَةُ الْوَاقِعَةِ	96	Makkah: Isipokua Aya ya 81-82 Zimeshushwa Madina
47	26	Shuara	سُورَةُ الشُّعَرَاءِ	227	Makkah: Isipokua Aya ya 197 na 224-227 Zimeshushwa Madina
48	27	Naml	سُورَةُ النَّمْلِ	93	Makkah
49	28	Qasas	سُورَةُ الْقَصَصِ	88	Makkah: Isipokua Aya ya 52-55 Zimeshushwa Madina na 85 Juhfa.
50	17	Bani Israil, Al Isra	سُورَةُ الْإِسْرَاءِ	111	Makkah: Isipokua Aya ya 26,32,33,57,73 na 80 Zimeshushwa Madina
51	10	Yunus	سُورَةُ يُونُسَ	109	Makkah: Isipokua Aya ya 40, 94,95, na 96 Zimeshushwa Madina
52	11	Hud	سُورَةُ هُودٍ	123	Makkah: Isipokua Aya ya 12,17 na 114 Zimeshushwa Madina
53	12	Yusuf	سُورَةُ يُوسُفَ	111	Makkah: Isipokua Aya ya 1,2,3 na 7 Zimeshushwa Madina
54	15	Hijr	سُورَةُ الْحِجْرِ	99	Makkah: Isipokua Aya ya 87 imeshushwa Madina
55	6	AnAam	سُورَةُ الْأَنْعَامِ	165	Makkah: Isipokua Aya ya 20,23,91,93,114,151,152 Na 153 Zimeshushwa Madina
56	37	Saffat	سُورَةُ الصَّافَّاتِ	182	Makkah
57	31	Luqman	سُورَةُ لُقْمَانَ	34	Makkah: Isipokua Aya ya 27-29 Zimeshushwa Madina
58	34	Saba	سُورَةُ سَبَإٍ	54	Makkah
59	39	Zumar	سُورَةُ الزُّمَرِ	75	Makkah

60	40	Ghafir	سُورَةُ غَافِرٍ	85	Makkah: Isipokua Aya ya 56-57 Zimeshushwa Madina
61	41	Hamim Sajdah	سُورَةُ فُصِّلَتْ	54	Makkah
62	42	Shura	سُورَةُ الشُّورَىٰ	53	Makkah: Isipokua Aya ya 23,24,25 na 27 Zimeshushwa Madina
63	43	Zukhruf	سُورَةُ الزُّخْرُفِ	89	Makkah: Isipokua Aya ya 54 imeshushwa Madina
64	44	Dukhan	سُورَةُ الدُّخَانِ	59	Makkah
65	45	Jathiyah	سُورَةُ الْجَاثِيَةِ	37	Makkah
66	46	Ahqaf	سُورَةُ الْأَحْقَافِ	35	Makkah: Isipokua Aya ya 10,15 na 35 Zimeshushwa Madina
67	51	Dhariyat	سُورَةُ الذَّارِيَاتِ	60	Makkah
68	88	Ghashiya	سُورَةُ الْغَاشِيَةِ	26	Madina
69	18	Kahf	سُورَةُ الْكَهْفِ	110	Makkah: Isipokua Aya ya 28, 81-101 Zimeshushwa Madina
70	16	Nahl	سُورَةُ النَّحْلِ	128	Makkah: Isipokua Aya ya 126,127,128 Zimeshushwa Madina
71	71	Nuh	سُورَةُ نُوحٍ	28	Makkah
72	14	Ibrahim	سُورَةُ إِبْرَاهِيمَ	52	Makkah: Isipokua Aya ya 28-29 Zimeshushwa Madina
73	21	Anbiya	سُورَةُ الْأَنْبِيَاءِ	112	Makkah
74	23	Muminun	سُورَةُ الْمُؤْمِنُونَ	118	Makkah
75	32	Sajdah	سُورَةُ السَّجْدَةِ	30	Makkah: Isipokua Aya ya 16-20 Zimeshushwa Madina
76	52	Tur	سُورَةُ الطُّورِ	49	Makkah
77	67	Mulk	سُورَةُ الْمُلْكِ	30	Makkah
78	69	Haqqah	سُورَةُ الْحَاقَّةِ	52	Makkah
79	70	Maarij	سُورَةُ الْمَعَارِجِ	44	Makkah
80	78	Naba	سُورَةُ النَّبَإِ	40	Makkah
81	79	Naziat	سُورَةُ النَّازِعَاتِ	46	Makkah
82	82	Infitar	سُورَةُ الْانفِطَارِ	19	Makkah
83	84	Inshiqaq	سُورَةُ الْانشِقَاقِ	25	Makkah
84	30	Rum	سُورَةُ الرُّومِ	60	Makkah: Isipokua Aya ya 17 Imeshushwa Madina
85	29	Ankabut	سُورَةُ الْعَنكَبُوتِ	85	Makkah: Isipokua Aya ya 1-11 Zimeshushwa Madina
86	83	Tatfif	سُورَةُ الْمُطَفِّفِينَ	36	Makkah
87	2	Baqarah	سُورَةُ الْبَقَرَةِ	286	Makkah: Isipokua Aya ya 281 imeshushwa Mina
88	8	Anfal	سُورَةُ الْأَنفَالِ	75	Madina: Isipokua Aya ya 30-36 Zimeshushwa Makkah
89	3	Aal-e-Imran	سُورَةُ آلِ عِمْرَانَ	200	Madina

90	33	Ahzab	سُورَةُ الْأَحْزَابِ	73	Madina
91	60	Mumtahana	سُورَةُ الْمُمْتَحَنَةِ	13	Madina
92	4	Nisa	سُورَةُ النِّسَاءِ	176	Madina
93	99	Zilzal	سُورَةُ الزَّلْزَلَةِ	8	Makkah
94	57	Hadid	سُورَةُ الْحَدِيدِ	29	Madina
95	47	Muhammad	سُورَةُ مُحَمَّدٍ	38	Madina
96	13	Ra'd	سُورَةُ الرَّعْدِ	43	Madina
97	55	Rahman	سُورَةُ الرَّحْمَٰنِ	78	Makkah
98	76	Dahr	سُورَةُ الْإِنْسَانِ	31	Madina
99	65	Talaq	سُورَةُ الطَّلَاقِ	12	Madina
100	98	Beyinnah	سُورَةُ الْبَيِّنَةِ	8	Madina
101	59	Hashr	سُورَةُ الْحَشْرِ	24	Madina
102	24	Nur	سُورَةُ النُّورِ	64	Madina
103	22	Hajj	سُورَةُ الْحَجِّ	78	Madina: Isipokua Aya ya 52-55 Zimeshushwa baina ya Makkah na Madina
104	63	Munafiqun	سُورَةُ الْمُنَافِقُونَ	11	Madina
105	58	Mujadila	سُورَةُ الْمُجَادِلَةِ	22	Madina
106	49	Hujurat	سُورَةُ الْحُجُرَاتِ	18	Madina
107	66	Tahrim	سُورَةُ التَّحْرِيمِ	12	Madina
108	64	Taghabun	سُورَةُ التَّغَابُنِ	18	Madina
109	61	Saff	سُورَةُ الصَّفِّ	14	Madina
110	62	Jumah	سُورَةُ الْجُمُعَةِ	11	Madina
111	48	Fat-h	سُورَةُ الْفَتْحِ	29	Madina Wakati wa kurudi kwenye Makubaliano ya Hudaybiyah
112	5	Maidah	سُورَةُ الْمَائِدَةِ	120	Madina: Isipokua Aya ya 3 imeshushwa Arafah kwenye Hija ya Kuaga
113	9	Taubah	سُورَةُ التَّوْبَةِ	129	Madina: Isipokua Aya ya 128-129 Zimeshushwa Makkah
114	110	Nasr	سُورَةُ النَّصْرِ	3	Madina: Imeshushwa Mina Ila Inahesabiwa kua ni ya Madina.

TAFSIR YA SURAT AL KAHF.

AS-HAB AL KAHF

Neno *Kahafa* kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye Kumaanisha Kufunika Sehemu Yenye Kua ni Hifadhi ya Kitu, Kuziba Shimo kubwa au Pango kubwa ambalo Linahifadhi kitu ndani yake, Kuingia Ndani ya Shimo kubwa au Pango kubwa au Hifadhi iliyomo ndani ya Kitu Fulani, Kuingia Ndani ya Shimo au Jiwe au Chini Ardhini.

Naam..neno *Kahafa* ndio lililotoa neno *Kahf* ambalo humaanisha Sehemu ya Kujifichia, Sehemu ya Kujihifadhia, Kujilinda kutokana na Hatari, Matatizo au Mashakil, Kuingia Mafichoni na pia neno *Kahf* hua Linamaanisha Pango.

Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atunufaishe na Manufaa yaliyomo ndani ya Qur'an iwe ni Nuru ya Nyoyo zetu na Muongozo wetu na Dhikr yetu na atujaalie Mwisho mema na awe ni mwenye kuridhika nasi na kutuingiza katika Rehma zake..Amiin ya Allah.

Kwani Sura hii imeitwa *Surat Al Kahf* au Sura ya Pango Kubwa kutokana na kua ndani yake inazungumzia visa Vitatu ambapo cha mwanzo miongoni mwao ni cha *As-hab Al Kahf yaani* Watu wa Pangoni, Kisa cha *Al Khidr* na kisa cha *Dhu Al Qaranayn* ni Sura ya 18 kimpangilio ndani ya Qur'an na ina aya 110 na ni Sura ya 69 Kushushwa.

Hivyo *Surat Al Kahf* ni miongoni mwa Sura za mwanzoni kushushwa katika wakati wa kipindi cha tatu cha Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akiishi katika mji wa Makkah. Ambapo katika wakati huu akiwa katika Mji wa Makkah basi Utume wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ulikua katika hali 4 zifuatazo:

1-Kudhihirishiwa Utume wake kwa kushushiwa kwake Mara ya kwanza Aya 5 za mwanzo za Surat Al Aalaq na kisha kuamrishwa kuutangazia Uislam Kimya kimya kwa baadhi ya watu maalum tu ndani ya Mji wa Makkah bila ya wengine kujua jambo ambalo lilichukua miaka mitatu.

2-Kipindi ambacho kilifuatua baada ya kuamrishwa kuutangazia Uislam kwa siri siri ambacho hiki kilikua ni ndani ya miaka miwili iliyofuata baada ya miaka mitatu ya hatua ya mwanzo ya Utume.

Ambapo ndani ya miaka miwili hii ya hatua ya pili ilikua tayari kuna upinzani kutoka kwa mtu mmoja mmoja pia na kisha zikafuata shutuma na mbinu za chini kwa chini kuupiga vita Uislam ikiwemo kuwawekea vikwazo Waislam wasiokua na kitu yaani masikini, watumwa, n.k.

3-Hiki ni kipindi kilichofuatia baada ya Kuingia mwaka wa 6 tangu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kupewa Utume, ambapo kipindi hiki kilidumu kwa mda wa miaka 6, na kilianzia baada ya kufariki Abu Talib na *Ummu ul Muuminin Khadijah Al Kubra Radhi Allahu Anha.*

Hiki ndio kipindi iliposhushwa Surat Al Kahf kwani ndio kipindi ambacho Waislam walianza Kubaguliwa, Kunyanyaswa, Kupigwa vita wazi wazi kiasi ya kua baadhi ikabidi waukimbie Mji wa Makkah Na kufanya Hijra ya Kuelekea katika Ardhi ya Uhabeshi.

4-Kipindi cha hali ya 4 ilikua ni kipindi ambacho kilidumu kwa mda wa miaka mitatu yaani kuanzia Mwaka wa 10 wa Utume hadi Mwaka wa 13 pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoamrishwa kufanya Hijra ya kuelekea katika Mji wa Madina.

Ambapo ndani ya kipindi hiki ndio *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* alihisi kua Watu wake wataangamia wote hivyo bora ahame yeye pamoja nao kwa kwanza kujaribu kuzungumza na Watu wa Mji wa Taif, huku watu wa Mji wa Makkah wakiwa wanajipanga kutafuta Njia ya Kuung'oa mzizi wa Tatizo lao linalowatia wazimu la kuanzishwa kwa Dini Mpya ya Kiislam, na hivyo kuamua kua Ufumbuzi ni Kumuua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo ndani ya Kipindi hiki ndio *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamfungulia Milango ya Nyoyo za Ansar wa Mji wa Madina na kukaribishwa kwenye Mji wa Madina

Hivyo *Surat Al Kahf* ambayo ni Sura iliyoshushwa ndani ya kipindi cha tatu cha wakati wa Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo amesema Imam Al Bukhari kua: **'Kuna mtu (aitwae Usayd Ibn Hudayr *Radhi Allahu Allahu Anhu) siku* moja alikua amekaa akisoma *Surat Al Kahf* huku katika pembeni yake kukiwa kuna Farasi ambae alikua amefungwa kamba na mara Kikatokea kiwingu na kuanza kumfunika, Hivyo Kutokana na tukio hilo basi Farasi akaanza Kulia kwa kelele, na hivyo Usayd Ibn Hudayr *Radhi Allahu Allahu Anhu* akasita kusoma Sura hio.**

Na Siku ya pili mtu (Usayd Ibn Hudayr *Radhi Allahu Allahu Anhu)* akaelekea kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumwambia kuhusiana na tukio hilo. Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia kua Hicho kilikua kiwingu kinachotokana na Utulivu unaopatikana pale inaposomwa Qur'an'

Na amesema Imam Muslim kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaehifadhi Aya 10 za Mwanzo za *Surat Al Kahf* basi atakua ni mwenye kuokolewa na mtihani dhidi ya Dajjal'***(Imam Muslim)*

Ambapo kwa upande wa Imam At Tirmidhii basi yeye pia amesema kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua yeyote yule atakaehifadhi aya 3 za mwanzo za *Surat Al Kahf* basi atakua ni mwenye kuokolewa na Dajjal'**

Na Imam Al Hakim Al Tirimidhi kua Amesema *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Yeyote yule atakaeisoma *Surat Al Kahf* basi atajaaliwa kua na Nur ambayo itamurika kutoka katika sehemu aliyopo hadi katika Mji wa Makkah, na atakaehifadhi aya 10 za Mwisho za Surat Al Kahf basi hatozidiwa na Dajjal hata kama atamtokea mbele yake'**. Ambapo hii ni Hadith ambayo *Al Faqih Al Muhaqqiq* Imam Ibn Hajar Al Haytami amesema kua ni Sahih.

Na akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: '**Yeyote yule atakaesoma *Surat Al Kahf* katika Usiku wa Kuamkia Siku ya Ijumaa basi atakua ni mwenye Nuru ambayo itamng'arisha kuanzia Ijumaa hio hadi Ijuma ijayo'** *(Imam At Tirmidhi)*

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Yeyote yule atakaesoma Surat Al Kahf Katika Siku ya Ijumaa, basi katika siku ya Malipo itakua kuna Nuru kwa ajili yake na kutakua kuna Nuru yake kutoka Ardhini hadi Mbinguni na Dhambi zake baina ya Ijumaa hio hadi inayofuatia zitakua ni zenye kusamehewa'**

Kwani katika Sunan Abu Daud kuna Hadith pia isemayo kua: **‘Yeyote yule atakaehifadhi Aya za Mwanzoni za *Surat Al Kahf* basi atakua huru dhidi ya Mitihani ya Dajjal kwani Kama (Dajjal) akija wakati mimi nikiwa Pamoja nanyi basi Mimi nitaingilia kati kwa ajili yenu. Lakini kama akija wakati mimi nikiwa siko pamoja nanyi basi kila mtu atapapatua kwa Nafsi yake, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atachukua nafasi yangu katika kumsaidia kila Muislam, Hivyo wale mtakao kuwepo miongoni mwenu katika wakati huo basi na wasome ufunguzi wa *Surat Al Kahf* kwani ndio Ulinzi dhidi yake.’**

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

Bismi Allahi AlRahmani AlRahiim.

Tafsir: ***Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwingi wa Huruma.***

Hii ni aya ya mwanzo ya Qur’an na pia ni Utangulizi na Ufunguzi wa kila kitu kinachofanywa na kila Mtu aliemuamini *Allah Subhanah wa Ta’ala.* Anasema *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Mushakikin Shaykh ul Islami* Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na ayah hii kua: ‘***Harfu Ba* iliyopo mwanzoni mwa ayah hii hua inamaanisha *Ilsaq* (kiunganishi) ‘Kwa’ ambacho kinaunganisha uanzaji wa kitendo na jina la *Allah Subhanah wa Ta’ala.’***

Neno *Allah* kwa lugha ya Kiarabu hua ni lenye kumaanisha Jina Tukufu ambalo ni la Muumba wa Kila kitu, kilichomo kwenye Ulimwengu unaoonekana na usioonekana, ambae ni Mmiliki wa kila kitu Mbinguni na Ardhini, ambae ndie mmiliki wa Sifa nzuri zote na Majina Matukufu yote. Hivyo Majina yote Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* na sifa zake Tukufu ambazo kwa ufahamu wa Ibn Adam hua haziwezi kufafanulika kikamilifu na ipasavyo kama inavyobidi kuelezewa zilizotajwa ndani ya Qur’an ni yenye kuweka wazi maana ya jina la *Allah Subhanah wa Ta’ala* kulingana na Ufahamu wa Ibn Adam.

Anasema *Hujjat ul Islami Mujaddid Ad Din, Zuhruf Ad Din Imam Al Shafii Al Thani* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: **'Allah ni Jina la yule ambae yupo hai, ambae ni mwenye sifa za kua ni Muumba na Mlezi juu ya kila kitu alichokiumba. Yeye ni mwenye upekee pale tunapozungumzia usahihi wa kuwepo kwake, na bila ya shaka hakuna kitu chengine chochote kile kilichokuwepo ambacho kinaweza kupewa kupewa sifa stahiki ya kuwepo kwake kitu hicho kutokana na utukufu wa kuwepo kwake. Kwani kile ambacho inabidi kiwepo hulingana na sifa ya kutoweka kwake, kwani kila kinachokuwepo basi lazima kitoweke. Isipokua kuwepo kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

Inabidi ujue kua Jina hili ‘*Allah*’ ni Jina Kubwa na Tukufu kuliko yote katika ya Majina 99 ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwa sababu jina hili ndilo linalojumuisha sifa zote za *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Kwani kila jina lake moja hua na maana moja, kama *Alimu, Qawiyum, Qayyum* n.k lakini jina hili la '*Allah*' ni jina maalum la *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Hakuna mwenye kutumia jina la *Allah* isipokua *Allah* mwenyewe. Iwe kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia nyengine, wakati majina mengine kama *Al Qadir, Al Alim, ArRahman* n,k yanaweza kutumika kwa njia nyengine. Lakini jina la *Allah* halitumiki kwa yeyote yule isipokua yeye na ndio maana likawa ndio jina Tukufu kuliko yote.'

Imam Jamal Islam Abu Qasim Al Qushayri basi anasema kua: **'Kilugha harfu *Ba* katika Neno *Bismi Allahi* hua kinawakilisha kiunganishi yaani *Bi-llah* humaanisha Kupitia kwa *Allah Subhanah***

wa Taa'la. **Ambapo mambo mapya hua ni yenye kubainishika na kupitia kwake yeye basi viumbe vilivyoumbwa huwepo. Na hua kamwe hamna katika viumbe vipya vilivyoumbwa *(hadith makhluq)* au mshikamano wa matukio yanayotokea sambamba *(Hasl Mansuq),* au kutokana na kitu kinachoonekana au kinacho hisika kihisia kwa athari zake, n.k. Au kitu chochote kutokana na jiwe au udongo au majani au miti au alama zinazobakia ardhini (*Rasm*) au mabaki yaliyosimama *(Talal)* au hukmu yeyote au sababu ambayo inayoonekana kuwepo kwake.**

Ambapo hua haviwezi kuwepo isipokua kwa kuwepo mwenye Hakika ya kuwepo. Na Hakika hio hua ni katika Mamlaka yake. Ambayo Mwanzo wake hua ni kutoka kwake na Mwisho wake hua ni kurudi kwake. Kupitia kwake yeye basi yule anaetangazia *Tawhid Allah* basi hua ni mwenye kupata na anaepinga hua ni mwenye kukosa Iman. Kupitia kwake yeye basi yule anaekubali hua ni mwenye kujua na kupitia kwake basi yule mwenye kuasi hua ni asiejua na kubakia nyuma.

Allah Subhanah wa Ta'ala **amesema '*Bismi Allahi*' hakusema '*Bi Allahi*'. Na kulingana na mitizamo ya baadhi ya watu basi husema kua hii ni njia yakutafuta Baraka kupitia katika kumtaja jina lake. Na kulingana na wengine basi basi hua ni kutokana na tofauti ya maneno haya '*Bismi Allahi*' na Kiapo '*Bi Allahi*'. Na kulingana na baadhi ya Wanazuoni basi pia tunaona kua wanasema kua ni kwa sababu ya '*Ism*' jina basi ndio kitu hua ni chenye kinaitwa '*Musamma*'.**

Ama kulingana na mtizamo wa wa watu wenye Ilm ya *Ruhaniyyat* ya Kiroho ya '*Irfan*' basi ili kupata usafi wa Moyo kutokana na mshikamano na kuikomboa Nafsi kutokana na vikwazo ili neno 'Allah' lipate kuingia ndani ya moyo uliokua msafi na nafsi iliyosafika.

Baada ya kuitaja ayah hii, basi baadhi ya watu hua wanakumbushwa kutokana na harfu '*Ba*' ambayo ni yenye kutokana na Wema au Ukarimu *(Birr)* na Mawalii wake na harfu '*Sin*' ni kutokana na Siri '*Sirr*' baina yake na wale aliowachagua na kutokana na harfu '*Mim*' kutokana na neno Rehma zake '*Manna*' kwa waja wake wenye Uwalii *(Ahl Al Walaya)*. Ambao hua wanajua kua kutokana na Rehma zake basi hua wenye kujua Siri zake, na kutokana na Rehma zake juu yao hua ni wenye kutekeleza maamrisho yake, na kutokana nae *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni wenye kujua uwezo wake.

Na kwa upande mwengine basi kuna wasemao kua: kutokana na kusikia *Bismi Allahi* hua ni wenye kukumbushwa kutokana na harfu '*Ba*' inayotokana na neno Wema au Ukarimu (*Baraa*) ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na harfu '*Sin*' kutokana na neno *Salama* na kutokua na kasoro na harfu 'Mim' inayotokana na neno Utukufu wake Mkubwa *(Majid*) katika Utukufu wa kuelezewa kwake. Wengine hua ni wenye kukumbushwa kutokana na harfu '*Ba*' kutokana na Uzuri wake wenye Upekee (*Baha*) na harfu '*Sin*' kutokana na neno Kung'ara kwa Nuru yake *(Sana),na harfu 'Mim' kutokana na Mamlaka yake 'Mulk'.*

Ama kwa upande wa Imam Abd Razak Al Kashani basi yeye anasema kua: '**Kupitia katika kutojidhihirisha, basi yule alie na hali ya *Al Wahid* (Upekee) basi hujionesha kupitia katika hali ya Al *Wahidiyyah* (Umoja). Hivyo hapa hali ya *Al Ayan Al Thabitah* (Utibitisho) ambayo hua ni utambulisho kwa ulimwengu kujionesha katika hali hii. Uthibitisho huu huendelea kujionesha katika sifa za kiumbaji. Kutokana na kutokea na hali hio ya kujionesha basi, hali hio ya *Al Tajalli Al Shuhudiyy (kujidhihirisha wazi na kushuhudiwa*) hupelekea kutokea maumbile ya jina yaani *Asmaiyyah*.**

Katika hali kama hii basi jina na sifa za Muumba hua ni zenye kuonekana wazi. Hivyo basi jina hili la *Allah* hua ni jina ambalo huonesha sifa za Muumba, na jina lake tukufu la Allah hua linaitwa *Al Asm al Adhim*. Kwa hivyo jina hili la *Allah* hua ni jina la mwanzo katika majina yake yote, na hivyo hivyo ndivyo hali inavyokua kwa sifa zake zote tukufu, kwani jina la *Allah* linajumuisha majina yake yote Matukufu na sifa zake zote tukufu.

Jina la *Allah* hua linayaunganisha pamoja majina yake yote matukufu na sifa zake zote tukufu, na hivyo *Hadhrat Ilahiyyah* (hudhihirisha sifa ya Uumbaji) hua inakua inakaa juu ya Majina yake yote Matukufu.

Ama kwa upande wa *Shaykh Al Akbar* Imam Ibn Arabi basi yeye anasema kua: **'Jina la *Allah* hua linawakilisha hali ya kuwepo kwake Muumbaji kupitia katika njia ya Hikma na Busara, kwa mfano: Jina la Muumba (*Al Asm Al Alam*) hua linatokana na vitu vilivyopewa majina. Kwa hivyo basi jina la Muumba hua linaashiria *Tanzih (Kutokuwepo Muingiliano)* baina ya muumbaji na viumbe. Na jina la Muumba hubainisha *Ithbat* (Uthibitisho) ya maumbile ya Sifa Tukufu. Hata hivyo hali ya yule aliepo hua hairuhusu kugawanyika kiidadi kwa sababu Muumbaji ni *Qiyam al Adad* (Alie mmoja Kiidadi). Majina ya muumbaji hua ni yenye cheo cha kuthibitisha sifa tukufu, kwa mfano *Al Alim* (Mwenye kujua juu ya kila kitu), *Al Qadir* (Mwenye uwezo wa kukadiria juu ya kila kitu) *Al Murid* (Mwenye uwezo wa Kutaka kila kitu), Al Samiu (Mwenye Kusikia kila kitu) *Al Basir* (Mwenye Kuona Kila kitu), n.k.'**

Anasema *Allaamah* Abu Bishr Ibn Amr Ibn Uthman Ibn Qanbar Al Basr maarufu kama Al Sibawayh anasema kua: '**Herufi *Alif na Lam* yaani *Al* ambazo haziwezi kutenganishwa peke yake mwanzoni mwa jina la *Allah* basi hua ni Muuganiko wa Jina hilo na wala halitokani na Neno au Jina lolote. Kwani Jina *Allah* kamwe haliwezi kua ni kifupi cha *Al-Ilah* kama wanavyodhani baadhi ya watu. Hivyo Jina la *Allah* ni Jina kamili la Muumba na hivyo halina ushabihiano na Jina jengine lolote la lugha yeyote. Hivyo basi Jina la *Allah* halitakiwi kutafsiriwa kwa lugha yeyote bali linatakiwa kubakia katika hali yake ya asili kama lilivyo yaani *Allah*!**'

Ama kwa upande wa Imam Nasir Ad Din Al Baydawi anasema kua: '**Muongozo huu wa kuanza na kila kitu na *Bismi Allahi* unamfunza Muumini kutafuta Baraka kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila jambo lake katika maisha yake.**'

Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Mushakiqin Shaykh ul Islami Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na ayah hii kua: '***Bismi Allahi* hua inamfunza Muislam kuomba msaada kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia katika Neema na Baraka zake katika kila kitu chake na hivyo hua ni yenye kumfanya Muislam kuanza kila kitu chake na *Dhikr Allah*. Na ndio maana katika kufanya kila kitu chako basi kuisoma ayah hii hua inapendekezwa na hua na hali ya *Mandub* katika Sharia za Fiqh'**

Katika kufafanua zaid maana aliyoinisha *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Muashakiqin Shaykh ul Islami Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi* katika kuielezea hali ya *Bismi Allah* kulingana na Sharia za *Fiqh* na matumizi yake basi tunaona kua:

1) ***Bismi Allah* hua ni *Fardhi*:** kuitamka pale Muislam anapotaka kuchinja mnyama kwa ajili ya kula au anaporusha Upinde, Mshale, Risasi wakati wa kuwinda au anapomuachia Mnyama wa kuwindia katika wakati wa kuwinda.

Na pia ni *Fardhi* kwa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii kuisoma katika Sala unaposoma *Surat Al Fatiha* au Mwanzoni mwa Sura nyengine yeyote isipokua *Surat At Tawba*

ile kwa sababu *Bismi Allah* hua ni Moja kati ya aya ya mwanzo katika kila Sura isipokua *Surat At Tawba.* Na kuisoma kwa *Bismi Allahi* kwa Sala za Kutoa Sauti hua ni Wajib kwa kila Sura isipokua *Surat At Tawba* au unapoanza katikati ya Sura. Kusoma *Bismi Allahi* kwa Sauti hua kunaulainisha Moyo wa Msomaji.

Kwani anasema Imam Abu Zakariyyah Sharaf An Nawawi kua: '**Mtu anaetaka kusoma basi asome *Bismi Allah Rahmani Rahim* mwanzoni mwa kila Sura isipokua *Surat Baraa'ah (At Tawba),* kwa sababu wengi miongoni mwa Wanazuoni wamesema kua hii ni aya popote pale itakapoandikwa ndani ya *Mus-haf*. Na imeandikwa mwanzoni mwa kila Sura isipokua katika *Surat At Tawbah*. Hivyo kama atasoma mwanzoni mwa kila Sura isipokua *Surat At Tawba* basi hua na uhakika kua amesoma *Qur'an* nzima au Sura nzima. Na kama atakua hakusoma *Bismi Allah* basi atakua ameiacha sehemu ya *Qur'a*n na hii ni kutokana na mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni'**

2) ***Bismi Allah* hua ni *Sunnah*** kuitamka wakati wa kusoma *Surat Al Fatiha* katika Sala kulingana na mtizamo wa Madhab ya Hanafi ambao ni mtizamo wa Imam Abu Hanifa, Imam Ibn Al Hammam na Imam Al Halabi.

3) ***Bismi Allah* hua si *Mustahab* wala si *Sunnah* na wala si *Makruh*** kuitamka katika wakati wa kusoma *Surat Al Fatiha* katika Sala kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Yusuf.

***4) Bismi Allah* hua ni Makruh** kuitamka katika wakati kuisoma *Surat At Tawba* ambayo haina *Bismi Allahi* mwanzoni mwake, ila kwa Mtizamo wa Imam Al Ramli basi hua ni Sunnah kuitamka unapoanza kati kati ya Sura hio ama kwa upande wa Imam Ibn Hajar Al Asqalani basi hua ni Sunnah kuisoma mwanzoni mwa *Surat Tawbah* na ni *Makruh* kuisoma wakati unapoanza kati kati ya *Surat At Tawba*.

Na pia hua ni *Makruh* kuitamka katika wakati wa kufanya mambo ambayo yana shaka ndani yake kwa mfano kama kuvuta sigara.

5) ***Bismi Allah* hua ni Mubah** kuitamka wakati wa kuanza kutembea, kukaa kitako au kusimama.

6) ***Bismi Allah* hua ni Haram** Kuitamka katika wakati wa kufanya mambo ya Haram, Kuitamka wakati unapokua na Janaba, Unapokua na Hedhi au Nifasi pale unapokua na nia ya kuisoma aya za Qur'an isipokua haiwi haram pale inapokua unafanya hivyo kwa sababu yua kutabarruk au kwa ajili ya kufanya Dhikr.

Ama kwa upande wa Shaykh Muhammad Al Amin Ash Shanqiiti basi yeye anasema kua: '**Wanazuoni wametofautiana juu juu ya *Bismi Allahi* kua ni aya mwanzoni mwa kila Sura au ni aya mwanzoni wa *Surat Al Fatiha* tu au ni aya kamili inayojitegemea kama aya nyengine ama la.**

Ama kulingana na aya isemayo:

﴿إِنَّهُۥ مِن سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُۥ بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ﴾

Innahu min Sulaymana wa-innahu bismi Allahi alrrahmani alrraheemi

Tafsir: ***Hii ni kutoka kwa Sulayman na hakika inasema Bismi Allahi Rahmani Rahim*** *(Surat An Naml 27:30)*

Basi bila ya shaka hii ni moja kati ya aya za Qur'an na hii ni kulingana na makubaliano ya *Ijmaa.* Ama kuhusiana na *Surat Baraat (At Tawbah*) Basi *Bismi Allahi* sio miongoni mwa aya za Sura hio, lakini kuna kutofautiana kuhusiana na hayo mambo mengine, kwani baadhi ya Wanazuoni wa *Usul wamesema kua Bismi Allahi si miongoni mwa Aya za Qur'an na baadhi wamesema kua ni miongoni mwa Aya ya Surat Al Fatiha tu. Na pia wako wanaosema kua Bismi Allahi ni Aya Mwanzoni mwa kila Sura, na huu ni Mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii.*
Ambapo kwa upande mwengine basi tunapoiangalia *Bismi Allahi Alrahmani Alrahimi*

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

Basi maneno *Bismi* katika *Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahimi* basi tunaona kua haya ni maneno mawili ambayo ni *Bi* na *Ism* na hivyo mwanzoni mwa neno *Ism* lenye kumaaanisha Jina kuna herufi *Alif* ambayo hata hivyo katika kutamkwa kwake basi hua haitamkwi *Alif* hii yaani inatakiwa iwe kama hivi:

بِاسْمِ

Na hii ni kwa sababu *Alif* imetokana na neno *Alafa* ambalo maana yake hua ni Kuunganisha Pamoja, Kuleta Pamoja, Kujumuisha, Kupatanisha, Makubaliano au Mshikamano.

Hivyo Herufi ya Alif katika Lugha ya Kiarabu kazi yake hua ni kuunganisha herufi mbili za tofauti kama herufi *Alif* katika neno *Bismi Allahi* ambapo inatakiwa kuwe na Alif baina ya Herufi *Ba Na Sin* lakini hua haiandikwi kwa sababu katika Lugha ya Kiarabu Herufi *Alif* hua ziko za aina mbili, aina ya kwanza hua ni ile inayojulikana kama *Alif Layyinah* au Alif Laini yaani Iliyotulia na hivyo hua ni isiyotamkwa na kuna *Alif Mutaharrikah* yaani Alif ya Muendelezo wa Sauti ambayo hua ina *Dhammah, Kasra au Fat-ha.*

Kwa upande mwengine basi *Alif Mutaharrika* hua pia inajulikana kama *Hamza* ambayo ni herufi inayotamkwa kutokea kwenye sehemu ya ndani ya mdomo yaani kooni kuelekea mbele ya mdomo. Na kuna aina kadhaa ambazo *Hamza* hua inaandikwa kwani kuna *Hamza* ambayo hua inaanzia mwanzoni mwa neno, kuna Hamza ambayo hua inaandikwa chini ya *Harfu Alif*, na hivyo hata *Alif* inapoandikwa mwanzoni mwa neno bila ya kua na *Hamza* hua ni *Hamza.* Ambapo inapotokea kua kuna *Hamza* kati kati ya neno basi hua ni yenye kuandikwa juu ya herufi Alif au Waw au pia huweza kuandikwa kwa kujitegemea peke yake.

Tunapoangalia kuhusiana na herufi *Hamz*a na herufi Alif basi tunaona kua kuna *Hamza Al Qati* ambayo ni ya Herufi ya Mkato isiyokua ya muunganisho wa neno kama vile vile kwa mfano wa jina la *Ahmad* na hivyo hua inabidi kutamkwa na hua pia inaandikwa juuya Herfui Alif, na pia kuna Hamza au Alif ambayo hua inajulikana kama *Al Wasl* ambayo hua ni *Alif* bila ya kua na Hamza juu yake na hivyo hua ni yeye kuwasilisha na kuyaunganisha maneno husika bila ya kutamkwa katika kusomwa kwake, ambapo miongoni mwa mifano wa aina hii ndio tunakutana nao katika maneno *Bismi Allah Al Rahman Al Rahim.*

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

Na hali hii ya muunganiko wa *Bismi* unatuonesha kua maneno haya ni sehemu moja ya Aya Sura, nahivyo yanaweza kuchanganywapamojakatika kusomwa kwake bila ya kusita, au kukatishwa kwani vyenginevyo basi ndani yake yangebeba *Alif Qati* au *Hamza al Qati* ndani yake.

Kwani Alif na Hamza hua zinatumika sana katika lugha ya Kiarabu katika njia tofauti kwa mfano:

1-*Alif Mamdudah* ambayo ni *Alif* ya Kuvuta au *Alif* ya Muendelezo ambayo hua inatumika kwa ajili ya kubeba Madda ambayo hua inawekwa juu yake kwa ajili ya kuuongeza nguvu sauti ya *Fat-ha*. Aina hii ya *Alif* pia hujulikana kama *Alif Ishbah* na mbali y akua ni yenye kuongeza nguvu sauti lakini pia hua ni yenye kupendezesha kwa upande wa usomaji na kuonesha ukamilifu wa Lugha ya Kiarabu.

Ambapo *Alif Mamduda* hu ani yenye kukaa mwisho wa neno lenye kubeba Kitenzi au Jina na inapokosekana basi hua inamaanisha urahisisho wa kitendo husika na kasi ya mtendaji. *Alif Mamduda* hujulikana pia kama *Alif Al Itlaq* au Alifu Isiyofungamana kwa sababu herufi inayomalizia hua ni yenye kushikamanishwa kisauti na herufi ya mwisho ya neno husika.

***2-Alif Al Fasilah* ambayo hua ni *Alif* inayowekwa baada ya *Harfu Waw* ya wingi kwa ajili ya kutofautisha baina ya herfui Waw na kile inachofuatia baada yake, ambapo pale inapotokea kua kiwakilishi cha wingi kinashikamanishwa na kitenzi katika sentensi basi *Alif Al Fasilah* hua haina haja kutumika.**

Na hivyo basi *Alif Al Fasilah* hua ni Alif ambayo inatofautisha baina ya herufi Nun ambayo hua inayowakilisha jinsia ya kike katika sehemu husika, na pia pale inapokua kuna Nun mbili zinapokua pamoja kwa sababu hua haipendezi inapokua kuna Nun za mfululizo.

3-*Alif Al Nun Al Khafifah* ambayo ni Alif Hafifu ya Nun Moja kwa mfano kwenye neno لنسفعنا La-Nasfaan ambapo inaposomwa basi inabidi kuwe kuna kupumzikia kutokana nayo Alif hii.

4-*Alif Aal Widh* ambayo ni Alif ya Mabadilisho inayotumika kwa ajili ya kubadilisha nukuu yenye kivumishi au *Tanwini* pale msomaji anaposimamia juu yake.

5-*Alif Al Istinkari* ambayo ni Alif ya kutokukubali au kupinga kwa mfano katika maneno انت قلت *AAnta Kalta yaani La Wewe hukusema hivyo.*

***6-Alif Al Nudbah* ambayo ni Alif ya Malalamiko.**

7-*Alif Al Tabi* ambayo ni *Alif* yenye kumaanisha kutowezekana kuwepo kwa hali ya kuelezea kinaxhotaka kuelezewa. Ambapo hi pia hua inaitwa *Alif Al Taghlat.*

***8-Alif Al Munqalibah an ya al Idhafat* ambayo ni *Alif* ambayo hua inabadilishwa kutokana na kiwakilishi kwa mfano *Ya,* kwenye *Ya Waylata* ياويلتئ badala ya kua *Ya Waylati*ياويلتي**

***9-Alif Muhawwalah* ambayo ni *Alif* iliyobadilika kutokana n akua mwanzo wake ilikua ni Herufi *Waw na Ya* kwa mfano kwenye neno Qala قل ambalo asili yake ni Qawla قول au katika neno *Ba'Aa* باع ambalo limetokana na neno *BayA'a* بيع.**

10-*Alif Tathniyah* ambayo ni Alif yenye kuwakilisha idadi ya Mbili kwamfano katika neno *Yajlisani* ياجلسن na pia hua ni yenye kumaanisha kivumishi cha kutuhumu.

11-*Alif al Jamaa* ambayo ni Alif ya kuongeza hali ya wingi wa vitu kwa mfano kwenye neno Masaajid مساجد.

12- *Alif Al Tanith* ambayo ni *Alif* ya kuligeuza neno kua katika hali ya jinsia ya Kike, kwa mfano kwenye neno *Hubla* ambayo hua ni *Alif Mamdudah* au kwenye neno *Hamra* ambayo hua ni *Alif Maqsura.*

13-*Alif Al Haqq* ambayo hua ni *Alif* ya Muendelezo

14-*Alif Al Takthir* ambayo hua ni Alif ya Wingi.

15-*Alif* ambayo hua inatumika kw ajili ya ubadilisha Vitenzi vya vipimo kwa mfano katika neno Aqsat au neno Ikhfa اخفاء

***16-Alif Al Tadhlil* ambayo hua n Alif ya Kudhalilisa au kushusha Hadhi kitu kwa mfano katika neno *Afdhalu* la maneno *Huwa Afdhalu minka* حو افعظل منك. Ambapo hali hii pia hutumika kuonesha hali ya Mshangao.**

***17-Alif Al Ibarah* ambayo ni Alif inayomaanisha hali ya sababu fulani.**

***18-Alif Al Istifham* ambayo ni Alif ya kuhoji ambayo hua inatumika katika hali ya kuuliza Masuali kwa njia tofauti.**

Ambapo katika Quran kua mifano mbali mbali ya matumizi ya Hamza na Alif kwa mfano:

Pale *Allah Subhanah wa Wa Ta'ala* alipoelezea kuhusiana na Kumhoji Nabii Isa Ibn Maryam kwa Masuali ambayo yatampelea Kukubali kitu anachouliza kama katika Surat Al Maidah Aya ya 116 ambayo imetumia neno AAnta أَأَنتَ pale ziliposema aya

﴿وَإِذْ قَالَ ٱللَّهُ يٰعِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ أَأَنتَ قُلتَ لِلنَّاسِ ٱتَّخِذُونِى وَأُمِّىَ إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ ٱللَّهِ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِىٓ أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِى بِحَقٍّ إِن كُنتُ قُلْتُهُۥ فَقَدْ عَلِمْتَهُۥ تَعْلَمُ مَا فِى نَفْسِى وَلَآ أَعْلَمُ مَا فِى نَفْسِكَ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّٰمُ ٱلْغُيُوبِ﴾

Wa-idh qala Allahu ya AAeesa ibna maryama aanta qulta lilnnasi ittakhithoonee waommiya ilahayni min dooni Allahi qala subhanaka ma yakoonu lee an aqoola ma laysa lee bihaqqin in kuntu qultuhu faqad AAalimtahu taAAlamu ma fee nafsee wala aAAlamu ma fee nafsika innaka anta AAallamu alghuyoobi *(Surat Al Maidah 5:116)*

Tafsir: ***Na atakaposema Allah (Katika siku ya Malipo): 'Ewe Isa Ibn Maryam, Jee uliwaambia watu wewe kua: 'Niabudini Mimi na Mama yangu kama Miungi miwili badala ya Allah Subhanah wa Ta'ala?''ambapo nae atasema: 'Utukufu ni wako pekee, kwa hakika si juu yangu mimi kusema ila ambacho sina haki ya kukisema, kwani kama ningekua nimesema kitu kama hicho basi wewe***

ungekua ni mwenye kujua juu yake. Kwani wewe ni mwenye kuju akile kilichomo ndani ya Nafsi yangu ijapokua mimi sijui kile kilichomo kwenye Nafsi yako. Kwani kwa Hakika ni wewe tu pekee ndie mwenye kujua yaliyofichikana na yasiyojulikana''

Mfano mwengine ni katika neno أَلَمْ katika *Surat Al Inshirah* pale iliposema:

﴿أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ﴾

Alam nashrah laka sadraka *(Surat Al Inshirah 94:1)*

Tafsir: ***Hivi Jee hatukukutanua kifua chako (Ewe Muhamamd Sallallahu Alayhi wa Salam)?***

Na pia katika kuthibitisha katika pale ilipotumia neno أَتَعْبُدُونَ katika *Surat As Saffat iliposema:*

﴿قَالَ أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْحِتُونَ﴾

Qala ataAAbudoona ma tanhitoona *(Surat As Saaffat 37:95)*

Tafsir: ***Akasema (Nabii Ibrahim) hivi Jee Mnaabudu yale ambayo nyinyi wenye mmeyachonga?***

Au katika neno أَصْطَفَى lililotumika katika aya isemayo:

﴿أَصْطَفَى ٱلْبَنَاتِ عَلَىٰ ٱلْبَنِينَ﴾

Astafa albanati AAala albaneena *(Surat As Saaffat 37:153)*

Tafsir: Hivi ***amechagua Watoto wa Kike kuliko Watoto wa Kiume?***

Na mfano wa *Alif* ya Kukanusha kama ilivyotumika katika neno أَفَأَ la aya ya 40 ya *Surat Al Isra:*

﴿أَفَأَصْفَاكُمْ رَبُّكُم بِٱلْبَنِينَ وَٱتَّخَذَ مِنَ ٱلْمَلآئِكَةِ إِنَاثاً إِنَّكُمْ لَتَقُولُونَ قَوْلاً عَظِيماً﴾

Afaasfakum rabbukum bialbaneena waittakhadha mina almala-ikati inathan innakum lataqooloona qawlan AAadheeman *(Surat Al Isra 17:40)*

Tafsir: ***Hivyo Jee Mola wenu (Enyi Msioamini) amekuchagulieni Watoto wa Kiume kwa ajili yenu na hivyo yeye akachukua Miongoni mwa Malaika Watoto wa Kike? Kwa Hakika Nyinyi mnazungumza mambo mabaya sana.***

Mfano mwengine ni katika kuonesha hali ya kukebehi na kejeli kama katika neno أَصَلَوَاتُكَla aya ya 87 ya *Surat Hud.*

﴿قَالُواْ يٰشُعَيْبُ أَصَلَوٰتُكَ تَأْمُرُكَ أَن نَّتْرُكَ مَا يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَآ أَوْ أَن نَّفْعَلَ فِيٓ أَمْوَالِنَا مَا نَشَاءُ إِنَّكَ لأَنتَ ٱلْحَلِيمُ ٱلرَّشِيدُ﴾

Qaloo ya shuAAaybu asalatuka ta/muruka an natruka ma yaAAbudu abaona aw an nafAAala fee amwalina ma nashao innaka laanta alhaleemu alrrasheedu(*Surat Hud 11:87)*

Tafsir: ***Wakasema: 'Ewe Shuayb Jee Ibada zako zimekuamrisha kua sisi tuachane na vile vilivyokua vikiabudiwa na Mababa zetu? Au tuachane na yale tunayoyapenda kwenye Mali zetu? Ama kwa Hakika wewe ni Muonyaji Ulioongoka'***

Alif yenye kuonesha hali ya Mshangao kama vile kwenye neno أَلَمْ aya ya 45 ya *Surat Al Furqan:*

﴿أَلَمْ تَرَ إِلَىٰ رَبِّكَ كَيْفَ مَدَّ ٱلظِّلَّ وَلَوْ شَآءَ لَجَعَلَهُ سَاكِناً ثُمَّ جَعَلْنَا ٱلشَّمْسَ عَلَيْهِ دَلِيلاً﴾

Alam tara ila rabbika kayfa madda al*dhdh*illa walaw shaa lajaAAalahu sakinan thumma jaAAalna alshshamsa AAalayhi daleelan *(Surat Al Furqan 25:45)*

Tafsir: ***Hivi Jee umeona wewe namna Mola wako anavyokitandaza Kivuli, Kwani akam anagetaka basi angekifanya kua si chenye kutembea, lakini Tumelifanya Jua kua ndio muongozi wake. (Kivuli ambapo hua kinajibana na kutoweka katika wakati wa mchana (wa Saa sita) Na kisha kinatokea tena baada ya kuelemea kwa Jua, kwani kama ingekua hakuna Jua basi ningekua pia hakuna kivuli).***

Mfano wa Alif inayoonesha utaratibu wa hali ya kuonesha utaratibu wa mwendo kihatua kama katika *Surat Al Hadid* kwenye maneno yasemayo أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ katika ya 16 iliposema:

﴿أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوٓاْ أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ ٱللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ ٱلْحَقِّ وَلاَ يَكُونُواْ كَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْكِتَابَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ ٱلأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ﴾

Alam ya/ni lilladheena amanoo an takhshaAAa quloobuhum lidhikri Allahi wama nazala mina alhaqqi wala yakoonoo kaalladheena ootoo alkitaba min qablu fatala AAalayhimu al-amadu faqasat quloobuhum wakatheerun minhum fasiqoona *(Surat Al Hadid 57:17)*

Tafsir: ***Hivi jee haujafika wakati kwenye Nyoyo za Wenye kumuamini Allah Subhanah wa Ta'ala kuathiriwa vizuri na athari za Ukumbusho (wa Qur'an) na kile ambacho kimeteremshwa ambacho ni cha haki. Ili wasije wakawa kama wale waliopokea Vitabu (Vya Taurat na Injil) na kisha Nyoyo zao zikawa ngumu? Na wengi wao ni Waasi.***

Alif hua pia ni yenye kuashiria Amrisho kama neno أَأَسْلَمْتُمْ katika aya ifuatayo:

﴿فَإِنْ حَآجُّوكَ فَقُلْ أَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِ وَقُل لِّلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْكِتَابَ وَٱلأُمِّيِّينَ أَأَسْلَمْتُمْ فَإِنْ أَسْلَمُواْ فَقَدِ ٱهْتَدَواْ وَّإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنَّمَا عَلَيْكَ ٱلْبَلاَغُ وَٱللَّهُ بَصِيرٌ بِٱلْعِبَادِ﴾

Fa-in hajjooka faqul aslamtu wajhiya lillahi wamani ittabaAAani waqul lilladheena ootoo alkitaba waal-ommiyyeena aaslamtum fa-in aslamoo faqadi ihtadaw wa-in tawallaw fa-innama AAalayka albalaghu waAllahu baseerun bialAAibadi *(Surat Al Imran 3:20)*

Tafsir: ***Hivyo kama wakigombana nawe (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) basi sema kua: 'Mimi nimejisalimisha kwa Allah na pia wale wenye kunifuata mimi' na waambie wale waliopewa Kitabu (Mayahudi na Wakristo) na wale wasiojua kusoma (Mapagani wa Kiarabu) kua: 'Hivi Jee na nyinyi mtajisalimisha katika Uislam?' na kama wakijisalimisha basi watakua ni walioongoka lakini kama wakikupa mgongo basi wajibu wako wewe ni kufikisha ujumbe, kwa Hakika Allah ni mwenye kuona kila kitu juu ya Waja wake.'***

Alif pia hu ani yenye kudhihirisha Usawa kama katika neno *Sawau* سَوَآءٍ katika ya ifuatayo:

﴿فَإِن تَوَلَّوْاْ فَقُلْ آذَنتُكُمْ عَلَىٰ سَوَآءٍ وَإِنْ أَدْرِيَ أَقَرِيبٌ أَم بَعِيدٌ مَّا تُوعَدُونَ﴾

Fa-in tawallaw faqul adhantukum AAala sawa-in wa-in adree aqareebun am baAAeedun ma tooAAadoona (Surat Al Anbiyah 21:109)

Tafsir: ***Lakini kama wao (wasioamini) watageuka (na kuukataa Uislam) basi sema: 'Nimekupeni tangazo (La vita) ambalo lijulikane kwa sote, na sijui kile ambacho mmeahidiwa (Adhabu ya Allah Subhanah wa Ta'ala) kama iko karibu ama mbali'***

Alif Al Nidaa au Alif ya Wito ambayo hua inatumika kuashiria aliekua karibu kama ilivyotumika katika maneno أَجَعَلْتُمْ katika aya ifuatayo:

﴿أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ ٱلْحَاجِّ وَعِمَارَةَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ كَمَنْ آمَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلآخِرِ وَجَاهَدَ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ لاَ يَسْتَوُونَ عِندَ ٱللَّهِ وَٱللَّهُ لاَ يَهْدِي ٱلْقَوْمَ ٱلظَّالِمِينَ﴾

AjaAAaltum siqayata alhajji waAAimarata almasjidi alharami kaman amana biAllahi waalyawmi al-akhiri wajahada fee sabeeli Allahi la yastawoona AAinda Allahi waAllahu la yahdee alqawma al*dhdha*limeena *(Surat AtTawba 9:19)*

Tafsir: ***Hivi Jee mnafikiria kua kugawa Maji kwa Mahujaji na usimamizi wa Masjid Al Haram ni sawa na thamani ya wale wenye kumuamini Allah Subhanah wa Ta'ala na Siku ya Mwisho, na kujitahidi katika kupigan akwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala? Na bila ya shaka Allah hawaongozi wale ambao ni Madhalimu.***

Au kabla ya Kivumishi cha Jina kama katika أَفِي ٱللَّهِ katika aya ifuatayo:

﴿قَالَتْ رُسُلُهُمْ أَفِي ٱللَّهِ شَكٌّ فَاطِرِ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ يَدْعُوكُمْ لِيَغْفِرَ لَكُمْ مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُؤَخِّرَكُمْ إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى قَالُوٓاْ إِنْ أَنتُمْ إِلاَّ بَشَرٌ مِّثْلُنَا تُرِيدُونَ أَن تَصُدُّونَا عَمَّا كَانَ يَعْبُدُ آبَآؤُنَا فَأْتُونَا بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ﴾

Qalat rusuluhum afee Allahi shakkun fatiri alssamawati waal-ardhi yadAAookum liyaghfira lakum min dhunoobikum wayu-akhkhirakum ila ajalin musamman qaloo in antum illa basharun mithluna tureedoona an tasuddoona AAamma kana yaAAbudu abaona fa/toona bisultanin mubeenin *(Surat Ibrahim 14:10)*

Tafsir: ***Mitume wao wakasema: 'Nini? Hivi jee kuna shaka juu ya kua Allah (Subhanah wa Ta'ala) ndie Muumbaji wa Mbingu na Ardhi?' hivyo anakuiteni nyinyi ilia pate kukusameheni dhambi zenu na kukuzidishieni juu ya majaaliwa yenu'ambapo nao wakasema: 'Nyinyi ni Ibn Adam kama sisi, na hivyo mnataka kutugeuza sisi kutokana na vile ambavyo Mababa zetu wamekua wakiviabudu? Basi tuleteeni uthibitisho wa wazi.'***

Alif katika kutambulisha Hoja nyengine kama ilivyotumika katika neno أَذَٰلِكَ pale zilipohoji aya kwa kusema:

﴿ قُلْ أَذَٰلِكَ خَيْرٌ أَمْ جَنَّةُ ٱلْخُلْدِ ٱلَّتِي وُعِدَ ٱلْمُتَّقُونَ كَانَتْ لَهُمْ جَزَآءً وَمَصِيراً ﴾

Qul adhalika khayrun am jannatu alkhuldi allatee wuAAida almuttaqoona kanat lahum jazaan wamaseeran *(Surat Al Furqan 25:15)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhamamd): 'Hivi jee Adhabu ni bora au Pepo ya Milele iliyoahidiwa kwa wenye Taqwa?' Itakua yao kama malipo ya mwisho mwema.***

Alif hua pia inatumika kulifanja neno liwe katika hali ya wakati usiokua na mwisho kama vile ilivyotumika kwenye neno أَأَنذَرْتَهُمْ pale ziliposema aya:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ سَوَآءٌ عَلَيْهِمْ أَأَنذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنْذِرْهُمْ لاَ يُؤْمِنُونَ﴾

Inna alladheena kafaroo sawaon AAalayhim aandhartahum am lam tundhirhum la yu/minoona *(Surat Al Baqara 2:6)*

Tafsir: ***Ama kwa hakika Wale wasioamini basi ni sawa kwao wao (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) kama utawaonya ama la, kwani hawatoamini.***

Baada ya kuangalia mitizamo hio kuhusiana na *Bismi Allahi* basi tunaona kua kuna umuhimu mkubwa sana kua unapoanza kufanya kitu chako na kauli ya *Bismi Allahi* katika kila jambo lako jema na linaloruhusika Kisharia hua pia ni mwenye kuonesha Shukrani kwa Mola wako kutokana na kukujaalia Neema zake zisizohesabika kutoka kwake, katika uhai wako hapa Ulimwenguni na hivyo hua ni mwenye kuukubali uwezo mkubwa wa Mola wako juu ya kila kitu alichokujaalia, huku yeye akiwa si mhitaji wa kitu chochote kutoka kwako.

Kwa maana hiyo basi Muislam anapokua ni mwenye kuzoea kuanza kufanya jambo kila jambo lake kwa *Bismi Allahi* basi hua ni mwenye kujichunga sana, katika mambo yake, na hivyo hua si mwenye kutaka kuingiza mambo yasiyofaa ndani ya jambo hilo, au mambo ya haram na hivo kumharibia jambo lake hilo, kwani kusema *Bismi Allahi* hua kunamkumbusha Muislam kua anaanza kufanya jambo ambalo lake hilo ambalo litapita katika njia za halali na hivyo kupata Baraka na Neema zaidi kutokana na kua limo ndani ya Maamrisho ya Mola wake na pia kwa kua hua haliendani kinyume na maamrisho ya Mola wake.

Na ndio maana akasema *Al Ghawth Al Adham Al Qutb Muhyi Ad Din Shaykh* Abd Al Qadir Al Jilani kua:

'***Bismi Allah* hua ni Hazina ya wale Ambao ni wenye kukumbuka.**
***Bismi Allah* hua ni Muhimu sana na ni ulinzi wenye nguvu kwa walio dhaifu.**
***Bismi Allah* hua ni Nuru kwa wenye kupenda na ni furaha kwa wenye kua na hamu.**
***Bismi Allah* hua ni liwazo kwa maumbile ya Nafsi zetu.**
***Bismi Allah* hua ni Ukombozi wa Miili yetu**.
***Bismi Allah* hua ni Nuru inayong'arisha vifua vyetu.**
***Bismi Allah* hua ni Mfumo wa kanuni unaoendesha kila jambo katika maisha yetu.**
***Bismi Allah* hua ni Taji la kila mwenye kujiamini.**
***Bismi Allah* hua ni Taa ya wenye kufikia malengo yao.**
***Bismi Allah* hua ni Maridhio ya mahitajio ya mwenye kuhitaji.**
***Bismi Allah* hua ni Jina la yule ambae anaempandisha darja mja mmoja na kumshusha darja Mja mwengine.**
***Bismi Allah* hua ni Jina la yule ambae anaeuhifadhi Moto wa Jahannam kwa ajili ya kuwachoma maadui zake kama malipo yao na anauhifadhi Uzuri wa Pepo kwa ajili ya ahadi ya Marafiki zake.**
***Bismi Allah* hua ni Jina la Yule ambae yuko peke yake asiekua na Mshirika.**
***Bismi Allah* hua ni Jina la Mwenye kuishi milele bila ya kua na Mwisho.**
***Bismi Allah* hua ni Jina la yule ambae mwenye uwezo wa Upekee bila ya kuhitaji usaidizi.**
***Bismi Allah* hua ni Dua ambayo hua ni utangulizi wa kila Sura katika *Qur'an*.'**

Naam, tunapoangalia kwa upande wa *I'lm Ruhaniyyat* basi wanasema Wanazuoni wenye I'lm hio kua: '**Kuna Majina 3000 ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Ambapo kati ya hayo basi Majina 1000 ni yenye kujulikana na Malaika pekee, Majina 1000 mengine pekee yanajulikana na Manabii, Majina 300 yametajwa kwenye *Tawrat*, Majina 300 yametajwa kwenye *Injeel*, Majina 300 Yametajwa kwenye *Zabur* na Majina 99 yametajwa kwenye *Qur'an* Tukufu. Hivyo Majina yote hua ni 2999. Jina moja lililobakia linajulikana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ambae amemjuulisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya Jina hilo na limo katika *Bismi Allahi Ar Rahmani Rahim*. Hivyo mwenye kuisoma aya hio basi hua ni sawa na mwenye kupata malipo ya aliesoma majina hayo 3000'**

Baada ya kuangalia maana na matumizi ya Jina la Allah kwa kifupi kulingana na mitizamo ya wanazuoni mbali mbali basi na tuangalie maana ya jina la pili lililoomo katika *Bismi Allahi Rahmani Rahim* ambalo ni *Rahman* na *Rahim*, ambayo ni majina yanayotokana na mzizi mmoja wa neno *Rahima* ambalo hua ni lenye kumaanisha Kupenda, Kua na Upole, Kua na Huruma, Kua na Ukarimu, kua na Wema, Kua na Rehema.

Na kama kawaida tunapozungumzia Sifa za Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Taa'ala* kimaana basi hua tunnajaribu tu kuelezea kulingana na mtizamo wa ufahamu wa Ibn Adam, kwani

ukweli ni kua kama anavyosema *Mujaddid Ad Din Hujjat ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali kua kwa vyovyote vile tutakavyojaribu kuelezea maana ya Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi kamwe hatutoweza kuelezea maana yake kikamilifu kama inavyostahiki, yaani tuchukulie mfano wa hili neno *Rahman* ambalo limetumika kwenye aya ifuatayo:

﴿قُلِ ٱدْعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدْعُواْ ٱلرَّحْمَٰنَ أَيّاً مَّا تَدْعُواْ فَلَهُ ٱلأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ﴾

Quli odAAoo Allaha awi odAAoo alrrahmana ayyan ma tadAAoo falahu al-asmao alhusna *(Surat Al Isra 17:110)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad): Muombe Allah au Muombe Mwingi wa Rehma, vyovyote vile utakavyomuomba kwani kwake yeye ndiko kwenye Umiliki wa Majina Matukufu.***

Naam, ayah hii ya *Surat Al Isra* inaweka wazi umuhimu wa kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kutumia Majina yake Matukufu ambapo Jina la *Al Rahman* linamaanisha Yule ambae ni mwenye Rehma nyingi sana kupita kiasi na hivyo kutokua na mfano wake katika Rehma zake, kwani yeye si mwenye kua na Rehma pekee tu bali pia hua ni mwenye kusababisha Rehma zake kuwafikia wale awatakao miongoni mwa waja wake waliomuamini kama inavyosema aya ifuatayo:

﴿هُوَ ٱلَّذِى يُصَلِّى عَلَيْكُمْ وَمَلاَئِكَتُهُ لِيُخْرِجَكُمْ مِّنَ ٱلظُّلُمَاتِ إِلَى ٱلنُّورِ وَكَانَ بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَحِيماً﴾

Huwa alladhee yusallee AAalaykum wamala-ikatuhu liyukhrijakum mina al*dhdh*ulumati ila alnnoori wakana bialmu/mineena raheeman *(Surat Al Ahzab 33:43)*

Tafsir: ***Ni yeye ambae ndie mwenye kukusalia, wewe na malaika wake, ili akutoe kutoka katika kiza na kukuingiza katika Nuru. Na ni yeye ambae kwa Waumini ni Mwingi wa Rehma.***

Kulingana na aya hizi basi tunaona kua *Ar Rahman* maana yake ni mwenye sifa ya kua na Rehma na *Ar Rahim* maana yake hua kutoa Rehma. Na kulingana na mtizamo wa *Shaykh Al Akbar Imam Muhyidiin* Ibn Al Arabi basi yeye anasema kua kuna: '**Neno *Ar Rahman* lina athari mbili ambapo ya kwanza ni *Athar bi al Dhat* na *Athar bi al Sual.***

Na tunapozungumzia *Athar bi al Dhat* basi hua tunazungumzia athari inayotokana na bainisho la Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia katika sifa za Rehma hizo. Kwani kimaumbile basi viumbe vyote vilivyopo hua ni vyenye kuanisha sifa ya kuwepo kwa Rehma zake. Ama kwa mtizamo mwengine basi tunapozungumzia *Athar bi al Sual* basi hua tunazungumzia athari ya Rehma ilivyogaiwa kwa viumbe. Hususan kwa viumbe Ibn Adam ambao wao hua ni wenye kupewa Rehma kulingana na jithada zao, kwa mfano pale wanapoomba kama inavyosema aya ifuatayo:

﴿إِنَّهُ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْ عِبَادِى يَقُولُونَ رَبَّنَآ آمَنَّا فَٱغْفِرْ لَنَا وَٱرْحَمْنَا وَأَنتَ خَيْرُ ٱلرَّاحِمِينَ﴾

Innahu kana fareequn min AAibadee yaqooloona rabbana amanna faighfir lana wairhamna waanta khayru alrrahimeena *(Surat Al Muuminun 23:109)*

*Tafsir: '**Bila ya shaka walikua ni miongoni mwa Makundi ya Waja wangu ambao waliokua wakisema: 'Ewe Mola wetu! Hakika sisi tumekuamini, Hivyo tusamehe, na utuingize katika Rehma zako, kwani kwa hakika wewe ni m-bora wa wenye Kuonesha Rehma**.'*

Yaani kutokana na jitihada hizo za kumuomba Mola wao basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kuwaingiza watu hao kwenye Rehma zake, kwani watu hao hua wanajulikama kama *Ahl al Hadhrah* yaani watu ambao wameingia kwenye hadhara ya Mola wao.

Sultan Al Mutakkalimin Mujaddid Ad Din Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr ad Din Al Razi kua: '**Katika *Bismi Allahi Rahmani Rahim*' kuna harfu 19, ambazo ni sawa na idadi ya Malaika wa Jahannam ambao ni 19 hivyo kila unaposema *Bismi Allahi Rahmani Rahim* basi unakua na matumaini ya kuvuka kizuizi cha adhabu ya kila mmoja kati ya Malaika hao 19 wa Moto.'** *(Na huo pia ndio mtizamo wa Mujaddid Ad Din Shaykh ul Islami Al Hafidh Shaykh Ibn Hajar Al Asqalani katika kitabu chake Al Majmaa Al Muasisi na pia Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr Al Ansari Al Qurtubi katika Ahkam Al Quran na Mujaddid Ad Din Imam Abd Rahman Al Suyuti katika Al Durr Al Mandhur).*

Tunaingia katika maana ya *Bismi Allahi Ar Rahmani Al Rahim* ambapo tunaona kua *Hujjat Al Islami Mujaddid Ad Din Az Zuhruf ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali anasema kua: '**Katika ayah hii basi tunaona kua ndani yake mmejumuishwa *Ilm* yote inayohusiana na Sifa za Majina Matukufu za *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na Ilm ya Sifa za *Ar Rahmani Ar Rahim* zimejumuishwa kwani hizi ni Sifa ambazo zimezipita Sifa zote Tukufu Kiuwezo na Kiilm. Na Sifa mbili hizi hua ni zenye kuleta hali ya hisia nzuri na zinazovutia tofauti na nyengine ambazo hua zinaamsha Ghadhabu au Khofu.**'

Ama kulingana na mtizamo wa Shaykh Al Akbar Imam Ibn Arabi basi tunaona kua yeye anasema kua: '**Jina la *Al Rahman* ni Sifa yenye kujumuisha ukubwa kamilifu wa Hikma kuhusiana na ulimwengu mzima kulingana na mapokezi ya mwanzoni mwa alie mwanzo. *Al Rahim* hua ni Sifa inayojumuisha ukubwa kamilifu kimaana kwa ajili ya Ibn Adam kuhusiana na Mwishoni mwa mwisho. Na hii ni kwa sababu wanasema wenye kujua kua: Ya Rahman kwa ajili ya Dunia na Akhera na Ya Rahim kwa ajili ya Akhera. Hii inamaanisha kuunyanyua Ukamilifu wa Ibn Adam na kuwakirimu kwa hali zote za ki ujumla na kimahsusi kwa mmoja mmoja, ni kudhihirisha Sifa ya Allah.'**

Ama kwa upande wa Imam Nasir Ad Din Al Khayr Abd Allah Ibn Umar Al Baydawi anasema kua: '**Maneno haya mawili *Al Rahmani Al Rahim* hua yanathibtisha thamani ya *mubalagha* (kutoa maana yenye uzito mkubwa wa kitu) kuhusiana na Rehma. Kwani sifa ya *Al Rahman* hua ni yenye kujumuisha jumla ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kila kitu katika ulimwengu huu, kwa Waumini na wasiokua Waumini, kuhusiana na hali ya maisha, riziki, afya, akili na ufahamu, n.k. na *Al Rahim* hua inajumuisha Sifa za *Allah Subhnah wa Ta'ala* anaetoa fadhila zake kwa Waumini, kwa kuwaongoza katika uongofu, Imani, Kufanya Mema na kuachana na Maovu katika uhai wa Ulimwenguni, na hapo hapo kuwalipa furaha ya Milele na mafanikio ya kweli kesho Akhera.'**

Ama kwa upande wa *Amir ul Muuminin Fi Al Hadith* Imam Abdullah Ibn Mubarak basi yeye anasema kua: '***Al Rahman* maana yake ni yule Mwenye Kujibu kama ikiwa utamuuomba, na *Al Rahim* maana yake hua ni yule mwenye Hasira kali usipomuomba'**

Na pia kuna wasemao kua *Al Rahman* maana yake hua ni kutoa riski kwa Viumbe wake na *Al Rahim* ni mwenye Kusamehe Dhambi za Walimuamini. Hivyo basi mtegemee *Allah Subhanah wa Ta'ala*

katika kutafuta riski yako, na mtegemee yeye katika kusamehe kasoro zako. Kwani kimaumbile Ibn Adam hua ni mwenye hali tatu zifuatazo:

‘Kwanza ni hali ya kutokuwepo kwa kiumbe kinachohitaji kuwepo. Pili ni hali ya kuishi kwa kiumbe anaetaka kuwepo Milele na Tatu ni hali ya mtu anaehitaji Usamehevu katika uhai wa Akhera, hivyo mja hua ni mwenye kumhitaji Mola wake na Sifa zake katika kutafakkari majina haya ambayo ni*: Allah Subahnah wa Ta’ala* ambae ndie Mwenye kumjaalia Mja huyo kuwepo kwake, *Al Rahman* ambae ndie anaetoa Riski kwa ajili ya Mja wake kuendelea na Uhai wake na *Al Rahim* ambae ndie mwenye Kusamehe Kasoro na makosa ya Mja katika siku ya Malipo’

Anasema Baddiuzzamman Said Nursi katika Risale Nuri kua: **‘Kauli ya *Bismi Allahi* imejaa Baraka ya hazina kiasi ya kua kutokana na kukuunganisha na *Allah Subhanah wa Taa’ala* basi hukubadilishia udhaifu wako na umasikini na kuuingiza katika ukumbi wa *Allah Subhanah wa Ta’ala*. Hivyo mtu anaenza jambo lake na *Bismi Allahi* basi hua ni mwenye kufanya jambo lake kwa jina la Mola wake na hivyo hua ni sawa na anajiunga na Jeshi na kisha akawa ni mwenye kufanya mambo hayo chini ya ngao ya jina la Taifa husika. Hua si mwenye kua na khofu na yeyote, kwani hufanya kila jambo lake kwa jina la Shariah husika na hivyo kua na ngao imara dhidi ya yeyote atakaepingana nae’**

Amesema Imam At Tabari Kua**: ‘Amesema Abu Said Al Khudri kua: ‘*RasulAllah Salallahu Alayhiwa Salam* kua: ‘Isa Ibn Maryam amesema kua *Ar Rahman* maana yake ni Mwingi wa Rehma hapa Duniani na *Ar Rahim* maana yake ni Mwingi wa Rehma kesho Akhera.’’’**

Na akasema Imam Hasan Al Basr kua**: ‘Ar Rahmani Jina ambalo limekatazwa kuitwa kwa kiumbe kwa sababu ni *Ism Al Adhim* kama ilivyokua kwa Al Khaliq ambalo haliwezi kutumika kwa Kiumbe.’**

Naam hio ni kuhusiana na *Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahiim* ama kuhusiana na sababu ya kushushwa kwake *Surat Al Kahf* basi anasema Imam Muhammad Ibn Is-haq kua: ‘**Katika kipindi hiki watu wa Quraysh wa Makkah walituma watu wawili ambao ni Nadir Ibn Harith na Uqba Ibn Abi Muit waende katika Mji wa Madina, ili kuzungumza na Mayahudi wa Mji huo kwa ajili ya kutaka kufahamu kuhusiana na Mtizamo wao kuhusiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na ujumbe wake. Hivyo Nadir Ibn Harith na Uqba Ibn Abi Muit walipokutana na Mayahudi hao basi Mayahudi hao wakawaambia Watu wa Makkah kua:**

‘Kama mnataka kujua kua yeye ni Mtume wa kweli ama la basi Muulizeni kuhusiana na mambo matatu, na kama akiyajibu kwa usahih kuhusiana na Masuali hayo basi atakua ndie Mtume wa kweli, lakini kama akijibu vyenginevyo basi mfanyeni mtakavyotaka. Hivyo Muulizeni Mtume huyo kuhusiana na Kisa cha Watu ambao walihama kutoka Katika Mji wao, ambacho ni kisa chenye upekee kabisa. Kisha Muulizeni kuhusiana na Mtu aliefunga safari na kusafiri kutoka katika upande mmoja ya Dunia hadi upande wa Pili. Na kisha Muulizeni kuhusiana na Roho ya Ibn Adam.’

Hali hii ilitokea kutokana na Makadirio ya m-bora zaidi wa kukadiria, bila ya wao Mayahudi wala watu wa Quraysh kujua Makadirio ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kuhusiana na wao kuwakilisha hoja hizo na hikma iliyomo ndani ya majibu yake Hoja zote tatu hizi ambazo ni zenye kujumuisha Mada zenye kufanana katika kuonesha hikma na mafunzo muhimu yaliyomo ndani yake Pamoja na kisa cha ziadi cha Al Khidr, ambapo vyote hivi vina mafunzo mengi ikiwemo kufanya Hijra kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala*, kama vile ambavyo walivyofanya vijana wa *Ash-hab Al Kahf* kwa ajili ya kuinusuru Imani ya Dini yao, Kufanya Hijra kwa ajili ya kutafuta Ilm kama alivyofanya Nabii

Musa ndani yake aya zilipozungumzia kuhusiana kuamrishwa kwake kufunga safari kwa ajiliya kuenda kusoma kwa yule mwenye Ilm zaidi yake yaani Al Khidr, kufanya Hijra kwa *Dhul Qarnayn* kwa ajili ya kusimamisha Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuondoa dhulma na kusimamia uadilifu.

Visa vyote hivi pia ni vyenye kutukumbusha kuhusiana na hali ya maumbile ya Roho kutoka katika hali moja na kuingia katika hali nyengine ambayo ni hali ya Barzakh ambayo ni hali ya baina ya mazingira ya Roho kua Ndani ya Mwili wa Ibn Adam hapa Duniani, na katika siku ya Kufufuliwa kesho Akhera ambapo Barzakh hua ni baada ya Kifo wakati Roho inapokua Kaburini na hivyo hali hii inatuwakilishia hali ya kua baina ya Uhai na Mauti.

Ambapo hali hii inawakilishwa katika kisa cha As-hab Al Kahf pale walipolala vijana hao kwa mda wa miaka 309 na kisha wakaamka, katika kisa cha Al Khidr inawakilishwa pale Nabii Musa alipokutana na Al Khidr katika Bahari mbili za maji chumvi na maji baridi yasiyoingiliana wala kuchanganyika baina yake, na katika mazingira ya uhai wake Al Khidr, katika Kisa cha Dhul Qarnayn inawakilishwa katika Kujenga kwake ukuta baina ya milima miwili kwa watu aliowaokoa na Juj ya Majuuj.

Na pia katika mazingira ya visa hivi basi tunakutana na Watu ambao wana Miujiza mbali ya kua wao si Mitume ambapo haya yanaonekana katika kupewa kwa watu wa *Ashab Al Kahf* na kuweza kulala usingizi kwa mda mrefu ambao haujawahi kulalwa na mtu yeyote hapo kabla, ambapo kwa upande wa Al Khidr basi ni katika kujua kwake mambo yasiyokua wazi kutokana na kupewa Ufunuo na Mola wake na kwa Dhul Qarnayn ni katika kupewa uwezo mkubwa sana wa kusimamia Uadilifu ardhini kutokana na maamrisho ya moja kwa moja kutoka kwa Mola wake.

Sasa tunarudi kwa Nadi Ibn harith na Uqba Ibn Abi Muit ambao baada ya kuambiwa kuhusiana na Hoja na Ushauri huo ambao ulikua na malengo ya kumtega na kumkwamisha kwa hoja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Basi Nadir Ibn Harith na Uqba Ibn Abi Muit wakafunga safari na kurudi katika Mji wa Makkah. Na walipofika wakafikisha Ujumbe wao huo kwa Wakuu wa watu wa Quraysh na hivyo nao wakatoka na kuenda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuulizia kuhusiana na Masuali yao hayo matatu.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakutana nao Wakuu hao wa Watu wa Quraysh na kusikiliza hoja zao na kisha akawaambia kua: **'Nendeni na Kesho Nitakupeni Jibu lenu.'** Ambapo katika kuwaahidi kwake huko basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakua ni mwenye kusema neno ***In-shaa Allah*** yaani ***Allah Akipenda,*** bali alisema tu *Nendeni na Kesho nitakupeni Jibu lenu.* Huku akiwa anategemea kua Malaika Jibril atamletea Majibu ya Masuali hayo kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Hivyo watu hao wa Quraysh wakatoka na kuamua kurudi kesho yake kama walivyoahidiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Lakini ilipofika kesho yake basi Malaika Jibril hakutokea, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* akasogeza Siku mbele hadi kesho yake lakini hata hivyo Malaika Jibril hakushuka pia*, Subhanah Allah!*

Kesho yake hio pia Malaika Jibril hakushuka hadi kufikia wiki mbili nzima ambapo Watu wa Quraysh wakaanza kushangiria kuhusiana na Kupata ushindi wa Hoja yao ambayo ndio kithibitisho wanachokitaka kua kama Kweli *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Mtume wa kweli basi na ajibu hoja zao hizo.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akaanza kua na wasi wasi na Mji wa Makkah ukaanza kua ni uliojaa tafrani kwa Waislam waliomo ndani yake kwani Jibril Hakushuka hata mara moja ndani ya siku hizo 14, ambapo hilo pia lilikua si jambo la kawaida kwake.

Hapa nataka kidogo tuulizane kua kama ikiwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikawilishiwa utekelezwaji wa Ahadi yake baada ya kutosema *In-shaa Allah,* jee hali itakua je kwetu sisi mimi na wewe?

Hivyo baada ya kupita wiki mbili basi siku iliyofuata ambayo ni sika ya 15 basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamuamrisha Malaika Jibril ashuke kwa ajili ya kuja kujibu hoja hio ya Mayahudi na Watu wa Quraysh wa Makkah.

Ambapo mara tu baada ya kushuka basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Malaika Jibril. **'Ewe Jibril imekuaje mbona Umekawia? Kiasi ya kua mimi mwenyewe nilikua tayari nimeshakua ni mwenye kujawa na wasiwasi'**

Ambapo Malaika *Jibril Alayhi Salam* nae akajibu kwa kusema kua:

﴿وَمَا نَتَنَزَّلُ إِلاَّ بِأَمْرِ رَبِّكَ لَهُ مَا بَيْنَ أَيْدِينَا وَمَا خَلْفَنَا وَمَا بَيْنَ ذٰلِكَ وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيّاً﴾

Wama natanazzalu illa bi-amri rabbika lahu ma bayna aydeena wama khalfana wama bayna dhalika wama kana rabbuka nasiyyan *(Surat Maryam 19:64)*

Tafsir: ***Na Sisi (Malaika) hua Hatushuki isipokua kwa Amri ya Mola wako (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salaam kwani Kwake yeye ndio Umiliki wa yaliyo Kabla yetu Na Yaliyo Baada yetu Na Yaliyo baina ya mawilo hayo Na kamwe Hakua Mola wako kua ni Mwenye Kusahau.***

Kwani aya hii inatuwekea wazi kwa kutuambia kua Malaika huwa hawashuki kuja Ulimwenguni isipokua kwa maamrisho ya Mola wao, kwa ajili tu ya kutekeleza lile waliloamrishwa kisha hua ni wenye kurudi mbinguni baada ya kumaliza kutekeleza amrisho hilo. Na hivyo kutokushuka kwake Malaika Jibril kamwe hakukua ni kwa sababu labda *Allah Subhanah wa Ta'ala* alisahau kumuamrisha Malaika Jibril kua ashuke.

La! Kwani hali haiko hivyo kwa sababu sifa ya kua na sahau, Hua ni sifa ya Kiumbe, yaani mimi na wewe lakini kwa upande wa Muumba ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi yeye kamwe hakuwahi kua, hana na wala hatokua na sifa hio ya kusahau. Hivyo tukio hili la kukawilishwa kushushwa kwa Malaika Jibril kuja kutoa jibu kumefanywa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ajili ya Hikma ya Kutufunza umuhimu wa kusema *In-shaa Allah*

Na umuhimu wa maneno haya mawili *In-shaa Allah* umeainisha ndani ya *Surat Al Kahf* huku ndani yake kukua na amrisho la kusema maneno hayo katika kuahidi kama tutakavyoona ndani ya Tafsiri yetu hapo baadae *In-Shaa Allah.*

Aya yetu hii pia inatuonesha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kujua juu ya kila kitu. Kabla yake, katika wake wake kiliopo kitu hicho na baada yake itakuaje iwe hapa Duniani au Akhera.

Amesema Imam Ibn Abu Hatim kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua : 'Kila Kile ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekihalalisha ndani ya Kitabu chake basi ni Halali na kile alichokiharamisha basi ni Haramu. Na kile ambacho hakukizungumzia ndani**

yake basi ni kutokana na kutokilia maanani kwa makusudi. Hivyo vichukulieni vile ambavyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuvitilia maanani kwa makusudi, kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* Hana sifa ya kusahau.'

Ambapo *Shaykh Ul Islami Al Faqih Al Muhaqqiq* Imam Ibn Hajar Al Haitami Al Shafii amesema kuhusiana na Hadith hii ya Imam Ibn Abi Hatim kua ni Hadith yenye Nguvu.

Hivyo baada ya Malaika Jibril kutoa jibu hilo ambalo limo kwenye aya ya 64 ya Surat Maryam, basi hapo hapo Malaika Jibril akatekeleza jukumu alilotumwa na Mola wake na lililomfanya ashuke katika siku hio baada ya kupita siku 15 za ukimya na jukumu hilo lilikua ni kufikisha Ujumbe wa aya za Mwanzoni za Surat Al Kahf ambapo ya kwanza ni ile iliyoanza kwa kusema baada ya *Bismi Allahi AlRahmani Al Rahiim kua*:

﴿ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ ٱلْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَل لَّهُ عِوَجَا﴾

Alhamdu lillahi alladhee anzala AAala AAabdihi alkitaba walam yajAAal lahu AAiwajan *(Surat Al Kahf 18:1)*

Tafsir: ***Shukrani Zote Anastahiki Allah (Subahanh wa Ta'ala) Ambae Ameshusha Kwa Mja Wake Kitabu Bila Ya Kukijaalia Ndani Yake (Kitabu hicho) AAIWAJAN (Kasoro, Upotovu, Ugumu, Uchafu n.k)***

Naam *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaaza na Aya hii ya Kwanza ya *Surat Al Kahf* baada ya *Bismi Allahi AlRahmani AlRahiimi* kwa kudhihirisha kua Shukran zote anastahiki yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala pekee* kutokana na Kumshushia Mtume wake *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* Ujumbe ambao hauna Shaka wala kasoro wala Upotovu ndani yake, na wala Kificho kwani kila kitu kikowazi ndani yake mbali ya kua baadhi walishakua na Wasiwasi kutokana na kuchelewa kwa Majibu ya Hoja iliyotolewa na Makafiri.

Ambapo tunaona kua aya yetu hii Neno *Awija* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye kumaanisha Kupinda, Kua na Kasoro, Kutokua Sawia, Kutokamilika, Kutotiwa Mkono na Kichafuliwa, Kisichokua Wazi, Kua na Maumbile yasiyokua Mazuri, Kua na Upotovu na pia humaanisha Kua na Ugumu mkubwa sana. Neno Awija Ndio lililotoa neno Iwajan ambalo humaanisha Upotovu au Uharibifu.

Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi anatuambia kua: '**Ndani katika Qur'an kuna hali ya matukio ambayo hua inajulikana kama *Taqdim wa Taakhir* (Kubainisha hali ya Utangulizi wa Kitu na hali ya Mwisho wa Kitu) ambayo ni mengi sana, kwa mfano pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala***

*Inatakiwa ifahamike kua '**Alhamd lillahi Aladhii anzala `al `abdihi al-kitab qayyiman wa lam yaj`al lahu iwaja' yaani 'Shukran zote anastahiki Allah yule ambae amemshushia Mja wake Kitabu kilichokamilia bila ya kukijaalia kua na kasoro.***

Ambapo Kwa upande wa *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin* Imam Fakhr Ad Din Al Razi na Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari basi wao wanasema kua Maana ya maneno yasemayo kua Hakukijaalia ndani yake kua na *Aiwajan* yanamaanisha kua Kitabu Cha Qur'an ni Kitabu ambacho Hakina Maneno Yanayopingana ndani yake, hakina Maneno yasiyokubalika na ufahamu na kutoingia akilini ndani yake kwa wale watakao tafakkari.

Na kisha Aya zikaendelea kusema kuhusiana na maneno ya Kitabu cha Qur'an kua:

﴿قَيِّماً لِّيُنْذِرَ بَأْساً شَدِيداً مِّن لَّدُنْهُ وَيُبَشِّرَ ٱلْمُؤْمِنِينَ ٱلَّذِينَ يَعْمَلُونَ ٱلصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْراً حَسَناً﴾

Qayyiman liyundhira ba/san shadeedan min ladunhu wayubashshira almu/mineena alladheena yaAAmaloona alssalihati anna lahum ajran hasanan *(Surat Al Kahf 18:2)*

Tafsir: **(Kimejaaliwa kua) Kiko Katika Mstari Sawia kwa Ajili ya Kuonya Adhabu Kali Sana Kwake yeye *(Allah Subhanah wa Ta'ala)* Na Kuwabashiria Waumini wale Ambao ni wenye Kufanya Mema Kua kutakuwepo kwa ajili yao Malipo Bora.**

Naam..baada ya aya kudhihirisha Ukamilifu wake na uwazi wa Quran basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anadhuhurisha Malengo ya Kitabu chake hicho na hivyo kuwaonya wale wanaokidharau na pia kudharau ujumbe wa Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha Kuwabashiria wale wakaokifuata Kitabu chake na Ujumbe wake kupitia kwa Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua watakua na malipo makubwa na mazuri sana.

Ambapo katika aya mbili hizi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaweka Uhakika, Usafi na Uzuri wa Qur'an Kabla ya Kujibu Hoja iliyowakilishwa na hivyo kua ni mwenye kuonya kua Msiyadharau nitakayo yadhihirisha kwani ni yenye Uhakika na hivyo Kama mkiyadharau basi kuna Adhabu kubwa sana inakusubirini.

Ambapo *Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Dina Al Razi anatuambia kua : '**Aya mbili hizi zimetumia maneno *Aiwajan* na *Qayyim* ambapo neno *Iwaj* linazungumzia Kuhusiana na Ukamilifu wa Ndani ya Qur'an na neno *Qayyim* linazungumzia kuhusiana na Uwezo wa Qur'an katika Kuwasimamia Ibn Adam kua katika Njia iliyonyooka.'**

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasisitizia kua Walioamini na watakaomaini Ujumbe wake basi Watakua katika hali hio ya Uzuri wa Malipo ya kua ndani ya Pepo Milele kama inavyosema aya:

﴿مَّاكِثِينَ فِيهِ أَبَداً﴾

Makitheena feehi abadan *(Surat Al Kahf 18:3)*

Tafsir: **Watabakia Ndani yake (Peponi) Daima.**

Tunapoiangalia aya yetu basi tunaona kua imetumia neno *Makatha* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kuishi, Kufanya Makazi, Kukaa, Kubakia, Kusubiri katika sehemu,

Neno *Makatha* ndio lililotoa neno *Mukthin* ambalo humaanisha Hatua kwa hatua, Taratibu kwa malengo yenye Umakini.

Na pia neno *Makatha* likatoa neno *Makithin* ambalo lenye kumaanisha wenye kubakia katika hali husika waliyokua nayo.

Kwa upande mwengine pia tunaona kua aya yetu hii pia imetumia neno *Abadan* ambalo wengi kwa kiswahili hua tunalitafsiri sivyo, au labda kwa kiswahili hua linatumika sivyo kwani hua linatumika katuka hali ya kukanusha.

Wakati neno *Abadan* maana yake hua Kudumu, Kukaa, Kuishi katika makazi au sehemu husika kwa mda mrefu sana. Ambapo neno *Abadan* hua pia ni lenye kusisitizia hali ya Kuendelea kubakia katika sehemu au hali husika kwa mda mrefu sana tena wa Miaka.

Kwani kwa Kilugha neno *Abada* hua linatumuka pale tunapozungumzia Mda mrefu usiokua na Mipaka yaani Daima au Milele.

Ambapo tunapozungumzia mda au wakati wenye mpaka au mipaka kama Masaa, Masiku,Wiki, Miezi au Miaka kadhaa basi wenye lugha yao hua wanatumia neno *Zaman*.

Hivyo katika aya yetu hii basi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala aliposema* kua Waliamini na watakaoamini na wakafanya mema basi Watalipwa Malipo Mazuri ya Pepo na kua: *Makithiina Fiihi Abadan,* Basi ni mwenye kutuonesha kua Ukubwa wa Wakati wa kubakia ndani ya hali ya Malipo hayo Mazuri kwa kutumia neno *Makithiina na Abadan,* yaani Watakaoamini Watabakia ndani ya hali nzuri ya Malipo hayo kwa mda mrefu usiokua na mipaka yaani Milele na hivyo Hawatotoka Tena ndani yake.

Naam..yaani hapa aya imetumia maneno haya mawili tu, lakini maana yake ni kubwa na pana sana kiasi ya kua tunapoizungumzia kiwakati basi ni sawa na wakati ambao ni wa kukaa ndani yake kwa Milele kusikokua na kikomo wala mwisho wake wala kutoka ndani yake sehemu husika wala kupungukiwa au kukatishiwa kwa hali ya raha iliyomo ndani yake wanayoipata watu hao wanaostahiki malipo hayo ambao ni wenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala na* kisha wakawa ni wenye kufanya Mema.

Hivyo baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutoa ahadi ya Malipo ya Makithina Fiihi Abadan yaani Kukaa Ndani ya Pepo Kwa Milele bila ya kutoka ndani yake Peponi humo wala kupunguziwa au kusitishishwa Raha zilizomo ndani yake kwa wale watakaomuamini na wakawa ni wenye kufanya mema.

Ambapo *Hujjat Ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali amesema kua Mfano wa Raha ya Peponi ni Mithil ya Raha Wanayoipata Mume na Mke, pale wanapoingiliana Kimwili, ambapo Raha hio huonjeka hapa Duniani kwa mda Mchache tu, lakini kwa upande wa Peponi basi Raha hio hua ni yenye Sifa 2 za *Makithina* na *Abadan* yaani ya Kudumu Milele ndani yake na isiokatika wala kupungua Utamu wa Ladha yake bali ni wenye kuendelea.

Yaani hii kama hapa Duniani basi Unaweza ukaingia Wazimu au Ukafa kabisa..La kwa Peponi Hakuna kua na Wazimu wala Kifo bali kuna muendelezo tu wa hali ya Raha husika Daima.

Kwani baada ya kudhihirisha juu ya halo watakayokua nayo Walioamini na pia kubainisha Kitakacho wafika Wasioamini basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kuwaonya Wale wasiomuamini ambao ni Wakristo, Mayahudi na Mapagani kwa kusema kitabu cha Qur'an kimekuja pia kwa ajili ya:

﴿وَيُنْذِرَ ٱلَّذِينَ قَالُواْ ٱتَّخَذَ ٱللَّهُ وَلَداً﴾

Wayundhira alladheena qaloo ittakhadha Allahu waladan *(Surat Al Kahf 18:4)*

Tafsir: ***Na kuwaonya wale ambao ni wenye kusema kua: 'Allah ana mtoto'.***

Kwani katika Kipindi ambacho alichokua akiishi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Kabla yake pia na baada yake na hadi hii leo pia basi kulikua na bado pia wapo watu ambao Wanaimani ya kua Mungu ni mwenye kua na Kizazi, kwa mfano Mayahudi ni wenye kusema kua Mungu Mtoto wake ni Uzayr. Na Wakristo ni wenye kusema kua Mungu Mtoto wake ni Masih. Na Mapagani wanasema kua Malaika ni Watoto wa Kike wa Mungu.

Hivyo Aya ni zenye Kukanusha Juu ya hayo na hapo hapo kuonya kuhusiana na Mitizamo yao hio ya Kiimani. Na haya yamezungumziwa kwenye *Surat At Tawba* pale iliposema:

﴿وَقَالَتِ ٱلْيَهُودُ عُزَيْرٌ ٱبْنُ ٱللَّهِ وَقَالَتِ ٱلنَّصَارَى ٱلْمَسِيحُ ٱبْنُ ٱللَّهِ ذَٰلِكَ قَوْلُهُم بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِـُٔونَ قَوْلَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِن قَبْلُ قَاتَلَهُمُ ٱللَّهُ أَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ﴾

Waqalati alyahoodu AAuzayrun ibnu Allahi waqalati alnnasara almaseehu ibnu Allahi dhalika qawluhum bi-afwahihim yudahi-oona qawla alladheena kafaroo min qablu qatalahumu Allahu anna yu/fakoona *(Surat At Tawba 9:30)*

Tafsir: ***Na Wanasema Mayahudi kua Uzays Ni Mtoto wa Allah Na Wanasema Manasara Kua Masih (Isa Ibn Maryam) ni Mtoto wa Allah Hizo Ndio Kauli zao Kutoka Midomoni mwao Wanaiga Kauli za Wale ambao Waliokufuru Kabla Yao Laana ya Allah iwe Juu yao Kwani Wako Mbali sana na Ukweli.***

Hivyo katika Surat yetu ya *Al Kahf* basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawaambia tena Watu wenye Mitizamo hio ya Kiimani kua:

﴿مَّا لَهُم بِهِۦ مِنْ عِلْمٍ وَلَا لِـَٔابَآئِهِمْ كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَٰهِهِمْ إِن يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا﴾

Ma lahum bihi min AAilmin wala li-aba-ihim kaburat kalimatan takhruju min afwahihim in yaqooloona illa kadhiban *(Surat Al Kahf 18:5)*

Tafsir: **Hawana Juu ya Jambo Hilo Ilm yake Na Wala hawakua na Ilm Nalo Wazee wao Ni Makubwa Sana Kiuasi Maneno (yao hayo) Yenye Kutoka Kwenye Midomo yao Hayo Wanayoyasema (Ya Kua Mungu ana Mtoto mara wa kiume ambae ni Uzayr, Mara Isa Mara wa Kike ambao ni Malaika) si chochote Isipokua ni Uongo Mtupu**.

Ambapo baada ya hapo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamliwaza Mtume wake Salallahu Alayhi wa Salam kuhusiana na Uzito wa Jukumu lake la kuufikisha ujumbe wake uliomo ndani ya Qur'an na namna Ulivyopokelewa kwa Upinzani mkubwa na watu wake kwa kusema:

﴿ فَلَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفْسَكَ عَلَىٰ آثَارِهِمْ إِن لَّمْ يُؤْمِنُواْ بِهَٰذَا ٱلْحَدِيثِ أَسَفاً ﴾

FalaAAallaka b<u>a</u>khiAAun nafsaka AAal<u>a</u> a<u>th</u><u>a</u>rihim in lam yu/minoo bih<u>adha</u> al<u>h</u>adeethi asaf<u>an</u>*(Surat Al Kahf 18:6)*

Tafsir: ***Kisha Huenda ikakubidi Ujiangamize Nafsi yako Kutokana na Athari zao (zitakazokuathiri) Kwa sababu ya Kutoamini Hiki Kisa kwa Huzuni (itakayokufika)***

Tunapoiangalia aya hii basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamdhihirishia Mtume wake kwa kumwambia kua Ingawa Umejitahidi sana kwa nguvu na uwezo wako wote kufikisha Ujumbe wa Qur'an lakini, kutokana na hali yako ya Kimaumbile basi Umekua na Khofu kubwa sana ndani ya Moyo na Nafsi yako kua pale Watu hawa waliotoa hoja yao ambayo Mimi nitaijibu Kiusahih halafu wao wakawa hawajakubaliana nayo hivyo unajiuliza Juu ya kile kitakachofuatia baada ya hapo kutokana na Onyo langu juu yao.

Yaani mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliomba kua Ajibiwe hoja yake hio lakini sasa hapo hapo amekua na khofu kubwa sana jee hali Itakuaje kama hoja yao ikajibiwa na kisha watu hao wa Makkah wakawa hawakuamini? Jee watapewa Adhabu gani? Wataangamizwa kama walivyoangamizwa watu wengine waliotangulia kabla yake ama la, au itakuaje?

Hivyo uzito wa Hisia hizi za Masuali yaliyomo ndani ya Nafsi yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa watu wa Makkah ulikua unamuumiza sana ndani ya Roho yake kiasi ya kua anahisi kua kama atakufa kwa maumivu ndani ya Nafsi na Moyo wake kwani yeye ni mwenye kua na Huruma sana kwa Ummah wake ambao ndani yake unajumuisha kila alianza kuishi baada ya kupata Utume wake, na ndio maana akasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana nae kwa kumpa majina yake mawili matukufu kama zilivyosema aya:

﴿لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾

Laqad j<u>a</u>akum rasoolun min anfusikum AAazeezun AAalayhi m<u>a</u> AAanittum <u>h</u>aree<u>s</u>un AAalaykum bialmu/mineena raoofun ra<u>h</u>eemun *(Surat At Tawbah 9:128)*

Tafsir: ***Kwa hakika amekujieni kwenu nyie Mtume (Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam)kutoka miongoni mwenu (ambae mnamjua). Inamuuma yeye kua nyinyi mdhurike au muingie matatizoni, kwani yeye kwa Waumini ni mwingi wa Upole na mwingi wa Huruma.***

Na hii ni kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwenyewe ni mwenye kuwapenda na kuwaonea huruma Viumbe wake kama anavyosema katika sehemu kadha ndani ya Qur'an ikiwemo ifuatayo:

﴿ وَلَوْلاَ فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ ٱللَّهَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴾

Walawl<u>a</u> fa<u>dh</u>lu All<u>a</u>hi AAalaykum wara<u>h</u>matuhu waanna All<u>a</u>ha raoofun ra<u>h</u>eemun*(Surat An Nur 24:20)*

Tafsir: ***Na kama isingekua Fadhila za Allah (Subhanah wa Ta'ala) juu yenu na Rehma zake (basi angekua tayari ameshakuadhibuni) na Allah (Subhanah wa Ta'ala) ni mwingi wa Upole na Huruma.***

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anakhofu kubwa sana kua huenda Watu hao hawatokubaliana nae kumfuata pale atakapojibu Hoja walizompa, na kisha huenda wataangamiza na yeye hataki Waangamizwe...ila hajui itakuaje baada yake na kwa kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kuona na kujua kula kitu basi hapa alikua akiielezea hali ya Uzito mkubwa sana aliyokua nayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani ya Nafsi yake, kwani kimaumbile basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni mtu mwenye Wingi wa Huruma kwa Ummah wake ni kama ilivyoelezewa kwenye Hadith ambayo inapatikana katika Sahih Muslim ambayo inasema;

Amesema *Rasul Allah Salallahi Alayhi wa Salam* kua**: 'Mfano wangu mimi na Watu wa Umma wangu, hua ni sawa na Mfano wa mtu aliekua sehemu ya Kiza kisha akawasha moto ili Moto huo umuangazie sehemu Umuangazie sehemu hio aliyokuwepo, Lakini sasa Moto huo ukawasababishia Wadudu wanaoruka ruka karibu kuangukia ndani yake na kila Mtu huyo akijaribu kuwapepea Wadudu hao wasiukaribie Moto basi Wadudu hao ndio kwanza wanamzidi nguvu na Kujitumbukiza Motoni Kwani hali yangu mimi ni kutafuta Njia ya kukuepusheni nyinyi na Moto lakini nyinyi mnajitumbukiza ndani yake'**

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na malengo ya kutumwa kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam pia* kua:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَاكَ إِلَّا رَحۡمَةٗ لِّلۡعَالَمِينَ﴾

Wam<u>a</u> arsaln<u>a</u>ka ill<u>a</u> ra<u>h</u>matan lilAA<u>a</u>lameena *(Al Anbiyah 21:107)*

Tafsir: ***Na Hatukukutuma wewe sisi isipokua uwe ni Rehma kwa Walimwengu.***

Na amesema Jubayr Ibn Mutim kua: **'Amesema baba yangu kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa salam* kua: 'Hakika mimi nna majina mengi, kwani mimi ni Muhammad, mimi ni Ahmad, mimi ni Mahi ambae kupitia kwake basi *Allah Subhanah wa Taala* ameibatilisha Ushirikiina, mimi ni *Hashir* (Mkusanyaji) ambae watu watakusanyiwa chini ya miguu yake, mimi ni Aqib ambae hakuna atakaefuatia baada yangu, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemwita Mwingi wa Ukarimu na mwingi wa Huruma''** *(Sahih Muslim)*

Ambapo kwa upande wa *Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Rehma kwa Waumini na kwa wasiokua Waumini kwani kutokana nae basi Wasioamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* wamekua salama tofauti na hali ilivyokua kwa watu wa aina hio katika nyakati za Mitume waliotangulia kabla yake.'**

Na anasema Imam Al Qadhi Iyad kua : **'Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia Malaika Jibril: 'Hivi jee kuna sehemu ya Rehma yangu hiii ambayo wewe pia imekugusa?' ambapo Malaika Jibril akasema kua: 'Naam..kwani mimi nilikua nna khofu juu ya kile kitakachonifika, lakini sasa hivi najisikia salama kutokana na pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala kua:***

﴿إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ۞ذِى قُوَّةٍ عِندَ ذِى ٱلْعَرْشِ مَكِينٍ۞ مُّطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ﴾

Innahu laqawlu rasoolin kareemin; Dhee quwwatin AAinda dhee alAAarshi makeenin ; MutaAAin thamma ameenin*(Surat Takwir 81:19-21)'*

Tafsir: ***Kwa hakika hii ni kauli (Qur'an imeshushwa) kupitia kwa Mjumbe (Malaika Jibril) mwenye Darja kubwa; Mwenye Nguvu kubwa sana na mwenye Darja kubwa mbele ya Mmiliki wa Arshi; Mtiifu na ni mwenye kuaminika.***

Hivyo maneno haya yanamaanisha *kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Rehma kwa Malaika pia, na kama alivyosema Imam Al Layth Al Samarqandi basi yeye amesema kua: **'Maana ya maneno yasemayo *Wama arsalnaka illa rahmatan lilAAalameena* ni kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Rehma kwa viumbe wote Wakiwemo Majini na Ibn Adam, kwani ni Rehma kwa Waumini kwa Kuwaongoza katika njia Sahih, ni Rehma kwa Wanafiq kwa kuwapa Usalama kutokana na kutouliwa ni Rehma kwa Makafiri kutokana na kuwacheleweshea Adhabu yao hapa Duniani.'**

Kisha baada ya hapo aya zinaendelea kufafaunua kama tunavyoona pale tunapoiangalia aya ya 7 ya *Surat Al Kahf* ambapo tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua:

﴿إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى ٱلْأَرْضِ زِينَةً لَّهَا لِنَبْلُوَهُمْ أَيُّهُم أَحْسَنُ عَمَلاً﴾

Inna jaAAalna ma AAala al-ardhi zeenatan laha linabluwahum ayyuhum ahsanu AAamalan*(Surat Al Kahf 18:7)*

Tafsir: ***Kwa Hakika Tumejaalia Yale yaliyopo Juu ya Ardhi Kua Ni Mapambo yake Ili Kuwajaribu watu Kuwajua ni wepi wenye Amali Bora zaid*** *(Surat Al Kahf 18:7)*

Naam..ingawa aya iko wazi kimaana kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameipamba Ardhi kwa Mapambo yenye kuvutia kwa ajili tu ya Kuwajaribu Ibn Adam ili wajulikane ni yupi na yupi ni mwenye Kupenda kufanya Amali njema.

Na ndio maana kwa upande wa *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abass *Radhi Allahu Anhu* basi yeye akasema kua: **'Maana ya neno *Zinatan* lililotumika hapa hua linamaanisha Wenye Ilm kua ndio mapambo ya juu Ardhi kutokana na Kufanya Mema yao.'**

Ambapo kwa Upande Imam Hasan Al Basr basi yeye amesema kua: **'*Zinatan* waliomaanishwa hapa ni wale Watu wenye kutumia mda wao kwa ajili ya kumtii Mola wao'**

Lakini kwa upande mwengine basi kuna baadhi miongoni mwetu wanaweza wakajiuliza suali lifuatalo: Hivi kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie Muumba wa Kila kitu na ndie mwenye kujua kila kitu, basi kwanini ikawa anasema kua Ameyajaalia Mapambo yaliyopo Juu Ardhini kwa sababu ya kuwajaribu Watu ili wajulikane wepi watakua wanapenda kufanya Mema? Hivyo jee hii inamaanisha kua yeye hawajuia ama vipi?

Kupata jibu la suali hili basi inabidi tukumbuke kua Miongoni mwa sifa za *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi mbali ya kua ni mwenye kujua juu ya kila kitu lakini pia ni kua ni mwenye Uadilifu. Hivyo yeye kama yeye anajua kua fulani atakua ni mtu asiependa kufanya mema na fulani atakua anapenda.

Hivyo amefanya mtihani huu ili sisi tupate kujuana nani ni mtu mwema na nani si mwema, na tupate kujijua sisi wenyewe ndani ya Nafsi zetu. Baada ya kudhirishishwa kua hili silo hili ndilo. Hivyo tupate kujijua na kushuhudiana kuhusiana na tuyafanyayo.

Na ndio maana akasema Imam Hasan Al Basr kua: '**Msiikumbatie Dunia kwa sababu ni sehemu ambayo Adam ameshushwa Ndani yake kwa ajili ya Kuadhibiwa tu.**'

Hivyo Dunia na yaliyomo Juu yake ni sehemu ya Majaribio ambayo alipewa Nabii Adam baada ya Kufeli kwa mara ya kwanza alipokua Peponi na hivyo akaadhibiwa kushuka Duniani na kupewa fursa ya pili kwa ajili ya kujirekebisha na kupata mafanikio ya Milele ambayo ni *Makithiina fiihi Abadan.*

Na ili kupata Mafanikio hayo basi ndio inabidi tufuzu mtihani kwanza unaotukabili hapa juu ya Ardhi kabla ya kukutana na yatakayofuatia Chini ya Ardhi na ndio maana akasema Umar Ibn Al Khattab. *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wallahi Naapa mie kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae hakuna Mola zaid yake kua Kama ingelikua nna Dhahabu na Fedha zote zilizopo Ulimwenguni nigezitoa mimi kwa ajili tu ya kujiokoa na Kitakachofuatia baada ya Kifo.'**

Allahuma Nsurna Fawqa AlArdhi w Tahta Al Ardhi wa Yawma Al Ardhi Alayh..Amiin,

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Dunia ni ya Imenawiri na Tamu, Hivyo Bila ya Shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakupeni Mtihani ndani yake ili akuangalieni Mtafanya nini, Hivyo Muogopeni Allah na iogopeni Mitihani..wakiwemo Wanawake'***(Sahih Muslim, Imam Ibn Jarir)*

Neno *Jaraza* kwa Kilugha hua linamaanisha Kukata, Kumtia Ari Mtu ili awe ni mwenye kufanya Kitu. Neno *Jaraza* ndio lililotoa neno *Ajraza* ambalo hua linamaanisha Kua Tasa. Kutoweza Kuzaa Mtoto kwa Ibn Adam au Mnyama na pia humaanisha Kutoweza Kuzaa Matunda Kwa Mti au Kutoweza Kuotesha kitu kwa Ardhi. Neno *Jaraza* pia limetoa neno Juruz ambalo humaanisha Ardhi Kame, au Kavu na pia humaanisha Mtu aliekufa bila ya Kuacha Mirathi kutokana na kua hana kitu.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kusema kua:

﴿وَإِنَّا لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيداً جُرُزاً﴾

Wa-inn<u>a</u> laj<u>a</u>AAiloona m<u>a</u> AAalayh<u>a</u> <u>s</u>aAAeedan juruz<u>a</u>n *(Surat Al Kahf 18:8)*

Tafsir: ***Kwa Hakika sis Tutajaalia Kilichopo Juu yake (Ardhi) Kua Ni Ardhi Kame Sana*** *(Surat Al Kahf 18:8)*

Ambapo anasema *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr* Ad Din Al Razi kua: **'Neno *Saaid* lililotumika hapa linamaanisha hali ya Ardhi ya Tambarare isiyokua na uwezo wa kuota kitu chochote juu yake.'**

Na neno *Juruz* hua linamaanisha Hali ya eneo la Ardhi ambalo ni Kame lakini lililozungukwa na sehemu iliiyoota Majani

Na hivyo aya hii kua ni yenye kudhihirisha kua mbali ya kua *Allah Subhanah wa Taa'ala* ameipamba Ardhi lakini hapo hapo anaouwezo wa kuifanya Jangwa isiyokua na uwezo wa kuotesha chochote juu yake.

Kwani maana ya maneno haya basi ni kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamwambia Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam kua:* **'Wenye akili na Ufaham hua kamwe hawezi kuhadaika na manufaa ya Uzuri ulipo Ardhini ambao ni wa mpito, kwani wakati wowote mapambao hayo yanaweza yakatoweka, na hivyo wenye akili na Ufaham hua ni wenye kukimbilia manufaa ya Kiakhera ambayo ni ya milele na yasiyotoweka'**

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Dunia ni Utajiri kwa wale wasiokua na kitu. Na hivyo ni wale wasiokua na Ufahamu tu ndio wanaoukumbatia Utajiri huo.'**

Na akasema Imam Abu Saud Muhammad Ibn Muhammad Al Hanafi kua: '**Yeyote yule mwenye Matendo mema yaliyo bora hua ni mwenye kuachana na Dunia yake. Kwani hua ni mwenye kutosheka na sehemu ndogo tu kutokana nayo Na hua ni mwenye kutumia kidogo hicho alichokua nacho kwa ajili ya Manufaa yaliyo bora zaid Na atakifurahia kukitumia kidogo hicho katika njia alizoziruhusu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Kusimamia Haki zake katika matumizi yake na kua ni mwenye shukrani na neema ya kidogo hicho. Na kamwe hatokitumia kwa kuendekeza Matamanio ya Nafsi yake, jambo ambalo ni tofauti na wafanyavyo wale wasioamini na wanaoendekeza matamanio ya nafsi zao.'**

Aya inayofutia ambayo ni aya ya 9 ya *Surat Al Kahf* na ndio Aya iliyobeba jina la *Sura* yaani *Surat Al Kahf* ni aya ambayo inayotuonesha kua tumeingia rasmin kwenye kisa cha *As-hab Al Kahf* kwa maneno yenye kusema:

﴿أَمْ حَسِبْتَ أَنَّ أَصْحَابَ ٱلْكَهْفِ وَٱلرَّقِيمِ كَانُواْ مِنْ آيَاتِنَا عَجَباً﴾

Am <u>h</u>asibta anna a<u>s</u>-<u>ha</u>ba alkahfi waalrraqeemi k<u>a</u>noo min <u>ay</u>atin<u>a</u> AAajab<u>a</u>n *(Surat Al Kahf 18:9)*

Tafsir: ***Hivi Nyinyi Mnahesabu (Au Mnadhania) Kua Watu wa Al Kahf Na Maandishi yao (Na Alama Yao) kua ni Miongoni mwa Maajabu ya Miujiza yetu?***

Ambapo neno *Raqama* kwa Lugha Ya Kiarabu hua linamaanisha Kuandika, Kupigia Mstari, Kuchora kwa Mistari, Kutia au Kuweka Alama maalum.

Neno *Raqama* ndio lililotoa neno *Raqimi* ambalo hua linamaanisha Maandiko, Maandishi, Michoro au Alama.

Kwani anasema *Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na aya yetu hii inayowazungumzia watu wa As-hab Al Kahf kua: **'Aya hii imetumia neno *Al Kahf* kumaanisha kitua kinachozungumziwa hapa ni Pango tena kubwa Sana, na hii ni kwa sababu Pango la Kawaida hua haliitwi *Kahf* bali hua linaitwa *Ghar.'***

Imam Fakhr Ad Din Al Razi anaendelea kutuambia kua: '**Ama kuhusiana na Al Raqiimi ni Maandiko yenye kuelezea Kisa Vijana hawa wa *As-hab Al Kahf.'*** Ambao huu pia ni Mtizamo wa Mujtahid Imam Abu Bakr Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii.

Na hii ni kwa sababu ya kua neno *Raqama* ndio lililotoa neno *Marquum* ambalo ndilo lililotumika kama ilivyosema aya ifuatayo:

﴿كِتَابٌ مَّرْقُومٌ﴾

Kitabun marqoomun*(Surat Al Mutaffifin 83:9)*

Tafsir: ***Kitabu Kilichorikodiwa.***

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Jurayj basi yeye anasema kua: ***'Al Raqiimi* ni Maandiko ambayo ndani yake yana tarehe ambayo Watu hao walizama kwenye Usingizi mzito hadi tarehe ya kuamka kwao'**

Ambapo kwa upande wa Imam Said Ibn Jubayr na Imam Mujahid Ibn Sulayman basi wao wanasema kua: **'*Al Raqiimi* ni Maandiko ambayo yanaelezea Kisa cha *As-hab Al Kahf*'.**

Na kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Sahal Al Tustari basi yeye anasema kua: **'Al Raqiimi ni Kiongozi wao miongoni mwao ambae alikua akiitwa Mbwa, ingawa walikua hawana Mbwa. Ambapo kuhusiana na kunyoosha miguu ya mbele ya Mbwa huyo basi kunamaanisha Kunyoosha miguu yaani kua na Msimamo katika Maamrisho na Makatazo ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

Ambapo kwa upande mwengine basi kuna Wanazuoni wanaosema kua *Al Raqiimi* ni Jina la Kijiji ambacho Vijana hao walikua wakiishi na kukikimbia, na kuna wasemao kua ni Eneo la Bonde ambalo Vijana hao walikimbilia, na kuna wanaosema kua ni eneo la Milima ambayo ndio yenye Pango hilo ambalo Vijana walikimbilia, na kuna wasemao kua ni Mbwa wao na kuna wasema kua ni Kitabu chenye Maandiko na Alama yao.

Ila mbali ya hayo yote lakini aya hii pia ina maneno makubwa zaid yenye Nguvu ambayo ni kifungio cha aya hii kinachowahoji Makafiri wa Makkah na Mayahudi kwa kusema kua: **'Akh! Hivi nyinyi ndio mmeona kua jambo kubwa sana na la Ajabu sana hilo la Kisa cha Watu wa *As-hab Al Kahf* na *Raqimi* wao na kulala kwao kwa miaka yote waliyolala? Hivi Jee hamkuona Miujiza Myengine Mikubwa yoote iliyojaa Ardhini na Mbinguni yenye kuthibitisha kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* kua ndie Mtume wake? Mpaka mkauliza kisuali kisichokua na uzito kama hicho?'**

AS-HAB AL KAHF WA KWANZA AMBAO NI WATU WATATU WENYE TAQWA.

Tunapongalia miongoni mwa mitizamo ya Wanazuoni kuhusiana na *Raqiimi* basi umo ule wa Mtizamo wa Sahaba aitwae Nu'man Ibn Bishr Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* ambae yeye anasema kua: **'Mimi nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akitaja kuhusiana na Al *Raqiimi* kuhusiana na kisa cha Watu watatu ambao walikua Safarini wakirudi katika Famili zao na mara ikanyesha Mvua kubwa sana, na hivyo Watu watatu hao wakakimbilia kujificha kwenye Pango.**

Ambapo wakati wakiwa kwenye Pango hilo basi mara likaanguka Jiwe kubwa sana kutoka Juu yao na kuuziba Mlango wa Pango hilo walilojifichia ndani yake, Hivyo mmoja kati ya Watu hao akasema kuwaambia wenzake kua: Hapa hatuna cha kufanya isipokua kila mmoja wetu aombe kutokana na Jambo jema zaid alilolifanya na hivyo huenda *Allah Subhanah wa Ta'ala* akatuingiza kwenye Rehma zake.

Ambapo mmoja wao akaanza kwa kusema kua: Mimi nilifanya Jambo moja ambalo naliona bora zaid, kwani nilikua na Wafanyakazi ambao niliwaajiri kwa ajili ya kunifanyia kazi kwa kiasi fulani cha pesa, Hivyo siku moja mfanyakazi mmoja akachelewa kuja, na akaja wakati wa mchana, hivyo nikakubaliana nae kumlipa nusu ya malipo ya siku, lakini hata hivyo hadi jioni basi yeye alifanya kazi mara mbili zaid na kuwafikia wale walioanza asubuhi, hivyo nami nikaona ni bora kumlipa kama nitakavyowalipa wengine kwa siku nzima kutokana na Jitihada zake.

‘Ambapo mmoja kati ya Wafanyakazi wenzake alipoona malipo hayo basi akasema Inakuaje unamlipa malipo sawa nasi wakati Yeye amefanya kazi Nusu siku?’

Hivyo mimi nikamjibu Mfanyakazi huyo kwa kumwambia: ‘Hakika mimi sikukudhulumuni nyinyi kutokana na makubaliano yetu na malipo niyokulipeni, na hivyo kuhusiana nae basi mimi nitamlipa kama nitakavyo kwa sababu kazi aliyoifanya ni yangu na pesa ni zangu.’

Hivyo Mfanyakazi huyo akakasirika na kuondoka bila ya kuchukua malipo yake ya siku hio, ambapo nami nikazichukua pesa zake na kuzihifadhi katika sehemu Salama baada ya kupita Mda wakatokea Ng'ombe ambao walikua wakiuzwa, Hivyo nikazichukua zile pesa na kununulia Ng'ombe hao hadi wakawa wengi.

Baada ya mda akaja kwangu Mtu mzima mzee fulani ambae sikuwa nikimjua, Mzee huyo alinifuata na Kuniambia kua alikua akinidai.

Hivyo nami Nikamwambia kua mimi sikumbuki, hivyo hebu nikumbushe ilikuaje?

Ambapo Nae akanielezea ilivyokua, hivyo nami nikakumbuka na kumwambia. ‘Naam..nakumbuka na nimekusubiri sana nikupe malipo yako.’ na hivyo nikampa Ng'ombe wake hao Lakini nae akasema: ‘Ewe Mja wa Allah Usinitanie wala Usinipe Zakkah ya kila mwaka bali nilipe tu kile ninachokudai’,

Nami nikamwambia: ‘Sikutanii wala sikupi Zakkah kwani hii ni Mali yako na mimi sina chochote kutokana nayo.’

Na kisha nikamkabidhi na akachukua: ‘Hivyo Ya Allah kama mimi nifanya hivyo kwa ajili yako basi Tuokoe.’ na Jiwe lililokua Mlangoni likasogea kidogo na wakaona Mwangaza wa Jua.

Na mtu wa pili kati ya Waliofungiwa ndani ya Pango hilo nae akasema: ‘Hakika mimi nilifanya Jambo moja ambalo ni Bora, ambalo ni kua nilikua na Pesa za ziada katika kipindi ambacho Watu walikua wanashida sana, hivyo Mwanammke mmoja akanifuata na kutaka Msaada kutoka kwangu ambapo nami Nikamwambia : ‘La siwezi kukusaidia hadi pale malipo yangu yatakapokua ni Mwili wako.’

Mwanamke huyo akageuka na kuondoka lakini akarudi mara ya pili na kuniomba msaada huku akiwa ni mwenye kuomba kwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na shida yake kua nimsaidie. Lakini na mimi nikamjibu la bila ya mwili wako mimi siwezi kukusaidia, hivyo Mwanamke huyo akaondoka tena.

Na akaenda kumwambia Mumewe kuhusiana nami ambapo nae akasema : 'Kubali ili uiokoe familia yako'. Mwanamke huyo akarudi tena kwangu na kuniomba tena nami nikamwambia kua bila ya mwili wake basi siwezi kumsaidia. Hivyo Mwanamke huyo akajisalimisha kwangu nami nikamkubalia na alipokua chini yangu nami kumfunua basi akaanza kutetemeka nami nikamuuliza Unatetemekea nini ambapo nae akasema kua: Namuogopa *Allah Rabbi Al Alamin.*

Ambapo nami nikasema: Hakika wewe ulikua ukimuogopa wakati ulipokua unamatatizo na mimi sikumuogopa wakati nilipokua na Raha.

Hivyo nikamuacha na kisha nikamlipa pesa alizokua akizihitaji kutokana na kumfunua na kuuona mwili wake, Hivyo ya Allah kama mimi nilifanya hivyo nilivyofanya kwa ajili yako basi nakuomba tuokoe na tatizo hili, na jiwe lililokua Mlangoni hapo likasogea kidogo kiasi ya kua watu hao wakawa wanaonana Sura zao kwa Mwangaza wa Jua.

Na mtu wa Tatu akasema: Hakika mimi nilifanya Jambo bora moja ambalo ni kua nilikua na Wazee wangu wawili ambao ni wazee sana na nilikua namiliki mifugo. Na nilikua na kawaida ya kuwapa Maziwa kila siku ninaporudi malishoni ambapo siku moja Mvua ilininyeshea wakati nikiwa Malishoni na hivyo nikachelewa kurudi hadi Usiku ndio nikawasili Nyumbani, nikawakama Wanyama wangu na kuwawacho bila ya kuwafunga na kuwakimbilia wazee wangu kuwapa Maziwa yao.

Lakini nikawakuta wao wakiwa wameshalala zamani, jambo hili lilinihuzunisha sana kwani nilishindwa kuwaamsha na ilinihuzunisha sana kua sikuweza kurudi kuwafungia vizuri Wanyama wangu lakini hata hivyo nilibakia nimekaa kitako pembeni ya wazee wangu na maziwa yangu hadi ilipoingia Alfajiri

Nikawaamsha Wazee wangu na kisha nikawapa wanywe maziwa yao, hivyo ya Allah Kama mimi nilifanya hivyo kwajili yako basi nakuomba tuokoe na jambo letu hili

Naam..Numan Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: Kwangu mimi ilikua kama namsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa ni mwenye kusema kua Mazingira ya watu hao yalikua kama ya wale waliofunikwa na Mlima lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawaokoa kutokana na Tatizo lao hilo na wakatoka salama'. Hivyo huo ni mtizamo wa Numan Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Watu wa Pangoni.

Na kwa upande mwengine basi aya zinaendelea kufafanua watu hao ni wa aina gani, na ndio maana ikawa kuna mitizamo miwili tofauti kuhusiana na watu wa Pangoni ambapo wa kwanza ni kua Watu watatu kama alivyosema Bishr Ibn Numan Al Ansari *Radhi Allahu Anhu.*

FITYATUN - AS-HAB ALKAHF – VIJANA SHUPAVU WENYE TAQWA WA PANGONI.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kuelezea kwenye aya kwa Kusema:

﴿إِذْ أَوَى ٱلْفِتْيَةُ إِلَى ٱلْكَهْفِ فَقَالُواْ رَبَّنَآ آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَداً﴾

Idh awa alfityatu ila alkahfi faqaloo rabbana atina min ladunka rahmatan wahayyi/ lana min amrina rashadan *(Surat Al Kahf 18:10)*

Tafsir: ***Pale Vijana walipokimbilia Katika Pango Na Kisha (Wakaomba Dua kwa) Kusema Ewe Mola wetu Tupo Kutoka kwako Rehma Na Utuhuishie (Ututilie Nguvu, Ututilie Uhai, Utufanikishie) Jambo letu hili Kiuongofu.***

Ambapo juu ya maneno yasemayo *rabbana atina min ladunka rahmatan basianasema Imam Abu Abd Allah Sahl Al Tustari kua:* **'Maneno haya yanamaanisha kua: Ewe Mola wetu tuingize kwenye Rehma ya kuendelea Kukukumbuka.'**

Hii ni aya ambayo imetumia Neno *Amrina* lenye asili ya Neno *Amara* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Amuru, Kuamrisha, Amri, Kulazimisha Kufanyika kwa kitu kwa Kutumia Nguvu ya Amrisho au Nguvu Ya Hoja Kiufaham.

Neno *Amara* ndio lililotoa neno *Amrun* ambalo hua linamaanisha Jambo Linalotakiwa kufanywa, Kitu kinachotakiwa kufanywa, Uwezo wa Kufanya Kitu au Jambo.

Ambapo tunapoangalia maana hii ya neno *Amara* basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema katika Qur'an kua:

﴿إِنَّ رَبَّكُمُ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَمَاوَاتِ وَٱلأَرْضَ فِى سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ ٱسْتَوَىٰ عَلَى ٱلْعَرْشِ يُغْشِى ٱلَّيْلَ ٱلنَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثاً وَٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ وَٱلنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ أَلاَ لَهُ ٱلْخَلْقُ وَٱلأَمْرُ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلْعَالَمِينَ﴾

Inna rabbakumu Allahu alladhee khalaqa alssamawati waal-ardha fee sittati ayyamin thumma istawa AAala alAAarshi yughshee allayla alnnahara yatlubuhu hatheethan waalshshamsa waalqamara waalnnujooma musakhkharatin bi-amrihi ala lahu alkhalqu waal-amru tabaraka Allahu rabbu alAAalameena*(Surat Al Araf 7:54)*

Tafsir: ***Hakika ya Mola wenu ni Allah, ambae ndie alieumba Mbingu na Ardhi katika siku sita na kisha akakaa juu ya Arshi yake, ni mwenye kuuleta Usiku kwa kuifunika Siku, huku ukiufuatia taratibu bila ya kuucheleweshe. Na yeye ndie alieumba Jua, Mwezi na Nyota zikiwa chini ya maamrisho yake. Kwa Hakika Al Khalq (Uumbaji) ni wake na Al Amru (Amrisho la kua kwa kitu kiwe) ni lake. Utukufu ni wake Allah Mola wa Ulimwengu wote.***

Hii ni aya ambayo imetumia maneno mawili ya *Al Amr na Al Khalq* sambamba kua ni sifa Tukufu za Uwezo Mkubwa na wenye upekee wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ambapo tunapozungumzia kuhusiana na Uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kufanya Jambo au kitu basi hua kunatofauti baina ya Neno *Amr* na neno *Khalq*.

Kwani *Khalq* ni neno lililotokana na neno *Khalaq* ambalo hua linamaanisha Kuumba, Kupima, Kuamua, Kutengeneza Kitu katika hali ya Umbo Fulani, Kufanya Kitu na pia humaanisha kua na Ukarimu.

Hivyo tofauti baina ya *Khalq* na *Amr* ni kua *Khalq* hua ni Sifa ya uwezo wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee wa Kuumba au kufanya kitu kimoja kutokana na asili ya kitu chengine kwa vitendo na *Amr* hua ni Sifa ya uwezo wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* wa kufanya kitu kimoja bila ya kuwepo kitu chengine chochote kwa kauli yaani kwa kuamrisha tu 'Kua' na kitu husika kikawa.

Na hivyo katika kuumba kwake Mbingu na Ardhi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuthibitishia kua hakua ni mwenye kutumia njia ya vitendo yaani *Khalq* tu bali pia alitumia njia ya kauli au Amri juu ya viumbe hivyo ya kua navyo vikawa, aliviita vije mbele yake na vikaja.

Ambapo maneno yote mawili haya hua hayapingani kimaana na asili ya neno *Badiiu* ambalo ndio lililotumika katika ile aya isemayo:

﴿بَدِيعُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ وَإِذَا قَضَىٰ أَمْراً فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ﴾

BadeeAAu alssamawati waal-ardhi wa-idha qadha amran fa-innama yaqoolu lahu kun fayakoonu.*(Surat Al Baqara 2:117)*

Tafsir: ***Muanzilishi wa Mbingu na Ardhi, anapotaka kitu kiwe, hukiambia kua na hua.***

Kwani neno *Badiu* limetokana na neno *Badaa* ambalo hua linamaanisha Kuvumbua Kitu kipya ambacho hakijawahi kufanya hapo kabla, Kuanzisha kitu kipya kabisa kisichokua na mfano wake.

Neno *Badaa* ndio lililotoa neno *Bidaa* kumaanisha Kuanzisha kitu ambacho hakikufanywa hapo kabla kwa maneno au kwa vitendo.

Hivyo neno *Badaa* ndio lililotoa neno *Badiu* ambalo ni sifa Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo humaanisha Kuanzisha Kitu, Kuumba Kitu. Kufanya Kitu kipya cha Upekee bila ya kuhitaji msaada wala kitu chengine chochote.

Na ili tufaham vizuri zaidi maana yake na tofauti yake maneno haya basi na tuangalie mfano wa aya ifuatayo iliyobeba maneno hayo katika kuelezea Maumbile ya Nabii Isa na Nabii Adam kwa kusema:

﴿إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِندَ ٱللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُن فَيَكُونُ﴾

Inna mathala AAeesa AAinda Allahi kamathali adama khalaqahu min turabin thumma qala lahu kun fayakoonu; *(Surat Al Imran 3:59)*

Tafsir: ***Hakika Mithili ya Isa mbele ya Allah ni kama mithili ya Adam, ameumbwa kutokana na Udongo kisha akaambiwa kua na akawa.***

Ambapo hapa tunaona kua neno *Khalaqa* limetumika kuelezea kuanzishwa kwa maumbile ya Nabii Isa kua ni mithili ya Nabii Adam ambae ni mwenye Kuumbwa kutokana na Udongo, ambao ulitumika kuanzisha *(Badaa)* kitu kipya kisichokua na mfano wake kiasi ya kua hata Malaika walishangaa sana walipokiona kitu hicho ambacho ni *Bashar* yaani Umbo la Mwili wa Ibn Adam na kisha baada ya hapo Maumbile hayo ya Kiwiliwili hicho yakapuliziwa Roho ndani yake, lakini bila ya Kua na Sifa za kua ni *Insan* yaani Mtu hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipokiamrisha kua Kiwe Mtu na hapo ndio kikawa Mtu.

Na hii haimaanishi kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakua na uwezo wa kumuumba Ibn Adam au Mbingu na Ardhi n,k kwa kutumia njia ya Amrisho, la. Kwani anao uwezo huo, lakini alifanya Kuumba hivyo kwa kutumia njia ya hatua kwa hatua kwa Hikma ya kutufunza Viumbe wake kutokua na papara n akua a Subra badala yake, kwani Subra ni miongoni mwa Sifa zake tukufu yeye Muumba *Allah Subhanah wa Taa'ala na* yeye mwenye ni mwenye kuwapenda wale Waja wake wenye Subra.

Ambapo tunapoangalia kisa cha watu wa *As-hab Al Kahf* basi tunaona kua ni walikua ni watu wenye kua na Subra pia na ndio maana wakawa ni wenye kumuomba Mola wao yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kutumia maneno katika aya yetu yasemayo: '***Rabbana Atina Min Ladunka Rahmatan wahayyilana Min Amrina Rashadan*** yaani ***Ewe Mola wetu Tupe Rehma Kutoka Kwako itakayolifanikisha Jambo letu hili kiuongofu.'*** Ambayo ni Dua waliyoisoma Watu hawa wa *Al Kahf* kwa ajili yakuomba waingizwe kwenye Rehma ili wapate Hifadhi ya kimwili na Kiroho na uongofu katika jambo lao wenye kuliamini na kulifanya kwa ajili ya Mola wao kua na Subra nalo.

Ambapo maneno haya yenye maombi ya Dua ni Miongoni mwa Dua Muhimu Sana kwa kila Muislam kua ni Mwenye Kutakiwa kuitumia pale anapotaka Kufanya Jambo la Halali, kwani kufanya hivyo hua ni Kuliingiza kwenye Uangalizi kamilifu wa *Allah Subhanah wa Ta'aal* na hivyo hua ni lenye Kua ni lenye Kuelekea kwenye Muelekeo wa kuliingiza kwenye Mafanikio ya Kidunia na Kiakhera Jambo husika na kukunufaisha kiroho na kimwili wewe uliomba.

Hivyo Waislam ni muhimu sana tujitahidi kujizoesha Kudumu nayo Dua hii pale unapotaka kutia nia, unapoanza kupanga au unapoanza kufanya kila kitu chako, mbali ya Kusema *Bismi Allah Rahmani Rahiim*

Kwani Wanasema Wanazuoni kuhusiana na aya zetu hizi mbili za *Surat Al Kahf* yaani aya ya 9 na aya ya 10 iliyotumia neno letu la leo *Amara* katika hali ya Amrina yaani Jambo letu kua:

Al Raqiim ni Bonde la ambalo lipo baina ya *Ghatafan* na *Aylat* katika maeneo ya Karibu na Falestina, na hili ndio lililokua eneo ambalo Pango la watu wa *As-hab Al Kahf* lilikuwepo. Ambao ni Mtizamo wa *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu.*

Ama kwa upande wa Imam Kaab Al Akhbar basi yeye anasema kua**: *'Al Raqiimi* ulikua ndio Mji wao'**

Na Imam Sayyid Ibn Musaayib basi yeye anasema kua**: 'Al Raqiimi ni Kipande cha Jiwe au Fedha chenye Umbo kama la Ubao wa Kuandikia ambacho juu yake kilikua na Majina ya watu wa *Al Kahf.'***

Ama kwa upande mwengine basi Wanazuoni wengi wanakubaliana kua Watu hawa wa *As-hab Al Kahf* walikua wakiishi katika wakati wa baina ya kipindi cha baada ya Wakati wa Nabii Isa Ibn Maryam *Alayhi Salam* Na Kabla ya wakati wa *Al Mustafa Nabii* Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na kuhusiana na Kisa chao basi Imam Abu Is-haq Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Al Nishapuri Ath Thalabi Al Shafii kua: **Katika wakati wa Kipindi cha Mamlaka ya Amir ul Muuminin Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* basi kuna Viongozi wa Mayahudi walimfuata Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na kumwambia kua: 'Umar wewe ndie Msimamizi wa Waislam baada ya kufariki Muhammad na Abu Bakr, hivyo sisi tunataka kukuuliza Wewe Masuali. Na kama ukitubainishia Ukweli wake basi sisi tutakubaliana na Utume wake Muhammad lakini jama ukishindwa basi Tutaukana.'**

Hivyo Umar Ibn Al Khattab akasema: 'Naam ulizeni mnayotaka kuuliza.'

Hivyo Mayahudi hao wakasema: Tuambie Jee Mbingu zinafungwa na nini?

Tuambie Jee ni Kaburi Gani linalotembea na Maiti wake?

Tuambie Jee ni nani alieionya Jamii yake wakati yeye si Ibn Adam wala si Jini?

Tuambie kuhusiana na Viumbe Watano ambao wametembea Ardhini lakini hawakutoka kwenye fuko la Uzazi?

Tuambie Kanga Dume akilia hua anasema nini?

Tuambie Jogoo akiwika hua anasema nini?

Farasi akilia hua anasema nini?

Chura akilia hua anasema nini?

Punda akilia hua anasema nini?

Na Ndege akilia hua anasema nini?

Ambapo baada ya kuulizwa masuali hayo basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akainamisha kichwa chake chini huku akifikiria kwa mda bila ya kupata jibu. Kisha akanyanyua kichwa na kusema: 'Itakua hakuna Kosa kama Umar akiulizwa Suali asilolijua na kisha nae akasema kua Sijui, Na Umar ameulizwa suali ambalo halijui..Hivyo Sijui.'

Hivyo Mayahudi hao wakanyanyuka na kusema: 'Na sisi tunashuhudia kua Muhammad hakua Mtume na Uislam sio Dini ya Haki'

Mayahudi hao wakataka kuondoka, lakini Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* akawaambia: Subirini hapo hapo!

Na kisha baada ya kuamrisha hivyo basi Sahaba Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* akatoka haraka sana kuelekea kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* na alipomkuta basi akamwambia: 'Ya Abu Al Hasan! Haraka sana Uokoe Uislam.'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akauliza: 'Jee kimetokea nini?'

Ambapo Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* akamuaelezea Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* juu ya Yaliyotokea.

Baada ya kusikia yaliyotokea basi Ali Ibn Talib *Radhi Allahu Anhu* akakimbilia haraka sana kwa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahi Anhu,* na mara alipofika tu basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahi Anhu* alinyanyuka kutoka katika sehemu ambayo alikua amekaa na kumsogelea na Kumkumbatia Ali Ibn Talib *Radhi Allahu Anhu huku* akimwambia: 'Samahani Sana ewe Abu Al Hasan kwani unaonekana kua tunakuita kila inapotokea Matatizo.'

Ambapo Ali Ibn Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema : 'Hamna Tatizo' na kisha akawageukia, Naam..niulizeni kila mnachotaka kuuliza kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amenifungulia mimi Milango 1000 ya Ilm iliyotifautiana mmoja baada ya mwengine

Hivyo Mayahudi hao wakauliza kama walivyouliza hapo awali, ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akawaambia kua: Nitakujibuni mimi lakini kwa sharti la kua, kama nikikujibuni kwa kutumia Kitabu chenu cha Taurat basi Mtaingia katika Uislam

Ambapo Mayahudi wakaubaliana na sharti hilo na Kisha Mayahudi hao wakauliza: 'Jee Mbingu hua zinafungwa na nini?'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Mbingu hua zinafungwa kutokana kwa Ushirikina, kwani Mtu au Jamii ikiwa ni yenye Kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Mbingu hua zinafungwa na hivyo hakuna Ovu linaloingia ndani yake'

Mayahudi wakasema: 'Kama ni Hivyo, Jee ufunguo wake ndio Upi?'

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ufunguo wake ni Shahada ya *La Ilaha Illa Allah Muhammada Rasul Allah!'*

Ambapo Mayahudi hao wakaangaliana na kisha wakasema: 'Kijana yuko sahih'

Kisha wakauliza: 'Haya tuambie kuhusiana na Kaburi lililotembea na Mtu wake.'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ni Samaki aliemmeza Nabii Yunus ambae alitembea kwenye Bahari 7 huku akiwa na Nabii Yunus ndani ya Tumbo lake'

Mayahudi wakasema: 'Naam..Haya tuelezee kuhusiana na Yule alieionya Jamii yake wakati yeye si Mtu Wala si Jini.'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ni Sisimizi alietajwa kwenye Kisa cha Nabii Sulayman Ibn Daud *Alayhim Salatu wa Salam* pale aliposema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّمۡلُ ٱدۡخُلُواْ مَسَٰكِنَكُمۡ لَا يَحۡطِمَنَّكُمۡ سُلَيۡمَٰنُ وَجُنُودُهُۥ وَهُمۡ لَا يَشۡعُرُونَ﴾

Ya ayyuha alnnamlu odkhuloo masakinakum la yahtimannakum sulaymanu wajunooduhu wahum la yashAAuroona *(Surat Al Naml 27:18)*

Tafsir: ***Enyi Sisimizi Ingieni Ndani ya Majumba Yenu Ili AsikutimbeniSulayman na Jeshi lake Wakati wao wakiwa hawakuoneni.***

Hivy Mayahudi hao wakuliza: 'Haya Tuambie Kuhusiana na Watano ambao walitembea Ardhini bila ya kuwahi kua ndani ya Fuko la Uzazi.'

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Watano ambao walitembea Ardhini bila ya kuwahi kua ndani ya Fuko la Uzazi, wa kwanza ni Adam na wa pili Hawa, na watatu ni Ngamia wa Nabii Salih, wan nne ni Kondo wa Nabii Ibrahim alieshushiwa alipotaka kumchinja Nabii Ismail na wa tano ni Nyoka wa Nabii Musa.'

Na baada ya kupata jibu kuhusiana na Viumbe watano waliotembea Ardhini lakini hawakuwahi kua ndani ya Fuko la Uzazi basi Mayahudi hao wakaendelea kumuuliza Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu kwa* kusema: 'Tuambie kuhusiana na Kanga Dume akilia hua anasemaje?'

Ali Ibn Abi *Talib Radhi Allahu* Anhu akasema: *'Al Rahman Aala Al Arshi Istawa* - Mwingi wa Rehma Yuko Juu ya Arshi Yake'

Mayahudi Wakauliza : 'Na Jogoo Akiwika?'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Hua anasema *Mkumbeni Allah Subhanah wa Ta'ala* Enyi Mlioghafilika nae.'

Mayahudi wakauliza tena: Na Farasi anapolia hua anasemaje?

Ali Ubn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Wakati Waumini wanapokua kwenye Vita vya Jihadi na Farasi akalia basi hua anasema kua: Ya Allah Wasaidie Waja Wako wanaokuamini Dhidi ya Makafiri.'

Mayahudi wakauliza : 'Jee Punda anapolia hua anasemaje?'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Hua anasema Allah amlaani Mkulima mwenye Kutoza Kodi kwa Ardhi Yake, na hua Wanalia Kwenye Macho ya Shaytan'

Mayahudi wakauliza: 'Na Jee Vyura wanapolia hua wanasemaje?'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Hua Wanasema Shukrani zote anastahiki Mola wangu ambae anaabudiwa kila sehemu hadi Chini ya Maji ya Kina cha Bahari'

Mayahudi wakuliza: 'Na Ndege akilia hua anasema nini?'

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: Hua Wanasema Allah Amlaani anaemchukua *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* na anaeichukia Familia ya watu wa Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam.'*

Mayahudi hawa waliokua wakiuliza masuali haya walikua ni Watu watatu, na hivyo baada ya kujibiwa basi Wawili kati yao wakasema kua: 'Hakika sisi tunashuhudia kua Hakuna Mola anaestahiki Kuabudiwa isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* na *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* ni Mtume wake.'

Ambapo Yahudi wa tatu akasema kumwambia Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Ewe Ali hakika Imani imeingia na kujaa kweli kwenye Nyoyo za wenzangu hawa wawili kutokana na Majibu yako, lakini hali haiko hivyo katika Moyo wangu kwani ingawa Umeingia Imani ya Dini ya Kiislam lakini bado nahisi kua Pengo ambalo halikujaa ndani yake hivyo nitakuuliza Suali moja la Mwisho ili tuangalie itakuaje Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akajibu: 'Usiwe na Khofu endelea Kuuliza Suali lako.'

Yahudi Huyo akasema: 'Ewe Ali Hebu niambie mimi kuhusiana na kisa cha watu wa Zamani ambao walilala kwenye Pango kwa mda wa miaka 309 kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawaamsha watu hao'

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Naam..bila ya shaka nitakuambia Ewe Yahudi kuhusiana na Watu wa Al Kahf, kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewaelezea kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwenye Qur'an kuhusiana nao.'

Kwani baada ya kusema maneno hayo basi Yahudi huyo akasema: 'Umekua ukituambia kuhusiana na uliyokua ukisoma kama uliehifadhi, hivyo kama ni kweli wewe ni mwenye kujua basi tuambie kuhusiana na Majina yao, Majina ya Wazee wao, Jina la Mji wao, Jina la Mfalme wao, Jina la Mbwa wao, Jina la Mlima waliokimbilia, Pango lao na tuambie kisa chao tangu mwanzo hadi mwisho'

Hivyo Ali Ibn Talib *Radhi Allahu Anhu* akakaa vizuri katika sehemu aliyokaa na kisha akamvuta *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwenye Ufahamu na Macho yake na kisha akaanza kwa kusema: 'Ewe Ndugu wa Waarabu, Hakika Kipenzi changu Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam ameniambia mie kua katika Ardhi ya Bezantiyun (Uturuki) kuna Mji ambao Ulikuq Unaitwa Ephesus. Ambapo baada ya Uislam kuwasili basi Mji huo unaitwa Tarsus, lakini katika enzi za Ujahiliyyah ulikua ukiitwa Ephesus.'

'Hivyo katika Mji huo kulikua na Mfalme Muadilifu ambae baada ya mikaa kadhaa alifariki na hivyo habari kuhusiana na kifo chake kikamfikia Mfalme wa Uajemi aitwae Duqyanus. Mfalme Duqyanus alikua ni Mfalme ambae ni Katili na ni Kafiri. Hivyo Mfalme Duqyanus akaliingiza Jeshi lake katika ardhi ya Ephesus na kuuteka Mji huo na kuuweka chini ya Mamlaka yake na kisha akajenga Kasri kubwa sana ndani yake.'

Na baada ya Ali Ibn Talib *Radhi Allahu Anhu* kusema maneno hayo basi yule Yahudi akarukia kwa kusema: 'Kama kweli wewe ni mwenye kujua basi tuelezee kuhusiana na Kasri hilo na Vyumba vyake.' Hivyo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ewe Ndugu zake Mayahudi! Duqyanus alijenga Kasri kubwa sana la Vigae na Vioo lililozungukwa na Ukuta wenye urefu wa Farasang 3 kwa tatu (Kilomita 3 Upana na Kilomita 3 Urefu).'

‘Kasri hilo ndani yake ilikua limesimamia Nguzo 4000 za Dhahabu na Taa 1000 za Dhahabu zenye kuningi'nia ndani yake ambazo zilikua zikiwashwa kila siku usiku huku ndani yake ikiwa kunafukizwa harufu ya mafuta mazuri yenye kunukia. Katika Ukuta wa upande wa Mashariki ya Kasri hilo kulikua na madirisha 180 na kwenye ukuta wa upande wa Magharibi pia, na hivyo ndani ya Kasri hilo kulikua kua Mwangaza wa Jua tangu linapochomza Jua hadi linapotua kupitia katika Dirisha moja baada ya Moja.’

‘Ambapo katikati ya Kasri hilo kuna Kiti kukubwa sana cha Kifalme cha Dhahabu ambacho kimepambwa kwa Vito mbali mbali vya Thamani, Kisha pembeni yake Kiti hicho kulikua kuna Viti vyengine vya Dhahabu na mapambo mengine ambapo vilikua ni 160 ambapo kwa upande wa Kulia vilikaa Viti 80 na kushoto pia 80. Viti hivyo 80 vya kulia vilikua Vikikaliwa na Wakuu wa Makabila ya Watu wake na upande wa Kushoto walikua wanakaa Magavana wake. Na kisha yeye Duqyanus hua anakaa katika kiti chake cha Kifalme kilichopo katikati.’

Kwani baada ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kuelezea kuhusiana na mpangilio wa Viti 80 vya Baraza la Mfalme Duqyanus na yeye mwenyewe basi Yule Myahudi akasema: ‘Ewe Ali hebu tuambie kuhusiana na Kofia ya Kifalme ya Duqyanus.’[

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: ‘Ewe Ndugu yangu, Kofia ya Kifalme ya Duqyanusilikua ni ya Dhahabu yenye miinuko 9 Ambapo kila muinuko umebeba Lulu ambayo ni yenye Kung'ara sana hata katika wakati wa Kiza

Mfalme Duqyanus katika Baraza lake alikua pia ana Vijana 50 ambao ni wenye kutokana na Wakuu wa Makabila ya watu wake na Magavana wake, ambao wote hao walikua ni wenye kuvaa Nguo za Kijani za Hariri huku wakiwa wamejifunga Mikanda myekundu Kiunoni.

Vijana hao 50 walikua pia wamevaa Dhhabu mikononi na Miguuni na pia Mikuki ya Dhahabu na walikua ni wenye kukaa Mbele yake yeye.

Na kisha Pembeni yake kabisa kulikua kuna Vijana 6, Watatu upande wa Kulia na watatu upande wa Kushoto. Hawa walikua ni vijana ambao alikua akiwaamini sana kutokana na Ubora wa Ufahamu wao na hivvyo alikua akisikiliza ushauri wao juu ya kila kitu.’

Kwani mara baada ya kuelezewa Vijana hao 6 basi Myahudi akasema: ‘Tuambie kuhusiana na Majina yao mmoja baada ya mwengine.’

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: ‘Ameniambia Mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Majina ya waliokua katika Mkono wa Kulia ni Tamlikha. Maksalmina na Muhsilmina, Na waliokua katika Upande wa Kushoto ni Martaliyus, Kashtus na Sadaniyus.

Na ilikua ni kawaida ya Mfalme Duqyanus kua kila siku anapokaa kwenye Kiti chake, huku akiwa amezungukwa na Watu wake basi Mlango wa eneo hilo hufunguliwa na kisha huingia Vijana Watatu.

Ambapo mmoja hua na Kikombe cha Dhahabu kilichotiwa Miski, wa pili hua na Kikombe cha Fedha kilichotiwa Marashi na Mwengine hua na Ndege mdogo mkononi, Ambapo wanapofika mbele ya Mfalme Duqyanus basi kijana mwenye Ndege kutoa sauti na hivyo ndege huyo huruka kutoka kwenye mikono yake na kutua kwa kijana wa pili mwenye Kikombe cha Marashi ambapo ndege huyo hutua na kujipaka marashi hayo kwa mabawa yake, na kisha

kijana huyo wa pili hutoa sauti ambayo humfanya Ndege huyo aruke kutoka kwake hadi kwa kijana mwenye kikombe cha Dhahabu cha Miski, ambapo pia hujipaka Miski hio kwa mabawa yake.

Na kisha kijana huyo wa tatu hutoa sauti ambayo humfanya Ndege huyo aruke kutoka kwenye Kikombe cha Miski na kukimbilia kwenye Kofia ya Kifalme ya Duqyanus na hivyo hua ni mwenye kutua juu ya Kichwa cha Duqyanus ambapo hujikunuta na kumwagia Mfalme Duqyanus mafuta mazuri ya Miski na Marashi ya Mawardi.

Mbali ya kua Mfalme Duqyanus alikua ni mwenye Nguvu ya Kijeshi lakini pia Duqyanus alikua ni mtu mwenye kujaaliwa Uzima wa Afya na mwili wenye Nguvu. Naam..bila ya shaka kama kawaida ya Ibn Adam anapojaaliwa na sifa kama hizi basi hua pia na hali kama zisemavyo aya:

﴿كَلَّآ إِنَّ ٱلۡإِنسَٰنَ لَيَطۡغَىٰٓ ۞ أَن رَّءَاهُ ٱسۡتَغۡنَىٰٓ﴾

Kall<u>a</u> inna al-ins<u>a</u>na laya<u>t</u>gha; An ra<u>a</u>hu istaghn<u>a</u> *(Surat Al Alaq 96:6-7)*

Tafsir: ***Hakika Ibn Adam hua ni mwenye kuvuka mipaka. Anapojiona kua anajitosheleza.***

Hivyo kutokana na Kujiona kua ana Ufalme Mkubwa, Jeshi Kubwa, Mali Nyingi, Afya na Nguvu basi Duqyanus akaanza kujiona kua hakuna kama yeye..kwani anajitosheleza!

Allah Subhanah wa Ta'ala **akamjaalia Mfalme Duqyanus akatawala ardhi ya Ephesus kwa mda wa Miaka 30 bila ya kuumwa hata na kichwa.**

Na hivyo akaanza kujitangazia kua yeye ndie Mungu na kuanza kutaka watu wake wawe ni wenye kumuomba maombi yao na kumsujudia, ambapo kila anaekubaliana nae basi humnyooshea mambo yake kutokana na Neema alizojaaliwa na Mola wake kwa ajili ya kunufaisha matamanio ya Nafsi yake. Na kila asieukubali Uungu wake basi na kutomtii basi adhabu yake Hua ni Kifo.

Mfalme Duqyanus aliendelea kudumu katika hali hii ya Udhalimu na ukatili kwa mda wa miaka kadha, hadi pale siku Moja alipopokea Habari kua kuna Jeshi kubwa sana linataka kuuvamia Utawala wake.

Habari hizi zilimshtua sana na kumhuzunisha kwani alikua akijua kua tayari Mamlaka yake yanahatarishwa na maadui zake hao. Hivyo akainamisha kichwa chake kwa huzuni na kwa mara ya kwanza basi kofia ya Kifalme aliyokua akiivaa ikamuanguka kutoka Kichwani mwake, jambo ambalo lilimshtua zaid kiasi ya kua khofu yake hio ilimpelekea kuishiwa na nguvu na hivyo yeye mwenyewe kuanguka chini kutoka kwenye kiti chake.

Kutokana na tukio hilo basi Kiongozi wa wale Vijana 6 wanaomzunguka Duqyanus na kusaidiana nae mawazo na maamuzi juu ya kila kitu ambae alikua akiitwa Tamlikha akatafakkar na kuanza kujiuliza kwa kusema: **'Ah..Hivi kama Duqyanus atakua ni Mungu kweli, kama anavyojidai basi kwanini leo hii akaanguka kwa Khofu? Hivi Mungu hua anakua na Khofu kweli? Kama ni Mungu kweli mbona anakula, anajisaidia. Analala n.k? Kusema kweli hizi alizokua nazo Duqynus si sifa za Kiungu, hivyo hawezi kua ni Mungu'**

Hivyo masuali haya yasiyokua na Majibu yalimuumiza kichwa Tamlikha kiasi ya kua katika siku hio waliporudi Vyumbani mwao ambapo kabla ya kulala basi hua wanakaa pamoja na kula chakula cha Usiku, lakini katika siku hio Tamlikha hakuweza kula kwa masuali aliyokua nayo akilini mwake. Hivyo wenzake wakamuuliza anaumwa au imekuaje?

Ambapo Tamlikha akasema: **'Hakika mimi nimekua nikifikiria kuhusiana na Mbingu na kumfikiria yule ambae amezisimamisha na kuzitandaza kama Paa Mbingu hizo bila ya kuwepo na Nguzo, Nimekua nikimfikiria yule ambaendie anaevitoa Jua na Mwezi kutoka upande wa Mashariki kisha akavizamisha Upande wa Magharibi Yule ambae ndie alizipamba Mbingu kwa Nyota Na pia nikamfikiria yule ambae ndie alieitandaza Ardhi tuliyokua sisi juu yake, na kuisimamisha Milima Juu yake na kuizungushia Bahari pembeni yake ili itulie.'**

'Na kisha nikajifikiria mimi mwenyewe, namna nilivyokua nilippkua Tumboni mwa Mama yangu, mpaka nikazaliwa na kufikia hadi hii leo kunilea na kua hivi nilivyokua na nimeona kua Kuna Muumba ambae ndie Mungu na wala si Duqyanus.'

Hivyo Vijana watano waliobakia nao waliposikia maneno hayo basi wote wakamkumbatia Tamlikha na kumwambia kua**: 'Na sisi sote pia tumekua tukijiuliza masuali hayo hayo. Lakini hatujui tufanye nini, Hivyo jee Tamlikha tufanyeje?'**

Tamlikha akajibu: **'Enyi Ndugu zangu ukweli ni kua hakuna njia nyengine isipokua kukimbia na kujiokoa kutoka chini ya Mamlaka ya Duqyanus kumkimbilia Mola wa Ulimwengu wote'**

Hivyo Tamlikha akawaambia wenzake hao Watano ambao ni Maksalmina, Muhsilmina, Martiliyus, Kashtus na Muhsilmina kua: **'Enyi Ndugu zangu ukweli ni kua hakuna njia nyengine isipokua kukimbia na kujiokoa kutoka chini ya Mamlaka ya Duqyanus kumkimbilia Mola wa Ulimwengu wote**

Kisha Vijana hao 6 Wakakubaliana juu ya maamuzi hayo ya Kuuhama Mji wa Ephesus kwa ajili ya Kuinusuru Imani yao na kujisalimisha chini ya Allah Subhanah wa Ta'ala. Kisha Tamlikha akatoka na kuenda Kununua Tende ambayo itakayowasaidia Njiani katika Safari yao hio ya kumkimbia Mfalme Duqyanus.

Na kisha Usiku wa Siku hio hio hawakulala bali waliamua kuanza Safari yao kuukimbia Mji huo.

Hivyo Wakapanda Farasi wao na kuanza Safari hadi walipofika masafa ya Kilomita 3 nje ya Mji huo wakasimama na kisha Tamlikha akasema: 'Enyi Ndugu zangu, bila ya shaka Mfalme wa Kidunia ameshaachana nasi na hivyo Mamlaka yake juu yetu yameshakatika, hivyo Tushuke kutoka kwenye Farasi wetu kisha tutembee kwa miguu ili Mungu Muumba Ulimwengu na kila kilichomo ndani yake apate kutuongoza

Hivyo Watu hao wakashuka kuoka kwenye Farasi wao na kisha wakaanza kutembea kwa miguu kwa masafa ya Kilomita zaid ya 7 hadi wakaanza kuhisis Maumivu kwenye miguu yao, kwa sababu hawakua ni watu waliozoea kutembea sana kwani walikua ni watu waishio ndani ya Kasri la Duqyanus tu miaka yote.

Katika safari yao hio mara wakakutana na mchungaji Kondoo ambae walimsalimia na kumuomba awasaide Maziwa. Na bila ya shaka Mchungaji huyo aliwakamua Kondoo wake Maziwa hayo nao Wakanywa na kula na Tende zao na wakati wamekaa wanakula basi

Mchungaji akawauliza kwa kusema: 'Hakika Nyinyi hamuonekani kua ni Wasafiri wa kawaida, kwani Sura zenu na Miili yenu inaonesha kua kama ni watu waliokua wakitoka kwenye Familia za Watu waliokua Juu Kidarja yaani kama Mnatoka kutoka kwenye Kasri la Mfalme. Ila sasa inaonekana pia kua Safari yenu sio rasmin yaani mnaonekana kua kama ni watu Mnaokimbia kitu, Hivyo Jee kimekukuteni nini?'

Tamlikha akasema: 'Naam..hakika sisi Tumetoka katika Imani isiyokua sahih na tunakimbilia kwenye Imani iliyokua Sahih ambayo haitutaki kusema uwongo, hivyo itabidi tukwambie ukweli kama ukweli huo utatusaidia.'

Mchungaji huyo akasema: 'Naam..inaonekana kua habari zenu zinavutia hivyo bila ya shaka Ukweli wenu utakusaidieni.'

Hivyo Tamlikha akaelezea yaliyotokea tangu mwanzo hadi mwisho na baada ya kumaliza kuelezea basi Mchungaji huyo akawainamia na kuwaomba kua na yeye anataka kua pamoja nao katika safari yao na kusema: 'Mnayoyaona nyie ndio niyaonayo mie hivyo nakuombeni nisubirini niwakabidhi Wanyama hawa kwa Mwenyewe na kisha nitarudi ili tuendelee pamoja na safari hii.'

Hivyo Mchungaji huyo akaondoka na kisha baada ya mda akarudi huku akiwa anafuatwa na mbwa wake.

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alipomtaja Mbwa basi Yahudi akasema: Ewe Ali, kama wewe ni mwenye kujua basi tuelezee kuhusiana na Mbwa huyo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Mbwa huyo alikua ni mwenye Weusi na Weupe na jina lake ni Qitmir.'

Ama Wanazuoni wametofautiana kimtizamo kuhusiana na Mbwa huyo ambapo *Bahr Al Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kua Mbwa huyo alikua na Mabaka Mabaka. Kwa Upande wa Imam Muqatil Ibn Sulayman basi yeye ansema kua Mbwa huyo alikua ni mwenye Rangi kama ya Manjano.

Na kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Kaab basi anasema kua Mbwa huyu alikua ni mwenye Rangi Manjano inayokaribia wekundu yaani kama Orange. Ama kwa upande wa Imam Abd Rahman Al Kalbi basi yeye anasema kua Mbwa huyu alikua ni Mweupe.

Kwani Wanazuoni pia wametofautiana kuhusiana na Jina lake pia kwani kuna Wasemao kua Sayyidna Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allah Anhu* hakusema kua Mbwa huyu alikua akiitwa Qitmir ambao ni mtizamo pia wa *Bahr Al Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* bali alisema kua Mbwa huyu alikua akiitwa Rayyan.

Ambapo kwa upande wa Imam Shuayb Al Jubai baso yeye amesema kua Mbwa huyu alikua akiitwa Hamra.

Na kwa upande wa Imam Ibn Fathawayh basi yeye amesema kua Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit amesema kua Mbwa huyu alikua akiitwa Qitmur. Na pia kuna wanaosema kua alikua akiitwa Qitfir.

Naam, kuna baadhi wanaweza wakajiuliza hivi kwanini Wanazuoni wakawa wanamzungumzia mnyama Mbwa ambae ni Mnyama asiekua nadhifu na asiekua na umuhimu basi jibu lake tutalipata baadae katika Aya kwani aya zimemzungumzia Mbwa husika katika kisa hiki.

Hivyo kwa Upande wa Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kuhusiana na Majina ya Watu hao na mbwa wao kua**: 'Mimi ni Miongoni mwa wenye kujua juu yao kwani watu hao walikua ni Tamlikha, Maksalmina, Martaliyis, Baynus, Sawamus na Dawanus Na kisha akaongezea Kashtus ambae ndie aliekua Mfugaji Kondoo akiwa pamoja na mbwa wake aitwae Qitmir'**

Baada ya Tamlikha na wenzake kua ni wenye kumsubiri Kashtus ambae ni yule Mfugaji aje kujiunga nao na kisha Mfugaji huyo akatokea huku akiwa anafuatwa na Mbwa wake, basi kina Tamlikha wakashtuka walipomuona mbwa huyo. Na hivyo wakaamua kumfukuza, na kukataa kufuatwa nae kwani walikua wanakhofu kua huenda akawa ni mwenye Kubweka njiani na kisha akawasaliti pale watakapokua wakitafutwa na kuwabidi kutotoa sauti na na kukaa kimya na hivyo kutokana na kubweka kwake mbwa huyo kunaweza kuwapelekea kukamatwa.

Hivyo Wakampopoa Mawe mbwa huyo ili akimbie lakini Mbwa huyo alipoona anapogwa mawe basi alisimama na kisha akasema kwa sauti yenye kufahamika na watu hao yenye kutoa maneno yasemayo kua: **'Enyi Watu Nakuombeni Msinifukuze, kwani mimi ni kama nyinyi naamini kua hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo niacheni niwe pamoja nanyi kwani nitakua nakulindeni kutokana na maadui zenu, kisha nami nitapata radhi za *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Ambapo hayo yalikua ni maneno yenye kuwashangaza kina Tamlikha kwani hawakiyategema hususan kutoka kwa kiumbe ambae ni Mbwa.

Hivyo wakamuachia na hivyo mbwa huyo akawaongoza, hadi wakafika kwenye Mlima ambapo wakamfuata Juu ya Mlima huo na kisha wakaona Jabali kubwa mbele yao na walipopanda juu yake basi ghafla wakakutana na Pango kubwa ambalo waliamua kuingia na kupumzika ndani yake.

Baada ya kuingia ndani yake basi wakaamua kua Wajihifadhi ili wapumzike kabla ya kuendelea na Safari yao. Katika kuangalia kwao mazingira ya Pango hilo basi wakaona Mlangoni mwake kuna Mti wenye Matunda yanayolika na pia kuna Chemchem ya Maji.

Hivyo wakala Matunda hayo na kisha wakanywa Maji hayo na kisha wakaomba dua kwa kusema kama zilivyosema Aya:

﴿رَبَّنَآ آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَداً﴾

Rabban<u>a</u> <u>a</u>tin<u>a</u> min ladunka ra<u>h</u>matan wahayyi/ lan<u>a</u> min amrin<u>a</u> rashad<u>a</u>n *(Surat Al Kahf 18:10)*

Tafsir: ***'Ewe Mola wetu Tupo Kutoka kwako Rehma Na Utuhuishie (Ututilie Nguvu, Ututilie Uhai, Utufanikishie) Jambo letu hili Kiuongofu.'***

Ambapo baada ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kuelezea hayo basi Yahudi akauliza kwa kusema: ' Ewe Ali, Hebu Tuambie kuhusiana na Jina la Mlima huo na Jina la Pango hilo.'

Hivyo Ali Ibn Abi *Talib Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ewe Ndugu wa Mayahudi. Jina la Mlima huo ni Najalus na Jina la Pango hilo ni Al Wasid ambapo baadhi wanasema kua Pango hilo linaitwa Khayram.'

Kwani baada ya Vijana hao na Mbwa wao kuomba Dua hio ya kutaka Hifadhi itokanayo na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'aala* juu yao na kuomba Uongofu kutokana na Fadhila zake *Allah Subhanau wa Ta'ala* juu yao katika kuitafuta njia ya Haki.

Basi Vijana hao wakajikuta katika hali ya kua Jua limeshatua hivyo na wao wakaamua bora Walale wapumzike ili wakiamka kesho yake basi wawe katika hali nzuri zaid isiyokua na uchofu wa Miili yao. Hivyo kila mmoja akatafuta Sehemu nzuri akajinyoosha huku Mbwa wao akiwa amekaa Mlangoni mwa Pango hilo huku Miguu yake ikiwa imeuelekea Mlango wa Pango hilo.

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anakielezea kile kilichofuatia baada ya Watu hao kuingia ndani ya Pango hilo na kupumzika katika aya iliyotumia neno *Dharaba* Ambapo ni miongoni mwa maneno ye ye maana kubwa na Nyingi na Tofauti katika Lugha ya Kiarabu.

Kwani neno *Dharaba* hua linamaanisha Kuponya, Kupiga Kipigo Kikubwa Au Kupiga Dharuba, Kuonesha Mfano. Kutoa Kigezo, Kumithilisha, Kufunga Safari, Kusafiri, Kujikinga, Kufunika, Kuhifadhi, Kulinganisha, Kuchukua Kitu, Kupigana, Kuchanganisha Vitu vingi kwa pamoja ili Kugawana Malipo makubwa zaid hapo baadae, Kuachia Kitu kilichozuiliwa n.k

***Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema katika aya hio kua:**

﴿فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي ٱلْكَهْفِ سِنِينَ عَدَداً﴾

Fadharabna aAala Adhanihim fii Al Kahfi Siniina aAdadan *(Surat Al Kahf 18:11)*

Tafsir: ***Hivyo Tukayafunika na Kuyaziba Masiko yao kihisia Wakiwa Ndani ya Pango Kwa Idadi ya Miaka mingi.***

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema katika Qur'an kuhusiana na watu wa *As-hab Al Kahf* pale walipoinga ndani ya Pango hilo na kuamua Kuomba Hifadhi na Uongofu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya Jambo lao na kisha wakapumzika kua aliyaziba Masikio yao kwa miaka Kadhaa.

Na anasema Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakashari kua: **'Aya inamaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliwashushia, Usingizi mzito Sana, usingizi ambao uliwapelekea Watu hao kua ni Wasiokua na hisia za Kusikia na hivyo hawakuweza kusikia Sauti ya Kitu chochote.'**

Naam..bila ya shaka Imam Al Zamakshari hakukosea na ni kwa Sababu Kimaumbile Mwili wa Kila Ibn Adam kutokana na Ukamilifu wake ambao ni wenye sifa ya kua na *Ahsanan Takwimin*. Basi unapolala hua ni wenye kupunguza kasi ya Ufanyaji kazi wa Kila Kiungo chake ndani yake na kwa baadhi hua ni vyenye kusita kabisa kufanya kazi katika wakati wa Usingizi hii ni kwa sababu Usingizi ni neema muhimu sana anayoihitaji kila Kiumbe hususan Ibn Adam kwa ajili ya kupata Utulivu, Kuwezesha kukua kwa viungo vya Mwili wake, kwani katika wakati unapopata Usingizi basi mwili wako huzalisha Kemikali za Serotonin, Epinephrine n.k ambazo hua ni zenye kuujenga Upya Mwili

kinguvu na kuuimarisha kiafya kwa ajili ya Kukabiliana na heka heka za kuendeleza malengo ya Maisha yetu katika siku inayofuatia ya Uhai wetu hapa Duniani na si katika nguvu za kufanyia kazi tu bali pia katika nguvu na uwezo wa kuendeleza vizazi yaani kuingiliana kimwili.

Hivyo unapokosekana usinginzi basi Mwili hua unakosa pia kujijenga na kujiimarisha kiulinzi kiasi ya kua inakua kuna uwezekano mkubwa sana wa kukusababishia maradhi ya Saratani kiasi ya kua shirika la Afya Ulimwenguni limeweka wazi kua Miongoni mwa sababu kuu za kuongezeka kwa Maradhi ya Saratani ikiwemo Saratani ya Tumbo, Tezi Dume, Saratani ya Maziwa n.k basi ni kukosekana kwa Usingizi hususan kwa wanaofanya kazi za usiku.

Na pia Usingizi hua ni wenye Kuutia Nguvu na kuurutubisha na kuunawirisha Ubongo na Ufaham wa Ibn Adam kwa kumuondolea na kuzifuta kumbukumbu zote za Taswira na Maneno zisizokua na maana na kutohitajika zililizohifadhiwa ndani yake kutokana na Matukio ya Siku nzima. Hivyo ukweli ni kua Usingizi ni Silaha ya Mwili na hivyo kila Mmoja wetu anatakiwa awe ni Mwenye kuitumia kwa ajili ya Manufaa yake.

Ambapo anasema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwita Uthman Ibn Mazhum na alipofika mbele yake basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ewe Uthman, hivi jee hutaki kushikamana na Sunnah Yangu?' Uthman Ibn Mazhum akasema: 'La, *Ya Rasul Allah!* Wallahi mimi ni mwenye kutafuta njia za kufuata Sunnah zako.'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kwa Hakika Mimi hua nalala, na nnasali, Nnafunga na nnafungua na nnaoa Wanawake. Hivyo Muogope *Allah Subhabah wa Ta'ala*, Ewe Uthman kwani Familia yako ina haki juu yako,wageni wako wana haki juu yako, kwa hakika hata Nafsi yako in haki yake juu yako, hivyo Funga na ufungue, Sali na Ulale pia' *(Sunan Abu Daud.)*

Katika hadithi nyengine pia katika Sahih Bukhari ambapo kuna Mwanammke alienda kushtaki kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Mumewe ni mwenye kufunga kila siku na ni mwenye kusimama kusali usiku kucha kila siku ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwita Sahaba wake huyo ambae ni Abd Allah Ibn Amr Ibn Al As *Radhi Allahu Anhu* na kumuuliza: **' Ewe Abd Allah Hivi jee ni kweli wewe ni mwenye kufunga kila siku na kusali usiku kucha kama nilivyosikia?'** Abd Allah Ibn Amr Ibn Al As *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Naam ni kweli.'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: **'Hutakiwi kufanya hivyo, bali funga kwa baadhi ya siku, fungua kwa baadhi ya siku, amka usali katika Usiku na pia Lala katika wakati wa Usiku, kwani Mwili wako una haki juu yako, Macho yako yana haki juu yako, Mke wako ana haki juu yako.'** *(Sahih Bukhari.)*

Hivyo Moja kati ya Haki za Mwili wako juu yako Ibn Adam ni Usingizi yaani Kuupumzisha. Na ndio maana *Hujjat Ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhamamd Ibn Muhamamd Ibn Muhammad Al Ghazali akasema kua Mtu unatakiwa ulale kwa masaa manane kila Siku.

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتاً﴾

WajaAalna Nawmakum Subatan *(Surat An Nabaa 78:9)*

Tafsir: **Tumejaalia Kulala kwenu Usingizi kua ni Kitu cha Mapumziko**

Naam, hayo ni maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Usingizi, na uthibitisho wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia Mtizamo wa *Hujjat Ul Islami* Imam Abu Hamid Muhamamd ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali kuhusiana na Usingizi, kwani kwa kila Ibn Adam basi kutopata Usingizi hua kuna madhara makubwa sana kwa Afya yake, Ufahamu wake na Muonekano wa Sura na Mwili wake.

Kwani kukosa Usingizi wa Kutosha humpelekea Ibn Adam Husika kua ni mwenye kua na Maradhi ya Kukoka Umakini, Kusahau, na kutoweza kuhifadhi mambo mapya ndani ya ufahamu klwani yaliyomo hayajapungua kutokana na kukosekana kwa usingizi, na hivyo kukuletea hali ya kukosa utulivu na kua na Hasira. Kukosa Usingizi wa kutosha kunasababisha Maradhi ya Kisukari, kupungua kwa uzito wa mwili kwa baadhi na pia kuzidi kwa uzito wa mwili kwa baadhi, Maradhi ya Moyo na Shinikizo la Damu, kwani unapolala basi Moyo wako hua ni wenye kupunguza kasi ya kufanya kazi na presha ya Damu hushuka na Pampu ya Moyo hua ni yenye kupumzika kwa kupunguza kasi ya kupiga kwake katika kuzungusha damu na Matatizo ya Kisaikolojoa na Akili.n.k

Ambayo yote hayo hutokana na kukosekana kwa Mapumziko stahiki ya Mwili ya Kimaumbile ambako kukosekana kwake hupelekea kupanguka kwa Mifumo yote ya Ufanyaji kazi ya ndani ya Mwili wa Ibn Adam ambapo athari zake huanza kuonekana pale mtu anapokosa usingizi kwa mda wa masaa 16, kwani hali hio huupelekea mfumo wa Damu wa Ibn Adam husika ambao ndio mfumo mkuu unaosimamiamifumo yote ya ufanyakazi ndani ya mwili kua ni sawa na mfumo wa Mtu mwenye Kilevi ndaniya Damu yake kwa asilimia 0.05%, ambayo hii nihali ambayo tayari Ib Adam hua huruhusiki kuendesha Chombo cha Moto. Hivyo Usingizi ni Silaha yako Ewe Muislam mwenzangu na hivyo itumie kuulinda Mwili wako.

Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua : '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Muumini mwenye Nguvu (Kiimani na Kiafya) ni bora Kuliko Muumini aliekua Dhaifu, inagawa kuna wema kwa wote, hivyo shikamana na kile kitakachokunufaisha na omba msaada wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wala usijihisi kua ni mtu usiekua na msaada, na kikikufika kitu chochote basi usiseme: 'Ya laiti kama ningefanya hili na hili basi ingekua hivi na hivi' kwankusema hivyo hua ni kwenye kumfungulia njia Ibilisi**.*(Sahih Muslim)*

Ambapo kwa upande mwengine basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua Tukawaziba Masikio yao wakati wakiwa ndani ya Pango kwa miaka Kadhaa. Hiyo hivi kwanini *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kuhusiana na Kuziba Masikio? Kwanini asiseme kua na Tukawaziba Macho yao? Au asiseme kua na Tukawaziba Pua zao? Lakini amesema Tukawaziba Masikio yao.

Naam..hii ni kwa sababu Ibn Adam anapolala basi Viungo vyake vyote vya hisia hua ni vyenye Kupumzika na hivyo vile vyenye kufanya kazi hua vinafanyakazi kwa sababu ya Umuhimu wake katika Kuulinda Mwili wa Ibn Adam.

Hivyo ili Mtu alale basi humbidi kufumba Macho, lakini hata hivyo wakati mtu huyo yuko hai basi humbidi kuvuta pumzi kwa kutumia Pua yake. Na ingawa Pua hua ina kazi kadhaa kwenye mwili wa Ibn Adam lakini in kazi kuu ni Mbili ambazo ni Kusaidia Mfumo wa Uvutaji hewa na pia kusaidia Mfumo wa Chakula katika kuhisi Ladha ya Chakula kutokana na Harufu na hivyo kuhisi juu ya kile kinachoingizwa Mdomoni kua kinafaa kuliwa ama la, kama ni kizuri ama ni kibaya.

Hivyo basi Wakati tunapolala basi Mfumo wa Hewa hua unafanya kazi lakini Mfumo wa Kuhisia Harufu hua unazima na kukata mawasiliano na Ubongo na hivyo hua haufanyi kazi moja kwa moja kama ufanyavyo katika wakati ambao tukiwa tuko macho.

Ambapo Mfumo wa Pua pia hua ni wenye kutusaidia katika kuhisi kwa Kunusa hali ya mazingira na kujua kua uko katika Hali ya Hatari ama ya salama ambao hata hivyo hua hauna nguvu pale tunapolala na hivyo hua ni vigumu kutusaidia kutuamsha pale inapotokea hatari inayoweza kuhisikana kwa njia ya Harufu, kama Moto, Moshi au Hewa ya Sumu n.k.

Lakini kwa upande wa Viungo vyengine basi hisia hizi za kuhisi hali ya Hatari pia hua zinapatikana katika kiungo cha Hisia cha Kusikilizia yaani Sikio.

Ambapo tunapozungumzia kuhusiana na hisia za Sikio basi hali hua ni Tofauti kabisa na Viungo vyengine vya hisia, kwani sikio hua ni lenye kusikia kutokana na Mtetemeko wa Hewa ambao unapotokea kulingana na kusababishwa na kitu fulani basi Masikio yetu hua ni yenye kusafirisha hisia hio hadi kwenye Ngoma ya Sikio ambayo nayo huisafirisha hadi kwenye Ubongo ambao nao huitafsiri Sauti hio kutokana na rekodi za sauti zilizohifadhiwa ndani yake. Na kisha kubainisha kua ni Sauti ya Nini na kama ni ya Hatari ama la.

Na kama si ya hatari basi Mwili uidharau sauti hio lakini kama ni ya hatari basi Mwili huchukua hatua ya kuupa habari Moyo ambao nao huongeza kasi ya Mapigo kwa ajili ya Kuzalisha kemikali ya Cortisol ambayo huutayarisha Mwili kua katika hali ya kua na hadhari ya kuchua hatua stahiki Itakayofuata kutokana na mazingira husika kama kukabiliana nayo au kujihami au kuikimbiia hatari ili kuuokoa Mwili dhidi ya Madhara ya Hatari hio.

Hivyo kutokana na Umuhimu wake basi Ubongo hua hauisitishi hisia ya Kusikia Sauti kupitia kwenye sikio, kwani hua unaendelea na Ufanyaji kazi wake katika wakati tunapolala ingawa hua unazichuja Sauti husika kulingana na Umuhimu wake.

Na ndio maana inakua vigumu sana Mtu kuweza kulala pale inapokua kuna zogo au sauti kubwa katika sehemu husika, kwa sababu mwili hua unakua hauna utulivu bali hua uko katika hali ya tahadhari na matayarisho ya kuchukua hatua kulingana na Sauti husika.

Kisa pia kinatuonesha kua Watu hawa pia walikua na Mnyama aina ya Mbwa. Na tunapozungumzia mnyama Mbwa basi tunaona kua ni Mnyama mwenye Hisia kali sana za Kusikia sauti kwani hua anaweza kusikia sauti kwa mara 4 zaid ya Ibn Adam. Na hivyo katika hali waliyokua nayo Watu hawa wa *As-hab Al Kahf* na hususan Mbwa wao, basi kimaumbile ilikua vigumu kwao wao kulala katika hali waliyolala huku Hisia za Masikio yao zikiwa zinafanya kazi.

Ingawa bila ya shaka tunakubaliana kua mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kila kitu kinawezekana kutokana uwezo wake na hivyo anaweza kuwalaza na wakalala kwa miaka yote hio bila ya hata kuwaziba masikio yao. Lakini ametaja kuzibwa kwa hisia zao za kusikia kupitia kwenye Masikio ili tupate kutafakkari umuhimu wa hisia za Kusikia na umuhimu wa viungo vya Masikio Katika Miili yetu na pia Uwezo wake *Allah Subhana wa Ta'ala* katika kuwapa hifadhi wale wanaokimbilia Hifadhi yake.

Na kwa upande mwengine tunapoaiangalia aya hii basi tunaona kua katika aya hii pia imezungumzia kipindi cha Wakati cha Miaka kwa kutumia neno *Siniina* lenye kutokana na neno *Sanah* pale iliposema:

﴿ فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي ٱلْكَهْفِ سِنِينَ عَدَداً﴾

Fadharabna aAala Adhanihim fii Al Kahfi Siniina aAdadan *(Surat Al Kahf 18:11)*

Tafsir: ***Hivyo Tukayafunika na Kuyaziba Masiko yao kihisia Wakiwa Ndani ya Pango Kwa Idadi ya Miaka mingi.***

Ambapo ingawa neno *Sanah* kimaana hua linaainisha Kipindi cha Wakati katika hali ya Miaka kama vile pia lilivyo neno *A'ama* ambalo hua linaainisha Kipindi cha Wakati katika Hali ya Miaka, kama namna yalivyotumika maneno hayo sambamba katika aya moja pale iliposema Qur'an katika Kisa cha Nabii Nuh kua:

﴿وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحاً إِلَىٰ قَوْمِهِ فَلَبِثَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلاَّ خَمْسِينَ عَاماً فَأَخَذَهُمُ ٱلطُّوفَانُ وَهُمْ ظَٰلِمُونَ﴾

Walaqad arsalna noohan ila qawmihi falabitha feehim alfa sanatin illa khamseena AAaman faakhadhahumu alttoofanu wahum *dh*alimoona. (*Surat Al Anqabut 29:14)*

Tafsir: ***Na kwa hakika tulimtuma Nuh kwa watu wake na akakaa pamoja nao miongoni mwao kwa miaka 1000 ila (toa) miaka 50 (akiwausia kumuamini Mungu mmoja na kutomshirikisha) na wakakumbwa na Tufani wakati wakiwa ni miongoni mwa walio madhalim.***

Ambapo Aya hii tunaona kua imeainisha Miaka 1000 kwa kutumia neno *Sanah* Kama lililotumika katika Aya yetu inayozungumzia Hali ya *As-hab Al Kahf* katika Kuzibwa kwao Masikio yao.

Na pia ikatumia neno *A'ama* kuainisha Miaka 50 kati ya 1000 aliyoishi Nabii Nuh pamoja na Watu wake.

Ambapo tunapoayaangalia maneno mawili haya ambayo ingawa kwa upande mmoja hua ni yenye maana moja lakini kwa Ama kwa upande *Allamah* Raghib Al Isfahan basi yeye anasema kua: **'Kimaana neno *Aám* ni sawa na neno *Sanah,* isipokua neno *Sanah* hua mara nyingi linatumika kumaanisha mwaka ambao una shida na matatizo au ukame ndani yake na ndio maana Ukame ukawa unaitwa *Sanah,* neno *Aám* hua linatumika kumaanisha mwaka ambao ndani yake mna utulivu na neema kama tunavyoona pale Allah *Subhanah wa Taála* aliposema katika *Surat Yusuf*:**

﴿ثُمَّ يَأْتِي مِن بَعْدِ ذَٰلِكَ عَامٌ فِيهِ يُغَاثُ ٱلنَّاسُ وَفِيهِ يَعْصِرُونَ﴾

Thumma ya/tee min baAAdi dhalika AAamun feehi yughathu alnnasu wafeehi yaAAsiroona *(Surat Yusuf 12:49)*

Tafsir: Na kisha utakuja baada ya hapo mwaka ambao watu watanufaika na mvua ya kutosha ambapo watakamua (ndani yake mvinyo na mafuta)' *(Surat Yusuf 12:49) (Allamah Raghib al-Asfahani Mufradaat Alfaaz al-Qurán 2/140)*

Ambapo hii ilikua ni kuhusiana na Namna Nabii Yusuf alipotabiri Ndoto ya Mfalme kuhusiana na Miaka 7 ya Mavuno na Miaka 7 ya Ukame.

Ama Imam Abu Hasan Ibrahim Ibn Umar Burhaan ad Din al Biqaa'i Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Neno *Sanah* hapa hua limetumika kuelezea maana mbaya ya siku za *Kufr* na *Aám* hapa hua limetumika kuelezea kua baada ya kukufuru kwao basi wakagharikishwa, na hapo maisha ya Nabii Nuh yakawa na wepesi na utulivu kutokana na imani ya Walioamini na Neema katika ardhi.'** *(Nazm Ad Durar (14/404))*

Imam Umar Ibn Ali Ibn 'Aadil Al Dimashqi Al Hanbali basi yeye anasema kua **'Mwanzoni aya imetumia neno *Sanah* na mwishoni ikatumia neno *Aám* ili kurahisisha utamkaji na hivyo kusiwe na uzito katika usomaji wa aya hio. Vile vile neno *Aám* limetumika kwa kuelezea miaka 50 ili kutilia mkazi kipindi ambacho Mtume wa *Allah Subhanah wa Taála* alipoachana na waovu hao, kua katika hali ya utulivu, Waarabu hutumia neno *Aám* kumaanisha Neema na neno *Sanah* kumaanisha Ukame'** (*Al Lubaab fi 'Ulum al-Kitab,* 12/429)

Kwani kwa maana hio basi Aya hii inatuonesha kua Watu hawa wa *As-hab Al Kahfi* Walikua katika ndani ya Hifadhi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani ya Miaka yote hio Waliyolala ambayo ilikua bado ni Miaka iliyojaa Mitihani ndani yake ambayo hata hivyo wao walisitiriwa na Mola wao kutokana nayo kutokana na kua na Ikhlasi katika Hijra yao na Dua yao

Yaani watu hawa walikua ni wenye kuzibwa masikio yao na Kulala ndani ya Kipindi chote ambacho kilikua ndani ya Miaka ya Kufr na hili linadhihirishwa kutokana na kua aya imetumia neno *Siniina* ambayo ni Miaka ya Mitihani na haikutumia neno *Aamun* ambayo ni miaka ya Raha na Utulivu.

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuelezea kilichofuatia kwa watu hao wa *As-hab Al Kahf* kwa kwa kusema:

﴿ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ الحِزْبَيْنِ أَحْصَىٰ لِمَا لَبِثُواْ أَمَداً﴾

Thumma baAAathn<u>a</u>hum linaAAlama ayyu al<u>h</u>izbayni a<u>hsa</u> lim<u>a</u> labithoo amad<u>a</u>n *(Surat Al Kahf 18:12)*

Tafsir: ***Kisha Tukawaamsha kutoka kwenye Usingizi wao Ili tupate Kuwajaribu Ni Wepi kati ya Makundi Mawili Bora katika Kuhesabu Kuhusiana na Kipindi Mda waliokaa katika hali waliyokua.***

Ambapo aya imetumia *Ahsa* linalotokana na neno *Hasa* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kurembea au Kupopoa kwa Kutumia Vijiwe vidogo vidogo.

Neno *Hasa* ndio lililotoa neno *Ahsa* Ambalo hua ni lente kumaanisha Hali ya Ubora katika Kuhesabu, Hali ya Ubora wa Kurikodi, Hali ya Ubora wa Kufanya Mahesabu na pia humaanisha Hali ya Ubora wa Kujua. Na ingawa Wanazuoni wa kipindi cha Mwanzoni cha Uislam wanakubaliana na maana niliyoitumia katika kutafsir kupitia katika neno *Ahsa.*

Lakini hata hivyo Wanazuoni wa baadae wa Tafsir akiwemo *Sultan Al Balagha Jarrah Allah* Imam Abu Qasim Al Zamakhshari na Wanazuoni wengineo hawakukubaliana na Tafsiri hii, kwani anasema Imam Al Zamakhshari ambae kama nilivyoanza na Cheo chake kua ni Sultan wa Lugha ya Kiarabu basi yeye anasema kua: **'Neno *Ahsa* lililotumika hapa halimaanishi kua Ni yupi au wepi wenye**

Kujua Hesabu zaid bali ni lenye kumaanisha ni wepi watakaofahamu zaidi au Watakaojua zaid.' na kama tulivyoona kua neno *Hasa* pia humaanisha Kujua.

Ambapo Mtizamo huu wa Jarrah Allah Imam Abu Qasim Mahmud Ibn Umar Al Zamakhshari ndio pia mtizamo wa Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abu Baqr Al Ansari Al Qurtubi. Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameyasema haya kama kwamba Kisa kimemalizika.

Lakini hata hivyo kisa hakijamalizika kwani ndio kwanza kinaanza isipokua *hapa Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuhitimishia Kisa kulingana na Malengo yake kua aliwalaza ili ije kujulikana ni nani mbora wa kuhesabu au ni nani mwenye kujua zaid, jambo ambalo ni kama atakavyobainisha hapo baadae katika aya.

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kuelezea kuhusiana na malengo ya kukielezea kisa hicho kwa Mtume wake *Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema kua:

﴿نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نبَأَهُم بِٱلْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُواْ بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى﴾

Nahnu naqussu AAalayka nabaahum bialhaqqi innahum fityatun amanoo birabbihim wazidnahum hudan *(Surat Al Kahf 18:13)*

Tafsir: ***Hakika Sisi Tunahadithia Juu yako wewe (Muhammad Salallahu Alayhi wa Sala) Habari zao Kwa Haki na kwa Kweli Hakika wao (Vijana hao) Walikua ni Vijana Shupavu, Walioamini Juu ya Mola wao Nasi Tukawazidishia wao Uongofu.***

Ambapo tunaona kua aya imetumia neno *Fityatun* linalotokana na Neno *Fataya* ambalo kwa Kilugha hua linamaanisha Kukua, Kua Balegh, Kua na Sifa za Kiume. Kua Shujaa, Kua Shupavu, Kua ni Mtu asiekua na woga, Kua Mkarimu.

Neno *Fataya* ndio lililotoa neno *Afta* ambalo hua linamaanisha Kutoa Ushauri, Kuusia, Kuelezea, Kutoa Hukmu au Maamuzi ya Kishariah.

Neno *Fataya* ndio lililotoa neno *Fatwa* ambalo hua linamaanisha Fatwa, Mtizamo au Hukmu kulingana na Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Neno *Fataya* ndio Lililotoa neno *Mufti* ambalo humaanisha Mtu Mwenye Ilm ya Dini ya Kiislam kuhusiana na Shariah za Dini ya Kiislam na hivyo kutoa Fatwa yaani Ufafanuzi Juu ya kitu kinachohitajika Kufafanuliwa.

Nadhani hapa kidogo tufafanue hapa kua kuna tofauti baina ya Qadhi na Mufti. Kwani Qadhi hua ni Mtu mwenye Ilm ya Dini Ya Kiislam kuhusiana na Sharia za Dini ya Kiislam ambazo hua anazitumia kwa ajili ya kutoa Hukmu baina ya pande mbili ambayo anapoitoa basi inabidi itekelezwe.

Na ingawa Mufti hua sio Qadhi na Qadhi hua si Mufti na ijapokua Mtu huyo huyo mmoja anaweza akawa Qadhi na akawa Mufti pia kutokana na kua na Uwezo wa Kutoa Fatwa na pia Kuhukumu.

Lakini kwa upande mwengine basi tunaona kua tofauti yao ni kua Mufti anaweza kujitolea Fatwa yeye mwenyewe na kwa watu wa Familia yake na Watu wengine. Lakini Qadhi hua hawezi kujihukumu kwani Qadhi Kazi yake ni Kupitisha Hukmu baina ya Pande 2 tofauti.

Hivyo tunaporudi kwenye aya yetubasi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawaelezea Vijana waliomo kwenye Kisa cha Pangoni kwa kuwapa sifa ya *Fityatun* kua ni Lenye Kumaanisha Vijana Mahiri au Shupavu ambao ni zaidi ya Wawili lakini wasiozidi 10 Kiidadi.

Hivyo hapa tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamuelezea Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kumwambia kua Kwa Hakika yeye anamuelezea Kisa cha Watu hawa kwa Ukweli na Uhakika.

Na kisha anaweka wazi kua walikua Vijana hao walikua ni *Fityatun* yaani Vijana Shupavu na wenye Msimamo juu ya Wanachokiamini. Kiasi ya kua walikua wako tayari kuachana na kila Kitu chao walichokua nacho katika Kasri la Duqyanus kwani walikua wakiishi kama Mawaziri ndani ya Kasri waliachana na Mapambo ya Dunia yao kwa ajili ya kumkimbilia Mola wao.

Ambapo kwa Imam Abu Abd Allah Sahl Al Tustari basi yeye anasema kuhusiana na aya hii kua: ***'Allah Subhanah wa Ta'ala* amaewaita vijana hawa kwa jina la Fitya kwa sababu walimuamini yeye bila ya kua na msaada wa njia yoyote na walikua ni wenye kujitolea kikamlifu kwa ajili yake na kauchana na kila kitu chao kidunia'**

Na hivyo kwa upande mwengine basi aya zinatuonesha pia sio katika kila kitu hua unatakiwa kutumia nguvu kwani baadhi ya Wakati hua ni Bora kuachana na baadhi ya Watu kabla ya wewe kudhurika au kusababisha Madhara zaid. Yaani Baadhi ya Wakati ni Bora Kuanza Upya Maisha yako Kivyako vyako.

Kwa upande mwengine basi tunaona kua ayah hii pia ni yenye kuenda sambamba na yale yanayotokea kwa Waislam waliomuamini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam na hivyo kua ni wenye kupingana na Udhalimu wa Makafiri wa Mji wa Makka.

Na hapa pia ndani ya Matukio haya na Sura hii basi ndio tunaona Ukubwa na Ujuzi na Makadirio ya Muumba wa Ulimwengu na kila kitu kichomo Ndani yake ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Miujiza ya Qur'an na ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani kama tulivyoona kua Makafiri walienda kuomba Ushauri kwa Mayahudi wa Makkah kutafuta njia ya Kumkwamisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Ujumbe wake na baada ya kupewa hoja basi wakaona kua wameshafanikiwa. Lakini..Subhanah Allah!

Walikua hawajui uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndio maana nae akawauliza Makafiri hao: Kua tukio hili la watu wa Pangoni ndio wameona kua ni Jambo la Ajabu sana?

Wakati Jambo la Ajabu ambalo wao hawalijui ni kua huko kutokana Kumkwamisha kwao *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kutumia Kisa hiki basi kumbe ndio imekua wamemletea Utatuzi wa hali ya mazingira waliyokua nayo Waislam katika wakati huo husika.

Kwani Allah *Subhanah wa Ta'ala* katika kukihadithia kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala* kisa hiki basi alikua pia anawafumbua Macho Waislam na kuwaambia kua Kua kulikua kuna *Fityatun* Vijana wasiofika 10 ambao Walikua ni Wanaoshindana na Ukarimu na kwa Ujasiri kiasi ya Kua walikua ambao Walikua na Hali Ngumu zaid yenu Waislam, kwani wao walikua Wadogo Kiumri na Kidogo Kiidadi.

Lakini kutokana na Kumuamini kwao *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuamua kutomshirikia *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuamua kuachana na kila kitu chao kwa ajili ya Kumkimbilia *Allah Subhanah*

wa Ta'ala basi Allah Subhanah wa Ta'ala aliwakimbilia na kuwazidishia Imani na kuwakumbatia katika hifadhi yake na kuwaongoza katika Njia ya Uongofu wakati wao walikua hawana hata Mtume hivyo hali itakuaje kwenu Nyie Waislam ambao Mnae Mtume ambae ni kipenzi cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndie kiumbe bora?

Hivyo Msitetereke wala msiwe na Khofu wala wasiwasi kwani kama mtakua na Msimamo wa kumfuata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na mkaachana na Matamanio ya Kidunia basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anakuahidini kua atakuongezeeni Imani. Atakuhifadhini, na Atakuongozeni katika Njia yake ili mpate kua ni Miongoni mwa Waliofaulu hapa Duniani na Kesho Akhera.

Fikiria kama Mayahudi na Makafiri wa Makkah wangekua Wanajua kua hizi hoja wanazotegemea kua zitawakwamisha Waislam kua majibu yake ndio yatakayowapa nguvu na Imani Waislam na kuwaonesha njia ya kutatulia Matatizo yao wanayokabiliana nayo basi jee wangeziibua Hoja hizi au Wangekatazana kua bora wasiziibue kwani zitawapa nguvu zaid Maadui zao?

Hivyo Naam bila ya shaka wasingehoji kama wangekua wanajua Matokeo yake hoja hizo. Lakini hawakujua na hii ni kwa sababu mwenye kujua ni Mwenyewe *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ni Bingwa wa Makadirio kwani akikadiriacho yeye hua tutake tusikate. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikadiria kua Waislam hao wafikwe na Mitihani ili kupimwa Imani zao na kisha ndani ya Makadirio yake hayo akakadiria kua Maadui wa Uislam Wategemo Mtego ambao utakapofyatuka basi badala ya kua ni wenye kusababisha Madhara uwe ni wenye kusababisha Manufaa makubwa zaid ya kuwazidishia Waislam Iman, Subra na kuwaonesha Muongozo wa njia ya kupitia kwenye aya hii ya *Fityatun.*

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuelezea kwa kusema:

﴿وَرَبَطْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُواْ فَقَالُواْ رَبُّنَا رَبُّ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ لَن نَّدْعُوَاْ مِن دُونِهِ إِلٰهاً لَّقَدْ قُلْنَا إِذاً شَطَطاً﴾

Warabat<u>n</u>a AAal<u>a</u> quloobihim i<u>dh</u> q<u>a</u>moo faq<u>a</u>loo rabbun<u>a</u> rabbu alssam<u>a</u>w<u>a</u>ti waal-ar<u>dh</u>i lan nadAAuwa min doonihi il<u>a</u>han laqad qulna i<u>dh</u>an sha<u>t</u>a<u>t</u>an *(Surat Al Kahf 18:14)*

Tafsir: ***Na Tukatia Nguvu Juu ya Nyoyo zao Waliposimamia katika Msimamo Kisha Wakasema kua Mola Wetu Ni Mola wa Mbingu Ardhi Hivyo Kamwe Hatutomuomba Mwengine Zaid yake Mungu (Wetu) huyo Kkwani Kwa hakika Tukiwa tumefanya Hivyo (Kwa kumuomba) Basi Itakua Tumesema Maneno ya Kufuru kubwa sana.***

Kama tunavyoona kua aya hii imetumia Neno *Rabata* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kufunga Kamba, Kufunga, Kuthibitisha, Kukiimarisha Kitu, Kufanya Kitu kua Madhubuti kwa Hoja au kwa Kukiongezea Nguvu, Kusimamisha Ngome, Kujitayarisha Kwa Nguvu na kiuwezo kwa ajili ya Kutegemea kupata Pigo, Dharuba au Athari kutoka katika upande wa Upinzani.

Kwani baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuwasifu *Fityatun* hao ambao ni Vijana wa Al Kahf kutokana na Ushupavu wao na msimamo wao katika kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha kudhihirisha kua alichokifanya kwao si chengine chochote isipokua kuwaongezea Imani na Kuwaongezea Nuru ya Muongozo basi akabainisha kilichotokea hadi Vijana hao wakapanda darja mbele ya Mola wao kwa kusema kama inavyoweka wazi Aya iliyotumia neno Rabatna kwa kusema:

Kwani hapa tunaona Aya kua zinahadithia kisa kwa Kutanguliza Mbele kwanza kudhihirisha matokeo ya malengo ya kilichotokea na kisha aya zinarudi nyuma kuelezea yaliyotokea kabla ya kutokea Matokeo ya kufikiwa Malengo husika Kwani Aya zimeturudisha katika Kutuelezea kule kilichotokea kwa Duqyanus pale vijana kumkataa Mfalme Duqyanus na hivyo kua na Msimamo wa kua Mungu wao ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawazidishia Nguvu kwenye Nyoyo zao Vijana hao na hivyo wakawa na Imani zaid na Subra ya kua tayari kuachana na watu wao pamoja na Duqyanus.

Na kisha baada ya kuweka wazi hayo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawageuzia Kibao Makafiri wa Makkah na Mayahudi na Hoja zao walizozitoa. Kwani kama tulivyosema kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliyakadiria haya yatokee katika Wakati amabo Makafiri hawakutegemea kua kutokana na hoja zao basi Watawasaidia Waislam na kuwazidishia Imani.

Kwani Kulingana na Wakati wa Matukio yaliyotokea katika Wakati wa *Rasul Alla Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni matukio Yaliyokua yakienda sambamba na yaliyotokea katika wakati wa Fityatun na Duqyanus basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawageuzia Kibao Makafiri hao kwa kuwahoji Sambamba kama walivyokua wakihoji Vijana wa *As-hab al Kahf* kuhusiana na watu wao kwa kusema kama ilivyosema aya.

﴿وَرَبَطْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُواْ فَقَالُواْ رَبُّنَا رَبُّ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ لَن نَّدْعُوَاْ مِن دُونِهِ إِلٰهاً لَّقَدْ قُلْنَا إِذاً شَطَطاً﴾

Warabatna AAala quloobihim idh qamoo faqaloo rabbuna rabbu alssamawati waal-ardhi lan nadAAuwa min doonihi ilahan laqad qulna idhan shatatan *(Surat Al Kahf 18:14)*

Tafsir: ***Na Tukatia Nguvu Juu ya Nyoyo zao Waliposimamia katika Msimamo Kisha Wakasema kua Mola Wetu Ni Mola wa Mbingu Ardhi Hivyo Kamwe Hatutomuomba Mwengine Zaid yake Mungu (Wetu) huyo Kkwani Kwa hakika Tukiwa tumefanya Hivyo (Kwa kumuomba) Basi Itakua Tumesema Maneno ya Kufuru kubwa sana.***

Na kama tunavyoona kua Maneno haya yanatudhihirishia kua kwa kila mwenye kutafakkar basi hua ni mwenye kupata Vithibitisho vilivyowazi juu ya kuwepo kwa Muumba wa kila kitu ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* asiekua na mshirika.

Na kwa maana hio basi wale wasioamini basi na watoe vithibitisho kuhusiana na Maumbile ya Kila kitu na kuhusiana na kile wanachokiamini wao ambacho hua Si chochote isipokua kumzushia uongo *Allah Subhanah wa Ta'ala* jambo ambalo ni Dhambi kubwa sana.

Huo ulikua ni Mtizamo wa Fityatun walipokua wakifahamishana miongoni mwao na kama tulivyosema kua hapa Aya zimeturudisha Nyuma kutuonesha namna yalivyokua Malengo yao kabla ya Kukimbilia kwao kwenye Pango ili kufanikisha Malengo yao.

Hivyo baada ya kuthibitishiana juu ya Imani yao baina yao basi ndio wakapanga mipango yao ya kuachana na Watu wao basi wakatahadharishana kama zisemavyo aya:

﴿وَإِذِ ٱعْتَزَلْتُمُوهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ إِلاَّ ٱللَّهَ فَأْوُوا إِلَى ٱلْكَهْفِ يَنْشُرْ لَكُمْ رَبُّكُم مِّن رَّحْمَتِهِ وَيُهَيِّئْ لَكُمْ مِّنْ أَمْرِكُمْ مِّرْفَقاً﴾

Wa-idhi iAAtazaltumoohum wama yaAAbudoona illa Allaha fa/woo ila alkahfi yanshur lakum rabbukum min rahmatihi wayuhayyi/ lakum min amrikum mirfaqan *(Surat Al Kahf 18:16)*

Tafsir: ***(Wakaambiana) Na Mtakapoachana nao wao Na Kile Wanachokiabudu, kisichokua Allah Basi Kimbilieni Kwenye Pango Atakutandazieni kwa ajili yenu Mola wenu Muelekeo au Njia Kutoka kwenye Rehma zake Na Atakuhuishieni Juu yenu Kutokana na Jambo lenu kwa kulipa Matokeo yenye Wepesi.***

Hivyo mbali ya kua hawa Vijana walikua wakiambiana wao kwa wao miongoni mwao, lakini pia tunarudi kwa Waislam na kuitumia aya hii na Mafunzo yake katika mazingira waliyokua nayo na pia tuliyokua nayo sisi leo hii.

Ambapo tunapoiangalia aya basi tunaona kua imetumia maneno mawili muhimu ambayo ni yenye kuwapelekea Watu kunufaika nayo pale Watakapokua ni wenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kikamilifu kwa Ikhalsi katika Jambo lao.

Ambapo maneno hayo ni *Yanshur* ambalo ni lenye kutokana na nemo *Nashara* ambalo humaanisha Kutandaza, Kutandika, Kukifufua Kitu kilichokufa, Kuongeza Uhai, Kufungua, Kuonesha na pia humaanisha Kutanua kitu kilichobana.

Na pia ikatumia neno *Mirfaqan* ambalo ni neno linalotokana na neno *Rafaqa* ambalo humaanisha Kua na Manufaa, Kusaidia. Kuhudumia, Kua Mkarimu na Mwenye Huruma, na pia humaanisha Kua na Urafiki wa Karibu na hii ni kwa sababu neno *Rafaqa* ndio lililotoa neno *Rafiqi* yaani Rafiki kama ilivyosema aya ifuatayo:

﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ فَأُوْلَئِكَ مَعَ ٱلَّذِينَ أَنْعَمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ ٱلنَّبِيِّينَ وَٱلصِّدِّيقِينَ وَٱلشُّهَدَآءِ وَٱلصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقاً﴾

Waman yutiAAi Allaha waalrrasoola faola-ika maAAa alladheena anAAama Allahu AAalayhim mina alnnabiyyeena waalssiddeeqeena waalshshuhada-i waalssaliheena wahasuna ola-ika rafeeqan*(Surat An Nisaa 4:69)*

Tafsir: ***Na wale ambao ni wenye Kumtii Allah Subhana wa Ta'ala na Mtume Salallahu Alayhi wa Salam watakua Pamoja na wale ambao Allah Subhanah wa Ta'ala amewaingiza kwenye Rehma zake miongoni mwa Mitume na Siddiqun na Mashahidi na Wafanyao Mema, na ni Marafiki wazuri walioje hao.***

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamalizia kuhusiana na sifa za watu wenye kuupata uhusiano huo wa Kirafiki na watu hao kutokana na Utifu wao kwa kusema:

﴿ذَٰلِكَ ٱلْفَضْلُ مِنَ ٱللَّهِ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ عَلِيماً ﴾

Thalika alfadhlu mina Allahi wakafa biAllahi AAaleeman*(Surat An Nisaa 4:70)*

Tafsir: ***Hizo ni Fadhila kutoka kwa Allah Subhanah wa Ta'ala na anatosheleza Allah kua ni Mwenye kujua kila kitu.***

Ambapo neno *Rafaqa* ndio lililotoa neno *Mirfaqa* ambalo humaanisha Sehemu ya Kuegemea, Sehemu ya Kukupa Nguvu na Kukusaidia kwa Ukarimu na Mapenzi na pia hua linamaanisha Mipango inayopangwa au inayofanyika kwa ajili ya Kumsaidia au kumrahisishia Mtu kitu kigumu au Jambo gumu, na pia Neno *Mirfaq* humaanisha Mto wa Kitandani au Kwenye Kiti au Majlis ambao Mtu hua unaweka Kichwa chako, ubavu wako, au unaegemea kwa ajili ya Kujipumzisha.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuwekea Wazi kua Tukimkimbilia basi atatutandazia hali ya Kuturahisishia Mambo yetu kutokana na Mapenzi na Rehma zake juu yetu. Watu hawa ambao ni Fityatun wakaingia Mafichoni Kwenye Al Kahf huku wakiwa ni wenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* awafanikishie Malengo yao kwa wepesi kutokana na Rehma zake na mapenzi yake juu ya Wanaomuamini.

Ambapo baada ya hapo ndio wakaomba ile dua ya aya ya 10 ambayo tumeshaiangalia hapo kabla yenye kusema:

﴿ رَبَّنَآ آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَداً﴾

Rabbana atina min ladunka rahmatan wahayyi/ lana min amrina rashadan *(Surat Al Kahf 18:10)*

Tafsir: ***'Ewe Mola wetu Tupo Kutoka kwako Rehma Na Utuhuishie (Ututilie Nguvu, Ututilie Uhai, Utufanikishie) Jambo letu hili Kiuongofu.'***

Na ingawa watu hawa walikimbilia Kwenye Pango lakini baadhi ya wakati inapotokea Mitihani basi hua si lazima kukimbilia Kwenye Mapango au Milimani au Misituni, bali hata Majumbani hua kunafaa na ndio maana akasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Al Qurtubi kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Mtakapokua mnakhofia Mitihani basi Jizuieni ndani ya Majumba yenu na kisha idhibitini Midomo yenu.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Bukhari basi yeye anasema kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Utafika wakati kwa watu ambapo hali ya mwenye Mali zaid miongoni mwa Waislam ni yule mwenye mbuzi wawili watatu. Ambao watakua wanamfuata kutoka Mlima mmoja kuelekea mlima mwengine, na kukimbilia kwenye sehemu zenye Mvua na kuzikimbia sehemu zenye Mitihani inayotokana na kuadhibiwa kutokana na kua na Imani ya Dini ya Kiislam.'**

Kwani alisema pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Utakuja Wakati ambao itakua hakuna hata Mtu mmoja ambae atakaekua salama kutokana na Dini yake isipokua wale waliokimbilia Milimani kujificha kutoka sehemu moja kukimbilia sehemu nyengine. Na Itafikia katika hali ya mazingira ambayo haitowezekana kwa mtu kuchuma kipato chake isipokua kwa kupitia njia za Kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Hivyo itakapofikia wakayi huo basi Mtu ataruhusika kukimbilia Mafichoni.'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakauliza: **'*Ya Rasul Allah!* Itawezekanaje kukimbilia Mafichoni wakati wewe umependekeza sisi kuoa Wanawake na kua na makazi?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Katika kipindi hiki matatizo ya Mtu yatakua yanatokana na Wazee wake, Na akiwa hana Wazee basi matatizo yatatokana na Mkewe Na akiwa hana Mke basi Matatizo yatatokana na Watoto wake. Na akiwa hana Watoto basi Matatizo yatatokana na Majirani zake.'**

Masahaba wakauliza: '**Itakuaje hivyo *Ya Rasul Allah?'***

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: '**Watamsema na kugombana nae kutokana na Kutokua na uwezo wa Kifedha na watamlazimisha kufanya mambo ambayo yatakua nje ya uwezo wake. Hivyo kutokana na hali hio basi Mtu atafanya mambo ambayo yatamuangamiza.'***(Imam Al Qurtubi)*

Na ingawa Aya na Hadith tunazoendelea nazo zinatuonesha kua inakubalika na ianpendekezwa kwa Mtu kua ni mwenye kujitenga na watu wake pale anapoona kua watu wake hao wanaweza wakamsababishia mangamizo yake mbele ya Mola wake.

Lakini pia kwa upande mwengine basi kama inawezekana basi kuwastahmilia watu hao pia hua inakubalika pale itakapokua mtu husika anao uwezo wa kujidhibiti kutokana na Uzito wa mitihani hio, Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pia kua: **'Muumini anaechanganyika na Waru huku akiwa na Subra ni Bora kuliko yule anaejitenga nao watu, kwani hua si mwenye kua na Subra.'**

Na tunapoawaangalia Masahaba Wanaojulikana kama Ahl Al Badr yaani waliopigana Vita vya Badr basi Tunaona kua baada ya kutokea Mtihani wa Kuuliwa *Amir ul Muuminin* Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu basi* watu wa Ahl Al Badr *Radhi Allahi Anhum* waliingia ndani ya Majumba yao, na hawaku wenye kutoka tena hadi pale walipotolewa kwa ajili ya Kuenda kuzikwa baada ya Kufariki kwao.

Ambapo kwa upande wa Imam Sufyan Ibn Ath Thawry pia nae alikimbilia Mafichoni baada ya kukumbwa na Mitihani iliyohatarisha Uhai wake. Na pia baada ya Kifariki kwake Imam Sufyan Ath Athawry basi Imam Sufyan Ibn Uyaynah alimuota Imam Ath Thawry akiwa anamuusia kwa kumuambia Kaa Mbali nao Watu, kwani ni mitihani mitupu.

Tunaporudi kwa Fityatun wetu ambao ni vijana waliomkimbia Mfalme Duqyanus na kukimbilia kwenye Pango na hivyo baada ya kuomba Dua yao ya kuomba Uongofu wa Jambo lao kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Wakalala, ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuelezea hali ilivyokua wakati walippkua wamelala ndani kati kati ya Pango hilo kwa kusema:

﴿وَتَرَى ٱلشَّمْسَ إِذَا طَلَعَت تَّزَاوَرُ عَن كَهْفِهِمْ ذَاتَ ٱلْيَمِينِ وَإِذَا غَرَبَت تَّقْرِضُهُمْ ذَاتَ ٱلشِّمَالِ وَهُمْ فِى فَجْوَةٍ مِّنْهُ ذَٰلِكَ مِنْ آيَاتِ ٱللَّهِ مَن يَهْدِ ٱللَّهُ فَهُوَ ٱلْمُهْتَدِ وَمَن يُضْلِلْ فَلَن تَجِدَ لَهُ وَلِيّاً مُّرْشِداً﴾

Watara alshshamsa idha talaAAat tazawaru AAan kahfihim dhata alyameeni wa-idha gharabat taqriduhum dhata alshshimali wahum fee fajwatin minhu dhalika min ayati Allahi

man yahdi Allahu fahuwa almuhtadi waman yudhlil falan tajida lahu waliyyan murshidan *(Surat Al Kahf 18:17)*

Tafsir: ***Na Ungeweza kuliona Jua Pale linapochomoza Likiinamia Kutoka Kwenye Pango lao Kwa Upande wa Kulia Na pale Linapozama Lilikua Likiwaepuka Kwa Upande wa Kushoto Huku wao waki Katikati yake (Pango hilo) Hizi Ni miongoni mwa dalili za Allah (Hivyo) Yule anaeongozwa na Allah Basi Hua ni Alieongozwa kiusahih Na Anaeptoshwa Basi Hamtopatia Rafiki wa Karibu wa kumuogoza.***

Hivyo aya zinatuonesha kua kutokana na Mazingira ya Pango hilo basi watu hawa walikua si wenye kupigwa na jua wala kuhisis joto au mvuke wake kwani walikua wako katika sehemu ambayo ni Salama ambayo haipigwi na jua ndani ya Mwaka mzima.

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuainishia kua Jua lilikua linawakimbia mbali ya kua Jua katika Mzunguko wake wa siku katika Mwaka basi hua linazunguka kulingana na Muonekano wa Dunia na hivyo kusababisha Msimu wa Miongo ya hali ya hewa.

Kwa mfano katika kipindi hiki cha Miezi mitatu ya Disemba, January na Febuari basi katika Mzunguko wake Jua huo linazungukia upande wa Kusini mwa Mstari wa Ikweta kutokea Mashariki kuelekea Magharibi. Na hivyo katika Kipindi hiki basi nchi za Kaskazini mwa Dunia hua ziko kwenye Msimu wa Baridi, theluji inashuka kw awigi sana na kwao wao wakati wa Machan hua ni mdogo sana kimasaa kulio Usiku na za Kusini mwa Dunia hua ziko katika Msimu wa Kiangazi ambapo nao kw aupande wao wakati wa mchana hua ni mrefu kuliko wakati wa Usiku.

Kisha Jua linarudi katikati kwenye Mstari wa Ikweta na taratibu kuelekea Kaskazini hadi unapofikia katika Miezi ya June July basi Jua hua linazungukia upande wa Kaskazini mwa Equator na Hivyo Nchi za Kaskazini hua zinaingia kwenye Wakati wa Kiangazi na ndio maana hua Wazungu wanakauja Sana Afrika katika kipindi hicho kwani kwao ni Joto.

Ambapo katika wakati huo wa June July basi Watu wa Kusini Mwa Dunia hua wanaingia kwenye Mzunguko wa kipindi cha Baridi ndio unakuta ardhi za Afrika Kusini, Australia, New Zealand n.k Theluji inashuka.

Hivyo katika Aya hii *Allah Subhanah w Ta'ala* anatudhubirishia kua Mbali ya kuwepo kwa Utofauti huo wa Mzunguko wa Jua basi hata hivyo watu hao hawakuweza kudhurika na Jua hilo wala kulihisi kwani walikuwepo ndani kivulini ambapo hata hivyo *Allah Subhanh wa Ta'ala* amesema kuhusiana na Kivuli cha Jua kua:

﴿أَلَمْ تَرَ إِلَىٰ رَبِّكَ كَيْفَ مَدَّ ٱلظِّلَّ وَلَوْ شَآءَ لَجَعَلَهُ سَاكِناً ثُمَّ جَعَلْنَا ٱلشَّمْسَ عَلَيْهِ دَلِيلاً﴾

Alam tara ila rabbika kayfa madda al*dhdh*illa walaw shaa lajaAAalahu sakinan thumma jaAAalna alshshamsa AAalayhi daleelan *(Surat Al Furqan 25:45)*

Tafsir: ***Hivi Jee umeona wewe namna Mola wako anavyokitandaza Kivuli, Kwani kama anagetaka basi angekifanya kua si chenye kutembea, lakini Tumelifanya Jua kua ndio muongozi wake. (Kivuli ambapo hua kinajibana na kutoweka katika wakati wa mchana (wa Saa sita) Na kisha kinatokea tena baada ya kuelemea kwa Jua , kwani kama ingekua hakuna Jua basi ningekua pia hakuna kivuli).***

Ambapo hii pia ni Dalili na Uthibitisho wa kua Qur'an ni Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie alieumba Sayari na Dunia na kila kitu na kisha akakijaalia kila kitu kua katika Mzunguko wake kulingana na Mazingira na Wakati na Sehemu husika kwa manufaa ya Viumbe wake kutokana na Makadirio yake kama zinavyosema Aya;

﴿وَآيَةٌ لَّهُمُ ٱلَّيْلُ نَسْلَخُ مِنْهُ ٱلنَّهَارَ فَإِذَا هُم مُّظْلِمُونَ ۞ وَٱلشَّمْسُ تَجْرِى لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ ٱلْعَزِيزِ ٱلْعَلِيمِ ۞ وَٱلْقَمَرَ قَدَّرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَٱلْعُرْجُونِ ٱلْقَدِيمِ ۞ لَا ٱلشَّمْسُ يَنۢبَغِى لَهَآ أَن تُدْرِكَ ٱلْقَمَرَ وَلَا ٱلَّيْلُ سَابِقُ ٱلنَّهَارِ وَكُلٌّ فِى فَلَكٍ يَسْبَحُونَ﴾

Waayatun lahumu allaylu naslakhu minhu alnnahara fa-idha hum muthlimoona; Waalshshamsu tajree limustaqarrin laha dhalika taqdeeru alAAazeezi alAAaleemi; Waalqamara qaddarnahu manazila hatta AAada kaalAAurjooni alqadeemi; La alshshamsu yanbaghee laha an tudrika alqamara wala allaylu sabiqu alnnahari wakullun fee falakin yasbahoona*(Surat Yasin 36:37-40)*

Tafsir: ***Na Aya zetu kwa ajili yao Ni Usiku Tunapoutoa Kutokana Na Mchana Na Kisha Kinaingia Kiza Na Jua Linapotembea Katika Mzunguko wake Hayo ni Makadirio Ya Mwenye Utukufu na Ilm juu ya Kila Kitu Na Mwezi Tumeukadiria Vituo Vyake Hadi Unarudi Katika Hali ya Kupinda kama Kijiti cha shada la Tende la zamani kwa kukauka. Si Jua Linaloukimbia Na Kuupita Mwezi Na Wala Si Usiku Unaoutangulia Mchana Na Kila Kimoja Kina Elea Katika Mhimili wake.***

Ama tunapozungumzia kuhusiana na Pango ambalo ndani yake kulikua kuna Vijana hawa wenye sifa ya Fityatun waliolazwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Miaka kadhaa huku Jua likiwakiuka na kuwakimbia ili lisiwachome na kuwaathiri na kuwamsha pia.

Ambapo Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na sehemu liliopo Pango hilo kwani kuna wasemao kua ni Uturuki kama tulivyoona hapo awali Lakini pia Imam Muhammad Ibn Is-haq basi yeye anasema kua Pango hilo liko *Nineveh* yaani katika maeno ya Mosul nchini Iraq.

Na kuna wanaosema kua ni katika Maeneo ya Qumran nchini Jordan.

Na pia kuna wanaoasema ni Katika Maeneo ya *Aylah* nchini Jordan pia kulingana na Mtizamo wa *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abas *Radhi Allahu Anhu.*
Na Anasema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na hali ya Watu hawa katika Kulala kwao huko kua: Walikua wakigeuzwa mara moja kwa mwaka ubavu wa upande mmoja kulalia Ubavu wa Upande wa Pili ili Ardhi isije ukaiharibu Miili yao, na hii siku ya kugeuzwa ilikua ni siku ya Ashura

Ambapo kwa Upande wa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kua Walikua wakigeuzwa mara mbili kwa mwaka.

Na tunapozungumzia kuhusiana na Kulala na kugeuzwa Usiku basi ukifuatilia utaona kua sio wao tu peke waliokua wakilala na kugeuzwa kwani kutokana na Ukamilifu wa Maumbile yetu Ibn Adam basi hata mimi na wewe. Kwani Tunapolala hua tu ageuka Usiku kutoka katika Upande mmoja

kuelekea upande mwengine na hii ni kutokana kua Mwili hua ni wenye kua na hisia za Uchovu wa kulali upande mmoja kutokana na kua mzunguko wa Damu katika viungo vya upande wa sehemu husika kua unapungua nguvu kutokana na kubinyika na hivyo kutupelekea kugeukia upande wa pili ili Mzuguko uendelee kama kawaida mwilini.

Hivyo kugeuka kwetu kusingewezekana kama si ukamilifu wa Ufanyaji kazi wa Mifumo ya Miili yetu yenye sifa ya kua na *Ahsana Taqwimin.* Ambapo hii ni Sifa aliyoipa mwenyewe Muumba *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwa maana hio basi hatuna budi nasi mimi na wewe kutafakkar juu ya Rehma hii aliyotujaalia *Allah Subhanah wa Ta'ala* ya kua ni wenye kuweza kugeuka wenyewe bila kuhisi wala kujua kutokana na yeye kua Ni mwenye kutujaalia Uwezo huo, ambao haukukatishii Usingizi wako wewe na wala yule ulielala nae karibu yako.

Hivyo kila unavyogeuka basi fahamu kua si kutokana na Uwezo wako bali ni kutokana na Ukamilfu wa Mola wako katika kukukadiria na kukuumba kwako na akakulea hadi ukafikia ulipofikia.

Hivyo nasi pia Tunageuzwa Usingizini na yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na majaaliwa na Rehma zake juu yetu. Na hivyo kutokana na hali ya mazingira waliyokua wamelala watu hao na kugeuzwa geuzwa kwao kulia na kushoto basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuelezea hali hio kwa kusema:

﴿وَتَحْسَبُهُمْ أَيْقَاظاً وَهُمْ رُقُودٌ وَنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ ٱلْيَمِينِ وَذَاتَ ٱلشِّمَالِ وَكَلْبُهُمْ بَاسِطٌ ذِرَاعَيْهِ بِٱلْوَصِيدِ لَوِ ٱطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَاراً وَلَمُلِئْتَ مِنْهُمْ رُعْباً﴾

Watahsabuhum ayqa*dh*an wahum ruqoodun wanuqallibuhum dhata alyameeni wadhata alshshimali wakalbuhum basitun dhiraAAayhi bialwaseedi lawi ittalaAAta AAalayhim lawallayta minhum firaran walamuli/ta minhum ruAAban*(*Surat Al Kahf 18:18)*

Tafsir: ***(Kama ungewaona) Ungewadhania kua wako Macho, wakati wakiwa wamelela, nasi tulikua tukiwageuza katika upande wa kulia kwao na kushoto kwao, huku Mbwa wao akiwa amenyoosha miguu yake kwenye mlango (wa kuingilia Pango hilo) kama ungewaona basi bila ya shaka ungegeuka na kukimbia kutokana nao na ungeshangazwa nao.***

Katika kuelezea Usingizi wao basi aya imetumia Neno *Ruqud* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kulala, Kusinzia, Kua Mregevu, Kua na hali ya Uchovu, Kua na Muonekano wa Mtu ambae ndie kwanza ameamka hata uso hajanawa.

Yaani kama *Rasul Salallahu Alayhi wa Salam,* au pia kama mimi na wewe tunaosoma Qur'an tungewaona Watu hao walivyokua *Ruqudun* (Wamelala Usingizi) basi tungedhania kua Wako macho, huku Mbwa wao akiwa amelala kwenye mlango wa Pango hilo, na bila ya shaka tungekimbia kutokana na muonekano wao unaoshangaza, Hivyo hapa tunaoneshana wa neno *Raqada* kwa Sababu neno hili ndio lililotoa neno *Marqad,* ambalo hua linamaanisha Kitanda au Sehemu ya Kulalia iwe kwa Mtu alie hai au aliefariki.

Katika Uumbwaji wa Dunia na kutofautiana baina ya Mchana na Usiku na kubadilika kwa ukubwa wake wa nyakati hizo kulingana na misimu tofauti ya Mwaka kutokana na Maumbile ya Duara ya Dunia basi anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿يُولِجُ ٱلَّيْلَ فِى ٱلنَّهَارِ وَيُولِجُ ٱلنَّهَارَ فِى ٱلَّيْلِ وَسَخَّرَ ٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِى لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ذَٰلِكُمُ ٱللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ ٱلْمُلْكُ وَٱلَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ﴾

Yooliju allayla fee alnnahari wayooliju alnnahara fee allayli wasakhkhara alshshamsa waalqamara kullun yajree li-ajalin musamman dhalikumu Allahu rabbukum lahu almulku waalladheena tadAAoona min doonihi ma yamlikoona min qitmeerin *(Surat Fatir 35:13)*

Tafsir: ***Anauingiza Usiku kwenye Mchana, na anauingiza Mchana kwenye Usiku na akavifanya Jua na Mwezi kua kila kimoja ni chenye kupita katika njia yake iliyojaaliwa. Huyo ndio Allah Mola wenu, yeye ndie Mwenye Mamlaka, na wale ambao mnao waomba zaidi yake hawamiliki chochote hata Qitmir (Ngozi Laini ya Kokwa ya Tende)***

Ambapo aya hii imetumia neno *Yuliiju* ambalo ni lenye kutokana na neno *Walaja* lenye kumaanisha Kuingia, Kupenya, Kulinda, Kukaribiana sana na Kutegemeana japo kua ni Tofauti Kimaumbile, hivyo basi japo kua Usiku na Mchana ni vitu vyenye maumbile tofauti kwani kimoja kina Kiza na chengine kina Nuru lakini vitu viwili hivi ni vyenye Kuingiliana na Kulindana kiasi ya kua Kimoja hakiwezi kuwepo kinapokosekana chengine.

Katika aya hii tunaona pia *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametumia neno *Qitmir* ambalo linamaanisha Ngozi laini na nyepesi sana inayokaa baina ya Kokwa ya Tende na Nyama ya Tende, hii ni ngozi ambayo wengi miongoni mwetu hua hawaioni kutokana na kua ni wenye kuitupa Kokwa ya Tende baada ya Kula Nyama ya Tende ambayo ndio Tende yenyewe na ndio yenye Manufaa kwa Mwili na yenye Ladha ya Utamu wenyewe.

Na hii hali ya maumbile ya Usiku na Mchana kutokana na makadirio yake katika kuumba kwake ni kwa ajili ya manufaa ya Viumbe vilivyomo ndani yake Ulimwenguni na ndio maana athari yake tukawa tunaihisi mpaka ndani ya miili yetu ambayo ni yenye maumbile bora na ukamilifu wa kipekee kama anavyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika *Qur'an* kua:

﴿لَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَانَ فِىٓ أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ﴾

Laqad khalaqna al-insana fee ahsani taqweemin *(Surat Tinn 95:4)*

*Tafsir***:** ***Kwa hakika tumemuumba Mtu katika Taqwim bora kabisa.***

Ambapo aya imetumia neno *Taqwim,* ambalo ni lenye kutokana na mzizi wa neno *Qa-Ma* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kua katika hali ya Kusimama Sawia, Kua Thabiti, Madhubuti, Kamilifu, Kua bila ya kasoro yeyote, Kua na Thamani, hali ya Usimamizi, Hali ya ulinzi, Hali ya mpangilio uliokamilika, hali ya Mfumo kamili, hali ya Umbo lililokamilika n.k

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesifia hali ya kua *Taqwim* lakini hii si *Taqwim* ya kawaida bali ni *Ahsani Taqwim* yaani *Taqwim* Bora. Hivyo basi *Taqwim* inayozungunziwa katika ayah hii ambayo

ni *Taqwim* bora humaanisha hali ya maumbile inayojumuisha Mfumo Kamilifu wa Mwili mzima wa Ibn Adam na ufanyaji kazi wake kuanzia ndani ya mwili wake ambamo mna Mifumo kamilifu tofauti ndani yake ikiwemo Mfumo wa Damu, Mfumo wa Chakula, Mfumo wa Ubongo, Mfumo wa Viungo, Mfumo wa Ufaham, Mfumo wa Hisia n.k ambayo hua ni yenye kuenda sambamba kiufanyaji kazi na Maumbile ya mfumo wa Viungo vya nje ya mwili na kukamilisha Muonekano mzuri wa Maumbile ya mwili wa Ibn Adam.

Miongoni mwa sifa bora za Ukamilifu huo ni kua na mfumo unaozalisha Kemikali ambazo hua ni zenye kua na kazi tofauti ndani ya Miili yetu, ambapo moja miongoni mwao kemikali hizo ni ile inayojulikana kwa jina la *Seratonin* ambayo huzalishwa na Mfumo Kamilifu wa Ubongo. *Seratonin* hua ni Kemikali inayohusiana na Uhifadhi wa Kumbukumbu, Ufaham, Hisia za Furaha, Mapenzi, Uchangamfu n.k

Kemikali ya *Seratonin* pia hua ni yenye kufanya kazi ya kumsababishia mtu kua na hali ya kuhisi Usingizi kutokana kua ni yenye kusaidia uzalishwaji wa Kemikali nyengine iitwayo *Melatonin* ambayo nayo huzalishwa katika Mfumo wa Ubongo na kisha kuingizwa ndani ya Mfumo wa Damu.

Melatonin hua ni kemikali ambayo ni yenye kusimamia Mfumo wa saa ya ndani ya Mwili wa Ibn Adam ambao ndio unaoutaarifu Mwili kua sasa hivi ni usiku na umefika mda wa Kulala ili mwili na ufaham upate kupumzika kwa ajili ya majukumu ya siku inayofuata na *Seratonin* hua ni yenye kusimamia Mtu kuchangamka na kua macho pale linapochomoza Jua kwa kuutayarisha mwili na ufaham baada ya kupumzika kwake na kumtaarifu mtu kua umefika wakati wa kuamka na kuushughulisha mwili, akili na ufaham kwa ajili ya majukumu ya siku mpya.

Hivyo basi kama ilivyokua kua kuna mategemeano baina ya uingiaji wa Usiku na Mchana kiulimwengu basi ndio hivyo ilivyokua kuna mategemeano baina ya Kemikali za *Seratonin na Melatonin* katika ufanyaji kazi wao kwa *Seratonin* kubainisha kua umefika wakati wa Mchana na kiza kinapoingia *Melatonin* kuubainishia mwili kua umefika wakati wa Usiku na hivyo mwili inabidi upumzike.

Katika kuthibitisha hili basi mbali ya kua katika wakati wa usiku mtu hua unahisi Usingizi zaidi kuliko wakati wa Mchana. Kiasi ya kua hata wale wanofanya kazi za kukesha Usiku basi Mchana hua hawezi kulala na kupata usingizi ambao ni sawa kama vile ambavyo wanaoupata kama wangelala wakati wa usiku.

Au kama mtu atasafiri kutoka upande mmoja wa Dunia kwa mfano kutoka Afrika kueleka Canada, au kutoka Afrika kuelekea Australia, basi kwa kua kuna utofauti wa mda wa kuingia Usiku na Mchana baina ya sehemu aliyotoka basi akifika sehemu aliyoeleka basi hatoweza kulala na kupata usingizi hata kama ikiwa ni usiku na hii ni kwa sababu uzalishwaji wa *Melatonin* katika mwili wake hua haujazoea mazingira mapya ya nyakati za kuzama na kuchomoza kwa Jua katika sehemu aliyowasili na hua bado unaendana na hali ya mazingira ya sehemu aliyokuwepo hapo kabla.

Hivyo mwanzoni mtu kama huyu hua ni mwenye kupata shida ya kulala na kupata usingizi kwa siku mbili tatu hadi pale atakapozoea mazingira hayo mapya na hivyo uzalishwaji huo wa kemikali za *Seratonin na Melatonin* ndani ya mwili wake ukae sawa na kua ni wenye kuendana sambamba na hali ya mazingira ya kuchomoza na kuzama kwa jua katika ardhi ya ugenini aliyokuwepo.

Mfano mwengine ni ule ambao wengi wetu tunaujua sana kutokana na kuumwa baadhi ya Maradhi tofauti katika uhai wetu, hivyo tuchukulie mfano wa mtu anaeumwa na Homa, Kifua, Jino, n.k basi hua tunajua kua mgonjwa hua ni mwenye kuzidiwa zaidi hali ya maradhi yake katika wakati wa usiku

kuliko katika wakati wa mchana, kiasi ya kua mtu hujiuliza inakuaje mpaka maradhi hayo hua yanajua kua umeingia usiku?

Hivyo Mfumo wa uzalishwaji wa *Seratonin* na *Melatonin* ndio unaoutaarifu mwili kuhusiana na mabadiliko ya nyakati za Usiku na Mchana katika maisha yetu Ulimwenguni na hii si kwetu sisi tu bali hata kwa Ndege, Wanyama wa ardhini na Samaki pia hua ni wenye miili yenye kujua mabadiliko hayo ya nyakati za kila siku, kwani pia kama wanyama wengine wangekua hawana ufaham huo ndani ya miili yao na hivyo kukosa hisia ya kuupumzisha mwili kwa kulala basi ingekua hatari sana.

Mabadiliko haya hua Usiku na Mchana hua ni kwa ajili ya manufaa ya yetu na kwa ajili ya Viumbe vilivyomo Ulimwenguni kama anavyosema mwenyewe Muumba katika aya zinazofuata:

﴿وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتاً ۞ وَجَعَلْنَا ٱللَّيْلَ لِبَاساً ۞ وَجَعَلْنَا ٱلنَّهَارَ مَعَاشاً﴾

WajaAAaln<u>a</u> nawmakum sub<u>a</u>t<u>a</u>n WajaAAaln<u>a</u> allayla lib<u>a</u>s<u>a</u>n; WajaAAaln<u>a</u> alnnah<u>a</u>ra maAA<u>a</u>sh<u>a</u>n*; (Surat An Nabaa 78:9-11)*

*Tafsir: **Na tukajaalia Usingizi kua ni Pumziko, Na tukaujaalia Usiku kua ni Libas (Vazi), Na Tukajaalia Mchana kua ni wa Maisha (kutafutia)***

Hivyo katika aya hizi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatubainishia Umuhimu na Manufaa yanayopatikana kutokana na kuwepo kwa Maumbile ya Usingizi, Usiku na Mchana kwa ajili ya Viumbe wake ambapo tunaona kua aya zimetumia neno *Subata* ambalo hua linamaanisha Kupumzika, Kutulia, Kujinyoosha, Kukatisha, Kusitisha, Kulala, Kusinzia Kunakotokana na Machofu.

Na hali za hatua za hisia ya Usingizi imetajwa mara kadhaa ndani ya Qur'an kwa kuainisha hali na hatua zake tofauti kimaumbile kama vile walivyoelezea Wansayansi wetu leo hii, na hii hali ya *Subatan* hua ni hali ya hatua ya mwisho ya Usingizi ambayo hua ni hali ya kulala kwa Usingizi mzito wa kutosha kuupumzisha mwili na ambao ndio unaompelekea mtu kua ni mwenye kuota ndani yake, ambapo hali ya kwanza ya hisia ya Usingizi hua ni ile ya *Sinatun* ambayo imetajwa katika sehemu yamwanzoni ya *Ayat Al Kursiy* ambayo imetumia neno *Sinatun* kwa kusema:

﴿ٱللَّهُ لاَ إِلَٰهَ إِلاَّ هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ﴾

All<u>a</u>hu l<u>a</u> il<u>a</u>ha ill<u>a</u> huwa al<u>h</u>ayyu alqayyoomu l<u>a</u> ta/khu<u>dh</u>uhu sinatun wal<u>a</u> nawmun *(Surat Al Baqara 2:255)*

*Tafsir: **Allah! La ilaha illa Huwa (Hakuna Mungu anaestahiki kuabudiwa isipokua yeye), Mwenye kuishi Milele, Mwenye kusimamia na kukipa Ulinzi kila kitu, Asiepitiwa na kusinzia na wala asiepitiwa na Usingizi.***

Ambapo neno *Sinatun* hua linatokana na neno *Wasana* ambalo hua linamaanisha Kua na hisia ya kutaka Kulala au Kusinzia ambayo hua ni hatua ya kwanza ya hisia ya Usingizi, na hivyo kumaanisha umuhimu wa udhaifu wa Ibn Adam wa kua ni mwenye kuhitaji mapumziko ya mwili wake kutokana na maumbile yake, lakini maana iliyotumika katika ayah hii haimzungumzii Kiumbe bali inamzungumzia Muumbaji, na hivyo kumuelezea kua ni asie kua na sifa za kiumbe, kwani yeye yuko

mbali na sifa za viumbe wake hahitaji kupumzika kwa sababu hana sifa ya kuchoka na hivyo hasinzii na wala halali.

Hivyo *Sinatun* hua ni sehemu ya hatua ya kwanza ya hisia ya Usingizi ambapo hatua ya pili hua ni *NaaAsa*. Ambalo ni neno linalomaanisha Kupumzika, Kua na Udhaifu wa Mwili kutokana na Machovu au Kuingia Ndani ya hatua ya Usingizi yaani Kulala kwa dakika kadhaa.

Ambapo tunaona katika Qur'an kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amelitumia neno *NaaAsa* mara mbili ambazo ni mara zinazoelezea hali ya kulala kwa dakika kadhaa, kwani aya zilizotumiwa ndani yake ni zile aya ambazo zainzungumzia hali ya Usingizi wa Watu ambao wako vitani, hivyo hua ni tofauti na Usingizi wa Nyumbani kwani hua ni usingizi wa kupunguza machovu kwa kiasi ya dakika kadhaa, ili angalau ukiamka uwe na umakini kidogo na nguvu mpya, Ambapo miongoni mwa aya hizo ni ile inayozungumzia tukio la vita vya Badr kama ilivyosema aya:

﴿إِذْ يُغَشِّيكُمُ ٱلنُّعَاسَ أَمَنَةً مِّنْهُ وَيُنَزِّلُ عَلَيْكُم مِّنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً لِّيُطَهِّرَكُمْ بِهِۦ وَيُذْهِبَ عَنكُمْ رِجْزَ ٱلشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَىٰ قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ ٱلْأَقْدَامَ﴾

Idh yughashsheekumu alnnuAAasa amanatan minhu wayunazzilu AAalaykum mina alssama-i maan liyutahhirakum bihi wayudhhiba AAankum rijza alshshaytani waliyarbita AAala quloobikum wayuthabbita bihi al-aqdama *(Surat Al Anfal 8:11)*

Tafsir: ***Na (kumbukeni) alipokufunikeni nyie na NuaAsa kama Amani kutoka kwake na akakutumieni Maji kutoka Mbinguni ili akutoharisheni na kukutoeni wasiwasi kutoka kwa shaytani na kuzithibitishia Nyoyo zenu na kuifanya miguu yenu iwe na nguvu***

Ambapo aya inafafanulika vizuri sana pale tunapoangalia ufafanuzi wa *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin* Imam Fakhr Ad Din Al Razi ambae anasema kua: '**Kutokanana kua kimaumbile ni vigumu kwa Mtu mwenye Khofu kupata usingizi na kulala, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua: '*Na (kumbukeni) alipokufunikeni nyie na NuaAsa*' ambayo ni miongoni mwa Miujiza yake ya kupitia na usingizi wa muda mfupi katika wakati huo, kwani kama wangelala moja kwa moja basi bila ya shaka Maadui zao wangewashambulia** '

Na anasema Imam Muhammad Ibn Is-haq kua: '**Amesema Ali Ibn Abi Talib *Radhi* *Allahu Anhu*** kua: '**Tulikua hatuna mpanda Farasi katika vita hivyo isipokua Miqdad Al Aswad. Nami sikuona yeyote yule miongoni mwetu isipokua alikua ni aliekua nimwenye kulala, ila *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alikua chini ya mti akilia na kuomba dua mpaka asubuhi**''

Na mara ya pili ni neno *NuaAsa* limetumika katika ile aya inayozungumzia tukio lililotokea baada ya Vita vya Uhud pale Waislam waliposhindwa baada ya Khalid Ibn Walid kuwaongoza Makafiri na kupata Ushindi kisha Abu Sufyan na Khalid Ibn Walid kurushiana maneno na *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na ushindi wao huo na kisha wakaondoka, na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kuhusiana na wapiganaji wa Upande wa Waislam na wartu wa Mji wa Madina kua:

﴿ثُمَّ أَنزَلَ عَلَيْكُمْ مِّنْ بَعْدِ ٱلْغَمِّ أَمَنَةً نُّعَاساً يَغْشَىٰ طَآئِفَةً مِّنْكُمْ وَطَآئِفَةٌ قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنْفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِٱللَّهِ غَيْرَ ٱلْحَقِّ ظَنَّ ٱلْجَاهِلِيَّةِ يَقُولُونَ هَلْ لَّنَا مِنَ ٱلأَمْرِ مِنْ شَيْءٍ قُلْ إِنَّ ٱلأَمْرَ كُلَّهُ لِلَّهِ يُخْفُونَ فِيۤ أَنْفُسِهِم مَّا لاَ يُبْدُونَ لَكَ يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ ٱلأَمْرِ شَيْءٌ مَّا قُتِلْنَا هَاهُنَا قُلْ لَّوْ كُنْتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ ٱلَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ ٱلْقَتْلُ إِلَىٰ مَضَاجِعِهِمْ وَلِيَبْتَلِيَ ٱللَّهُ مَا فِي صُدُورِكُمْ وَلِيُمَحِّصَ مَا فِي قُلُوبِكُمْ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ﴾

Thumma anzala AAalaykum min baAAdi alghammi amanatan nuAAasan yaghsha ta-ifatan minkum wata-ifatun qad ahammat-hum anfusuhum ya*dh*unnoona biAllahi ghayra alhaqqi *dh*anna aljahiliyyati yaqooloona hal lana mina al-amri min shay-in qul inna al-amra kullahu lillahi yukhfoona fee anfusihim ma la yubdoona laka yaqooloona law kana lana mina al-amri shay-on ma qutilna hahuna qul law kuntum fee buyootikum labaraza alladheena kutiba AAalayhimu alqatlu ila madhajiAAihim waliyabtaliya Allahu ma fee sudoorikum waliyumahhisa ma fee quloobikum waAllahu AAaleemun bidhati alssudoori *(Surat Al Imraan 3:154)*

Tafsir: ***Na kisha akakushushieni juu yenu baada ya kutokua na utulivu (wa kiakili), Amani ya NuaAsa iliyokufunikeni watu miongoni mwenu lakini watu wengine walikuwa wakifikiria nafsi zao (namna ya kujikoa) wakimdhania sivyo Allah, dhana za kijahiliya wakasema: 'Hivi imetuhusu nini sisi jambo hili?'. Waambie (Ewe Muhammad) Jambo hili linamhusu Allah pekee. Walikua wanaficha kwenye Nafsi zao kile ambacho hawataki kukuambia kwa kusema kua: 'Kama ingekua sisi tunakauli juu ya jambo hili basi tusingeuliwa' Waambie kua: 'Kama mngebakia katika majumba yenu basi wale ambao waliokua wameandikiwa kifo wangefika kwenye sehemu waliyoandikiwa Kufa' Ili awajaribu kuhusiana na kilichomo ndani ya vifua vyenu na kuyatoa yaliyomo ndani ya Nyoyo zenu. Na kwa hakika Allah ni mwenye kujua yaliyomo ndani ya Vifua.***

Ambapo kwa upande wa Abd Allah Ibn Abbas anasema kua: '**Baada ya Vita vya Uhud na Abu Sufyan kuondoka basi *Rasul Allah Salallahu A'alayhi wa Salam* akatuma mtu akawaangalie jee Wameelekea wapi Makafiri hao, katika Mji wa Makkah au Madina kushambulia, lakini ikaonekana kua Makafiri hao wamerudi Makkah hivyo Waislam wakapata afueni na Utulivu hivyo *NuaAsa* ikawakumba Waislam hao**'

Ambapo kwa Upande wa Imam Abd Rahman Al Suddi basi yeye nasema kua: '**Wanafiq hawakuweza kujua kama Makafiri wameshinda ama wameshindwa, na hawakuamini ni kwanini Makafiri wa Makkah hawakuuvamia Mji wa Madina hivyo wakawa wanahaha, na ndio maana aya ikasema kua lakini watu wengine waliokua wakifikiria nafsi zao**'

Na akasema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: '***NuaAsa* katika wakati wa Vita hua ni kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* lakini katika wakati wa Sala hua ni kutoka kwa Shaytan.**'

Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi basi yeye anasema kua: '***NuaAsa* katika Vita hua ni kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa sababu usingizi huo humjia mtu katika wakati wa vita pale anapokua ni mwenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee wakati *NuaAsa* katika Sala hua ni wenye kutokana na sababu ya kua mbali na *Allah Subhanah wa Ta'ala***'

Hivyo *NuaAsa* hua ni wenye kumaanisha usingizi wa mapumziko ya mda mfupi baada ya kuchoka kutokanana kua katika mazingira ya hatari na yenye kuchosha iwe mchana au usiku. Kisha baada ya hatua hio ya *NuAas* basi inafuatia hatu ya hali ya usingizi wa *Hujuu* ambao ni wenye kutokana na neno *Hajaa* ambalo ndio lililotumika katika aya ifuatayo:

﴿كَانُواْ قَلِيلاً مِّن ٱللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ۞ وَبِٱلأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ﴾

Kanoo qaleelan mina allayli ma yahjaAAoona; Wabial-ashari hum yastaghfiroona *(Surat Adh Dhariyat 51:17-18)*

Tafsi: ***'Walikua kidoogo tu katika wakati wa Usiku yahjaAAoona, na katika mda wa kabla ya Alfajir walikua wakifanya Istighfar'***

Ambapo ayah hii inayowazungumzia Waislam wenye sifa ya *Muhsinun* yaani wenye kufanya mema kua ni wenye kulala kidogo tu usiku na kisha kuamka na kusali kutokana na Taqwa na Matumaini yao kwa Mola wao, hivyo ayah hii imetumia neno *YahjaAAoona* linalotokana na neno *Hajaa* ambalo hua ni lenye kumaanisha: Kusinzia na Kulala kwa kwa mda mfupi pia kunakotokana na kua katika sehemu yenye ukimya na utulivu wa wakati wa Usiku.

Na baada ya *Hajaa,* ndio inafuatia hali ya usingizi *ya Subatan* ambao tulioanza nao katika kuzungumzia neema ya Usingizi katika aya isemayo *WajaAAalna nawmakum subatan (Surat An Nabaa 78:9)* kisha inafuatia hali ya usingizi wa *Ruquud* ambalo ni neno linalotokana na neno *Raqada* ambalo ni lenye kumaanisha Kulala kwa Mda mrefu au Kupumzika kwa mda mrefu, Kua Mchovu sana kiasi ya kua hakuna kinachotakikana katika hali hio isipokua Kulala tu. Ambapo neno *Raqada* ndio lililotoa neno *Marqad* ambalo maana yake hua ni Kitanda, Seehemu ya Kulalia, na pia humaanisha Kaburi.

Neno hili limetumika katika *Surat Al Qahf* katika kuelezea hali ya kulala ya watu ambao wanajulikana kama *As-hab Al Qahf* ambao ni *Maksalmina, Tamlikha, Martunas, Baynunas, Saarnunas, Zunwanas, Kashfitatnunas* na Mbwa wao ambae ni mwenye kuitwa *Qitmiir,* ambapo *Allah Subhanaha wa Ta'ala* anatuelezea hali yao hio ya Kulala ilivyokua kwa kusema:

﴿وَتَحْسَبُهُمْ أَيْقَاظاً وَهُمْ رُقُودٌ وَنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ ٱلْيَمِينِ وَذَاتَ ٱلشِّمَالِ وَكَلْبُهُمْ بَاسِطٌ ذِرَاعَيْهِ بِٱلْوَصِيدِ لَوِ ٱطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَاراً وَلَمُلِئْتَ مِنْهُمْ رُعْباً﴾

Watahsabuhum ayqadhan wahum ruqoodun wanuqallibuhum dhata alyameeni wadhata alshshimali wakalbuhum basitun dhiraAAayhi bialwaseedi lawi ittalaAAta AAalayhim lawallayta minhum firaran walamuli/ta minhum ruAAban *(Surat Qahf 18:18)*

Tafsir: ***Na kama ungewaona basi ungedhani kua wako macho, huku wakiwa katika Ruquudun. Na tuliwageuza kuliani mwao na kushotoni mwao na Mbwa wao akiwa amenyoosha miguu yake kwenye Mlango wa kuingilia (Pangoni) Kama ungewaona basi ungerudi nyuma na kukimbia kutokana kupigwa na mshangao mkubwa sana.***

﴿وَلَبِثُواْ فِي كَهْفِهِمْ ثَلاثَ مِئَةٍ سِنِينَ وَٱزْدَادُواْ تِسْعاً﴾

Walabithoo fee kahfihim thalatha mi-atin sineena waizdadoo tisAAan *(Surat Al Qahf 18:25)*

Tafsir: ***'Na walikaa kwenye Pango lao kwa miaka mia tatu na uongeze (miaka) tisa'***

Ambapo tunaona kua aya inasema kua Watu hawa walilala kwa miaka 309 huku macho yao yakiwa wazi. Aya vile vile zinatuwekea wazi pia umuhimu wa kugeuka wakati wa Kulala, kwani ingwa tumesema kua Misuli ya Mwili hua inapumzika kufanya kazi na kuregea katika wakati wa kulala lakini kuna hisia ambazo hua zinafanya kazi kwa asilimia ndogo sana, kama hisia ya Maumivu na kusikia, na ndio maana mtu unapolala basi ukichoka upande mmoja hua unageuza mwili wako bila ya kujijua na kulalia upande mwengine wa mwili wako, na hivyo hua unafanya si kwa amri yako bali ni kutokana na amri ya Mola wako ambae ndie anaekugeuza upande mwengine kulingana na makadirio yake aliyokukadiria kutokana na ukamilifu wa maumbile yako.

Neno *Ruqud* pia limetumiwa na aya ya *Surat Yasin* 36:52 basi nayo pia imetumia neno *Raqada* katika hali ya *Marqadina* yaani Malazi au Vitanda vyetu vya kupumzikia pale ziliposema:

﴿قَالُواْ يٰوَيْلَنَا مَن بَعَثَنَا مِن مَّرْقَدِنَا هَذَا مَا وَعَدَ ٱلرَّحْمٰنُ وَصَدَقَ ٱلْمُرْسَلُونَ﴾

Qaloo ya waylana man baAAathana min marqadina hadha ma waAAada alrrahmanu wasadaqa almursaloona*(Surat Yasin 36:52)*

Tafsir: ***Watakaposema watu hao: 'Ole wetu sisi, Nini Nani alietufufua kutoka kwenye sehemu yetu ya kupumzikia' (ambapo nao wataambiwa): 'Hiki ndio kile ambacho Mwingi wa Rehma alikuahidini na walichosadikisha Mitume'***

Ambapo anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Baina ya Kupulizwa Baragumu kutakua na kipindi cha Arubaini Abu Hurayra *Radhi Allahu Anhu* akamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema kua: *Ya Rasul Allah* hivi Unamaanisha Arubaini Masiku au?'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Siwezi kusema chochote zaid'**

Masahaba Wakauliza: 'Unamaanisha Arubaini miezi?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La siwezi kusema'**

Masahaba wakauliza: 'Arubaini Miaka?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Siwezi kusema chochote, lakini baada ya hapo Allah atajaalia Maji kushuka kutoka Mbinguni na kisha Watu watachipua kama inavyochipua Mimea, kwani ni kitu kimoja tu cha Ibn Adam ambacho hakitooza ambacho ni kimfupa kidogo cha mwisho cha Uti wa mgongo, ambacho ndicho kitakachochipua Ibn Adam kutokana nacho katika Siku ya Malipo'** *(Sahih Muslim)*

Naam..hii ni hadith ambayo inatuelezea kuhusiana na tukio la Kupulizwa kwa Baragumu mara 2 yaani katika siku ya Kiama. Ambapo anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* na Ubay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Baragumu litapulizwa mara mbili, ambapo litakapopulizwa mara ya kwanza basi adhabu za Kaburi zitasitishwa na hivyo Watu watalala usingizi hadi litakapopigwa kwa mara ya pili ndio watu wataamka na kutakua na kipindi cha miaka arubaini baina yake**'

Hivyo ni baadhi ya vithibitisho vinavyothibitisha aina za usingizi, muhimu wake na manufaa yake juu yetu kwa kulingana na mtizamo wa Qur'an na kisayansi, ambapo tunapoangalia kwa upande wa

Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi tunaona kua zimetajwa aina tatu za usingizi wa mchana pale aliposema: '**Kulala asubuhi mapema hua ni kuusaliti ujahilia, kulala mchana hua ni sahih na kulala jioni hua hua ujinga**' *(Imam Ibn Hajar Al Asqalani katika Fat-h Al Bar)*

Aina hizo za Usingizi ni *Ghaylula* ambao ni usingizi wa baada ya Sala ya Alfajir ambao ni *makruh* na haupendekezwi kwani husababishia kupungua kwa riziki kutokana na kua huo na wakati wa kujishughulisha kwa matayarisho ya kutafuta riziki. Na kuna Usingizi uitwao Qaylula ambao ni Usingizi aliokua akiutumia *Rasul Allah Salallahu Alayhi Salam* kwa ajili ya kumuwezesha kuamka usiku kusali *Salat Tahajjud*.

Huu hua ni usingizi wa saa moja baada ya *Salat Al Dhuhur* hua si wa muda mrefu, kwani humalizika kabla ya kuingia *Salat Al Asr* usingizi huu huzidisha umakini wa Mwili na Ufaham wa mtu. Halafu kuna *Faylula* ambao ni usingizi wa baada ya *Salat Al Asr* mpaka Maghrib ambao huifanya siku kua fupi na hivyo ni siku hio hua ni siku isiyokua na faida kwa kutowezekana kuzalisha chochote ndani yake

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatubainishia umuhimu wa Usingizi kua tumejaaliwa kua nao kwa sababu ya kua ni wenye kuipumzisha Miili ya viumbe ili iwe na nguvu na uwezo zaid kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake hapa Ulimwenguni kwa manufaa ya kiakhera kwa kusema na tukaujaalia Usiku kua ni *Libas*

﴿وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتاً ۞ وَجَعَلْنَا ٱللَّيْلَ لِبَاساً﴾

WajaAAaln<u>a</u> nawmakum sub<u>a</u>t<u>a</u>n WajaAAaln<u>a</u> allayla lib<u>a</u>s<u>a</u>n; *(Surat An Nabaa 78:9-10)*

Tafsir: ***Na tukajaalia Usingizi kua ni Pumziko, Na tukaujaalia Usiku kua ni Libas (Vazi).***

Ambapo tunapoangalia neno *Libas* basi tunaona kua ni neno lililotumika pia katika aya nyingi ikiwemo katika aya zisemayo:

﴿هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَأَنتُمْ لِبَاسٌ لَّهُنَّ﴾

Hunna lib<u>a</u>sun lakum waantum lib<u>a</u>sun lahunna *(Surat Al Baqara 2:187)*

Tafsir: ***Wao (Wake zenu) ni Lîbas kwenu na nyie (Waume zao) ni Lîbas kwao.***

Neno *Lîbas* kwa kiarabu lina maana ya Stara, Hifadhi, Nguo au Vazi, na kama inavyojulikana kazi ya Vazi ni kuvaliwa ili Kuulinda na Kuuhifadhi mwili wa *Bani Adam* na athari za nje kama vile jua, baridi, mvua n.k, kusitiri sehemu za siri ambazo ni aibu kuzionesha, Kuupendezesha mwili n,k basi ndio vile vile, wanavyositiriana, wanavyoridhishana, wanavyopeana utulivu na kuheshimiana na kulindana Mume na Mke kutokana na matamanio ya nje yaliyokatazwa, na hivyo kuwapelekea kusaidiana si kutokana na athari za nje tu bali na katika kumcha Mola wao pale wanapotimiza matamanio hayo katika njia inayoruhusika kisharia.

Ingawa Allah *Subhanahu wa Ta'ala* amewajaalia *Bani Adam, Lîbas* kua kama Stara na pambo la Miili yao, lakini pia amewajaalia *Lîbas* ya *Taqwa* ambayo ni pambo la *Nafsi* na hua ni *Lîbas* bora zaid kwani hua ni yenye kuupa Moyo na Nafsi utulivu zaid kama zinavyosema aya.

﴿يَٰبَنِيٓ آدَمَ قَدۡ أَنزَلۡنَا عَلَيۡكُمۡ لِبَاسٗا يُوَارِي سَوۡءَٰتِكُمۡ وَرِيشٗا وَلِبَاسُ ٱلتَّقۡوَىٰ ذَٰلِكَ خَيۡرٞۚ ذَٰلِكَ مِنۡ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ لَعَلَّهُمۡ يَذَّكَّرُونَ﴾

Ya banee adama qad anzalna AAalaykum libasan yuwaree saw-atikum wareeshan walibasu alttaqwa dhalika khayrun dhalika min ayati Allahi laAAallahum yadhdhakkaroona *(Surat Al A'raf 7:26)*

Tafsir: ***Enyi Bani Adam! Tumekushushieni Lîbas (Mavazi) juu yenu ili mjifunike na pia kua kama Rish (Mapambo); na Lîbas (Mavazi) ya Taqwa, ni bora zaid. Hizo ni miongoni mwa aya (Dalili, alama, ushahidi, nk) za Allah ili mpate kukumbuka.***

Hivyo basi tunapoangalia kwa upande wa Usiku kua ni *Libas* kama isemavyo aya*:*

﴿وَجَعَلۡنَا ٱلَّيۡلَ لِبَاسٗا﴾

WajaAAalna allayla libasan; *(Surat An Nabaa 78:9)*

Tafsir: ***Na tukaujaalia Usiku kua ni Libas***

Hapa tunaona kua aya inamaanisha kua Usiku mbali ya kua umejaaliwa kua ni Vazi na Pambo la Dunia ambalo linawatofautishia Viumbe wanaoishi Ulimwenguni ili maumbile yao yaweze kujua kuhusiana na mda wanaoishi ndani yake na mabadiliko ya nyakati na mambo yao mbali mbali yanayotokea katika maisha yao, lakini pia Usiku umekua ni *Libasi* pia kwa kumaanisha kua ni sehemu ya Kituliza na Kuipumzisha Miili ya viumbe wanaoishi Ulimwenguni na Kupata Stara na Hifadhi ya Miili yao na Ufaham wao ndani ya Makazi yao.

Kwani unapoingia Usiku, *Melatonin* zinazalishwa na mtu unahisi usingizi na kuanza kulala basi mara tu unapoingia kwenye usingizi Mwili wako wote hua ni wenye kupunguza kasi ya ufanyaji kazi wa viungo vyake na kuvipumzisha, kwa mfano unapolala basi Ufaham wako hufuta kila kitu ambacho hakina maana wala umuhimu ndani yake, na kubakisha yale yenye maana na umuhimu tu ndani yake ambayo nayo huyahifadhi kwa ajili ya kuja kuyakumbuka baadae, na ndio maana wakati muhimu wa kuhifadhi kitu akilini hususan kwa wanafunzi wafanyao Mitihani basi hua si kabla ya kulala bali hua baada ya kuamka mapema kabla ya Alfajir.

Unapolala pia Misuli husitisha ufanyaji kazi wake na kupumzika, Ubongo huongeza uzalishwaji wa Kemikali ndani ya mwili ikiwemo zile zenye asili ya *Protein za Cytokines* ambazo ni zenye kusimamia Ulinzi wa kipigana na maradhi mbali mbali na uponeshaji wa ndani na nje ya mwili wako, kwani bila ya kuzalishwa kwake basi kinga ya mwili wako hua dhaifu na katika kipindi hiki ambacho umelala ndio pia mwili wako unakua kimaumbile kwani ndani ya mwili wako mnazalishwa kemikali za kuukuza mwili kimaumbile kutokana na *Pituitary Gland*, na hapo hapo huachiwa Kemikali za kuzuia hisia za kutaka kujisaidia na hivyo kukupelekea kutotaka kuenda chooni mara kwa mara, kwa ajili ya kujisaidia wakati wa Usiku. n.k

Hivyo kimaumbile Usingizi una faida nyingi sana na ndio maanaukawa unahesabika kua ni miongoni mwa haki za mwili wa Ibd Adam kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumwambia Abd Allah Ibn Amr *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua anapenda kusali usiku kucha kua: '**Sali na pia Lala, kwani mwili wako una haki yake juu yako**' *(Sahih Bukhari)* na akasema tena

kua: '**Yeyote yule atakaehisi usingizi wakati anasali, basi na akalale mpaka umtoke usingizi wake, kwani kusali huku akiwa na usingizi mtu hua hajui kama anaomba msamaha au anaiombea mabaya Nafsi yake'** *(Sahih Bukhari)*

Hivyo Usingizi ni Silaha yako ya Kimaumbile kwa ajili ya Manufaa ya Mwili wako na Ufaham wako, na inakubidi kuitumia ipasavyo. Kwani usipoituima ipasavyo basi hua umeuvunjia haki yake Mwili wako na Ufaham wao, na hivyo hua ni sawa Upanga usiokua na Makali, yaani hua ni mwenye kukosa Afya na Umakini wa Mwili wako kutokana na kuchoka na kutokua na mapumziko ya kutosha ya kiufaham na kimwili.

Na tunapozungumzia kuhusiana na kuutumia ipasavyo Usingizi wako kwa ajili ya Manufaa yako basi hua ni kama alivyosema *Mujaddid Ad Din Hujjat Ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammahd Al Ghazali ambae amesema: '**Faham kua Usiku na Mchana unajumuisha masaa 24: Hivyo usilale zaidi ya masaa manane, kwani hayo hua yanatosheleza kwa ajili yako. Na hii ni kwa mfano kama ulikua umeandikiwa uishi miaka 60 basi utakua umetumia miaka 20 ambayo ni robo tatu ya uhai wako.**'

Hio ni kuhusiana na umuhimu wa neema ya Usingizi na Usiku kwa Viumbe ambayo tumejaaliwa na Muumba kama ilivyosema mwenyewe ndani ya Qur'an, na hivyo kututhibitishia kua yuko Muumba wa Kila Kitu ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo tumalizie kuhusiana na Mchana kama ilivyolezewa na Aya ya *11 ya Surat An Nabaa* ambayo inasema:

﴿وَجَعَلْنَا ٱلنَّهَارَ مَعَاشاً﴾

WajaAAaln<u>a</u> alnnah<u>a</u>ra maAA<u>a</u>sh<u>a</u>n*; (Surat An Nabaa 78:11)*

*Tafsir: **Na Tukajaalia Mchana kua ni wa Maisha (kutafutia)***

Kama tulivyoona kua aya mbili zilizofuata kabla ya hii zilikua zinazungumzia Usingizi na Usiku zimetumia maneno *Subata* na *Libasa* kumaanisha kua Nyakati hizo ni maalum kwa ajili ya Stara, Hifadhi, Utulivu na Mapumziko, ambapo aya hii inazungumzia Mchana imetumia neno *MaaAshan.*

Neno *MaaAshan* linatokana na neno *Aasha* ambalo hua ni lenye kumaanisha Kuishi, Kuishi maisha kwa kutumaia njia fulani, Kutumia mda wa maisha kwa kupitia njia au mfumo fulani, ambapo neno *MaaAshan* hua linamaanisha Maisha, Kuhangaikia mahitaji ya Maisha au wakati wa kutafutia riziki.

Ama kwa upande wa Imam Sahl Al Tustari basi yeye anasema kuhusiana na *MaaAshan* kua: '**Hii inamanisha kua ni Nuru ya Nyoyo kupitia katika Kumkumbuka kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ndio mahitaji ya Roho na Nafsi na Akili, Kama ilivyokua kwa mahitaji ya Malaika kwani wao Maisha yao ni katika Dhikr kiasi ya kua kama wakizuiwa kufanya Dhikr basi wataangamia, lakini tunapozungumzia aina nyengine ya maisha basi hua ni kama wanavyoishi watu wengine wa kawaida kama kula kunywa, kujistiri n,k.**

Tunaporudi katika Kisa chetu basi tunaoa kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamuelezea Mtume wake Salallahu Alayhi wa Salam kuhusiana na Watu hao kiasi ya kua Mimi na wewe tunaosoma Tunajihisi kua kama tumeingia kwenye Pango na kuwaona.

Kwani Anasema kua Ingawa Watu Hawa walikua Wamelala lakini hata hivyo Muonekano wao ulikua ni wa Kushangaza na Kuogopesha na Kushtua.

Na bila ya shaka Kama Muumba ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua: **Kama Ungewaona basi Ungewatizama mara moja tu na kisha Ukageuka na Kukimbia kwa kasi sana kutoka kwenye Pango hilo kutokana na Muoenekano wao wa Kutisha, basi tujue kua Muonekano wao ulikua ni wa Kushtua na Kutosha kweli.**

Ama kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Sahal Al Tustari basi yeye anatuambia kuhusiana nah ai ya watu haw ana muonekano wao kua: **'Ilikua kama utawaangalia kwa mtizamo wa Nafsi yako basi ungeingiwa na khofu na kukimbia kutokana na hali ya kutisha kwao, lakini kama ungekua unawaangalia kutokana na mtizamo wa kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ungeona na kujua uhakika wa kuwepo kwa umoja wa Muumba'**

Na kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Al Qurtubi basi yeye anasema kuhusiana na Muonekano wao watu hao kua: **'Kutokana na kua Walikua Wamelala huku Macho yao yako wazi basi hiki ni kitu ambacho ni chenye kushtua**.' Lakini mbali ya hivyo basi inawezekana ikawa ni katika hali nyengine yenye kutisha zaidi ya muonekano wao ndio Unaoshtua..*w Allahu Aalam.*

Ambapo kuhusiana na Mbwa basi amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Yeyote yule atakaefuga Mbwa, isipokua kwa ajili ya Kuwindia, kwa ajili ya Ulinzi wa Mifugo (Na Nyumbani) na Shambani basi atakua ni mwenye kupunguziwa (Qayrat) vipimo viwili kutoka katika Mema yake ya kila siku.'**

Ambapo kwa upande mwengine basi na tujiulize kama Aya imempandisha Darja Mbwa na kumtaja kutokana kua ni mwenye kua pamoja na Waja wema hawa, basi jee ni kipi kilichotufanya mimi nawe kutotaka kua karibu na Waja wema?

Na ndio maana akasema Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Kua ni Mwenye Ilmu kama unaweza, Kama huwezi basi kua ni mwenye kutafuta Ilm, Kama huwezi basi wapende wale wenye kutoa na kutafuta Ilm, na kama huwezi hata hivyo basi usiwachukie wenye kutoa na kutafuta Ilm '**

Hivyo Wakati kina Tamlikha wakiwa katika Hali ya *Ruquud* yaani Kulala Usingizi mzito sana kiasi ya kua haiwezekani kusikia wala kuhisis kitu chochote kwa muda mrefu sana.

Basi tunarudi kwa upande wa Mfalme Duqyanus ambae katika Siku Waliyotoroka kina Tamlikha basi yeye asubuhi yake alikua anasafari kuelekea kwenye moja kati ya Sherehe za Sikukuu za Watu wake Na hivyo Jioni aliporudi Kwenye Kasri lake na kuwaulizia kina Tamlikha basi akapata habari ya kua Vijana wake hao wamepata Mungu mwengine zaid yake Duqyanus na hivyo wamkua waasi na wameamua kuuhama Mji.

Ambapo baada ya Duqyanus kusikia habari hio basi nae akakusanya Jeshi lake ambalo lilikua na wingi mkubwa sana wa Wapiganaji waliopanda Farasi kwani walikua ni watu 80,000, Ambao hawa walikua ni maalum kwa ajili ya kuatafuta kina Tamlikha na lazima wapatikane kwa njia moja au Nyengine.

Kwani kama hawakupatikana basi tayari Uwezo wake kama Mungu unakua umeshaingia dosari kubwa sana. Hivyo Jeshi hilo lililokua likiongozwa na Wataalamu Mahiri wa kusoma Athari za Nyayo za Farasi na za Ibn Adam, likaanza safari yake kwa kutafuta Nyayo zao hadi wakazipata.

Na baada ya kuzipata wakaanza kuzifuatilia hatua baada ya hatua hadi wakafikia kwenye Mlima ambao waliupanda kina Tamlikha na kukutana na Jabali na kisha wakaliona Al Kahf.

Walipolikaribia Al Kahf hilo wakamuona mbwa ambae aliekua amelala kwenye Mlango wa Pango hilo na wakaangalia vizuri kwa Ndani yake basi Wakawaonga Fityatun hao wakiwa wamelalala fofofo! Na Wataalamu hao walipowaona watu hao basi Wakashtuka kwa Namna walivyokua Wamelala.

Na kisha kimya kimya wakarudi nyuma na kumpelekea Habari Duqyanus ambae alikua tayari ameshapiga Kambi chini ya Mlima huo. Hivyo alipopata habari ya Kuonekana kwao na muonekano wao wa kushtua, basi nae akaamua bora akawaangalie ili kuhakikisha kua Jee ndio wao ama la. Hivyo Duqyanus akapanda juu ya Mlima huo na Jeshi lake taratibu kimya kimya ili wasiwaamshe Vijana hao na kisha wakakimbilia ndani zaid Pangoni au kujificha.

Wakapanda hadi wakafika Pangoni ambapo Duqyanus akasogelea Mlango wa Pango hilo na kumuona Mbwa alielala na kisha alipoangalia ndani akawaona kina Tamlikha wakiwa wamelala usingizi Mzito sana huku macho yao yakiwa wazi.

Duqyanus akasita huku akiwa amepigwa na Bumbuwazi. Hivyo Duqyanus akapanda juu ya Mlima huo na Jeshi lake taratibu kimya kimya ili wasiwaamshe Vijana hao na kisha wakakimbilia ndani zaid Pangoni au kujificha, kwani alikua haamini kua *As-hab Al Kahf au Fityatun* hao walikua wamelala Ama la, kwani Macho yao wazi lakini wametulia Tulii.

Na kisha alipozindukana kutokana na Bumbuwazi lake akashuka chini na kuwaambia watu wake: Hawa Vijana kutokana na Kunisaliti kwao basi nitawapa Adhabu ambayo hawakuwahi kuiona. Na haitokua Adhabu nyengine yeyote isipokua kujenga Ukuta Usiku Huu Huu ili kuuziba Mlango wa Pango kabla hawajaamka ili wasitoke tena.

Hivyo kanileteeni Mafundi Waashi na vifaa vyao kamilifu waujenge Ukuta haraka sana leo leo sasa hivi na hapa tukumbuke kua tunamzungumzia Mfalme Duqyanus ni Mfalme anaehesabiwa na kujihesabu kua ni Mungu hivyo amri yake haidharauliki, kwa hivyo wakaitwa Wajenzi wa Mfalme na vifaa vyao na happ hapo ukaanza kujengwa Ukuta kwa ajili ya Kuliziba Pango hilo, huku vijana hao wakiwa wamelala ndani yake hawana hata habari, na wachilia mbali wao wenyewe kua si wenye kuhisi wala kusikia lakini Mbwa wao pia ambae ni Mnyama mwenye kusikia Sauti mara 4 zaid ya Ibn Adam basi nae pia hakuweza kusikia Sauti yeyote.

Hivyo Ukuta huo ukajengwa na kumalizika, na baada ya kumalizika Mfalme Duqyanus akatabasam kwa tabasam la Ushindi usiokua na Upinzani huku akiwa ameridhika sana na hivyo akaskika akisema kuwaambia watu wake: **‘Hawa Vijana wamesema kua Mimi sio Mungu wao, na Mungu wao Yuko Juu Mbinguni. Hivyo Basi wacha tuone huyo Mungu wao aliekua Mbiguni ashuke chini kisha aje kuwatoa Vijana wake hawa kama kweli wao ni wasema kweli.’** Na kisha Mfalme Duqyanus akaondoka na Jeshi lake na kurudi katika Kasri lake na kuendelea na Majukumu ya Mamalaka yake katika eneo la Ardhi yake.

Baada ya kupita mda usiojulikana basi vijana waliokua Pangoni yaani Tamlikha na wenzake wakazindukana bila ya kujua walikua wamelala kwa mda gani kwani fikiria zao ni kua wamelala jana usiku na kuamka asubuhi ya siku ya pili. Lakini sasa walipoamka wakashtuka na kujihisi kua wameshachelewa kufanya Ibada kwa ajili ya Mola wao kutokana na machofu ya safari yaliyowapelekea kupata Usingizi wao mzito sana.

Lakini kumbe kuamka kwao kulikua ni kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimtuma Malaika Jibril akawapulizia watu hao Roho zao na wakaamka baada ya kuchomoza Jua, kwani walikua wameshalala kwa miaka 309 bila ya Kujijua.

Ambapo vijana hawa wakiongozwa na Tamlikha walipoamka na kuona Mwangaza wa Jua basi walisema huku wakilaumiana kua:

‘**Ya Allah Hakika Sisi tumeshazikosa Ibada za Usiku wa Jana kwa ajili ya Mola wetu, hivyo wacha tuwahi kukimbilia kwenye chemchem uliyopo Mlangoni tujisafishe tuwe Wasafi ili Tumuabudu Mola wetu.’**

Hivyo wakasimama na kikimbilia kwenye Chem chem ya Maji waliyokunywa walipowasili kwenye Pango hilo, Lakini hata hivyo Walipofika kwenye Chemchem hio basi wakakuta kitu ambacho hawakukitegemea.

Kwani sehemu iliiyokua na Chemchem hio ilikua Kavu na imejaa Vumbo Juu yake kama kwamba haikua sehemu hio ndio iloyokua imejaa Maji meupe na matamu walipowadia kwenye Pango hilo hapo kabla. Na bila ya shaka walipoangalia Ule Mti uliokua una Matunda ambayo walichuma na kuyala basi waliuona Mti huo kua Mkavuu kama Kuni na hauna hata dalili ya kua ulikua na Majani wacha mbali Matunda.

Vijana Hao Wakatizamna kwa Mshangao kwani wamejikuta katika hali ya Maajabu ambayo hawakuitegemea wala hawakuwahi kuisikia ndani ya Maisha yao yote katika Kuishi kwao Duniani mbali ya kua Waliku ni wenye Ilm kubwa Sana.

Hivyo wakaambiana kwa kusema; ‘**Haya ni Maajabu yalioje, inakujae hadi Chemchem Ikawa ni yenye kukauka ndani ya Usiku Mmoja na ardhi yake kua kavu namna hii na huu Mti kua ni wenye Kukauka kama uliokua Jangwani kwa miaka na miaka?**’

Kwani baada ya kuona kua wamekosa Maji na wamekosa Chakula pia basi hapo hapo wakaanza kujihisi kua na hali ya kuona njaa na kutokana na hali ya Mazingira yao basi Wakaona kua kitu muhimu kuliko yote kwa hali waliyokua nayo ni kua Lazima wapate chakula kwanza japo kidogo.

Hivyo wakakaa na kuamua kua mmoja wao atoke ili aende Mjini akanunue chakula kutokana na baadhi ya Pesa walizokua nazo. Lakini hapo hapo wakawa ni wenye wasiwasi na hivyo wakaulizana: Lakini Jee Sisi Tumelala kwa mda gani? Au tumelala kwa mda mrefu zaid mbona mazingira yamebadilika na tunaona njaa Sana kiasi hiki pia?

Ambapo Baadhi yao wakasema: **Inawezakana kua tumelala kwa zaidi ya siku moja au zaid kwa machovu ya Safari katika Kuimbia kwetu ambapo kutokana na Ukubwa wa Imani yao na kumtegemea Mola wao basi wakasema**:

‘Kwa Hakika hakuna Miongoni mwetu anaejua ni kwa mda gani Sisi tumekua ni wenye kulala hapa Bali ni Mola wetu Pekee ndie anaejua kwa mda gani sisi tumekua ni wenye kulala hapa’

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaielezea hali ya mazingira ilivyokua ndani ya Pango hilo katika wakati wa tukio kwa kusema ndani ya Qur'an kua:

﴿وَكَذٰلِكَ بَعَثْنَاهُمْ لِيَتَسَآءَلُوا بَيْنَهُمْ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ كَم لَبِثْتُمْ قَالُواْ لَبِثْنَا يَوْماً أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ قَالُواْ رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ فَٱبْعَثُواْ أَحَدَكُمْ بِوَرِقِكُمْ هَـٰذِهِ إِلَىٰ ٱلْمَدِينَةِ فَلْيَنْظُرْ أَيُّهَآ أَزْكَىٰ طَعَاماً فَلْيَأْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِّنْهُ وَلْيَتَلَطَّفْ وَلاَ يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَداً﴾

Waka<u>dha</u>lika baAAathn<u>a</u>hum liyatas<u>a</u>aloo baynahum q<u>a</u>la q<u>a</u>-ilun minhum kam labithtum q<u>a</u>loo labithn<u>a</u> yawman aw baAA<u>d</u>a yawmin q<u>a</u>loo rabbukum aAAlamu bim<u>a</u> labithtum faibAAathoo a<u>h</u>adakum biwariqikum h<u>adh</u>ihi il<u>a</u> almadeenati falyan<u>*dh*</u>ur ayyuh<u>a</u> azk<u>a</u> <u>t</u>aAA<u>a</u>man falya/tikum birizqin minhu <u>walyatalattaf</u> wal<u>a</u> yushAAiranna bikum a<u>h</u>ad<u>a</u>n*(Surat Al Kahf 18:19)***

Tafsir: ***Na Kadhalika (Kama tulivyowalaza kwa Mda mrefu basi ndivyo pia) Tukawamsha, Ili wapate Kuulizana baina yao Akasema mwenye Kusema Miongoni mwao Hivi Jee Tumelala kwa mda gani? Wakasema: 'Tumelala kwa Siku Moja au Baadhi tu ya Wakati wa siku Moja' wakasema : 'Mola wenu ndie ajuae Kuhusiana na Mlivyolala Hivyo Mtumeni mmoja wenu Pamoja na Fedha yenu hii Kuelekea Mjini Aangalie Ni kipi Chakula Bora cha Halali zaid Ili Akuleteeni Kutokana nayo Riziki hio Na Wacha Awe Makini Wala Asijue Mtu yeyote kuhusiana nanyi.***

Kwa upande mwengine tunaona kua aya yetu hii imetumia neno lisemalo *Walyatalattaf*. Ambalo ni lenye kutokana na neno *Latif*. Na Neno *Latif* maana yake hua ni Kua Makarimu, Mpole, Mtaratibu,Kua Makini na kitu katika kukiangalia au kukihudumia ili kisije kujaribika, Kua na Mtizamo Mpana na pia humaanisha Mtu anaefaham.

Hivyo neno *Walyatalattaf* hua linamaanisha na Mtu husika anatakiwa awe na umakini, tahadhari na awe na Ukarimu na upole.

Na hivi Ndivyo walivyohusiana Kina Tamlikha kua Mtu atakaetoka kuenda mjini basi Awe Na Tahdhari kubwa na awe mpole asije akasababisha Matatizo yatakayopelekea kuwasaliti wenzake n.k.

Kwani tumelitafsiri neno hili si kwa ajili ya kujua maana tu baki poa kwa ajili ya kukumbushana kua neno hili Ndio neno ambalo liko Katikati ya Qur'an

Yaani Mas-haf nzima ukitaka kuangalia na kuigawa nusu kwa nusu basi kati kati yake hua ni kwenye neno hili *Walyatalattaf*.

Kwani anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr Al Ansari Al Qurtubi kua: '**Ama kuhusiana na idadi ya Herufi zake na Juzuu basi amesema Salam Al Himani kua: Al Hajjaj Ibn Yusuf aliwakusanya Wasomaji wa Qur'an, Waliohifadhi na Waandishi na Kuwahoji, kwa kusema jee katika Qur'an mna Herufi ngapi?**

Nami nilikuwemo kwenye wenye Kuulizwa hivyo tukazihesabu na kukubaliana kua Qur'an ina herufi 340,740 Kisha Hajjaj Ibn Yusuf akaniuliza Jee ni Herufi Gani inamalizia Sehemu ya Mwanzo ya Katikati ya Qur'an nami nikasema ni katika *Surat Al Kahf* katika herufi *Fe* ya neno *Walyatallataf* :

﴿وَلْيَتَلَطَّفْ﴾

Walyatallataf *(Surat Al Kahf 18:19)*

Tafsir: ***Na wacha awe Makini kwa ukarimu.***

Ambapo neno hili lina herufi 7, na herufi *Waw, Lam, Ya na Ta* ziko katika nusu ya kwanza ya Qur'an na herufi *Lam,Tta na Fa* ziko kwenye nusu ya pili ya Qur'an.

Akaniuliza Niambie kuhusiana na Sehemu zake 3 nasi tukamwambia inaanzia mwanzoni mwa *Surat Tawba* 9:10, ya pili mwanzoni mwa *Surat Ash Shuara* 26:100 na ya tatu ni kuanzia hapo mpaka mwisho wa Qur'an.

Hivyo aya za *Surat Al Kahf* zinaendelea kutuelezea kwanini Watu hawa wa As-hab Al kahf walitahadharishana kabla ya Tamlikha kutoka nje ya Pango kwa kusema kua:

﴿ إِنَّهُمْ إِن يَظْهَرُواْ عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِى مِلَّتِهِمْ وَلَن تُفْلِحُوٓاْ إِذاً أَبَداً ﴾

Innahum in ya*dh*haroo AAalaykum yarjumookum aw yuAAeedookum fee millatihim walan tuflihoo ithan abadan*(Surat Al Kahf 18:20)*

Tafsir: ***Kwani wakijua kuhusiana nanyi basi watakupigeni Mawe au watakurudisheni nyinyi katika Dini yao na hivyo kamwe hamtokua ni wenye kufuzu.***

Hivyo Aya zinatuonesha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anadhihirisha kua ni kutokana na Mamlaka yake, Uwezo wake, Makadirio yake na kila Sifa yake iliyo njema kua ndio kulikopelekea Kuwalaza Watu hawa wa *As-hab Al Kahf* na kutokana nazo pia Sifa zake hizo Tukufu basi ndio alivyowaamsha baada ya kulala usingizi mzito unaofanana na kama wa Kifo. Ambapo tunapoiangalia aya basi pia tunaona kua imesema kua:

Waka*dha*lika baAAathn*a*hum liyatas*a*aloo baynahum - ***Na Kadhalika (Kama tulivyowalaza kwa Mda mrefu basi ndivyo pia) Tukawamsha Ili wapate Kuulizana baina yao.***

Ambapo kwenye hili neno *Liyatasaalu* mwanzoni mwake mna Herufi *Lam* ambapo hii inajulikana kama *Lam al Sayrurah* yaani Lam ya Kuashiria Muendelezo wa tukio Ambapo herufi *Lam* hii pia hua inajulikana kama *Lam Al Aqibah* yaani ya Hakiba. Hivyo Herufi Hii ya *Lam* iliyotumika hapa hua sio *Lam Al Sababiyah* - Yaani *Lam* Yenye kuonesha Sababu. Na kwa kua hii si *Lam Al Sababiyah* basi maneno haya hua hayamaanishia kua Kuamshwa Kwa Sababu Waulizane. *La.*

Kwa sababu hilo sio lengo lilikousudiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua watu hawa walale kisha waamke waulizane kuhusiana na mda waliolala. Na kwa maana hio basi Wanazuoni wakasema kua hii ni *Lam Al Sayrurah* yaani *Lam* ya Muendelezo wa Kinachofuatia katika Tukio Husika. Na hivyo hua Inamaanisha kua Waliamshwa ili waate Kuendelea Miujiza ya Ndani ya kisa chao baada ya kulala kwao na kuamka kwao. Nadhani Tumefahamiana.

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kuwaelezea watu hawa kisa chao basi tunaona kua bado anatilia mkazo na kututhibitishia juu ya Ucha Mungu watu hawa na Umakini wao na Tahadhari katika kitu chao wakifanyacho kwa ajili ya Mola Wao. Na ndio maana Walipotahamaki kuhusiana na hali

ya njaa waliyokua nayo basi walishauriana kua wamtume mtu mmoja miongoni mwao aende Mjini kwa kunyatia ili asije akajulikana.

Na akishafika huko basi awe Makini pia kwa kutakiwa kununua Chakula chenye sifa ya *Azka Ta'aama* yaani Chakula Kilicho Bora na Kitukufu kwa Uzuri, Utamu na Uhalali wake..

Aya yetu hii tunaoiona kua imetumia neno *Wariqikum* litokanano na neno *Waraqa* ambalo Kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kuchipua au Kutoa Majani kwa Mti.

Neno *Waraqa* ndio lililotoa neno *Warqun* ambalo hua linamaanisha Majani, Waraka au Kurasa ua Karatasi, Mwanzoni mwa Unawiri wa Kitu, Uzuri wa Kitu na pia humaanisha Vijana wa Katika Jamii.

Naaam..Neno *Waraqa* limetoa poa neno *Wariqun* ambalo humaanisha Pesa za Fedha, Gwaru au Pesa ambayo si ya Karatasi.

Hivyo baada ya kukubaliana juu ya kumtuma mtu atakaechukua Wariqun yao ili wanunulie chakula cha halali basi akasema Tamlikha kua: **'Enyi Ndugu zangu, hakuna hata mmoja miongoni mwetu atakaeweza kufanya hivyo isipokua mimi, nnaweza kufanya hivyo kiurahisi ila sasa hizi nguo zangu zitauza kwani watu watanijua. Hivyo ewe Mfugaji, vua Nguo zako na mimi na vua zangu kisha mimi nitavaa nguo zako za Ufugaji na kuelekea Mjini kwa ajili ya Jambo hilo na wewe utavaa nguo zangu na kubakia hapa.'**

Hivyo Wakabadilishana nguo zao hizo na kisha baada ya Tamlikha kuvaa nguo zinazomuonesha kua kama Mfugaji Mbuzi na Kondoo basi akatoka taratibu kutoka kwenye Pango hilo huku akiwa na wasiwasi sana. Na hivyo katika kutoka kwake alikua ananyatia na kujificha ficha chini ya Miti.

Na katika kutembea kwake kuelekea Mjini basi kila sehsemu anayopita anaona iko tofauti na ilivyokua Jana yake alipopita na Wenzake kabla ya kulala na kuamka kwao, Jambo hili lilimshangaza sana kwani mazingira yote ya nje ya Pango yalikua yamebadilika hadi Miti yote ilikua imebadilika kwani sio kabisa iliyokua hapo kabla. Hivyo akawa anajiulia kimetokea nini? Mbona hali imekua hivi Ghafla Moja.

Katika kutembea kwake ikawa hadi anaogopa asije akapotea na hivyo akawa anaweka alama za siri njiani ili asije akapotea njia wakati atakaporudi.

Kwani Katika kutembea kwake Ghafla Tamlikha kwa mbali akaona Lango kubwa sana linaloashiria kua mbele yake sehemu hio kua kuna Mji. Hivyo akajiuliza huu ndio Mji gani tena? Na alipokua akikaribia karibu akaona kua Lango hilo limepakwa rangi ya kijana halafu juu kina maneno yasemayo: ***'La Ilaha Illa Allah wa A'isa Ibn Maryam Ruhi Allah Alayhi Salatu wa Salam'*** Yaani Hakuna Mungu isipokua Allah na Isa Ibn Maryam ni Ruhi wa Allah Sala na Salam ziwe juu yake

Naam..kabla ya kuendelea kwanza inabidi tufahamishane kua hii ni Shahada ya Wafuasi wa Ummah wa Isa Ibn Maryam katika wakati wake kabla ya kuja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiwasilimisha wafuasi wa Dini ya Kikristo alikua akiwaambia waseme *La Ilaha Illa Allah* Muhammad *Rasul Allah* wa Isa Ruhi Allah, Ambapo hio pi ni shahada ya Mkristo anapoingia kwenye Uislam.

Ambapo aina hii ya shahada mbali ya kua ni yenye kuthibitisha kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Mtume wake, lakini pia shahada hii

inathibitisha kua Nabii Isa ni Kiumbe aliepuliziwa Roho na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo hawezi kua ni Muumba.

Hivyo wacha tufafanue kwa kuanza na maana ya neno *Ruhi* ambalo ndio lililotoa Jina la Nabii Isa *Alayhi Salam* yaani *Ruhi Allah.*

Ambapo neno *Ruhi* linatokana na neno *Raha* ambalo humaanisha Kuenda sehemu Katika Wakati wa Jioni, Kufanya Kitu katika wakati wa Jioni.

Neno *Raha* ndio lililotoa neno *Rihun* ambalo humaanisha Upepo, Nguvu, Mamlaka, Utawala, Ushindi, Msaada dhidi ya Maadui na pia humaanisha Rehma au Kitu Kizuri na Kisafi.

Na tunapozungumzia Upepo katika Qur'an basi kama ikiwa utatajwa katika hali ya Umoja yaani kwa kutumia neno *Rihan* basi hua unamaanisha kua ni Adhabu.

Ili kupata kufaham zaidi maana ya *Rihan* ambayo ni hali ya umoja ya Upepo ambao humaanisha Maangamizi basi na tuangalie kama vile ilivyotumika katika aya zifuatazo:

﴿وَأَمَا عَادٌ فَأُهْلِكُواْ بِرِيحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ۞ سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَانِيَةَ أَيَّامٍ حُسُوماً فَتَرَى ٱلْقَوْمَ فِيهَا صَرْعَىٰ كَأَنَّهُمْ أَعْجَازُ نَخْلٍ خَاوِيَةٍ ۞ فَهَلْ تَرَىٰ لَهُم مِّن بَاقِيَةٍ﴾

Waamma AAadun faohlikoo bireehin sarsarin AAatiyatin; Sakhkharaha AAalayhim sabAAa layalin wathamaniyata ayyamin husooman fatara alqawma feeha sarAAa kaannahum aAAjazu nakhlin khawiyatun; Fahal tara lahum min baqiyatin *(Surat Al Haaqa 69:6-8)*

Tafsir: **Na ama *Aad* wameangamizwa kwa Upepo Mkali sana. Alioulazimisha Allah Juu yao kwa usiku saba na michana minane mfululizo, kiasi ya kua ungeweza kuona watu wa jamii yao wameangushwa, kama kwamba ni mabua ya magogo ya Mitende. Jee mnaona mabaki yao?**

Subhana Allah! Aya inawazungumzia watu wa *Al Ahqaf* ambayo ni maeneo yenye udongo mgumu mwekundu unaoambatana na chungu nyingi sana za mkusanyiko wa Mchanga wa Jangwani zilizopinda pinda na kuchora maumbo ya nusu mwezi ya chungu za nyingi mchanga.

Ambapo haya hayakua ni maeneo yeyote isipokua maeneo ya Watu wa Kabila la *Aad,* ambao ni watu wa Nabii Hud ambapo kama tulivyosema kua Kabila au Jamii ya watu wa *Aad* walikua ni wenye kuishi katika maeneo ya *Al Ahqaf* ya upande wa Kusini yaani kwa maana hio, basi watu hawa walikua ni waishio katika eneo la Ardhi ya baina ya Hadhramawt nchini Yemen na Oman, ambapo pia kuna baadhi ya wasemao kua eneo hili pia limeingia mpaka katika sehemu ya Kusini ya Ardhi ya Saudia.

Ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliwatumia Mtume wao ambae ni Nabii Hud aliewausia lakini wakamkanusha kwa sababu ya neema waliyojaaliwa na Mola wao kama alivyowakumbusha Nabii wao huyo kwa kusema:

﴿أَوَ عَجِبْتُمْ أَن جَآءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ وَٱذْكُرُوٓاْ إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِن بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادَكُمْ فِى ٱلْخَلْقِ بَسْطَةً فَٱذْكُرُوٓاْ آلآءَ ٱللَّهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Awa AAajibtum an jaakum dhikrun min rabbikum AAala rajulin minkum liyunthirakum waodhkuroo idh jaAAalakum khulafaa min baAAdi qawmi noohin wazadakum fee alkhalqi bastatan faodhkuroo alaa Allahi laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Araf 7:69)***

Tafsir: ***Hivi jee mnastaajabu kua umekuja ukumbusho kutoka kwa Mola wenu kupitia kwa Mtu ambae ni kutoka miongoni mwenu, na Kumbukeni kua amekujaalieni kua Makhalifa baada ya Watu wa Nabii Nuh, na Kakuzidishieni Maumbile makubwa miongoni mwa Viumbe hivyo Kumbukeni Neema za Allah ili muwe ni wenye kufuzu***

Ambapo watu hawa wanasifiwa kua walikua na sifa ya watu wenye Maumbile ambayo hawakuwahi kupewa watu wengine na kuiainisha sifa hio kwa kuumia neno *Bastatan* ambalo ni lenye kutokana na neno *Basata* ambalo hua linamaanisha Kukuza, Kuongeza Ukubwa, Kuvuta kama mpira mpaka mwisho wa uvutwaji wake, Kutanua, Kutosheleza Ukubwa wake, Kupata Kitu kwa wingi zaidi ya Kutosha.

Hivyo basi aya inatuwekea wazi kua Miili ya Watu hawa ilikua haina Mfano wake Kiukubwa, Kinguvu, Kiafya, Kiurefu na Kiupana ambapo anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Urefu wa kila mmoja kati ya Watu hawa ulikua ni Dhiraa 80**' Na Dhiraa Moja na Robo hua na ukubwa wa Futi 2, sasa hapa tunazungumzia Urefu wa mtu mwenye urefu wa Futi 120.

Watu hawa pia walikua na Mali nyingi sana kiasi ya kua walikua wakifanya *Israfu* kwa kujenga Majumba ya Dhahabu kwa ajili ya kujionesha tu, bila ya kua ni wenye kukaa ndani yake, na pia kutokana na Ukubwa wao basi walikua wakivamia Mji wa watu wengine basi walikua wakiteketea kila kitu kwa kutumia nguvu kubwa sana.

﴿أَتَبْنُونَ بِكُلِّ رِيعٍ آيَةً تَعْبَثُونَ ۞ وَتَتَّخِذُونَ مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ۞ وَإِذَا بَطَشْتُمْ بَطَشْتُمْ جَبَّارِينَ ۞ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ﴾

Atabnoona bikulli reeAAin ayatan taAAbathoona; Watattakhidhoona masaniAAa laAAallakum takhludoona; Wa-idha batashtum batashtum jabbareena; Faittaqoo Allaha waateeAAooni*(Surat Ash Shuara 26:128-131)*

Tafsir: ***Mnajenga katika Kile sehemu iliyo juu Makasri Makubwa, wakati hamuishi ndani yake? Na Mnajichukulia Makasri Mazuri kama kwamba Mtaishi Ndani yake Milele. Na Mkivamia Mnavima Kama Majabari. Mcheni Allah na nitiini mimi.***

Tunapoiangalia aya ya 128 inasema kua *Atabnuuna bikulli riiaAain ayatin taAabathuuna* yaani Nabii Hud anawaambia watu wake kua wanajenga katika kila sehemu iliyo juu Makasri Makubwa ambayo hawaishi ndani yake.

Halafu aya hii imetumia neno *RiiAAin* ambalo ni lenye kutokana na neno *Ra'Aa* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kuona, Kutizama, Kufikiria, Kua na Mtizamo au Kuhukumu baada ya kuona. Neno *RaA'a* ndio lililotoa neno *Ri'ya* ambalo ni lenye kuonesha Sifa isiyotakiwa katika Uislam ambayo ni sifa mbaya ya Kujiona, Kujionesha, au Kujivuna.

Hivyo Basi Nabii Hud alikua akiwalaumu watu wake kutokana na Sifa hio mbaya ya Kujionesha na Kujivuna kwa kujenga Majumba ambayo hawayahijati na wala hawayatumii kwa jambo lolote isipokua Kuonesha Uwezo wao.

Na tunapoiangalia aya ya 129 basi tunaona kua katika kuyaelezea Majumba hayo imetumia neno *MasaniA'aa* ambalo linamaanisha kitu kinachotokana na Usanii mkubwa sana wa Kiumbe anapofanya kitu kwa kutumia akili, nguvu, wakati na jitihada kubwa sana mpaka kitu kipendeze sana, yaani watu hawa walikua hawajali mda wanaotumia, na uwezo gani wala mali gani, kwani kwao wao mda si muhimu kwa sababu wanaona kua wanao wa kutosha kwani wataishi milele, hivyo kila kitu chao walikua wanakitumia kwa ajili ya Mapambo ya Dunia kwa kuona kua wataishi Milele, na hivyo kua ni wenye kupingana na maumbile ya viumbe ambavyo vina maumbile ya kua ni vyenye kukikimbilia Kifo. Hivyo aya hii inatuwekea wazi umuhimu wa kutotumia Mda mwingi kwa ajili ya Dunia.

Ambapo aya ya 130 nayo imetumia maneno yenye kuainisha sifa zinazotokana na neno *Batashta* na neno *Jabar*.

Ambapo neno *Batashta* hua linamaanisha Kukamata kwa nguvu, Kuzidi nguvu, Kudhuumu au Kuua kwa Kutumia Nguvu, ambapo hili ni neno lililotumika mara 10 tu ndani ya Qur'an na mara mbili miongoni mwao ni katika aya hii katika kuelezea Uovu wa watu hawa wa *Al Ahqaf*.

Kisha aya ikatumia neno *Jabbar* ambalo tunapo lizungumzia kwa Viumbe basi hua ni sifa ya Mtu asiekua na Huruma juu ya wale ambao waliokua chini yake na hivyo kua ni wenye kusababisha madhara na dhulma kubwa kwa wale wasiokua na nguvu dhidi yake kutokana na Nguvu zake.

Naam aya tatu hizi zinabainisha miongoni mwa makosa waliyokua wakiyafanya watu hawa wa Nabii Hud. Lakini mbali ya Ukubwa wao basi hawakuweza kujilinda na adhabu kutoka kwa Mola wao, kwani baada ya kumuasi Mola wao na kuadhibiwa kwa Upepo kama inavyosema *Surat Al Haaqa 69:6-8* Ambapo katika Aya yetu hii *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuainishia namna hali halisi ilivyokua kwa kututolea Mfano hai wa Magogo ya Miti ya Mitende.

Kwa kua sisi kwetu Mitende sio Mingi basi na tuchukulie Mfano wa Magogo ya Mnazi namna Mti wake Ulivyojishona kwa umadhubuti wa nyuzi zake ndani yake. Hivyo chukua mfano huo wa gogo la Mti wa Mnazi kisha ingiza akilini inakua kuaje mpaka linakua Bua. Ambapo tunapozungumzia Bua basi hua tunazungumzia kitu ambacho chepesi hakina kitu ndani yake na hivyo kinapeperushwa kwa urahisi na Upepo wa kawaida tu.

Hivyo baada ya kupata picha hio, basi rudisha akili yako kwa Miili ya Watu hawa wa Nabii Hud, wenye Urefu wa Futi 100 kisha na ukubwa wao wote huo, basi hawakuweza kufanya chochote ilipowadia adhabu ya Mola wao na badala yake wakawa wamebakia kama Mabua mepesi yanayo peperushwa na Upepo.

Na katika kuthibitisha wepesi wao huo wa kua kama mabua na mbali ya kua na Miili mikubwa kuliko watu wengine wote Ulimwenguni waliowahi kuumbwa, Basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anahoji:

﴿ فَهَلْ تَرَىٰ لَهُم مِّن بَاقِيَةٍ﴾

Fahal tar<u>a</u> lahum min b<u>a</u>qiyatin *(Surat Al Haaqa 69:6-8)*

Tafsir: **Hivi Jee mnaona mabaki yao?**

Hivyo basi Upepo wenye hali ya Umoja hua ni Adhabu kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama ilivyosema aya yetu hii:

﴿وَأَمَا عَادٌ فَأُهْلِكُواْ بِرِيحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ﴾

Waamma AAadun faohlikoo bireehin sarsarin AAatiyatin*(Surat Al Haaqa 69:6-8)*

Tafsir: **Na ama *Aad* wameangamizwa kwa Upepo Mkali sana.**

Ambapo Upepo huo umeainishwa sifa yake kwa kutumia neno *Sarsarin* linatokana na Neno *Sarra* lenye kumaanisha Kulia au Kuvuma kwa Sauti kubwa sana. Hivyo neno *Sarsarin* linamaanisha Upepo Mkali wenye ngumu sana na unapovuma hua unatoa sauti kubwa sana. Na pia neno *Sarsarin* hua linamaanisha Upepo Mkali sana wenye Baridi kali sana.

Na Anasem Imam Is-haq Ibn Bishr kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* aliuamrisha Upepo uwapulize watu wa Nabii Hud, hivyo Upepo huo ulijikusanya kisha ukapuliza bila ya kua na mipaka yake wala mwisho wake, yaani kama Mvuke ambao unaotoka kwenye tundu za Pua za Fahali (Ng'ombe Dume mwenye Hasira kubwa sana) mpaka Ardhi ikatetemeka na Malaika wakasema: Ya Allah! Kwa hali hii Viumbe hawa hawatoweza kuustahamilia Upepo huu, kwani Utaangamiza kila kitu kilichomo katika Ardhi yao kuanzia Juu ya Ardhi mpaka nchini yake.'**

Upepo Huu ulikua Mkali Sana kiasi ya kua ukikupuliza basi unachana ngozi yako na kukitoa kila kitu ndani ya mwili wako na kutokea upande wa pili wa mwili wako Upepo huo ulikua ni wenye kuvuma na kutoa Sauti Kali sana mara 1000 zaidi ya sauti Upepo wa kawaida unapovuma.

Upepo huo haukua ni wenye kuvuma labda kwa mda wa saa moja au mawili, bali ulivuma kwa wiki nzima usiku na mchana bila ya kupungua kasi wala nguvu yake katika kuangamiza kwake! Kwani wiki nzima hii ilikua hakuna kwa kukimbilia wala kwa kujifichia isipokua kwa Nabii Hud aliekua ndani ya Rehma za Allah.

Kwa wale ambao wameshawahi kuishia katika nchi zenye Theluji na Baridi Kali basi hua kuna Upepo fulani hivi katika kipindi cha Baridi ukikupiga kama hujavaa Gloves mikononi mwako basi hata ukiingiza Mkono wako kwenye mfuko wa Jeans iliyobana basi mkono wako huo kwa upande wa nje yake hua unauhisi Kama unajichinja kwa maumivu, kutokana na kupigwa na Upepo wa Baridi. Au Unakua unahisi kama unaungua maji ya Moto mkono wako huo kutokana na Baridi hio, na ndio maana basi baadhi ya Wanazuoni wakasema kua Upepo huo ulikua ni wa Moto kutokana na ukali wake.
Ila hapa mimi nimetumia mfano wa Upepo ulio katika hali ya wingi yaa *Al Riyyah* wa Baridi kali, sasa usiseme kuhusiana na Upepo huo wa *Rihun* walioletewa watu wa Nabii Hud, tena ukiwa na Kusudio Maalum la Kuadhibu na kuangamiza, kama unatafakkari na kuzingatia basi utaona uzito wa hoja hii iliyobainishwa hapa na aya hii.

Ambapo anasema Imam Al Suddi kua kua: **Watu hawa wa Hud walipopelekewa Upepo huo kwanza waliona ukali wake kwa kupeperushwa Ngamia wao na wakajikuta na wao pia wamekua miongoni mwao, kwani kila aliekimbilia Ndani Nyumbani kwake basi Upepo ulimfuata huko huko na kumtoa nje kwa kumpeperusha mpaka wakaaangamia wote na baada**

ya kuangamizwa kwao huko basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akatuma Ndege kwa ajili ya kuyabeba mabua ya Miili yao na kuitupa baharini

Na unapotajwa katika hali ya Wingi yaani Al *Riyyah* basi hua Rehma katika mfano wa aya zifuatayo:

﴿وَأَرْسَلْنَا ٱلرِّيَاحَ لَوَاقِحَ فَأَنزَلْنَا مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَاءً فَأَسْقَيْنَاكُمُوهُ وَمَآ أَنْتُمْ لَهُ بِخَازِنِينَ﴾

Waarsaln<u>a</u> alrriy<u>aha</u> law<u>a</u>qi<u>h</u>a faanzaln<u>a</u> mina alssam<u>a</u>-i m<u>a</u>an faasqayn<u>a</u>kumoohu wam<u>a</u> antum lahu bikh<u>a</u>zineena *(Surat Al Hijr 15:22)*

*Tafsir: **Na tunatuma Upepo Mwingi wenye kupandikiza, Na kisha tunateremsha kutoka Mbinguni Maji na kukupeni nyinyi mkanywa, na sio nyinyi ambao ndio wenye hazina yake.***

Ambapo Aya imetumia neno *Lawaqiha* ambalo ni leye kutokana na neno *Laqaha* lenye kumaanisha Kutia Mimba, Kupandikiza, Kurutubisha, Kusababishia Kuzaa, Kutoa Matunda kutokana na kilichopandikizwa, Kusababisha Mawingu kutoa Mvua na pia huaanisha Kutia Chanjo.

Hivyo maneno *Alrriy<u>aha</u> law<u>a</u>qi<u>h</u>a* hua yanamaanisha Aina ya Upepo mwingi ambao ni wenye kunyanyua na kuyakusanya Mawingu ambayo ni yenye kuzalisha Mvua, Upepo ambao ni wenye kubeba Mvuke wa Maji kutoka Baharini kuelekea Juu ardhini kisha ukasababisha Mawingu ya Mvua, na pia yanamaanisha Upepo ambao hua ni wenye Kubeba Unga (*Pollen*) laini wa Mbegu za Uzazi za Maua Jike na Dume na Kuzipandikiza katika Maua.

Ambapo kwa upane wa Imam Abu Al Thana Shihab Ad Din Sayyid Mahmud Ibn Abd Allah Al Husayni Al Alusi Al Baghdad anasema kuhusiana na Upepo huu kua: '**Huu hua ni Mzunguko wa Upepo ambao hua unasambaa katika sehemu tofauti kwa sababu kama Upepo unakusanywa pamoja na kuelekezwa katika sehemu moja au muelekeo mmoja basi Upepo huo hua na Nguvu kubwa sana ya Maangamizo ya kuangamiza kila kitu katika njia yake. Kwa hivyo basi Upepo huu unachukuliwa kua ni Upepo Mwingi unaosambaa na kupepea sehemu tofauti na kutawanyika katika pande tofauti na muhimu kuliko yote ni kua aina hii ya wingi wa Upepo hua unasaidia kuchanganya Mawingu, na kusafisha hali ya hewa na kupandikiza Mawingu.**'

Ambapo kwa Mtizamo wa *Shaykh ul Islami Imam* Muhammad Tahir Ibn Ashur basi yeye anasema kua: '**Upepo hua ni wenye kusafirisha Unga wa uzazi wa Maua kutoka katika Mti wa Kike kuupeleka katika Mti wa Kiume na hapo hapo Mti wa kike hua tayari uliokwisha pandikizwa na utazaa na matokeo yake hua ni kupatikana kwa mazao**.'

Ambapo Imam Ibn Ashur anaendelea kutuambia kua: '**Upepo unaobashiria Bashirio Jema la Mvua hua ni Upepo Mlaini, Mwepesi na wenye Rehma ndani yake'** kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَهُوَ ٱلَّذِى يُرْسِلُ ٱلرِّيَاحَ بُشْرىً بَيْنَ يَدَىْ رَحْمَتِهِ حَتَّىٰٓ إِذَآ أَقَلَّتْ سَحَاباً ثِقَالاً سُقْنَاهُ لِبَلَدٍ مَّيِّتٍ فَأَنْزَلْنَا بِهِ ٱلْمَآءَ فَأَخْرَجْنَا بِهِ مِن كُلِّ ٱلثَّمَرَاتِ كَذٰلِكَ نُخْرِجُ ٱلْمَوْتَىٰ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ﴾

Wahuwa alladhee yursilu alrriyaha bushran bayna yaday rahmatihi hatta idha aqallat sahaban thiqalan suqnahu libaladin mayyitin faanzalna bihi almaa faakhrajna bihi min kulli alththamarati kadhalika nukhriju almawta laAAallakum tadhakkaroona *(Surat Al Araf 7:57)*

Tafsir: ***Yeye ndie ambae anaeshusha Upepo Mwingi kua bashirio jema linalobainisha msaada wa Rehma zake, mpaka unapobeba Mawingu yaliyojaa na kisha tunayasukuma katika Ardhi iliyokufa na kisha tunashusha Maji juu yake na kisha hutoa kutokana nayo kila aina ya Matunda, na mithili yake tutakavyowafufua waliokufa ili mpate kukumbuka.***

Neno *Raha* ndio lililotoa neno *Ruh* ambalo hua linamaanisha vitu viwili sambamba ambavyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* huwashushia Ujumbe kwa njia moja au Nyengine Wale Waja wake aliowachagua ambavyo ni *Wahyi na Ilham.* Ambapo vitu viwili hivi hua ni Vyenye Kuzihuisha Nyoyo kutokana na Kifo cha Ujinga.

Neno Ruh pia humaanisha Roho, Pulizio la Uhai, Nafsi, Hisia, Kitabu cha Qur'an, Raha na Furaha, Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Wajumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* wakiwemo *Mitumwa na Malaika.*

Hivyo Nabii Isa *Alayhi Salatu wa Salam* ameitwa *Ruhi Allah* kwa sababu katika Kuumbwa kwake Alikua ni mwenye Kupuliziwa mara mara mbili kwanza alipuliziwa Maryam bint Imran kwenye Nguo yake na Malaika Jibril ambapo ndio ikatunga Mimba yake na ikaambiwa iwe na ikawa Mimba hio na mara ya pili ni alipopuliziwa Roho kama wanavyopuliziwa Ibn Adam wengine wote wanapokua tumboni mwa Mama zao baada ya siku 120.

Kwani pia kwanza tulisema kua Duqyanus aliliziba Pango la Watu wa As-hab Al Kahf kwa Ukuta na akataka Wafe ndani yake wasitoke. Hivyo kuna watakojiuliza ilikuaje Wakatoka? Na pia tulisema pia kua kina Tamlikha walilala kwa miaka 309 sasa ilikuaje hadi hata nguo zao hazikuharibika, wakati hali hii hua ni sawa na ile hali ya Uzayr.

FITYATUN - AS-HAB ALKAHF NI MITHILI YA UZAYR IBN SURAYAH.

Ambapo majibu ya Masuali yote mawili haya tunayapata pale tunapokua tunajua maana ya *Ayat Al Kursiyu* ambayo ndani yake imebeba Majina Mwili Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yaliyomo ndani yake ambayo ni *Al Hayyu Al Qayyum* pale iliposema:

﴿ٱللَّهُ لاَ إِلَٰهَ إِلاَّ هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ لاَ تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلاَ نَوْمٌ لَّهُ مَا فِى ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَا فِى ٱلأَرْضِ مَن ذَا ٱلَّذِى يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلاَّ بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلاَ يُحِيطُونَ بِشَىْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلاَّ بِمَا شَآءَ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضَ وَلاَ يَؤُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ ٱلْعَلِىُّ ٱلْعَظِيمُ﴾

Allahu la ilaha illa huwa alhayyu alqayyoomu la ta/khudhuhu sinatun wala nawmun lahu ma fee alssamawati wama fee al-ardhi man dha alladhee yashfaAAu AAindahu illa bi-idhnihi yaAAlamu ma bayna aydeehim wama khalfahum wala yuheetoona bishay-in min AAilmihi illa

bima shaa wasiAAa kursiyyuhu alssamawati waal-ardha wala yaooduhu hifdhuhuma wahuwa alAAaliyyu alAAadheemu *(Aya Al Qursy - Surat Al Baqara 2:255)*

Tafsir: ***Allah! La ilaha illa Huwa Hakuna anaestahiki Kuabudiwa Isipokua Yeye (Yeye Allah Subhanah wa Ta'ala) Ni Mwenye Uhai wa Milele na ndie Mwenye Kujisimamia juu ya Kila kitu na ndie Msimamizi juu ya Kila kitu (Yeye ndie ambae) Haimpitii Hali ya Kusinzia wala ya Kulala Usingizi Kwake yeye Ndio kwenye Umiliki wa Kila Kilichomo Mbinguni na Ardhini Jee Ni Nani yule Ambae atakaeweza Kuingilia Mambo yake (Allah Subhanah wa Ta'ala) Bila ya Idhini yake? (Allah Subhnah wa Ta'ala) Kwani yeye (Allah Subhanah wa Ta'ala) Ni mwenye Kujua juu ya kila kitu Kabla ya kutokea kwake na Baada ya Kutokea kwake na Hakuna atakaekua na Chochote kutokana na Ilm yake Isipokua kwa kile akitakacho (kijulikane) Na Arshi yake (Ukubwa wake) Imeenea Mbinguni na Ardhini na wala hachoki katika kuvihifadhi na kuvisimamia vitu (Vilivyomo ndani yake Mbinguni na Ardhini) Na Yeye ndie Aliejuu Kidarja na Kiutukufu hakuna alie zaidi yake***

Hii ni Aya ambayo ndani yake inabeba ujumbe Mzito sana, kwani inaelezea mambo mengi ambayo wengi hatuyajui kutokana na Ufinyu wa Ufaham wetu. Na aya inathamani na manufaa Makubwa Sana ambayo pia wengi wetu hatuyajui na hatuyathamini, kwa sababu ni kawaida ya yule asiekijua kitu basi kua ndie asiekithamini.

Hivyo basi tunafahamishana ili angalau tupate kuyajua baadhi ya Mambo hayo, kwani hatuwezi kuelezana yote, kwa sababu tukitaka kuelezana yote basi hatuwezi kuyamaliza yote leo hii ambapo Miongoni mwa Mambo tusiyoyajua sisi Waislam wa leo Kuhusiana na Aya hii basi ni Sifa Tukufu na Majina Matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na hivyo tunashindwa Kufaham na Kuelewa Ukubwa wa Uwezo wa juu ya kila kitu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama ilivyobainisha *Ayat Al Kursiyu*. Na Ukweli ni kua Hili sio Jambo Dogo la Kulidharau au la kutokukumbushana kwa sababu linaweza kumpelekea Mtu kua ni Mnafiq na kila mtu anajua sehemu ya Mnafiq baada ya Kufariki kwake na kesho Akhera kama zinavyoonesha Aya na Hadith.

Na kutokana na kutojua Uwezo na Ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Maana ya maneno ya *Ayat Al Kursiyyu* basi ndio maana unakuta watu wanaulizana Kuhusiana kwanini baadhi ya Matukio Muhimu ya Kiislam yawe yatofautiane kiwakati Duniani na hivyo Wasiojua kua ni wenye Kutaka kua lazima yawe ni yenye kutokea katika hali ya Umoja Duniani kote, Ambapo hapa tunachukulia mfano wa Usiku wa *Laylat Al Qadr*, Funga ya Arafa, Idd, n.k

Ambapo Mara nyingi watu wanashindwa kufaham kua Moja kati ya Sifa za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Al Hakim yaani ni Mwingi wa Hikma, pia ni *Al Aadil* yaani ni Mwingi wa Uadilifu. Na Tunapozungumzia kuhusiana na sifa za Hikma na Uadilifu basi ndani yake ndio tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni Mwenye Kufanya kila kitu chake kwa Hikma zake na kukisimamia kwa Uadilifu wake. Hivyo hua ni Mwenye Kumlipa Mja wake kwa Uadilifu kulingana na Amali yake
Kwani tunapoiangalia *Aya Al Kursiy* basi tunaona hizi sifa 2 za *Al Hayyu Al Qayyum*, ambayo ni sifa zinatupa Majibu ya Masuali yetu yote haya wanayoulizana wale wasiojua.

Kwa Sababu tunapozungumzia *Al Hayy* kwa Ufaham wa Kibinadam basi hua inamaanisha kua Ni Mwenye Kuishi Milele, na tunapozungumzia Kuishi basi hua tunazungumzia kuwepo kwa kitu husika, na tunapozungumzia kuhusu Milele basi hua tunazungumzia hali ya Kitu kua katika Kutokua na Mwanzo wala mwisho na kutokana na kutokua na Mwanzo wala mwisho basi kitu hicho hua katika kila sehemu kipo na kila wakati kipo.

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Sifa hii ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua inatubainishia kua kwake yeye hua Hakuna Mipaka ya kuwepo kwake na pia hakuna mipaka ya kutokuwepo kwake katika ila sehemu na katika kila wakati.

Yaani alikuwepo, yupo na atakuwepo kwa Mda wote na Katika sehemu yeyote kabla ya kuwepo kwake sehemu hio na baada ya kuwepo kwake sehemu hio na hii ni kwa Sababu yeye ndie Muumba Kwani kwa Kiumbe Jambo hili hua haliwezekani kwa sababu kiumbe hua na mipaka ya Wakati wa kuwepo kwake ambao hua ni hali inayolingana na mazingira yake na tukio la kuwepo kwake katika sehemu husika.

Kwani Sifa ya pili ya Jina Tukufu la *Allah Subhanah wa Ta'ala* liliopo ndani ya aya hii baada ya Sifa ya Al Hayyu, basi ni sifa ya *Al Qayyum*. Ambapo hii ni Sifa ambayo yenye Kumaanisha kua yeye *Allah Subhanah Wa Ta'ala* ni Mwenye Kujisimamia kila Kitu juu yake, ambapo sifa hii hua inaenda Sambamba na sifa ya *Al Ghaniyuu.*

Yaani ni Tajiri mwenye kila kitu na asiehitaji kitu chochote kutoka kwa yeyote, ambapo hapo hapo katika kua na Utajiri wake huo basi kwake yeye hakipungui kitu chochote katika Kutoa kwake kwa ajili ya kuwapa Viumbe wake. Hivyo kwa upande mwengine hii hua ni sawa na hali ya Sifa *Al Qayyum* kwani katika Kusimamia kwake juu ya viumbe wake basi hua ni mwenye Kusimamia kwa Ukamilifu kila kitu alichokiumba tangu kuanzia kabla ya kuwepo kwake kitu hicho mpaka kutokea kwake na pia baada ya kutoweka kwake kitu hicho Hapa Duniani na kesho Akhera pia.

Bila ya shaka! Hutokua na Shaka kuwa Kina *Fityatun* hawa walikua chini ya Usimamizi Kamilifu wa kila kitu kwa Ukamilifu kama anavyotaka yeye na kwa kadiri ya mda anaotaka yeye, yeye ambae asiekua na mwanzo wala mwisho mwenye Uhai wa Milele ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Ambapo kama hapa haiko wazi basi tuchukue mfano wa Uzayr Ibn Suraiyah ambae yeye alikua ni Mwanzuoni wa watu wa Bani Israil, aliekimbia baada ya kuvamiwa Mji wao wa Jerusalem na kisha kutekwa na Jeshi la Nebuchardneza, katika kukimbia kwake Jeshi la Nebuchardneza basi alikua na Punda wake na Zabibu zake, na katika safari yake akapita kwenye Mji uliokua upo Juu chini kutokana na kuangamia kwake hivyo akashangaa na kujiuliza jee itawezekanaje kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* awafufue Watu wote wakiwemo hao katika Mji huo uliokua juu chini katika siku ya Malipo?

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamuonesha kwa Kumuua yeye pamoja na Punda wake kwa muda wa Miaka 100. Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamfufua Uzayr kisha akamuuliza kupitia kwa Malaika Jibril: **'Hivi jee unadhai ulikua umelala kwa mda wa miaka Mingapi?'** ambapo nae akajibu kama walivyojibu watu wa *As-hab Al Kahf*, yaani kua alikua amelala kwa mda wa Siku moja au Masaa kadhaa tu, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamwambia kua alikua amelala kwa mda wa miaka 100 akamwambia amuangalie Punda wake alipoangalia akaona kua Kamba ya Punda imefunga Skeletan ya Mifupa ya Punda.

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamwambia angalia nitakavyoweza kufufua kwa kwanza kuisimamisha Mifupa na kuivisha Nyama na kisha kuivisha Ngozi na kisha kumuamrisha Kiumbe awe na atakua.

Na hayo yakatokea mbele ya Macho yake kwa Punda wake Kujiunga Mfupa mmoja baada ya mmoja na kujivisha Nyama na Ngozi na mwisho Punda huyo akaambiwa awe na akawa Punda mzima kama alivyoku ahapo kabla. Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamwambia Uzayr Angalia Zabibu zako.

Uzayr katika Mkono kwenye Mfuko wake kakuta Zabibu kama ndio kwanza kazichuma sasa hivi hata hazijakauka zina na utomvu utomvu wake mbali ya kua zilikaa ndani ya Mfuko wa Uzayr kwa miaka 100. Kama kinavyoelezewa kisa hiki kwenye Qur'an:

﴿أَوْ كَٱلَّذِى مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِىَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّىٰ يُحْيِى هَٰذِهِ ٱللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا فَأَمَاتَهُ ٱللَّهُ مِئَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهُ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ قَالَ لَبِثْتُ يَوْماً أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ قَالَ بَل لَّبِثْتَ مِئَةَ عَامٍ فَٱنْظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ وَٱنْظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ آيَةً لِلنَّاسِ وَٱنْظُرْ إِلَى ٱلعِظَامِ كَيْفَ نُنْشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْماً فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

Aw kaalla<u>dh</u>ee marra AAala qaryatin wahiya kha<u>w</u>iyatun AAala AAurooshiha qala anna yu<u>h</u>yee ha<u>dh</u>ihi Allahu baAAda mawtiha faamatahu Allahu mi-ata AAamin thumma baAAathahu qala kam labithta qala labithtu yawman aw baAAda yawmin qala bal labithta mi-ata AAamin faon*<u>dh</u>*ur ila taAAamika washarabika lam yatasannah waon*<u>dh</u>*ur ila himarika walinajAAalaka ayatan lilnnasi waon*<u>th</u>*ur ila alAAi*<u>dh</u>*ami kayfa nunshizuha thumma naksooha lahman falamma tabayyana lahu qala aAAlamu anna Allaha AAala kulli shay-in qadeerun*_(Surat Al Baqara 2:259)_**

Tafsir: ***Au kama yule ambae aliepita katika Mji ambao ulikua umeteremshwa juu chini ya Mapaa yake, nae akasema: 'Duh! Hivi itakuaje Allah Subhanah wa Ta'ala awe ni mwenye kuweza kuuhuisha huu baada ya kufa kwake?' Hivyo Allah akamsababishia Kufa kwa mda wa miaka 100 na kisha akamfufua. Na kumuuliza: 'Hivi Jee kwa mda gani ulikua umekufa?' ambapo ane akajibu: 'Nadhani ni kwa mda wa siku au kwa seheu tu ya siku moja' (Allah Subhanah wa Ta'ala akamwambia): 'La, hakika wewe ulikua katika hali ya kufa kwa mda wa miaka 100 Angalia Chakula chako na Kinywaji chako, havikubadilika. Na muangalie Punda wako! Hivyotunakufanya wewe kua Dalili kwa Watu. Angalia Mifupa na namna tunavyoiunganisha na kuivisha Nyama' na hivyo hili lilipokua wazi basi akasema: 'Najua sasa hivi kua Kwa Hakika Allah ni mwenye kuweza kufanya kila kitu.'***

Ambapo amesema Imam Ibn Fathawayh kua: **'Amesema Wahab Ibn Munabih kua Peponi, hakuna Mwamba wala Punda isipokua Mbwa wa watu wa As-hab Al Kahf na Punda wa (Jeremiyah) Uzayr ambae *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimsababishia kufariki kwa miaka 100 na kisha akamfufua.'** Hivyo Uzayr akarudi katika Mji wake akawakuta watu wake wote waliokua vijana na watoto katika wakati wake wameshakua vizee.

Neno Uzayr limetokana na neno Azar kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kuzuia, Kugeuka Upande wa pili, Kuunga Mkono au Kusaidia .

Hivyo Uzair hua linamanisha Jina la Mtu ambae *Allah Subhanah wa Taala* amemuelezea katika Qur-an kama alivyosema katika aya ya 259 ya Surat Al Baqara ambapo ndani yake tunaona kua Uzayr ni Mtu ambae katoka katika Upande Mmoja wa Maisha akaingizwa kwenye Upande wa Pili kisha akageuzwa na kurudishwa kwenye upande wa Mwanzo hapa hapa Duniani.

Na ingawa Wakristo na Mayahudi hua wanamwita Ezra. Lakini kwa upande wa Kiislam basi kuna tofauti ya Mitizamo juu ya jina lake na hii ni kulingana na namna tukio lilivyotajwa ndani ya Qur-an na maana ya Neno Ezra kama tulivyoona hapo awali.

Ambapo kimaana ya juu juu tu basi tunapoangalia tukio hili basi tunaona kua na Tofauti na Tukio la Watu wa Ashab Al Kahf ambao wao Walilazwa kwa miaka 309 lakini huyu Aliuliwa kisha akafufuliwa baada ya miaka 100. Hiyo yote ni Miujiza na Dalili za kuwepo kwake Muumba.

Ingawa wengi miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua aya zinamzungumzia Uzair katika tukio hili lakini pia kuna Wanazuoni wenye Mtizamo tofauti kuhusiana na mhusika alielengwa hapa. Ambapo kwa upande wa *Amir Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu, Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Ubbay Ibn Qaab *Radhi Allahu Anhu,* Imam Hasan Al Basr, Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi n.k badi wao wanasema kua ni Uzair.

Ambapo kwa upande wa Imam Wahb Ibn Munabih, Imam Abd Allah Ibn Ubayd Allah basi wao wanasema kua ni Aramiyah yaani Jeremiah.
Na kuna wanaosema kua Huyu Mtu alikua ni Hizqil yaani yule aliemtahadharisha Nabii Musa akimbie kutoka katika Misri. Na pia kuna wasemao kua huyu alikua ni Al Khidr.

Ama kuhusiana na Mji husika basi Wanazuoni wanasema kua Ulikua ni Jerusalem baada ya kuvamiwa na Mfalme Nebuchadnezzer.

Ambao huo ni Mtizamo wa Imam Ikrimah, Imam Wahb Ibn Munabih na Imam Al Rabi.

Ama kuhusiana na Imam Al Dahaq Ibn Muhazim basi anasema kua huu Mji ulikua ni wa Quds.

Ambapo kwa upande wa Imam Abd Rahman Al Sudi basi yeye anasema kua huu Mji ulikua ni Mji uitwao Salamabad.

Wakati Imam Al Qalbi basi yeye amesema kua ulikua unaitwa Dayr Sayarabad ambao pia unajulikana kama Dayr Sarahqil.
Na kuna wasemao kua unaitwa Anab ambao haukua mbali na Jerusalem.

Imam Wahb Ibn Munabih anasema kua: **Wakati Mfalme Nebuchadnezer alipouvamia Mji wa Jerusalem, na kuwaua Watu wa Bani Israil na wengine kuwafanya Watumwa wao basi Jeremiah alikimbia kutoka katika Mji huo. Hadi pale Mfalme Nebuchadnezer alipomaliza Uvamizi wake na kuondoka na Watumwa na kurudi katika Mji wake wa Babylon, ndio Jeremiah akarudi katika Mji huo huku akiwa juu ya Punda wake akiwa na Mkebe wake wa Juisi ya Zabibu na Tini.**

Na alipofika katika Mji wa Jerusalem, akasimama na kuangalia namna ulivyoangamizwa mji huo, na hivyo akasema:

﴿ أَنَّىٰ يُحۡيِۦ هَٰذِهِ ٱللَّهُ بَعۡدَ مَوۡتِهَاۖ ﴾

Anna yuhyee hadhihi Allahu baAAda mawtiha*(Surat Al Baqara 2:259)*

Tafsir: ***Itakuaje Auhuishe Huu Mji Allah Baada ya Mauti Yake?***

Na kisha Jeremiah akashuka kutoka kwenye Punda wake na akamfunga Punda huyo kwa Kamba Mpya kabisa chini ya Kivuli cha Mti akapimzika na kisha Allah Subhanah wa Taala akamjaali kua na Usingizi nae akalala. Ambapo katika Kulala kwake basi Allah Subhanah wa Taala akauchukua Uhai wake kwa muda wa Miaka 100.

Na pia ukachukuliwa Uhai wa Punda wake lakini Juisi yake na Tini yake ikawa iko vile vile kama ilivyokua sekunde chache kabla yake. Na Vile vile *Allah Subhanah wa Taala* akamficha Jeremiah na Punda wake kutokana na Macho ya Wanyama Wasimle na Watu wasimuone kisha Wakamzika.

Naam...ingawa hali hii aliyokua nayo Jeremiah na Punda Wake ilidumu kwa miaka 100. Lakini ulipoingia mwaka wa 70, yaani miaka 30 kabla ya kutimia miaka 100 basi *Allah Subhanah wa Taala* akamjaalia Mfalme wa Uajemi aitwae Yushak kua na hamu ya kuelekea katika Mji wa Jerusalem kwa ajili ya kuujenga Mji huo upya.

Katika wakati wa ujengwaji huo basi Mfalme Nubuchadnezer akafariki Dunia, na watu wa Bani Israil waliokua Babylon wakarudi Mjini Jerusalem, na kuishi ndani yake kwa miaka 30.

Kwa upande mwengine basi pia kuna mtizamo mwengine ambao ni wa wale wasemeo kua huyu alikua ni Uzayr ambao tulisema kua ni mtizamo wa Bab Al Ilm Ali Ibn Abi Talib na Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhum* Ambapo wao wanasema kua:

Wakati Nebuchadnezzer alipouangamiza Mji wa Jerusalem, basi aliwakata vichwa watu 40000 ambao walikua ni wasomaji wa Taurat na Wanazuoni wa Bani Israil. Ambapo miongoni mwao alikuwemo pia Baba ya Uzayr na Babu yake, na katika kipindi hiki Uzayr alikua bado ni kijana Mdogo aliekua akijifunza Taurat. Hivyo Ezra alikua ni miongoni mwa waliotekwa na kuchukuliwa kufanywa Watumwa katika Mji wa Babylon.

Na kisha baada ya kufika kwenye ardhi ya Babylon na kukaa kwa mda basi akaondoka na kuelekea kwenye ukingo wa Mto Tigris, pamoja na Punda wake na akakutana na Mji ambao ulikua hauna Mtu ndani yake kwani ulikua ni Mji ambao ulikumbwa na Maangamizo.
Katika kutembea kwake huku akishangaa juu ya kilichoufika Mji huo basi akakuta Mizabibu ambayo hata hivyo ilikua na Zabibu, hivyo akachuma na kufanya sharbati na nyengine akatia mkobani mwake. Hivyo baada ya kumaliza ndio akajiuliza:

﴿ أَنَّىٰ يُحْيِـۦ هَٰذِهِ ٱللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۖ ﴾

Anna yuhyee hadhihi Allahu baAAda mawtiha*(Surat Al Baqara 2:259)*

Tafsir: ***Itakuaje Auhuishe Huu Mji Allah Baada ya Mauti Yake?***

Ambapo tunapomzungumzia Uzayr na tukio hili na Suali hili basi inabidi tukumbuke kua Huyu alikua ni Mtu ambae ametoka katika kizazi cha Nabii Harun na ndani ya Familia ya Wanazuoni wenye Kuijua Taurat Yenyewe ya asili.

Hivyo hapa hakujiuliza kwa kutokana na kua na shaka bali alijiuliza kutokana na Kuona Maajabu yaliyopo Mbele yake. Kisha nae akamfunga Punda wake na akalala na akatolewa Roho yake. Na baada ya kupita Miaka 100 basi *Allah Subhanah wa Taala* akamfufua Uzayr.

Ambapo kwa wanaosema kua ni Jeremia basi wanasema kua: '**A*llah Subhanah wa Taala* kwanza aliyafufua Macho ya Mtu huyo, na hivyo yakawa yako hai yanaona bila ya kuwepo kwa kiwili wili chenyewe, kwani kiwili wili kilikua bado kimekufa.'**

Kwani Imam Wahb Ibn Munabih anasema kua: '**Kisha baada ya kufufuliwa kwa Macho yake Jeremiyah ambayo yalikua yako hai peke yake, basi *Allah Subhanah wa Taala* akaanza kuyaonesha Macho hayo namna Unavyofufuliwa Mwili wake Jeremiah mbele ya macho yake. Kwa kuunganishwa Mifupa kuvishwa Nyama kupitishwa mishipa ya damu na kisha kuvishwa Ngozi.'**

Yaani haya ni Mambo ya Miujiza ya hali ya juu kabisa, ambapo ingawa kwa Ibn Adam hua ni vigumu kuamini na ndio maana *Allah Subhanah wa Taala* akaamua Kumuonesha Mtu huyu Uwezo wake.'

Kua kwake yeye kila kitu kinawezekana tena kirahisi sana, na kisha *Allah Subhanah wa Taala* akakielezea kisa kwenye kitabu chake kitukufu ili mimi na wewe na wasiokua na yakini tupate kujua juu ya uwezo wake huo.

'Ambapo baada ya kukamilika kufufuliwa kwa Mwili wake mbele ya macho yake basi Jeremiyah akaona Mifupa ya mnyama mwengine myeupee imetawanyika mbele yake na hapo akakumbuka kua alikua na Punda hivyo akajua kua hio ni mifupa ya Punda wake.

Na mara akasikia sauti ikiamrisha kwa kusema: Ewe Mifupa iliyokwisha Oza kwa mda mrefu na kutawanyika, Allah anakuamrisha ujikusanye pamoja.

Na mifupa hio ikajikusanya pamoja mbele yake Jeremiyah.

Kisha sauti hio ikasema:Allah anakuamrisha ewe mwenye Mifupa kua ujivishe Nyama, Mishipa ya Damu na Ngozi.

Ambapo mara Mifupa hio ya Punda huyo ikaanza kujivisha Nyama, ikajifunga kwa Mishipa ya Damu na kisha ikajivisha Ngozi.

Hivyo mbele yake Jeremeiyah ikawa kuna Umbo la Punda kama aliavyokua Punda wake lakini umbo hilo limekaa tulii kama Sanam.

Kisha Sauti ikaamrisha kwa kusema: Ewe Punda Allah anakuamrisha uwe hai. Na hapo hapo Punda huyo akawa hai na kusogea karibu mbele yake Jeremiah.

Ambapo anasema Imam Ibn Fathawayh kua: **Amesema Wahb Ibn Munabih kua: Peponi Hakuna Mnyama wa aina ya Mbwa wala wa aina ya Punda. Isipokua Mbwa wa watu wa As-hab Al Kahf na Punda Jeremiyah ambao ni wanyama wawili hawa wa aina zao watakaokua Peponi kutokana na kua walijaaliwa kufa kwa mamia ya Miaka na wakafufuliwa tena pamoja na watu wao.'**

Hivyo basi *Allah Subhanah wa Taala* akamdhihirishia Uzayr hali ilivyokua na namna mda ulivyoenda wakati yeye alipokua katika hio hali aliyoiona kua ni masaa machache kama zinavyosema aya:

﴿ ثُمَّ بَعَثَهُ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ قَالَ لَبِثْتُ يَوْماً أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ قَالَ بَل لَّبِثْتَ مِئَةَ عَامٍ فَٱنْظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ وَٱنْظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ﴾

Thumma baAAathahu qala kam labithta qala labithtu yawman aw baAAda yawmin qala bal labithta mi-ata AAamin faondhur ila taAAamika washarabika lam yatasannah waondhur ila himarika *(Surat Al Baqara 2:259)*

Tafsir: ***Na kisha akamfufua. Na kumuuliza: 'Hivi Jee kwa mda gani ulikua umekufa?' ambapo ane akajibu: 'Nadhani ni kwa mda wa siku au kwa seheu tu ya siku moja' (Allah Subhanah wa Ta'ala akamwambia): 'La, hakika wewe ulikua katika hali ya kufa kwa mda wa miaka 100 Angalia Chakula chako na Kinywaji chako, havikubadilika. Na muangalie Punda wako!'***

Na kisha baada ya kuoneshwa Miujiza ya vile vilivyohifadhiwa bila ya kuharibika kwa Miaka 100 yaani Chakula chake na Kinywaji chake na kubakia katika hali ya kua kama ndio kwanza vimetayarishwa kwa ajili yake. Basi *Allah Subhanah wa Taala* akamuonesha Uzayr kuhusiana na yule aliekua katika hali kama yake yaani Punda wake kama zilivyosema Aya.

Na kuna baadhi ya Wanazuoni wanasema kua Hali ya Punda wake baada ya kufufuliwa Uzayr basi ilikua ni ya Punda aliyekufa mwili wote na Mifupa yake imetawanyika, lakini Kichwa chake Punda huyu kilikua hakija haribika na hivyo baada ya kuambiwa ambuangalie na aangalie kinachotokea basi Mifupa ya Punda huyo ikajiunga pamoja.

Na kisha Punda huyo akawa ni mwenye kusimama pale pale alipomfunga na Kamba yake bado ikiwa mpya. Ambao huu ni mtizamo wa Imam Dahaq Ibn Muzahim na Imam Qatadah Al Sadusi.

Ambapo Mtizamo wa Wanazuoni wengine ni kua huyu Punda alikua wote katika hali ya Mifupa iliyotawanyika hapa na pale baada ya kufariki kwake miaka 100 iliyopita.

Na kutokana na kua Wafuasi wa Dini ya Kikristo ni wenye kuamini kua Nabii Isa ni Mtoto wa Mungu, na hii ni kutokana na Maumbile aliyozaliwa, na kwa upande wa Wafuasi wa Dini ya Uyahudi nao pia Wanaamini kua Uzayr ni Mtoto wa Mungu, na hii ni kutokana na tukio hili la Kuuliwa na kisha Kufufuliwa baada ya miaka 100, na kuambiwa kua:

﴿ وَلِنَجْعَلَكَ آيَةً لِلنَّاسِ وَٱنْظُرْ إِلَى ٱلعِظَامِ كَيْفَ نُنْشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْماً فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

WalinajAAalaka ayatan lilnnasi waonthur ila alAAidhami kayfa nunshizuha thumma naksooha lahman falamma tabayyana lahu qala aAAlamu anna Allaha AAala kulli shay-in qadeerun*(Surat Al Baqara 2:259)*

Tafsir: ***Hivyo tunakufanya wewe kua Dalili kwa Watu. Angalia Mifupa na namna tunavyoiunganisha na kuivisha Nyama' na hivyo hili lilipokua wazi basi akasema: 'Najua sasa hivi kua Kwa Hakika Allah ni mwenye kuweza kufanya kila kitu.'***

Ambapo anasema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu kua: '**Baada ya *Allah Subhanah wa Taala* kumfufua Uzayr baada ya kumfisha ya kwa Muda wa miaka 100. Basi Uzayr akapanda Punda wake huyo na kuanza Safari ya kuelekea kwenye Mji wa watu wake, hadi akafika kwenye Mji wa Watu wake.**

‘Na alipofika katika Mji huo basi hakua ni mwenye Kuyafahamu Makazi yake aliyokua akiishi hapo Kabla alipokua Mdogo, na pia hakukua na hata mtu mmoja aliekua akimjua Uzayr hata kidogo.
Lakini hata hivyo baada ya muda mrefu Uzayr akajaribu kubahatisha, kutafuta sehemu aliyokulia na alipofika katika eneo hilo akakutana na Bibi Kizee sana, ambae alikua ni Kipofu na hata kutembea hawezi.’

Uzayr akakumbuka kua huyo Bibi alikua ni Mfanyakazi wake, ambapo Uzayr alipoondoka katika Mji huo basi Mfanyakazi huyo alikua na Umri wa miaka 20.

Hivyo Uzayr akamuuliza Bibi huyo: 'Hivi Jee hapa ndipo alipokua akiishi Uzayr'?’

Bibi huyo akajibu: \Naam hapa ndio Nyumbani kwake, ila Hakuna aliekua akimuuliza kwa Muda mrefh kwani watu wameshamsahau aliondoka miaka mingi saana.

Uzayr akasema: Hakika mimi ndio Uzayr mwenyewe.

Bibi huyo akasema: Subhanah Allah! Uzayr ametoweka kwa mda wa zaidi ya miaka mia.

Uzayr akasema: Hakika mie ndie Uzayr kwani Allah alinisababishia kufariki kwa miaka 100 na kisha akanifufua.

Yule Bibi akasema: Mimi Namjua Uzayr, kwani alikua ni mtu ambae ni Mcha Mungu na akiomba Dua basi Dua zake hujibiwa, alikua akiwaombea wagonjwa hua wanapona.

Hivyo kama wewe kweli ndie Uzayr basi niombee nipate kuona kisha nitapata kukuona na kukujua kua kweli wewe ni Uzayr. Ambapo Uzayr akamuombea Bibi huyo na kisha akampapasa Uso wake na Allah Subhanah wa Taala akamjaalia Bibi huyo kua ni mwenye kuona.

Na kisha Uzayr akamkamata Mkono Bibi huyo na kumwambia Simama Utembee kwa Idhini ya Allah. Bibi huyo akasimama na kumwangalia Uzayr na hapo hapo akamjua kua kweli yeye ndie Uzayr.

Tunapoangalia katika kipindi cha uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akijaribu kuwausia Mayahudi wa Madina kuhusiana na Imani Dini ya Kiislam basi nao Mayahudi hao walipingana nae kwa kusema kama anavyosema Bahr ul Ilm Abd Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu kua: **Siku Moja Salam Ibn Muhkam, Nuuman ibn Abu Awf na Shas Ibn Qays walimfuata Rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Na kumwambia kua: ‘Ewe Muhammad Inakuaje kua wewe unatutegemea kua sisi tukufuate wakati wewe huamini kua Uzayr ni Mtoto wa Allah?’**

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha aya isemayo:

﴿وَقَالَتِ ٱلۡيَهُودُ عُزَيۡرٌ ٱبۡنُ ٱللَّهِ وَقَالَتِ ٱلنَّصَارَى ٱلۡمَسِيحُ ٱبۡنُ ٱللَّهِ ذَٰلِكَ قَوۡلُهُم بِأَفۡوَٰهِهِمۡ يُضَاهِـُٔونَ قَوۡلَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِن قَبۡلُ قَٰتَلَهُمُ ٱللَّهُ أَنَّىٰ يُؤۡفَكُونَ﴾

Waqalati alyahoodu AAuzayrun ibnu Allahi waqalati alnnasara almaseehu ibnu Allahi dhalika qawluhum bi-afwahihim yudahi-oona qawla alladheena kafaroo min qablu qatalahumu Allahu anna yu/fakoona*(Surat At Tawba 9:30)*

Tafsir: ***Na Wanasema Mayahudi kua Uzayr ni Mtoto wa Mungu Na Wanasema Manasara Masih ni Mtoto wa Mungu Hizo ni Kauli zao Kutoka Midomoni mwao Wanaiga Kauli za wale ambao waliokufuru Kabla yao Laana ya Allah iwe juu yao Wako Mbali sana na Ukweli.***

Na kwa upande mwengine basi Anasema pia Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas **Radhi Allahu Anhu** kua: **Kuna kipindi watu wa Bani Israil walikua waasi sana mbele ya Mola wao, hivyo Allah Subhanah wa Taala akaifuta Tawrat yote kutoka kwenye vifua vyao. Na pia wakaipoteza Tawrat waliyoiandika ambayo ilitekwa baada ya vita na Maadui zao.**

Ambapo katika kipindi hiki Uzayr alikua amekimbikia Milimani, na hivyo akaomba Dua kwa Allah Subhanah wa Taala kua akumbushwe tena Tawrat kwenye ufahamu wake na akakumbushwa.

Lakini hata hivyo watu wa Bani Israil wakawa hawamuaminia kutokana na Tawrat hio aliyokua akiisoma kutoka kifuani mwake. Hadi pale Allah Subhanah wa Taala Alipojaalia kupatikana tena kwa Tawrati iliyotekwa na Maadui zao, na kisha Mayahudi wakamsikiliza Uzayr akiwa ni mwenye kuisoma Tawrat kutoka Moyoni mwake na kuilinganisha na Tawrat iliyopatikana baada ya kutekwa.

Na walipoona kua ni kweli Tawrati ya Uzayr aisomayo haina tofauti na Tawrat waliyoipata, basi ndio wakaamua kusema kua Uzayr ni Mtoto wa Mungu.

Naam..aya yetu imemalizia kwa kusema:

﴿ قَاتَلَهُمُ ٱللَّهُ أَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ﴾

Qatalahumu Allahu anna yu/fakoona*(Surat At Tawba 9:30)*

Tafsir: ***Laana ya Allah iwe juu yao Wako Mbali sana na Ukweli.***

Qatalahumu Allahu Ambapo tumetafsiri kwa maana ya kua: ***Laana ya Allah iwe juu yao***

Hivyo ingawa neno *Qatalahumu* linatokana na neno *Qatala* lenye kumaanisha Kukatili, Kuua au Kuchinja.

Lakini linapotumika katika hali hii ya kuambatanishwa na Muumba yaani Allah basi hua linamaanisha: **Laana za Allah Subhanah wa Ta'ala ziwe juu yao watu waliozungumziwa kwenye ayah hii.'**

Naam..tunarudi kwa Tamlikha ambae baada ya kusoma Maneno aliyoyaona Juu la lango la Mji huo, basi hakua ni mwenye kuamini macho yake kwani Jana tu yeye na Wenzake walikuimbia Mji kwa sababu Mungu wa Mji huo alikua ni Duqyanus. Lakini leo hii Ghafla moja hali imebadilika, hivyo Tamlikha akachanganyikiwa kisha akafikicha macho yake kwa mikono yake na kuyafumbua tena huku akijiuliza Macho yangu hayaoni yamejaa Usingizi bado au mimi nimepotea njia zaid.

Lakini kila akiangalia Masafa na Upande alipelekea basi anaona sio makubwa kiasi ya kua awe amepotea Njia.

Hivyo akanyanyua uso juu tena kusoma maneno yaliyoandikwa kwenye Lango hilo na akaona kua Macho yake hayamdaganyi, ila mazingira yamebadilika kweli tena sana. Na hana la kufanya kwani wenzake wanamsubiri ili wapate chakula atakachowapelekea ambacho wanakitegemea hivyo Tamlikha akajizidishia Imani ndani ya Moyo kua yuko kwenye Mji uliokua salama.

Hivyo Taratibu akaingia kwenye Mji huo kwa kupitia kwenye Lango hilo na kujikuta akiwa na watu ambao wengi wao wamekaa na kusomeshana Injil, kwa lugha ngeni kidogo na hakuna hata mtu mmoja ambae yeye anamjua miongoni mwa watu hao, na akaona haina haja ya kushangaa sana hadi akagundulikana kua ni Mgeni au Mkimbizi au Muasi hivyo, basi akaendelea kutembea ndani na mara katika kutembea kwake akakutana na Duka linalouza Mikate.

Hivyo akaingia kwenye Duka hilo na kusalimia na kisha akamuuliza Muuza Duka kwa kusema: **‘Ewe Muuza Mikate, mimi ni mgeni hapa hebu niambie huu mji wenu unaitwaje?’**

Ambapo Muuza Mikate akasema: ‘**Huu Mji Unaitwa Ephesus’**

Tamlikha akauliza tena: ‘**Na Jee Mfalme wenu anaitwaje?’**

Muuza Mikate akasema: **‘Anaitwa Abd Rahman’**

Tamlikha akasema: **‘Kama Unasema Kweli basi hali yangu mie nazidi kujiona kua ni Mgeni na kila kitu changu ni cha Kigeni, hivyo hebu Mkate kwa pesa hii’**

Na Kisha Tamlikha akaingiza Mkono Mfukoni na kutoa ile Pesa aliyopewa na wenzake ambayo ilikua ni Pesa iliyokua ikitumika katika Mji huo huo pale kable ya Kulala kwao Lakini bila ya yeye kujua kua Imepita Miaka 309 tangu Pesa yake hio aliyoitoa kua ni yenye kutumika.

Na hivyo alipoitoa na kumpa Muuza Mikate basi Muuza Mikate akaipokea Pesa hio huku akiwa na Mshangao Mkubwa sana, kwani Pesa aliyopewa na Tamlikha ilikua ni Kubwa zaid kiumbo na ni nzito kuliko Pesa wanazotumia wao leo hii kwenye mji wao, na yeye Muuzaji Mikate huyo hajawahi kuiona tangu azaliwe aina hio ya Pesa hivyo akasema kumwambia Tamlikha: **‘Hivi umeipata wapi Fedha hii? Au umegundua Hazina Ardhini wewe? Hebu Niambie ilikuaje? Na kisha itabidi namimi unigaie pia la kama si hivyo basi itanibidi nipeleke Habari kwa Mfalme ili ajue kuhusiana na wewe na hio Hazina uliyoivumbua.’**

Tamlikha akasema: **‘Subhanah Allah! Hazina gani unayoizungumzia wewe? Kwani hii ni Dirham yangu ambayo niliipata baada ya Kuuza Tende zangu siku mbili tatu zilizopita wakati Mfalme Duqyanus Alipokua anatawala, hivyo hakuna hazina yeyote.’**

Kusikia maneno hayo basi Muuza mikate akaja juu na kusema: **‘Ama wewe ni Mtu mbaya na Mchoyo sana yaani Umeokota Hazina halafu bado hujatosheka Unataka kua nayo peke yako, halafu unajidai kuhusiana na mambo yasiyoingia Akilini kuhusiana na Mfalme ambae alikua akijiita Mungu ambae alifariki Miaka 300 iliyopita, Hivyo Usinitae, tugawane hazina hio au nitakupeleka kwa Mfalme’**

Na kisha hapo hapo akamrukia Tamlikha na kumkunja Nguo yake aliyovaa ya Ufugaji wa Kondoo na kusema kwa sauti: ‘**Twende kwa Mfalme!’**

Wakati tukio hili la kukunjwa kwake Tamlikha linatokea lilimchanganya akilini kwani nae alikua katika hali aya mtu asiejua kinachoendelea kwa sababu anayoambiwa hayaingii akilini na anayoysema yeye ambayo ni ya kweli basi Muuza Mikate anaona kua hayaingii Akilini.

Hivyo tukio hili pia likapelekea watu waliokuwepo katika eneo hilo nao kuanza kuwazunguka Taikha na Muuza Mikate wakitaka kujua kulikoni. Hivyo Muuza Mikate akaelezea na kisha baada ta kusikia habari hio basi Watu wakaamua kua Tamlikha apelekwe kwa Mfalme ili ikaamuliwe kesi yake kwa kuonesha wapi alipogundua Hazina hio.

Hivyo Tamlikha akachukuliwa huku akiwa katika hali ya kukunjwa ili asikimbie hadi kwenye Kasri la Mfalme na kisha Walinzi wa Kasri wakapewa habari na hivyo nao wakaipeleka mbele ya Mfalme. Mfalme alipopata Habari hio akaomba kua Tamlikha aletwe mbele yake ili amhoji. Na hivyo Tamlikha akaletwa mbele ya Mfalme huku akiwa anatetemeka kwa khofu.

Lakini Mfalme alipomuona katika hali hio basi akamwambia Tamlikha kua**: Usiwe na Khofu kwani Sheria Yetu kupitia kwa alivyotuamrisha Isa Ibn Maryam inasema kua sisi tunatakiwa tuchukue asilimia 5% tu ya Mali yako na hivyo iliyobakia itakua ni yako utaifanya utakavyo.'**

Hiyvo Tamlikha akajitetea kwa kusema: '**Ewe Mfalme Mtukufu, hakika mimi si mtu niliogundua wala kuokota Hazina ya aina yeyote, hii Pesa niliyokua nayo ni yangu na ndio hii hii niliyokua nayo ambayo Juzi tu nililipwa baada ya kuuza Tende nilizokua nazo, na mimi ni Mwenyeji wa Mji huu hivyo nakuomba uniruhusu kuthibitisha hilo.'**

Watu waliopo kwenye Baraza ya Mbele ya Mfalme wakatizamana, huku wakiwa wamejawa na Mshangao.

Kisha Mfalme akasema: '**Sawa ila sasa Tutathibitishaje kua wewe ni Mtu wa Mji huuHivi jee kuna Mtu yeyote yule ambae ni Maarufu unamjua na anakujua ili ututajie Jina tumwite athibitishe hilo?'**

Tamlikha akasema **'Naam'** na kisha akataja Majina ya Watu 20 waliokua ni Mawaziri wa Duqyanus akataja na Vyeo vyao, na Majina hayo yaliwashangaza zaid watu hao, kwani hakuna hata mmoja miongoni mwa wenye Majina hayo alikua ni mwenye kujulikana. Kwani Hali ya Baraza ikawa Kimyaa kila mtu anamuangalia Tamlikha kwa mshangao mkubwa zaidi, kwani habari zake ni ngeni sana na za Kushangaza.

Hivyo Mfalme akamuuliza Tamlikha: **'Haya Majina na Vyeo vyote ulivyovitaja basi Hawajulikani watu hawa, hawa unaowazungumzia wewe si watu wa Kizazi chetu na wala hakujawahi kua na Watu kama hao wenye Vyeo na Majina hayo'**

Mfalme akaendelea kusema: **'Hivyo Nakupa Nafasi ya Mwisho, kua kama wewe kweli ni Miongoni mwa watu wangu basi tupeleke katika Nyumba unayoishi'**

Tamlikha akasema: **'Shukran, nitafanya hivyo, hivyo twendeni'**

Hivyo Mfalme akawatuma watu wake watoke pamoja na Tamlikha hadi katika Nyumba anayosema kua anaishi, na Watu hao wakatoka, na Tamlikha hadi kwenye upande ambao Walikua wanakaa wazee wa Tamlikha, na kisha alipofika akaikuta Nyumba yao kwenye sehemu hio. Na walipofika akasema: **'Humu ndimo ninamoishi'**

Na hivyo Mlango ukagongwa na Watu wa Mfalme na ulipofunguliwa akatokea Mtu mzima Kizee sana ambae alikua na muonekano wa kua ameshtuka kutokana na Kuona Watu wa Mfalme Mlangoni mwake. Hivyo akawauliza watu hao: **'Enyi Watu wa Mfalme, Vipi Salama? Kuna nini tena?'**

Watu hao wakasema: **'Salama, ila huyu bwana hapa anasema kua yeye anakaa kwenye nyumba hii, hivyo Mfalme ametutuma tuthibititishe.'**

Yule mzee akazidi kushtuka, kwani yeye ndie mwenye Nyumba amezaliwa humo na amekulia humo na kuishi humo miaka yote halafu mzee halafu ghafla moja anaambiwa kua Mwenye Katokea na hii inamaanisha kua yeye si Mwenye Nyumba. Hivyo Mzee huyo akajawa na Khofu iliyochanganyika na Hasira, hivyo akamwangalia Tamlikha na kisha akamuuliza: **'Hivi kwanini wewe Kijana unasema usiyoyajua? Kwanini unasema unavyosema? Jee imekuaje? Na Wewe ni nani hasa?'**

Tamlikha akasema: **'Mimi naitwa Tamlikha Ibn Filastin na hii ni Nyumba ya wazee wangu'**

Baada ya kusikia hayo, Mzee akashtuka zaid na kuchanganyikiwa na kusema: **'Unasema ni Nani?'**

Tamlikha akasema : **'Mimi ni Tamlikha Ibn Filastin'**

Ambapo baada ya kusikia meneno hayo Yule mzee akaishiwa na nguvu na akaanguka chini, alipokuja juu akaikamata mikono ya Tamlikha na kuibusu na kusema: **'Bila ya shaka wewe ndie yule Babu Yangu' Yule Mzee akaendelea kusema: Wallahi nnaapa mimi kwa Mungu wa Al Kaabah kua huyu Mzee ndie Babu yangu ambae alikua ni miongoni mwa Vijana waliomkimbia Duqyanus kwa ajili ya kumkimbilia Mola wa Ulimwengu wote, na tuliambiwa sisi kua watarudi tena kwa mara ya Mwisho.'**

Hivyo Tamlikha akakaribishwa ndani ya Nyumba na kisha Wajumbe wa Mfalme Abd Rahman wakarudisha habari kwa Mfalme, Ambapo Mfalme alipopata habari ya Tamlikha basi akapanda Farasi wake na Walinzi wake wakaelekea moja kwa moja hadi kwenye Nyumba ya Tamlikha huku wakiwa na hamu kubwa sana ya kujua kisa cha Tamlikha na wenzake kwa ukamilifu.

Na walipofika Mfalme akashuka kutoka juu ya Farasi wake huku akiwa na Furaha na kisha akamchukua Tamlikha na Familia yake kuenda nae kwenye Kasri lake ili kumhoji zaidi.

Ambapo Njiani watu walikua wakimzonga kwa kila mmoja kutaka kumbusu mkono au mguu wake. Na walipofika kwenye Kasri basi Tamlikha akaelezea yaliyotokea yote tangu mwanzo hadi mwisho.

Baada ya kumaliza kuelezea basi Mfalme akasema: **'Sasa itabidi utupeleke kwa wenzako ili nao tuwaone.'**

Tamlikha akasema : **'Wako kwenye hilo pango nimewawacha hivyo twendeni nikawapelekee chakula tukawachukue.'**

Na Ingawa Mfalme na watu wake walikua ni wafuasi wa Nabii Isa *Alayhi Salam* lakini kwenye Mji huo pia kulikua kuna watu wasiomuamini Nabii Isa.

Ambapo nao walikua na kiongozi wao. Hivyo walipopata habari hio ya Tamlikha na kusikia kua Mfalme anatoka na Tamlikha na Watu wake kwa ajili ya kuelekea kwenye Al Kahf.

Basi nao wakaunganisha katika Msafara huo ili kuona hayo yaliyotokea. Hivyo Msafara huo uliokua ukiongozwa na Tamlikha na Mfalme na watu wengine ukaelekea kwenye eneo la Pango walilojificha wenzake Tamlikha.

Na walipokaribia basi Tamlikha akamwambia Mfalme na watu wake kua: **'Tumekaribia hivyo itabidi Nyote mshuke kwenye Farasi wenu kisha tuende kwa miguu kwa sababu sitaki wenzangu wawe ni wenye kusikia sauti za Kwato za Farasi kwani watajawa na Khofu na kuona kua nimewasaliti Na kisha sijui watachukua hatua gani kutokana na kutuona kwao kwani huenda Wakadhani kua Duqyanus amewafuata ili awaue.'**

Hivyo Mfalme na watu wake wakakubaliana na Shauri hilo na wakashuka na kutembea kwa miguu. Na kisha walipokaribia kwenye Jabali basi Tamlikha akamwambia Mfalme kua: **'Hapa sasa itabidi mnisubiri ili niende nikawaelezee kwanza yaliyotokea'**

Kisha Tamlikha alipoingia ndani na kukukutana na wenzake basi wenzake hao walifurahi sana kumuona kua amerudi salama na kumkumbatia kwa Furaha huku wakisema: **'Sifa zote Anastahiki Mola wetu kwa kukuongoza na kukuokoa wewe na kutokana na Duqyanus.'**

Ambapo Tamlikha akawatuliza na kuwaambia kua: 'Imetosha kuhusiana na kumzungumzia na kumkumbuka Duqyanus, Ila sasa hivi inabidi nikuulozeni tena lile suali tulilojiuliza mwanzo ambalo ni Hivi Jee mnadhani tulilala kwa Mda wa Siku ngapi?'

Na Wenzake hao wakarudia kujibu vile vile kua: '**Hatukulala mda mrefu sana kwani tumelala kwa mda siku Moja au sehemu ya siku moja.'**

Tamlikha akajibu kwa kusema; **'La! Hakika sisi tulikua tumelala kwa mda wa Miaka 309 Kwani hivi sasa ninavyozungumza basi Duqyanus ameshafariki tena sio leo bali kwa karne na ziliopita. Na watu wa Mji wetu wote wamebadilika kuna vizazi vipya kabisa ambao wote ni wenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na wanatawaliwa na Mfalme aitwae Abd Rahman ambae yeye na watu wake wako chini ya Mlima wanakusubirini wakupokeeni kwa ari na furaha'**

Baada ya As-hab Al Kahf kuyasikia maneno hayo basi hawakuweza kuyaamini masikio yao juu ya yale wanayoyasikia, kua wamelala miaka 309 wakati kwao wao ilikua ni kama kulala ndani ya masaa kadhaa tu. Na mbali ya hivyo lakini pia Watu wao wote wamekua ni wenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wamekuja na Mfalme wao kwa ajili yao.

Naam..nadhani kama ingekua mimi na wewe leo hii na namna tunavyopenda Vyeo na Umaarufu na kua Karibu na wenye Mamlaka Kutokana na kua na Imani Dhaifu basi bila ya shaka tungetoka moja kwa moja kwa ajili ya Mapokezi hayo ya kupokewa na Mfalme na kurudi katika Maisha ya Kuishi ndani ya Kasri la Kifalme.

Lakini hapa tunawazungumzia Vijana ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewapa jina la *Fityatun* yaani Vijana Mashujaa wasiofika 10 wenye Msimamo thabiti wa Imani yao kiasi ya kua Wamekua Werevu wasiojali chochote isipokua kua karibu na Mola wao. Hivyo Fityatun hao wakaangaliana na kutafakkari kisha wakasema: **'Ewe Tamlikha, hakika wewe unataka kutufanya sisi kua ni Mtihani kwa ajili ya Ibn Adam'**

Hivyo Tamlikha akauliza: **'Kwa hivyo Jee mnataka tufanyeje?'**

Vijana hao wakasema: **‘Nyanyua Mikono yako Juu nasi tunyanyue yetu kwa ajili ya Kumuomba Mola wetu ili atudhihirishie Khatma yetu’**

Hivyo Tamlikha akanyanyua Mikono yake juu, kisha na wenzake hao nao wakanyanyua mikono yao Juu na kisha Tamlikha akasema: ‘**Ya Allah, Kutokana na Maajabu na Miujiza uliyotuonesha sisi ndani ya Nafsi zetu na Waja wako wengineo waliopo nje ya Pango, basi tunakuomba kua huu uwe uthibitisho tosha kwa Walimwengu, na hivyo tuchukue tuwe karibu nawe na tupate kua mbali na Walimwengu.’**

Hivyo baada ya kuomba Dua yao hio basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawajibu Dua hio kwa kumtuma *Malakat Al Mawt* na kuzichukua Roho zao *As-hab Al Kahf* hapo hapo wote kwa pamoja.

Na kisha baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akaujaalia Mlango wa Pango hilo ambao hapo awali Ulikua ni wenye kua wazi hadi wakaingia ndani yake Vijana hawa wa *As-hab Al Kahf* na kisha ukawa ni mwenye kuzibwa na Mfalme Duqyanus, na kisha pia kua Mlango huo kua ni wenye kua wazi baada ya Miaka 309 katika Siku waliyoamka kina Tamlikha kutokana na Uwezo wake na Usimamizi wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yao na juu ya Pango lao.

Basi hapo hapo katika siku hii ya Kufa kwao Kina Tamlikha basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliujaalia Mlango huo kua ni wenye kufunga na hivyo kwa watu waliokua nje ilikua ni vigumu kujua kua kama kuna Pango sehemu hio au kama Kulikua na Mlango katika Sehemu hio, kwani katika kuziba kwake basi hakukuonekana hata ule ufa, na ukuta ulikua kama kwamba tangu Mlima huo Ulipoumbwa basi haujawahi hata kuguswa katika sehemu hio?

Kwani *Allah Subhahan wa Ta'ala* analielezea tukio hili pale aliposema katika Qur'an kua:

﴿وَكَذَٰلِكَ أَعْثَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوٓاْ أَنَّ وَعْدَ ٱللَّهِ حَقٌّ وَأَنَّ ٱلسَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا﴾

Waka<u>dha</u>lika aAAtharn<u>a</u> AAalayhim liyaAAlamoo anna waAAda All<u>a</u>hi <u>h</u>aqqun waanna als<u>a</u>AAata l<u>a</u> rayba feeh<u>a</u> *(Surat Al Kahf 18:21)*

*Tafsir**: Na Kadhalika tumelifanya Jambo lao kua ni lenye kujulikana na watu ili wapate kujua kua Ahadi ya Allah (Subhanah wa Ta’ala) ni ya kweli na hivyo hakuna shaka kuhusiana na Saa ya siku ya Malipo.***

Subhanah Allah, Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kuhusiana na kisa hiki cha watu hawa kua ni Uthibitisho wa kua kama alivyoahidi kua Tutafufuliwa kama walivyofufuliwa wao na Saa ya Kiama ipo kama ilivyoahidiwa na Mwenyewe Muumba. Hivyo kwa wale wenye kubisha basi huu ni uthibitisho tosha.

Ambapo anasema Imam Abu Abd Allah Sahl Al Tustari : **‘Kwa muonekano wa nje hii inamaanisha kuashiria Mamlaka na kwa muonekano wa ndani basi hua inamaanisha *Nafs Al Ruh*, Ufahamu *Fahm Al Aql* na Mitihani ya Moyo kupitia katika kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta’ala*’**

Naam..tunaporudi katika kisa chetu basi Mfalme na watu wake walikaa chini ya Mlima kwa siku nzima bila ya Kuona Dalili ya Tamlikha wala Fityanus wenzake.

Hivyo ilipofika jioni yake Basi Mfalme akaamrisha watu wapande na kukaribia hadi kwenye Jabali kisha wachungulie Nyuma yake kua jee kuna nini? Na bila ya Shaka walipoanda juu yake Jabali hilo

na walipoangalia Upande wa Pili wakakutana na Ukuta mkubwa sana wa Mlima. Ambapo ukuta huo haukuonesha hata dalili hata ile ya kuguswa

Watu hao wakashangaa na kua na masuali mengi yasiyokua na Majibu, ikiwepo Tamlikha na wenzake wameyayukia wapi? Kwani haiwezekani kua wamekimbia au wameondoka kutokana n akua kama wangekua wameondoka basi waliondoka vipi wakati Jabali lililouzunguka Mlango wa Pango alilolielezea Tamlikha lilikua liko wazi kutokana na mitizamo ya macho yao na hivyo katika siku hio nzima na hivyo haiwezekani kuingia au kutoka au kupita kakika eneo hilo lenye Jabali hilo na kuelekea sehemu nyengine bila ya wao kuwaona.

Hivyo na wao wakajikuta katika hali kama aliyokua nayo Tamlikha hapo kabla alipowasili kwenye mji wao..yaani hali ya Kutoamini macho yao juu ya kile walichokua wakikiona na baada ya Watu wa Mfalme kutoona Kitu chochote mbele yao basi wakampa Habari mfalme ambapo nae akaja kuthibitisha juu ya hilo. Mfalme akatoa amri kua sehemu yote hio ya eneo hilo ipekuliwe juu chini kwani labda huenda ikawa kuna Mlango wa Siri wasioijua wao.

Hivyo Watu wakakusanyika na kulizingira eneo hilo na kulipekua hatua baada ya hatua bila ya kupatikana mafanikio yeyote. Na hivyo Wakakubaliana kua kweli kina Tamlikha walikua ni watu wa Miujiza katika kuishi kwao miaka yote waliyoishi ndani ya pango na pia ni wenye Miujiza katika kutoweka kwao.

Hivyo Mfalme akakubali na kuthibitisha kua hii yote ilikua ni Miujiza ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kuonesha Rehma na uwezo wake juu ya Viumbe wake, na Mfalme akaamrisha kua katika sehemu hio itabidi Ujengwe Msikiti ambao utakua ni wenye Kusaliwa na pia kua kama Athari ya Kumbukumbu juu ya Tukio hilo.

Hivyo baada ya Mfalme kutoa tangazo hilo, basi wale wasioamini miongoni mwao wakasema la, hawa watu hawakufariki wakati wakiwa katika Dini yenu, bali walifariki wakati wakiwa kwemye Dini yetu. Hivyo Sisi tutajenga Hekalu katika sehemu hii, na hivyo wakawa ni wenye kupingana na Amri ya Mfalme basi ikabidi itokee Tafrani kubwa sana kwani kila upande ulikua ukiamini na kusema wao ndio wana haki zaidi ya kujenga Jengo la kuabudia katika eneo hilo kwani watu hao walikua ni watu wa upande wake.

Hivyo yakatokea mapigano makubwa hadi wale wasiokua ni wenye kuamini wakashindwa na kuuawa, Na Hivyo Mfalme akawa ni mwenye kushinda na kuamrisha kujengwa kwa Msikiti kwenye eneo hilo. *Ambapo Allah Subhanah wa Ta'ala* anielezea hali ilivyokua katika eneo la tuki kwa kusema ndani ya maneno yanayofuatia ya Aya ya 21 ya *Surat Al Kahf* yasemayo:

﴿وَكَذٰلِكَ أَعْثَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوٓاْ أَنَّ وَعْدَ ٱللَّهِ حَقٌّ وَأَنَّ ٱلسَّاعَةَ لاَ رَيْبَ فِيهَا إِذْ يَتَنَازَعُونَ بَيْنَهُمْ أَمْرَهُمْ فَقَالُواْ ٱبْنُواْ عَلَيْهِمْ بُنْيَاناً رَّبُّهُمْ أَعْلَمُ بِهِمْ قَالَ ٱلَّذِينَ غَلَبُواْ عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِمْ مَّسْجِداً﴾

Wakadhalika aAAtharna AAalayhim liyaAAlamoo anna waAAda Allahi haqqun waanna alsaAAata la rayba feeha idh yatanazaAAoona baynahum amrahum faqaloo ibnoo AAalayhim bunyanan rabbuhum aAAlamu bihim qala alladheena ghalaboo AAala amrihim lanattakhidhanna AAalayhim masjidan*(Surat Al Kahf 18:21)*

*Tafsir**: Na Kadhalika tumelifanya Jambo lao kua ni lenye kujulikana na watu ili wapate kujua kua Ahadi ya Allah (Subhanah wa Ta'ala) ni ya kweli na hivyo hakuna shaka kuhusiana na Saa***

ya siku ya Malipo. Wakati wao (watu wa Mji huo) walipoanza kubishana miongoni mwao juu yao basi wakasema: 'Jengeni Jengo juu yao, Mola wao ni mwenye kujua zaidi juu yao' na kisha wale walioshinda Hoja wakasema: Kwa Hakika tutajenga Jengo la Ibada juu yao.
Ambapo katika Aya hii basi tunaona kua ndani yake mna Hukmu inayotudhihirishia kua inaruhusika kujenga Msikiti kwenye Sehemu yenye Kaburi, na ianruhusika kusali Ndani yake Miskiti hio, iwe karibu husika limo ndani ya Msikiti kama ilivyokua kwenye Masjid An Nabawi mjini Madina ambalo Ndaniyake mna Kaburi la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, au iwe liko pembeni yake au mbele au nyuma yake kama kwenye eneo la ardhi Masjid Al Aqsa n.k.

Kwani Kutokana na aya hii tunaona kua watu waliowaona *As-hab Al Kahf* baada ya kulala pangoni kwa miaka 300 wakaamka na kisha wakafa baada ya kuonekana kufa kwao, wale waliowaona wakasema: '**Tuwajengee jengo juu yao**' na wengine wakasema: '**Kwa hakika tutawajengea jengo la kuabudia juu yao**', maana ya maneno haya katika aya hii yanaonesha kua kauli ya kwanza ilisemwa na Washirikina na kauli ya pili ilisemwa na wenye kuamini Mungu mmoja. Aya inaelezea kauli zote mbili bila ya kuonesha kupinga au kukataza jambo hilo, na kama ingelikua jambo hilo si sahih basi aya hiyo ingelionesha kukosoa kosa hilo kwa njia moja ama nyengine.

Kutokana na aya hii kukubaliana na kauli zote mbili basi inatoa ushahidi tosha kua jambo hili halikukatazwa kisharia. Ukweli ni kua aya inawakilisha kauli ya Walioamini Mungu mmoja katika njia inayoonesha kuisifu kauli yao dhidi ya kauli ya Washirikina ambayo imefunikwa na mashaka wakati kauli ya Walioamini Mungu mmoja ni yenye maamuzi ya mwisho, Kwa hakika tutawajengea jengo, na inatokana na mtazamo wa Iman. Hawakutaka kujenga jengo tu, bali walitaka kujenga sehemu ya kuabudia. Kauli hii inonesha kua watu hao walikua wakimjua Mungu na wanakubaliana na kuabudu na kusali.

Anasema Imam Fakhr Ad Din Al Razi katika *Tafsir al Kabir* kuhusiana na kauli ya Kwa hakika tutawajengea sehemu ya kuabudia juu yao kua ni sehemu ya '**Kumuabudia Mungu na huku ikiwa na maana ya kuyahifadhi mabaki yao watu hao wa *As-hab Al Kahf* .**'

Imam Al Shawkani yeye anasema kua: '**Kutajwa kwa jengo la kuabudia kunamaanisha kua 'Wale walioshinda hoja yao' ni Waislam. Lakini ikasemekana kua ni watu wa Mfalme na Sultan wa watu waliotajwa hapo, kwani wao ndio walioshinda hoja dhidi ya wenzao, na mtazamo wa kwanza ndio bora zaid**'.

Imam Al Zajaj nae akasema kua: **'Hii inaonesha kua jambo hilo lilipowekwa wazi, Walioamini walishinda kutokana na sababu ya ushahidi wa kufufuliwa na pia Miskiti ni kwa ajili ya Walioamini'**. Hivyo ndivyo ilivyotajwa katika *Qur'an* kuhusiana na suali la kujenga Miskiti juu ya Makaburi.

Ushahidi uliopo katika *Sunnah* ni ule uliotajwa katika *Hadith* ya Abu Nusayr isemayo kua amesema Imam Abd Al Razaq, kua kutokana kwa Ma'mar kutokana na Muhammad Ibn Muslim Ibn Shihab Al Zuhri ambae amesema kua: '**Abu Basir *Radhi Allahu Anhu* alikimbia kutoka kwa Washirikina baada ya Mkataba wa Hudaybiyyah. Akakimbilia katika mwambao wa bahari na Abu Jandal Ibn Suhayl Ibn 'Amr *Radhi Allahu Anhu* nae akamfuata huko baada ya kukimbia kutoka kwa Washirikina. Wakaungana na Waislam wengine wapatao 300. Abu Basir alikua akiwasalisha na kisha husema, 'Allahu Akbar, yeyote yule atakae mnusuru (*yansur Allah)* Allah basi atalindwa na Allah'**.

Wakati Abu Jandal alipoungana nao aliwasalisha sala zao. Na haukupita msafara hata mmoja wa *Quraysh* isipokua waliuvamia na kuua kila mtu na kuchukua kila kitu. Maquraysh

wakatuma ujumbe kwa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* wakimuomba kwa ajili Mungu na kwa ajili ya jamaa zake, kua awarudishe (Kina Abu Basir na wengineo), na kwa yeyote yule miongoni mwao atakae rudi basi atakua salama. Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* akamuandikia barua Abu Jandal na Abu Basir *Radhi Allahu Anhum* kuwaambia wao na wale waliokua pamoja nao warudi majumbani kwao na familia zao. Barua hiyo ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* ilipelekwa kwa Abu Jandal na Abu Basir *Radhi Allahu Anhum* ambae ilimfikia wakati akiwa mwishoni mwa uhai wake. Alikufa huku akiwa na barua hiyo mikononi mwake akiisoma. Hivyo Abu Jandal *Radhi Allahu Anhu* alimzika Abu Basir *Radhi Allahu Anhu* katika sehemu hiyo hiyo aliyofia na kisha akajenga Msikiti juu ya kaburi lake.'

Na kutokana na ushahidi wa Masahaba wa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam,* jambo hili limewekwa wazi katika utofauti wao katika maziko ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*. Hivi ndivyo alisema Imam Malik kuhusiana na tofauti zao kuhusiana na sehemu ya kumzika kua: **'Baadhi ya watu walitaka akazikwe kwenye Minbar, wengine wakashauri kua akazikwe katika Makaburi ya Baqi. Mara akawasili Abu Bakr na kusema: 'Nimemsikia Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* akisema kua: 'Hakuna Mtume aliekufa isipokua alizikwa katika sehemu hiyo hiyo aliyofia, hivyo chimbeni kaburi lake hapo hapo'''.**

Ushahidi uliokuwepo hapa ni kua Masahaba walitaka kumzika katika Minbar, ambayo kwa hakika ni sehemu iliyopo ndani ya Msikiti na hakuna hata mmoja alietolea ukali ushauri huo, Abu Bakr *Radhi Allahu Anhum* alipinga ushauri huo si kutokana na kua hairuhusiwi kumzika ndani ya Msikiti, bali kutokana kushikamana na amri yake ya kua azikwe katika sehemu ile ile ambayo ilipotolewa roho yake takatifu.

Tunapoangalia kuhusu sehemu aliyozikiwa Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* tunaona kua roho yake ilichukuliwa wakati akiwa yupo katika chumba cha Aisha *Radhi Allahu Anha*. Ukuta wa chumba hiki ulikua umeungana na Msikiti katika sehemu ambayo Waumini walikua wakisalia, hivyo hali ya chumba hiki na kulingana na Msikiti ni sawa sawa na hali ambayo tuliyokua nayo sasa hivi ambayo Mawalii wa Mwenyezi Mungu wamezikwa huku Makaburi yao yakiwa yameungana na Msikiti na watu wakiwa wanasali katika eneo la Msikiti.

Kuna wale wanaopinga hili kwa kusema kua hali hii inaruhusika kwa ajili ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* tu, jawabu juu ya jambo hili ni kua, ili kutoa hoja hii inabidi mtu atoe pia na ushahidi, na msingi wa hukmu ni kua, hukmu hua ya jumla hadi pale inapopatikana uthibitisho kuthibisha vyengineyo, na hapa hakuna ushahidi huo, hivyo hoja hiyo hua kaikubaliki. Ikiwa tutakubali kua hali hii inaruhusika kwa ajili ya Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam* tu (Jambo ambalo tumeshalithibitisha kua haiwezekani), basi jibu litakua Abu Bakr As Sidiq na Umar Ibn ul Khattab *Radhi Allahu Anhum* nao pia walizikwa ndani ya chumba hicho, na chumba hicho kimeungana na Msikiti, hivyo jee hali hii pia imeruhusika kwa Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum*?.

Masahaba waliendelea kusali ndani ya msikiti wa Madina ambao umeungana na chumba hicho chenye Makaburi matatu ndani yake, na *Aisha Radhi Allahu Anha aliishi* ndani ya chumba hicho, alisali sala zake za Fardhi na *Sunnah* ndani ya chumba hicho pia. Jee hii haitoshelezi kuonesha kua huu ni ushahidi wa vitendo na makubaliano ya Masahaba?

Kwa upande mwengine basi Kuyageuza makaburi kua Misikiti kumekatazwa na Nabii Muhammad *Salallahu A'layhi wa Salam*, na hili ni jambo tofauti na kujenga Msikiti katika maeneo yenye Makaburi iwe yameungana na Msikiti ama la. Aisha anasema kua Nabii Muhammad *Salallahu*

A'layhi wa Salam amesema, '**Allah *Subhanah wa Ta'ala* amewalaani Mayahudi na Wakristo [kwani] Makaburi ya Mitume wao wameyageuza kua Miskiti**', na katika *Hadith* iliyokaririwa na Muslim ina maneno yaliyotaja '**Makaburi ya Mitume wao na Watu wema**'

Wanazuoni wa Ummah hawakufahamu kutokana na *Hadith* hizi kua zina nia ya kukataza Miskiti kuungana na Makaburi, bali walitafsiri kisahihi kama inavyotakia kua kuyageuza Makaburi yenyewe kua ni sehemu ya kuisujudia hivyo watu kusujudia juu yake na kumuabudia mtu aliekuwemo ndani ya Kaburi kama wafanyavyo Mayahudi na Wakiristo. *Qur'an* inasema:

﴿ٱتَّخَذُوٓاْ أَحۡبَارَهُمۡ وَرُهۡبَانَهُمۡ أَرۡبَاباً مِّن دُونِ ٱللَّهِ وَٱلۡمَسِيحَ ٱبۡنَ مَرۡيَمَ وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلاَّ لِيَعۡبُدُوٓاْ إِلَٰهاً وَاحِداً لاَّ إِلَٰهَ إِلاَّ هُوَ سُبۡحَانَهُ عَمَّا يُشۡرِكُونَ﴾

Ittakhadhoo ahbarahum waruhbanahum arbaban min dooni Allahi waalmaseeha ibna maryama wama omiroo illa liyaAAbudoo ilahan wahidan la ilaha illa huwa subhanahu AAamma yushrikoona *(Surat At Tawba 9:31).*

Tafsir: ***Wao (Mayahudi na Wakristo) wamewafanya Rabbi wao na Watawa wao kua ni Miungu yao badala ya Allah (kwa kuwatii katika mambo waliyoyahalalisha au kuharamisha kutokana na matamanio yao bila ya kuamrishwa na Allah) na (wakamfanya kua ni Mungu wao) Isa Ibn Mariam wakati wao (Mayahudi na Wakristo) wameamrishwa (katika Taurati na ijnil) kutomuabudu yeyote isipokua Allah La illaha illa huwa (Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ispokua yeye) Sifa zote zinamstahiki yeye (yeye yuko mbali na juu sana) na wanavyomshirikisha.***

Waislam inawabidi kufahamu ni kitu gani hasa kilichokatazwa na sio kuangalia nini wamefanya Waislam wenzao ndani ya Miskiti yao na kudai kua *Hadith* hiyo inazungumzia Waislam. Hivi ndivyo vile Khawarij walivyofanya, *Allahuma nsurna*.

Abd Allah Ibn Umar alisema: '**Wamechukua aya (za *Qur'an*) ambazo zimeshushwa kuwazungumzia Makafiri, na wao wakazitumia kuwazungumzia Waislam**'. Hakuna Kanisa wala Sinagogi hata moja ambalo liko kama Miskiti ambao una Makaburi ambao baadhi ya watu wanasisitizia madai yao kua *Hadith* hii inayazungumzia.

Wanazuoni wameifahamu maana ya *Hadith* hizi kwa mtazamo wa kina wa ufahamu, ambao wameuweka wazi katika ufafanuzi wao. Shaykh Al Sindi anasema kuhusiana na *Hadith* hiyo kua: '**Kilichokusudiwa kutokana na kauli hii ni kuuonya Ummah kuhusiana na kulifanya Kaburi lake kua kama vile walivyofanya Mayahudi na Wakristo kwa Makaburi ya Mitume wao, ambalo ni kuyafanya na kuyageuza Miskiti aidha kwa kuyasujudia kwa njia ya kuyatukuza ama kuyafanya kua Kibla cha kukielekea wakati wa sala zao. Wamesema kua kujenga jengo la Msikiti karibu na mtu mwema ili kutafuta baraka zake haijakatazwa**'

Imam Ibn Hajar Asqalani na wafasiri wengine wa vitabu vya *Hadith*, wamezungumzia kauli ya Al Baydawi ambae alisema kua : '**Kwa kua Mayahudi walikua wakisujudia makaburi ya Mitume wao kwa kuyatukuza ki darja, na walikua wakiyafanya kua ndio Kibla chao pale wakati wanapotaka kusali, kwa kusali huku macho yao yakiwa yanayatazama makaburi hayo, hivyo wameyafanya kua ni masanamu, Allah amewalaani na pia amewakataza na kuwazuia Waislamu kufanya kama hivyo pia. Lakini kujenga Msikiti karibu na watu wema, au kusali pembeni ya kaburi lake katika kuomba msaada kupitia kwao au kwa ajili ya athari za Ibada**

kumfikia, na wala si kwa sababu ya kumtukuza au kumuelekea na kuyatazama [wakati wa kusali] basi hakuna kosa lolote juu ya hili. *(Ibn Hajr al-Asqalani, Fath al-Baari toleo la. 3 uk. 208*) **Hamuoni kaburi la Nabii Isma'il katika msikiti wa Makkah? Na Miskiti wa Makkah ndio msikiti bora kuliko yote ambao mtu akiambiwa achague kusali atauchagua. Hivyo makatazo ya kusali Makaburini yanahusiana na Makaburi yaliyokua wazi kutokana na uchafu uliokuwemo ndani yake.**'

Al Mubarkafuri anasema kuhusiana na *Al Tawrabishati* katika tafsiri yake ya Jami'i Imam Al Tirmidhii kua, '***Al Tawrabishati* amesema kua imekatazwa kwa njia mbili: Kwanza ni kua wao (Mayahudi na Wakristo) walikua wakisujudia makaburi ya Mtume wao katika kuwatukuza na hivyo hukusudia kufanya Ibada. Pili ni kua walikua wanakusudia kusali katika Makaburi ya Mitume wao na kuyaelekea Makaburi yao wanaposali na kumuabudu Mungu. Wanachukulia mambo hayo kua ni bora kuyafanya hapo kwa sababu ndio sehemu bora kwa Mungu na inahusisha mambo mawili**.'

Kutokana na misingi hiyo, tunaona kua Hukmu ya kusali katika Misikiti ambayo ina makaburi ni Sahih ikiwa Makaburi hayo yapo katika sehemu ambayo watu hawasali tofauti na Msikiti, na hakuna kinachofanya kusiruhusiwe au kuchukiza kuhusiana na kusali katika Msikiti ulioungana na ukuta wa Makaburi. Hata hivyo ikiwa Kaburi liko ndani ya Msikiti basi Sala itakayosaliwa humo ndani itakua haikubaliki kutokana na Mtizamo wa *Madhhab* ya Imam Hanbal, na Inaruhusika na ni Sahih kutokana na Mitizamo ya *Madhhab* mengine matatu ya Imam Abu hanifa, Imam Malik na Imam Al Shafi'i; isipokua wao wanasema kua haipendezi kwa kaburi kua mbele ya yule anaesali kutokana na kufanana baina ya hilo na kulisalia kaburi hilo. *Wa Allahu A'lam*!

Tunaporudi katika kisa chetu basi anasema Imam Ath Thalabi kua**: 'Siku Moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* amjaalie kuonana na Vijana hao. Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Huwezi kuwaona Vijana hao katika hali kua ni wenye kuishi Ulimwenguni lakini unaweza kuwaona kwa njia nyengine, hivyo chagua Mashaba zako wanne kisha uwatume waende kuwaona Watu hao na kisha Wawaite katika Kukuamini wewe na Uislam.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akamuuliza Malaika Jibril: **'Hivi Jee nitawezaje kuwatuma Masahaba zangu kuwaona watu hao.'**

Kwani Malaika Jibril akamwambia: **'Tandika chini Kilemba chako kisha katika Pembe moja Mwambie Abu Bakr Akae, na katika pembe ya pili Umar katika ya tatu Ali na katika ya nne Abu Dhar *(Radhi Allahu Anhum)*'**

Kisha Uamrishe Upepo Mlaini ambao ndio aliokua akiutumia Sulayman Ibn Daud kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameuarishe nawe pia uwe ni wenye kukutii Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akafanya kama alivyoambiwa na kisha akauamrisha Upepo uwabebe Masahaba hao hadi kwenye Pango hilo.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoafanya hivyo basi haikuchukua hata sekunde wakajikuta wamo kwenye Pango hio na hapo Masahaba hao wakatoa Salam.

Na mara *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawarudishia Roho zao nao wakaamka na kuitikia Salam ya Masahaba hao wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Masahaba hao wakasema '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Muhammad Ibn Abdullah anakusalimieni.'**

Ambapo nao wakajibu: **‘Sala na Salam zimfikie *Muhammad Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati Mbingu na Ardhi bado zipo Ulimwenguni kutokana na juu yenu kutokana na Mliyotutaarifu.’**

Na kisha Masahaba zake wakakaa na Kuzungumza nao watu hao nao wakamuamini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha Wakajinyoosha na kurudi katika hali kama waliyokua nayo hapo. Nayo hapo kabla ambayo watabakia nayo hadi katika wakati ambao atakapokuja Mahdi na hapo pia wataamshwa tena na kusalimiana nae na kisha watalala hadi siku ya Kufufliwa.

Baada ya Hapo Masahaba hao wakakaa juu ya Kilemba na Upepo ukawachukua kuwarudisha kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini kabla hawajafika basi Malaika Jibril akashuka na kumuelezea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yaliyotokea. Hivyo Masahaba hao walipofika basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza pia yaliyotokea ambapo nao wakasema:

‘Ya Rasul Allah hakika sisi tumekutana nao na tukasalimiana nao na wakapokea salam zetu na tukawaelezea kuhusiana na Ujumbe wako uliokuja nao na wao wamekubaliana nao na wakashuhudia, kua Hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa Haki isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wewe ni Mtume wake Na kisha wakamtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kuwapandisha Darja ya kupokea Ujumbe wako moja kwa moja a wamekusalia na kukualimia sana.’

Hivyo *Rasul Allah Salallahi Alayhi wa Salam* akasema: **‘Ya Allah nakuomba usinitenganishe mimi na Ndugu zangu, wala na Niwapendao na nakuomba uwasamehe wanipendao, wanaoipenda Familia yangu, Masahaba zangu na Ummah wangu.’**

Na tunaporudi kwenye kisa kama kinavyosimuliwa na *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* basi tunaona kua baada ya *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kumalizia kukielezea kisa hicho cha *As-hab Al Kahf* yaani Kina Tamlikha, Maksalmina, Muhsilmina, Martiliyus, Kashtus na Muhsilmina na mfugaji na mbwa aitwae Qitmir.

Basi Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akamuuliza Yahudi aliekua akimhoji kuhusiana na watu hao kwa kusema: **‘Ewe Yahudi, nakuuliza mimi kwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Watu hawa na nilivyoelezea Jee ni sawasawa kama ilivyoelezewa kwenye *Tawrat* yenu ama la?’**

Ambapo Yahudi huyo akajibu kwa kusema: **‘Ewe Abu Al Hasan nakuomba Usiniite tena Yahudi, kwani na mimi pia nashuhudia kua hakuna Mola anaestahiki Kuabudiwa kwa Haki isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* ni Mtume wake.’**

Kisha Yahudi huyo aliesilimu akamalizia kwa kusema; ‘**Kwani kwa hakika Ewe Abu Al Hasan katika kukielezea kwako kisa hiki basi hukua ni mwenye kuongeza wala kupunguza hata herufi moja ndani yake, na kwa hakika wewe Abu Al Hasan kweli ni Mlango wa Ilm wa Ummah Huu.’**

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kusema katika Katika Qur'an kua:

﴿سَيَقُولُونَ ثَلاثَةٌ رَّابِعُهُمْ كَلْبُهُمْ وَيَقُولُونَ خَمْسَةٌ سَادِسُهُمْ كَلْبُهُمْ رَجْماً بِالْغَيْبِ وَيَقُولُونَ سَبْعَةٌ وَثَامِنُهُمْ كَلْبُهُمْ قُل رَّبِّي أَعْلَمُ بِعِدَّتِهِم مَّا يَعْلَمُهُمْ إِلاَّ قَلِيلٌ فَلاَ تُمَارِ فِيهِمْ إِلاَّ مِرَآءً ظَاهِراً وَلاَ تَسْتَفْتِ فِيهِمْ مِّنْهُمْ أَحَداً﴾

Sayaqooloona thalathatun rabiAAuhum kalbuhum wayaqooloona khamsatun sadisuhum kalbuhum rajman bialghaybi wayaqooloona sabAAatun wathaminuhum kalbuhum qul rabbee aAAlamu biAAiddatihim ma yaAAlamuhum illa qaleelun fala tumari feehim illa miraan *dha*hiran wala tastafti feehim minhum ahadan*(Surat Al Kahf 18:22)*

Tafsir: ***Kuna (Watu) Wasemao kua (As-hab Al Kahf) ni watatu Na Wa Nne ni Mbwa wao Na Kuna Wasemao kua ni Watano Na Wa Sita ni Mbwa wao Wanaagua Juu ya Yasiyoonekana Na Kuna wasemao kua ni Saba Na Wa Nane ni Mbwa wao Sema kua Mola wangu Ndie ajuae Juu ya Idadi yao Na Hakuna anaejua Juu yao Isipokua ni Wachache tu Hivyo Msibishane juu yao Isipokua kwa Vithibitisho Vilivyodhahiri (tulivyokushushieni kuhusiana nao) Na wala Msiwaulize kufutailia (Watu wa Ahl Al Kitab) kuhusiana nao kutoka hata kwa mmoja miongoni mwao.***

Ambap aya imetumia Neno *Rajama* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kupiga Mawe, Kupopoa Mawe, Kurusha Mawe kwa ajili ya Kuagua Kitu au Jambo, Kuagua, Kuhitimisha kitu bila ya kua na Uthibitisho wa kutosha, Kushambulia kwa Mawe Kuchukia, Kufukuza, Kuweka Jiwe juu ya Kaburi,.

Neno *Rajama* ndio lililotoa neno Rajiim ambalo tunalitumia sana tunapotaka Ulinzi wa Allah Subhanah wa Ta'ala kwa kusema *Audhu bi Allahi minna Al Shaytani Al Rajiim.* Na hivyo hapa maneno *Shaytani al Rajiim* hua yaamaanisha Kiumbe Shaytan alielaaniwa na kufukizwa Kwa kutolewa nje ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Hivyo ayah hii ya 22 ya *Surat Al Kahf* ambayo ndio Aya inayotufungia kisa cha *As-hab Al Kahf* au kama alivyowaita mwenyewe *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa jina la Fityatun yaani Vijana Shupafu wasiofika kumi kiidadi wenye msimamo thabiti juu ya Mola wao, na aya hii ya 22 ni Aya ambayo imetumia neno *Rajama* katika hali ya *Rajman* yaani Kuagua bila y akua na vithibitisho. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatubainishia namna walivyokua *Rajman Bi Al Ghaybi* yaani Wakiagua Juu ya Yasionekana wala kujulikana bila ya kua na vithibitisho watu wasiojua kuhusiana na Idadi ya Watu hawa wa *As-hab Al Kahf.*

Na hivyo katika Kuwaelezea kwake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua Watu hao wenye kuagua wameagua kua ni kuanzia Idadi ya Watu watatu hadi saba. Na hivyo hii ni yenye kuthibitisha kuhusiana na Uhalisia wa hali yao ya kua na sifa ya Fityatun yaani Vijana Shupavu wenye Msimamo ambao idadi yao haifiki Kumi. Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kua ni Wachache tu ndio wanaojua kuhusiana na Idadi yao.

Ama kuhusiana na maneno haya basi Anasema *Jarrah Allah Sultan Al Balagha* Imam Abu Qasim Al Zamakshari kua : **'Alisema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Hakika mimi ni miongoni mwa hao wachache wenye Kujua waliotajwa kwenye aya hii, na naweza kusema huku nikiwa na uhakika kua Vijana hao walikua ni watu Saba pamoja na Mbwa wao.'**

Ambapo kauli hii pia ameinukuu na Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Al Qurtubi na pia Imam Muhammad Ibn Jarir At Tabari. Na hivyo *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kamalizia kwa kusema: **'Walikua ni Tamlikha, Maksalmina, Martaliyus, Baynus, Sawamus, Dawanus na Kashtus na Mbwa wao ni Qitmir.'**

Na pia katika ayah hii pia tunoana kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema katika hii pia kua: '***Fala tumari feehim illa miraan*** **yaani Hivyo Msibishane juu yao isipokua kwa Vithibitisho.'**

Ambapo Neno *Miraan* ni lenye kutokana na neno *Marra* ambalo humaanisha, Kupita, Kupitia, Kuendelea na mwendo, hatua au Safari. Neno *Marra* ndio lililotoa neno *Miratun* ambalo hua linamaanisha Uwezo Mkubwa wa Kiakili, Kua na Uwezo wa Kuhukumu kitu kwa kutumia Akili na Ufaham, Kua na Busara.

Na hivyo aya kua ni nyenye kututhibitishia kua mbali ya uajabu wake lakini Hiki ni kisa cha kweli na chenye uhakika na vithibitisho kama alivyovielezea mwenyewe *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambavyo ni visivyopingika kiakili kulingana na Kudhihirishwa kwa vithibitisho vyake na Qur'an hivyo haina haja ya kubishana kuhusiana nao kama walikua wangapi n.k na wala kua na shaka kuhusiana nao.

Na kama tulivyosema tulipoanza nacho kisa hiki katika utangulizi wake kuhusiana na umuhimu wa kusema *In-shaa Allah* pale tunapoahidi kitu baada *ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuahidi bila kusema *In-shaa Allah* na hivyo Malaika Jibril akachelewa kushuka kwa ajili ya kumuwezesha kutekelezea Ahadi yake. Na Alipoulizwa Malaika Jibri kwanini akachelewa basi akasema kua Wao Malaika hua hawashuki isipokua kwa Ruhusa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae hana Sifa ya Kusahau.

Hivyo baada ya aya kukielezea kisa hicho cha *Ashab Al Kahf* ambacho *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliahidi kua atakielezea baada ya kuelezewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatoa Onyo lenye kudhihirisha sababu ya kuchelewa kupatikana kwa ufafanuzi wa hoja ya Makafiri kuhusiana na waliyoyataka kufafanuliwa kwa kusema:

﴿ وَلاَ تَقُولَنَّ لِشَيْءٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذٰلِكَ غَداً ۞ إِلاَّ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ وَٱذْكُر رَّبَّكَ إِذَا نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰ أَن يَهْدِيَنِ رَبِّي لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا رَشَداً ﴾

Wala taqoolanna lishay-in innee faAAilun dhalika ghadan; Illa an yashaa Allahu waodhkur rabbaka idha naseeta waqul AAasa an yahdiyani rabbee li-aqraba min hadha rashadan (*Surat Al Kahf 18:23-24)*

Tafsir: ***Na Wala Usiseme Juu ya Chochote kile Kua Nitafanya hilo Kesho Isipokua kwa kusema In-shaa Allah (Kama Allah Akitaka) Na Mkumbuke Mola wako Na Ukisahau basi Sema Huenda Ataniongoza Mola wangu Ataniongoza zaid Kuukaribia Ukweli zaid kuliko hivi katika Njia hii.***

Naam..anasema *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin* Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: **Ushaulivu hua ni wenye kutokana na Vishawishi vya Shaytan, ambapo ni pale Mtu anapokua anamkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ndio Shaytan huondoka. Na hivyo mtu anapokua anamkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kila Wakati basi hua inakua vigumu kwa mtu husika kusahu sahau. Kwani Aya hii inatilia mkazo Umuhimu wa kusema**

In-shaa Allah* na hivyo basi hata kama mtu umeahidi na kisha ukasahau kusema *In-shaa Allah* lakini baadae ukakumbuka basi unatakiwa useme *In-shaa Allah.'

Ambapo anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: **'Kama Mtu ataahidi kufanya kitu na kisha akakumbuka kua kumbe hakusema *In-shaa Allah,* mtu huyo anaruhusika kusema japo baadae hata kama itakua amekumbuka baada Ya Mwaka.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa basi yeye anasema kua: ***'In-shaa Allah* itakayosemwa baadae hua haihesabiki, kwani *In-shaa Allah* inayotakiwa ni ile ya kutamkwa katika wakati wa makubaliano ya Ahadi husika, hivyo kwa kua kusema *In-shaa Allah* baadae hua hakuhesabiki basi na ahadi husika pia hua haihesabiki au haina uzito pale isipokua na *In-shaa Allah* ndani yake. Na inapotamkwa *In-shaa Allah* katika wakati husika basi huongeza baraka ndani ya jambo husika'**

Hivyo ayah hii pia inatusisitizia umuhimu kwa kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale mtu anapokosea au anaposahau, yaani hii inakua ni sawa na kama vile ilivyotoeka kwenye tukio linaelezewa kwenye Hadith yenye kuelezea namna *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walipolala na kisha kuamka wakati jua lilipochomoza na hivyo kua ni wenye kuukosa wakati wa Sala ya Alfajir kama alivyosema Abd Allah Ibn Qatadah kua:

'Amesema Baba yangu kua siku moja wakati tulipokua safarini Pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na baadi ya watu wengine wakasema: 'Tunatamani kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anagepumzika Pamoja nasi katika wakati wa mwishoni wa Usiku' ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Nna khofu kua mkilala basi tutaikosa Sala ya Al Fajir' hivyo Bilali akasema: 'Mimi nitakuamsheni' hivyo watu wote wakalala, na kisha Bilali akaweka kichwa chake kwenye Shehena yake ya Rahila yake na mara nae usingizi ukamchukua na akalala.'

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamka wakati Jua lishaanza kuchomoza na hivyo akasema: 'Ewe Bilal vipi kuhusiana na Kauli yako?' ambapo nae akajibu: 'Wallahi mimi sijawahi kulala usingizi kama huu wa leo' na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: '*Allah* hua ni mwenye kuzichukua Roho zenu pale atakapo na huziachia pale atakapo, Ewe Bilal Nyanyuka Uadhini' kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatia Udhu na Jua lilipokua limeshachomoza na linang'ara basi akasimama na kusali'*(*Imam Bukhari)*

Ambapo kwa upande wa Imam At Tirmidhii basi yeye ameizungumzia Hadith hii kwa mtizamo wenye maneno tofauti kidogo kwani ndani yake Imam At Tirmidhii amesema kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Amesema Abu Qatadah kua: 'Imesemwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Pamoja na baadhi ya Masahaba waliikosa Sala wakati wakiwa wamelala. Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hua si kudharau pale inapokosekana Sala bila ya kukusudia kutokana na kulala usingizi, bali dharau hua ni pale inaposeakana wakati mtu akiwa macho. Hivyo Mtu akaisahau au akiikosa Sala kutokana na Kulala basi mwache na aisali haraka sana pale atakapokumbuka''''***(*Sunan At Tirmdhii)*

Na amesema Imam Abu Zakariyah Sharaf An Nawawi kua: **'Kuna makubaliano ya Wanazuoni wale ambao niwenye kuaminika katika mitizamo yao kua ni wajibu wa kila anaesahau kusali kulipa sala hio kwa kusali Sala ya Qadha'** kwa amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Yeyote yule anaesahau Kusali basi ni lazima kwake kuisali pale anapokumbuka'(***Sahih Muslim)*

Hivyo kutokana na maneno ya Aya hizi basi tunaona kua: **Unapotaka kufanya Jambo la baadae na hivyo ukawa ni mwenye Kusema In-Shaa Allah, basi unakua ni mwenye kumuachia *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya Maamuzi ya Ufanywaji wa Jambo hilo na hivyo hua ni mwenye Kuliombea Baraka za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake**

Hivyo Tusisahau kusema Inshaa Allah kwani hua kunaongeza Baraka juu ya Jambo husika.

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua**: Sulayman Ibn Daud alisema kua: Hakika ya leo usiku mimi nitalala na wake zangu wote mmoja baada ya mwengine na hivyo kila mmoja atapata Mtoto ambae atakua ni mwenye kupigana Jihadi kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.***

Ambapo akaambiwa: Sema *In-Shaa Allah* lakini hakusema. Na hivyo ingawa alilala na wake zake wote lakini hakuna hata mke wake hata mmoja aliepata Mtoto isipokua mmoja tu, ambapo hata hivyo mtoto huyo alikua na matatizo.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hivyo kama angesema *In-Shaa Allah* basi asingekua ni mwenye kuvunja nadhiri yake lakini angekua ni mwenye kutimiza malengo yake.**

Naam baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kusisitizia Umuhimu wa kusema *In-shaa Allah* pale tunapopanga kuhusiana na yajayo tusiyoyayajua uhalisia wake na hivyo kua ni wenye kukumbushwa kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kikamilifu katika kufanikisha mipago hio huku tukitakiwa kua ni wenye kuonesha jitihada katika kujaribu kufikia malengo hayo kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie pekee mwenye kuona na kujua juu ya kila kitu, basi aya zinaendelea kusema kua:

﴿ وَلَبِثُواْ فِي كَهْفِهِمْ ثَلاثَ مِئَةٍ سِنِينَ وَٱزْدَادُواْ تِسْعاً ۞ قُلِ ٱللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُواْ لَهُ غَيْبُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ أَبْصِرْ بِهِ وَأَسْمِعْ مَا لَهُم مِّن دُونِهِ مِن وَلِيٍّ وَلاَ يُشْرِكُ فِي حُكْمِهِ أَحَداً ﴾

Walabithuu fii Kahfihim, Thalatha Mia-tin Siniina wazdaduu Tis-aAn *(Surat Al Kahf 18:25)*

Tafsir: **Na Wakabakia Ndani ya Pango lao hilo Miaka Mia tatu Na Kuongeza Miaka tisa.**

Na kama tunakumbuka basi aya ya Awali iliyozungumzia kuhusiana na Miaka waliyolala watu hao ndani ya Pango haikua ni yenye kusema kua walilala miaka mingapi, bali ilisema kua ni kwa miaka kadhaa pale iliposema:

﴿ فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي ٱلْكَهْفِ سِنِينَ عَدَداً﴾

Fadharabna aAala Adhanihim fii Al Kahfi Siniina aAdadan *(Surat Al Kahf 18:11)*

*Tafsir: **Hivyo Tukayafunika n Kuyaziba Masiko yao kihisia Wakiwa Ndani ya Pango Kwa Idadi ya Miaka mingi.***

Hivyo tunapoangalia Aya hizi basi tunaona kua si aya zenye kujirudia, ila maneno haya ni yenye kujirudia kutokana na kua kwanza tuliangalia mtizamo wa Masahaba juu ya kisa hiki ambapo ndani

yake ndio walisema kua ni miaka 309, na wao walisema hivyo kutokana na Ainisho la aya hii ya 18:25 kua ni miaka 309.

Ambapo hata hivyo basi tunapoangalia zaidi basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Taala* anafafanua zaid kwa kusema kua:

﴿قُلِ ٱللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُواْ لَهُ غَيْبُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ أَبْصِرْ بِهِ وَأَسْمِعْ مَا لَهُم مِّن دُونِهِ مِن وَلِيٍّ وَلاَ يُشْرِكُ فِي حُكْمِهِ أَحَداً ﴾

Quli Allahu aAAlamu bima labithoo lahu ghaybu alssamawati waal-ardhi absir bihi waasmiAA ma lahum min doonihi min waliyyin wala yushriku fee hukmihi ahadan*(Surat Al Kahf 18:26)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad) Allah ni Mwenye kujua Kua Walilala mda gani Kwani ni kwake yeye ndio kwenye kujulikana kuhusiana na yasiyojulikana Ya Mbinguni na Ardhini anaona Wazi Ndani yake kila kitu Na ni Mwenye Kusikia Juu ya kila kilichomo ndani yake Na Wala Havina zaidi yake Msimamizi Na Hakumfanya kua Mshirika Katika Maamuzi na Hukmu zake yeyote yule.***

Kwani anasema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua: **'Aya hizi zinamaanisha kutuambia kua: Watu ni wenye kusema kua Watu wa As-hab Al Kahf walikaa Pangoni kwa mda wa miaka 309, lakini hata hivyo ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie mwenyewe kujua zaid juu yao na ni mda gani walibakia ndani ya Pango hilo.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Ad Dahhaq Ibn Muzahim, Imam Mujahid Ibn Sulayman na wengineo basi ni wenye kusema kua: **'Aya hizi zinamaanisha kutuambia kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatufahamisha kua Watu hao walilala ndani ya Pango kwa mda huo yaani wa miaka 309, na hivyo kua ni aya zenye kufunga milango ya Masuali kuhusiana na mda waliolala watu hao.'**

Ambapo tunaporudi kwa Imam Is-haq Ibn Marduwayh basi yeye anasema kua: **'Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: Kwanza yalishuka maneno ya Aya yasemayo:**

﴿ وَلَبِثُواْ فِي كَهْفِهِمْ ثَلاثَ مِئَةٍ﴾

Walabithuu fii Kahfihim, Thalatha Mia-tin. *(Surat Al Kahf 18:25)*

Tafsir: ***Na Wakabakia Ndani ya Pango lao hilo kwa mda wa Mia tatu.***

Hivyo Masahaba wakauliza: '300 Siku, miezi au Miaka?' Hivyo aya ikamalizia:

﴿ وَٱزْدَادُواْ تِسْعاً ﴾

Wazdaduu Tisa-an *(Surat Al Kahf 18:25)*

Tafsir: ***Na Kuongeza Miaka tisa***

Naam..hivyo baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kumuelezea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Kisa cha watu wa As-hab Al Kahf basi anaendelea kumwambia Mtume wake huyo Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

﴿وَٱتْلُ مَآ أُوْحِيَ إِلَيْكَ مِن كِتَابِ رَبِّكَ لاَ مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ وَلَن تَجِدَ مِن دُونِهِ مُلْتَحَداً ﴾

Waotlu ma oohiya ilayka min kitabi rabbika la mubaddila likalimatihi walan tajida min doonihi multahadan*(Surat Al Kahf 18:27)*

Tafsir: ***Na Wasomee Kile Ulichoshushiwa (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Kutoka Katika Kitabu cha Mola wako Kwani hakuna atakaeweza Kubadilisha Maneno yake Na haitowezekana Kupata Zaidi Yake (Allah Subhanah wa Ta'ala) wa Kukupokea na kukuhifadhi***

Na tunapoziangalia aya hizi basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Taala* anamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Isome Qur'an Ewe Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* ili watu waisikie wapate kuijua na kisha Tekeleza maamrisho yake kwani hakuna kitakachobadilika kutoka katika maamrisho yake na makatazo yake na kwako wewe hakuna kwa kukimbilia wala kwa kuegemea isipokua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

Ambapo kama ilivyokua kwa wengi Miongoni mwa Mitume ni kua wenye kukubalika kirahisi zaid na wale wasiokua na kitu katika Jamii kuliko wale wenye Mali na Mamlaka kwa sababu wengi miongoni mwa wenye Mali na Mamlaka hua wanakhofu ya kupoteza Vyeo vyao katika Jamii na Mali zao, kutokana na kuwepo kwa Utume wa Mtume Husika katika Jamii husika Na hivyo watu hao hua ni wenye kumpiga vita Mtume husika ambapo hali hii pia ndivyo ilivyokua kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani alipigwa Vita na Viongozi wa Mji wa Makkah na akawa ni mwenye kukubalika zaid na wale wasiokua na kitu, Masikini na Watumwa.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa na Ukaribu sana na Masahaba zake hao ambao ni watu wa chini kwani hayo ndio pia Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutowabagua wasiokua na kitu Na kutojipandisha Darja kwa wenye kua na Mamlaka na Mali, kutodhulumiana, Kutodharauliana, n.k

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema: **'Sifa zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae amejaalia kua katika Ummah wangu kuna watu kama hawa ambao nimeamrishwa kua nao karibu.'**

Tatizo ni kua kwa upande wa Watu wa Kabila la Quraysh waliokua na Mamlaka na Mali walikua wakiwachukia Masikini na kutokana na kuwadharau kwao basi walikua hawakai nao katika sehemu moja kama Barazani, kwenye vikao vyao n.k kwani Waliokua juu ndio wenye sauti na maamuzi hivyo waliochini hawana chao isipokua kutekeleza.

Na ingawa baadhi ya miongoni mwa waliokua na Mali na Mamlaka walikua wanataka kua Waislam kutokana na kuona Nguvu ya Uislam lakini sasa tatizo ni kua Wao hawawezi kukaa pamoja na kua sawa na Masikini na waliokua Watumwa. Hivyo wakataka baadhi ya Misimamo yenye maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ibadilishwe ili iwe ni yenye kuendana na Darja na hali zao na kisha ndio wanaweza kuingia katika Uislam..yaani kama inavyobadilishwa Katiba.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Wasomee Ujumbe ambao Hukmu na maamrisho yake kamwe haiwezekani kubadilika na kua kama watakavyo wao.

﴿وَٱصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ ٱلَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِٱلْغَدَوٰةِ وَٱلْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ وَلاَ تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ ٱلْحَيَاةِ ٱلدُّنْيَا وَلاَ تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَن ذِكْرِنَا وَٱتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطاً﴾

Waisbir nafsaka maAAa alladheena yadAAoona rabbahum bialghadati waalAAashiyyi yureedoona wajhahu wala taAAdu AAaynaka AAanhum tureedu zeenata alhayati alddunya wala tutiAA man aghfalna qalbahu AAan dhikrina waittabaAAa hawahu wakana amruhu furutan *(Surat Al Kahf 18:28)*

Tafsir: ***Na Isubirishe Nafsi yako Pamoja na wale Wanaomuita, Na Kumuomba na Kumtukuza Mola wao Asubuhi Na Jioni Wakiwa ni wenye kuutaka Muonekano wake Na wala Usiyaruhusu Macho yako kutokua nao Kutokana na Kutaka Mapambo Ya Maisha ya Kidunia Wala Usimtii Yule ambae tumeughafilisha Moyo wake. Kutokana na Kutukumbuka sisi Na Akawa ni Mwenye kufuata Matamanio yake na yakawa mambo yake yameharibika.***

Hivyo baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutakiwa na baadhi ya watu kua ili wamfuate basi na abadilishe baadhi ya Mitizamo ya Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamtilia Mkazo kua Afikishe Ujumbe aliopewa kwenye Qur'an kama alivyoshuhiwa asibadilishe kitu kwani hakuna atakaeweza kubadilisha maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hakuna wa kumkimbilia zaid yake.

Ambapo tunapoiangalia aya hii basi ndio tunafaham kwanini Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii alikua mbali ya kujua kwake kote kutoka na Ilm aliyokua nayo basi Alikua kila akiulizwa suali alikua hajibu mpaka afikirie kwanza na hivyo akaulizwa: **'Hivi kwanini ewe Al Shafii Lazima Ufikirie sana kabla ya kujibu unayouliuzwa?'**

Ambapo nae akajibu kwa kusema: **Kwa Sababu naangalia Suali lilivyo na namna ya kulijibu ili lisije jibu lake likawa ni Mtihani kwangu katika siku ya Malipo. Kwani Najiuliza Ni Sehemu gani ya Mbingu na Ardhi itakayokubalki kunifadhi mimi kutokana na Adhabu za Allah kama nikijibu kinyume na maamrisho yake *Allah Subhanah wa Ta'ala* na pia kama ikiwa ni kinyume na alivyoamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Naam..hivyo walivyokua Wenye kujua kina Al Imam Al Shafii Tofauti na wengi wetu sisi leo hii kwani hatujui halafu hapo hapo tunakimbilia haraka zaid kujibu tunayoulizwa na hivyo kua ni wenye kujiangamiza wenyewe kwa kutoa Fatwa zisizokua na mbele wala nyuma na hivyo kua ni wenye kubadilisha maamrisho na kupotosha zaidi wasiojua

Kwani baada ya hapo basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawasifu Masahaba hao wasiokua na uwezo na wanaodharaulika wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini ni wenye Imani kubwa sana kutokana na kua ni wenye kujisalimisha kikamilifu kwa *Allah Subhanah wa Taala* na Mtume wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Kwani Mapambo ya Dini ya Kiislam hua hayahesabiwi kutokana na wingi wa Mapambo ya Kidunia bali ni Kutokana na Wingi wa Imani na Utiifu wa Mamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuachana na Makatazo yake.

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Shikamana nao na kua na subira nao hao Wanaodharaulika, wenye kutafuta Ridhaa yangu kwa kunikumbuka na kuniomba kila wakati asubuhi na Mchana na wala Usiwatii hao Wakuu wa Quraysh walioghafilika nami kutokana na mapambo ya Dunia.

Ambapo anasema Sahl Ibn Hunayf *Radhi Allahu Anhu* kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ndani ya moja kati ya Nyumba zake pale wakati aya hii iliposhushwa. Na hivyo baada ya kushushwa aya hii basi akayoka nje kwa ajili ya kuwatafuta wale ambao ameaambiwa ashikamane nao, na akawakuta baadhi ya Masahaba zake wakiwa wamejikusana pamoja huku wakiwa ni wenye kufanya *Dhikr Allah.* Ambapo baadhi miongoni mwao walikua na Nywele Timtim, wengine wakiwa Ngozi zilizokauka na kukakamaa na wengine wakiwa na Kipande kimoja tu cha nguo cha kujihifadhia.'**

'Hivyo alipowaona basi akakaa kitako pamoja nao na kisha akasema 'Ametukuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae amejaalia miongoni mwa Wafuasi wangu kua ni wale ambao ameniamrisha kua ni mwnye kushikamana nao.''

Kwani Miongoni mwa Makafiri wa Makkah waliokua wakitaka baadhi ya Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala yabadilishwe* kuhusiana na Matajiri kuchanganyika na masikini na wasiokua na kitu basi yumo pia yule aliekua akiitwa Uyaynah Ibn Hisn ambae alimwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Sahaba Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Ya *Rasul Allah* Hakika Harufu ya Mwili wa Salman Al Farsi inakirihisha sana kwetu sisi, na hivyo tunakuomba kua bora utuchagulie sisi siku ambayo itakua ni kwa ajili yetu tu kukaa na kuzungumza na wewe bila ya hao wengine kuwepo, na wao wachagulie siku yao bila ya kuwepo sisi.'**

Naam..hivyo ndivyo walivyokua baadhi ya Watu Wenye Darja katika Jamii za Watu wa Quraysh katika wakati huo, ambapo watu hawa walikua wakijulikana pia kama *Mualiffatul Al Qulub.* Yaani watu wenye Nyoyo ambazo ni zenye kutaka kuliwazwa, kwani wanataka kua Waislam lakini kwa masharti wanayoyataka wao kutokana na matamamio ya Nyoyo zao. Kwani Nyoyo zao bado hazijaikubali ipasavyo Imani ya Dini ya Kiislam.

Na *Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi basi yeye anasema kua: **'Watu hawa walikua na hali ya Mghafiliko wa Nyoyo zao na ndio maana *Subhanah wa Ta'ala* akasema kuhusiana na mwenye sifa hizo kua ni *Aghfalna Qalbahu* yaani ni Watu waliopigwa na Mghafiliko wa Moyo na kupotea'**

Kisha baada ya kuamrisha maamrisho hayo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatoa onyo tena lenye khiyari ndani yake katika aya inayofuatia ambayo ni aya ya 29 ambayo ndani yake imetumia neno *Sardaqah* lenye kuamanisha Kufunika kitu kwa kutumia Mfuniko kama Kawa, Kufunika kitu au sehemu kwa kutumia Kipenu au Paa, Kujenga au kuweka Tabaka la Kitu juu ya Kitu, Kuziba kitu kw akutumia Vumbi au Moshi, na pia humaanisha Sehemu yenye Ukuta wenye Ulinzi mkubwa sana uliozunguka na kutofautisha vilivyomo ndani yake kutokana na vilivyo nje yake kiasi ya kua haiwezekani hata kusikia sauti ya kinachotokea nje ukiwa ndani na wala sauti ya kinachoendelea ndani yake ukiwa nje.

Imam Al Tustari anasema kua: '**Al Ghafla yaani mghafiliko hua ni kupoteza wakati kwa kufanya mambo yasiyokua na maana kwani Moyo hua una vifo 1000, ambapo kifo cha mwisho hua ni kukatwa kutokana na kutomkubali *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Moyo pia una Maisha 1000 ambapo wa mwisho wake hua ni katika kukutana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na uwezo wake. Hivyo kutokana na Dhambi basi Moyo hua ni wenye kufa kidogo kidogo, na kutokana na kila jambo jema basi Moyo hua ni wenye kupata uhai kidogo kidogo.'**

Hivyo katika kuonya kwake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaelezea kuhusiana na kile kitakachowafika watakaopingana na maamrisho yake kua amewataarishia adhabu ya Moto uliokua katika hali ya *Suradiq* kwa kusema:

﴿وَقُلِ ٱلۡحَقُّ مِن رَّبِّكُمۡ فَمَن شَآءَ فَلۡيُؤۡمِن وَمَن شَآءَ فَلۡيَكۡفُرۡ إِنَّآ أَعۡتَدۡنَا لِلظَّٰلِمِينَ نَارًا أَحَاطَ بِهِمۡ سُرَادِقُهَا وَإِن يَسۡتَغِيثُواْ يُغَاثُواْ بِمَآءٖ كَٱلۡمُهۡلِ يَشۡوِي ٱلۡوُجُوهَ بِئۡسَ ٱلشَّرَابُ وَسَآءَتۡ مُرۡتَفَقًا﴾

Waquli alhaqqu min rabbikum faman shaa falyu/min waman shaa falyakfur inna aAAtadna lil*dhdha*limeena naran ahata bihim suradiquha wa-in yastagheedhoo yughathoo bima-in kaalmuhli yashwee alwujooha bi/sa alshsharabu wasaat murtafaqan*(*Surat Al Kahf 18:29)*

Tafsir: ***Na Sema (ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam kua): Ukweli ni kutoka Kwa Mola wenu Kwa anaetaka Basi Ataamini Na Kwa Anaetaka Basi Ataukufuru (Atapingana nao) Na kwa hakika sisi tumewatayarishia Wenye Kufanya Maovu, Moto Ambao Utawazunguka Kwa Ukuta wake Paa lake Madhubuti sana Na Kama Wakiomba msaada Basi Watapewa Msaada wa Maji ambayo ni Mafuta Mazito Yanayochemka ambayo mvuke wake Utavua Ngozi za Nyuso zao (Hicho) Ni kinywaji Kibaya Sana Na Ni makazi mabaya sana ya sehemu hio (ya Moto uliiozungukwa kwa kuta na kipaa cha Moto)***

Subhana Allah! Kabla ya kuendelea basi kwanza Tumuombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* atuepushe na Moto huo..Aamiin

Naam, hivyo aya inatuonesha namna *Allah Subhanah wa Ta'ala* anavyotoa Onyo kali sana kwa Viumbe wake ambao ni Ibn Adam na Majini, lakini hapo hapo katika kutuonya kwake basi anatudhihirishia kua sisi wenyewe mimi na wewe tuna uhuru wa khiari ya kuchagua kuukubali Ukweli wake ama kuukataa na kupingana nao Ambapo kwa kila atakaeukataa na kupingana na Ukweli huo aliokuja nao *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi atakua ni miongoni mwa *Al Dhalimiina* yaani waliofanya Dhulma na hivyo kua ni wenye kujidhulumu na hivyo Malipo yao yatakua ni Moto wenye mazingira ya Suradiq.

Ambapo Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'*Suradiq* Ya Moto wa Jahannam Hua ni sehemu yenye Kuzungukwa na Kuta 4, ambapo kila Ukuta basi Upana wake ni sawa na safari ya masafa ya miaka 40.'** *(Imam At Tirmidhii)*

Na anasema *Al Muhaqqik Shayh Ul Islami,* Imam Al Fatawi Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: **'Amesema Al Ya'ala Ibn Ummayh *Radhi Allahu Anhu* kua*: 'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua Jahannam ni Bahari'**

Na hivyo akaulizwa*: Ya Rasul Allah* ni Bahari Kivipi?' *Ambapo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasoma maneno ya aya hii yasemayo: '*Inna aAAtadna lildhdhalimeena naran ahata bihim suradiquha* (*Na kwa hakika sisi tumewatayarishia Wenye Kufanya Maovu, Moto Ambao Utawazunguka Kwa Ukuta wake na Paa lake Madhubuti sana*).'

Tumuombe *Allah Subhabah wa Ta'ala* atujaalie kua ni wenye kushikamana na Haki na kuachana na *Batil...Amiin*

Kwani katika kuielezea Adhabu itakayowakuta waliojidhulumu kwa kupingana na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua Baada ya Watu hao kuingizwa kwenye Suradiq yaani Chumba kilichozibwa kwa kuta Madhubuti za moto na kufunikwa Paa la Moto Juu yake.

Basi Watu wataomba Msaada wa Kinywaji na hivyo Aya zinasema kua watapewa Kinywaji *Ka al Muhli*. Ambapo Neno *Muhli* ni lenye Kutokana na neno *Mahala* ambalo hua linaamanisha Kufanya Kitu kwa Taratibu na Polepole sana, Kua na Subra Katika Kufanya Kitendo Fulani, Kutokua na Haraka wala Papara katika Ufanyaji wa Kitu Husika.

Ambapo neno *Mahala* ndio lililotoa neno *Mahhil* ambalo ni lenye kumaanisha Kuruhusu Kuchelewa au kukawia kwa kitu, Kucheleweshe au Kakawiza, Kuakhirisha, Kuachana na Kitu Taratibu.

Kwani neno *Mahala* ndio lililotoa neno *Muhl* ambalo ndilo lililotumika katika aya yetu hii na ijapokua kuna baadhi wametafsiri neno hili kua ni Shaba ya Moto, na bila ya shaka hawajakosea lakini ukweli ni kua neno hili hua linaashiria Hali ya Kinywaji Chochote kile ambacho Ni Kimoto Sana chenye hali ya kama Ujiuji unaotokota kwa kuchemka kwa umoto na uzito wake kutoka chini ya Sufuria la Moto na kuja juu taratibu kwa wingi wa moto wake.

Hivyo ndani yake neno hili basi hua mnaingia kila kitu kimoto kinachochemka na kutokota taratibu kama Uji iwe Uji, iwe Shaba, iwe Dhahabu, iwe Fedha, iwe Chuma, iwe Volkano n.k

Ambapo Aya hii pia imetumia neno *Murtafaqa* ambalo tumeshalitafsiri hapo kabla na kusema kua limetokana na neno *Rafaqa* ambalo humaanisha Kua na Manufaa, Kusaidia, Kuhudumia, Kua Mkarimu na Mwenye Huruma, na pia humaanisha Kua na Urafiki wa Karibu na hii ni kwa sababu neno Rafaqa ndio lililotoa neno *Rafiqi* yaani Rafiki.

Na neno *Rafaqa* ndio lililotoa neno *Mirfaqa* ambalo humaanisha Sehemu ya Kuegemea, Sehemu ya Kukupa Nguvu na Kukusaidia kwa Ukarimu na Mapenzi na pia hua linamaanisha Mipango inayopangwa au inayofanyika kwa ajili ya kumsaidia au kumrahisishia Mtu jambo gumu.

Neno *Mirfaq* humaanisha Mto wa Kitandani au Kwenye Kiti au *Majlis* ambao Mtu hua unaweka Kichwa chako, ubavu wako, au unaegemea kwa ajili ya Kujipumzisha. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua sehemu hio ya *Suradiq* ni *Wasaat Murtafaqa*, yaani ni sehemu ya Makazi Mabaya sana ya kufikia kutokana na ukubwa na ukali wa Moto wake.

Baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuwazungumzia wale ambao ni wenye kujidhulumu nafsi zao kutokana na Kutoamini Ujumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Watapewa adhabu kali sana ya Moto uliokua Ndani ya Kuta nne na Paa lake na Kunyweshwa Uji Wa Moto basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawabashiria na kuwaahidi wale ambao watakaouamini Ujumbe huo na hivyo kua ni wenye kufuzu kua *La NudhiaAu* ,ambapo neno *Nudhiau* linalotokana na Neno *Dha'aa* kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye kumaanisha Kuangamia, Kupotea,

Kudharaulika, Kukosekana, Kutokumbukwa au Kutokumbukika au Kutojali. Na hivyo *neno La NudhiAu* hua linamanisha Hatutodharau wala Kusahau wala kuwakosesha Malipo yao kwa kusema kua:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّالِحَاتِ إِنَّا لاَ نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلاً ۞ أُوْلَئِكَ لَهُمْ جَنَّاتُ عَدْنٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهِمُ ٱلأَنْهَارُ يُحَلَّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِن ذَهَبٍ وَيَلْبَسُونَ ثِيَاباً خُضْراً مِّن سُنْدُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ مُّتَّكِئِينَ فِيهَا عَلَى ٱلأَرَآئِكِ نِعْمَ ٱلثَّوَابُ وَحَسُنَتْ مُرْتَفَقاً﴾

Inna alladheena amanoo waAAamiloo alssalihati inna la nudeeAAu ajra man ahsana AAamalan; Ola-ika lahum jannatu AAadnin tajree min tahtihimu al-anharu yuhallawna feeha min asawira min dhahabin wayalbasoona thiyaban khudran min sundusin wa-istabraqin muttaki-eena feeha AAala al-ara-iki niAAma alththawabu wahasunat murtafaqan. *(Surat Al Kahf 18:30-31)*

Tafsir: ***Kwa Hakika wale ambao wataoakua ni wenye Kuamini Wakafanya mambo Mema Kwa Hakika sisi Hatutoyapoteza, Hatutoyasahau, hatutoyadharau Malipo Ya Wale Waliofanya Mema Kwani Wao hao ni Juu yao Bustani za Peponi zenye Kutiririka kutoka Chini yake Mito Na Watapambwa Ndani yake Kwa Mapambo ya Mikononi Yanayotokana na Dhahabu Na Watavaa Mavazi ya Rangi ya Kijani Yenye Unyororo wa Hariri yenye Maua ya Dhahabu na Fedha Wataegemea Ndani yake Kwenye Viti Vya Kifalme vilivyosimama Sawia Kwa Mapambo ya Mikononi Yanayotokana na Dhahabu Na Watavaa Mavazi ya Rangi ya Kijani yenye Unyororo wa Hariri yenye Maua ya Dhahabu na Fedha Wataegemea Ndani yake Kwenye Viti Vya Kifalme vilivyosimama Sawia Ni ya aina ya Neema Nzuri Sana ya Malipo Na Ni aina Nzuri Sana ya Makazi.***

Naam..Allah Subhanah wa Ta'ala Atujaalie kua ni wenye Kunufaika na Ujumbe wake, tuwe ni wenye kufanya Mema atakayoridhika nayo ili tupate kua ni miongoni mwa Watakaonufaika na Neema ya Malipo yaliyotajwa kwenye Aya hii na Nyenginezo…Amiin.

Na Watu wanaozungumziwa na aya hizi ni wale watu ambao ni wenye Kufanya yale waliyoamrishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Ikhlasi yaani kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala tu* peke yake na kwa kupitia katika Njia za Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Imam Al Tustari anasema kua: '**Tabia njema hua ni kua na msimamo katika kushikamana na Sunnah, hivyo mithali ya Sunnah katika Dunia hii hua ni sawa na Pepo kwa upande wa Akhera, kwani yeyote yule atakaeingia ndani ya Pepo basi hua ni mwenye kua na Usalama, hivyo yeyote yule atakaeshikamana na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hapa Duniani hua ni mwenye kua Salama kutokana na Maovu'**

Imam Al Tustari akasema tena kua: **'Hatopata ufunuo yule mtu ambae si mwenye kuyafukia matamanio ya Nafsi yake ndani ya Ardhi.'** Ambapo akaulizwa : '**Hivi jee Mtu atayafukiaje matamanio ya nafsi yake ndani ya udongo?'** ambapo anae akajibu: **'Huiua Nafsi yake kwa kushikamana na Sunna na kisha huizika kwa kushikamana na Sunnah *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hii ni kwa sababu kila kituo cha Mja, kama vile Khofu. Matumanini,**

Mahabba, Kujidhibiti, Kutamani, Kuridhika, Kuamini hua kina mipaka yake isipokua katika Sunna kwani hua hakuna mipaka wala mwisho'

Ambapo Imam Matta Ibn Ahamd aliulizwa: **'Nini maana ya manenno yasemayo kua Sunna haina mwisho?' ambapo nae akajibu: 'Hakuna aliekua na Khofu kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama vile alivyokua na Khofu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, ambapo hali hii pia ipo katika Mahabba, Hamu, Kujidhibiti, Kudhika kwake, utukufu wake, tabia zake na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kuhusiana nae kua '**

﴿ وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴾

Wa-innaka laAAala khuluqin AAa*dh*eemin*(Surat Al Qalam 68:4)*

Tafsir: **Na kwa hakika kwako wewe (Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam) kuna Sifa bora zaidi kitabia.**

Hivyo aya hizi za 30-31 za *Surat Al Kahf* zinatuonesha namna watakavyokua watu wa Peponi katika muonekano wa Mavazi yao.

Ambapo tunaona kua ingawa Hapa Duniani Mapambo ya Dhahabu yamekatazwa na kuharamishwa kwa Wanaume wa Kiislam kuvaliwa lakini yatakua ni yenye kuruhusiwa katika Maisha ya Peponi na hivyo Wanaume hao kuonekana Kama Wafalme na kuvutia zaidi.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Mapambo ya Peponi ya Muumini yatakua ni yenye kumfikia katika sehemu ambazo maji ya Udhu hua yanafikia'** *(Imam Muslim)*

Na hivyo hii ni yenye kutuonesha Umuhimu wa Kutia Udhu wa Sala na Faida zake. Ambapo amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kwa Hakika Ni Muumini wa kweli tu ndie anaesimamia Udhu wake Kikamilifu'**

Kwani kuna baadhi wanaweza wakajiuliza: Hivi Jee Kama Mapambo hayo ya Dhahabu yatakua yanawafikia watu na kuwafunika hadi katika Sehemu za Viungo vyao wanazotilia Udhu, basi jee Hawatokua ni wenye kuhisi Uzito na hivyo Dhahabu hio kua ni Kero kwa uzito badalanya Pambo?

Naam..Jibu la Suali hili tunalipata kwa Imam Iqrimah Mawla Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae yeye anatuambia kua: **'Watu wa Peponi watakua ni wenye kupambwa na mapambo ya kuvaa ya Dhahabu na Fedha na Lulu. Ambayo hata hivyo hayatokua na uzito kwao wao kwani yatakua ni yenye kuumbwa kutokana na Maumbile ya Nuru.'**

Hivyo basi Dhahabu hizo na Lulu na Fedha hizo hazitokua za Mawe bali zitakua za Nuru, sasa Tujiulize hivi kama Ikiwa Dhahabu ya Dunia inatokana na Jiwe na Inang'ara kwa uzuri wake Wenye kutoa Nuru ya Kuvutia hivyo Jee hali itakuaje kwa Dhahabu ambayo imeumbwa kwa Maumbile ya Nuru tena ya Peponi?

Aya zinaendelea kusema kua Watu hao watakua ni wenye kuvaa Nguo za Rangi ya Kijani na hii ni kwa sababu rangi ya Kijani ni rangi yenye kuvutia na kuyapa utulivu Macho ya mwenye kutizama Rangi hio na pia ni rangi yenye kuonesha Unawiri wa Maumbile ya Peponi na kuhusiana na Sundus

wa Istabraq basi Wanazuoni wanasema pia kua hizi ni aina mbili tofaufi za Kitambaa cha aina ya Hariri laini na yenye kung'ara ya Peponi.

Ambapo aina ya Istabraq hua ni Maalum kwa ajili ya Kuvaliwa ndani ya Nguo yaani hua ndio nguo ya juu baada ya Ngozi na Sundus hua ni Nguo ya Juu yake.

Kisha baada ya kueleza hali hiyo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatutolea Mfano wa Vijana Wawili na Mashamba mawili katika Sura yetu hii ambayo nddani yake inatusisitizia umuhimu wa kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Ikhlas katika kila kitu ndani ya Maisha yetu.

VIJANA WAWILI NA MASHAMBA MAWILI.

Neno *Dharaba* kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye maana nyingi sana miongoni mwa maneno ya Kiarabu.

Kwani hua linamaanisja Kupiga Dharuba, Kupiga, Kuponesha, Kutoa Mfano, Kutoa Mithali, Kutoa Kigezo, Kutoa Kitendawili au Chemsha Bongo,Kulinganisha, Kuchanga Vitu kwa Kuvipiga Pamoja kwa mfano kama Karata, Kufunga Safari. Kufunika, Kuachana na Kitu, Kuzuia, Kupigana, Kutafuta Njia, Kuachia Kitu, Kutafuta Maisha.

Neno *Dharaba* pia humaanisha sehemu Ngumu Sana na kavu sana ya Ardhi ambayo hua inaitwa *Dharib* ambayo pia humaanisha Bonde lililojaa Mchanga.

Ambapo Mara nyingi sana *Allah Subhanah wa Ta'alaa* amekua akitumia neno *Dharaba* ndani ya Qur'an kwa ajili ya Kututaka tuhamishe akili yetu kutoka kila kitu na kuiweka katika Jambo husika ambalo hua analizungumzia ndani ya aya husika baada ya neno ***Dharaba.***

Yaani inatakiwa Mtu uwe kama Ulipigwa Dharuba ya Kibao cha Uso kwa ajili kuirudisha Akili yako katika Jambo husika.

Naam..hivyo nasi tuko katika *Surat Al Kahf* ambapo leo tunaingia katika aya ya 32 ambayo imeanza na neno lenye asili ya Dharaba ambalo ni neno *Waidhrib* liliopo katika hali ya amrisho ambalo amepewa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kutubainishia Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:

﴿وَٱضۡرِبۡ لَهُم مَّثَلٗا رَّجُلَيۡنِ جَعَلۡنَا لِأَحَدِهِمَا جَنَّتَيۡنِ مِنۡ أَعۡنَابٖ وَحَفَفۡنَاهُمَا بِنَخۡلٖ وَجَعَلۡنَا بَيۡنَهُمَا
زَرۡعٗا ۞ كِلۡتَا ٱلۡجَنَّتَيۡنِ ءَاتَتۡ أُكُلَهَا وَلَمۡ تَظۡلِم مِّنۡهُ شَيۡـٔٗاۚ وَفَجَّرۡنَا خِلَٰلَهُمَا نَهَرٗا ۞ وَكَانَ لَهُۥ ثَمَرٞ فَقَالَ
لِصَٰحِبِهِۦ وَهُوَ يُحَاوِرُهُۥٓ أَنَا۠ أَكۡثَرُ مِنكَ مَالٗا وَأَعَزُّ نَفَرٗا ۞ وَدَخَلَ جَنَّتَهُۥ وَهُوَ ظَالِمٞ لِّنَفۡسِهِۦ قَالَ مَآ أَظُنُّ
أَن تَبِيدَ هَٰذِهِۦٓ أَبَدٗا ۞ وَمَآ أَظُنُّ ٱلسَّاعَةَ قَآئِمَةٗ وَلَئِن رُّدِدتُّ إِلَىٰ رَبِّي لَأَجِدَنَّ خَيۡرٗا مِّنۡهَا مُنقَلَبٗا﴾

Waidhrib lahum mathalan rajulayni jaAAalna li-ahadihima jannatayni min aAAnabin wahafafnahuma binakhlin wajaAAalna baynahuma zarAAan; Kilta aljannatayni atat okulaha walam tadhlim minhu shay-an wafajjarna khilalahuma naharan; Wakana lahu thamarun faqala lisahibihi wahuwa yuhawiruhu ana aktharu minka malan waaAAazzu nafaran; Wadakhala jannatahu wahuwa dhalimun linafsihi qala ma athunnu an tabeeda hadhihi abadan; Wama adhunnu alssaAAata qa-imatan wala-in ruditu ila rabbee laajidanna khayran minha munqalaban *(Surat AlKahf 18:32-37)*

Tafsir: ***Na Wapigie Kwa Ajili yao Mithali au Mfano Watu Wawili Ambao Tumejaalia Kwa Mmoja Miongoni mwao Bustani Mbili Zenye kutokana na Mizabibu (yaani za Mizabibu) Na Kisha Tukazizungushia Kwa Mitende Na Tukajaalia Yake Mimea ya Mazao Iliyostawi Vizuri sana Kila Bustani Moja kati ya Hizi Mazao yake Na Wala Hakuna Kilichoharibika Ndani yake Chochote Kile Na kisha Tukamwagia Katikati yake (Kwa) Mto wa Maji Na hivyo Akawa (Yule Mwenye Shamba hilo) Mwenye kua na Mazao(Mengi Sana) Na Hivyo akasema (Kumwambia mwenzake asiekua na kitu) Huku Akiwa Katika Mazungumzo yake ya Kawaida (Akisema kua) Mimi ni Zaid yako Kwa Mali Na Ni Mtu Nnaeheshimika Zaid Na Hivyo Mtu huyo akaingia Kwenye Shamba lake Na Huku akiwa ni mwenye Kujidhulumu Ndani ya Nafsi yake Kwa kusema (kumwambia Mwenzake huyo asiekua na kitu kua) Ama Mimi Sidhanii Kua Litaangamia hili Shamba langu Na Wala Sidhani kua Kua saa ya Kiama Itawadia Na hata Kama Nikirudishwa Kwa Mola Wangu Nitapata Kheri Zaid ya Hii Inanisubiri.***

Naam..Hii ni Dharuba ambayo mfano wake ni halisi na uliowazi na ingawa hatujamalizana nao lakini kitafsiri tu basi tunaona namna anavyokua Ibn Adam pale anapojiona anajitosheleza kama zilivyosema aya kua:

﴿كَلَّآ إِنَّ ٱلۡإِنسَٰنَ لَيَطۡغَىٰٓ ۞ أَن رَّءَاهُ ٱسۡتَغۡنَىٰٓ﴾

Kalla Inna Al Insana Layatgha Anraahu Istaghna *(Surat Al Alaq 96:6-7)*

Tafsir: ***La Hakika Ibn Adam hua anavuka Mipaka pale anapojiona kua anajitosheleza.***

Na bila ya Shaka wengi wetu wako hivi yaani wanapopata na kua na Neema Basi hujiona kua ndio wao tu.

Kama alivyokua huyu Kijana katika Mfano huu ulioelezewa na Aya ambae ameingia kwenye shamba lake ambalo limenawiri na kustawi vizuri sana na hivyo, na hivyo kujiona kua Yuko Juu kuliko mwenzake kwani yeye ana Mashamba na Mali na anaheshimika lakini mwenzake ni hohe hae hana mbele wala nyuma.

Na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kuhusiana na huyu kijana kua alikua ni mwenye kujidhulumu Nafsi yake kutokana na kujisifu kwake, kwani anaona kua kila alichokua nacho kimetokana na Jitihada na akili zake. Na hivyo huenda mwenzake huyo anaezungumza nae na kujitambia mbele yake basi hana kitu kwa sababu hana akili au labda hapendwi na Mola wake. Na hivyo yeye kwa kua amejaaliwa Mali na Watoto na kila kitu basi bila ya shaka na Akhera pia atapata zaid ya hivyo alivyokua navyo katika wakati huo.

Hali hii pia Wanayo Viongozi wa nchi za Magharibi kwani Wanapokaa Madarakani hua Wanajiona ni wao tu na hivyo hufanya wanavyotaka kwa wengine ikiwemo kuwalazimisha watu kufuata mila

na desturi zao Potofu ziendazo kinyume na maumbile ya Ibn Adam za Upinde wa Mvua yaani Ndoa za Jinsia Moja.

Naam...Hivyo baada ya Kijana mwenye Mashamba yaliyonawiri kujisifia Mbele ya Mwenzake kuhusiana na Neema aliyojaaliwa na kuona kua Haitoangamia Mali hio na wala Kiama hakitotokea na hata kama kikitokea basi yeye atakua na Mali zaidi basi aya zinaendelea kutuambia kuhusiana na hali aliyokua nayo Rafiki anaeambiwa Maneno hayo kua alimgeukia Rafiki yake huyo na kuanza kumhoji kwa kusema:

﴿قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ وَهُوَ يُحَاوِرُهُ أَكَفَرْتَ بِٱلَّذِى خَلَقَكَ مِن تُرَابٍ ثُمَّ مِن نُّطْفَةٍ ثُمَّ سَوَّاكَ رَجُلاً ❁ لَّكِنَّ هُوَ ٱللَّهُ رَبِّى وَلاَ أُشْرِكُ بِرَبِّى أَحَداً ❁ وَلَوْلآ إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَآءَ ٱللَّهُ لاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِٱللَّهِ إِن تَرَنِ أَنَاْ أَقَلَّ مِنكَ مَالاً وَوَلَداً ﴾

Qala lahu sahibuhu wahuwa yuhawiruhu akafarta bialladhee khalaqaka min turabin thumma min nutfatin thumma sawwaka rajulan; Lakinna huwa Allahu rabbee wala oshriku birabbee ahadan; Walawla ith dakhalta jannataka qulta ma shaa Allahu la quwwata illa biAllahi in tarani ana aqalla minka malan wawaladan*(Surat Al Kahf 18:37-39)*

Tafsir: ***Akasema Sahiba yake Huku akiwa katika Mzungumzo ya Kawaida : 'Hivi Wewe Unamkufuru Yule Ambae Amekuumba Kutokana na Udongo? Na Kisha Akakutoa Kutokana na Maji ya Uzazi? Na Kisha akakukamilisha kua Mtu? Lakini (Kwa upande wangu) Yeye(Huyo unaemkufuru mbali ya kua amakuumba) Ni Allah na Ndie Mola wangu Na Kwangu Mimi sitomshirikisha Mola wangu na Yeyote Ingekua Bora Angalau Kama Ungeingia Kwenye Shamba lako Huku Ukisema Ma-Shaa Allah la Quwwata Illa Bi Allahi (Ametaka iwe Allah Hakuna Uwezo ila Kutoka kwa Allah) Kama Unaniona mimi Niko Chini Zaidi yako Kwa Mali na Watoto.***

Kabla ya kuendela basi inatibidi tukumbushane kua maneno *Bismi Allahi Ma-Shaa Allah la Quwwata Illa Bi Allahi* hua ni Dua nzuri sana kuitumia pale unapotaka kuanzisha kitu chako ambacho ili kukifanya basi inabidi uingie ndani ya sehemu fulani, kwa mfano kama kwenye biashara au ofisi n.k hivyo unapoingia ndani yake sehemu hio basi unatumia maneno haya kwa ajili ya kuongeza barka juu ya jambo lako na pia kuondoa husda na kijicho.

Na tunaporudi katika aya yetu basi tunaona kua Mbali ya Kuoneshwa Mali ya Mashamba na kwa Wingi wa Watoto na kudhauriliwa Kutokana na Umasikini na kutokua na Watoto lakini tunaona kua Rafiki huyu anaedharaulika kutokana na Kutokua na Mali kua ni Rafiki Bora kutokana na Kua na Utajiri wa Imani na Ikhlasi na Taqwa.

Na ndio maana tukaambiwa kua : **'Rafiki Utakaekutana nae kila siku na kisha Akakuusia Kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* bila ya kukupa chochote ni bora kuliko Rafiki ambae kila Siku ukikutana nae basi yeye anakunyooshea Mkono na kukuwekea Pesa ndani ya Mkono wako.'**

Kwani kama akitokea Mtu na ikawa kila siku Asubuhi anatoka Nyumbani kwake anakaa Barazani na kisha anatoa Pesa kuwapa Watu na mwengine akawa ni mwenye Kutoka asubuhi na kisha akukaa Barazani kwake na kisha akawa ni mwenye Kutoa Ilm ya Dini ya Kiislam basi Wallahi Watu wengi Sana watamzonga yule anaegawa Pesa kiasi ya kua hadi atajifungia Ndani mwake asitoke kutoa Pesa

tena. Ambapo kwa Yule mwenye Kutoa Ilm ya Bure basi nae atakosa Watu wanaotaka kusomeshwa kiasi ya kua Ataona kua atavunjika Moyo na atarudi ndani mwake na kusema wacha anaetaka nimsubiri aje ndani bora kuliko kusubiri nje kwa Masaa bila ya kupata Mtu wa Kumgaia Ilm ya Bure.

Na ndio Maana *Allah Subhabah wa Ta'ala* akamwambia Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* katika Aya hii kua Wapigie Dharuba hii hao ili Waliosinzia na Kulala Waamke. Na kwa kutuonesha namna Kijana alivyokua hakutetereka mbali ya kua ni mwenye kudharauliwa kutokana na kutokua na chochote kama walivyokua Waislam wa Mji wa Makkah wa Mwanzoni mwa Utume kama tulivyoelezea katika sababu ya kuteremshwa Sura hii. Basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa hikma zake anatufunza kua, Kua na Imani ya Kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Utajiri tosha.

Ambapo tunapoangalia zaid basi tunaona kua Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Watu wawili hawa. Kwani kuna Wanaosema kua hawa walikua ni watu wawili ambao Walikua ni wenye kuishi ndani ya Mji wa Makkah ambao walikua ni Abu Salamah aliekua hana kitu na Aswad Ibn Abd Adul Asad ambae ndie aliekua na Mashamba mawili hayo.

Na kuna Wanaosema kua Watu wawili hawa walionukuliwa kwenye Aya hii walikua ni watu wa Bani Israil na mfano wa Mithali ya kisa chao imenukuliwa kwa ajili ya Kutoa Fundisho.

Na kuna wasemao kua Watu wawili hawa walikua ni Myahudi aitwae Uyaynah Ibn Hisn ambae alikua na Mashamba mawili hayo na Muumini alikua ni Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu.* Ambapo Uyaynah Ibn Hisn ndie alieomba kua atengewe wakati wake na Wenzake wa Kukaa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* bila ya kuwepo Masahaba wengineo ambao ni Masikini na Nguo zao ni za Kimasikini sana na hivyo wao kina Uyaynah hawawezi kukaa pamoja nao.

Na kwa Upande mwengine basi anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhu Allahu Anhu* kua: Watu Wawili hawa walikua ni Watoto wa Mfalme wa Bani Israil, ambapo mmoja alikua ni mwenye kuutumia Utajiri wa Mali yake kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na mwengine alikua ni Mtu ambae asieamini kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.'*

Na Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamzidishia Mtu huyo Mali zaid kutokana na Mashamba yake mawili hayo, ili kumjaribu na katika wakati huo ndugu yake huyo alikua hana kitu Na hii ni kawaida ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale mtu anapokua hamuamini yeye na kutomkubali kua ndie Mola wake basi humpa Mali hapa Duniani ili apotoke zaid na kisha aje kukutana na Adhabu kali sana inayostahiki kumkuta katika siku ya Malipo kutokana na kutoamini kwake na kukufuru kwake.

Na kama tulivyoona katika Aya kua Ndugu yake huyu Mwenye kuamini alimuusia mwenzake kwa kumwambia Ni Bora kwako kama Ungeingia ndani ya Shamba lako huku ukisema *Ma Shaa Allah! La Quwwata Illa Bi Allah.* Ambapo mbali ya maneno haya ya *Ma Shaa Allah La Quwwata Illa Bi Allah* mbali ya kua ni yenye *Dhikr* na Kumtukuza *Allah Subahnah wa Ta'ala* na kumsifu kua kila Alichokitaka Kua kimekua na hakuna mwenye Uwezo wa Juu ya hili ila yeye.

Lakini pia Maneno *Ma Shaa Allah* yanapotumika pale mtu unapokiona kitu kizuri kilichoumbika Kimaumbile na kukuvutia basi hua ni yenye Kuondoa Husda, Kijicho na Wivu kutoka kwa Muangaliaji na Msemaji, na hii ni kwa sababu baadhi ya wakati athari ya husda hua ni yenye kutokea kwa mtu dhidi ya mtu mwengine na kumuathiri bila ya mtu husika kukusudia kufanya husda.

Hivyo Inapendekezwa kwa Kila Muislam pale anapoona Kitu kitakachomfurahisha kutokana na kumvutia iwe Mazingira ya Kitu, Iwe Maumbile ya Kitu, Iwe Kiumbe mwenzake, Mafanikio ya Mwenzake, Iwe Mali n.k basi anatakiwa aseme *Ma-Shaa Allah.* Na kama ikiwa Utasema *Ma-Shaa*

Allah La Quwwata Illa Bi Allah Basi hua ni mwenye kupata Malipo zaidi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo amesema Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* kua: Aliniambia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Hivi Jee nikuambie kuhusiana na Hazina ya Peponi? Ni kusema *La Hawla wala Quwwata Illa Bi Allah'***

Na alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ***'La Hawla wala Quwwata Illa Bi Allah*** **hua inamaanisha hakuna njia ya usalama dhidi ya ujinga au dhidi ya kudumu katika kufanya maovu kutokana na ujinga, isipokua kwa kupitia kwako wewe (Allah Subhanah wa Ta'ala) hakuna uwezo wa kufanya yale uliyotuamrisha kikanuni, na wala hakuna uwezo wa kufanikisha juu yake, isipokua kwa msaada wako''**

Imam Al Tustari anasema kua*: **'La Hawla wala Quwwata Illa Bi Allah'*** **hua kunamaanisha Hakika sisi hatuna uwezo wa kufanya yale uliyotuamrisha kikanuni, na wala hatuna uwezo wa kufanikisha juu yake, na wala hatuna chenye kutubainishia kuhusiana na mwisho wetu isipokua kwa msaada wako'**

Aliulizwa Imam Al Tustari: **'Hivi jee kuna kitu gani bora zaidi ambacho Ibn Adam anaweza kupewa na Mola wake'** ambapo nae akajibu: **'Ilm ambayo kutokana nayo itakua ni yenye kumpelekea kua ni mwenye kuzidi kumhitajia Mola wake.'**

Naam..hivyo aya zinaendelea kutuarifu kuhusiana na Kijana aliekua akimuusia mwenzake kua alitakiwa aseme *Ma Shaa Allah La Quwwata Illa Bi Allah* kua baada ya hayo basi akasema:

﴿فعسىٰ رَبِّي أَن يُؤْتِيَنِ خَيْراً مِّن جَنَّتِكَ وَيُرْسِلَ عَلَيْهَا حُسْبَاناً مِّنَ ٱلسَّمَآءِ فَتُصْبِحَ صَعِيداً زَلَقاً ۞أَوْ يُصْبِحَ مَآؤُهَا غَوْراً فَلَن تَسْتَطِيعَ لَهُ طَلَباً﴾

FaAAasa rabbee an yu/tiyani khayran min jannatika wayursila AAalayha husbanan mina alssama-i fatusbiha saAAeedan zalaqan; Aw yusbiha maoha ghawran falan tastateeAAa lahu talaban*(Surat Al Kahf 18: 40-41)*

Tafsir: ***Huenda Mola wangu Akanipa Mimi Kheri Bora zaidi ya Shamba Lako Na Kisha akaishushia Juu yake (Shamba Lako) Radi Kutoka Mbinguni Na Kisha Ikawa ni sehemu ya Ardhi yenye vumbi lenye utelezi Au Akayazamisha Maji yake Na Kisha ukawa huwezi kuyapata tena.***

Ambapo haya yalikua ni Majibu aliyojibiwa Kijana aliekua akifikiria kua kamwe Bustani yake haiwezi kuangamia Na hivyo Kijana mwenye Kujua uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua mbali ya kua yeye ndie aliemjaalia kua na kila kitu chake anachojisifia kutokana na uwezo wake basi pia ni *Allah Sunhanah wa Ta'ala* pekee ambae ni mwenye uwezo wa kumpokonya Mali hio kwa njia tofauti ambazo ni vigumu kufikirika wala kudhibitika kwa asieamini.

Kwa mfano Kusababisha kuipiga Radi na kuyaunguza Mazao yote ya shamba hilo na kisha Eneo hilo kubakia na Jivu tupu juu yake au Kuyakausha maji anayoyategemea na kisha mazao yake kutokua na uwezo wa kunawiri na kukauka na kuharibika badala yake na hivyo majigambo yake hayo kua ya bure kwani baada ya matokeo kama hayo basi Kijana huyo hatokua na cha kujisifia. Hata hivyo mbali

ya kuambiwa hivyo lakini kijana huyo hakua ni mwenye Kutafakkari na kuamini kua hayo aliyousiwa yanaweza yakatokea, na hii ni kwa sababu Kijana alikua akijihisi kua yuko Kileleni hivyo hakuna wa kumteremsha chini.

Wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema katika *Surat An Nisaa* kua:

﴿وَٱعْبُدُواْ ٱللَّهَ وَلاَ تُشْرِكُواْ بِهِ شَيْئاً وَبِٱلْوَالِدَيْنِ إِحْسَاناً وَبِذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَامَىٰ وَٱلْمَسَاكِينِ وَٱلْجَارِ ذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْجَارِ ٱلْجُنُبِ وَٱلصَّاحِبِ بِٱلْجَنْبِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ إِنَّ ٱللَّهَ لاَ يُحِبُّ مَن كَانَ مُخْتَالاً فَخُوراً﴾

WaoAAbudoo Allaha wala tushrikoo bihi shay-an wabialwalidayni ihsanan wabidhee alqurba waalyatama waalmasakeeni waaljari dhee alqurba waaljari aljunubi waalssahibi bialjanbi waibni alssabeeli wama malakat aymanukum inna Allaha la yuhibbu man kana mukhtalan fakhooran*(Surat An Nisaa 4:36)*

Tafsir: ***Na Muabudu Allah Na wala Usimshirikishe Na Chochote Na kwa Wazee Wawili Wafanyie wema Na Kwa Ndugu wa Karibu Na Kwa Mayatima Na Kwa Masikini Na Kwa Majirani wa Karibu Kwa Udugu Na Kwa Majirani wa Mbali kwa Udugu Na Marafiki wa Karibuu Na Kwa Wasafiri Na Wenye Kumilikiwa na Mikono yenu ya Kulia Hakika Ya Allah Hampendi Yule Ambae ni Mwenye Kujiona na kujisifu.***

Ambapo kwani kwa upande mmoja basi hii ni Aya ambayo inatuonesha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* Hawapendi watu wenye kujiona na kujisifu kwa maneno mbele za Watu wengine kama Alivyofanya Kijana mwenye Mashamba Mawili yaliyonawiri kwenye Kisa chetu cha *Surat Al Kahf*.

Lakini kwa upande wa Pili hii pia tunapoiangalia Aya hii basi tunaona kua ni Aya inayohimiza Kuhusiana na Usimamizi wa Haki kwa Mpangilio wake kuanzia kwa Muumba hadi kwa Viumbe kwa Viumbe Miongoni mwao, na kisha ndio ikamalizia kkwa kutoa na Onyo la *kua Allah Subhanah wa Ta'ala* hapendi Wenye Kujiona na Kujitamba kwa Fakhari.

Kwani Tuapoangalia Majukumu ya Utekelezaji wa Haki basi tunaona kua Kwanza kuna Haki ya Kila Mja kwa *Allah Subhanah wa Taala* Ya Kuabudu na kisha kuna Haki ya Kuwafanyia Wema Wazee, Na Ndugu na Mayatima, Na Masikini na Majirani wa Udugu na Majirani wa Umbali Na Marafiki na Wasafiri na Waliochini yetu yaani Wafanyakazi Au Watumwa na Mateka.

Na hili ni Jambo ambalo tushawahi kulizungumzia hapo Kabla na kufahamishana kua Hii aya na Nyenginezo kama hii, kwani ziko kadhaa ikiwemo Aya zinazoamrisha wanaostahiki kupewa Zakkah na Sadaqa.

Kwani aya hii na nyenginezo zenye kuainisha Mpangilio wa Haki Baina ya Mja Na Mola wake na Viumbe wenzake kama huu basi hua ni Aya zinazoamrisha kwa Msisitizo wenye Kutufunza Umuhimu wa Kua na Umoja katika Dini ya Kiislam.

Na hivyo katika Kuainisha kwake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatubainishia kua Umoja wa Kiislam unaanzia Katika Kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Kumuabudu na kutomshirikisha.

Na kisha Umoja huo unaanzia Kwenye Familia kwanza Kwa Wazee, kisha kwa Ndugu, Kisha Mayatima, Masikini, Kwa Majirani na Kwa Wasafiri wanaopita kwenye ardhi ya Jamii husika.

Na hivyo kutubainishia kua Waislam tunatakiwa Kushikamana kupitia kwa Muumba kisha Kwenye Familia hadi mwisho wa mpangilio uliotajwa na Aya, na hivyo ndivyo inavyotakiwa katika Mfumo wa Maisha ya Muislam katika Kila Ibada yake na kila kitu chake ikiwemo Ibada ya Kufunga Mwezi wa Ramadhan yaani Ufunge kwa kushikamana na Jamii yako, kwani unapofunga na Kufungua kwa kufuata Muandamo wa Mwezi wa Sehemu uliyokuwepo pamoja na wenzako wa karibu yako basi unakua ni mwenye kusimamia na kutekeleza Jukumu lako juu ya Haki za Waliokaribu yako kama alivyoamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* katika Aya kwani ukifanya vyenginevyo kwa Kufunga na kufungua kwa kufuata Mwezi wa Kimataifa na hivyo kua ni mwenye kutofautiana na Walio Karibu yako katika Jamii Yako basi unakua umewavunjia haki yao Kifamilia, Kiudugu, Kijirani nk na kujionesha kua wewe ni bora zaidi yao.

Na utakua na sifa ya *Mukhtala Fakhuran* Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* hawapendi Watu wenye Sifa hio na kutokana kuchikiza kwa Sifa hio Mbele ya Allah ndio Maana ikaamrishwa Tufunge na Kufungua kwa Pamoja Kijamii ili usiwe na ufa wala utengano baina yetu katika Jamii ya Kiislam.

Kwani baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kudhihirisha kua Hawapendi watu Wenye Kujifakharisha Na Kujitangazia katika Mambo yao kama alivyotoa Mfano katika kisa hiki cha Vijana wawili ambapo mmoja miongoni mwao kua ni mwenye kua na Mashamba mawili. Basi anatudhihirishia kile ambacho alikifanya na kikamtokea kwa Mtu huyo kwa kusema:

﴿وَأُحِيطَ بِثَمَرِهِ فَأَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَّيْهِ عَلَى مَآ أَنْفَقَ فِيهَا وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَيَقُولُ يٰلَيْتَنِي لَمْ أُشْرِكْ بِرَبِّي أَحَداً ﴾

Waoheeta bithamarihi faasbaha yuqallibu kaffayhi AAala ma anfaqa feeha wahiya khawiyatun AAala AAurooshiha wayaqoolu ya laytanee lam oshrik birabbee ahadan *(Surat Al Kahf 18:42)*

Tafsir: ***Na Hivyo yakavamiwa Mazao yake (Kwa Maangamizo ya Moto)na Akabakia akipiga Mikono yake kwa Huzuni kubwa sana Kutokana na Aliyokwishatoa kwa kutumia juu ya Shamba lake Na Huku kila Kitu kimeshatekea Kwenye Vitegemezi vyake (vya Miti inayochomekwa Kwa ajili ya Kuizuia Mizabibu hio isianguke chini) Akabakia Akisema : 'Ole Wangu mimi Bora Nisingemshirikisha Mola wangu na Chochote'***

Subhanah Allah! Kwani Huu ulikua ni mtihani Mkubwa Sana. Kwani Aya zinatuonesha kua Baada ya Kijana huyu kujisifia kutokana na Kuona namna Lilivyonawiri Shamba Lake la Mizabibu likiwa limejaa Zabibu na Mitende na Maji yanayotiririka ndani yake, akajiona kua ameshakua Tajiri zaid ya Alivyokua hapo kabla kwani ameingiza Pesa zake zote katika Shamba lake hilo na Shamba hilo Limetoa Zabibu na Tende si Mchezo. Na kisha baada ya hapo akausiwa na Rafiki yake kua aoneshe Shukran na asimkufuru Mola wake.

Lakini nae hakufanya hivyo kwa sababu kama tulivyosema kua alikua anajiona yuko juu sana hivyo hawezi kushuka chini kwa Ufakhari wake uliotokana na neema alizopewa na Mola wake. Hivyo Jioni hio Marafiki wawilo hao wakaondoka kutoka katika Shamba hilo na kisha kila mmoja akaelekea katika hamsini zake. Ambapo ilipowadia Siku ya pili Asubuhi basi Kijana huyo akaelekea Shambani kwake kwa ajili ya kuvuna lakini alipofika Shambani kwake basi akakuta Mizabibu yote imeungua kwa Moto ambao haujulikani hat ulitokea wapi na wala ulianzia wapi, na cha kushangaza ni kua

kawaida Mizabibu hua inapopandwa basi pembeni yake huchomekwa Vijiti kwa ajili ya kuufunga Mzabibi na Vijiti hivyo ili kuufanya Mzabibu huo Usianguke chini bali uwe ni wenye kuelekea juu, kwani kama hukufanya hivyo basi Zabibu zikizaliwa zitaanguka na kugusa udongo na kisha kuharibika kabla ya kuwiva.

Sasa katika Aya hii basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua Mizabibu hio Ilizungukwa na kuetekea huku kikiwa imebakia kwenye Vijiti vyake hivyo. Haya yalikua ni maajabu yenye kuonesha kua Moto huo haukuwa ni Moto uliowashwa na Ibn Adam, ambapo labda tutasema kua yule kijana mwengine alirudi na kulitia moto shamba Kwani kama angefanya hivyo basi kisingebakia kitu, hadi vile vijiti vingeungua kwa moto na hivyo angekuta Jivu Tupu.

Lakini hapa hali haikua hivyo kwani Mizabibu Iliangamia ila Vijiti vya kuizuia Mizabibu vilibakia. Yaani kama kule kulikoungua shoka Lakini Mpini ukabakia, Huo ndio Uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambao unadhihirishwa a maneno yasemayo La Quwwata Illa Bi Allah! kama kwenye kisa cha Nabii Ibrahim Moto ulipomalizika basi Nabii Ibrahim alitoka akiwa salama.

Na tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anazungumzia kuhusiana na Shamba moja wakati hapo awali alisema kua kijana alijaaliwa kua na Mashamba Mawili, hivyo hii haimaanishi kua liliangamia ni shamba moja tu,bali inamaanisha kua mashamba mawili haya yameangamia kwa muangamizo mmoja kama kwamba hayakua ni mashamba mawili bali ni moja kutokana na muangamizo wake.

Na kisha *Allah Subhabah wa Ta'ala* anaendelea kututhibitishia kua *La Quwwata Illa Bi Allah* yaani Hakuna Nguvu Isipokua kutoka kwa Allah kwa kusema kuhusiana na Kijana anaeelezewa kwenye Mithali yetu na pia kwa kila mmoja Miongoni mwetu kua:

﴿وَلَمْ تَكُن لَّهُ فِئَةٌ يَنصُرُونَهُ مِن دُونِ ٱللَّهِ وَمَا كَانَ مُنْتَصِراً ﴾

Walam takun lahu fi-atun yan<u>s</u>uroonahu min dooni All<u>a</u>hi wam<u>a</u> k<u>a</u>na muntas<u>i</u>r<u>a</u>n *(Surat Al Kahf 18:43)*

Tafsir: ***Na Wala Hakuwa Na Kundi La Watu kwa ajili yake Wa Kumnusuru Yeye Dhidi ya Allah Na Wala Hakua yeye ni Miongoni mwa wenye kuweza kujinusuru.***

Hivyo Aya zinatuonesha kua Kujisifia kwake kote Kiumbe Ibn Adam hua hakumfai kitu na wala hakutomfaa kitu hata awe na uwezo wa Kiasi gani, Yaani hata Awe na Jeshi la Wapiganaji wa Dunia nzima, Awe Na Mali, Awe na Hazina ya Dunia nzima, Awe na Wafuasi wengi sana n.k

Kwani kama ikiwa Mtu huyo ni mwenye kupingana na Muumba wake *yaani Allah Subhanah wa Ta'ala* basi atakua ni mwenye kula hasara na kuangamia tu kwani hakuna wa Kumnusuru wala Kitakachomnusuru na wala hatoweza kujinusuru yeye mwenyewe Nafsi yake.

Isipokua kwa Njia ya Kuomba Msamaha kwa Mola wake.Kwani kama kijana huyu angekua ni mwenye Kumsikiliza wasia wa Rafiki yake na kutafakkari na kutanabahi basi angenusurika na kua Mashamba yake kua Salama badala yake na pia angejinusuru yeye mwenyewe pia Nafsi yake.Ambapo kwa upande wake kijana huyu alitanabahi wakati tayari akiwa katika hali ya Kuchelewa na hivyo kutanabahi kwake kukawa ni sawa na Majuto ambayo ni Mjukuu

Kisha aya zinaendelea kwa kusema:

﴿هُنَالِكَ ٱلْوَلَايَةُ لِلَّهِ ٱلْحَقِّ هُوَ خَيْرٌ ثَوَاباً وَخَيْرٌ عُقْباً﴾

Hunalika alwalayatu lillahi alhaqqi huwa khayrun thawaban wakhayrun AAuqban *(Surat Al Kahf 18:44)*

Tafsir: ***Katika Kama haya Ulinzi na Uhifadhi Hua ni Kutoka kwa Allah Mungu wa Kweli na wa Haki Yeye ndie M-bora Wa Kulipa Malipo ya Thawabu Na Ndie mwenye Ubora wa Mwishoni mwa Matokeo.***

Kwani Aya inatudhihirishia kua Kila kitu kinachofanywa kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni chenye mwisho mema na ni chenye kulipwa kikamilifu malipo ya Thawabu zake na mwishoni mwake Kitu hicho basi kutakua na malipp bora zaid na aliefanya Kitu hicho kamwe hatokua ni mwenye kujuta kwani mwisho huo wa matokeo unaozungumziwa hapa ni katika Siku ya Malipo. Na si hivyo katika yanayofanywa na Muumini wa kweli basi kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu.

Bali pia hata mitihani yote anayoipata Muumini na kisha Muumini husika akawa ni mwenye Kua na Subra na kumtegemea Mola wake basi Muumini huyo hua ni mwenye kufutiwa Dhambi zake na Kuongezewa Thawabu na hivyo kua ni mwenye kulipwa kwa kupata Matokeo bora katika Siku ya Malipo ambae ndie aliempa Neema ya Mali hio.

Na badala yake akawa ni mwenye kujiona na kujisifu huku akijihesabia kua kila alichokipata na kua nacho basi ni chenye kutokana na Ufahamu wake bila kujua kua hata huo Ufahamu wake na Jitihada zake pia zimetoka kwa Mola wake na hivyo akaona kua hazitotoweka neema hizo.

Ambapo matokeo yake *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamuonesha Uwezo wake kupitia katika Mijuiza yake.

Kwani Kama ilivyokua katika kisa cha *Fityatun* yaani Watu wa *As-hab Al Kahf* kua kuna Mithili yake pia ambao ni wale waliotajwa kwenye Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama tulivyoona hapo mwanzoni ambao ni watu watatu walipojificha Mvua kisha Likaanguka Jiwe na kuzima mlango wa Pango walilojifichia na kutoweza kutoka nje hadi pale walipoamua kufanya Tawwasul kwa kupitia Amali zao njema zaid ndio Jiwe hilo likasogea na Wakatoka.

Basi kwa upande wa Watu waeili hawa wa Shambani wa Surat Al Kahf basi pia kuna kisa chengine Mithili ya kisa chao hawa ambacho nacho kimetajwa kwenye *Surat Al Qalam* kuanzia katika Aya ya 17 hadi ya 33. Na Wanasema Wanazuoni kua Hapo zamani katika wakati wa kipindi cha Watu wa Ahl Al Kitab yaani kabla ya kuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi kulikua kuna Mzee mmoja ambae alikua ni mcha Mungu sana.

Ambapo Mzee huyu alikua na Familia yake yenye Watoto Kadhaa ambao ni wakubwa na alikua na pia alikua akimiliki Shamba kubwa sana.

Na kutokana na Ucha Mungu wake Mzee huyo basi ilikua ni kawaida yake kua kila mara anapovuna kutoka katika Shamba lake basi hua ni mwenye kugawa mazao hayo katika sehemu mbili: Ambapo sehemu moja huiweka kwa ajili ya Familia yake na sehemu iloyobakia huitoa kwa Ajili ya *Allah Sunhanah wa Ta'ala* na hivyo sehemu hii huitumia kwa ajili ya kutoa Sadaqa kwa Majirani zake na Masikini na Wasiokua na uwezo na Wapita njia.

Ambapo Jambo hili halikua ni lenye kuwapendezesha watoto wake, kwani watoto hao walikua wakiona kua Baba yao anatupa Mali yao kwa kuigawa badala ya kuiuza na kujiongezea Mali na Utajiri. Hivyo Wakawa wanasema kua : **'Hakika Baba yetu sisi ni Mjinga sana kwani Ufahamu wake ni mdogo, yaani badala ya Kuuza mazao yaliyobakia akapata Pesa basi yeye ni mwenye kugawa bure, hivyo kama ingekua ni sisi basi aah tungetumia chetu na kilichobakia tungeuza na kunufaika zaid na Shamba hili'**

Naam..Vijana hawa walisahau kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kuona na kujua juu ya kila kitu. Na hivyo kwa hikma zake akaamua kuwaonesha Uzuri wa Baba yao waliekua wanamuona kua Mjinga na hana akili. Na kisha akawaonesha Ujinga wao mbali ya kujiona kua wana akili. Na Ujinga huu wa watoto hawa ndio Ujinga unaotawala kwenye Nyoyo za Waislam leo hii katika Jamii yetu

Hivyo ulipowadia wakati alioukadiria Muumba basi akaichukua Roho ya Baba yao watoto hao na kisha akawaachia Watoto Mtihani uliokuwepo mbele yao kama zinavyosema aya.

﴿إِنَّا بَلَوْنَاهُمْ كَمَا بَلَوْنَآ أَصْحَابَ ٱلْجَنَّةِ إِذْ أَقْسَمُواْ لَيَصْرِمُنَّهَا مُصْبِحِينَ ۞ وَلاَ يَسْتَثْنُونَ ۞ فَطَافَ عَلَيْهَا طَآئِفٌ مِّن رَّبِّكَ وَهُمْ نَآئِمُونَ ۞ فَأَصْبَحَتْ كَٱلصَّرِيمِ ۞ ۞ فَتَنَادَوْاْ مُصْبِحِينَ ۞ أَنِ ٱغْدُواْ عَلَىٰ حَرْثِكُمْ إِن كُنتُمْ صَارِمِينَ ۞ فَٱنطَلَقُواْ وَهُمْ يَتَخَافَتُونَ ۞ أَن لاَّ يَدْخُلَنَّهَا ٱلْيَوْمَ عَلَيْكُمْ مِّسْكِينٌ ۞ وَغَدَوْاْ عَلَىٰ حَرْدٍ قَادِرِينَ ۞ فَلَمَّا رَأَوْهَا قَالُوٓاْ إِنَّا لَضَآلُّونَ ۞ بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ۞ قَالَ أَوْسَطُهُمْ أَلَمْ أَقُلْ لَّكُمْ لَوْلاَ تُسَبِّحُونَ ۞ قَالُواْ سُبْحَانَ رَبِّنَآ إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ۞ فَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَلاَوَمُونَ ۞ قَالُواْ يٰوَيْلَنَا إِنَّا كُنَّا طَاغِينَ ۞ عَسَىٰ رَبُّنَآ أَن يُبْدِلَنَا خَيْراً مِّنْهَآ إِنَّآ إِلَىٰ رَبِّنَا رَاغِبُونَ ۞ كَذٰلِكَ ٱلْعَذَابُ وَلَعَذَابُ ٱلآخِرَةِ أَكْبَرُ لَوْ كَانُواْ يَعْلَمُونَ﴾

Inna balawnahum kama balawna as-haba aljannati idh aqsamoo layasrimunnaha musbiheena; Wala yastathnoona; Fatafa AAalayha ta-ifun min rabbika wahum na-imoona; Faasbahat kaalssareemi; Fatanadaw musbiheena; Ani ighdoo AAala harthikum in kuntum sarimeena; Faintalaqoo wahum yatakhafatoona; An la yadkhulannaha alyawma AAalaykum miskeenun; Waghadaw AAala hardin qadireena; Falamma raawha qaloo inna ladhalloona; Bal nahnu mahroomoona Qala awsatuhum alam aqul lakum lawla tusabbihoona Qaloo subhana rabbina inna kunna *dha*limeena; Faaqbala baAAduhum AAala baAAdhin yatalawamoona; Qaloo ya waylana inna kunna tagheena; AAasa rabbuna an yubdilana khayran minha inna ila rabbina raghiboona; Kadhalika alAAadhabu walaAAadhabu al-akhirati akbaru law kanoo yaAAlamoona *(Surat Al Qalam 68:17-33)*

Tafsir: ***Kwa Hakika tuliwajaribu wao kama tulivyowajaribu watu wa Shambani, pale walipoapa kuyachuma Matunda (asubuhi yake) Pale alipoapa kuyachuma Matnda ya shambani mwao katika***

wakati wa asubuhi yake bila ya kusema In-shaa Allah. Na kisha kikapita kitu (Moto) katika shamba lao kutoka kwa Mola wako katika wakati wa usiku yake na kuchoma kila kitu wakati wao wakiwa wamealala. Na hivyo Shamba hilo likawa jeusi katika wakati wa asubuhi kama sehemu ya usiku wa kiza kikubwa sana. Hivyo wakaitana pale ulipoingia wakati wa asubuhi huku wakisema: 'Nendeni katika katika mashamba yenu asubuhi kama mtataka kuyachuma matunda yenu.' Hiyvo wakatoka na kuzungumza kwa sauti za chini wakisema: 'Hakuna Masikini hata mmoja atakaeingia kwenu leo hii' na hivyo wakaenda katika asubuhi hio wakiwa na nia thabiti wakidhania kua wanao uwezo (wa kuwazuia Masikini kutokana na kuchuma matunda yao katika Shamba lao ndani ya siku hio). Lakini walipofika na kuona Shambani wakasema: 'Lo! Kwa hakika sisi tumepotea' na kisha wakasema: 'La bali tumekataliwa Mazao yetu.' Na mbora miongoni mwao akasema: 'Hivi jee sikukuambieni mimi kwanini hamsemi In-Shaa Allah?' nao wakasema: 'Utukufu ni wa Mola wetu, kwani kwa hakika sisi tumekua ni wenye kujidhulumu' na kisha wakageukiana na kulaumiana. Na kusema: 'Ole wetu kwa hakika sisi tulikua ni wenye kuvuka mipaka kwa maovu. Na tunatumai kua Mola wetu atatubadilishia Shmab lililobora zaidi ya hili, kwani kwa hakika sisi tunarudi kwa Mola wetu (ili atusamehe makosa yetu). Hayo ndio Malipo (ya hapa Duniani) lakini kwa ukweli basi Adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi kama wangekua wanajua.'

Ambapo anasema Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua: '**Imam Qatadah Al Sadusi aliulizwa kuhusiana na Watu hawa kama walikua ni: 'Waliokua wakimuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* ama la.' Ambapo nae akasema: 'Mnanipa Majukumu makubwa sana katika Masuali yenu mnayoniuliza.''**

Ambapo visa vyote viwili hivi vya Mashamba au Mabustani mbali ya kua ni vyenye kutudhidhirishia uuhimu wa kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila kitu na kusema In-shaa Allah katika kuahidi mambo yajayo lakini pia ni vyenye kutufunza kua Rehma na usamehevu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mkubwa sana na hivyo tusivunjikeMoyo baada ya kufanya maovu kwani ni maumbile ya Ibn Adam kukosea, lakini pia ni maumbile ya Ibn Adam kujirekebiesha pale anapokosea, na hivyo tunapozungumzia kuhusiana na makosa ya kumkosea *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ni wajibu wetu kuomba Msamaha kwake kwa Ikhlasi na kutokana na Usamehevu wake na rehma zake basi bila ya shaka atatusamehe.

Hivyo tumeona namna *Allah Subhanah wa Ta'ala* anavyotuonesha na kutufunza Umuhimu wa kua ni wenye kumtegemea yeye katika Kila kitu. Ambapo jambo hili halikumrishwa juu yetu sisi tu bali limeamrishwa kwa kila mtu mwenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo hapo hapo kutudhihirishia kua Kila tulichokua nacho Ibn Adam basi kutokana na Majaaliwa yake juu yetu na hivyo tunatakiwa kuonesha Shukran kwa Kutuneemesha kwake juu yetu.

Kwani Tumeona Mifano miwili ya Vijana na Mashamba yao ambapo mmoja ulikua ni kwenye Sura yetu tunaendelea nayo kuifafanua Tafsir yake na mfano wa pili ni kwenye Surat Al Qalam. Ambayo vyote ni vyenye kutuonesha kua Allah Subhanah wa Ta'ala anatuneemesha si kwa ajili ya Manufaa ya Kidunia tu, bali kwa ajili ya manufaa ya Kiakhera zaidi. Kwani tunachoneemeshwa Duniani hua ni kwa asilimia 30 kwa ajili ya Dunia na Asilimia 70 kwa ajili ya Akhera. Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatudhihirishia haya tena katika Aya inayofuatia baada ya ile tuliyomalizana nayo katika *Surat Al Kahf* kwa kusema kua:

﴿وَٱضْرِبْ لَهُم مَّثَلَ ٱلْحَيَاةِ ٱلدُّنْيَا كَمَآءٍ أَنْزَلْنَاهُ مِنَ ٱلسَّمَاءِ فَٱخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ ٱلأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيماً تَذْرُوهُ ٱلرِّيَاحُ وَكَانَ ٱللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِراً﴾

Waidhrib lahum mathala alhayati alddunya kama-in anzalnahu mina alssama-i faikhtalata bihi nabatu al-ardhi faasbaha hasheeman tathroohu alrriyahu wakana Allahu AAala kulli shay-in muqtadiran*(Surat Al Kahf 18:45)*

Tafsir: ***Wapigie (tena) Dharuba hao Mithali ya Maisha ya Dunia Kua Kama Vile Maji Yanayoanguka Kutoka Mbingui Na Kisha Yakachanganyika Na Mimea ya Ardhini Na Kisha ikawa Imenawiri Lakini Baadae Ikakauka na Kukatika kwa Upepo Na kwa hakika Allah Juu ya Kila kitu ni mwenye Kuweza.***

Subhanah Allah!

Naam..hii ni Dharuba nyegine ya kibao cha Uso inayotutaka mimi nawe tutafakkari zaid! Kwani Dharuba ya kibao hiki imetufikia mara tu baada ya kumalizika Dharuba ya Vijana wenye Mashamba, yaani kwa kifupi hapa kuna Dharuba mbili zinazotutaka tuache kusinzia, tumepigwa ya kwanza kwenye shavu la kulia na kisha hii iya aya hii ni ya shavu la Kushoto.

Hivyo Dharuba zote mbili hizi zinatutaka tuzindukani ili tupate kujua kua Maisha ya Kidunia kua si chochote si lolote. Ila Jee tutazindukana kweli? kwani kila mtu ameghafilika na Maisha ya Kiakhera kwa Dunia yake.

Kwani hapa tunaona kua aya zinasema kua Maisha ya Dunia ni kama Maji ya Mvua yanayoshuka kisha yakaimwagilia na Kuistawisha Mimea ardhini na kisha Maji hayo yakatoweka Ndani ya Ardhi kwani Maji yanapokaa sehemu hua si ya Kudumu na hivyo mwisho wake hutoweka kwa kuingia Ardhini. Hivyo Jee na sisi Tutadumu?

Hivyo inabidi tujue kua vyovyote vile itakavyokua hata Tudumu kwa miaka 500 ndani yake basi bila ya shaka mwanzoni Tutanawiri na kua na Miili ya Vijana Shababi kama inavyonawiri mimea baada ya kwamwagia Maji ya Mvua. Lakini hata hivyo mwishowe miili yetu itakauka na kunywea kama inavyonywea Mimea baada ya kukosa Mvua na kutoweka kwa Maji yake.

Hivyo basi ni Aya zinatuwekea wazi kua tujitahidi tusisahau kuhusiana na Mola wetu na pia Kuhusiana na tunakoelekea yaani Akhera kwani tukijisahau na kughafilika na Akhera basi tutajikuta katika hali ya Miongoni mwa wenye Majuto makubwa sana na *Allah Subhabah wa Ta'ala* anatuzindua kwa Dharuba za Mithali kama hizi kwa sababu ya kutupenda na kutuonea huruma Waja wake.

Na ndio maana akatuusia pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: '**Dunia hii ni Tamu sana na Imenawiri sana. Lakini Hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemjaalia Ibn Adam kua ni Khalifa wake Juu ya Ardhi hii ya Dunia na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakua ni mwenye kumfuatilia kwa kumuangalia anaishi vipi kitabia juu yake**. **Kwa hivyo basi Jilindeni Dhidi ya Dunia kwa kutoikumbatia na pia Jilindeni Dhidi ya Wanawake. Kwani Mitihani ya Mwanzo iliyotokea baina ya watu wa Bani Israil ilikua ni kutokana na Wanawake***(Sahih Muslim)*

Ama kwa hakika ndani ya Aya hii na Hadithi hii basi mna mafunzo tosha na yaliyowazi Kua Maisha ya Dunia hii ukiingia Ndani yake basi kuna Mitihani mingi sana ambayo lazima utakumbana nayo kwani kukosana nayo hua haiwezekani kwa sababu hali inakua kama vile ambavyo haiwezekani kwa Mtu ambae anaevuka Mto kwa Miguu kisha asiroe kutokana na Maji yake.

Lakini hata hivyo Mtu anaevuka Mto hua na Tahadhari ya kutoweka mguu kwenye sehemu yenye kina kirefu cha Maji kwani mguu utazama na huenda nae akaangamia. Hivyo Nasi pia tunatakiwa kua na Umakini wa Kujilinda na Mitihani ya Kidunia ili tusije tukaangamia, na bila ya shaka moja kati ya Njia ya Kujilinda hua ni Kukinai Ulichojaaliwa na Mola wako kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Amefuzu Yule Mtu ambae ni Muislam na kisha akajaaliwa mahitaji ya kiasi chake nae akaridhika kutokana na Majaaliwa hayo.'** *(Sahih Muslim)*

Tunaenedela na aya inayofuatia ambayo ni yenye asili ya Neno *Zana* ambalo kwa Kilugha hua linamanisha Kupamba, Kutia Nanga au Kudodesha. Neno *Zana* Ndio lililotoa neno *Zinatun* ambalo humaanisha Mapambo au Madodesho yaani Vitu Ambavyo Vinatiwa Kwenye Kitu chengine na hivyo Kitu hicho kulichotiwa Vitu hivyo kuonekana kua ni Chenye Kuvutia na Kutamanisha. Neno *Zana* pia limetoa neno *Zayyana* lenye Kumaanisha Kitu Kilichopambwa.

Ambapo aya hio ni yenye kusema:

﴿ٱلْمَالُ وَٱلْبَنُونَ زِينَةُ ٱلْحَيَاةِ ٱلدُّنْيَا وَٱلْبَاقِيَاتُ ٱلصَّالِحَاتُ خَيْرٌ عِندَ رَبِّكَ ثَوَاباً وَخَيْرٌ أَمَلاً﴾

Almalu waalbanuuna zeenatu alhayati alddunya waalbaqiyatu alssalihatu khayrun AAinda rabbika thawaban wakhayrun amalan *(Surat Al Kahf 18:46)*

Tafsir: ***Mali Na Watoto Ni Mapambo Ya Maisha ya Duniani Na Yanayobakia Mambo Mema Ni Bora Mbele ya Mola wako Kwa Malipo ya Thawabu Na Ni Bora kwa kuyategemea.***

Naam...Hii ni aya ambayo wengi wetu wanaijua, wanainukuu na wanaifahamu kimaana..Alhamd lillah. Ambapo tunaona ndani yake kua Mbali ya kua Watu ni wenye kupenda Mali na Watoto na hivyo hua ni wenye kujisifu pale Watu wanapokua Matajiri au Wanapokua wana Watoto wengi na hivyo kua ameendeleza na amebakisha Kizazi na hivyo kua ni mwenye kutajwa hapa Duniani hata baada ya kufariki kwake kupitia kwa Watoto wake.

Lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatutahadharisha kwa kusema kua hayo yote ni Mapambo ya Kidunia na hivyo huenda yasikufae kitu katika Maisha ya Akhera na ubaya ni kua huenda vitu hivyo tunavyoviona kua ni vizuri vinavutia na kuvipenda ambavyo ni Mali na Watoto vikawa ni Mtihani kwetu katika Siku ya Malipo kwani tutaulizwa tulivisimamiaje. Hapo sasa ndio Mtihani kwa sababu Utaulizwa Mali yako uliichumaje na uliitumia vipi?

Na hatari zaid hapa kwenye watoto, kwani kila wakiwa wengi basi ndio inazidi kua mingi juu yako. Kwani kama hukuwasimamia na kuwapatia Ilm ya Dini ya Kiislam na kuwale katika Misingi ya Dini ya Kiislamu, basi bila ya Shaka katika Siku ya Malipo itakapokua sote hatuna chochote hata ile Nguo hatuna, basi Watoto wako hao watakua wanakutafuta kwa udi na uvumba na wewe unawakimbia wao kwa kila njia huku nawe ukiwatafuta Wazee wako ili uwatupie Mzigo wa Dhambi zako kutokana na kutokusomesha Dini yako kama vile ambavyo Watoto wako wanakutafuta wewe ili wakutupie Mzigo huo.

Kwani sasa hivi Mzee hapa Duniani unatumia Mamilioni ya Shilingi kwa ajili ya Kumpatia Mtoto wako ili awe Daktari, au Injinia, au Pilot n.k na hivyo hujali kuhusiana na Ilm ya Dini yake kwani unajali kuhusiana na Dunia yake tu.

Basi fahamu kua Unayomtafutia ni Mapambo tu ya Dunia na wakati yeye mwenyewe kwako wewe amekua ni pambo la Dunia yako na kisha wewe unamchanganya kwenye mapambo zaid kisha

matokeo yake itakua maharibiko matupu, Yaani inakua kama vile Mwanamke alieumbwa na Kujaaliwa Uzuri wa Kimaumbile Mola wake na kisha akapiga sindano Lips zake, akachonga Pua na Kidevu chake, akajitia Silicone Kifuani na Makalioni na kila kitu cha bandia alichojihisi kua kina kasoro kwa udogo wake kwenye mwili wake akapachika juu yake kutokana na kudhania kua kufanya hivyo kunamfanya awe mzuri zaidi na mwisho wake akawa anatisha kama Shaytani.

Yaani baada ya kupendeza akawa ni mwenye Kutisha. Basi hivyo ndivyo hali inavyokua pale Unapomsomesha Mtoto Ilm ya Kidunia Tu bila ya kumsimamia juu ya Ilm ya Dini yake, kwani atakuja kuchusha tu kimaisha na kitabia hapo baadae na atawachusha Wenzake na kisha atakuja kukuchusha wewe mwenyewe katika Siku ya Malipo na hivyo Utamkimbia huku nae akikufukuzia.

Sasa sijui utakimbulia mpaka wapi kwa sababu na yeye hakuachii anadima na wewe tu mpaka apate Penanti aondoke na Ushindi dhidi yako.

Naam hivyo Alhamd lillah hii ni kwa kifupi kuhusiana na Mtihani wa Mapambo ya Maisha ya Kidunia ya Mali na Watoto. Na hii ni kama itakua hukuyasimamia ipasavyo mambo mawili hayo, kwani ukisimamia ipasavyo basi bila ya shaka yatakua ni yenye kukunufaisha Duniani na Akhera kwani utakua ni mwenye kuonesha Shukran kwa aliekujaalia Neema mbili hizo.

Kwani tunaona kua Aya imemalizia kwa kutuusia kuhusiana na *Al Baqiyatu Al Salihatu*

Ambapo neno *Baqiya* hua Linamaanisha Kilichobakia, Kinachoendelea kuwepo, Kinachodumu na pia humaanisha Kitu kisichokwisha. Ambapo neno Baqiya Limetumika Mara kadhaa katika Qur'an ikiwepo pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Zakkah na Sadaqah kua:

﴿بَقِيَّةُ ٱللَّهِ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ وَمَآ أَنَا۠ عَلَيۡكُم بِحَفِيظٖ﴾

Baqiyyatu Allahi Khayrun Lakum In Kuntum Mu/miniina wa ana aAlaykum Bikhafiidhin *(Surat Hud 11:86)*

Tafsir: ***Kilichobakishwa na Allah kwa ajili yenu Ni Chenye Kheri (au ni Bora) Kwenu Kama Nyinyi Mkiwa Ni wenye Kuamini Na Wala Mimi (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Sikuwekwa juu yenu Kwa ajili ya Kukusimamieni.***

Na pia pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliposema:

﴿فَلَوۡلَا كَانَ مِنَ ٱلۡقُرُونِ مِن قَبۡلِكُمۡ أُوْلُواْ بَقِيَّةٖ يَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡفَسَادِ فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا قَلِيلٗا مِّمَّنۡ أَنجَيۡنَا مِنۡهُمۡ وَٱتَّبَعَ ٱلَّذِينَ ظَلَمُواْ مَآ أُتۡرِفُواْ فِيهِ وَكَانُواْ مُجۡرِمِينَ﴾

Falawl<u>a</u> k<u>a</u>na mina alqurooni min qablikum oloo baqiyyatin yanhawna AAani alfas<u>a</u>di fee al-ard<u>i</u> ill<u>a</u> qaleelan mimman anjayn<u>a</u> minhum waittabaAAa alla<u>dh</u>eena *<u>dh</u>*alamoo m<u>a</u> otrifoo feehi wak<u>a</u>noo mujrimeena. *(Surat Hud 11:116)*

Tafsiri: ***Na Lau kama Wangekua Miongoni mwa Jamii Ziliizotangulia Kabla yenu Ni Watu wenye Ilm na Busara Wenye Kukatazana Kuhusiana na Ufisadi Juu ya Ardhi Isipokua Kidogo Tu Miongoni mwao Tuliowaokoa kutokana nao Na (Wengineo) Wakawafuata wale ambao***

Waliojidhulumu Kuendekeza (Starehe) zilliyomo ndani yake(Duniani)Na hivyo Wakawa ni Wahalifu.

Ambapo hizi ni Aya zinatuonesha kua Neno Baqqiyah hua Linamaanisha Kitu Kulichobakia, Humaanisha Ziada ya Kitu na pia humaanisha aina ya Watu Katika Jamii Fulani ambao wao ni wenye Ubora wa Ufahamu, Akili, Hikma, Busara na Ucha Mungu. Kama ilivyoelezewa kwenye Aya ya Surat Hud ambayo inawaelezea Watu Waliochaguliwa na kuokolewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na Ukubwa wa Ilm yao na Ucha Mungu wao.

Hivyo kama ni hivyo basi *Jee Baqaiyyatu Al Salihatu* maana yake ni Nini?

Naam..Hivyo Allah Subhana wa Taala anatuambia kua *Baqaiyyatu Al Salihatu Khayrun Ain-da* Rabbika Yaani Mambo Mema Mliyoyatanguliza na yakabakia kwa Mola wenu kama Malipo ya kufanya Mema kwenu ni Bora Kiamali kwa kuyategemea, ambapo neno la Mwisho la Aya yetu hii ni *Amala* ambalo ni lenye asili ya herufi za *Alif Lam na Mim.* Na neno *Amala* hua linamaanisha Kutegemea, Kuamini na pia Kutumai.

Ambapo ndani ya Neno *Amala* basi kuna neno *Amala* Ambalo hua linamaanisha Tegemeo Bora linalotokana na Kufanywa kwa Mambo au Amali zilizo bora ndani yake. Na pia ndani yake Neno *Amala* kuna neno *Amal* ambalo humaanisha Tegemeo Silo au Bovu au Lisilofaa ambalo hua ni lenye kutokana na kufanywa kwa mambo au Amali ambazo sizo.

Kama vile alivyosema *Allah Subhanah wa Taala* alipomwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Makafiri katika aya ifuatayo:

﴿رُّبَمَا يَوَدُّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ لَوۡ كَانُواْ مُسۡلِمِينَ ۞ ذَرۡهُمۡ يَأۡكُلُواْ وَيَتَمَتَّعُواْ وَيُلۡهِهِمُ ٱلۡأَمَلُ فَسَوۡفَ يَعۡلَمُونَ﴾

Rubama yawaddu alladheena kafaroo law kanoo muslimeena; Dharhum ya/kuloo wayatamattaAAoo wayulhihimu al-amalu fasawfa yaAAlamoona *(Surat Al Hijr 15: 2-3)*

Tafsir: ***Huenda Wakatamani wale ambao Wamaekufuru Kua Bora Wangekua Waislam Hivyo Waachie Wale Na Wastarehe Na Wajibebeshe Matumaini mabovu Na Kisha Ndio watakuja kujua.***

Naam..Hivyo basi kutokana na aya zetu hizi basi tunaona kua neno *Amala* limetoa neno *Amala* ambalo hua linamaanisha Matumaini Bora yanayotokana na Ufanywaji wa Amali Njema zitakazokubalika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na likatoa neno *Amala* ambalo linamaanisha Matumaini Finyu au Sio kwani ni yenye kutokana na Ufanywaji wa Amali ambazo sizo au zisizokubalika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ama kw aupande mwengine basi tunaona kua Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na maana ya sehemu ya pili ya Aya hii ambayo ni yenye kuhusiana na *Al Baqiyat Al Salihatu.*

Kwani kwa upande Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye pamoja na Imam Said Ibn Jubayr wanasema kua: ***'Al Baqiyat Al Salihatu* iliyokusudiwa hapa hua ni yenye kumaanisha Malipo ya Amali za Sala Tano za Kila Siku.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Mujahid Ibn Sulayman na Imam At Ibn Abi Rabah basi wao wanasema kua: ***'Al Baqiyat Salihatu* zilizokusudiwa hapa basi ni *Tasbih* yaani *Subhanah Allah. Tahmid* yaani *Alhamd lillah, Tahlil* yaani *La Ilaha Illa Allah* na *Takbir* yaani *Allahu Akbar'***

Ambapo tunapoyaangalia maneno haya ambayo ni yenye kuingia kwenye *Dhikr Allah* basi tunaona kua yenye kutumika ndani ya Sala pia. Kwa hivyo tunaweza kusema kua Mitizamo hii miwili inafungamana na hii ni kwa sababu Ibada ya Sala ni yenye kujumisha ndani yake *Dua* na *Dhikr Allah*.

Ambapo Imam Al Hakim Al Tirmidhii anatuambia kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kuwaambia Masahaba zake: Iwachieni Huru Pepo**

Hivyo Masahaba wakashangaa, na kuuliza kwa kusema: *Ya Rasul Allah* kwani kuna adui gani alietokea na kuizuia?

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* akasema: 'La Bali Mnatakiwa Muiachie Huru Pepo yenu kutokana na Moto, Kwa kusema *Subhanah Allah. Wa Alhamd lillah, wa La Ilaha Illah Allah wa Allahu Akbar* Kwani Katika Siku ya Malipo Maneno haya yatakuja kua ndio yatakayokulindeni na ndio *Al Baqiyat Al Salihat.'*

Na anasema *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin* Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua: **Amesema *Mujaddid Ad Din Hujjat Ul Islami Imam Al Shafii Al Thani* Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: 'Kusema *Subhanah Allah* hua kunamaanisha kuelezea kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mkamilifu asiekua na kasoro yeyote**

Kusema Alhamd lillah kunamaanisha kuelezea kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndio Chanzo cha Kila Kilicho kizuri na kilicho bora na hivyo anastahiki kushukuriwa na kusifiwa.

Kusema *La Ilaha Illah Allah* kunamaanisha kuelezea kua Hakuna Chanzo chengine cha Kila kitu isipokua yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kusema *Allahu Akbar* hua kunamaanisha kuelezea kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mkubwa sana na haelezeki kiufahamu bali huelezeka kutokana na Dalili za Kuwepo kwake Kiukubwa.'

Hivyo *Allah Subhanah wa Taala* anatuambia kua *Al Baqiyat Al Salihat Khayrun aAinda Rabbika.Y*aani Mambo Mema Mliyoyatanguliza na yakabakia kwa Mola wenu kama Malipo ya kufanya Mema kwenu ni Bora Kiamali kwa kuyategemea.

Katika Kuifafanua Aya hii basi tunaona ni yenye kutukumbushana kua Ujumbe Muhimu kuliko yote ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametaka kutufikisha ili tupate kutafakkari na kuzingatia ni kua: '**Kama kweli sisi ni Wenye Akili na Kutafakkari basi tunatakiwa kujitahid kukimbilia Mapambo yanayotokana na Amali zenye Malipo ya Kiakhera ambayo ndio ya Kudumu Hivyo tunatakiwa Tujipambe kwa kushindana kufanya Amali njema zaid ambazo hazitoharibika kutokana na kufanywa kwa Ikhlasi.**

Na wala tusiwe ni wenye kujali kuhusiana na Mapambo ya Kidunia na kujisifu kutokana na Kua na ali nyingi au Watoto wengi, na wale tusioneane choyo kwa Mali wala kwa Watoto wengi au Tusishindane kwa na Watoto. Kwani Ingawa tunaona kua Mali hua ni yenye kutuhakikishia Maisha Mazuri Duniani, na Watoto ni wenye kutuhakikishia kuendelea kuwepo kwa Vizazi vyetu.

Lakini Kukimbilia kufanya mema hua ni Kujihakikishia maisha bora ya Kidunia na Kiakhera pia Na hii ni kwa Sababu ya kua kama Amali Njema zikifanywa kwa Ikhlasi yaani si kwa ajili ya mwengine yeyote Isipokua kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi kila amali husika itakayofanywa kwa njia hio hua ni *Al Baqiyat Al Salihat* ambayo ndio itakayotufaa kesho Akhera.

Hivyo mtu unaweza ukawa na Mali nyingi na watoto wengi lakini ukawa ni mwenye kukosa Radhi za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kukosa Amali njema zilizo bora ambazo unaweza kuzitegemea na matokeo yake ukaangamia..Allah atunusuru na hilo..Amiin.

Baada ya kutukumbusha juu ya hayo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kusema katika Aya inayofuatia ni aya amabyoimetumia Neno Baraza ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kutokeza, Kuchomoza, Kuenda Mbele, Kuongoza, Kuonekana baada ya Kutoweka na pia humaanisha Kudhihirika. Na neno Baraza ndio lililotoa neno Barizatun ambalo hua linamaanisha Kutokea.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatukumbusha kuhusiana na Siku ya Malipo kwa kusema katika aya iliyotumia Neno *Barizatun* kua:

﴿وَيَوْمَ نُسَيِّرُ ٱلْجِبَالَ وَتَرَى ٱلأَرْضَ بَارِزَةً وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَداً﴾

Wayawma nusayyiru aljibala watara al-ardha barizatan wahasharnahum falam nughadir minhum ahadan *(Surat Al Kahf 18:47)*

Tafsir: ***Na Katika Siku Tutakapoifanya Itoweke Milima Na Kisha Mtaiona Ardhi Imetandazwa na kuonekana kama sehemu iliyokaa sawa na kutokeza kwa mbele zaidi Na Kisha Tutawakusanya Na Kutomuacha Nyuma Miongoni mwao Hata Mmoja.***

Subhanah Allah! Ama hapa kulingana na haya maneno na uhalisia ulivyo basi inabidi kila mmoja wetu awe ni mwenye kulihisi tukio hili ndani ya Moyo na Nafsi yake. Hivyo kama hujalihisi basi inabidi ujiulize, hivii Jee kweli mimi nnazo hisia za Kimaumbile za Kiibn Adama ama la?

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuelezea kua Siku hio Majabali au Milima itatoweka kama vile alivyoelezea katika Katika *Surat Ta-Ha* pale aliposema:

﴿وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ ٱلْجِبَالِ فَقُلْ يَنسِفُهَا رَبِّي نَسْفاً ❁ فَيَذَرُهَا قَاعاً صَفْصَفاً ❁ لاَّ تَرَىٰ فِيهَا عِوَجاً وَلآ أَمْتاً﴾

Wayas-aloonaka AAani aljibali faqul yansifuha rabbee nasfan; Fayadharuha qaAAan safsafan; La tara feeha AAiwajan wala amtan*(Surat Ta-Ha 20:105-107)*

Tafsir: ***Na Wanakuuliza Kuhusiana na Majabali/Milima Hivyo Waambie Atayapeperusha Mola wangu katika hali ya Mpeperusho wa Vumbi Na Ataidhihirisha Kua Kama Tambarare iliyotandikwa na kutulia Na Wala Hamatoona Ndani yake Mnyanyuko Wala Bonde.***

Kwani Aya zinatuelezea kua Mbali ya Ukubwa wake Majabali ambayo Leo hii Watu wanayachimba kwa Mashine Zenye Nguvu kubwa sana na kisha Kufanya Mashimo ndani yake kama wafanyavyo Panya Buku ardhini. Na kisha Wakawa ni wenye Kupitisha Barabara ndani yake na zikapita Gari, Malori na Treni na huku Majabali hio ikiwa haina habari wala kuhisi wala kuanguka au kumomonyoka kutokana na Ugumu wake. Ambapo Milima hio ndio Pingili zinazoifanya Ardhi Itulie kama zinavyosema aya kua:

﴿وَجَعَلْنَا فِي ٱلْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَن تَمِيدَ بِهِمْ وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجاً سُبُلاً لَّعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ﴾

WajaAAaln<u>a</u> fee al-ar<u>dh</u>i raw<u>a</u>siya an tameeda bihim wajaAAaln<u>a</u> feeh<u>a</u> fij<u>a</u>jan subulan laAAallahum yahtadoona *(Surat Al A nbiyah 21:31)*

Tafsir: ***Na Tukajaalia Kwenye Ardhi Milima Madhubuti Ili Kuizuia Isitetemeke pamoja nayo Na kisha tukajaalia ndaniyake Njia kubwa za kupitia ili wakapate muongozo.***

Hivyo mbali ya Ukubwa wake na Uzito wake na Ugumu wake na Kazi yake ya Kimaumbile Majabali kua ni Kuizuia Ardhi isicheze, na hii ni kutokana na kua Mlima hua ni wenye Kuzama kuenda Chini ya Ardhi kwa umbali wa mara mbili ya namna ulivyotokeza Juu ya Ardhi na hivyo kuipa umadhubuti Ardhi, lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaielezea Milima kua katika siku hio itakua ni Nusayyiru.

Naam..hapa inabidi tutafakkari tena vizuri zaidi kwani Neno Nusayyiru linatokana na neno Sara yaani Kutembea, Kua katika Mwendo, Kua Safarini, Kua katika hali ya kutoka katika sehemu moja kuelekea kwenye sehemu Nyengine. Ambapo neno Sara ndio lililotoa neno Sayara yaani Gari.

Sasa tunaporudi kwenye Neno Nusayyiru basi tunaona kua Aya inatufahamisha kua Mwendo wa Milima hio utakua si kama wa Mlima bali ni wa kama kitu ambacho ni Chepesi sana kinachoenda kwa kasi kubwa.

Na hivyo basi kutudhihirishia kua Milima hio itakua kama tunavyoona Vumbi namna unavyokuja Upepo na kisha Ukalipeperusha ambapo kufumba na kufumbua likatoweka lote.

Na hivyo Ardhi ikawa ni yenye kuonekana tambarare kama baraza iliyotokeza nje ya Nyumba kwa sababu hakuna Milima wala mabonde hivyo Kitu kimenyooka yaani katika Siku hio itakua hakuna sehemu ya Kujifichia, kwani Ardhi itakua Barizatan - Tambarare haina bonde wa mnyanyuko wa kujifichia Nyuma yake.

Na kisha Ibn Adam na Majini watawekwa na Kupangwa kwa Safu huku wakiwa hawana Mali, wala Nguo wala Viatu kama anavyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Aya inayoendelea baada ya hii kwa kusema:

﴿ وَعُرِضُواْ عَلَىٰ رَبِّكَ صَفّاً لَّقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ بَلْ زَعَمْتُمْ أَن لَّن نَّجْعَلَ لَكُمْ مَّوْعِداً ﴾

WaAAuri<u>d</u>oo AAal<u>a</u> rabbika <u>s</u>affan laqad ji/tumoon<u>a</u> kam<u>a</u> khalaqn<u>a</u>kum awwala marratin bal zaAAamtum allan najAAala lakum mawAAid<u>a</u>n*(Surat Al Kahf 18:48)***

*Tafsir**: Na Watakusanywa Mbele ya Mola wako Katika Safu (Na Wataambiwa)Kwa Hakika Mmerudi kwetu Kama Tulivyokuumbeni Kama Tulivyokuumbeni mara ya Kwanza, wakati Nyinyi Mlifikiria Kua Hatutojaalia Sisi Kukutana nanyi.***

Hivyo hii ni ahadi ya kua tutarudi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama tulivyokuja hapo awali Ulimwenguni, yaani Bila ya Kitu chochote hata nguo zetu kwani vyote hivyo havina thamani katika siku hio, chenye thamani ni kile Ulichokitanguliza hapo kabla. Na kama hukitanguliza basi maana yake kua ulikua ukidhania kua haitotokea siku ambayo utakuja kukutana na Mola wako. Ambapo haya yanafafanuliwa zaid na ile aya isemayo:

﴿وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فُرَادَىٰ كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَتَرَكْتُمْ مَّا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ شُفَعَآءَكُمُ ٱلَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَآءُ لَقَد تَّقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنكُم مَّا كُنتُمْ تَزْعُمُونَ﴾

Walaqad ji/tumoon<u>a</u> fur<u>a</u>d<u>a</u> kam<u>a</u> khalaqn<u>a</u>kum awwala marratin wataraktum m<u>a</u> khawwaln<u>a</u>kum war<u>a</u>a *<u>dh</u>*uhoorikum wam<u>a</u> nar<u>a</u> maAAakum shufaAA<u>a</u>akumu all<u>adh</u>eena zaAAamtum annahum feekum shurak<u>a</u>o laqad taqa<u>tt</u>aAAa baynakum w<u>adh</u>alla AAankum m<u>a</u> kuntum tazAAumoona*(*Surat Al Anaam 6:94)*

*Tafsir: **Na Kwa Hakika Mmerudi Kwetu Watupu Peke Yenu Kama tulivyokuumbeni Kwa Mara ya Kwanza Na Mmeachana navyo Vile Tulivyokupeni (Kwa kuneemesheni Miongoni mwa Neema zetu Duniani) na tunaona kuhudhuria kwenu kumekua bila ya kua na Pamoja nanyi wale wale waombezi wenu ambao mlikua mkiwachukulia kua ni washirika wenu, kwa hakika umevunjwa uhusiano baina yenu na wao na kila mlichokua mikijidai nacho kimetoweka.***

Ambapo anasema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu kua: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mtafufuliwa Mkiwa Miguu Chini, Hamna Nguo na wala Hamjatahiriwa.'**

N anasema Imam Muslim Ibn Hajjaj kua: **Amesema Abdullah Ibn Ashshkhir *Radhi Allahu Anhu* kua Mimi nilienda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Na nikamkuta akiwa anasoma Surat Al At Takathur na kisha akasema: Ibn Adam hua ni mwenye kusema Mali yangu! Mali Yangu! Hivyo Jee Enyi Ibn Adam mnamiliki nini Nyinyi katika Utajiri wenu zaid ya Kile ambacho tayari mmeshakitumia, au kile ambacho mmeshakila, au kile ambacho mmeshakichakaza? Au kila ambacho mmekitolea Sadakah? Hivyo jee mna kitu chochote kilichobakia?.'**

Na amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Aliuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema kua: 'Hivi Jee ni nani mwenye kuhesabu kua Mali ya Wairith wake ni bora kuliko mali yake?' Masahaba wakajibu: 'Ya Rasul Allah, hakuna hata moja miongoni mwetu isipokua ni mwenye kupenda Mali yake zaidi' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Mali ya kila mmoja wenu miongoni mwenu hua ni ile ambayo ameitumia vyema katika Maisha yake, na mali ya Warithi wake ni ile aliyoibakisha baad ay kufariki kwake'*(Sahih Bukhari)'***

Naam..kwani Hadith hizi zinatukumbusha kua kwetu sisi Ibn Adam kilicho chini ya Umiliki wetu ni kile tu ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametujaalia kua navyo kama miongoni mwa neema zake juu yetu tena kile tulichokitumia kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu ndio kitakachotufaa katika siku ya Malipo.

Hivyo vyengine vyote ambavyo tumetumia kwa njia sio basi havina maana na vitakua ni mtihani juu yetu.

Kwani amesema Abu Umamah *Radhi Allahu Anhu* kua: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Enyi Watu kama ikiwa Mtatumia kutokana na kile kilichocha ziada kwenu basi hio itakua ndio kheri yenu Lakini kama mkikizuia basi hio itakua ni shari kwenu**(Imam Muslim)

Ambapo kutokana na kua ni mwenye kutupenda kwake basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndio maana akatutaka kua tuwe ni wenye kujali kile tunachokitanguliza katika siku ya malipo kwa kutuhimiza kutoa Sadaka na Zakkah na kutuombea dua kwa kusema: '**Ya Allah Mlipe Fidia yule anaetoa kwa ajili yako, na Ya Allah Muangamize Yule Mtu Mbakhili mwenye kuzuia kutoa'**(Imam Bukhari)

Kwani aya yetu hii ya 48 ya Surat Al Kahf baada ya Kutuarifu sote kua tutafufuliwa bila ya kua na kitu chochote isipokua Amali zetu basi inamalizia kwa kusema kua Makafiri watahojiwa kwa kuambiwa kua: **Nyinyi Mlikua si wenye kuamini juu ya haya ya leo kufufuliwa, na mkamshirikisha *Allah Subhabah wa Ta'ala* na Miungu wengine, hivyo mbona mmekuja bila ya Miungu hio? Jee atakuombeeni nani leo hii?'**

Bada ya ayah io basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuelezea kwa kusema kua:

﴿وَوُضِعَ ٱلْكِتَابُ فَتَرَى ٱلْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يٰوَيْلَتَنَا مَا لِهٰذَا ٱلْكِتَابِ لاَ يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلاَ كَبِيرَةً إِلاَّ أَحْصَاهَا وَوَجَدُواْ مَا عَمِلُواْ حَاضِراً وَلاَ يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَداً﴾

Wawu<u>dh</u>iAAa alkit<u>a</u>bu fatar<u>a</u> almujrimeena mushfiqeena mimm<u>a</u> feehi wayaqooloona y<u>a</u> waylatan<u>a</u> m<u>a</u> lih<u>atha</u> alkit<u>a</u>bi l<u>a</u> yugh<u>a</u>diru <u>s</u>agheeratan wal<u>a</u> kabeeratan ill<u>a</u> a<u>hsa</u>h<u>a</u> wawajadoo m<u>a</u> AAamiloo <u>hadh</u>iran wal<u>a</u> ya*<u>*dh*</u>*<u>lim</u>u rabbuka a<u>h</u>ad<u>a</u>n *(Surat Al kahf 19:49)*

*Tafsir**: Na Kitawekwa Kitabu Na Utawaona Wahalifu (Wenye Makosa ya Kumuasi Allah Subhanah wa Ta'ala) Wakiwa wamejawa na Khofu Kuhusiana na kilochomo ndani yake Na Watasema Ole wetu Ni Kitabu Gani hiki Ambacho Hakijawacha Mambo Madogo ndani yake Wala Mambo Makubwa ndani yake Iisipokua Kimeainisha kiidadi ndani yake Na Watakuta Kila Walichokifanya Kikiwa Mbele yao Hadharani Na Wala Hamdhulumu Mola wako Hata Mmoja.***

Naam...bila ya shaka hii ni aya ambayo ndani yake ina maneno ambayo anaambiwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana yale yatakayotokea katika siku ya Malipo : Na hali watakayokua nayo wale wenye kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua Wakishapewa Vitabu vyao vya Amali zao na wakishavifungua kuangalia yaliyomo ndani yake basi Watasema kwa Mshangao Mkubwa sana wenye kupelekea kutaka kuvilaani vitabu vyao kutokana na Maovu yao yaliyoainishwa ndani yake ambayo waliyafanya hapo kabla walipokua Duniani.

Hivyo watauliza Ni Kitabu gani hiki ambacho hakijaacha hata chembe ya yale tuliyokua tukiyafanya tulipokua Duniani..yaani kimeainisha Kila kitu basi mpaka haya madogo madogo pia? Lo! Ole wetu.

Kwani ingawa kwa uoande mmoja hii ndivyo itakavyokua hali ya wasioamini, lakini kwa upande mwengine basi hali hii pia itakua kwangu mimi na wewe ambao ni wenye kumuamini *Allah*

Subhanah wa Ta'ala. Kwani tutakuja Kujuta na kujiuliza hivi kwanini mpaka mimi mpaka huu mtizamo wa Jicho ambao niliambiwa kua niuinamishe hususan katika mwezi wa Ramadhani basi nikawa sikuinamisha kutokana na kudhania kua ni kitu kidogo sana?

Ole wangu mimi leo hii kwani hadi Mtizamo wa Jicho umeandikwa ndani ya Kitabu na kuniongezea Dhambi zangu..

Hivyo aya zinatuonesha kua kua mbali ya kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye Uwezo wa kuwaadhibu watu hao kutokana na kujua kwake kila kitu chao kwani yeye ni mwenye Sifa Tukufu ya Kujua kula kitu ndani nje.

Na kwa kutokana na kua na Sifa hio basi ya *Al Aalimun* yaani Mwenye kujua juu ya kila kitu basi ndio maana pia akawa na Sifa ya Al Hakim ambayo ni sifa ya Kuana wingi wa Hikma.

Na kutokana na kua ni mwenye wingi wa Hikma basi ndio maana akaamua kua katika siku atampa kila mtu kitabu chake mkononi ili aweze kujithibitishia kwa ushahidi kua kweli mimi nilifanya hili na hili na hili na hivyo leo hii nastahiki hiki kitakachonifika.

Yaani kama ni Adhabu basi Mtu akikisoma kitabu chake mwenyewe tu kabla ya hata viungo vyake kutoa Ushahidi basi mtu huyo atajua kua leo hapa kazi ipo tena sio ndogo.

Kwani anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Jariri At Tabari kua **Amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: Ndani yake vitabu hivyo kuna vitu ambavyo tumaviona ni vidogo na visivyokua na maana, lakini ukweli ni kua vitakuwemo kwani hata kitendo cha kucheka basi kitakuwemo ndani yake.'**

Hivi mara ngapi sisi mimi na wewe leo hii tunaona watu wanafanya mambo sio halafu tunacheka?

Hivi Jee ni mara ngapi Watu wanawatania wengine kwa kasoro zao kisha Watu tunacheka?

Hivi Jee ni Mara ngapi unakuta Vijana wanakaa kisha anapita Mzee kisha wanamjambishia, halafu wengie wanacheka?

Hivyo hayo ni baadhi tu ya mambo ambayo tutakuja kuyakuta kwenye vitabu vyetu halafu tutakuja kujuta kwa kusema hivi kwanini mimi nikacheka wakati pale fulani alipokua akimfanyia Dhihaka mwenzake na kumuudhi mwenzake huyo?

Na ndio maana akasema tena *Bahr ul Im* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: **Linahesabiwa hadi Tabasamu linalotokana na Kufanyiwa Dhihaka kwa mwislam mwenzako ambalo hili hua linahesabiwa ni dogo lakini pia ndani yake kuna Kicheko unachokitoa baada ya kudhihakiwa kwa Muislam mwezako.**

Naam..haya ni baadhi makosa madogo ambayo sisi leo tunayachukulia kua ni mambo ya kawaida haya uzito wowote. Na tunayafanya pia katika Mwezi wa Ramadhani bila ya kujua kua tunajipunguzia Malipo na Darja za kila Ibada zetu. *Na Allah Subhanah wa Ta'ala* anailezea hali hii katika sehemu nyengine kwa kusema:

﴿ وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ فَيَقُولُ يٰلَيْتَنِي لَمْ أُوتَ كِتَابِيَهْ ۞ وَلَمْ أَدْرِ مَا حِسَابِيَهْ ﴾

Waamma man ootiya kitabahu bishimalihi fayaqoolu ya laytanee lam oota kitabiyah; Walam adri ma hisabiyah. *(Surat Al Haqqa 69:25-26)*

Tafsir: **Na Ama kwa Yule Atakaepewa Kitabu chake Kwa Mkono wake wa Kushoto Basi Atasema: 'Looo Ole wangu Mimi Bora hata nisingepewa Kitabu Changu Na Hivyo ningekua Sijui Ipi Hisabu yangu'**

Hivyo baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuelezea yatakayowakuta wale watakaokua ni wenye kufanya Maovu. Basi anatutanabaisha tena upya kama alivyofanya hapo kabla katika sehemu kadhaa ndani ya Qur'an kihusiana na ni nani adui yetu mkuu Ibn Adam kwa kutuambia kua:

﴿وَإِذَا قُلْنَا لِلْمَلآئِكَةِ ٱسْجُدُواْ لِآدَمَ فَسَجَدُوٓاْ إِلاَّ إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ ٱلْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ
أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَآءَ مِن دُونِى وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلاً﴾

Wa-idh qulna lilmala-ikati osjudoo li-adama fasajadoo illa ibleesa kana mina aljinni fafasaqa AAan amri rabbihi afatattakhidhoonahu wadhurriyyatahu awliyaa min doonee wahum lakum AAaduwwun bi/sa lildhdhalimeena badalan *(Surat Al Kajf 18:50)*

Tafsir: ***Na (Kumbuka ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam pale) Tulipowaambia Malaika Msujudieni Adam Hivyo Wakasjudu Isipokua Ibilisi Kwani alikua ni Miongoni mwa Majini Hivyo Akafaya Uasi juu ya Amri ya Mola wake Hivyo Jee Nyinyi Mtamchukulia yeye (Ibilis) Na Kizazi chake Kua Ni Wasaidizi wenu? Kuliko Mimi (Ambae ndie Mola wenu?) Wakati yeye (Ibilisi) kwenu nyie ni Adui Yenu! (Huo) Ni Udhalimu mkubwa sana Badala yake***

Naam..tumesema kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema mara kadhaa kuhusiana na uhusiano wa Ibilisi kimaumbile dhidi ya Ibn Adam ambapo haya ameyasema katika Aya Kadhaa ikwemo katika Surat Al Baqara aya ya 34, Surat Al Araf aya ya 11 na 12 na katika aya ya 61 na 62 katika Surat Bani Israil ambayo inajulikana pia kama Surat Al Israa.

Na hivyo kwa kukumbushana tena kwa waliosahau basi amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Malaika wameumbwa kwa Nuru na Ibilisi ameumbwa kwa Moto na Ibn Adam ameumbwa kwa kile mlichoelzewa Yaani Ibn Adam ameumbwa kwa Udogo wa mfinyanzi.**

Kwani Ibilis alikua akiiishi pamoja na Malaika Mbinguni, na hivyo alikua ni kiumbe ambae ni Mcha Mungu sana kiasi ya kua alikua ni mwenye kuwafikia Malaika kwa Ucha Mungu wake.
Na hivyo nae akawa anajumuishwa pamoja na Malaika katika Majukumu, kutokana na kufanana nao katika Ibada.

Na ndio maana alipoumbwa Nabii Adam na Malaika wakaambiwa wamsujudie Adam basi amrisho hili nalo likamujumuisha nae Ibilisi ndani yake, ambapo hata hivyo nae hakutekeleza Amrisho hilo kwa Kiburi chake na kujiona kwanza kua yeye si Malaika bali ni Jini na pili kua yeye ni bora kuliko Adam.

Kwani Miongoni mwa Maimamu wenye Ilm na Wlaiokua na Majibu ya Mkato alikuwemo yule aiwate Imam Abd Rahman Al Shaabi. Ambapo siku moja katika kusomesha kwake basi aliulizwa na Mwanafunzi wake: '**Ya Imam Hivi Ibilisi ana Mke?'**

Ambapo Imam Abd Rahman Al Shaabi akajibu: '**Kusema kweli hasa mimi sikuwahi kuhudhuria Harusi yake.'**

Naam..huyo ndio Imam Al Shaabi na Majibu yake, ila sasa mara tu baada ya kutoa jibu hilo basi akakumbuka aya ya 50 ya Surat Al Kahf hivyo baada ya Imam Al Shaabi kukumbuka aya hii basi akajiuliza itakuaje Ibilisi awe na kizazi kama hana mke? Hivyo hapo hapo akamjibu mwanafunzi wake huyo kwa kumwambia: **'Naam..bila ya shaka Ibilisi anae mke wake.'**

Kwani kama tulivyosema kua Ibilisi alikua ni kiumbe Mcha Mungu sana kiasi ya kua alikua akifananishwa na Malaika kwa Ucha Mungu, na alikua anachukia sana wanaomuasi Allah Subhanah wa Ta'ala kiasi ya kua siku moja katika kupita kwake katika maeneo ya Mbiguni Peponi.

Basi aliona Maandishi yesemayo kua: '**Iko siku Mmoja miongoni mwa wakaazi wa Mbinguni Peponi atamuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala***' hivyo baada ya Ibilisi kuona Tangazo hilo limejitokeza Mbinguni basi akamuomba Allah Subhanah wa Ta'ala amuwezeshe kumjua Kiumbe huyo ili amshughulikie kabla hajaasi. Allah Subhanah wa Ta'ala akamwambia kua awe na Subra kwani atamjua tu karibuni.

Naam..Ibilisi akawa na Subira akimsubiri huyo atakaemuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* Mbinguni, kwani hata Malaika wenyewe walikua hawamjui ni nani atakaeasi miongoni mwao. Na wao Malaika walikua wakimheshimu sana Ibilisi kutokana na Ucha Mungu wake.
Ambapo baada ya kuumbwa kwa Adam na kisha Malaika kupewa Amri ya Kumsujudia na kisha Ibilisi akagoma kumsujudia basi ndi ikadhihirika kua Kiumbe ambae alitangaziwa kua ataasi si kiumbe mwengine yeyote yule isipokua Ibilisi.

Na hali hii ilitokea bila ya yeye mwenyewe kujijua kwani alikua tayari kumuadhibu muasi huyo bila ya kujua kua kama wa kuadhibiwa basi Atakua ni yeye tu.

Na baada ya kudhihirika kua Muasi alietangaziwa hapo kabla aliku ni Ibilisi basi Malaika walishtuka na kushangazwa kwani wao hawakuweza kudhania wala kufikiria kua Kiumbe anaejitahidi kufikia Ubora wa Juu kama Ibilisi basi huenda akaanguka Chini kwenye kina kirefu sana cha Maangamizi.

Hivyo Malaika Jibril alilia sana yalipotokea haya na kumwambia *Allah Subhanah wa Ta'ala*: **Ya Allah hakika sisi ni Viumbe dhaifu Kiasi ya kua hatuwezi kukabiliana na Mitihani utakayotupa, hivyo nna khofu usije nasi ukatupa mitihani kisha tukafeli**

Naam..bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni muweza juu ya kila kitu na ndio maana akasema Imam Hasan Al Basr kua: '**Ewe Ibn Adam usijione na kuridhika kwa Ucha Mungu wako, kwani Hata Ibilisi alikua Mcha Mungu Sana lakini mwisho wake akawa ni mwenye kuangamia.'** Ya Allah tupe Khatma njema..Aamiin

Ambapo mbali ya kua *Allah Subhanah wa Taala* amekua ni mwenye kutuonya Ibn Adam kuhusiana na Uadui wa kimaumbile baina yetu na Ibilisi lakini kutokana na kua Nafsi za Ibn Adam ni zenye kupenda kuendekeza Matamanio yake basi wengi sana tena kwa asilimia kubwa miongoni mwa Ibn Adam tumejikuta kua tuko katika Mtihani mkubwa wa kupigana dhidi ya Matamanio ya Nafsi zetu

Kwani ingawa Kimaumbile Nafsi hua ni yenye kumjua Muumbaji wake na kuchukua dhamana ya kumtii na kufuata maamrisho yake tena kwa makubaliano maalum ambayo yanajulikana kama

Mithaqan Ghalidha yaani Makubaliano ya Ahadi nzito sana lakini hapo hapo bado Ibn Adam tumekua ni wenye kuvutiwa zaid na Ulaghai na hadaa za Ibilisi dhidi yetu.

Na kutokana na kutupenda kwake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndio amekua ni mwenye kutufadhili dursa maalum za kujaribu kujirekebisha ikiwemo kufanya Istighfar yaani kuomba msamaha na pia kutujaalia kipindi kama hiki cha mwezi wa Ramadhan ili tuweze kujiokoa kutokana na mashakil ya Dunia na mazonge ya Ibilis. Ambapo hata hivyo bado unakuta watu wanautumia mda wao sivyo hususan katika wakati kama huo wa kuchuma ambao tumefadhiliwa ili kua na Taqwa au Ucha Mungu.

Na tunapozungumzia kuhusiana na Taqwa basi hua tunazungumzia ile hali ambayo Imam Hasan Al Basr aliielezea kwa kusema: **'Taqwa ni Kujitenga kutokana na kila kile ambacho kimekatazwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kutekeleza kile ambacho kimeamrishwa na Allah kua kitekelezwe.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Qatadah Al Sadusi basi yeye anasema kua: '**Haiwezekani kwa Mtu kua na Taqwa hadi pale atakapoachana na Kile Cha Halali yake kutokana na kuogopa kuangukia kwenye kile kilicho Haram.'**

Nadhani hapa kuna baadhi watakua hawajafaham, hivyo tunarudi kwenye mfano wa Imam Sufyan Ath Thawry ambae siku moja aliingia kwa Rafiki yake ambae ni Sonara na baada ya kusalimiana nae na kukaa kitako, basi Imam Sufyan Ath Thawry akaangusha Dinari ya Dhahabu ambayo ni yake mwenyewe na ni yenye kutokana na kichumo chake chae halali.

Hivyo Imam Sufyan Ath Thawry akainama na kutaka kuiokota Dinari hio lakini alipoinama basi akaona kua hapo chini kua Dinari mbili za Dhahabu. Baada ya kuona hivyo basi Imam Sufyan Ath Thawry akanyanyuka bila ya kuokota Dinari yake hio.

Na alipoulizwa kwanini hakuiokota basi alisema kua: **'Hapa Chini kuna Dinari 2 na siijui yangu ni ipi hivyo naogopa kuokota Dinari ambayo si yangu na kisha ikawa nimekula haram.'**

Naam..hayo ndio maana ya maneno ya Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua: '**Haiwezekani kwa Mtu kua na Taqwa hadi pale atakapoachana na Kile Cha Halali yake kutokana na kuogopa kuangukia kwenye kile kilicho Haram.'**

Kwani baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutuonya kuhusiana na Ibilisi basi aya za Surat Al Kahf zinaendelea kutuambia kua:

﴿ مَّآ أَشْهَدتُّهُمْ خَلْقَ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ وَلاَ خَلْقَ أَنْفُسِهِمْ وَمَا كُنتُ مُتَّخِذَ ٱلْمُضِلِّينَ عَضُداً ﴾

Ma ashhadtuhum khalqa alssamawati waal-ardhi wala khalqa anfusihim wama kuntu muttakhidha almudilleena AAadudan*(Surat Al Kahf 18:51)*

Tafsir: Sikuwashuhudisha (Ibilisi na Kizazi chake) Katika Uumbaji wa Mbingu Na Wa Ardhi Na Wala Katika Uumbaji Wa Nafsi zao Na Wala Sikuwa Mwenye Kuchukua Wapotovu Kua ni Wasaidizi

Na katika aya hii basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatubainishia kua kwa hakika yeye kutokana na uwezo wake basi hakuwahi kua ni mwenye kuwashuhudisha yaani kwa kutaka wawepo Ibilisi na Kizazi chake Pale alipokua akitaka kuiumba Mbingu na Ardhi.

Na wala alipowaumba hakua ni mwenye kutaka wala kuhitaji ushauri wao labda na hii ni kutokana kua yeye si mwenye kua na sifa ya kuhitaji kitu chochote kwani ni mwenye sifa ya Al Ghanniyu yaani mwenye Utajiri na uwezo wa kujitosheleza kikamilifu na pia anao uwezo wa kuwatosheleza viumbe wake wote bila ya kupungukiwa kwa uwezo huo na bila ya kuhitaji msaada wowote.

Hivyo kwetu sisi Ibn Adam tunatakiwa tujue kua haaina maana ya kumfanya Ibilisi kua ni Msaidizi wetu au rafiki yetu kwani yeye mwenyewe ni kama sisi yaani ameumbwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala na* hivyo kumhitajia Ibilisi na kumfanya kua ni rafiki ni jambo la kijinga sana na ni la kujidhulumu.

Kwani kwetu sisi wa kumtegemea ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* peke yake. Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* pia ni mwenye sifa ya kua ni Mwenye kuwasimamia kikamilifu viumbe wake na hivyo kwa wale wanaomtii basi huwafanya kua ni wenye ukaribu nae zaid kwa kuwapenda na kuwahudumia zaid kwa kila wakitakacho.

Na kutokana na kua ni kua na sifa hio basi kwake yeye hua pia Si mwenye kua na ukaribu na wale wanaomuasi akiwemo Ibilisi ambao yuko katika mstari wa mbele katika kuwapotosha Ibn Adam kutokana na njia ya kumfikia *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuupata uokovu wake ambayo ni njia iliyonyooka.

Hivyo basi haiwezekani kwake yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua na Ukaribu na Ibilisi kwa sababu yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwenyewe Kamwe hakua ni mwenye kumkaribisha karibu nae tangu pale alipoamua kua ni muasi. Na kwa maana hio ni Ujinga pia kwa Ibn Adam kua ni wenye kutaka kuusogeza karibu uhusiano wa baina ya Ibilisi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* hawezi kua na ukaribu na wale wanaowapotosha viumbe wake.

Ambapo Aya zinaendelea kututaarifu kuhusiana na siku ya Malipo ambapo wale waliokua wakimshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* watakua na hali inayoelezewa kwa kusema:

﴿وَيَوْمَ يَقُولُ نَادُواْ شُرَكَآئِيَ ٱلَّذِينَ زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُواْ لَهُمْ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُم مَّوْبِقاً ﴾

Wayawma yaqoolu nadoo shuraka-iya alladheena zaAAamtum fadaAAawhum falam yastajeeboo lahum wajaAAalna baynahum mawbiqan *(Surat Al Kahf 18:52)*

Tafsir: ***Na (Kumbuka Ewe Muhammad) Katika Siku ambayo Atakaposema (Allah Subhanah wa Ta'ala) Waiteni Washirika wenu Mliokua mkinishirikisha nao Hivyo Nao (watu hao) Watawaita (Miungu wao hao) Lakini nao (Miungu wao hao) Hawatowajibu wao (Watu hao) Na Tutajaalia Baina yao Maangamizo.***

Aya imetumia neno Mawbiqan linatokana na neno Wabaqa ambalo humaanisha Maangamizo Na hivyo neno *Mawbiqah* hua linamaanisha Sehemu ya Maangamizo, Ghuba ya Maanganizo. Bonde la Maangamizo. Ambapo kwa upande wa Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* amesema kua Mawbiqa ni **'Bonde katika Mabonde ya Motoni'**

Na kwa upande wa Imam Iqrimah basi yeye amesema kua: **‘Mawbiqa ni mto wa Moto ambao ni wenye kutiririka Pembeni ya Moto wa Jahannam Ambapo ndani yake Mto huo Mna Nyoka ukubwa wake ni kama Punda ambao ni wenye rangi nyeusi’**. Allah atunusuru na Moto huo..amiin.

Hivyo basi aya i atudhihirishia kua kila Mtu ambae ni mwenye sifa ya kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala na* Mungu mwengine amjuae yeye ambae hata hivyo si Mungu kwani Mungu ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu Basi katika siku ya malipo ataambiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua Muite yule Mungu wako ambae ulikua ukimshirikisha nami. Hivyo hapo watu hao watawaita Miungu wao hao, yaani wanaoabudu Masanam watawaita Masanam hayo kwa majina yao. Wnaoabudu Wanyama watawaita Wanyama hao, Wanaoabudu Moto watauita Moto huo. nk

Lakini hata hivyo Miungu hio haitoikitikia na hii ni kwa sababu wao si Miungu, kwani Mungu mwenyewe *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie atakaekua ni mwenye Kudhihirisha Uungu wake kwa wale wasiomkubali na hivyo kuonesha kua anastahiki kuitwa Mungu na watu hai ndio watajua kua kumbe kweli *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee na ndie aliekua anaestahiki kuabudiwa.

Lakini sasa tatizo ni kua wakati wanagundua uhalisia wa jambo hilo basi wameshachelewa tena sana.

Na ndio maana akasema Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali kua: **‘Uhai wa Duniani nia Ndoto ya Usingizini, ambapo kuamka kwake ni pale unapoingia Kaburini’**

Na hivyo washirikina hao hawatoweza tena kuepuka maangamizo ya Milele yao wao na ya Miungu wao hao.

Naam..*Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuambia katika aya kua:

﴿ وَرَأَى ٱلْمُجْرِمُونَ ٱلنَّارَ فَظَنُّوٓاْ أَنَّهُمْ مُّوَاقِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُواْ عَنْهَا مَصْرِفاً ﴾

Waraa almujrimoona alnnara fa*dh*annoo annahum muwaqiAAooha walam yajidoo AAanha masrifan*(*Surat Al Kahf 18:53)*

Tafsir: ***Na Wataona Wahalifu walioasi Moto Na Watajawa na Khofu Basi Wataangukia Ndani yake Na Hawatopata Kutokana nao Njia ya kujiokolea.***

Subhanah Allah! Nadhani tuombe Dua kwanza kwa kusema: **Ya Allah hakika sisi tunashuhudia kua hakuna Mola anaestahiki Kuabudiwa kwa Haki, Isipokua wewe na tunakuomba Msamaha Na tunakuomba Pepo na Tunakuomba Utuepushe na Moto, Kwani kwa hakika wewe ni Msahmehevu, unaependa kusamehe hivyo Tunakuomba tusamehe ya Rabbi!..Allhuam Amiin**

Kwani ingawa aya inawazungumzia Wale watakaomuasi Allah Subhanah wa Ta'ala na wengi wetu hua wanadhani kua watu hao ni makafiri tu, bila kukumbuka kua sisi Waislam wa leo tuna Makosa mengi sana na Ibada zetu zina kasoro nyingi sana.

Na Ndio maana Wanazuoni waliotangulia ambao ni wenye kujua zaid basi walikua wakisema kua Sisi tunafanya Istighfar kwa sababu ya Itighfar zetu Yaani wao ambao ni wacha Mungu walioachana na Dunia yao na Dua zao zinajibiwa hapo hapo basi walikua wakifanya Istighfar kwa sababu tu ya kua Wanafanya Istighfar lakini Hizo istighfar zao zina kasoro ndani yake.

Sasa ikiwa wao walikua wanafanya Istighfae kwa sababu ya kasoro za Istighfar zao, jee mimi na wewe tusiofanya Istighfar tunatakiwa tufanye nini?

Hapa kwenye jibu la Suali hili ndio kuna Mtihani kwa sababu sisi tuko mbali sana na Wacha Mungu tena sana, yaani hata vumbi lao linathamani kuliko mimi na wewe. Hivyo cha kufanya mimi nawe ni kujitahidi kujidhibitj na kujilinda dhindi ya dhambi na kujaribu kujinufaisha kwa kadri tutakavyoweza kwa manufaa ya mwezi wa Ramadhani.

Kwani kama tunavyoona kua aya zinasema kua Watu wenye kufanya maasi basi katika siku ya Malipo Wataangukia Motoni kabla ya kuufikia huo Moto wenyewe. Yaani ile khofu tu ya kuuona Moto basi moja kwa moja inakupelekea kuangukia ndani yake Motoni.

Sasa ili hapa tufahamu vizuri zaidi aina ya khofu na ukali wa moto basi Tukumbushane ile hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoasema kua: **Katika Siku ya Malipo basi Wasioamini watauona Moto kutoka katika Umbali wa Masafa ya Umbali wa safari ya Miaka 40***(Musnad Imam Ahmad)*

Kisha hebu tufikirie Moto uko mbali kwa masafa ya Safari ya Miaka 40, yaani hio ni zaidi ya mara 40 ya Safari ya kutoka Duniani kuenda Kwenye Sayari ya Mars.

Ambapo ni Safari moja hua ni ya kilomita 300 Milioni na huchukua miezi 7. Na Sayari ya Mars hua haiwezekani kuonekana kwa macho, labda mara moja moja usiku hali inaporuhusu basi huonekana kama Nyota. Kisha weka akilini kua Moto utakua na Umbali wa Nyota mara 40 na Moto huo utakua unaonekana ukubwa wake na kutisha kwake kwa macho kabla ya hata kufikiwa.

Hivyo Moto ni Maangamizo makubwa sana kiasi ya kua hayafikiri akilini na ndio maana nikaona bora Tuombe dua tuepushwe nao kabla kuendelea.

Kwani anasema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: **‘Siku Moja Malaika Jibril alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku akiwa katika hali ya kua ni mwenye Khofu kubwa sana Hii ni hali ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuwahi kumuona nayo hapo kabla, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Malaika Jibril Jee Imekuaje?’**

Malaika Jibril akasema: ‘**Ya Rasul Allah Hakika mimi nimeona Hali ya Jahannam, ambayo hakuna hata Mmoja atakaeona hali hio isipokua Atakua ni mwenye kufanya kila njia hadi aepukane nao Moto huo’**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Malaika Jibril kua amuelezee juu ya hayo aliyoyaona.

Naam Malaika Jibril akasema: **‘Wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipouumba Moto wa Jahannam, basi aliuchochea Moto kwa miaka 1000 hadi Ukawa Mwekundu, Kisha Akauchochea kwa mda wa miaka 1000 hadi ukawa Mweupe. Na kisha Akauchochea tena kwa miaka 1000 hadi ukawa Mweusi na hio ndio hali hali uliyokua nayo leo hii Moto huo.’**

Cheche za Mkaa wa Moto huo wa Jahannam hazikai kimya, Wallahi! Kama cheche Moja tu yenye ukubwa wa Tundu ya Sindano ikichiwa hapa Ulimwenguni basi Ulimwengu wote utaungua na kutekea n akua Mkaa Kabisa.

Kama Nguo za Mtu aliekua Motoni Jahannam zitachukuliwa na kuning'inizwa Ulimwenguni baina ya Mbingu na Ardhi basi Mvuke wake tu utaangamiza kila kitu Ulimwenguni

Kama ukichukuliwa Mnyororo wa Moto wa Salaasil kama ilivyotajwa kwenye Qur'an na kuwekwa Juu ya Mlima, basi Mlima Huo wote utayeyuka na kubakia Bonde kubwa badala yake. Kama Mtu wa Mashariki mwa Dunia akipewa Adhabu ya Moto wa Jahannam basi hata Watu waliopo upande wa Magharibi mwa Dunia wataungua kutokana na Ukali wa Moto wake

Ukali wa Moto wa Jahannam ni Mkali sana na Unaunguza Hadi Ndani kwa kina kirefu, ambapo Mapambo ya Watu wa Motoni yatakua ni Minyororo ya Chuma, Kinywaji Chake kitakua ni Usaha Uchemkao na Nguo zake zitakua ni Moto

Kisha Malaika Jibril akaendelea kwa kusema kua: '**Moto wa Jahannam una milango 7, na kila Mwanamme na Mwanamke alieandikiwa kupita kwenye Milango hio basi hua na sifa zake.'**

Hapa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: **Hivi Jee Milango hio ni kama Milango ya Majumba ya Duniani au?**

Malaika Jubril akasema: **La, Kwani hio ni Milango Mikubwa sana na Mipana Sana – Kwani upana wake ni Safari ya Miaka 70 na kila mlango unau kali wa Moto zaidi ya uliotangulia kabla yake**. **Na Wenye Kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* watabururwa kwenye Milango hio na kupokewa kwa kufungwa Minyororo na Vyuma vya Shingoni na Mikononi, Wataingizwa Minyororo hio Midomoni mwao na itatokea katika sehemu zao za siri za Nyuma.**

Kwa Kila Ibn Adam atakaeingia Motoni basi atakua pamoja na Shaytani wake ambapo watabururwa wote na Malaika wa Motoni na kuwainguza Motoni, na kila wakijitahid kutoka basi hurudishwa tena ndani yake Moto huo

Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Malaika Jibril**: Hivi Jee ni Nani hao watakaoingizwa kwenye Milango hio ya Jahannam?**

Ambapo Malaika Jibril akasema**: 'Mlango wa Mwisho wa chini kabisa ni wa Munafiqiin - Wanfiq, pamoja na watu wa Fir'awn na watu wa Maidah (wa Nabii Isa) Moto uliopo hapo unaitwa Hawiyah.**

Mlango wa Darja inayofuatia juu yake ni wa Jahiim ambao ni wa Mushrikiin - Wanaomshirikisha Allah.

Ama Watu Wanaouabudu Moto watakua kwenye Mlango wa Tatu ambao ni wenye kuitwa Saqar.

Ibilisi na Wafuasi wake watakua kwenye Darja ya Nne inayoitwa Lazaa.

Mlango wa Tano ni wa Mayahudi na Unaitwa Hutama.

Wakristo watakua kwenye Mlango wa Sita kwenye Moto Uitwao Sair.'

Baada ya kuuelezea mlango wa 6 basi Malaika Jibril akakaa Kimyaa..Hajui aseme nini kwani kifuatacho ni kipigo kibaya zaidi. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Malaika

Jibril: '**Mbona Umekaa Kimyaa? Vipi Mlango wa Saba unahusiana na watu gani ewe Malaika Jibril?'**

Malaika Jibril akasema huku akiwa anamuonea Haya Mbora wa Viumbe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kumwambia: **'Mlango wa Saba ni kwa baadhi ya watu wa Ummah waki ambao ndani yake ataingia kila yule ambae atakua ni mwenye kufanya dhamnbi kubwa na kisha akawa ni mwenye kufariki bila ya kuomba masamaha kwa Mola wake.'**

Naam..hivyo Kujizoesha kufanya Istighfar kutoka Moyoni kutakupelekea kuepuka kuingia kwenye Mlango wa 7 wa Jahannam! Kwani baada ya Kusikia Maneno hayo kutoka kwa Malaika Jibril, basi Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akaanguka hapo hapo na kupoteza Fahamu.

Malaika Jibril akainama na kukaa kitako kisha akakichukua Kichwa cha *Rasul Salallahu Alayhi wa Salam* na kukiweka juu ya Mapaja yake huku akimuonea huruma. Baada ya mda kupita basi **Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam** akazindukana na kisha akauliza: **'Hivi Jee Kweli Miongoni mwa Watu wa Ummah wangu Wataingia Motoni?'**

Malaika Jibril akajibu: '**Naam, Wale watakaofanya Maovu Makubwa na kisha wakawa si wenye Kutubu kabla ya Kufariki kwao'**

Na baada ya Uthibitisho huo basi hapo hapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaanza kulia, na Malaika Jibril nae akaanza kulia pia. Na baada ya tukio hilo *basi Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa hana raha, ikawa hatoki Nyumbani kwake isipokua kwa ajili ya Kusalisha, huku akiwa analia tangu mwanzo wa Sala mpaka mwisho wa Sala. na kisha akimaliza Hurudi ndani na kujifungia.

Subhanah Allah! Sijui Tunafahamiana sijui ama la? Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* analia kwa sababu yangu mimi na wewe tusiotaka kujizoesha Kufanya Istighfar kua mwisho wetu tutapotea mbali ya kua tunasali na kufanya Ibada nyenginezo zote. Allah atustiri na pia atujaalie kua ni wenye kudumu na Istighfar...Allahuma Amiin.

Hali hii ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kulia na kutojichanganya na watu iliendelea kwa siku 3, ambapo baada ya siku 3 basi Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* akaenda Nyumbani kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumgongea Mlango.

Lakini Mlango huo haukufunguliwa. Baada ya Abu *Bakr Radhi Allahu Anhu* basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* nae akaenda kugonga Mlango lakinu nae pia hakufunguliwa. Na Badae akafuatia Salman Al Farisy Radhi Allahu Anhu, akaenda kugonga lakini pia Mlango haukufunguliwa. Hivyo Salman Al Farsry Radhi Allahu Anhu akasimama kwa mda akijiukiza imekuaje, kisha akaamua kurudi Nyumbani kwake, lakini njiani akaona kua Nyumbani hakukaliki bila ya kujua kinachoendelea. Hivyo akarudi tena kwa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasimama huku akifikiria agonge tena Mlango ama la.

Baada ya kutafakkari basi Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* akaona kua Mtu atakaeweza kufunguliwa Mlango huu ni Fatma Bint Rasul tu. Hivyo akageuka na kuelekea kwa Fatma Bint Rasul Radhi Allahu Anha na kumgongea na kumjuulisha yaliyotokea. Hivyo Fatma Bint Rasul Allah *Salallahu Alayhi wa Salam* akajitayarisha kisha akaongozana na Salman Ibn Farsy hadi kwa Rasul Allah *Salallahu Alayhi wa Salam.*Na alipofika akagonga Mlango na kujitambulisha kua anaegonga ni Fatma Bint Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Wakati anajitambulisha basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua yuko katika Sijda akilia kuuombea Ummah wake,ambapo baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusikia Sauti ya Fatma binti yake basi akanyanyuka kutoka kwenye Sijda na kuuliza kwa kusema:

‘Ewe Utulivu wa Macho na Moyo wangu, Fatma..Kuna nini?’

Kisha akaamrisha kua Mlango ufunguliwe, na ulipofunguliwa Fatma *bint Rasul Allah Salallahu* Alayhi wa Salam akaingia Ndani Na alipokutana na Uso wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kuuona kwa namna ulivyosawijika basi Fatma Radhi Allahu Anha nae akaanza kulia kwa Khofu huku akiuliza imekuaje?

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam akamwambia Fatma Radhi Allahu Anha kua: **‘Amekuja Malaika Jibril na kuniambia kua Sehemu ya Juu kabisa ya Moto itakua ni sehemu ya Waja wangu waliofanya Maasi bila ya Kutubu Kabla ya kufariki kwao, hivyo hili ndio Jambo lililonihuzunisha sana.’**

Fatma *Bint Rasul Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Baba yake: ‘**Hivi Jee watu hao wataingizwa Motoni kwa namna gani?’**

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: **‘Malaika watawabururа wao kwenye Moto wa Jahannam, lakini Nyuso zao watu hao hazitokua na rangi Nyeusi, wala macho yao hayatokua na rangi ya Buluu, Midomo yao haitofungwa, hawatokua na Shaytan pamoja nao na wala hawatofungwa Minyororo wala Vyuma.’**

Hivyo Fatma Bint Rasul Salallahu Alayhi wa Salam akauliza: **‘Sasa wataingizwa kwa hali gani?’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **‘Wanaume watabururwa kwa Ndevu zao na Wanawake watabururwa kwa Nywele zao na hivyo Watu hao Wanawake na Wanaume, Wazee na Vijana watalia kutokana na Maumivu na Maadhiriko, na watakapoletwa kwenye Moto wa Jahannam basi Malik Malaika wa Moto wa Jahannam atauliza: ‘Hawa ndio kina Nani? Kwani wanautofauti na waru wengine Nyuso zao si nyeusi, Macho yao si ya Bluu, Midomo yao haijafungwa, hakuna Shaytan alieandamana nao na wala hawajafungwa Minyororo wala Vyuma?’**

Kwani Hapo Malik Malaika Msimamizi wa Moto wa Jahannam atawaita watu hao kwa kusema: **‘Enyi Waaasi, Nyinyi ndio kina nani?’**

Watu hao watasema kua: ‘**Sisi ndio wale ambao tulishushiwa Qur'an na kufaridhishiwa kufunga Mwezi wa Ramadhani’**

Ambapo Malik atasema: **‘Ah, Lakini mbona Qur'an ilishushwa kwa watu wa *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam?’***

Watu hao watasema: **‘Naam, sisi ni watu wa Ummah wa Muhammad’**

Malaika Malik atawauliza tena watu hao: **‘Hivi Jee Qur’an haikukuonyeninyinyi kuhusiana na kutlmuasi Allah Subhanah wa Ta’ala?’**

Kisha watu hao watakapouona Mlango wa Moto ukifunguliwa basi Watamuomba Malik kua awaruhusu wazililie Nafsi zao Kabla ya kuingizwa Motoni.

Ambapo Malik atawaruhusu na hivyo watu hao Watalia hadi Machozi yao yatakauka na watatokwa na Machozi ya Damu, na kisha Malik atawaambia Watu hao: '**Ya Laiti kamavilio vyneu hivyo vingekua vimetokea katika wakati mlipokua Duniani,kwani msingekua ni wenye kulia leo hii'**

Na baada ya kulia kwao Waislam hao wataingizwa ndani ya Moto huo lakini nao watasema: **'La Ilaha Illah Allah.'** Na hivyo Moto huo badala ya kuwavamia Moto basi utasita. Na hivyo Malaika Malik atauuliza Moto Huo kwanini ukasita kuwachoma Moto watu hao.

Ambapo Moto utasema: **Jee nitawachomaje mimi watu hawa wakati Ndimi zao zimetamka kauli ya kumpwekesha Allah?**

Hivyo Malik atauamrisha Moto huo uwachome lakini Moto utagoma, na kisha Malik atasema kua Watu hao watachomwa pale Allah Subhanah wa Ta'ala atakapoamrisha kua Wachomwe.

Hivyo Mto huo utaanza kuwachoma Watu hao kuanzia Miguuni, na kwa baadhi utawafikia Viunoni, na wengine hadi Shingoni. Malik atauamrisha Moto huo kua usizichome Nyoyo za Watu hao wala Nyuso zao, Kwa sababu Watu hao walikua ni wenye Kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wenye Kufunga Saumu ya Mwezi wa Ramadhan.

Watu hawa watabakia Motoni na kuunguzwa hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapotaka kusitishwa kwa Adhabu yao hio ambapo katika kipindi chote hicho basi watu hao watakua wakimuomba Allah kwa *Kumtukuza Ya Hanaan Ya Manan, Ya Arhama Rahimin*

Hadi pale itakapofikia wakati ambapo Allah Subhanah wa Ta'ala atamwambia Malaika Jibril akaangalie kuhusiana na Watu wa Ummah wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam waliokuwepo Motoni. Hivyo Malaika Jibril ataenda hadi katika Jahannam na kisha atamkuta Malik akiwa katikati ya Moto huo.

Na baada ya Malik kumuona Malaika Jibril basi atamuuliza amekuja kufuata nini? Malaika Jibril atakuja atamwambia kua amekuja kuiangalia hali ya watu wa Ummah wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* uliokua haukutubu kabla kufariki kwake uko katika hali gani?

Ambapo Malik atasema**: Watu wake wako katika hali mbaya Sana na hawawezi kutoka ndani ya Moto huu, na moto unawaunguza viungo vyao vyote isipokua Nyuso zao na Nyoyo zao Na hii ni kwa Sababu Nyoyo zao na Nyuso zao zilikua zimebeba Nuru ya Iman**

Hivyo Malaika Jibril atataka awaone watu hao, na arakapooneshwa na watu hao wakamuona Malaika Jibril basi watajua kua huyu sie Malaika wa Adhabu kutokana na Muonekano wake.

Hivyo watauliza: **Huyu ndio nani?**

Nao Wataambiwa kua: **'Huyu ndie Malaika Jibril *Alayhi Salam* aliekua akimshushia wahy na kumsomesha Qur'an Muhammad *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Ambapo baada ya kusikia jina lake kua ni Malaika Jibril basi watu hao watanadia kwa kumuomba Malaika Jibril kwa kusema: **'Ewe Malaika Jibril, Tupelekee Salam zetu kwa Kiongozi wetu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na mwambie kua Dhambi zetu zimetutenganisha nae na zinatuangamiza'**

Hivyo Malaika Jibril ataondoka na kurudi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kufikisha habari za watu hao na hali yao.

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atauliza: **'Jee wamekupa Ujumbe gani?'**

Malaika Jibril atasema: **'Wameomba kua wafikishiwe salam zao kwa *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na hali yao.'**Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamruhusu Malaika Jibril kufikishwa salam hizo *kwa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo Malaika Jibril atakimbilia Katika Pepo atakayokua anaishi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae atakua amepumzika kwenye Kasri la Lulu lenye Milango 4000 ambapo kila Mlango mmoja unapofunguliwa hufunguka kwa Milango 2 ya Dhahabu.

Malaika Jibril atamsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha atamwambia kua ametoka Kuonana na Watu wa Ummah wake waliopo Motoni, na kisha atamfikishia Ujumbe wao.

Na baada ya kusikia habari hizo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nae atakimbilia kwenye Arshi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kusjudu na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa sifa nzuri zaid ambazo kamwe hakuwahi kumtukuza nazo hapo kabla.

Na kisha Baada ya hapo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: '**Ewe Muhammad Nyanyua Uso wako, na kisha Omba unachotaka na bila ya shaka Utakubaliwa Uombezi wako.'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* atasema: '**Ya Rabb Maamuzi yako yamepita dhidi ya Waliofanya Dhambi miongoni mwa watu wa Ummah Wangu na wameshaadhibiwa sana kwa makosa yao, hivyo Nakuomba Nikubalie Uombezi wangu Juu yao'**
Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema kumwambia Mtume wake, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam kua: **'Amrisho limeshapitishwa jwa ajili ya Uombezi wako juu yao watu wa Ummah wako, hivyo nenda katika Moto wa Jahannam kamtoe kila Mtu aliesema La Ilaha Illa Allah.'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ataenda hadi kwa Malik Na hapo Malika atasimama kwa Heshima na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* atasema: '**Ewe Malika Vipi hali ya waliofanya Maovu miongoni mwa watu wangu?'**

Malik atasema: **'Ya Rasul Allah, Hakika ya Moto umeshawaunguza sana kila sehemu ya Ngozi zao na Maini yao.'**

Kisha baada ya Hapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Atafunguliwa Mlango ambapo nae atawaona Watu wake hao, na watu hao watamuona yeye na kumnadia kwa kusema: **'Ya Rasul Allah Moto umetuunguza ngozi zetu zote na Maini yetu.'**

Na hapo hapo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam atawatoa watu wake hao mmoja baada ya Mmoja mbali ya kua wameungua kama Mkaa. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* atawaongoza watu hao katika Mto wa Ridhwan ambao upo chini ya Mlango wa Kuingilia Peponi na kisha atawakogesha na baada ya kukoga kwao basi watabadilika muonekano wa Maumbile yao baada ya kua weusi kama mkaa watakua ni vijana wanaopendeza.

Na nyusoni mwao watakua na muhuri usemao: **'Huyu ndio yule mtu ambae alikua Jahannam lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala akamuachia* huru kutokana nao baadae.'**

Na kisha Watu hao Wataingizwa Peponi ambapo anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua Wale waliokua Kwenye Moto ambao hawakua Waislam basi watatamani kua na wao wangekua kama hao Waislam ambapo baadae watatolewa kwenye Moto kwa kusema:

﴿ رُّبَمَا يَوَدُّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ لَوۡ كَانُواْ مُسۡلِمِينَ ﴾

Rubama yawaddu alladheena kafaroo law kanoo muslimeena*(Surat AlHijr 15:2)*

Tafsir: ***Mara Nyingi watataka wale wambao ni waliokufuruna hivy kau si Waislam kua bora na wao wangekua Waislam.'***

Hio ndio Thamani ya Imani ya Dini ya Kiislam Huruma *ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Ummah wake na Umuhimu wa Kua ni mwenye Kudumu katika kufanya Istighfar.

Aya zinaendela kutonesha kuhusiana namaumbile ya Ibn Adam, kama anavyosema *Ali Ibn Abi Talib Radhi Allahu Anhu kua:***Katika Usiku wa Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimtembelea Fatima (Bint *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*) Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokaribishwa ndani basi akauliza kwa kusema: Jee Mtasali Sala ya Usiku hii leo?'**

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **Hivyo mimi nikasema: Lakini Ya Rasul Allah Roho zetu ziko chini ya Usimamizi wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo kama akipenda Atatuamsha**

Ambapo baada ya kutoa Jibu hili basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akapigwa na mshangao, na kisha hapo hapo hakusema chochote zaidi yake bali aligeuka na kutoka ndani ya Nyumba yao hio na kuenda zake. Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **'Nilimsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati anatoka huku akiwa amelipiga Kofi Paja lake na kisha akasema: *Inna Al Insana Akthara Shay-an Jadal* (Hakika Ibn Adam ni mwenye kupenda katika kilakitu kua ni kujadili).**

Naa haya ni maneno ya aya ya 54 ya Surat Al Kahf ambayo sababu yakushuka kwake ni kama tulivyoanza nayo hadith iliyomo katika Musnad Imam Ahamd Ibn Hanbal ambapo ndani yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alihoji kuhusiana na *Qiyam Al Layl* kwa Bint yake na kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhum* na akajibiwa kua kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* akiwajaalia kuamka basi watasali, hivyo nae akatoka ndani ya nyumba hio huku akisema maneno ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameafikiana nayo na kuyashusha katika aya ifuatayo:

﴿ وَلَقَدۡ صَرَّفۡنَا فِي هَٰذَا ٱلۡقُرۡآنِ لِلنَّاسِ مِن كُلِّ مَثَلٖۚ وَكَانَ ٱلۡإِنسَٰنُ أَكۡثَرَ شَيۡءٖ جَدَلٗا ﴾

Walaqad sarrafna fee hadha alqur-ani lilnnasi min kulli mathalin wakana al-insanu akthara shay-in jadalan *(Surat Al Kahf 18:54)*

Tafsir: ***Na kwa hakika tumeelezea ndani ya hii Qur'an Juu ya kila aina ya Mithali Lakini Daima Ibn Adam Ni Mwenye kupenda Kujadili sana***

Naam..Wengi sana miongoni mwa Wasiojua kati yetu hua na sifa ya Ukaidi na ni wenye kupenda kujadili mambo wasiyoyajua kwa hoja zisizokua za msingi, wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* wamekataza hayo.

Neno *Jadala* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kupindisha kitu kwa Nguvu, Kunyonga Kitu kwa Nguvu, Kua na Nguvu, Kuhoji, Kujadili, Kubishana na pia humaanisha Kugombana

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaelezea maumbile ya Ibn Adam kua mbali ya kua ni mwenye kuwekewa wazi mambo mengi sana kwa Mifano ya wazi ndani ya Qur'an lakini bado Ibn Adam amekua ni mwenye kupenda kubisha na kujadili juu ya kila kitu.

Yaani..mbali ya Ibn Adam kujua na Uwezo wa *Allah Subhanah wa Taa'ala* na kua yeye ndie Muumba wa kila kitu ikiwemo Ibn Adam mwenyewe na hivyo Allah Subhanah wa Ta'ala ni mwenye kujua kuhusiana lipi ni Bora na lipo ni Baya kwa Viumbe wake hao aliewaumba na hivyo kimantiki na kiakili basi Viumbe hao wanatakiwa wakubaliane na Muumba wao kua hili linafaa na hili halifai.

Lakini hata hivyo Ibn Adam bado anaendelea kubisha na kujadili juu ya Maamrisho na Makatazo Ya Mola wake,na *Allah Subhanah wa Ta'ala* anabainisha tena kuhusiana na haya katika Qur'an pale aliposema:

﴿ أَوَلَمْ يَرَ ٱلْإِنسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِن نُّطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴾

Awa lam yara al-insanu anna khalaqnahu min nutfatin fa-idha huwa khaseemun mubeenun*(Surat Yasin 36:77)*

Tafsir: ***Hivi Jee Haoni Mtu Kua Tumemuumba Kutokana na Mchanganyiko wa Maji ya Mwanamme na Mwanamke Kisha yeye Amekua ni Mpinzani aliewazi***

Na akasema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na haya pia kua:

﴿ وَقَالُوٓاْ أَءَالِهَتُنَا خَيْرٌ أَمْ هُوَ مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلاَّ جَدَلاَ بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ ﴾

Waqaloo aalihatuna khayrun am huwa ma daraboohu laka illa jadalan bal hum qawmun khasimoona *(Surat Az Zukhruf 43:58)*

Tafsir: ***Na Wakasema: 'Jee Miungu yetu ni bora au yeye' Ama wao Hawakutolei wao kwako (mifano) Isipokua kwa ajili ya Kujadiliana na kubishana nawe La! Bali wao Ni Watu wenye Kupenda kubishana na Kugombana)***

Subhanah Allah!

Haya sio maneno ya uwongo, wala si ya kuzuliana bali ni Maneno ya Muumba kuhusiana na Viumbe wake ambae anawajua ndani nje kiasi ya kua hawawezi kuficha kitu chochote kwake wala wao wenyewe hawawezi kujificha kutokana nae.

Maam..bila ya shaka haina haja kuainisha mambo yanayojumuisha Haki za Allah Subhanah wa Ta'ala ambayo ni wajibu wetu kuyatekeleza lakini bado unakuta Ibn Adam wanahoji na kujadili kwanini?

Kwani kwa leo tumalizie na mfano wa Imam Muhammad Idris Al Shafii pale alipomwambia mwanafunzi wake aliekua akipenda kujadili kua: **'Hivi inakuaje kua mimi nnasema kile ambacho amekisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* halafu wewe unasema kua mbona Ataa, Hasan Al Basr, Ibrahim Ibn Adham wamesema hivi?'**

Hivyo katika mifano ya aya zetu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaelezea maumbile ya Ibn Adam kua mbali ya kua ni mwenye kuwekewa wazi mambo mengi sana kwa Mifano ya wazi ndani ya Qur'an lakini bado Ibn Adam amekua ni mwenye kupenda kubisha na kujadili juu ya kila kitu.

Kwani miongoni mwa mifano ya wazi ya Ubishi na kupenda kujadili na kupinga kwa Ibn Adam ni pamoja na kuhusiana na Hukmu ya Talaka 3 kwa mpigo kua ni Talaka tatu ambapo hii ni kulingana na kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusema kuhusiana na Masahaba zake Abu Bakr na Umar *Radhi Allahi Anhu* kua: '***Iqtadu Bi Al Ladhiina Min BaAdi, Abi Bakrin wa Umar.***'Yaani **Wafuateni Watakaobakia Baada yangu Abu Bakr na Umar***(At Tirmidhi, Ibn Majah)*

Ambapo neno *Iqtidaa* limetokaa na neno *Qidwa* ambalo linamaanisha Kua na Sifa ya Mfano wa Kuigwa.

Hivyo tunaona kua hili ni Amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua atakapokua hayupo basi tufuate mifano ya Masahaba zake wawili hao ambao ni Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum*.

Ambapo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ndie alietoa Fatwa ya kua Talaka tatu kwa pamoja hua ni Tatu. Na Wanazuoni wamekubaliana juu ya Fatwa hio ya Umar Radhi Allahu Anhu Kama vile walivtokubakiana kuhusiana na Fatwa yake ya kua *Salat Taraweh* inapendekezwa kuisali Jamaa na kwa rakaa 20.

Lakini hapo unakuta watu wanajadili,wanapinga wanasema La Talaka 3 kwa kauli moja ni Talaka 1.

Jambo ambalo so sahih kulingana na kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kwa makubaliano ya Wanazuoni pia kwani kusema hivyo hua ni kuenda kinyume na maneno ya *Rasul Allh Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na si hivyo tu, bali mfano mwengine ni katika Hukmu za Kiislam za Mirathi ambazo zinasimamia Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Lakini unakuta leo bado watu wanaojiita Waislam wanakaa na kujadiliana na kugombana kuhusiana na mirathi na kufikishana kwenye Mahkama za Serikali badala yake na hivyo kua ni wenye kutokukubaliana na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kuna pia Mtizamo wa Mwandamo wa mwezi kua kila sehemu na Muandamo wake katika Ramadhan, Laylat Al Qadr, Idd Al Fitr, Arafah, Idd Al Adhha n.k.

Ambayo haya ni Makubaliano ya Wanazuoni kutokana na Fatwa ya Sahaba Mwanazuoni *Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu* ambae mbali y akua alikua akiishi na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini pia aliombewa dua mara kadhaa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Kua **'Ya Allah Mjaalie Ibn Abbas awe ni mwenye Ufahamu wa Dini na wa Ufafanuzi wa Qur'an.'** na pia alimuombea tena pale aliokua akikipapasa kichwa cha Abd Allah Ibn Abbas **Radhi Allahu Anhu** huku akisema: '**Ya Allah Kijaalie kichwa hiki kiwe ni chenye kujaa Ilm na Hikma, na ufafanuzi, mkusanyie Ilm yote na Hikma uliyowapa Ibn Adam ndani ya Moyo wake.'***(Fadhail Sahaba)*

Na kila mmoja wetu anakubaliana kua Dua ya *Rasul Alah Salallahu Alayhi wa Salam* hairudi bila ya Kukubaliwa na hili linaonekana wazi pia tunapoangalia Ukubwa wa Il. Aliokua nao Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kwani ingawa alikua Mtoto mdogo lakini Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikua hatoi Fatwa bila kumsikiliza Ibn Abbas kwanza. Halafu bado watu wanapinga na kukaa na kujadili kua kipindi hicho ilikua hakuna mawasiliano ya Tv wala Mtandao.

Subhanah Allah! Na hio ni baadhi tu lakini ukweli ni kua mifano inayothibitisha maana ya maneno ya aya yetu hii iko mingi sana hususan katika wakati huu wa kipindi cha uhai wetu, na amesema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika aya nyengine kuhusiana na mithal hizo kua:

﴿وَلَقَدْ صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ فِى هَٰذَا ٱلْقُرْآنِ مِن كُلِّ مَثَلٍ فَأَبَىٰٓ أَكْثَرُ ٱلنَّاسِ إِلاَّ كُفُوراً ﴾

Walaqad sarrafna lilnnasi fee hadha alqur-ani min kulli mathalin faaba aktharu alnnasi illa kufooran*(Surat Al Isra 17:89)*

Tafsir: ***Na kwa hakika tumeelezea kwa watu ndani ya hii Qur'an kila aina ya mithali,lakini hawakua wengi miongoni mwa watu isipokua ni wenye kupinga.***

Baada ya kumalizana na aya hio basi na tuangalie neno *Man'A* ambalo hua linamanisha Kukataa Kitu, Kuzuilika Kutokana na Kitu, Kukatazwa Kitu. Kukataliwa Kitu na pia humaanisha Kulindika. Kupata Hifadhi au Ulinzi kutokana na kitu.

Kwani neno *ManaA* ndio lililotumika katika aya ya 55 ambayo ndani yake imesema kua:

﴿ وَمَا مَنَعَ ٱلنَّاسَ أَن يُؤْمِنُوٓاْ إِذْ جَآءَهُمُ ٱلْهُدَىٰ وَيَسْتَغْفِرُواْ رَبَّهُمْ إِلاَّ أَن تَأْتِيَهُمْ سُنَّةُ ٱلأَوَّلِينَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ ٱلْعَذَابُ قُبُلاً ﴾

Wama manaAAa alnnasa an yu/minoo idh jaahumu alhuda wayastaghfiroo rabbahum illa an ta/tiyahum sunnatu al-awwaleena aw ya/tiyahumu alAAadhabu qubulan*(Surat Al Kahf 18:55)*

*Tafsir:****Na Hawakuzuilika Watu Kutokana na Kuamini Wakati Umewajia Uongofu Na Kutokana na Kufanya Istighfar (Kuomba Msamaha) Kwa Mola wao Isipokua kwa kurudiwa Njia za Waliowatangulia kabla yao Au Kufikiwa na Adhabu ya Kukabiliana nayo.***

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutufafanulia Ubishi wa Ibn Adam kua kutokana na Ukaidi wake basi mbali ya kua hakuzuiliwa kufuata njia anayoelekezwa na Mola wake kupitia katika Uongofu autumao kwa Mitume wake kwa ajili ya kuwaongoa Ibn Adam.

Na kuwaelekeza katika njia iliyonyooka, na hakuzuiliwa Mtu kuomba Msamaha yaani hakuambiwa kua Husamehewi kama ukikosea na kisha ukaomba msaada, bali ni kinyume chake kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kuweka wazi kua yeye ni msahemevu na ni mwenye kupenda wale wanaorudi kwake kwa ajili ya kuomba msamaha na hivyo atawasamehe.

Lakini bado kwa ubishi wake na kupenda kujadili basi Ibn Adam amekua ni mwenye Tabia ya kusubiri kama walivyokua wakisubiri wale wa vizazi vilivyotangulia kabla yake, yaani hadi iwafikie Adhabu ndio anapoanza kuzidukana kua duh! Subhanah Allah! Kumbe kweli.

Na hapo ndio atakapoanza kuomba Msamaha wakati ambao msamaha huo hautomfaa kitu kwani tayari Anakabiliana na Adhabu aliyokua akiisubiri kwa ubishi wake.

Na hivyo hali inakua kama mtu ambae amekimbilia kufunga mlango wa Banda la Farasi ili Farasi asikimbie kutoka Bandani wakati Farasi huyo tayari ameshatoka na kukimbia zamani.

Na hali hii hua ni hali ya kufuata Ubishi unaotokana na Kibri cha Jamii za Watu wa Mitume waliotangulia hapo kabla.

Imam Al Tustari anasema: **'Uongofu uliwajia kupitia kwenye njia ya Uongofu, ambao njia ya kuufikia ilikua imezibwa kwa ajili yao, kwani Uongofu na Imani ilizuiliwa kutowafikia kutokana na hukmu iliyipitishwa juu yao '**

Naam *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuambia katika aya ya 56 ya Surat Al Kahf kua:

﴿ وَمَا نُرْسِلُ ٱلْمُرْسَلِينَ إِلاَّ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ وَيُجَادِلُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ بِٱلْبَاطِلِ لِيُدْحِضُواْ بِهِ ٱلْحَقَّ وَٱتَّخَذُوٓاْ آيَاتِى وَمَا أُنْذِرُواْ هُزُواً ﴾

Wama nursilu almursaleena illa mubashshireena wamundhireena wayujadilu alladheena kafaroo bialbatili liyudhidoo bihi alhaqqa waittakhadhoo ayatee wama ondhiroo huzuwan*(Surat Al Kahf 18:56)*

Tafsir: ***Na Hatutumi sisi Mitume Isipokuwa Kwa ajili ya Kubashiria Habari njema Na Waonyaji Na Wanajadili Wale Ambao Wanaokufuru Kwa Hoja za Uongo Zisizokubalika Ili Kupinga Juu ya Ukweli Na Wamezichukulia Aya Zangu Na Juu ya yale walionywa Kua ni Utani.***

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua Hakua yeye ni Mwenye kuwatuma Mitume wake kwa Watu wake isipokua kwa ajili ya kazi Mbili.

Ambapo kwanza ni kwa ajili ya Kuwabashiria habari njema watu hao aliowatumia Mtume kama watakua ni wenye kufuata Mamrisho *yake Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Malipo yao ni Pepo. Kwani hakuna mbora wa Kulipa kwa Ukarimu kama *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Pili ni kwa ajili ya kuwaonya watu hao kuhusiana na Kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kufahamisha watu kua kama hawatotekeleza Maamrisho yake *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Watu hao Malipo yao yatakua ni Adhabu kali sana kwani hakuna mwenye kuadhibu kwa adhabu kali sana kama *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani mbali ya Kubashiriwa habari njema kama Watafuata maamrisho wa Mitume wao na kuonywa kuhusiana na Adhabu kali kama watawaaso Mitume hao. Lakini wale Wenye Kupinga juu ya Mitume hao yaani Makafiri wamekua ni wenye Kujadili na kisha kutoa hoja zisizokua za Msingi na za Uongo kwa ajili tu ya Kupingana na Ukweli wanaoambiwa na Mitume wao kuhusiana na Mola wao.

Na si hivyo tu bali wameenda mbali zaid kwa kufanya Kejili ma kuuchukulia Ujumbe wa Mitume wao waliotumiwa kwa ajili ya Kuwabashiria Mema na kuwaonya kua Wayasemayo Mitume wao hao sio ya kweli bali ni Maskhara na Utani tu. Subhanah Allah.

Allah atunusuru na haya kwani tunapoangalia katika wakati wetu basi haya tunayaona wazi pale watu wa Magharibi wanapomfanyia dhihaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema kua Watoto wadogo wasitofautishwe Kua huyu ni wa kike na huyu ni wa kiume kwani wao wenye hawajafikia wakati wa kuamua kua watakua ni wa Jinsia gani.

Yaani Mtu akishafikia Umri wa Miaka 18 ndio ataamua mwenyewe kama anataka kua Mwanamme au Mwanamke, na anataka kuolewa na Mwanamke au na Mwanamme. Imefikia hali katika Vyuo vya Magharibi ukiulizwa Jee Ibn Adam wana Jinsia ngapi basi ukijibu ni Jinsia 2 ya Kike na Kiume, basi Umefeli na unawekewa rongi kubwa sana.

Kwani Allah Subhanah wa Ta'ala anaendelea kusema kwa Kuhoji katika aya ya 57 ya Surat Al Kahf kua:

﴿وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ فَأَعْرَضَ عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ إِنَّا جَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْراً وَإِن تَدْعُهُمْ إِلَى ٱلْهُدَىٰ فَلَنْ يَهْتَدُوٓاْ إِذاً أَبَداً﴾

Waman adhlamu mimman dhukkira bi-ayati rabbihi faaAArada AAanha wanasiya ma qaddamat yadahu inna jaAAalna AAala quloobihim akinnatan an yafqahoohu wafee adhanihim waqran wa-in tadAAuhum ila alhuda falan yahtadoo idhan abadan*(Surat Al Kahf 18:57)*

Tafsir: ***Na Ni Nani Mwenye Kufanya Dhulma Zaid Ya Yule anaekumbushwa Juu ya Aya Za Mola wake Lakini Akazipa Mgongo Na Kusahau Yaliyotangulizwa na Mikono yake Hakika sisi Tumejaalia Juu ya Nyoyo zao Mapazia Ili Wasiifaham Na Ndani ya Masikio yao Na Hata Kama Ukiwaita (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Katika Njia ya Uongofu Basi Hawatoongoka Hata iwe vipi kwa Milele.***

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anahoji kwa Kuuliza Hivi Jee ni nani aliepotoka zaid ya yule ambae amefikishiwa Ujumbe wetu, na Akaona Vithibitisho vyetu, Na Maandiko yetu na kisha badala yake akawa ni mwenye kuzipuuza Aya hizo na kuachana nazo kwa kuzipa Mgongo kua hazifai? Huku akiwa ni mwenye kusahau juu ya ni nini alichokituma mbele ya Haki.
Kwani Ibn Adam ni mwenye Maumbile ya Kusahau ambayo nayo ni Neema bora miongoni mwa neema zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yetu. Kwani ingekua hakuna kusahau basi ingekua hakuna kulala wala kupumzika kimwili wala kiufaham, na ingekua Balaa kubwa sana na tungeshindwa kufikia Malengo yetu aliyotuumbia *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni ya Kumuabudu yeye.

Ila sasa Neema hio ya Sahau hua ni maangamizo kwa Ibn Adam pale anapokua ni mwenye kumsahau Mola wake, na Ujumbe wake, na Kusahau kuhusiana na Akhera. Kwani hii humpelekea Mtu kua ni mwenye kufanya Maovu kwa Viungo vya Mwili wake na kuyatanguliza mbele ya Mola wake bila ya kujali kitakachofuata baada yake.

Kwani inapofikia hali kama hii kwa Ibn Adam basi Ibn Adam Husika hua Na Kibri na Kujiona na kuingia katika hali ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamwambia Mtume wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Hata Uwaongoe vipi watu hao basi kamwe hawatoongoka, kwani kutokana na Kibri na kujiona kwao Basi tayari tumeshawafunika Mapazia kwenye Nyoyo zao na kuwatia Uziwi ndani ya Masikio yako**

Angalia *Allah Subhanah wa Ta'ala* anavyoelezea hali ya kuziba kwa hisia kusikia. Hakusema kua tumeyaziba Masikio yao bali kasema tumeshawaziba ndani ya Masikio yao. Yaani Kuyaziba Masikio hua ni kama kwa kutia Pamba au kuvaa Earphone kwenye Mlango wa kuingilia ndani ya sikio ambapo hata hivyo Unapofanya hivyo basi hua uanzuia baadhi tu ya sauti na kuna baadhi unakua unazisikia.

Lakini hapa *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kuhusiana na kuziba ndani ya Sikio yaani Kuiziba Ngoma ya Sikio ambayo ndio inayotafsiri Mlio wa Sauti ndani ya Sikio na hivyo mtu ukawa unajua kua hii ni sauti ya Salama. Hii ya Hatari, huyu ni Abd Al Basit Abd al Samad, au Al Qari Hasan Saleh na huyu ni Ummu Kulthoum, n.k

Hivyo Ngoma ya Sikio ya Watu hao hua Imezibwa na hivyo haisikii wala haitafsiri chochote. Kwa hivyo wewe utawapigia kelele hawa Jamaa mpaka utaingia wazimu lakini kamwe hawatokua ni wenye kukusikia kwani Ngoma ya Masikio yao Imezibwa kabisa kwa sababu tu ya Kibr chao kilichowapelekea kumsahau Mola wao na ujumbe wake juu yake. Allah atunusuru na mtihani huo..Aamiin

Tunaingia katika aya ya 58 ya Surat Al Kahf ambapo ndani yake basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Taala* anamwambia Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua:.

﴿وَرَبُّكَ ٱلْغَفُورُ ذُو ٱلرَّحْمَةِ لَوْ يُؤَاخِذُهُم بِمَا كَسَبُواْ لَعَجَّلَ لَهُمُ ٱلْعَذَابَ بَل لَّهُم مَّوْعِدٌ لَّن يَجِدُواْ مِن دُونِهِ مَوْئِلاً﴾

Warabbuka alghafooru thoo alrrahmati law yu-akhidhuhum bima kasaboo laAAajjala lahumu alAAadhaba bal lahum mawAAidun lan yajidoo min doonihi maw-ilan*(Surat Al Kahf 18:58)*

Tafsir: ***Na Mola wako Ni mwingi wa Usamehevu Na Ndie Mmiliki wa Rehma Hivyo Lau Kama angewachukulia Kutokana na Waliyoyachuma Basi kwa Hakika Angejaalia kwao wao(Kwa haraka sana kufikwa na) Adhabu Lakini Bila ya shaka wao wana Mda wao (Walioekewa) Ambao Kamwe Hawatoweza Kutokana na kuepukana nao.***

Kwani *Allah Subhaah wa Ta'ala* anamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua yeye Allah ni *Al Ghafuru.*

Ambapo neno Al Ghafuru hua ni Jina la Sifa tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yenye kumaanisha kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye Kutuzuia na kutulinda sisi Viumbe wake kutokana na kufanya dhambi na makosa yanayotokana na kasoro zetu za Kimaumbile za Viumbe na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuzuia kwa Huruma na Ukarimu wake.

Na tunapozungumzia kuhusiana na Ulinzi wake unaotokana na Sifa Tukufu ya *Al Ghafuru* basi ndani yake hua mna hifadhi za aina 2:

1-Hifadhi ya Kutuzuia Ibn Adam kutokana na Kufanya Dhambi kutokana na udhaifu wa Kimaumbile

2-Hifadhi ya kutuzuia Tusifikwe na Adhabu zake kutokana na makosa tuliyoyafanya kutokana na Udhaifu wetu wa kimaumbile

Kwani kutokana na Sifa yake Tukufu ya Ukarimu na sifa yake ya Al Ghafuru basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekua ni mwenye kuwasamehe viumbe wake wote ambao watakaorudi kwake na kumuomba msamaha kwa Ikhlasi. Na katika kuomba Msamaha kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi mtu kama unaweza kulia basi unatakiwa ulie japo mara moja ndani ya mwezi huu kwa ajili ya kujutia Madhambi yako.

Na ndio maana akasema Imam Sufyan Ath Thawry kua: '**Kuna sehemu 10 za Kulia Machozi ambapo katika sehemu hizo basi ni sehemu moja tu ndio hua ni kwa Ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala. Hivyo Ewe Muislam jitahidi angalua ikutokezee japo mara moja tu ndani ya Mwaka mzima utokwe na chozi kwa ajili ya Mola wako, kwani hio itakutosheleza sana kwa ajili ya kufutia Madhambi yako.'**

Na akasema Abd Allah Ibn Umar Radhi Allahu Anhu kua: **'Kwangu mimi ni bora kutokwa na Tone moja tu la Machozi ya kulia kwa ajili ya Kumuomba msamaha *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuliko kutoa Sadaqa Dinari za Dhahabu.'**

Mbali ya kua na Sifa Tukufu ya Al Ghafuru kama tulielezea hapo kabla lakini pia Miongoni mwa Sifa Tukufu za Allah Subhanah wa Ta'ala ni ile Al Sabur.

Na Sifa Tukufu ya Al Sabur imetokana na neno Sabara ambalo hua linamaanisha Kua na Subira, Kujifunga, Kujizuia, Kustahmili, Kuachana na kile kilichoharamishwa, Kushikamana na kile kinachoingia Akilini na kilichoamrishwa.

Kwani hata mwezi wa Ramadhan pia hua unajulikana kama ni mwezi wa Subira na hii ni kwa sababu ya kua ndio mwezi ambao ndani yake Waislam tunatakiwa kua Na Subra na Ustahmilivu katika kuyadhibiti Matamanio ya Nafsi zetu ambapo Kujizuia kwetu huko ndiko kunatupelekea kua na Malipo makubwa zaid mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwenye Sifa ya Al Sabur.

Ambapo Sifa hii Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ya Al Sabur hua inamaanisha kua Yeye ndie mwenye Sifa ya Kua na Subra kubwa sana na Ustahmili kuliko yeyote yule.

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuthibitishia hili pia katika aya yetu hii ya 58 ya Surat Al Kahf kwa kusema kua: Lau Kama Angawachukulia wale wanaomuasi kutokana na Walichokichuma kwa mikono yao basi bila ya shaka Watu hao wangefikwa na Adhabu kubwa sana tena kwa haraka sana. Lakini hata hivyo kutokana na Utukufu wa Sifa yake ya Al Sabur basi amewaaachia watu hao wafanye watakavyo hadi pale utakapowadia mda wao aliowawekea wa kuwashughulikia

Kwani hapa inabidi turudi nyuma mwanzoni mwa Aya hii ambapo tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amejisifu kwa sifa Tukufu za *Al Ghafuru Dhul Rahmati* yaani Msamehevu na Mwenye Umiliki wa Rehma.

Na hivyo tukizichukua sifa 2 hizi na kisha tukaziweka mbele ya Al Sabur basi tunaona kua Subira na Ustahmilivu wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni wenye kutokana na Utajiri wa Rehma zake kiasi ya

kua hua ni mwenye kuwapatia riziki zao wanaomuasi na huwapa mda watu hao wa kutafakkar na kutubu mbali ya kua wanastahiki kuadhibiwa hapo hapo kwa maovu yao. Na ukishafika mda wao na wakawa hawakutubu basi hapo inakua hakuna cha kuwaokoa kutokana na Adhabu zake, kama vile alivyowaadhibu watu waliotangulia kama zinavyoelezea aya inayofutia ambayo imetumia neno Halaka.

Neno Halaka kwa lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kuhiliki, Kufa, Kuangamia, Kupotea au Kuharibika.

Ambapo na neno hili ambalo tunapoliangalia kimaana basi linatuonesha Umuhimu wa kujua kusoma Qur'an kwa umakini na hii ni kwa sababu neno Halaka Ingawa limefanana kimatamshi na neno Khalaqa isipokua ila kutokana na Utofauti wa Herufi ya kwanza ambapo neno la kwanza limeanzia na herufi Ha na kumalizia na Kaf na la pili limeanzia

Na neno la pili limeanzia na Herufi Kha na kumalizia na herufi Qaf.

Ambapo kimaana basi maneno haya kutokana na kutofautiana kwa herufi hizo tu basi maana yote hua pia ni yenye kubadilika na hii ni kwa sababu neno Halaka humaanisha Kuhilikisha au kuangamiza na neno Khalaqa humaanisha Kuumba. Hivyo unaposoma katika aya na kisha ukabadilisha kidogo tu matamshi basi unakua tayari umeshabadilisha maana nzima ya Aya.

Hivyo katika aya inayofuatia ambamo ndani yake tunaona kua Allah Subhanah wa Ta'ala anatuambia kua:

﴿وَتِلْكَ ٱلْقُرَىٰ أَهْلَكْنَاهُمْ لَمَّا ظَلَمُواْ وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِم مَّوْعِداً﴾

Watilka alqura ahlaknahum lamma *th*alamoo wajaAAalna limahlikihim mawAAidan*(Surat Al Kahf 18:59)*

Tafsir: ***Na Hio Miji (ya watu Wa Mitume waliotangulia) Tuliowaangamiza Pale Walipofanya Maovu Basi na Tuliwajaalia Kuaangamia kwao kunakotokana na Mda Maalum uliokwisha pangwa.***

Naam..hapa tunaona kua Allah Subhanah wa Ta'ala anaielezea Miji ya watu wa Mitume waliotangulia walioangamizwa kutokana na Dhambi zao kwa kutumia neno Tilka ambalo ni lenye kuashiria vitu vilivyopo karibu na hivyo ni vyenye kuonekana na kua ni vithibitisho vya wazi ambavyo kila mmoja anaeambiwa juu yake ni mwenye kuviona na kuvijua.

Kwani kwa kutumia neno hili la Ishara basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaonesha kusisitizia kweke Mithali au mifano ya wazi kwa watu ili wapate kutafakkari kuhusiana kilichowafika wale waliotangulia kabla yao kutokana na Ukaidi wao na kubisha kwao.

Ambapo katika kutoa mifano kwake hio basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameiashiria Miji ya watu walioangamizwa hapo kabla, kwani hii ilikua ni Miji ambayo inafahamika na watu wa kabila la Quraysh Kwani baadhi yao kama Mji wa watu wa ilikua iko baina ya njia za Misafara yao ya kibiashara kuelekea katika ardhi ya Sham.

Kwa mfano Mji wa Madain Salih ambao ndio uliokua mji wa Watu wa Nabii Saleh uko katika maeneo ya Ardhi ya Al Ula ambalo ni eneo la Mji uliopo katika umbali wa Kilomita 400 Kaskazini Magharibi ya Mji wa Madina na Kilomita 500 kutoka kusini Mashariki ya ardhi ya Jordan.

Hivyo basi Watu wa Mji wa Makka walikua wakipita katika maeneo hayo na kuona na kujua kua eneo hilo lilikua na la watu wa Nabii Salih na hivyo walikua wanakijua kilichowakuta watu hao baada ya kumuasi Mtume wao na kupingana na maamrisho ya Mola wao.

Na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawa ni mwenye kuashiria maeneo ya Miji hio kama kwamba ipo mbele ya Macho yao kutokana na kufahamika kwao.

Kwani katika aya hii pia tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametumia neno *Maw-Aaidan* katika kudhihirisha kipindi cha Wakati maalum alioahidiwa.

Ambapo neno hili limetokana na neno *WaA'ada* ambalo ndio pia lililotoa neno *Mia'Ad* yaani Miadi linalomaanisha Wakati au Wakati wa Makubaliano au Sehemu ya Makubaliano.

Na ingawa Neno WaA'ada hua linamaanisha Kuweka Ahadi au Kutoa kauli yenye Kuahidi Kitu.

Lakini tunapozungumzia kuhusiana na Neno hili basi tunaona kua linatofautiana kimaana na neno Ahadi ambalo linatokana na neno Ahida hua linamaanisha Makubaliano, Maamrisho, Jukumu, Dhamana, Kiapo na pia humaanisha Kipindi cha Wakati wa Makubaliano.

Lakini pia tunapozungumzia kuhusiana na neno *WaA'ada* basi hua linamaanisha Ahadi ya Makubaliano Juu ya Kitu au Ahadi yenye Onyo na Vitisho vya Adhabu kali sana ndani yake baada ya Kufikia mda Fulani.

Na kwa maana hio basi maneno ya Aya hii yanatuonesha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatudhihirishia kua Maangamizo ya Watu hao wa Miji hio ilitokana na Maonyo na Vitisho ambavyo waliwekewa ndani ya Mda Maalum.

Kwani kama tulivyoona katika sababu ya Kushushwa Sura hii basi hapa Allah Subhanah wa Ta'ala alikua anawaahidi kwa kuwaonya pia Makafiri wa Makkah kua watafikwa na yaliyowafika wale waliotangulia kabla yao pale mda wao utakapomalizika na kisha wakawa hawakukubaliana na maamrisho ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Ambayo ni Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani ukishafikia wakati huo wa mwishoni mwa Miadi au ahadi hio ya Adhabu basi itakua hakuna kurudi nyuma tena kwani kila aliekua ni mwenye kupinga basi ataangamia.

Na bila ya shaka Miadi hii ilitimia pale mnamo mwaka wa pili Al Hijra katika Vita vya Badr ambavyo Makafiri wengi waliangamia bila ya kutegemea ndani yake.

﴿وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِفَتَاهُ لآ أَبْرَحُ حَتَّىٰٓ أَبْلُغَ مَجْمَعَ ٱلْبَحْرَيْنِ أَوْ أَمْضِىَ حُقُباً﴾

Wa-idh qala moosa lifatahu la abrahu hatta ablugha majmaAAa albahrayni aw amdiya huquban; *(Surat Al Kahf 18:60-61)*

Tafsir: ***'Na (Kumbuka) wakati Musa aliposema kumwambia Mwanafunzi wake; 'Sitosita kusafiri mpaka nifike kwenye sehemu iliyoungana Bahari mbili au mpaka nitimize miaka na miaka katika kusafiri kwangu'.***

KISA CHA AL KHIDR NA NABII MUSA ALAYHI SALAAM

Siku moja Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alikua amekaa na watu wa *Ahl al Kitab*. Mmoja miongoni mwao akasema: **Ya Ibn Abbas! Nawf mtoto wa mke wa Kaab anadai kua Musa aliekua akitafuta I'lm alikua ni Musa Ibn Manaseh!**

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Nawf amesema Uongo! Kwani Ubay Ibn Kab ameniambia mimi kua amesema *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* kua Musa ambae ni Nabii wa Bani Israil alimuuliza Mola wake: Ya Rabb! Kama ikiwa kuna yeyote miongoni mwa Waja wako ambae ana *I'lm* zaidi yangu basi nielekeze alipo nimfuate**'

Allah Subhanah wa Ta'ala akamjibu: '**Naam yupo mtu mwenye I'lm zaidi yako'**.

Kisha akamfahamisha alipo mtu huyo na kumfahamisha Nabii Musa sehemu atakayoweza kuonana nae. Ambapo anasema Imam Abu Abd Rahman Muhammad Ibn Al Husayn Ibn Muhammad Ibn Musa Ibn Khalid Ibn Salim Ibn Zawwiyah Ibn Saif Ibn Qabisa Al Azdi Al Sulami Al Shafii Al Nishapuri kua:

'Kuna Watu kutokana na kutokua na Ilm, basi katika kusoma kwao Qur'an kwa mfano katika kisa cha Nabii Musa na Al Khidhr hua Wanaona kua Al Khidhr yuko Juu zaid ya Nabii Musa Na hii ni kwa Sababu hua hawajui kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* humjaalia kila Kiumbe wake uwezo wake, kulingana na Majaaliwa yake juu ya Kiumbe husika hususan pale inapoonekana kua Nabii Musa aliambiwa aende akajifunze kwa Al Khidhr'

'***Allah Subhanah wa Ta'ala* hua anawatofautisha baadhi ya Waja wake kulingana na Mda na Wakati husika. Kwa Mfano Mitume hua Wanajaaliwa kua na Uwezo wa Kufanya Miujiza wakati Waja wengine hua hawajaaliwi kua na Sifa hio. Ambapo kwa upande mwengine kuna Waja ambao hua Wanajaaliwa vile ambavyo hawakujaaliwa kua navyo Mitume.**'

'**Kwa Mfano Maryam Bint Imran alijaaliwa kupokea chakula alichokua akiletewa Chumbani mwake, Lakini hakuna Mtume hata mmoja ambae alifanyiwa Mijuiza hio. Au Asif Ibn Barhiya alikileta Kiti cha Malkia wa Sheba Bilqis mbele ya Nabii Sulayman Lakini hapo hapo Asif Ibn Barkhiya mwenyewe hakua ni Mtume wala Nabii na wala hili halithibitishi kua Asif Ibn Barkhiya alikua ni bora kuliko Nabii Sulayman.nk'**

'**Hivyo Al Khidhr alijaaliwa kua na Ilm zaidi ya Nabii lakini hakuwa yuko juu zaidi ya Nabii Musa, kwa Sababu kama Al Khidhr angeona sehemu ndogo tu ya yale aliyoyaona Nabii Musa kuhusiana na Mola wake basi bila ya shaka Al Khidhr asingeweza Kustahmili kutokana na Maumbile ya mwili wake na hivyo angeangamia moja kwa moja kiasi ya kua kisingebakia hata kitu kimoja cha sehemu ya Mwili wake'**

Anasema Harun Ibn Atrah kua amemsikia baba yake kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Nabii Musa alimuuliza Mola wake: 'Ya Rabbi Jee ni yupi miongoni mwa waja wako ni kipenzi zaidi kwako?'**

Allah Subhanah wa Ta'ala akajibu: '**Ni yule ambae anaenikimbuka kila mara na hivyo kamwe hanisahau**'.

Nabii Musa akauliza tena: '**Jee ni yupi miongoni mwa waja wako ambae ni Muadilifu zaidi**?'

Allah Subhanah wa Ta'ala akasema: '**Ni yule ambae anaetoa Hukmu kwa Uadilifu na akawa si mwenye kufuata Matamanio yake'**.

Nabii Musa akauliza: '**Jee ni yupi miongoni mwa waja wako ni Mwenye I'lm zaidi**?'

Allah Subhanah wa Ta'ala Akajibu: '**Mwenye ilmu zaidi miongoni mwa waja wangu ni yule ambae anaejifunza kile ambacho watu Wanaojifunza hukifanyia jitihada wakijue ili wawe bora zaidi. Labda huenda atakipata katika maneno ambayo yatamuongoza katika njia iliyonyooka au kitamuokoa na uovu**.'

Nabii Musa akauliza: '**Jee katika Ulimwengu huu mwenye I'lm zaid yangu**?'

Allah Subhanah wa Ta'ala Aakajibu: '**Naam**'

Nabii Musa akauliza: '**Jee nitampata wapi?'**

Allah Subhanah wa Ta'ala Akajibu: '**Katika mwambao wa bahari, juu ya jiwe ambapo huwaachia huru samaki**', kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamfanya samaki kua ni alama na muongozo kwa Musa kwa kusema: '**Funga safari na chukua samaki wa kukausha, na samaki huyo atakapokua hai basi ndio utakua umempata mtu wako.'**

Na kw aupande mwengine kuna wasemao kua Nabii Musa alimshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* baada ya kumpa *Tawrat* kisha akauliza: '**Ewe Mola wangu Jee hii Ilm uliyonipa mie, kuna mtu yeyeote yule ambae umemjaalia kua nayo zaidi yangu?**'
Nabii Musa akaambiwa kua: '**Ewe Musa Kuna mtu ambae anaishi kisiwani, huyu ana ilm kubwa sana kwani Ilm yako kwake yeye hua ni sawa na tone la Bahari ambapo Ilim yake yeye ndio Bahari yenyewe.**'

Nabii Musa akasema: '**Ewe Mola wangu nijaalie mie kua ni mwenye heshima ya kukutana nae mtu huyo.'** *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kumwambia Nabii Musa: **'Ewe Musa chukua samaki kisha nenda katika sehemu ambayo bahari ya Aqabah na Bahari ya Suez zimekutana na utamkuta amekaa hapo, alama yako itakua ni Samaki wako atakapokua hai'**

Nabii Musa akauliza kwa kusema: 'Ewe Mola wangu, Jee mtu huyo huyo ni miongoni mwa Manabii au ni miongoni mwa Mitume?'' *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kumwambia Nabii Musa: '**Hakika yeye ni miongoni mwa Manabii ambapo wewe ni miongoni mwa Mitume**.'

Hivyo Nabii Musa akaamua kufunga safari hio yeye pamoja na Mwanafunzi wake aitwae Joshua kwa ajili ya kumtafuta Mtu huyo mwenye zaidi ili apate kuongeza mafunzo kwenye ufaham wake.

Hivyo ndani ya kisa hiki tutakachokiangalia katika kurasa zinazofuatia basi ndani yake mna mafunzo mengi ambapo kwa hapa mwanzoni tu basi tayari tumeshapata mafunzo yafuatayo:

1-Ingawa H*ata Allah Subhanah wa Ta'ala* alimsifia Nabii Musa kua alijaaliwa Kupewa Hikma na Ilmu kama zilivyosema Aya kua:

﴿وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَٱسْتَوَىٰٓ ءَاتَيْنَاهُ حُكْماً وَعِلْماً وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ﴾

Walamm<u>a</u> balagha ashuddahu waistaw<u>a</u> <u>a</u>tayn<u>a</u>hu <u>h</u>ukman waAAilman waka<u>dha</u>lika najzee almu<u>h</u>sineena *(Surat Al Qasas 28:14)*

*Tafsir: **Na alipobaleghe akawa na nguvu na kukamilia, tukampa hikma na Ilmu na kadhalika hivyo ndivyo tunavyowalipa wenye kufanya mema.***

Anasema *Sultan Al Balagha* Imam Abu Al Qasim Al Zamakhshari kua: '**Neno *Istaw*a lililotumika hapa hua linamaanisha kukua kwa mwili hadi kufikia kilele kiasi ya kua hakuna uwezekano wa kukua zaid.**'

Aya imetumia neno *Balagha* ambalo kwa lugha ya Kiswahili hua tunasema Baleghe basi hua linamaanisha Kufikia, Kukua, Kupea, Kukua Kiufaham, Kilugha, kua na ubora wa hali ya juu. Na pia imesema kua Nabii Musa alijaaliwa Hikma, yaani Ilm, Akili, Ufaham na Busara.

Naam..hayo ni maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Nabii Musa kua Alipopea Kiumri na kukamilia kimwili na kiufaham basi Alipewa Hikma na Ilmu.

Lakini hata hivyo Tunapozungumzia kuhusiana na sifa mbili hizi za kua na Ilm na Hikma basi tunaona kua hizi ni sifa za *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo yeye kama Muumba basi Hikma zake na Ilm yake hua hazina Mipaka yaani hazina Mwanzo wala Mwisho.

Lakini tunapozungumzia kiumbe basi yeye hua ni mwenye kua na Mipaka yake katika mambo hayo. Yaani hata ajaaliwe vipi basi haiwezekani kwake kua na ukamilifu katika Sifa hizo kwa sababu yeye ni Kiumbe tu. Na kwa kua ni Kiumbe basi bila ya shaka itakua kuna Kiumbe mwengine aliekua juu zaid yake. Kwani *Allah Subhanah wa Taala* amesema pia kua:

﴿نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَّن نَّشَآءُ وَفَوْقَ كُلِّ ذِى عِلْمٍ عَلِيمٌ﴾

NarfaAAu daraj<u>a</u>tin man nash<u>a</u>o wafawqa kulli <u>dhi</u>AAilmin AAaleemun *(Surat Yusuf 12:76)*

*Tafsir: **Hakika sisi humpandisha darja tumtakae Na Kwa kila alie juu kwa Ilm, basi kuna ajuae zaid.***

2-Ingawa Ibn Adam Unaweza kujaaliwa kua na Ilm na Hikma kama alivyojaaliwa Nabii Musa lakini hata hivyo haitakiwi Ubweteke na kuridhika na kijiona kua wewe unajua basi ndio basi tena haina haja kuendelea kutafuta Ilm

Ambapo hili ndio tatizo kubwa sana walilokua nalo watu wengi katika Jamii yetu Waislam na pia wengi Miongoni mwa Maimamu wetu leo hii

Yaani hua wanaridhika na walichokipata na kua nacho wanasahau kua katika Kutafuta Ilm hua hakuna Kutosheka kwani Kutafuta Ilm ni Ibada kwani jambo la Muhimu zaidi katika Maisha hua ni

kuendelea kutafuta na kukuza I'lm katika ufahamu wetu kwa amnufaa yetu ya Kidnia na Kiakhera na ndio maana Nabii Musa akasema hatositisha safari yake hadi aonane na aliemzidi ki'Ilm hata kama atatumia miaka na miaka.

Hivyo Ibn Adam haifai kusema au kuona kua: Unajua sana au Umesoma sana, n.k kwani I'lm na Hikma zetu ni Tone katika Maji ya Bahari! Kwani kama ikiwa Nabii Musa aliondolewa Hikma kwa kujiona ana Hikma, Jee itakuaje kwangu mie na wewe?

Na wenye kujua hua kamwe hawajioni kua wana Il'm na ndio maana akasema *Hujjat Ul Islam Mujaddid Ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad A Ghazali Al Tusi Al Shafii ambae mpaka sasa hakuna aliekua na sifa ya *Hujjat ul Islami* yaani uthibitisho wa Uislam isipokua yeye kutokana na wingi na Ukubwa wa Ilm yake, na hivyo anasema *Sultan Al Mutakallimin Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: '**Uwezo na *I'lm* ya Imam Abu Hamid Al Ghazali ilikua kama vile *Allah Subhanahu wa Ta'ala* amezikusanya *I'lm* zote kwa pamoja, halafu akamuonesha Imam Al Ghazal**'.

Na Imam Al Haramayn Abu Al Ma'ali Al Juwayni ambae alimsomesha Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali kwa muda wa miaka 5 alisema kua: '**Al Ghazali ni Bahari inayokata kiu ya *I'lm***'.

Na pia Imam Muhammad Ibn Yahya ambae alikua ni mwanafunzi wa *Hujjat Ul Islam Mujaddidi Ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii alisema kua: **'Imam Al Ghazal alikua ni Imam Al Shafi'i wa pili**'.

Hivyo basi mbali ya kusifiwa kote huko lakini *Hujjat Ul Islam Mujaddidi Ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad A Ghazali Al Tusi Al Shafii yeye mwenyewe anasema kua: '**Hakika mimi kila nikizidi kusoma basi ndio hua najiona kua kumbe mimi sijui kitu chochote'**

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaanza kutuelezea kisa cha Al Khidhr na Nabii Musa kwa kusema:

﴿وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِفَتَاهُ لآ أَبْرَحُ حَتَّىٰٓ أَبْلُغَ مَجْمَعَ ٱلْبَحْرَيْنِ أَوْ أَمْضِيَ حُقُباً﴾

Wa-idh qala moosa lifatahu la abrahu hatta ablugha majmaAAa albahrayni aw amdiya huquban; *(Surat Al Kahf 18:60-61)*

Tafsir: ***'Na (Kumbuka) wakati Musa aliposema kumwambia Mwanafunzi wake; 'Sitosita kusafiri mpaka nifike kwenye sehemu iliyoungana Bahari mbili au mpaka nitumize miaka na miaka katika kusafiri kwangu'.***

Hapa tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kumuelezea mtu aliekua amefuatana na Nabii Musa katika safari yake hio kwa kutumia neno *Fatahu* ambalo linatokana neno *Fatiya* ambalo hua linamaanisha Kua Kijana, Kua alie baleghe, Kua Jasiri, Kua Mkarimu au kua na sifa za Mwanamme aliekamilia.

Neno *Fatiya* hua pia linamaanisha Msaidizi anaekua nae mtu katika mambo yake ambae hua ni Kijana Shababi wa Kiume, Mfanyakazi.

Ambapo tunaona kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua; '**Kama mmoja wenu akimwita mfanyakazi wake basi na amwite *Fata* (kama ni mwanamme) au *Fatat* (Kama ni Mwanamke) na asimwite Mtumwa'**

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliposema kua Nabii Musa alisema kumwambia *Li Fatahu* basi alikua akimaanisha kua Nabii Musa alimwambia Msaidizi wake ambae kiumri alikua ni mdogo kuliko yeye kwani huyu alikua ni kijana ambae amekamilia kimwili na kiujasiri. Huyu *Fatahu* hakua mtu mwengine yeyote yule isipokua alikua ni Joshua Ibn Nun, ambae ndie yule aliekua wa Mwanzo kuingia kwenye Bahari pale watu wa Bani Israil walipokua wanafukuziwa na Fir'awn na jeshi lake, kabla ya kugharikishwa kwao.

Hivyo kutokana na Ujasiri wake na namna alivyokua akimuamini Nabii Musa na pia akimuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Joshua alikua ndio mtu wa mwanzo kuingia Baharini na Farasi wake na kisha akazama lakini akawa yuko hai ndani yake, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamuonesha Muujiza kupitia kwake, kwani ingawa alizama lakini akaja juu na wala hakufariki bali alikua hai ndani ya Maji yeye na Farasi wake, na mbali ya hivyo, lakini Joshua pia alikua ni Mrithi wa Uongozi wa Nabii Musa juu ya watu wa Bani Israil. hivyo ndivyo Walivyokua na Imani wale walioamini kweli Mitume wa Allah Subhanah wa Ta'ala na ndivyo namna *Allah Subhanah wa Ta'ala* alivyowaokoa na kuwaongoza baada ya wao kujitolea kwa ajili ya Mola wao.

Ambapo anasema *Sultan Al Balagha Jarrah Allah* Imam Abu Qasim Al Zamakshari kua: '***Majmaaa Al Bahrain* yaani Munganisho wa Bahari Mbili inamaanisha pia kua ni *Al Bahrain Al I'lm* yaani Bahari Mbili za Ilm'** Hivyo kutokana na Mtizamo huo basi tunaona kua hapa zinazungumziwa Bahari mbili za Ilm ya Nabii Musa na ya huyu Mja ambae aliambiwa akakutane nae, kwani kila mmoja wao miongn mwao amejaaliwa kuna na Bahari y Ilm ambayo hakujaaliwa kua nayo mwenzake**.**

Hivyo kutokana na Mtizamo huu basi tunaona kua Hapa ndani yake aya hii mnazungumziwa pia kuhusiana na Mkisanyiko wa Bahari mbili za Ilm yaani Bahari ya Ilm ya Nabii Musa na Bahari ya Ilm ya Al Khidhr, kwani kila mmoja miongoni mwao amejaaliwa kua na Bahari ya Ilm tofauti na Ilm ya Mwenzake yaani kuna kutofautiana kwa Ilm zao.

Kwani katika kuonesha Jitihada zake Nabii Musa katika kutilia mkazo umuhimu wa kutafuta Ilm kwake yeye, na hivyo aya kua ni yenyekutufunzasisi pia umihimu huo basi tunaona kua Nabii Musa ametumia neno Huquba

Ambapo neno Huquba linatokana na neno Haqiba ambalo linamaanisha Kuzuiliwa kitu, Mwaka ambao Umezuiliwa au umenyimwa Mvua na hivyo kunyimwa Mazao kutokana na kukosa Mvua.

Hivyo neno Huquban lililotumika hapa linamaanisha Muda mredu sana, Kipindi kama cha Miaka 80 yaani kama kipindi cha Malipo ya *Laylat ul Qadr* kwetu sisi Waislam wa leo na pia hua linamaanisha Kipindi kisichokua na Mwisho.

Subhanah Allah.

Hivyo kwa upande mmoja aya inatuonesha Umuhimu wa kutafuta Ilm kiasi ya kua Nabii Musa alikua yuko tayari kuutumia Uhai wake wote uliobakia kuishi kwa ajili tu ya Kutafuta Ilm kutoka kwa yule mwenye kujua zaid yake yaani Al Khidhr

Na kama Nabii Musa alikua yuko Tayari kutumia miaka 80 kwa ajili ya kutafuta Ilm tu, basi hii inamaanisha kua Kutafuta Ilm yenye Manufaa kwa ajili ya Dini yako na Akhera yako na ukaipata basi hua ni sawa kupata malipo ya kufanikiwa kupata fadhila za Laylat ul Qadr.

Na ndio maaana ukaambiwa *Al Ulamaa Warathat Al Anbiyah*..yaani Maulamaa Wenye Ilm ndio Warithi wa Mitume. Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ وَمِنَ ٱلنَّاسِ وَٱلدَّوَآبِّ وَٱلۡأَنۡعَامِ مُخۡتَلِفٌ أَلۡوَانُهُۥ كَذَٰلِكَ إِنَّمَا يَخۡشَى ٱللَّهَ مِنۡ عِبَادِهِ ٱلۡعُلَمَٰٓؤُاْ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٞ ﴾

Wamina alnnasi waalddawabbi waal-anAAami mukhtalifun alwanuhu kadhalika innama yakhsha Allaha min AAibadihi alAAulamao inna Allaha AAazeezun ghafoorun*(Surat Fatir 35:28)*

Tafsir: ***Na Miongoni mwa watu Na Viumbe Hai Na Wanyama Walivyotofautiana kwa Rangi zao Basi Kadhalika Na Hakika ya Wanaomuogopa Allah Miongoni Mwa Waja wake Ni Wanazuoni Hakika ya Allah ni Mtukufu na Msamehevu.***

Ambapo baada ya aya kutuainishia utofauti baina ya Viumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi inatudhidhirishia kua haiwezekani kwa watu wote kua aina moja kwanilazima watofautiane na kutofautiana kwao mbele ya *Allah Subhanah wa Taala* hua kunatokana na Ucha Mungu wao mbele yake, ambapo wale wenye kujitolea kikamilifu kwa ajili yake ndio wa bora mbele yake nah awa si wengine bali ni Wanazuoni wa Qur'an na Sunnah ndio wenye kumuogopa kweli *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hii ni kutokana na kua ni wenye kumujua kupitia katika Sifa zake na Majina yake.

Ambapo amesema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mtu mwenye Ilm hasa hua ni yule ambae hawakatishi Tamaa watu kuhusiana na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na wala hawarahisishii watu kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na wala hawafanyi watu kujihisi ua wako salama kutokana na Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na wala haachani na Qur'an wala kuipa mgongo au kuegemea chengine zaidi ya Qur'an. Kwani kwa hakika hakuna Uzuriwa kufanya Amali njema bila ya kua na Ilm juu ya Amali hio, Hakuna kua na Ilm kwa yule ambaye ni mwenye kutokua na Ufahamu juu ya fani husika na Hakuna kisomo cha Qur'an kwa yule ambae si mwenye kutafakkari.'**

Ama kwa upande wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Ilm hua si kua na sifa ya kunukuu sana, bali Ilm hua ni kumuogopa sana *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

Na akasema Imam Al Rabi Ibn Anas akua: **'Yule asiemuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua si Mwanazuoni.'**

Na Said Ibn Ibrahim aliulizwa kuhusiana na ni nani Kiongozi wa Wanazuoni wa Mji wa Madina ambapo nae akasema: **'Ni yule mwenye kumuogopa zaidi *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Na akasema *Hujjat Il Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhamamd Al Ghazali kua: **'Mtu mwenye Ilm hua kamwe habadilishwi Mtizamo wake kutokana na kupewa Mali.'**

Ambapo amesema Imam Ibn Abi Hayyan Al Taymi kua: **'Wanazuoni wako wa aina 3: Kwanza wale wenye *kumjua Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuyajua Maamrisho yake; Pili ni wale wenye kumjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini si wenye Kuyajua Maamrisho yake na Tatu ni wale wsiomjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini ni wenye kuyajua Maamrisho yake. Ambapo miongoni mwa Wanazuoni watatu hawa basi Mwanazuoni wa kweli ni yule mwenye Kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

Na amaesema Imam Ibn Attiyah kua: **'Maana ya Aya hii inatuonesha kua sio kwamba hakuna yeyote yule anaemuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* isipokua Wanazuoni, bali kutumia kwake ayah hii neno 'Innama' basi imekua ni yenye kutilia mkazo kua Sifa kuu ya Wanazuoni basi ni kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo hii haimaanishi kua wale wasiokua Wanazuoni hawawezi kua na sifa ya kua hawamuogopi *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Ambapo kuna wasemao kua hua linamaanisha kipindi cha miaka kuanzia mwaka Mmoja mpaka miaka Thamanini, lakini pia kuna waliolitafsiri kama vile lilivyotumika katika aya ifuatayo:

﴿لاَّبِثِينَ فِيهَآ أَحْقَاباً﴾

L<u>a</u>bitheena feeh<u>a</u> a<u>h</u>q<u>a</u>b<u>a</u>n*(Surat An Nabaa 78:23)*

Tafsir: ***Na watakaa ndani yake kwa miaka.***

Ambapo kwa upande wa *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allah Anhu*, Imam Qatadah Ibn Diama na Imam Ibn Zayd basiyeye anasema kua: '**Neno *Huquban* hua linatumika kwa kuainisha kipindi kirefu cha Miaka ambacho hua kinaweza kikafikia urefu wa Milele**'

Na hivyo basi Aya hii hua inatuonesha umuhimu wa kua na jitihada za Kutafuta *Ilm*, kiasi ya kua mtu unatakiwa usiachane nazo juhudi hizo za kutafuta *Ilm* hata kama itakuchukua miaka na miaka mpaka kuipata, kwani Ilm ni hazina yenye thamani kubwa sana, kwa sababu kidarja basi baada ya Imani ya kumjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* a, ambacho ndio kitu chenye thamani kubwa zaidi basi kinachofuatia ni Ilm kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an:

﴿يَأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُواْ فِي ٱلْمَجَالِسِ فَٱفْسَحُواْ يَفْسَحِ ٱللَّهُ لَكُمْ وَإِذَا قِيلَ ٱنشُزُواْ فَانشُزُواْ يَرْفَعِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْعِلْمَ دَرَجَاتٍ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ﴾

Y<u>a</u> ayyuh<u>a</u> all<u>adh</u>eena <u>a</u>manoo i<u>dha</u> qeela lakum tafassa<u>h</u>oo fee almaj<u>a</u>lisi faifsa<u>h</u>oo yafsa<u>h</u>i All<u>a</u>hu lakum wa-i<u>dha</u> qeela onshuzoo faonshuzoo yarfaAAi All<u>a</u>hu all<u>adh</u>eena <u>a</u>manoo minkum waall<u>adh</u>eena ootoo alAAilma daraj<u>a</u>tin waAll<u>a</u>hu bim<u>a</u> taAAmaloona khabeerun *(Surat Al Mujaddila 58:11)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini kama mkiambiwa wekeni nafasi kwenye sehemu mnazokaa na kujadiliana mambo tofauti basi wekeni nafasi, kwani Allah atakuwekeeni nafasi (Katika Rehma zake), na mkiambiwa nyanyukeni (mkafanye mema kwa ajili ya Allah)basi nyanyukeni, kwani Allah huwanyanyua darja wale walioamini miongoni mwenu na wale waliopewa I'lm, na Allah ni mwenye habari juu ya kila mnachokifanya.***

Hivyo basi bila ya shaka Ilm ni kitu chenye thamani kubwa sana, ambacho kimaumbile kinawezekana kiurahisi kubakia ndani ya Ufahau wako kama utakitafuta na kisha kukiweka ndani yake, kwani amesema Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhamamd Ibn Muhammad Ibn Muhamamd Al Ghazali kua: **'Ufahamu wa Ibn Adam ni kama Ardhi yenye Rutba na mbegu ndani yake, hivyo ukiitilia maji ardhi hio basi mbegu hio itachipua na kukua'** yaani Ufahamau wa Ibn Adam ni kitu ambacho kimeumbwa kwa ajili ya kuhifadhi Ilm ndani yake na hivyo ukiijaza Ilm ndani yake basi Bila ya shaka itahifadhika na kukua ndani yake na kuchipua na kuonekana nje ya mwili wa Ibn Adam husika katika maneno yake na vitendo vyake.

Na hivyo inabidi tuutumie wakati wetu tulionao kwa ajili ya kutafuta Ilm kwani anasema Imam Muhyi Ad Din Ibn Arabi kua: '**Wakati wa kitu hua ni katika kuwepo kwake kitu hicho kwenye mazingira yake'** hivyo basi wakati hua una thamani pale unapokuwepo na kitu chenye thmani hubadilishwa kwa kitu chengine chenye thamani zaidi yake au mithili yake, na baada ya Uhai na Imani basi hakuna kitu chenye thamani kama Ilm na ndio maana akasema Imam Abu Abd Rahman Muhammad Ibn Al Husayn Ibn Muhammad Ibn Musa Ibn Khalid Ibn Salim Ibn Zawwiyah Ibn Saif Ibn Qabisa Al Azdi Al Sulami Al Shafii Al Nishapuri kua: '**Amesema Imam Al Tustari kua: Fahamu kua Wakati ni kitu chenye thamani kubwa sana, hivyo usiutumie wakati wako isipokua kwa kitu chenye thamani zaidi mbele yako na mbele ya Mola wako'**

Ambapo kwa upande mwengine basi kwa kutumia maana ya *Huquban* yenye kumaanisha Ukame au kutokua na Mvua basi pia inaingia maana yake kua Nabii Musa aliamua kutafuta Ilm kwa vyovyote vile itakavyokua kupitia kwa mtu huyo alieahidiwa kua amepewa *Ilm Ladduni* kua atampatia Ilm.

Na tunapozungumzia kutafuta Ilm basi hua hakuna wakati kwani kama tunavyoona kua hapa tayari Nabii Musa alikua ameshapewa Utume na ameshafanya Miujiza mingi na ameshapewa Tawrat hivyo inamaana kua alikua keshapita zaidi ya Umri wa miaka 50.

Ambapo kwa Upande mwengine pia kuna mfano mzuri sana wa miongoni mwa Maimamu walioishi katika karne ya 3 Al Hijra ambae ni mwanazuoni mkubwa sana wa Madhhab ya Imam Al Shafii aitwae *Al Faqih Imam* Abu Bakr Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Abd Allah Al Qaffal Al Marwazi Al Shashi Al Khurasan Al Shafii, ambae ni maarufu kama Imam Al Qaffal au Imam Al Marwazi au pia Imam Al Shashi.

Imam Al Qaffal alikua ni Muislam wa kawaida tu, kama walivyo Waislam wengine ambao ni Maamuma, na alikua ni fundi wa Kufuli na ndio maana akaitwa *Al Qaffal* kwa sababu neno Kufuli limetokana na neno *Qaffal* ambalo ni la Kiarabu. Hivyo mpaka Imam Al Qaffal anafikia Umri wa miaka 40 basi alikua hana Ilm ya aina yeyote, isipokua kuchonga funguo na kutengeneza Kufuli.

Siku moja akasikia kua kuna Al Qaffal ambae mwengine ambae alitengeneza Kufuli ndogo sana yenye uzito wa nusu gramu, na hivyo watu wakamsifu sana Al Qaffal huyo kwa ujuzi wake, kutokana na kusifiwa kwa Al Qaffal huyo basi Imam Al Qaffal akataka avuje rikodi ya Al Qaffal huyo anaesifiwa na hivyo nae akatengeneza Kufuli ambayo ni ndogo kwa mara tatu zaidi. Na kisha akaifanyia maonesho kufuli hio kwa watu lakini hata hivyo hakuna hata mtu mmoja alievutiwa na kumpa Imam Al Qaffal hongera stahiki.

Tukio hili ilimvunja moyo sana, na wakati analalamika basi mmoja katia ya marafiki zake akamwambia kua: '**Heshima ya Mtu hua haipandi Darja kwa kutokana na kutengeza kufuli, bali hupanda darja kutokana na kua na I'lm'** ambapo na Imam Al Qaffal nae akasema: '**Hakika mimi nitakua ni mwenye kutafuta Ilm na nitakua ni mwenye Ilm'**

Na bila ya shaka Imam Al Qaffal wakati huo akiwa na miaka 40, basi akajitahid hadi akafikia malengo yake ya kutafuta Ilm kwa kumchagua mmoja kati ya Wanazuoni wakubwa kua ni mwalimu wake ambae siku ya kwanza tu alimfundisha maneno yafuatayo yaliyomo mwanzoni mwa kitabu cha Mukhtasar Al Muzani cha Imam Al Muzani, ambae ni mwanafunzi wa Imam Al Shafii, ambapo maneno hayo yanaema: '***Hadha Kitab Ikhtasarat'*** Imam Al Qaffal aliporudi nyumbani akayakariri maneno haya usiku wote, hadi akapata usingizi.

Lakini alipoamka asubuhi ikawa ameyasahau maneno hayo, akaona hii sasa ishakua kazi kubwa sana, kwani maneno matatu tu yameshinda kuyahifadhi jee atafika? Hivyo akatoka nje na akakutana na Jirani yake ambae ni mwanamke na kuumuuliza Imam Al Qaffal: '**Ya Al Qaffal! Ni kitabu gani hicho ambacho jana sisi hatukulala kwa sababu ya wewe kua ni mwenye kurdia rudia kwa sauti *Hadha Kitab Ikhtasarat*?**'

Hapo Imam Al Qaffal akasema: '**Naam..Al Hamdlillah *Hadha Kitab Al Ikhtasarat***' kisha akaelekea kwa Mwalimu wake na kumuelezea alivyovunjika Moyo kutokana na kisa chake, ambapo mwalimu wake huyo akamwambia: '**Usijaribu kuifanya kasoro hio kua ni kipingamizi kwako wewe na kutokua na hamu ya kutoendelea kutafuta Ilm**, **kwani ukiendelea kuhifadhi kidogo kidogo basi mwisho wake ufahamu wako utakua ni wenye kuzoea na kua na maumbile ya kuhifadhi unayoyasoma.**'

Huu ulikua ni ushauri ambao ulimfanya Imam Al Qaffal kua kama anavyosema Imam Al Samaani kuhusiana nae kua: **'Imam Al Qaffal Al Marwazi Al Shashi alikua mpole na mkarimu miongoni mwa Maimamu wa Madhhab ya Imam Al Shafii na alikua akihesabiwa kua ni miongoni mwa Maimamu wenye nguvu kubwa sana ya Ufaham wa juu wa Ilm kuliko Imam yeyote yule katika wakati wake.'**

Imam Al Samaani anaendeea kusema kua: **'Imam Al Qaffal Al Marwazi Al Shashi alikua na upekee katika wakati wake kwa Ilm ya Fiqh, Kwa kuhifadhi, kwa Ucha Mungu na kua na Taqwa, na hii ni kwa sababu Imam Al Qaffal Al Marwazi alikua amesoma vitabu ambavyo ilikua hakuna alievisoma na wala hakuna aliekua navyo vitabu hivyo.'**

Na kwa upande wa Al Faqih Imam Nasir Ibn Umar basi anasema kua**: 'Katika wakati wake ilikua hakuna mtu mwenye Ilm kama Abu Bakr Al Qaffal, na hakutokua na mtu mwengine mithili yake kwani sisi tulikua tukisema: 'Abu Bakr Al Qaffal ni Malaika mwenye Umbo la Ibn Adam ambae kazi yake ni kuhadithia na kuzungumza Ilm ili watu waandike. Imam Al Qaffal al Marwazi alikua ni kiongozi wa Fiqh na alikua ni mfano wa watu walioachana na dunia hii'.**

Katika kipindi cha Uhai wake na kutokana na Ilm yake basi Imam Al Qafal alifanikiwa kuibadilisha Fiqh ya Utawala wa ardhi yake ambayo ilikua ikifuata Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa na kuufanya Utawala wa Sultan Mahmoud wa ardhi ya Marwaz kua ni yenye kufuata Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kutokana na nguvu ya hoja zake na wingi wa Ilm yake, kwani Imam Al Qaffal Al Shashi Al Marwazi Al Shafii alifanikiwa kua ndio nguzo ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kwa upande wa *Tariqah* ya Khurasan.

Na tunasema kua ni *Tariqah* ya Khurasan kwa sababu hapo kabla ya kuja *Hujjat ul Islami Mujaddid Ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali katika karne ya 5 Al Hijra basi Wafuasi wa Skuli ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii walikua wamegawika katika matawi mawili, yenye Fiqh zinazofanana lakini zenye kutofautiana kidoogo kimitizamo na kulikua na *Tariqah* ya Baghdad na *Tariqah* ya Khurasan, na alikua ni *Hujjat ul Islami* Imam Abu

Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali ambae ndie alieziunganisha *Tariqah* mbili hizi. Na kuzifanya kua *Tariqah* Moja.

Hivyo huo ni mfano miongoni mwa mifano bora ya mtu kutotakiwa kujiona kua umepitwa na wakati wa kusoma kutokana na kua na umri mkubwa kwani wakati ni kitu chenye thamani kubwa sana hivyo utumie kwa ajili ya kutafuta Ilm itakayo kunufaisha na akhera yako.

Kwani Imam Al Qaffal kaanza kusoma wakati akiwa na umri wa miaka 40, na katika kisa chetu basi tunaona kua Nabii Musa akiwa anakaribia miaka 50 basi ameamua kutafuta Ilm kutoka kwa Al Khidhr ambae ni mtu alieambiwa amtafute kwani ana Ilm zaid yake na katika kuonesha azma yake hio basi akamwambia Joshua ambae ni Msaidizi wake kua, atamtafuta mwenye Ilm huyo hadi amuone hata kama itachukua milele.

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Kama Mtu atakua ni mwenye kupenda kutafuta Ilm, basi milango ya Pepo itafunguka kwa ajili yake, *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataridhika na mja wake huyo, na hivyo mwili wake hautoliwa na funza Kaburini na Peponi atakua ni rafiki yake Al Khidhr**'

Hivyo baada ya kuweka ahadi hio basi Nabii Musa na Joshua wakajitayarisha kwa safari na walipokamilisha matayarisho wakaanza safari yao huku wakiwa na chakula chao ambacho ndani yake mna mikate na samaki wa kubanika ambae walifahamishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* wapi watampata watampata Samaki huyo. Safari ilikua ndefu na ilichukua mda mrefu, lakini hata hivyo kutokana na ari yao basi hawakua ni wenye kusikia uchovu sana na walifanikiwa kuwasili katika maeneo ambayo kwa mbali waliyoana kua yanafaa kupiga kambi kutokana na uzuri wa muonekano wa mandhari yake kutoka kwa mbali, na hivyo walipoyakaribia basi ilikua tayari kiza cha usiku kimeshaingia.

Hivyo wakapiga kambi katika eneo hilo ambalo lilikua na jiwe kubwa sana na chemchem ya maji, hivyo wakafanya Ibada zao kisha wakala na wakapumzika hadi Alfajir mapema ambapo waliamka na kisha wakasali na kufunga funga mizigo yao na kuanza kuendelea na safari yao, ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anailezea hali hio kwa kusema:

﴿فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنِهِمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا فَٱتَّخَذَ سَبِيلَهُۥ فِى ٱلْبَحْرِ سَرَبًا﴾

Falamma balagha majmaAAa baynihima nasiya hootahuma faittakhadha sabeelahu fee albahri saraban *(Surat Al Kahf 18:61)*

Tafsir: ***Lakini walipofika katika maungano ya bahari mbili, (wakaona kua) wamesahau Samaki wao. Na akatelezea kwenye maji kama kwenye njia'***

Katika kumuelezea samaki huyu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametumia neno *Hutta* ambalo hua linamaanisha Kurukaruka, Kutembea tembea katika sehemu tofauti kwa ajili ya kutafuta chakula na pia hua linamaanisha Samaki.

Aya pia imetumia neno *Saraba* ambalo hua ni lenye kumaanisha Kuenda kwa Uhuru, Kuelea, Kukimbia, Kuenda kwa dhahiri, Kuteleza au Kutiririka. Neno *Saraba* hua pia linamaanisha Chungu ya Mchanga ambao haujashikamana. Ambapo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* anasema kua neno *Saraba* hua linamaanisha kua Samaki huyu alipotoka kwenye Mfuko na kisha kuangukia

ardhini kuelekea Baharini basi alikua ni mwenye kuacha alama katika kutiririka kwake kwenye mchanga uliopo hapo kuelekea kwenye maji.

Hivyo inamaanisha kua baada ya kuondoka kwao kutoka kwenye sehemu waliyopiga kambi wakagundua kua Samaki hayumo kwenye sehemu waliyomuweka hapo kabla na hii ni kutokana na hali ya kua Nabii Musa alisahau kuulizia kuhusiana na yule Samaki wakati walipokua wanakula na Joshua nae pia alisahau kukumbusha kuhusiana na Samaki huyo wakati wa kula.

Ambapo anasema Abd Rahman Ibn Zayd kua: '**Maajabu yalioje kwa samaki ambae alikua tayari aliwe lakini akabadilika na kua mzima na kutelezea Baharini, kwani ilikua ni kipande cha Samaki.'**

Na waligundua juu ya tukio hili la kutoweka samaki wao pale mara baada ya Nabii Musa kua ni mwenye kuhisi njaa, hivyo akamwambia Joshua kama zinavyobainisha aya kwa kusema:

﴿فَلَمَّا جَاوَزَا قَالَ لِفَتَاهُ آتِنَا غَدَآءَنَا لَقَدْ لَقِينَا مِن سَفَرِنَا هَٰذَا نَصَباً ۞ قَالَ أَرَأَيْتَ إِذْ أَوَيْنَآ إِلَى ٱلصَّخْرَةِ فَإِنِّي نَسِيتُ ٱلْحُوتَ وَمَآ أَنْسَانِيهُ إِلاَّ ٱلشَّيْطَانُ أَنْ أَذْكُرَهُ وَٱتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي ٱلْبَحْرِ عَجَباً﴾

Falamma jawaza qala lifatahu atina ghadaana laqad laqeena min safarina hadha nasaban; Qala araayta idh awayna ila alssakhrati fa-innee naseetu alhoota wama ansaneehu illa alshshaytanu an adhkurahu waittakhadha sabeelahu fee albahri AAajaban *(Surat Al Kahf 18:62-63)*

Tafsir: ***Na Kisha walipopita (katika sehemu waliyokubaliana) akasema (Musa) kumwambia Msaidizi wake: 'Tutolee chakula chetu cha asubuhi kwani kwa hakika tumekutana na uchovu katika safari yetu hii.' Akasema (Joshua) Hivi jee unakumbuka tulipopumzika kwenye jiwe? kwa hakika mimi nimemsahau (samaki katika sehemu hio) na hakuna isipokua shaytan ndie alienifanya nisahau kumkumbuka, na akafuata njia yake Baharini kimaajabu.***

Aya zinatuonesha kua baada ya safari ndefu Nabii Musa akawa anahisi kuchoka hivyo akaona kua umefika wakati wa kula ili kuipa miili nguvu kwa ajili ya kuendelea na safari, hivyo Nabii Musa akamwamia Joshua kua atayarishe chakula kwani washatembea kwa mda mrefu, ambapo baada ya kuamriwa hivyo basi Joshua nae akakumbuka kua yule samaki ametoka kwenye mkoba na kuelekea Baharini.

Na hii inaonesha kua Joshua aidha aliona namna samaki alivyotoka na kukimbilia baharini kwa urahisi na kushindwa kumzuia kutokana na maajabu ya Miujiza aliyoiona ya samaki aliebanikwa, ambae ni kipande kugeuka kua mzima na mwenye kuishi na kukimbilia Bahari. Au pia inamaanisha kua Joshua hakumuona samaki huyo wakati anatoka kwenye mkoba na kukimbilia Baharini, lakini aliona alama ya njia aliyoiachwa Samaki huyo wakati akikimbilia kwa kuteleza kuelekea Baharani kwa urahisi sana.

Hivyo mbali ya kua aliona moja kati ya matukio hayo ya Maajabu lakini hapo hapo aya zinaonesha kua Joshua alisahau kabisa kumwambia Nabii Musa kuhusiana na tukio hilo, ambapo kuna baadhi wanaweza wakajiuliza ilikuje mpaka Joshua akasahau kuhusiana na tukio la ajabu kama hili?

Hivyo anasema *Jarrah Allah* Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua: '**Inabidi tufahamu kua Joshua hapa alikua na Mmoja kati ya Watu watukufu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hivyo alikua akiona mambo mengi yanayotokea ya kimiujiza'.** Hivyo haiwezekani kua kwake yeye kila anachokiona cha Miujiza amuelezee au amuulize Nabii Musa.

Ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Saib Al Kalbi kua: '**Joshua alikoga kwenye chemchem ya maji iliyokua ikitiririka katika sehemu hio na maji yake yakaingia kwenye mkoba ambao ndani yake alikuwemo samaki wao, na samaki huyo akawa hai na kuruka ruka kutokana na maji hayo na kutumbukia kwenye maji'.**

Hivyo Nabii Musa baada ya kusikia kuhusiana na habari hio ya samaki wao aliekua *sarraba* basi hali ikawa kama zinavyosema aya:

﴿قَالَ ذَٰلِكَ مَا كُنَّا نَبْغِ فَٱرْتَدَّا عَلَىٰٓ ءَاثَارِهِمَا قَصَصاً﴾

Qala dhalika ma kunna nabghi fairtadda AAala atharihima qasasan*(Surat Al Kahf 18:64)*

Tafsir: **Akasema (Nabii Musa) : 'Hicho ndicho tulichokua tukikitafuta' kisha wakarudi kupitia katika athari zao (nyayo zao) kuzifuata.**

Allah Subhana wa Ta'ala anatuonesha utajiri wa Lugha ya Kiarabu na uzuri wa mpangilio wake ndani ya Quran na hivyo kuturahishia kutiririka nazo aya zake, kwani aya zote za kisa hiki zimemalizia na *fat-ha* ambapo tunapoiangalia aya hii basi tunaona kua imemalizia na maneno *Atharihima Qasasan* ambapo *Athari* maana yake hua ni Athari Au Hatua au Nyayo na neno *Qasasan* linamaanisha Kuweka au kupiga Muhuri, Kurudia kitu, Kufuata kitu na pia humaanisha kuhadithia Kisa au kuhadithia Hadith au Kutaja kitu.

Hivyo basi baada ya kugundua kua wanachokifuata na kukitafuta wamekiacha nyuma na wameshakipita basi Nabii Musa na Joshua waligeuka na kuanza kufuata hatua za nyayo zao walizopita hapo kabla ili wafike kwa urahisi pale katika sehemu ambayo walipopiga kambi jana yake. Na hii inatufunza pia umuhimu wa kutovunjika Moyo katika kutafuta Ilm na pia kutovunjika moyo pale unapoona kua badala ya kuenda mbele basi wewe umerudi nyuma,kwani baadhi ya wakati katika Maisha hua inatubidi kurudi nyuma hatua mbili tatu kwanza ili baadae tuweze kukimbilia mbele na kuruka kwa hatua mara dufu zaidi kwani Nabii Musa ilimibidi akirudie kile ambacho ameshakipita hapo kabla.

Nao wakarudi moja kwa moja huku njaa yote na machovu yakiwa yamekata, kwani habari hizi zilimtia ari kubwa sana Nabii Musa na Joshua na hivyo haraka sana wakakimbilia walipotoka, na walipofika..*Subhnah Allah* anaelezea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema:

﴿فَوَجَدَا عَبْداً مِّنْ عِبَادِنَآ ءَاتَيْنَاهُ رَحْمَةً مِّنْ عِندِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِن لَّدُنَّا عِلْماً﴾

Fawajada AAabdan min AAibadina ataynahu rahmatan min AAindina waAAallamnahu min ladunna AAilman*(Surat Al Kahf 18:65)*

Tafsir: ***Kisha wakampata mja miongoni mwa waja wetu ambae tumempa Rehma na tukamfundisha kutoka kwetu I'lmu.***

Anasema *Sultan Al Balagha Jarrah Allah* Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua: '**Mtu huyo alikua ni Al Khidhr neno lenye kumaanisha mwenye Rangi ya Kijani, na walimkuta akiwa amelala huku akiwa amejifunika shuka kuanzia kichwani mpaka miguuni, alikua ni mtu ambae amepewa Ilm iliyofichika na isiyojulikana.**'

Ambapo kuhusiana na ni kwa nini akawa anaitwa *Al Khidhr* yaani mwenye rangi ya Kijani basi Wanazuoni wametofautiana juu yake, kwani wapo wanaosema kua ameitwa wa Kijani kwa sababu Hikma na Busara zake ni zenye kunawirisha Ufaham, ambapo kwa upande mwengine basi anasema Abu Hurayra *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua *Al Khidhr* ameitwa hiyo kwa sababu alikaa kwenye ardhi ambayo ni kame yenye majani makavu na ardhi hio ikawa na rangi ya Kijani kutokana na kuguswa nae.'**

Kwani neno *Al Khidhr* linatokana na neno *Khadhira* ambalo hua linamaanisha Kua na Rangi ya Kijani, Kua na Majani ya rangi ya kijani kilichopea na Kunawiri.

Hivyo Al Khidhr alikua ni Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae amepewa Ilm maalum kupitia kwa njia ya *Wahy* kwa njia ya *Ilham* ambayo hua wanapewa Mitume na Manabii na Waja wema.

Ambapo wanazuoni wanasema kua Al Khidhr alikua akiitwa Balya Ibn Malkan Ibn Flakh Ibn Anmbar Ibn Salakh Ibn Arfakhszyad Ibn Sam Ibn Nuh Ibn Lamek Ibn Mutawasiliykh Ibn Idris Ibn Yard Ibn Mahalail Ibn Qayanyn Ibn Yanasy Ibn Seith Ibn Adam.

Ambapo kwa upande wa *Hujjat ul Islami Mujaddid Ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali basi anatuambia kuhusiana na Ilm aliyokua nayo Al Khidhr kwa kuaianishia aina za Ilm pale aliposema: '**Ama kuhusiana na I'lm basi hua kuna aina mbili. Ambapo ya kwanza hua ni Ilm ambayo hua ni *Taa'lim Al Insan* yaani inayotokana kwa njia ya kufudishwa na Mtu ambayo imegawika katika sehemu mbili**:

Ya kwanza hua ni Kusoma kwa kupitia njia ya kufudishwa na wengine na ya pili hua ni kwa kupitia njia ya Mtu kusoma kwa kujifunza mwenyewe kwa kwa kutumia Ufaham wake.

Aina ya pili ya Ilm hua ni Ilm ambayo hua ni *Taa'alim Al Rabbana* ambayo hii hupatikana kwa kupitia kwa njia ya *Allah Subhanah waTa'ala,* hii nayo pia imegawika katika sehemu mbili ambazo ni:

Ya kwanza hua ni Ilm kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuwashushia Manabii wake ambayo hua inaitwa *Al Ilm Al Anbiyah.*

Ya pili hua ni Ilm kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* moja kwa moja kwa moja kwa waja wake aliowachagua hii hua inaitwa *Al Ilm Al Laduni*'

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuthibitisha katika sehemu ya mwisho wa moja kati ya Aya ndefu za Qur'an kuhusiana na namna anavyowapa Waja wake Ilm kwa kusema:

﴿ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَيُعَلِّمُكُمُ ٱللَّهُ وَٱللَّهُ بِكُلِّ شَيۡءٍ عَلِيمٌ ﴾

Waittaqoo Allaha wayuAAallimukumu Allahu waAllahu bikulli shay-in AAaleemun *(Surat Al Baqara 2:282)*

Tafsir: **Na Muogopeni Allah Na Atakufundisheni Allah Na Allah Juu ya Kila kitu Ni Mwenye Kujua.**

Ambapo tunaona katika aya hii kua Allah Subhanah wa Ta'ala anaahidi kua Mtu yeyote yule atakaekua na Taqwa basi bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamfundisha Ilm ambayo hakuwahi kuijua wala hakuwahi kuisoma au kusomeshwa

Na tunapoayaangalia maneno haya basi tunaona kua Ujinga wa wale wasiokua na Ufahamu na hivyo wao kila siku wanapoambiwa mambo basi hua ni wenye kutaka Vithibitisho vya Aya na Hadith kwani vyenginevyo basi kwao wao itakua ni Bidaa au Uzushi japo jambo hilo likiwa ni Jema.

Hivyo Waislam inabidi tujue kua kuna Mambo ambayo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam hakuyafanya wala hakuyasema.

Lakini kuna Maimamu wanaoaminika kutokana na Ucha Mungu wao basi Wameyasema kua ni bora kuyafanya katika Siku fulani au ni bora kuyafanya kwa Mpangilio fulani.n.k

Hivyo hawa Maimamu hua hawazushi bali wanasema kutokana na Ucha Mungu wao kutokana na kua ni wenye kufundishwa na Mola wao. Kwani ndio maana Imam Umar Al Bulqini alipoulizwa Hivi wewe umeipata Ilm yako yote hii?

Basi nae akasema:

﴿وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَيُعَلِّمُكُمُ ٱللَّهُ وَٱللَّهُ بِكُلِّ شَيۡءٍ عَلِيمٌ﴾

Na ndio maana unakuta Watu kama Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhamamd Ibn Muhammad Ibn Muhamamd Al Ghazali, Sultani Al Mutakkalimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi, Shaykh Al Akbar Imam Ibn Arabi, Imam Abd Al Qadir Al Jaylani, Imam Al Sulami, Imam Al Shaarani, Imam Al Qushayr, Imam Al Shadhili, Imam Alawi Al Haddad, Imam Al Nabhani, Imam Al Barzanji, n.k

Kuna mambo ambayo wameyasema, mipangilio ambayo wameipanga kwa kwa ajili ya mambo fulani yenye Manufaa kwa Jamii za Kiislam.

Kwa mfano aina fulani za Awrad (Nyiradi) za Nyakati fulani, Dhikr Allah za aina fulani kwa mda fulani, Siku fulani za Kufunga, Mpangilio fulani wa Kisomo cha Dua, Aya au Sura za Qur'an, Kisomo fulani ndani ya Sala Fulani, n.k kutokana na Kujua kwao baada ya kufundishwa na Mola wao.

Kwani asieamini kuhusiana na Ilm za Aina hii basi hua ni Mjinga asiejua na asiefahamu maana ya Aya hii ya ndani ya 282 ya Surat Al Baqara. Kwani amesema Imam Malik Ibn Anas kua: **'Yule mtu mwenye Ilm ya Dhahir basi hua ni mwenye kua na uwezo wa kupata Ilm ya Ghayb'**

Na hii ni kwa sababu kama Mtu atakua ni mwenye kuifanyia kazi Ilm ya Dhahir basi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atampa mtu huyo na Ilm ya Ghayb

Ambapo kwa Upande wa Imam Abu Talib Al Makki basi yeye amesema kua: **'Ilm ya Dhahir na Ilm ya Batin hua ni vitu visivyotenganishika kwani hua ni sawa na Mwili wa Ibn Adam na Moyo uliomo ndani yake. Hivyo kama ukiwa unayo Ilm ya Dhahir basi bila ya shaka Ilm ya Batin hua ni yenye kutiririka ndani ya Moyo wako wenye kujaa hikma kuelekea kwenye Nyoyo za wengine'**

Na tunapozungumzia kuhusiana na Ilm ya Batin basi hua pia ndio Ilm Ladun ambayo aliyopewa Al Khidhr na kama ile aliyokua nayo Asif Ibn Barkhiya Aliekua Waziri wa Nabii Sulayman aliekileta kiti cha Bilqis kwa kasi ya kupepesa macho tu.

Kwani neno Batin linatokana na neno Batana ambalo humaanisha Kuingia ndani kabisa ya Kitu, Kufichikana, Kupenya Ndani, Kumchagua Mtu na kumfanya kua mtu wa Karibu sana ambae ni mwenye takriban kujua kila kitu chako. Neno Batana ndio lililotoa neno Butuni yaani Tumbo au Uutumbo ambao hukaa Ndani.

Hivyo Ilm Laduni ambayo ni Ilm kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuelekea kwa Mja wake Kutokana na ukaribu wa Mja huyo kwa Mola wake kiutiifu na kimapenzi kutokana na kua na Ilm juu ya Mola wake na hivyo hua ni mwenye kumjua hasa Mola wake.

Na kutokana na Mja kumjua kwake huko Mola wake na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuujua na kuuthamini Ukaribu huo basi Kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* huamua kumpa Ilm ya Batin yaani Ilm ya ndani ya mambo yasiyojulikana na wengineo.

Na hapa sasa tunarudi tena kwa mwenyewe yule kiumbe ambae aliekua na sifa kama Mtu alieoneshwa Maktaba ya Ilm na Mola wake na hivyo nae akaingia ndani yake na kukaa na kuikomba Ilm hio kwani kila akiikomba basi ndio kwanza alikua akijiona kua bado hajatosheka kwani hana Ilm hata chembe.

Naam..huyu si mwengine isipokua Hujjat Ul Islami Imam Al Shafii Al Thani Mujaddi Ad Din Az Zukhruf Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii ambae yeye anatuambia tena kua; **'Fahamuni kua Ilm Ya Kiakhera hua ni Ilm za aina mbili ambapo ya kwanza hua ni ile ijulikanayo kama Ilm Mukashifi ambayo hupatikana kwa nji ya Uvumbuzi na Kugundua, ambapo malengo ya Ilm zote hua ni kwa ajili ya Kuipata Ilm hii. Kisha aina ya pili hua ni Ilm Ilajiyyah ambayo ni Ilm inayotisha kwani kwa mtu asiekua na ilm kisha akaipata Ilm hii basi Atapotoka na Kukufuru.Hivyo kitu kinachotakiwa katika Ilm hii ni Kuiamini tu na si zaidi. Na watu wenye mambo ya Uzushi hua kamwe hawawezi kua nayo Ilm hii. Kwani Ilm hii hua ni yenye Kuchipua na kuchomoza kutoka kwenye Nyoyo zilizokua safi kabisa, yaani kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna aina mbili za Ilm ambazo zina siri kubwa sana na ni wale wenye hikma ya hali ya juu tu ndio wanaozijua ilm hizo. Hivyo Ilm ya Dhahir inahitajika kwa ajili ya Kutii Maamrisho na Kuachana na Makatazo ya *Allah Subhanah wa Ta'al*a na hupatikana kwa kusoma na kuifanyia kazi na kisha baada ya hapo ndio hupatikana Ilm Al Laduni.'**

Ambapo kuhusiana na Al Khidhr kua ni Nabii ama La basi anasema *Sultan Al Mutakallimin Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: '**Al Khidhr alikua ni Mja aliechaguliwa Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupata Unabii kwa njia ya Rehma na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kuhusiana nae kua *'Ataynahu Rahmah' yaani Tumempa Rehma* . Hii hua ni**

alama ya Unabii kwani kila '*Nubuwah*' yaani Unabii hua ni Rehma lakini si kila Rehma hua Unabii, na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kua '*WaAAallamnahu min ladunna Aailman* yaani *Na tukamfundisha kutoka kwetu I'lmu.*' Ambapo hii inamaanisha kua mja huyu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakufundishwa na Mtu wala na Mwalimu bali alifundishwa moja kwa moja na *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Ambapo kwa upande wa *Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din* Abu Bakr Ibn Arabi basi yeye anasem kua: **'Mawalii hua wana I'lm ambazo hua hazipatikani kwa Mitume, kwani I'lm aliyokua nayo Al Khidhr ambayo Nabii Musa hakua nayo ilikua ni *Ilm Ladduni* ambayo ni I'lm iliyofichikana. Hii hua ni Ilm ambayo ipo kwenye *harfu Waw* ambayo hua ni harfu iliyofichikana baina ya harfu *Kaf* na harfu *Nun* katika neno la *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambalo ni *KuN* yaani Kua.**

Kwani unapolitamka neno *KuN* basi hua lina harfu tatu ambapo ya kwanza ni harfu iliyowazi na ya mwisho ni harfu Nun ambayo pia iko wazi na katikati yake kuna harfu *Waw* ambayo imefichikana, na hivyo neno hili hua linajumuisha yaliyowazi na yaliyofichikana. Na hivyo kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie Mungu wa Haki na ndie mwenye sifa zinazobainisha yaliyowazi na yaliyofichikana.

Na pia hua linamaanisha *Insan Al Kamil* yaani Mtu aliekamilia ambae ndie Khalifa wake hapa ardhini na mpangilio wake ambao *Allah Subhanh wa Ta'ala* anaudhihirisha katika maneno yake ambayo anasema:

﴿إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَآ أَرَدْنَاهُ أَن نَّقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ﴾

Innama qawluna lishay-in idha aradnahu an naqoola lahu kun fayakoonu *(Surat An Nahl 16:40)*

Tafsir: ***Kwa hakika! Kauli yetu juu kitu tunachokikusudia, ni kukiambia Kua na kinakua***

Hivyo ametoa Herufi tatu, mbili zilizo wazi na moja iliyofichikana, ambapo katika hali hii basi *Insan Al Kamil* yani Mtu aliekamilia hua ni mwenye kua na Mamlaka ya Ukhalifa wa haki kama ilivyo baina ya herufi ya kabla yake na baada yake katika neno Kun.'

Kwa upande mwengine basi kuna wasemao kua *Ilm Ladunni* hua pia ndio ile inayojulikana kama *Ilm Al Batin* (yaani Ilm Iliyofichikana na hivyo hua inajulikana na watu waliojaaliwa tu na *Allah Subhanah wa Ta'ala*) ambayo hua ni tofauti na *Ilm Adh Dhahir* ambayo hua ni Ilm iliyo wazi, kwani *Ilm Adh Dhahir* hua inapatikana kutokana na kusomeshwa na kusoma vitabu ambapo *Ilm Batin* hutokana na mtu husika kua ni mwenye kufanyia kazi yale anayoyajua yanayotokana na *Ilm Adh Dhahir* na hivyo hua na uzoefu ambao humpelekea kua na uwezo wa kufungua Milango ya kua na *Ilm Batin.*

Hii inakua kama vile ambavyo amesema Abu Hurayra *Radhi Allahu Anhu* katika hadith iliyomo kwenye *Sahih Bukhari* ambayo anasema kua yeye amesomeshwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Ilm za aina mbili yaani *Ilm Adh Dhahir* ambayo ni I'lm ya Hadith na *Ilm Al Batin* ambayo ni siri yake, hadithi hio inasema kua; **'Hakika mimi nimepata Ilm za aina mbili kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, ya kwanza tayari nimeshaisambaza ama hii ya pili kama nikiinukuu basi nitakatwa Shingo.'**

Ama kuhusiana na maisha yake anayoishi na uhai wake Al Khidhr basi kuna kutofautiana kimtizamo kwani kuna mitizamo mingi sana kuhusiana nae kwani kuna wasemao kua alianzia kuishi uhai wake

duniani katika kipindi cha Nabii Adam na ndie aliemzika Nabii Adam na kuna wasemao kua aliishi pia katika wakati wa Nabii Nuh, na pia alikuwa akiishi katika kipindi cha Nabii Ibrahim, na katika kisa cha Dhul Qarnayn na katika hiki kisa cha Nabii Musa na pia yumo katika kisa cha Nabii Sulayman na hata katika kisa cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pia yumo, hivyo kama nikimuelezea kwa kina kuhusiana na Maisha yake na Uhai wake basi bila ya shaka itabidi niandike kitabu kizima peke yake.

Kwa hivyo tutamzungumzia kwa juu juu kuhusiana na uhai wake ili tupate kufaham kuhusiana nae japo kidogo katika kisa hiki cha Nabii Musa. Ambapo inabidi tufaham kua Wanazuoni wanasema kua kimaumbile Uhai umegawika katika Darja tano tofauti ambazo ni:

1- Darja ya Kwanza ambayo ni ya Uhai wa Maisha tunaoishi sisi viumbe Ibn Adam wa kawaida ambao hua ni wenye mipaka ya mahitajio ya Kimaumbile ambayo yanahitajikana kila kumbe Ibn Adam.

2- Darja ya Pili ambayo ni ya Uhai wanaoishi Viumbe kama Al Khidr na Nabii Ilyas ambao hua una mipaka lakini haifikii mipaka iliyomo katika darja ya Uhai wa aina ya kwanza, kwani darja hii kimaumbile hua inawaruhusu viumbe wake kua katika sehemu tofauti katika wakati mmoja, na hivyo hua wanaweza kula na kunywa kama sisi lakini hapo hapo huwa hawafanya hivyo kwa sababu ya Ulazima kama ilivyo kwetu sisi ambao ili tuishi basi kula hua ni lazima lakini kwao wao hua si lazima kufanya hivyo, kwani wanaweza kuishi bila ya kula kwa mda mrefu zaidi na bila ya kudhurika kiafya na hivyo basi hata maumbile ya miili yao hua si yenye kuathirika na athari ya wakati kwa mfano kuzeeka, kutoweka katika sehemu moja na kutokea katika sehemu nyengine kwa haraka sana. n.k

3- Darja ya Tatu ambayo ni ya Uhai wa maisha ya Viumbe kama Nabii Idris na Nabii Isa. Ambao wao maumbile yao yapo katika hali ambayo haihitaji mahitajio ya Kibinadam kwani maumbile yao hua yapo kama maumbile ya Kimalaika ambao wanaishi Mbinguni lakini wakiwa na miili ya Kibinadam.

***4*- Darja ya Nne ambayo ni ya Uhai wa Maisha ya Waumini waliofanikiwa kupata Ushahidi baada ya kufariki kutokana na kujitolea muhanga kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Hivyo hua wamejaaliwa wapo katka mazingira ya Kua ni wenye kuishi kama wlivyokua wakiishi Ulimwenguni lakini wakiwa na raha ya kila aina ndani yake, na hivyo hua hawajioni kua wamekufa kama vile ambavyo wanavyojiona Ibn Adam wengine walioko Makaburini baada ya kufariki kwao. Yaani ili kuelewa vizuri hali hii basi kwa kifupi tuchukulie mfano wa hali ya mtu ambae amelala na kisha akaota yuko Peponi na hivyo hua ni mwenye kuomba asizindukane katika ndoto yake kutokana na uzuri wa ndoto hio.**

***5*- Darja ya Tano ambayo ni ya Uhai wa Maisha ya Kiroho baada ya kufariki na kuingia Kaburini, ambayo kwa upande mwengine hua pia ni ya Mtu aliekufa na akajijua kua amekufa na hivyo hua anaishi maisha ya kiroho ambayo mfano wake pia hua ni kama wa mtu alielala na kisha akaanza kuota ndani ya usingizi wake huo, ambapo hali yake katika mazingira hayo ya kaburini hua yanategemea na namna alivyokua akiishi Duniani kabla ya kuingia Kaburini.**

Yaani kama alikua ni Mtiifu kwa Mola wake basi atakua katika hali nzuri ambayo inafanana na ya Mashahidi na hivyo atakua katika hali kama ya mtu ambae anaota na kisha kutokana na raha na uzuri wa Ndoto hio kua yuko Peponi basi ataomba ndoto hio iendelee milele.

Lakini kama alikua si mwenye kua na Utiifu kwa Mola wake na hivyo kua ni muasi basi ali ya mtu huyu mfano wake hua ni kama mtu alielala na kisha akaota ndoto ya jinamizi na yenye kutisha kwani anapata adhabu sawia na za watu wa Mtoni na hivyo hua anataka kuzindukana lakini sasa haiwezekani, kwa sababu anaezindukana kutoka ndotoni hua ni alie hai tu.

Hivyo basi kulingana na mitizamo ya Wanazuoni tunaona kua Al Khidhr yupo hai katika hali ya maumbile ya Uhai wa darja ya pili ambayo ni hali aliyokua nayo Nabii Ilyas pia.

Na ndio maana Wanazuoni wa Tafsir wamekua wakisema kua: **'Kuna Manabii wanne ambao wapo hai, ambapo wawili kati yao wanaishi Duniani na wawili wanaishi Mbinguni. Wanaoishi Duniani ni Al Khidhr na Ilyas na wanaishi Mbinguni ni Idris na Isa.**'

akasema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Amr Ibn Dinar kua; '**Al Khidhr na Ilyas watakua hai wanaoishi hapa Duniani hadi pale itakapokua hakuna Qur'an Duniani**'

Ambapo amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Al Khidhr anaishi Baharini na Ilyas anaishi Ardhini ambapo wawili hawa hua nin wenye kukutana kila siku usiku katika Ukuta wa Dhul Qarnayn baina ya Watu na Juj wa Majuj, na pia hua wanafanya Ibada ya Hija pamoja kila mwaka na wanakunywa maji ya Zamzam ambayo huwatosheleza kwa mwaka mzima.**'

Akasema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* tena pia kua: '**Katika Maziko ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikuja mtu ambae ana ndevu za rangi nyekundu, ambae alipita huku akiwa analia na kisha akawageukia Masahaba na akasema: 'Kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndiko kwenye Uliwazo wa kila Mtihani na fidia ya kila kilichopotea hivyo mgeukieni Allah kwa kuomba Msamaha na kwa kila mnachokitamani.**' **Hivyo Masahaba wakaulizana kama wanamjua mu huyo, ambapo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* na Ali Ibn Abi Talib *Radhih Allahu Anhu* wakasema: 'Naam yule ni ndugu yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, *Al Khidhr Alayhi Salam.*'**

Na akasema tena Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mimi nilitoka siku moja na *Rasul Alla Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo mara ghafla tukasiia sauti kutoka kwa baadhi ya watu, ambpo nae akasema**: **'Anas hebu kaangalie kuna nini tena?' Hivyo mimi nikaenda na nilipofika nikakuta kuna mtu anaomba Dua kwa kusema kua: 'Ya Allah! Nijaalie mimi kua ni miongoni mwa watu wa Ummah wa Muhammad ambao umeujaalia kua ni wenye kuingizwa kwenye rehma zako na kusamehewa, na maombi yao kua ni yenye kukubaliwa, na toba zao kukubaliwa'**

Hivyo mimi nikarudi kwa *Rasul Allah Salallau A'layhi wa Salam* na kumwambia kuhusiana na niliyoyaona na kuniambia kua: 'Nenda kamwambie kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anakuuliza: 'Wewe ni Nani?' Nami nikarudi kwa mu huyo na kumpa ujumbe wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nae akasema: 'Mwambie kua mimi ni Ndugu yake, yaani Al Khidr na mwambie kua aniombee kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua anijaalie niwe miongoni mwa watu wa Ummah wa Muhammad ambao umeujaalia kua ni wenye kuingizwa kwenye

rehma zako na kusamehewa, na maombi yao kua ni yenye kukubaliwa, na toba zao kukubaliwa'''

Ama kwa upande wa *Shaykh al Islami Muhyi Ad Din* Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi basi anasema kuhusiana na Al Khidhr kua: '**Ama kuhusiana na yaliyotufikia sisi kuhusiana na Al Khidhr kutoka kwa Wanafiqh wanaokubalika ni kua: 'Kuhusiana na kisa cha Al Khidhr kumtembelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa salam* baada ya kufariki kwake basi ni kua imenukuliwa na Imam Al Shafii katika kitabu chake cha Al Umm kupitia katika sanad ambayo ni dhaifu ya nukuu hio. Ambamo hata hivyo (Imam Al Shafii) hakutaja jina la Al Khidhr bali alisema tu kua: 'Masahaba walisikia kua kuna mtu aliesema kadha wa kadha. 'Jina la Al Khidhr halikutajwa na Imam Al Shafii isipokua baadhi ya Wanafiqh wetu ambao ni wenye uthibitisho wao wenyewe ndio wakaandika jina la Al Khidhr. Hivyo Mtizamo sahih ni kua Al Khidhr yuko hai na anaishi na hii ni kulingana na wengi miongoni mwa wanazuoni.**''

Na kwa upande wa *Shaykh al Islami Imam* Shams Ad Din Al Ramli *Al Shafii* basi yeye anasema kuhusiana na Al Khidhr na Nabii Ilyas kua: '**Al Khidhr ni Nabii na wala si Walii na hii ni kulingana na Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni, kama vile ambavyo alivyosema Al Khidhr ndani ya Qur'an kua: 'Sikufanya haya kwa hiari yangu' na kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua: 'Tumempa Rehma kutoka kwetu' ambayo hua inamaanisha kua ni Wahy na Unabii'**

'Na hivyo Kauli hii ya kua amejaaliwa Rehma ambayo inamaanisha *Wahy* na Unabii hua haimaanishi kua ni Uwalii. Na huo ndio uhalisi ulivyo hata kama baadhi ya Wanazuoni wanasema kua si Nabii. Na mtizamo sahih ni kua bado yuko hai kama alivyosema Imam Ibn Salah, kua: 'Wengi miongoni mwa Wanazuoni wamekubaliana kua yuko hai kwani hata watu wa kawaida wanaamini juu ya hili' na Imam An Nawawi amesem kua: 'Wengi miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua Al Khidhr anaishi miongoni mwetu, na juu ya hili pia wanakubaliana Watu wenye Ilm ya *Tasawwuf* na watu Wacha Mungu, ambao wamethibitisha kua wamemuona kwa kupitia njia ya kupata ufunuo, na wakakutana nae katika hali ya kawaida, na kupata Ilm kutoka kwake, baada ya kumuuliza masuali na kupata majibu ya masuali hayo kutoka kwake na pia kutokana na kuonekana kwake katika sehemu takatifu mara nyingi sana. Hivyo basi Al Khidhr ni Ibn Adam na wala si Malaika na sehemu ya makazi yake yapo kama yalipo makazi ya Ilyas ambapo ni katika ardhi ya Uarabuni.''

Ambapo anasema Imam Abd Raḥmān Ibn Alī Ibn. Muḥammad Abu Al Farash Ibn Al Jawzy kua: **'Bilal Al Khawas alikutana na Al Khidhr na kumuuliza: 'Jee unasemaje kuhusiana na Imam Al Shafii' Al Khidhr akasema: 'Hakika yeye Al Shafii ni Nguzo ya Mawalii' Bilal Al Khawas akauliza: 'Na Ahmad Ibn Hnabal?' Al Khiudhr akasema: 'Yeye ni Siddiq''**

Na kwa upande wa Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Abd Rahman Al Sakhawi basi anasema kua: '**Ni jambo lialojulikana sana ua An Nawawi alikua akikutana na na Al Khidhr na kuzungumza nae kuhusiana na mengi katika Ufunuo wake**' ambapo Imam An Nawawi alikua kumwita *Al Khidhr* kwa jina la Abu Al Abbas.

Naam, hio ni kwa ufupi kuhusiana na Uhai na Maisha ya Al Khidhr, hivyo tunarudi kwa Nabii Musa katika sehemu aliyokutana na Al Khidhr katika kisa kinachoitwa pia kama Qisa Al mustaqila ni kisa ambacho kinaupekee wa kujitegemea katika kuelezewa kwake, na kisa cha Nabii Musana Al Khidr kimeitwa hivyo kwa sababu ni kisa ambacho kimezungumziwa katika Surat Al Kahf katika hali ya kujitegemea peke yake tangu mwanzo hadi mwisho wake.

QISA AL MUSTAQILLA - NABII MUSA NA AL KHIDHR

Nabii Musa na Joshua wakamkuta Al Khidhr akiwa anasali katika Msala wa rangi ya Kijani ambao unaelea juu ya maji, wakamsubiri mpaka alipomaliza kisha wakamsalimia na Al Khidhr kwa kusema: '***Asalaam Alaykum***'. Na Al Khidhr akaitikia salam hio kwa kusema: '***Wa Alaykum Salaam* ewe Mtume wa Bani Israil**' Nabii Musa akashangaa na kumuuliza Al Khidhr: '**Umejuaje kua mimi ni Mtume wa Bani Israil?**'

Al Khidhr akasema: '**Aliekutuma kwangu ndie alieniambia kua nani anakuja kwangu**' na kisha Al Khidhr akamwambia Nabii Musa: '**Ewe Musa kama umekuja kuuliza suali basi uliza, na usikilize jibu lake, kisha uendelee na majukumu yako, nami niendelee na majukumu yangu, ili usinipelekee mimi kua ni mwenye kusimamisha majukumu yangu mbele ya Mola wangu, na pia usijipelekee wewe ambae ni Mtume mwenye majukumu makubwa zaidi mbele ya Mola wako,kua ni mwenye kusimamisha majukumu yako mbele ya Mola wako, nami sitaki kua ni mwenye kukosea katika kutekeleza majukumu yangu.**'

Nabii Musa akasema; '**La, Hakuna suali, ila Mola wangu amenituma nije kwako ili nipate kujifunza miongoni mwa Hikma alizokuajaalia wewe kua nazo**.'

Wakati wanazungumza mara akatokea Ndege ambae akanywa maji na kisha akaondoka, Al Khidhr akasema: '**Ewe Musa! Kua muangalifu kwani wewe ni mwenye Ilm zaidi miongoni mwa watu wa Bani Israil na miongoni mwa watu wa Ulimwenguni katika wakati huu, lakini Ilm yako na yangu na ya waliotangulia kabla yetu na ya watakaokuja baada yetu basi hua si zaidi ya maji aliyochukua ndege kwenye mdomo wake kutoka kwenye Bahari**, **ukilinganisha na Ilm ya *Allah Subhanah wa Ta'ala***.'

Nabii Musa akasema kama inavyosema aya ifuatayo:

﴿قَالَ لَهُ مُوسَىٰ هَلْ أَتَّبِعُكَ عَلَىٰ أَن تُعَلِّمَنِ مِمَّا عُلِّمْتَ رُشْداً﴾

Qala lahu moosa hal attabiAAuka AAala an tuAAallimani mimma AAullimta rushdan *(Surat Al Kahf 18:65)*

Tafsir: ***Akasema Musa (kumwambia Al Khidhr): 'Jee nikufate ili upate kunifundisha sehemu ya kile ulichofundishwa kwa uongofu?'***

Kwani aya inatuonesha namna Nabii Musa alivyokua na Unyenyekevu, mbali ya kua yeye Mwenyewe Kimaumbile Nabii Musa alikua ni Mtu ambae Mtata na Mwenye Misimamo na Mkaidi kwa kuwatetea Wale walio chini yake na pia kuetetea haki zake.

Ambapo sifa hizi tunaziona kimaumbile katika Kisa chake na hii ni kwa sababu alilelewa na Fir'awn tangu utotoni mazingira ambayo yalimpelekea kua Matata kwa sababu alikua akiandaliwa kukabiliana na Utata wa Mtu ambae hajawahi kutokea Ulimwenguni yaani Fir'awn

Na ndio Maana Nabii Musa akaua, Nabii Musa alinyanyua Jiwe lililofunika Kisima peke yake wakati jiwe hilo lilikua ni lenye kuhitaji watu 10 kulinyanyua. Nabii Musa alimpiga Kibao *Malakat Al Mauti*, Nabii Musa ndie alietaka kumuona *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Nabii Musa ndie aliemkomalia Nabii

Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* kua arudi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* mara 5 kwa ajili ya kupunguziwa Idadi ya sala kwa ajili yetu.

Na bado kwani zilipofika Sala 5 basi Nabii Musa akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua rudi tena kwa Mola wako upunguziwe Sala hizo kwani watu wako hawatoweza, ambapo *Rasul Allah Salallahu* akasema : **'La Mimi naona haya siwezi tena kurudi kuomba kupinguziwa kwani nishaomba sana.'**

Nabii Musa ndie aliemkabili *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumhoji Kwa kumuuliza Hivi inakuaje ewe Muhammad unasema kua Wanazuoni wako kua ni sawa na Mitume wa Banii Israil. Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akathibitishia kwa kumuita Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammd Al Ghazali na Nabii Musa akamhoji Imam Al Ghazali na kujithibitishia ukweli huo.

Kama ilivyoelezewa na Imam Abu Hasan Al Shadhili ambae alienda katika ardhi ya Al Quds na alipofika katika Masjid Al Aqsa basi kuna la Mlango wa chumba linaloitwa *Baab Al Ghazal* ambamo ndani yake ndimo alimoishi Hujjat Ul Islam Imam Al Ghazali kwa mda wa miaka 10 na kuandika ndani yake kitabu cha Ihya Ulum Ad Din ambacho Imam Al Sadafi anasema kua kwa mfano itokezee kua Qur'an itoweke na Vitabu vyote vya hadith vitoweke kisha ibakie hio Ihya ya Imam Al Ghazali tu peke yake na kisha Waislan wakaisoma basi Waislam wanakuja juu upya na Imani yao na ndio maana Maimamu wote wa Tariqa (isipokua Abd Qadir Al Jaylani kwa sababu yeye aliishi kipondi kimoja na Imam Al Ghazali) basi baada ya kuhifadhi Qur'an na vitabu vya Hadith basi wanainywa Ihya Ulum Ad Din yote ya Imam Al Ghazal ndani ya nyoyo zao..yaani huwezi kua Imam Muanzilishi wa Tariqa bila kuihifadhi Qur'an, Hadith na Ihya Ulim Ad Din.

Hivyo kina Imam Al Shadhili wa Shadhiliya, Imam Alawi Al Haddad wa Alawiyyah, Imam An Naqshbandi wa Naqshbandiya, Imam Al Askari wa Askarriyah na wengineo wote wameinywa Ihya ulum Ad Din.

Sasa Imam Al Shadhili alipoingia kwenye Chumba hicho cha Imam Al Ghazali basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamfunulia Ulimwengu alioko *Hujjat Ul Islami* baada ya kufariki kwake ambapo ndani yake Imam Al Shadhili akamuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa amekaa na Mitume wenzake wakiwemo wa Banii Israil wote.

Kisha akamuona Nabii Musa akimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: '**Ewe Muhammad, hivi inakuaje hadi ukasema kua Wanazuoni wako ni Warithi wa Mitume? Hivi Jee hii inamaanisha kua Wanazuoni wako ni sawa na sisi Mitume wa Bani Israil?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akatabasam na kisha akasema: '**Naam ewe Musa! Au unataka uthibitisho?'**

Nabii Musa akasema: '**Naam'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: '**Uko wapi ewe Al Ghazali? Hebu njoo hapa'**

Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazal akaingia kwenye Hadhara ya Mitume hao wa Allah Subhanah wa Ta'ala na na kuelekea mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kutoa Salam na Mitume hao wakaitikia.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akamuelekeza kwa Nabii Musa na kusema: '**Uthibitisho wangu huo hapo'**

Imam Al Ghazali akawa anaangaliana na Nabii Musa, Nabii Musa akamuangalia Imam Al Ghazal na kisha akamuuliza: '**Wewe ndio nani?'**

Hujjat Ul Islami akasema: '**Mimi ni Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii'**

Nabii Musa akakunja na kusema: '**Sikukuuliza mimi Nasaba yako bali nimekuuliza tu wewe ndio Nani?'**

Hujjat Ul Imam Al Ghazali *akamgeukia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema: '**Ya Rasul Allah! Jee Nimajibu Kalimu Allah au Nisijibu?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akatabasam na kusema: **'Kua huru ewe Al Ghazal na Mjibu'**

Hujjat Ul Islami Imam Al Ghazali akasema : '**Kumbuka ya Kallimu Allah Musa kua pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipokuuliza:**

﴿وَمَا تِلْكَ بِيَمِينِكَ يٰمُوسَىٰ﴾

Wama Tilka Biyaminiika ya Musa*? (Surat Ta-Ha 20-17)*

*Tafsir**: Na ni nini Hicho Mkononi mwako ewe Musa?***

Nawe ukajibu:

﴿ هِيَ عَصَايَ أَتَوَكَّأُ عَلَيْهَا وَأَهُشُّ بِهَا عَلَىٰ غَنَمِي وَلِيَ فِيهَا مَآرِبُ أُخْرَىٰ﴾

Hiya Aasaya Atawakkau Aalayha Waahushu biha Aala al ghanami Waliya fiiha maribu al ukhra *(Surat Ta-Ha 20-18)*

*Tafsir**: Hii ni fimbo yangu Ambayo hua naiegemea Na naitumia kupukutishia (Majani) kwa ajili ya Kondoo wangu na kutokana nayo hua nafanyia mambo mengi***

'Hivyo ewe Musa! Umesahau kua mbali ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikua anajua kila kitu kuhusiana na Fimbo yako, lakini alikuukiza suali moja tu ambalo ni: 'Ni nini hicho mkononi mwako?'

'Ambapo ulikua unatajiwa ujibu kua hii ni fimbo.'

'Lakini wewe ukajibu hii ni fimbo yangu nnayoitumia kwa kuiegemea. Kwa kuangushia majani wanyama wangu na pia naitumia kwa matumizi mengine'

Hapo Nabii Musa akakaa kimya, hajui aseme nini kwani ameshashindwa kihoja, hivyo Nabii Musa akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: 'Kwa hakaka hujakosea ewe Muhammad Uko sahih kua Wanazuoni wako ni Warithi wa Mitume'

Rasul Allah Salallahu Alayhi w Salam **akawauliza Manabii na Mitume wa Banii Israil: Hivi Jee katika watu wote wa Ummah wenu yupo Mtu kama Al Ghazali?**

Nabii Musa na Nabii Isa wakajibu: 'La Hakuna.'

Naam..hayo ndio aliyoonyeshwa Imam Abu Hasan Al Shadhili na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Hujjat ul Islami Imam Al Ghazali na Nabii Musa.

Na pia Nabii Musa pia ndie aliemhoji Nabii Adam na kumuuliza: '**Hivi kwanini wewe Adam ukapelekea sisi kua ni wenye kushushwa Ulimwenguni kuja kujaribiwa wakati ilikua tuwe Peponi raha mustarehe?'**

Ambapo Nabii Adam akamwambia Nabii Musa: **'Ewe Musa hakika wewe ulijaaliwa kua ni mwenye kuzungumza na *Allah Subhanah wa Ta'ala,* hiyvo kanini hukumuuliza wewe kuhusiana na suali hilo?. Hivyo Inakuaje Ewe Musa unanilaumu mimi juu jambo ambalo *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikua ameshalikadiria kua litokee?' Nabii Musa akakaa kimya.**

Naam..hio ni mifano tu ya Ujabari na utata wa *Nabiyyu Allahi* Musa Alayhi Salam, na hii ni kwa sababu ya maumbile yake yalikua ni kwa ajili ya kukabiliana kwa Ujabari dhidi ya Fir'awn amabe alikua ni Mtata mwenye Kibr sana. Hivyo kila mmoja wetu anaemwita Mtoto wake Musa basi na atafakkar yalivyokua mazito Majukumu ya Nabii Musa.

Lakini sio hivyo tu kwani mbali ya Ujabari wake. Ukaidi wake na Utata wake pale inapostahiki lakini Nabii Musa alikua ni Mcha Mungu na pia ni Mtu Mwenye Unyenyekevu pale inapostahiki kua na Unyenyekevu kama inavyotuonesha Aya kulingana na maneno aliyoyatumia kumuomba Al Khidhr.

Ambapo aya inatufahamisha namna inavyotakiwa mtu mwenye kutafuta Ilm awe na hali gani mbele ya yule anaetaka kupata Ilm kutoka kwake, yaani kama alivyosema *Mujaddid Ad Dini Imam Fakhr Ad Din Al Razi* kuhusiana na aya hii kua : **'Aya inatuonesha kua Mwanafunzi anatakiwa awe na unyenyekevu mbele ya Mwalimu wake**' kwani aya inatuonesha namna Nabii Musa anavyokubaliana na hali ya kua ingawa yeye ni Mtume wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini hapo hapo kuna mambo yeye bado ana ujinga nayo yaani hayajui. Hivyo basi anakubali kua mjinga na hivyo kua ni mwenye kuomba ruhusa ili apate kufundishwa hayo asiyoyajua.

Na kutokana na Nabii Musa kua na hali hio basi Al Khidhr akamuwekewa wazi Nabii Musa kwa kumwabia kua:

﴿قَالَ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْراً ❁ وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَىٰ مَا لَمْ تُحِطْ بِهِ خُبْراً﴾

Qala innaka lan tastateeAAa maAAiya sabran; Wakayfa tasbiru AAala ma lam tuhit bihi khubran*(Surat Al Kahf 18:67-68)*

Tafsir: ***Akasema (Al Khidhr) 'Kwa Hakika wewe hutoweza kua na subira nami; Na vipi utasubira juu ya kile ambacho hujapewa Habari juu yake?'***

Ambapo neno *Hata* hua linamaanisha Kuangalia, Kusimamia, Kulinda, Kuhifadhi, Kuzunguka kama ngao kwa ajili ya kukinga.

Neno *Hata* limetoa neno *Ahata* ambalo humaanisha Kuzunguka Kiufahamu, Kutanabahi kutokana na kujua. Hivyo neno *Tuhi*t hua linamaanisha Kuzunguka kitu kiufaham yaani Kukijua ndani nje.

Na hivyo hapa Nabii Musa alikamua akiambiwa kwa kuhojiwa Na hii inatuonesha kua bila ya shaka Al Khdir alikua akipewa habari na Mola wake kama tutakavyoona hapo baadae katika kisa chetu hiki. Ambapo kutokana na kua ni mwenye kua na Habari juu ya vitu hivyo basi kwake yeye ilikua ni rahisi kujua matokeo ya yale mambo anayoyaona sasa hivi kua baadae matokeo yake yatakuaje.

Na ni maumbile ya Kiibn Adam kuhusiana na kile asichokijua kukiona kua ni cha kijinga na kisichokua na maana wala umuhimu. Na katika kila lifanywalo na mwenzake ambalo kama hulifaham basi unaweza ukamuona mwenzako kua anafanya Ujinga au anafanya israfu au anajitia hasara n.k Na hivyo kutokana na kumjali kwako mtu huyo basi unaweza kushindwa kua na subra nae na hivyo kuona bora kuingilia ndani ya mipango yake kwa kumkosoa au kumlaumu.

Hivyo Al Khidhr anamwabia Nabii Musa kua Ilm aliyokua nayo yeye ni tofauti na namna yanavyoonekana maisha kwani yeye ni mwenye kua na habari juu ya yale ambayo wengine hawana habari nayo, na hivyo basi kwake yeye Al Khidhr kutokana na kua na habari ya yasiyojulikana habari yake hua ni mwenye kuweza kuona kuhusiana na kile kinachoonekana kua ni faida kwa wengine kua kwake yeye hua ni hasara, na hasara kua ni faida, na ukatili hua unaweza ukawa ni huruma na kulipa wema kutokana na uovu huweza kua ni Uadilifu, hii yote ni kutokana na Hikma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Hivyo kwa Nabii Musa inaweza ikawa mtihani kwake na hivyo kushindwa kua na Subra juu ya mambo ambayo hana habari nayo wala matokeo yake, lakini Al Khidhr ana habari ya matokeo ya mambo hayo kwani yeye Al Khidhr amepewa Ilm ambayo Nabii Musa hakupewa na hapo hapo Nabii Musa amepewa Ilm zaidi ya Al Khidhr. Hivyo Nabii Musa akasema:

﴿قَالَ سَتَجِدُنِيٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ صَابِراً وَلاَ أَعْصِى لَكَ أَمْراً﴾

Qala satajidunee in shaa Allahu sabiran wala aAAsee laka amran*(Surat Al Kahf 18:69)*

Tafsir: ***Akasema (Nabii Musa) 'In shaa Allah utanikuta mimi kua ni mwenye kua na Subra na wala sitoasi amri yako'.***

Naam..hii ni ahadi ambayo anaitoa Nabii Musa kumwambia Al Khidhr, Huku akiwa ni mwenye kutumia kauli ya In-shaa Allah kama vile ilivyokua kwenye kisa cha Vijana wenye Bustani mbili.

Na kama tunakumbuka basi katika Utangulizi na kuzungumzia Asbab Nuzuli au Sababu ya kushushwa Sura hii basi tuliezea kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitakiwa aelezee kuhusiana na As-hab Al Kahf, Dhulqarnayn na Habari ya Roho. Ambapo nae akaahidi kua kesha ataelezea huku akitegemea kua Malaika Jibril atamshushia Wahy kuhusiana na Majibu hayo, lakini *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* hakusema In-shaa Allah katika kuahidi wake.

Na matokeo yake basi Kesho zikaja na kuondoka hadi ikafikia wiki mbili kiasi ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake wakawa na Wasiwasi mkubwa sana. Lakini katika siku ya 15 basi Malaika Jibril akashuka na Sura hii.

Ambapo tulisema kua tukio hili ni funzo kwetu sisi Waislam kua tusisahau kusema *In-shaa Allah* katika kuahidi kwetu.

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimsahaulisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo haku ni mwenye kusema Inshaa Allah kwa makusudi Ili *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba na Waislam kwa ujumla tupate kujua Umuhimu na athari ya kusema *In-shaa Allah* katika kuahidi kwetu.

Yaani kua unaposema Inshaa Allah basi hua umemkabidhi *Allah Subhanah wa Ta'ala* utekelezwaji wa ahadi yako hio na hivyo inakua rahisi kutekelezeka kwa Rehma zake. Na ndio maana Allah Subhanah wa Ta'ala anarudia tena kauli hii ya *In-shaa Allahu* katika sura hii lakini katika Matukio tofauti ndani yake ili kututilia na sisi mkazo kua tusisahau kusema maneno hayo katika kuahidi kwetu.

Hapa Nabii Musa anaweka wazi kwa kuahidi kua hatomuasi Mwalimu wake huyo kutokana na namna alivyokua na hamu na ari ya kutaka kujifunza kutoka kwake, na hivyo atakua na Subra juu ya kila kitu kitakachotokea, *In-shaa Allah,* yaani kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* akimjaalia kumuwezesha kua na Subra juu ya jambo husika, kwani ingawa Nabii Musa anahesabika kua ni miongoni mwa Manabii wenye Subra na azma kubwa yaani *Ulu ul Azmin minna Rusul* lakini hata hivyo hajui hali itakuaje hapo baadae kwani katika mambo ambayo mtu anaweza akaahidi lakini akashindwa kutimiza ahadi yake hapo baadae kutokana na hali ya mazingira basi ni Subra, yaani mtu unaweza ukaahidi kua utakua mstahmilivu lakini ukweli ni kua kimaumbile basi kila mtu anakua na mipaka yake ya kua na Subra.

Na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akatufundisha ndani ya Qur'an kuomba dua iliyomo ndani ya aya ifuatayo:

﴿لاَ يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفْساً إِلاَّ وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا ٱكْتَسَبَتْ رَبَّنَا لاَ تُؤَاخِذْنَا إِن نَّسِينَآ أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلاَ تَحْمِلْ عَلَيْنَآ إِصْراً كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلاَ تُحَمِّلْنَا مَا لاَ طَاقَةَ لَنَا بِهِ وَٱعْفُ عَنَّا وَٱغْفِرْ لَنَا وَٱرْحَمْنَآ أَنتَ مَوْلاَنَا فَٱنْصُرْنَا عَلَى ٱلْقَوْمِ ٱلْكَافِرِينَ﴾

La yukallifu Allahu nafsan illa wusAAaha laha ma kasabat waAAalayha ma iktasabat rabbana la tu-akhidhna in naseena aw akhta/na rabbana wala tahmil AAalayna isran kama hamaltahu AAala alladheena min qablina rabbana wala tuhammilna ma la taqata lana bihi waoAAfu AAanna waighfir lana wairhamna anta mawlana faonsurna AAala alqawmi alkafireena *(Surat Al Baqara 2:286)*

Tafsir: ***Haikalifishi Allah Nafsi (ya mtu yeyote)isipokua juu ya kile inachokiweza, inalipwa (Nafsi ya Mtu) kutokana na (mema) iliyoyachuma na itaadhibiwa kutokana na (dhambi) ilizozichuma. 'Ewe Mola wetu Usituadhibu kutokana na tulichokisahau au tulichokikosea. Ewe Mola wetu usitubebeshe mizigo kama ulivyowabebesha waliotangulia kabla yetu. Ewe Mola wetu Usitubebeshe mizigo zaidi ya uwezo wetu, Tusamehe na utuingize kweye Msamaha wako na utuingize kwenye Rehma zako kwani wewe ndie Msimamizi wetu na tunusuru dhidi ya watu wenye kukufuru'***

Ambapo katika kutilia mkazo umuhimu wa Dua iliyomo ndani ya aya hii basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kuhusiana na aya hii pamoja na ile kabla ya aya hii yaani aya ya 287 ya *Surat Al Baqara* kua: '**Hakika mimi nimepewa aya mbili ambazo zilikuwemo kwenye hazina iliyomo chini ya Arshi, ambazo hakuwahi kupewa Mtume yeyote yule hapo kabla.**'

Hivyo Al Khidhr akakubaliana na ahadi hio ya Nabii Musa kua atakua na Subra, na kukubali kua atafuatana nae lakini kwa sharti la kumpa tahadhari Nabii Musa kwa kumwambia kua yeye anajua kua inawezekana kua na Subra kutokana na Vitendo vyangu lakini itakua vigumu kutofanya lolote dhidi ya vitendo vyangu hivyo utashindwa kujizuia na utataka kuniuliza masuali, hivyo basi usiniulize chochote mpaka pale mimi mwenyewe nitakapoona kua tayari umefika mda wa kukufafanulia, kama zilivyosema aya:

﴿قَالَ فَإِنِ ٱتَّبَعْتَنِي فَلَا تَسْأَلْنِي عَن شَيْءٍ حَتَّىٰٓ أُحْدِثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا﴾

Qala fa-ini ittabaAAtanee fala tas-alnee AAan shay-in hatta ohditha laka minhu dhikran*(Surat Al Kahf 18:70)*

Tafsir: ***Akasema (Al Khidhr) 'Hivyo kama utanifuata basi usiniulize chochote hadi pale nitakapo kuhadithia mimi kutokana nalo ukumbusho wake'***

Hivyo Al Khidhr akamalizia Ibada zake na kisha akaondoka yeye na Nabii Musa na Joshua ambao walikua wanamfuata nyuma yake, wakatembea kwa takriban masafa ya Parasang 2 yaani Kilomita 12, hivyo kwa kua Nabii Musa na Joshua hawakuwahi kula pale walipokumbuka kuhusiana na Samaki wao na walipomuona kua katoweka basi njaa yao yote ilitoweka, na hawakuihisi tena baada ya kukutana na Al Khidhr mpaka baada ya masafa hayo ya kilomita 12, hivyo Nabii Musa akasema: '**Hakika mimi nimechoka na siwezi kuendelea zaidi na safari, mpaka baada ya kula**' hivyo wakakaa kitako na *Allah Subhanah wa Ta'ala* akajaalia wakaona mbele yao Malaika ambae amekuja na sahani za vyakula, ambapo sahani moja miongoni mwao ilikua imeshapikwa na mbili zikawa bado hazijapikwa, kisha wakaambiwa kua iliyopikwa ni ya Al Khidhr a ambazo hazijapikwa ni za Musa na Joshua.

Nabii Musa akanyanyuka na kutafuta kuni yeye na Joshua kwa ajili ya kukipika chakula chao, huku Al Khidhr akiwa amekaa na kuwasubiri mpaka kilipokua tayari chakula chao na wakakaa na kuanza kula pamoja huku Al Khidhr akiwa ni mwenye kusema: '**Namshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Rehma zake na hikma zake, kwani amemtumia Mja wake mwenye Subra chakula kilichokua kimeshapikwa ili ale bila ya kutumia jitihada yeyote , na akamtumiia mja wake asiekua na Subra chakula ambacho hakijapikwa ili apate kula baada ya kufanya jitihada.**'

Ambapo anasema Ubayy Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Al Khidhr na Nabii Musa waliendelea na safari yao, pembeni ya mwambao wa Bahari, mara wakaliona Jahazi linapita na wakaomba wachukuliwe na Jahazi hilo, wakachukuliwa bila ya Malipo yeyote, na walipofika bali baharini basi Al Khidhr akachukua shoka na kulitoboa Jahazi hilo, ili maji yapate kuingia ndani yake. Hivyo Musa akachukua nguo yake na kuiziba sehemu hio. Nabii Musa akasema: 'Jee umelitoboa ili uwazamishe watu wake? Hakika watu hawa wametuchukua na kutufanyia ukarimu halafu wewe umetoboa tundu kwenye Jahazi lao.**'''

Allah Subhanah wa Ta'ala anatuelezea hali hio katika aya ifuatayo ambayo inasema:

﴿فَٱنطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا رَكِبَا فِي ٱلسَّفِينَةِ خَرَقَهَا قَالَ أَخَرَقْتَهَا لِتُغْرِقَ أَهْلَهَا لَقَدْ جِئْتَ شَيْئًا إِمْرًا﴾

Faintalaqa hatta idha rakiba fee alssafeenati kharaqaha qala akharaqtaha litughriqa ahlaha laqad ji/ta shay-an imran*(Surat Al Kahf 18:71)*

Tafsir: ***Hivyo wakaondoka na kufuatana pamoja mpaka wakapanda kwenye Jahazi. (Al Khidhr) Akalitoboa, akasema (Nabii Musa); 'Umelitoboa ili uwagharikishe watu wake, kwa hakika umefanya jambo kubwa sana (kutokana na Ubaya wake)'***

Aya imetumia neno *Intalaqa* ambalo ni lenye kutokana na neno *Talaqa* hua linamaanisha Talaka, Kuacha, Kua huru kutokana na Ushirika wa kitu, Kukataa kukubaliana juu ya Usimamizi wa kitu. Ambapo neno *Intalaqa* hua linamaanisha Kuanza kufanya Jambo au kitu, Kuanza kuondoka au kua Huru.

Tunapoiangalia aya basi imetumia neno *Imran* ambao limetokana na neno *Amara* ambalo hua ni leneye kumaanisha Amri, Amuru au Jambo ambalo hua ni lenye kusababisha Matokeo fulani baada ya kufanywa kwake. Ambapo tunapozungumzia Amri kwa upande wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi jambo hilo hua halina matokeo yeyote isipokua mazuri na yenye manufaa ndani yake kutokana na hikma zake. Lakini tunapozungumzia Amri kutoka kwa upande wa Kiumbe basi hua kuna yenye kusababsisha Matokeo mazuri na pia hua kuna yenye kusababisha matokeo mabaya.

Hivyo hapa Nabii Musa alikua akimwambia Al Khidhr kua kwa hakika wewe umefanya Jambo lenye Amrisho ambalo ni lenye matokeo makubwa sana kutokana na ubaya wake, kwani litaiamrisha Jahazi hio kuzama na kuwagharikisha watu wote waliomo ndani ya Jahazi hilo ambao waliwasaidia wao hapo kabla.

Na anasema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua; '**Nabii Musa akasema ndani ya Nafsi yake, Hivi nnafanya nini mie na Mtu huyu, wakati kama ningekua na watu wa Bani Israil basi ningekua nawasomea *Tawrat* sasa hivi na kuwaamrisha kufanya mema na wangekua wananitii.**'

Ambapo Al Khidhr akamwambia Nabii Musa: '**Jee nikuambie ulikua unasema nini ndani ya Nafsi yako?**' Nabii Musa akasema: '**Naam, niambie**' Al Khidhr akasema: '**Ulikua unasema kua :** '**Hivi nnafanya nini mie na Mtu huyu, wakati kama ningekua na watu wa Bani Israil basi ningekua nawasomea *Tawrat* sasa hivi na kuwaamrisha kufanya mema na wangekua wananitii**'' Nabii Musa akakaa kimya.

Wanazuoni wanasema kua kutokana na aya hii ya Al Khidhr kuonesha kua ni mwenye kulitoboa Jahazi basi ndani yake ndio tunapata **Uthibitisho wa Hukmu ndani yake ya kua Msimamizi wa Kitu au Mali ya Yatima Mali ya Mtu wa karibu yake au alie chini ya Mamlaka yake basi hua anaruhusika kuipunguza au kuizuia kutompa pale anapoona kua kufanya hivyo katika wakati huo kutakua na manufaa juu ya mwenye mali hio, labda kwa mfano kwa kuogopa kua akimkabidhi Mtu huyo basi labda ataifanyia Israfu na ataituma katika hali isiyokubalika kisharia na kupelekea kujiangamiza au kusababisha maasi kwa Mola wake.**

Hivyo Nabii Musa alipomuona Al Khidhr anatoboa Jahazi basi akashtuka sana na kuona huyu Al Khidhr sasa anataka kusababisha maafa makubwa sana, kwani anataka kuwazamisha watu wote waliomo ndani ya Jahazi na hii ni kwa sababu Nabii Musa alikua amesahau kua sio kila kinachotiwa kwenye Maji kikawa na kisha kikatobolewa basi hua ni chenye kuzama, kwani hata Yuhanz ambae ni mama yake Nabii Musa basi aliamrishwa na Mola wake kua amtie kwenye kisanduku Nabii Musa kisha amtie Mtoni huku akiwa ameachia kitundu kama sehemu ya kupitia hewa ndani ya kisanduku hicho, na ada ya kisanduku hicho kutiwa mtoni basi Nabii Musa hakua ni mwenye kuzama bali alikua

ndani ya Rehma baada yake na matokeo yake akapata mafanikio kwa kuokotwa na kulelewa ndani ya Kasri la Kifalme, kama zilivyosema aya:

﴿أَنِ ٱقْذِفِيهِ فِي ٱلتَّابُوتِ فَٱقْذِفِيهِ فِي ٱلْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ ٱلْيَمُّ بِٱلسَّاحِلِ يَأْخُذْهُ عَدُوٌّ لِّي وَعَدُوٌّ لَّهُ وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِّنِّي وَلِتُصْنَعَ عَلَىٰ عَيْنِيٓ﴾

Ani iqdhifeehi fee alttabooti faiqdhifeehi fee alyammi falyulqihi alyammu bialssahili ya/khudhhu AAaduwwun lee waAAaduwwun lahu waalqaytu AAalayka mahabbatan minnee walitusnaAAa AAala AAaynee *(Surat Al Ta-Ha 20:39)*

Tafsir: ***(Tukamwambia Yuhanz) Mtie ndani ya Tabut na kisha kitie ndani ya Mto, kisha Mto utakichukua mpaka ukingoni, na atachukuliwa na adui yangu na adui yake. Na nitakupamba kwa mapenzi kutoka kwangu, ili uwe ni mwenye kulelewa kutoka chini ya uangalizi wangu.***

Hivyo baada ya Al Khidhr kumwambia Nabii Musa juu yake anachokifiria basi akasema kwa kumuuliza Nabii Musa:

﴿قَالَ أَلَمْ أَقُلْ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْراً﴾

Qala alam aqul innaka lan tastateeAAa maAAiya sabran *(Surat Al Kahf 18:72)*

Tafsir: ***Akasema (Al Khidhr): 'Hivi jee sikukuambia mimi kua kwa hakika wewe hutoweza kua na Subra nami?'***

Yaani hapa Al Khidhr anamuwekea wazi Nabii Musa kua hili jambo alilolifanya basi amelifanya kwa makusudi, kwani kwa hakika yeye anajua anachokifanya, kutokana na kua na habari juu ya tukio litakalofuata baada yake, ambapo Nabii Musa hana habari juu ya matokeo ya tukio hilo. Hivyo jee kwanini Nabii Musa anakua hana Subra?

Hivyo Nabii Musa akajitetea kwa unyenyekevu mbele ya Mwalimu wake huyo alietumwa akasome kwake, kwani anaona kua Mwalimu huyu tayari anayajua mengi nisiyoyajua mimi, hivyo kama sikujitetea basi nitakosa faida nyingi kutoka kwake hivyo akasema:

﴿قَالَ لاَ تُؤَاخِذْنِي بِمَا نَسِيتُ وَلاَ تُرْهِقْنِي مِنْ أَمْرِي عُسْراً﴾

Qala la tu-akhidhnee bima naseetu wala turhiqnee min amree AAusran*(Surat Al Kahf 18:73)*

Tafsir: ***Akasema (Nabii Musa): 'Usinichukulie (Vibaya) kutokana na nilicho kisahau na wala usiniadhibu kwa kunifanyia uzito juu ya jambo langu hili zito'***

Ambapo tunaona kua katika kujitetea kwake basi Nabii Musa ametumia maneno mawili mazito kwenye kauli yake, ambapo neno la kwanza ni pale aliposema *La Tu-akhidhnii* ambalo ni neno *Akhadha* lenye kikanushi cha harfu *Lam* kabla yake. Ambapo neno *Akhadha* hua linamaanisha Kuchukua, Kupokea, Kukubali, Kunyang'anya, Kuadhibu, Kukamata, Kutia mikononi, Kuzuia na pia humaanisha Kushikamanisha.

Hivyo basi Nabii Musa alitumia kauli ambayo ni yenye hoja nzito ndani yake kwa kusema kua Usinichukulie Vibaya, au usinilaumu kutokana na kile ambacho ni kitu kinachotokana na maumbile ya kila Ibn Adam ambacho ni kughafilika na kusahau kutokana na tukio husika na uzito wake, kwani kitendo kinachofanywa kutokana na hisia za kimaumbile za kusahau hua hakiwezi kuhesabiwa na kisha kushikamanishwa na Adhabu, na hapo hapo kauli hii inaonesha kuomba msamaha ndani yake kwani kosa lililofanyika halikufanywa kwa kukusudiwa.

Nabii Musa pia akatoa hoja ya pili kwa kutumia neno *Wala Turhiqnee* ambalo ni neno *Rahaqa* lenye kikanushi cha *harfu Lam* pia kabla yake. Ambapo neno *Rahaqa* hua linamaanisha Kufuatilia kwa Karibu, Kufunika, Kua na Ujinga, Kutokua na Adabu, Kuharakisha, Kufikia, Kuchukulia, Kunyanyasa, Kudhulumu, Kukandamiza na pia Kuwekea Vikwazo, au Kuwekea Ugumu.

Hivyo Nabii Musa anamwambia Al Khidhr kwa kumtaka asimlaumu kwa kosa ambalo hakulikusudia na wala asimuwekee vikwazo katika jambo lake hilo gumu na zito la kutafuta Ilm kutoka kwake na hivyo kumpelekea kuishiwa na subra zaidi, hivyo amstahmilie ili anufaike zaidi. Na hapo Al Khidhr akamstahmilia Nabii Musa na kumruhusu kufuatana nae huku wakiendelea katika safari yao hio mpaka wakafika katika sehemu nyengine ya nchi kavu na kushuka kwenye Jahazi hilo katika miunaoitwa Ayla Mji wa Aylah ambao kwa kiyahudi hua unaitwa mji wa Eilat, upo kusini mwa nchi ya Falestina Ambayo leo imekua Israel, mji huu wa *Eilat* upo katika mwambao wa Bahari nyekundu katika Ghuba ya Aqaba, Ghuba ambayo inapakanisha mipaka ya nchi 4 za Kiarabu ambazo ni: Misri, Falestina, Jordan na Saudia.

Hivyo Nabii Musa na Al Khidr walipofika katika mji wa Aylah, wakawa wanatembea kwa miguu kama zinavyosema aya:

﴿فَٱنطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا لَقِيَا غُلَٰمٗا فَقَتَلَهُۥ قَالَ أَقَتَلۡتَ نَفۡسَۢا زَكِيَّۢةَۢ بِغَيۡرِ نَفۡسٖ لَّقَدۡ جِئۡتَ شَيۡـٔٗا نُّكۡرٗا﴾

Faintalaqa hatta idha laqiya ghulaman faqatalahu qala aqatalta nafsan zakiyyatan bighayri nafsin laqad ji/ta shay-an nukran*(Surat Al Kahf 18:74)*

Tafsir: ***Hivyo wakaendelea (na safari yao) mpaka wakakuta Mtoto, kisha (Al Khidhr) akamuua. Akasema (Nabii Musa) : 'Umeiua Nafsi isiyokua na kosa ambayo haikuua Nafsi nyengine, kwa hakika wewe Umefanya jambo baya sana****.'**

Katika kutembea kwao basi wakakutana na watoto 10 ambao walikua wanacheza, na mmoja miongoni mwao alikua ni mzuri sana na mwenye uso wenye kung'ara na kuvutia.

Ambapo tunapoiangalia zaid aya hii basi kutokana na maneno yake basi tunaona kua imetumia neno *Ghulaman,* ambapo neno hili pia lilitumika pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipoelezea ndani ya kitabu chake kuhusiana na kisa cha Nabii Yusuf basi alipoingizwa Kisimani kisha akatolewa na Wasafiri, basi yule aliemtoa Nabii Yusuf Kisimani ambae jina lake ni Malik Ibn Duar alisema kumwambia Tajiri yake:

﴿وَجَآءَتۡ سَيَّارَةٞ فَأَرۡسَلُواْ وَارِدَهُمۡ فَأَدۡلَىٰ دَلۡوَهُۥۖ قَالَ يَٰبُشۡرَىٰ هَٰذَا غُلَٰمٞۚ وَأَسَرُّوهُ بِضَٰعَةٗۚ وَٱللَّهُ عَلِيمُۢ بِمَا يَعۡمَلُونَ﴾

Wajaat sayyaratun faarsaloo waridahum faadla dalwahu qala ya bushra hadha ghulamun waasarroohu bidhaAAatan waAllahu AAaleemun bima yaAAmaloona *(Surat Yusuf 12:19)*

Tafsir: ***Ukaja Msafara kisha wakamtuma Mchotaji Maji na aliposhusha ndoo yake (Kisimani) akasema: Habari Nzuri zilioje! Huyu ni Kijana Mdogo! wakamficha kama bidhaa na kwa hakika Allah ni mwenye kujua juu ya walilolifanya.***

Hivyo neno *Ghulamun* hua linamaanisha Mtoto Mdogo wa Kiume, Kijana mdogo wa Kiume ambae bado hajabalegh. Na kwa maana hio basi Hapa Nabii Musa alikua akilaumu kuhusiana na kifo cha huyu Mtoto Kijana mdogo ambae hata hivyo alikua hajafikia Umri hata wa miaka 14 na hivyo si *Mukallaf* yaani si mtu mwenye kuandikiwa na kuhesabiwa Makosa yake mbele ya Mola wake.

Ambapo wanazuoni wametofutiana juu ya jina lake, kwani kuna wasemao kua alikua akiitwa Hasanud, na kuna wasemao kua alikua akiitwa Simiuin na kuna wesemao kua ni Hison na wengine wanasema kua ni Hussayn na Baba yake alikua anaitwa Malas na Mama yake alikua akiitwa Rahmah ambapo huu ni mtizamo wa Imam Wahb Ibn Munabih.

Hivyo Al Khidhr akamvizia na kumkamata mtoto huyo bila ya kuoenakana na yeyote isipokua na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na wale aliofuatana nao na kisha akamuua, ama kuhusiana na alivyomuua basi kuna wasema kua Al Khidhr alimpiga Jiwe mtoto huyo, na kuna wasemao kua alimkata kichwa, na pia kuna wasemao kua alimpiga kichwa chake na ukuta wa kisima kilichopo katika eneo hilo, ambapo baada ya Al Khidhr kumuua mtoto huyo basi Nabii Musa akasema: ***'Umeiua Nafsi isiyokua na kosa ambayo haikuua Nafsi nyengine, kwa hakika wewe Umefanya jambo baya sana.'***

Ambapo *Nafsi Zakkiyah* hua inamaanisha Nafsi ambayo ni safi haina kosa aidha kwa kutokana na kua mwenye Nafsi hio kua ni mtu ambae hajafikia Umri wa kua ni *Mukallaf* yaani hajafikia Umri wa kubaleghe na hivyo hawezi kuhesabiwa kua ana dhambi kwani haandikia dhambi. Na pia *Nafsi Zakkiyah* hua inamaanisha kua nafsi ya Mtu ambae alifanya Dhambi lakini baadae akawa ni mwenye kutubu kwa Mola wake.

Naam, katika kumkosoa Al Khidr katika Jahazi, basi Nabii Musa alitumia neno *Shay-an Imran!* Ambalo maana yake ni Jambo litakalokua na matokeo mabaya yaani Dhambi kubwa, na kwa vile Jahazi halikuzama basi ile dhambi haikua kubwa sana.

Lakini katika tukio hili la kuua basi tunaona kua Nabii Musa anakosoa kwa kutumia neno *Shay-an Nukran!!*

Ambapo neno *Nukran* maana yake hua ni Dhambi Kubwa ambayo Uzito na Kuchukiza kwake ni Kukubwa, kiasi ya kua huweza kumpelekea Mtu kuachana na mtu aliefanya kosa hilo na kumchukia sana kwani anastahiki kuadhibiwa kwa kosa hilo la kumuua mtu asiekua na hatia hata Adhabu yake pia hua ni kubwa sana...Kwani Hukm ya jambo alilolifanya Al Khidr mbele ya Nabii Musa hua ni Kifo!

Hivyo akasema Al Khidhr kumwambia Nabii Musa kua:

﴿قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَّكَ إِنَّكَ لَن تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْراً﴾

Qala alam aqul laka innaka lan tastateeAAa maAAiya sabran *(Surat Al Kahf 18:74)*

Tafsir: ***Akasema (Al Khidhr); 'Jee sikukuambia mie Wewe kua kwa hakika hutoweza wewe kua na Subra nami?'***

Ambapo anasema *Jarrah Allah Sultan Al Balagha* Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua: '**Al Khidhr hapa amerudia maneno yake yale yale ya mwanzo, lakini safari hii akaongezea na neno *Laka* yaani 'Wewe' kumtilia mkazo Musa kuhusiana na uhakika wa manenoyake aliyoyasema hapo kabla**.'

Hivyo Nabii Musa akasema:

﴿قَالَ إِن سَأَلْتُكَ عَن شَيْءٍ بَعْدَهَا فَلاَ تُصَاحِبْنِي قَدْ بَلَغْتَ مِن لَّدُنِّي عُذْراً﴾

Qala in saaltuka AAan shay-in baAAdaha fala tusahibnee qad balaghta min ladunnee AAudhran *(Surat Al Kahf 18:76)*

Tafsir: ***Akasema (Nabii Musa): 'Kama nikikuuliza juu ya kitu chengine chochote kile baada yake basi usiwe na urafiki nami kwani kwa hakika utakua umepata kutoka kwangu Udhuru.***'

Ambapo neno *Balaghta* linatokana na neno *Balagha* ambalo hua inamaanisha Kuwasili, Kufikia mwisho, Kufikia Malengo, Kupata kinachotakiwa, Kupea, Kukaribia na pia humaanisha Kubaleghe.

Hivyo Nabii Musa aliendelea kumuomba msamaha Al Khidhr kutokana na kile ambacho alichokikosea na kukirudia tena kwa mara ya pili mbali ya kua alikua tayari ameshapewa Onyo kua hatoweza kua na subra juu ya yale asiyokua na habari nayo, kutokana na ukweli huo basi akaamua kumuwekea wazi Al Khidhr kua kama Nabii Musa akirudia tena kosa hilo basi na aachane nae kwani itakua tayari ameshapata udhuru wa kuachana na Nabii Musa kutokana na kutokua na Subra.

Ambapo anasema Ubbay Ibn Ka'ab *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliisoma aya hii na kisha akamsalia Musa na kisha akasema: 'Musa alikua akiona haya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kurudia kuuliza kwake**''

Hapa tunaona kua Nabii Musa alikua pia amesahau kuhuisiana na aliyoyafanya yeye pale alipompigia ngumi Fatun ambae ndio yule mtu wa Misri aliekua akipigana na Samirii, ambapo Nabii Musa akamuua Mtu huyo bila ya kukusudia kutokana na ngumi hio, kama zilivyosema aya:

﴿وَدَخَلَ ٱلْمَدِينَةَ عَلَىٰ حِينِ غَفْلَةٍ مِّنْ أَهْلِهَا فَوَجَدَ فِيهَا رَجُلَيْنِ يَقْتَتِلاَنِ هَـٰذَا مِن شِيعَتِهِ وَهَـٰذَا مِنْ عَدُوِّهِ فَٱسْتَغَاثَهُ ٱلَّذِى مِن شِيعَتِهِ عَلَى ٱلَّذِى مِنْ عَدُوِّهِ فَوَكَزَهُ مُوسَىٰ فَقَضَىٰ عَلَيْهِ قَالَ هَـٰذَا مِنْ عَمَلِ ٱلشَّيْطَانِ إِنَّهُ عَدُوٌّ مُّضِلٌّ مُّبِينٌ﴾

Wadakhala almadeenata AAala heeni ghaflatin min ahliha fawajada feeha rajulayni yaqtatilani hadha min sheeAAatihi wahadha min AAaduwwihi faistaghadhahu alladhee min sheeAAatihi AAala alladhee min AAaduwwihi fawakazahu moosa faqadha AAalayhi qala hadha min AAamali alshshaytani innahu AAaduwwun mudhillun mubeenun *(Surat Al Qasas 28:15)*

Tafsir: ***Na akaingia katika Mji wakati ambao wate wake walikua wameghafilika. Na akakuta watu wawili wanapigana. Mmoja ni mtu wa upande wake (wa Bani Israil) na mwengine ni wa upande wa adui yake (Mtu wa Fir'awn), akaomba msaada mtu wa upande wake dhidi ya adui yake. Hivyo Musa akampiga Ngumi na akammaliza. Na kisha akasema hii ni amali ya Shaytan, hakika yeye ni adui mpotovu aliewazi.***

Na hivyo tukio hili la Al Khidr la kuua kwa kukusudia ambalo ni tofauti na lile tukio la Nabii Musa la kuua bila ya kukusudia yote kwa pamoja yanatuonesha kua tukio la kitu au jambo lolote lile hua haliko kama linavyoonekana kwa nje au kwa juu juu tu, bali inabidi uwe na Ilm ya ndani ya kina ndio utaweza kujua matokeo yake, kwani kwa upande wa Nabii Musa hapa alijaaliwa kutokewa na tukio hili kua ni kama sababu ya kumfanya yeye awe ni mwenye kuikimbia ardhi ya nchi ya Misri, kwa ajili ya kutayarishwa kupewa Majukumu mazito ya Utume na Mola wake.

Hivyo ingawa tukio lilikua ni baya lakini lilikua na malengo mema yatakayosababisha baadae matokeo mazuri zaidi ndani yake, ambapo hali hii pia ipo kwa tukio la Al Khidhr alipomuua Mtoto huyu kama tutakavyoona hapo baadae kulingana na namna zilivyofafanua aya.

Hivyo Al Khidhr akamsamehe Nabii Musa na kwa pamoja wakaendelea na safari yao kama zinavyosema aya:

﴿فَٱنطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَآ أَتَيَآ أَهْلَ قَرْيَةٍ ٱسْتَطْعَمَآ أَهْلَهَا فَأَبَوْاْ أَن يُضَيِّفُوهُمَا فَوَجَدَا فِيهَا جِدَاراً يُرِيدُ أَن يَنقَضَّ فَأَقَامَهُ قَالَ لَوْ شِئْتَ لاَتَّخَذْتَ عَلَيْهِ أَجْراً﴾

Fain<u>t</u>alaq<u>a</u> <u>h</u>att<u>a</u> i<u>dha</u> atay<u>a</u> ahla qaryatin ista<u>t</u>AAam<u>a</u> ahlah<u>a</u> faabaw an yu<u>dh</u>ayyifoohum<u>a</u> fawajad<u>a</u> feeh<u>a</u> jid<u>a</u>ran yureedu an yanqa<u>dhdh</u>a faaq<u>a</u>mahu q<u>a</u>la law shi/ta laittakha<u>dh</u>ta AAalayhi ajr<u>a</u>n*(Surat Al Kahf 18:77)*

Tafsir: ***Hivyo wakaendelea na safari yao mpaka wakakuta watu wa Mji, wakawaomba watu wa Mji huo chakula, lakini wakakataa kuwakaribisha, n wakakuta ndani yake (Mji huo) Ukuta unaotaka kuanguka nae (Al Khidhr) akaunyanyua, akasema (Musa): 'Kama ungetaka basi bila ya shaka ungechukua Ujira kutoka kwao'***

Ambapo Wanazuoni wametofautiana kuhusina na jina la mji huo, kwani kuna wanaosema kua ni Antakiya ambao upo Uturuki na kuna wasemao kua ni mji wa Nazareti na Al Khidhr, Nabii Musa na Joshua waliwasili katika Mji huo katika wakati wa Usiku. Ambapo anasema Qatadah Ibn Diamah Al Sadusi kua: '**Watu wa Mji huo walikua ni Wabakhili sana na walikua hawawapi wasafiri haki zao.**'

Kwani katika usiku wa siku hio wakati walipowasili katika Mji huo basi Al Khidr, Nabii Musa na Joshua walikua na Njaa kali sana, walikua wamechoka na ilikua ni katika wakati wa kipindi cha Baridi na hawakua ni wenye kupata sehemu ya kujihifadhi na hali ya hewa ya Baridi, wala ya kupumzikia wala chakula cha kutia matumboni mwao kwa ajili ya kuwapa nguvu ya kuongezea miili yao kuzalisha joto zaid Ili kukabiliana na hali ya baridi kwani watu wa mji huo waliwakataa kabisa kabisa.

Hivi ndivyo hali inavyokua pale *Allah Subhanah wa Taala* anapoamua kumjaribu Mja wake ampendae ili arudi kwake kisha ampandishe darja. Kwani mtu kua katika hali kama hio

umeshatembea kwa mda mrefu sana kwa miguu kisha unawasili kwenye mji wenye baridi kali tena usiku kisha unakosa msaada.

Hivyo katika kupita kwao na kukosa matumaini ya kusaidiwa basi wakaamua kua wachague sehemu ambayo haipigwi na Upepo sana ili wasije wakaganda kwa baridi ya usiku. Na kisha wakajifunika kwa vizigo vyao na kulala pembeni ya ukuta wa Nyumba moja waliyoiona kua itawafaa zaid kulingana na hali yao, na wakajibanza na kulala hadi asubuhi na kisha Al Fajir Mapema wakaamka kwa ajili ya kuendelea na safari yao ili kua mbali zaid na Mji huo na watu wao wasiokua na huruma wala ukarimu, kwani kua mbali nao ni bora zaid kuliko kua karibu pamoja nao.

Kwani wakati wanakusanya Vitu vyao kwa ajili ya safari yao mara Al Khidhr akaona kua kumbe ukuta waliolala chini yake ulikua unaufa mkubwa na hivyo ni bahati yao tu kua haukuwaangukia katika usiku huo. Hivyo Al Khidhr akaweka pembeni vitu vyake na kisha akaanza kuubomoa ukuta huo wote wenye ufa huo. Huku Nabii Musa Na Joshua wakimuangalia kwa mshangao.

Na kisha baada ya hapo akaujenga tena upya Ukuta huo ambao ulikua ni wa kukandika kwa Udongo. Na *Allah Subhanah wa Taala* akajaalia kua Ukuta huo ukamalizika kujungwa kwa haraka sana hata kabla watu wa mji huo hawajaamka vizuri na kuanza pirika pirika zao za kila siku na kuona tukio hilo Na kutaka kuanza kuuliza ilikuaje mpaka wakauvunja Ukuta na kisha wakaujenga. Na baada ya kuujenga ukuta huo basi Al Khidhr akakusanya vitu vyake na kisha akamwambia Nabii Musa kua waendelee na safari yao

Ambapo wa upande wa Imam Said Ibn Jubayr basi anasema kua: '**Al Khidhr aliunyoosha ukuta huo kwa kutumia mikono yake**' na baada ya kumaliza kuuinua Ukuta huo basi Nabii Musa akamwambia Al Khidhr kua: '**Kama ungetaka basi bila ya shaka, usinge ujenga ukuta huo hadi pale watu wa mji huu kukulipa ujira wako au kwa kutupatia chakula**'

Ambapo hapa Nabii Musa alikua amesahau kua haya aliyoyafanya Al Khidhr pia kua ni sawa na yale aliyoyafanya yeye hapo kabla alipowasili katika mji wa Madyan, baada ya kuwasaidia *Imraatayn* wakati alipowakuta wakiwa ni wenye kusubiri kuwanywesha maji wanyama wao katika mji wa Madyan pale ziliposema aya:

﴿وَلَمَّا وَرَدَ مَآءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةً مِّنَ ٱلنَّاسِ يَسْقُونَ وَوَجَدَ مِن دُونِهِمُ ٱمْرَأَتَيْنِ تَذُودَانِ قَالَ مَا خَطْبُكُمَا قَالَتَا لاَ نَسْقِى حَتَّىٰ يُصْدِرَ ٱلرِّعَآءُ وَأَبُونَا شَيْخٌ كَبِيرٌ۝ فَسَقَىٰ لَهُمَا ثُمَّ تَوَلَّىٰٓ إِلَى ٱلظِّلِّ فَقَالَ رَبِّ إِنِّى لِمَآ أَنزَلْتَ إِلَىَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ﴾

Walamma warada maa madyana wajada AAalayhi ommatan mina alnnasi yasqoona wawajada min doonihimu imraatayni tadhoodani qala ma khatbukuma qalata la nasqee hatta yusdira alrriAAao waaboona shaykhun kabeerun; Fasaqa lahuma thumma tawalla ila al*dhdh*illi faqala rabbi innee lima anzalta ilayya min khayrin faqeerun *(Surat Al Qasas 28:23-24)*

Tafsir: ***Na alipowasili kwenye sehemu inayonyweshewa Maji ya Madyan, akaona kundi la Wanaume wakinyweshea (Maji wanyama wao). Na pembeni yao akaona Wanawake wawili wakiwazuia wanyama wao, akasema (Nabii Musa): 'Mnataka kufanya nini?'Nao wakasema: 'Hatuwezi kuwanywesha Wanyama wetu mpaka Wafugaji waondoe Wanyama wao na Baba yetu***

ni Mzee sana; Hivyo akawanyweshea Maji Wanyama wao na kisha akarudi kivulini na akasema: 'Ewe Mola wangu, Hakika mimi ni mwenye kuhitaji kheri yeyote ile utakayonipa'

Hivyo baada ya Nabii Musa kushauri juu ya lile ambalo hakuombwa ushauri juu yake, wakati na yeye pia alifanya kama alivyofanya mwenzake kwa kuwasidia *Imraatayn* bila ya kudai malipo kutoka kwao katika wakati huo, basi Al Khidr akamwambia Nabii Musa kua umefika muda wa kuachana baina yao kama zinavyosema aya:

﴿قَالَ هَٰذَا فِرَاقُ بَيْنِي وَبَيْنِكَ سَأُنَبِّئُكَ بِتَأْوِيلِ مَا لَمْ تَسْتَطِع عَّلَيْهِ صَبْراً﴾

Qala hadha firaqu baynee wabaynika saonabbi-oka bita/weeli ma lam tastaṯiAA AAalayhi sabran *(SuratAl Kahf 18:78)*

Tafsir: ***Akasema (Al Khidhr kumwambia Nabii Musa) : 'Hapa ndio muachano wetu baina yako na baina yangu, hivyo nitakupa habari ya tafsiri ya yale ambayo umeshindwa kua na Subra nayo'***

Ambapo Al Khidhr akatilia mkazo na kuthibitisha kuachana baina yake yeye Al Khidhr na baina ya Nabii Musa kunakotokana na kuvunjika kwa makubaliano baina yao baina ya Nabii Musa na yeye Al Khidhr, kwani Nabii Musa tayari ameshavunja masharti mara tatu ambayo hapo awali alikubaliana nae kua ataweza kua na subra na yale asiyokua na habari nayo hivyo Nabii Musa alifeli katika hali zifuatazo.

Alifeli mtihani wa kwanza kwenye Jahazi kutokana na kusahau Masharti ya Mtihani wake.

Akafeli mtihani wa pili kwenye Mauaji ya yule kijana kutokana na Mazingira ya Mtihani huo yaliyompelekea kudai maelezo kuhusiana na tukio hilo ambayo hakutakiwa ayadai.

Na pia akafeli Mtihani wa tatu na wa Mwisho kutokana na kukusudia kufeli mtihani huo ili awachane na Al Khidhr kwa kutoa ushauri ambao hakutakiwa autoe!

Lakini sasa kabla ya kuachana huko baina yao basi kwanza inabidi Al Khidhr amfafanulie Nabii Musa yale ambayo alishindwa kua na ustahmilivu nayo juu yake, hivyo akaanza kufafanua maana ya yale mambo matatu aliyoyafanya hapo kabla mbele ya Nabii Musa kwa kusema:

﴿أَمَّا ٱلسَّفِينَةُ فَكَانَتْ لِمَسَاكِينَ يَعْمَلُونَ فِي ٱلْبَحْرِ فَأَرَدتُّ أَنْ أَعِيبَهَا وَكَانَ وَرَآءَهُم مَّلِكٌ يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ غَصْباً﴾

Amma alssafeenatu fakanat limasakeena yaAAmaloona fee albahri faaradtu an aAAeebaha wakana waraahum malikun ya/khudhu kulla safeenatin ghasban *(SuratAl Kahf 18:79)*

Tafsir: ***(Akasema Al Khidhr kumwambia Nabii Musa)'Ama Kuhusiana na Jahazi, basi lilikua ni la Masikini waliokua wakifanyia kazi baharini, hivyo nilitaka kulitia kasoro, kwa sababu kabla yao kulikua kuna Mfalme ambae alikua akiliteka kila Jahazi kwa nguvu'***

Neno *Aba* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kitu Kibaya, Kuharibika, Kua na Kasoro, Kua na Kosa, Kutokua na hali inayokubalika.

Neno *Aba* ndio lililotoa neno A'aib yaani Jambo la Aibu au Jambo la Kujiharibia na hivyo kutokukubalika.

Hivyo Aya zinaguonesha kua Al Khidhr anamwambia Nabii Musa kua Yeye alikua na Habari juu ya Hali ya Jahazi walilopanda, juu ya Wamiliki wake na juu yatakayotokea mbele yao watu hao katika Safari yao na Jahazi lao. Na kutokana na kua ni mwenye kujua juu ya hayo na kujua juu ya umuhimu wa Jahazi hilo kua ni lenye kutegemewa na Wamiliki wake ambao ni Masikini.

Na Sifa ya uzima na uzuri wa Jahazi hilo basi bila ya shaka hapo baadae lingetekwa Nyara na Mfalme ambae ni mwenye kukagua na kuyachukua Majahazi yote yaliyokua mazima na mazuri.

Hivyo kutokana na kujua kwake Al Khidhr Juu ya hayo basi akaamua Kulitia Aibu Jahazi hilo, yaani Kulifanya lisikubalike kwa Kulitoboa na hivyo kua ni lenye sifa ya Kuvujisha au kupiyisha Maji na kuyokana na kua na hali hio basi bila ya shaka halitotakiaa na Mfalme huyo kutokana na Kasoro yake hio mbali ya kua na Uzuri wa Muonekano wa Nje yake

Kwani tangu lini Mtu mwenye Mamlaka akapanda Gari bovu lenye Kutoa Moshi na kuvujisha katika wakati wa Mvua? Yaani hata kama Gari hilo likiwa na jina kubwa kama Aurus Senat, Alfa Romeo, Lambargini, Mercedes, Audi n.k

Lakani kama likiwa linatoa Moshi mweusi au Maji mpaka ndani ikinyesha Mvua basi hakuna Kiongozi atakaelitaka kwani lina aibu na hivyo litamuaibisha. Ila kwa mimi na wewe aaaah tutapigana kwa ajili ya jina lake tu. Naam hivyo ndio maana Al Khidhr akaamua kuliaibisha Jahazi hilo.

Ambapo anasema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Ama kuhusiana na Safina basi lilikua linamilikiwa na Masikini, ingawa lilikua lina thamani ya Dinar 1000, kwani Msafiri ni masikini hata kama akiwa na Dirham 1000**'

Ambapo anasema Imam Ka'ab Al Ahbar kua: '**Jahazi hili lilikua linamilikiwa na ndugu 10 ambao walilirithi kutoka kwa baba yao.**'

Ambapo kutokana na aya hii basi anasema *Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: **'Imam Muhammad Idris Al Shafii alihitimisha kutokana na aya hii kua:** '**Fukara hua na hali mbaya zaidi kuliko Masikini, kwani ingawa watu hawa walikua wanamiliki Jahazi lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliwaita kua ni Maskini**'

Ambapo neno *Fuqara* hua ni lenye kutokana na neno *Faqura* ambalo hua linaaamanisha Mtu Aliekua Maskini, Mtu Mwenye Shida Kubwa na Nyingi sana. Hivyo neno *Fuqara* hua linatumika kumaanisha Mtu ambae anawategemea watu wengine kwa ajili ya mahitajio yake ya kimaisha kutokana na sababu mbali mbali za kimaumbile ikiwemo Uzee, Ulemavu au kutokana na mitihani mbali mbali ya kimaisha, na ndio maana neno *Faqira* hua pia linamaanisha Kuzidiwa na Mithani ambayo huweza kumpelekea Mtu kuhisi uzito wa maumivu ya Mtihani huo ndani ya Uti wa Mgongo, na neno *Faqiratun* hua linamaanisha Mtihani wa Kuvunjika Mgongo.

Ambapo kwa upande wa neno *Masakin* hua linatokana na neno *Sakana* ambalo hua linamaanisha Kutulia, Kukaa Kimya, Kusimama tulii. Hivyo neno *Masakin* hua linamaanisha Mnyenyekevu, Mtulivu, Masikini, Mtu anaestahiki kusaidiwa kutokana na Udhaifu au Unyenyekevu wake.

Neno *Sakana* ndio pia lililotoa neno *Sikin* yaani Kisu ambacho Kimeitwa hivyo kwa sababu Kisu ndio chanzo cha Kukifanya Kiumbe Kitulie baada ya Kuchinjwa kwake.

Ambapo kwa upande wa *Imam Muhyi Ad Din* Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi basi yeye anasema kua: '**Maneno haya mawili Fukara na Masakin hua yana maana moja yanapokua yametumika katika sehemu tofauti, lakini yanapotumika katika sehemu moja hua yana maana tofauti**.'

Miongoni mwa mifano ya matumizi ya maneno haya mawili katika sehemu moja basi hua ni katika ile aya ya hukumu ya miongoni mwa wanaostahiki kupewa Zakkah ambayo inasema:

﴿إِنَّمَا ٱلصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَاكِينِ وَٱلْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَٱلْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَارِمِينَ وَفِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ فَرِيضَةً مِّنَ ٱللَّهِ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾

Innama alssadaqatu lilfuqara-i waalmasakeeni waalAAamileena AAalayha waalmu-allafati quloobuhum wafee alrriqabi waalgharimeena wafee sabeeli Allahi waibni alssabeeli fareedatan mina Allahi waAllahu AAaleemun hakeemun *(Surat At Tawba 9:60)*

Tafsir: ***Kwa hakika Sadaka (Zakkah) ni kwa ajili ya Mafukara na Masikini na wanaoisimamia (Katika kuikusanya na Kugawa) na kwa ambao Nyoyo zao zimeinamia katika Uislam, na kuwaachia huru waliokamatwa, na wenye madeni, na kwa ajili ya njia ya Allah, na wasafiri hua ni Wajibu kutoka kwa Allah, na Allah ni Mwingi wa kujua na ni Mwingi wa Hikma.***

Na Wanazuoni wametofautiana katika maana ya maneno haya mawili kutokana na yalivyotumika hapa kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii na wafuasi wa Maddhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: '**Fukara hua ni tu mwenye shida zaidi fuliko Masikini na hii ni kutokana na mpangilio wa maneno haya yaliyotajwa kwenye aya hii, kwani mwanzo ametajwa Fukara na kisha baadae ndio akatajwa Masikini.**'

Na kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanjfa na Maddhhab ya Imam Malik Ibn Anas basi waao wanasem kua: '**Maskini ndie mwenye shida zaidi kuliko Fukara.**'

Kwa kumalizia basi kuhusiana na Fukra na Masikini basi tunaona kua:

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanafafanua maana mbili hizi kwa kusema: '**Masikini hua ni mtu ambae hana kitu kabisa. Fukara hua ni mtu ambae anacho kitu kidogo ambacho hata hivyo hakimtoshi kwa mahitaji yake ya kila siku**'

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas basi wao wanafafanua maana mbili hizi kwa kusema: '**Masikini hua ni mtu ambae hana kitu kabisa na hivyo hua anaomba watu msaada. Fukara hua hana kitu hata kidogo lakini hata hivyo haombi kwa watu.**'

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii basi wao wanafafanua maana mbili hizi kwa kusema: '**Fukara hua ni mtu ambae hana kitu kabisa. Maskini hua ni mtu ambae anacho kitu kidogo ambacho hata hivyo hakimtoshi kwa mahitaji yake ya kila siku**'

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanafafanua maana mbili hizi kwa kusema: '**Fukara hua ni mtu ambae hana hata kitu kitachomtosheleza hata nusu ya mahitaji**

yake. Maskini hua ni mtu ambae anacho kitu kidogo ambacho ni zaidi ya nusu ya mahitaji yake na hivyo hua hakimtoshi kwa mahitaji yake ya kila siku'

Ambapo anasema Imam Abu Jafar Muhammad Ibn Jarir At Tabari kua : '**Amesema Abu Hurayra *Radhi Allahu Anhu* kua :** '***Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Masikini wa kweli hua si yule ambae anaenda na kuwaomba watu kwa ajili ya Tende moja mbili, au kwa kula chakula mdomo mmoja au miwili, bali ni yule ambae anaeona haya kuomba, soma kama unataka: '*La yas-aloona alnnasa ilhafan*''**

Ambapo maneno yasemayo *La yas-aloona alnnasa ilhafan ni* yale yaliyomo katika aya isemayo:

﴿ لِلْفُقَرَآءِ ٱلَّذِينَ أُحصِرُواْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ لاَ يَسْتَطِيعُونَ ضَرْباً فِى ٱلأَرْضِ يَحْسَبُهُمُ ٱلْجَاهِلُ أَغْنِيَآءَ مِنَ ٱلتَّعَفُّفِ تَعْرِفُهُم بِسِيمَاهُمْ لاَ يَسْأَلُونَ ٱلنَّاسَ إِلْحَافاً وَمَا تُنفِقُواْ مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ﴾

Lilfuqara-i alladheena ohsiroo fee sabeeli Allahi la yastateeAAoona darban fee al-ardhi yahsabuhumu aljahilu aghniyaa mina alttaAAaffufi taAArifuhum biseemahum la yas-aloona alnnasa ilhafan wama tunfiqoo min khayrin fa-inna Allaha bihi AAaleemun *(Surat Al Baqara 2:173)*

Tafsir: ***(Sadaka hua ni) Kwa Mafukara ambao wamezuilika kujitolea kwa ajili ya Allah, na hawawezi kutembea Ardhini (kwa ajili ya kufanya kazi au biashara), na wale wasiowajua huwadhania kua ni matajiri kutokana na kujiheshimu kwao. Unaweza kuwajua kutokana na alama yao, hua hawawaombi watu kwa kukera, na chochote kile mtakachotumia kwa ajili ya kheri basi Allah anajua juu yake.***

Hivyo katika hadithi hii tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametumia neno Masikini na kuifafanua hali yao katika aya inayozungumzia Fukara, na hii ni kutokana na kuingiliana kimaana na kimatumizi kwa maneno hayo. Hivyo basi kuna watu wa aina mbili wasiokua na uwezo, kuna wale ambao hua ni wenye kuomba na wale wasioomba.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakua ni mwenye kutofautisha baina ya hali za watu wawili hawa, na kutokana na aya hii basi tunaweza kusema kua Faqir hua ni yule ambae si mwenye kuomba na Masikini hua ni mwenye kuomba.

Na kuhusiana na neno *Wara'a* lililotumika katika aya hii basi kwa upande wa Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Waarabu hua ni walio tofautiana katika matumizi ya neno *Waraa* katika hali tatu tofauti ambapo hua ni kua linaweza likatumika katika kila hali na katika kila sehemu na katika hali ya mkabala**'

Ambapo neno *Waraa* limetumika tena katika zile aya zinazosema:

﴿مِّن وَرَآئِهِ جَهَنَّمُ وَيُسْقَىٰ مِن مَّآءٍ صَدِيدٍ﴾

Min wara-ihi jahannamu wayusqa min ma-in sadeedin *(Surat Ibrahim 14:16)*

*Tafsir:(**Wara-ihi**)**Mbele yake (Kila Kiongozi aliekua Dhalimu) kuna Jahannam na atanyweshwa maji yenye kuchemka sana.***

Na katika ile aya isemayo:

﴿لَعَلِّيٓ أَعۡمَلُ صَٰلِحٗا فِيمَا تَرَكۡتُ كَلَّآۚ إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَآئِلُهَاۖ وَمِن وَرَآئِهِم بَرۡزَخٌ إِلَىٰ يَوۡمِ يُبۡعَثُونَ﴾

LaAAallee aAAmalu salihan feema taraktu kalla innaha kalimatun huwa qa-iluha wamin wara-ihim barzakhun ila yawmi yubAAathoona *(Surat Al Muuminuun 23:100)*

*Tafsr: **Ili nipate kufanya mema kutokana na kile nilichokiwacha nyuma, la, bali hayo ni maneno tu anayozungumza na nyuma (wara-ihim) yao kuna Barzakh (pazia) mpaka katika siku watakayofufuliwa.***

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimbainishia Al Khidhr kuhusiana na Mfalme aliekuwepo kabla yao ambae alikua analiteka nyara kila Jahazi ambalo lisilokua na kasoro na kisha hulitaifisha na kulifanya kua ni lake, hivyo Al Khidhr akalitoboa Jahazi hilo ili lisitaifishwe kwani kutokana na hali yake hio basi litakua tayari lina kasoro na hivyo ingawa Nabii Musa aliona kua Al Khidhr amefanya makosa makubwa lakini kumbe amefanya wema badala yake.

Ambapo Wanazuoni wametofautiana juu ya jina la Mfalme huyu kwani kuna wasemao kua alikua akiitwa Jolanda, ambapo Imam Muhammad Ibn Is-haq basi yeye anasema kua alikua anaitwa Marwan Ibn Julandi Al Urdun, na pia kuna wasemao kua alikua akiitwa Hadad Ibn Badad.

Kisha *Al Khidhr* akasema kumwambia Nabii Musa kua:

﴿وَأَمَّا ٱلۡغُلَٰمُ فَكَانَ أَبَوَاهُ مُؤۡمِنَيۡنِ فَخَشِينَآ أَن يُرۡهِقَهُمَا طُغۡيَٰنٗا وَكُفۡرٗا ۝ فَأَرَدۡنَآ أَن يُبۡدِلَهُمَا رَبُّهُمَا خَيۡرٗا مِّنۡهُ زَكَوٰةٗ وَأَقۡرَبَ رُحۡمٗا﴾

Waamma alghulamu fakana abawahu mu/minayni fakhasheena an yurhiqahuma tughyanan wakufran, Faaradna an yubdilahuma rabbuhuma khayran minhu zakatan waaqraba ruhman *(SuratAl Kahf 18:80)*

*Tafsir: **Ama kuhusiana na yule kijana, basi walikua wazazi wake ni Waumini wawili hivyo tulikua na khofu kua atawaangamiza kwa Uasi na Dhulma. Hivyo tukataka awabadilishie Mola wao kwa yule alie bora zaidi katika usafi na kuwakaribia kihuruma na kimapenzi.***

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Mtoto wa Kiume ambae Al Khidhr alimuua basi alimuuwa akiwa ni Mshirikina, hivyo kama angefikia umri wa kubaleghe basi angepingana na wazee wake kwa uasi na Ushirikina**'*(Imam Abu Daud)*

Kwa upande mwengine basi siku moja Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa kuhusiana na mateka ambao ni vijana wadogo waliotekwa vitani kama wauliwe ama la?: Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akamwambia aliemuuliza suali hilo kwa kusema*:* '**Kama wewe ni Al Khidhr na**

hivyo unao uwezo wa kutofautisha baina ya Muumini na Mshirikina, basi unaweza kuwaua, lakini wewe si Al Khidhr hivyo waachie huru'

Aya imetumia neno *Badala* ambao ni lenye kumaanisha Kubadilisha, Kuchukua kitu kimoja kutoka katika sehemu yake na kukiweka kitu chengine kwenye sehemu ya kitu hicho kilichoondolewa, Kupata kitu chengine badala ya kile kilichokuwepo hapo awali.

Ambapo tunaona kua aya imemalizia na neno *Ruhman* ambalo ni lenye kutokana na neno Rahma ambalo ni lenye kumaaisha Rahma, Rehma, Kupenda, Kua na Huruma, Kufadhilia au Kusaidia na pia neno Rahma hua linamaanisha Uhusiano wa Jamaa na pia humaanisha Fuko la Uzazi ambalo hua anakaa mtoto ndani yake anapokua ndani ya tumbo la mama.

Kutokana na maana hio basi Wanazuoni wanasema kua hapa Al Khidhr aliposema kua **Faaradna an yubdilahuma rabbuhuma khayran minhu zakatan waaqraba ruhman** yaani ***Hivyo tukataka awabadilishie Mola wao kwa yule alie bora zaidi katika usafi na kuwakaribia kihuruma na kimapenzi.*** Basi alikua akimaanisha hivyo, na pia kuna wanaosema kua alikua akimaanisha kua ***Hivyo tukataka awabadilishie Mola wao kwa yule alie bora zaidi katika usafi na kua ni mwenye ukaribu zaidi na fuko la uzazi la Mama yake kwa kutoa watoto bora na wenye Imam juu ya Allah Subhanah wa Ta'ala, na ndio maana tunapoangalia mtizamo wa Imam Jafar Ibn Muhammad basi akawa anasema kua Familia hii ilipata mtoto wa Kike baada yake ambae kutokana nae walizaliwa Manabii 70.***

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Saib Al Kalbi basi yeye anasema kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **aliwabadilishia hawa wazazi badala yake mtoto wa kike ambae aliolewa na Nabii na akazaa watoto ambao ni Manabii pia.**'

Kisha Al Khidhr akaendelea kumuelezea Nabii Musa kwa kusema kua:

﴿وَأَمَّا ٱلْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِى ٱلْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُۥ كَنزٌ لَّهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحاً فَأَرَادَ رَبُّكَ أَن يَبْلُغَآ أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنزَهُمَا رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ وَمَا فَعَلْتُهُۥ عَنْ أَمْرِى ذَٰلِكَ تَأْوِيلُ مَا لَمْ تَسْطِع عَّلَيْهِ صَبْراً﴾

Waamma aljidaru fakana lighulamayni yateemayni fee almadeenati wakana tahtahu kanzun lahuma wakana aboohuma salihan faarada rabbuka an yablugha ashuddahuma wayastakhrija kanzahuma rahmatan min rabbika wama faAAaltuhu AAan amree dhalika ta/weelu ma lam tastiAA AAalayhi sabran *(Surat Al Kahf 18:82)*

Tafsir: ***Ama kuhusiana na Ukuta basi ulikua ni wa Watoto wawili wa kiume Mayatima katika Mji na chini yake kulikua na hazina kwa ajili yao na baba yao alikua ni Mtu mwema. Hivyo alitaka Mola wako kua wabaleghe na kisha waichukue hazina yao kama Rehma kutoka kwa Mola wako, nami sikutekeleza hivyo kwa amri yangu tu. Hio ndio maana ya yale uliyoshindwa kua na Subra nayo.***

Ambapo Wanazuoni wanasema kua Ukuta huo ulikua ni wa Mayatima wawili ambao walikua wakiitwa Asra na Sarim. Ambao walikua ni watoto wa Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae alikua ni Mcha Mungu sana na alikua akijulikana kwa jina la Mukannas. Na pia kuna wasemao kua Mcha Mungu huyu hakua ni watoto wake mayatima hawa, bali walikua ni wenye kutokana na kizazi

chake, hivyo kutokana na Ucha Mungu wake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawa ni mwenye kumhifadhia kizazi chake hicho kilichotokana nae.

Hivyo Al Khidhr alipewa habari ya kua ukuta huo umehifadhi hazina chini yake ambapo alipouangalia basi akauona kua ukuta huo unataka kuanguka na akaamrishwa aujenge na hii ni kutokana na kua watu waliokua wanaishi kwenye mji huo hawakua ni watu wenye sifa nzuri basi bila ya shaka kama ukuta utaanguka na watu hao wakaiona hazina hio basi takua rahisi kwao kuihodhi na kuwadhulumu mayatima hao haki yao.

Na amesema Imam Ibn Mardawiyah kua: '**Amesema Jabir kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *'Allah Subhanah wa Ta'ala* huhifadhi mema ya Mja wake Mwema kwa ajili ya Mtoto wake, na Mtoto wa Mtoto wake na jamaa zake**''

Na akasema Imam Ibn Abi Hatim Abd Rahman Ibn Muhammad Ibn Idris Ibn Al Mundhir Al Hanzali Al Razi Al Shafii kua : '**Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hupatanisha Mja na mema yake na mema ya mtoto wa mja wake huyo na humlinda na kumhifadhi yeye na wanaomzunguka kwa wema**'

Imam Ahmad Ibn Muhammad Ath Thalabi anaendelea kutuambia kua; '**Siku Moja kuna mtu mmoja aliingia katika makazi ya Khalifa Harun Rashid kwa ajili ya kutaka kumuua Khalifa Harun Rashid**. **Lakini alipoingia ndani hakuweza kumfanya chochote Khalifa Harun Rashid na hivyo akamwachia Khalifa Harun Rashid: 'Hivyo Khalifa Harun Rashid alipoulizwa alifanya nini mpaka akawa ni mwenye kuokoka kutokana na kuuliwa na mtu huyo basi akasema: 'Nilisema: 'Ewe yule ambae uliwahifadhi watoto wawili kutokana na Ucha Mungu wa Baba yao, basi nihifadhi mimi kutokana na Ucha Mungu wa Mababa zangu waliotangulia kabla yangu''**'''

Na kutokana na aya hii na vithibitisho hivyo basi wenye kujua walikua waliwaombea Dua Watoto wao Ili wawe ni wenye Kupata Ilm ya Dini yao na kuwasimamia ili wawe waja wema kwa ajili ya akhera yao.

Tofauti na sisi leo hii ambao ni wenye kuwasimamia watoto wetu juu ya Ilm ya Kidunia na kudharau kuhusiana na kuwasimamia katika Ilm ya Dini. Na hii ni kutokana na Ujinga wetu. Wakati mmoja kati ya Maimamu ambae alikua ni mwanafunzi wa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* na pia alimuoa Binti wa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*.

Ambapo Imam Huyu hakua Imam mwengine yeyote isipokua Imam Sayyid Ibn Mussayib basi yeye alikua mwenye kumwambia mtoto wake: '**Ewe Mtoto wangu Mdogo wa Kiume, nitaongeza Dua zangu juu yako, na hivyo huenda nikapata hifadhi kupitia kwako**' na kisha huisoma aya hii ya *Surat Al Kahf 18:82* isemayo:

﴿وَأَمَّا ٱلْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِى ٱلْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُۥ كَنزٌ لَّهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحاً فَأَرَادَ رَبُّكَ أَن يَبْلُغَآ أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنزَهُمَا رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ وَمَا فَعَلْتُهُۥ عَنْ أَمْرِى ذَٰلِكَ تَأْوِيلُ مَا لَمْ تَسْطِع عَّلَيْهِ صَبْراً﴾

Waamma aljidaru fakana lighulamayni yateemayni fee almadeenati wakana tahtahu kanzun lahuma wakana aboohuma salihan faarada rabbuka an yablugha ashuddahuma wayastakhrija

kanzahuma rahmatan min rabbika wama faAAaltuhu AAan amree dhalika ta/weelu ma lam tastiAA AAalayhi sabran *(Surat Al Kahf 18:82)*

Tafsir: ***Ama kuhusiana na Ukuta basi ulikua ni wa Watoto wawili wa kiume Mayatima katika Mji na chini yake kulikua na hazina kwa ajili yao na baba yao alikua ni Mtu mwema. Hivyo alitaka Mola wako kua wabaleghe na kisha waichukue hazina yao kama Rehma kutoka kwa Mola wako, nami sikutekeleza hivyo kwa amri yangu tu. Hio ndio maana ya yale uliyoshindwa kua na Subra nayo.***

Na pia kuhusiana na aya hii basi kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Muhammad Ath Thalabi basi yeye anasema kua: '**Abu Darda *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Maana ya maneno yasemamayo: W*akana tahtahu kanzun lahuma*' yaani '*na chini yake kulikua na hazina kwa ajili yao*' basi yalikua yanamaanisha kua hazina hio ilikua ni Dhahabu na Fedha, na baba yao ambae alikua akiitwa Kashish alikua Mcha Mungu aliekua kwenye Msitari ulionyooka. Walihifadhiwa kwa sababu ya Baba yao, ingawa haukuzungumziwa ucha Mungu wao. Lakini baina yao na Baba yao ambae walihifadhiwa kutokana nae basi kuna Mababa 7''**

Sijui tumefahamu kuhusiana na maneno haya ama la. Ila kama hatujafahamiana basi inatubidi tufahamu kua Unapofanya Mema basi hua si kwa ajili yao tu, kwani Mema yako hua ni yenye kukupandisha Darja wwewe mwenyewe Mbele ya Mola wako, na pia hukinufaisha Kizazi chako

Na manufaa hayo hua hayawanufaishi watoto wako tu bali pia neema zake huweza kuwafikia hata Wajukuu zako na Virembwe wao. Na hizo ndio fadhila za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa waja wake wafanyao mema.

Kwani inabidi kila mmoja wetu ajiulize kwa kusema Hivi kwanini mimi na wewe hatupendi kufanya mema na badala yake tunafanya maasi tu? wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi aa Salam* kupitia kwenye Qur'an na Hadith basi tayari ameshatuelezea Manufaa yake? Hivi jee tunasubiri nini?

Hivi Jee tunajali Akhera yetu? Na manufaa ya Vizazi vyetu? Baada ya kufariki kwetu? Hivi Jee tunawajli kweli watoto wetu na vizazi vyetu? Kwa Sababu kama tunajali basi tungefanya mema alikotuamrisha Mola wetu na kuachana na makatazo ya Mola wetu

Hivyo kwa upande wa hazina hio basi Wanazuoni wametofautiana pia kwani kuna wasemo kua: Hazina hio ilikua ni Kartasi zilizoandikwa Ilm Kubwa ndani yake, na huu ni mtizamo wa Said Ibn Jubayr, ambapo kwa upande wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kua: Ni pande la Dhahabu na kwa upande wa Ikrimah basi amesema kua ni Hazina hio ni Mali pia kuna wasemo kua ilikua ni hazina ya mali na dhahabu.

Tunapoziangalia aya tatu hizi alizotumia Al Khidhr katika kumfafanulia kwake Nabii Musa juu ya yale aliyoshindwa kua na ustahamilivu nayo kutokana na kutokua na Ilm nayo, na hivyo yeye Al Khidhr kuyabainisha kwa sababu ya kua na Ilm nayo basi alitumia maneno matatu tofauti katika kila tukio kulingana na mazingira yake ambapo maneno matatu hayo yote yametokana na neno *Rada.*

Neno *Rada* hua ni lenye kumaanisha Kutafuta, Kuomba kitu kwa upole, Kutaka, Kutembea tembea kwa taratibu. Neno *Rada* ndio lililotoa neno *Iradatun* ambalo humaanisha Khiari, Kua na Uhuru wa Kutaka kufanya kitu au jambo. Neno *Rada* ndio lililotoa maneno *Faaradtu, Faaradna, Faarada*

ambayo Al Khidhr aliyatumia kuwakilisha namna ya utekelezaji wa Majukumu hayo ulikua unatokana na matakwa ya nani.

Ambapo Al Khidhr alipoelezea tukio la kwenye Jahazi katika *Surat Al Qasas 18:79* basi alisema:

﴿فَأَرَدتُّ أَنْ أَعِيبَهَا﴾

‘***Faaradtu an aAAeebaha’*** yaani ‘**Hivyo *nilitaka mimi Aibu (Kulitia kasoro)’***

Na hivyo alitumia neno *Faaradtu* kuwakilisha hoja yake kua Jambo hilo halikutokana na Amri ya A*llah Subhana wa Ta’ala,* kwani yeye Al Khidhr alifanya hivyo kutokana na kupewa Habari na *Allah Subhanaha wa Ta’ala* kuhusiana na hali ya maisha ya wenye Jahazi na hali ya Jahazi lenyewe na namna wanavyolitegemea, na pia kupewa habari kuhusiana na namna Mfalme huyo anavyotaifisha Majahazi.

Hivyo kutokana na kupewa habari hizo basi akajua kua jukumu lake yeye ni kulitia aibu au kulitia kasoro jahazi hilo, kutokana na Ufahamu wake aliojaaliwa na Mola wake yaani hii inakua na kama alivyonasibisha Nabii Ibrahim pale aliposema.

﴿ٱلَّذِى خَلَقَنِى فَهُوَ يَهْدِينِ ۝ وَٱلَّذِى هُوَ يُطْعِمُنِى وَيَسْقِينِ ۝ وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ﴾

Alla<u>dh</u>ee khalaqanee fahuwa yahdeeni; Waalla<u>dh</u>ee huwa yu<u>t</u>AAimunee wayasqeeni; Wa-i<u>dh</u>a mari<u>dh</u>tu fahuwa yashfeeni *(Surat Ash Shuara 26:78-81)*

Tafsir: ***(Kwani) Ni yeye ndie alieniumba na akaniongoza; Na ndie anaenilisha na kuninywesha; Na ninapoumwa ndie anaenipa afya’***

Ambapo hapa Nabii Ibrahim amenasibisha kuumwa kwake kua hua ni kutokana na yeye mwenyewe na hali ya afya yake na kupona kwake hua kunatokana na Mola wake.

Na kisha Al Khidhr alipoelezea tukio la Kumuua yule mtoto katika aya ya *Surat Al Qasas 18:81 basi alisema:*

﴿فَأَرَدْنَآ أَن يُبْدِلَهُمَا رَبُّهُمَا﴾

‘***Faaradn<u>a</u> an yubdilahum<u>a</u> rabbuhum<u>a</u>***’ yaani ‘**Hivyo Tulitaka awabadilishie Mola wao**’ na hivyo alitumia neno *Faaradna* kuwakilisha hoja yake katika hali ya kua jambo hilo lilitokana na Amri ya *Allah Subhnah wa Ta’ala* na pia lilitokana na Khiari yake yeye Mtekelezaji, yaani yeye aliamrishwa afanye hivyo na akatekeleza pia kutokana na yeye mwenyewe kua ni mwenye kutaka kufanya hivyo baada ya kupewa habari hio juu yake.

Na kisha Al Khidhr alipoelezea tukio la Kuujenga Ukuta wa Nyumba uliokua unataka kuanguka katika aya ya *Surat Al Qasas 18:82* basi alisema:

﴿فَأَرَادَ رَبُّكَ﴾

‘***Faar<u>a</u>da rabbuka***’ yaani ‘**Hivyo Alitaka Mola wako**’

Na hivyo alitumia neno *Faarada* kuwakilisha hoja yake katika hali ya kua jambo hilo lilitokana na Amri ya *Allah Subhnah wa Ta'ala* bila ya yeye kutaka na hii ni kwa sababu yeye hakua ni mwenye kujua matokeo yake yatakuaje hapo baadae, isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie mwenye kujua, na hivyo kututhibitishia kua, hakuna anaejua kuhusiana na *Ghayb* isipokua *Allah Subhnah wa Ta'ala* na hivyo kutokana na Hikma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi humfunulia habari hizo amtakae juu ya yale ayatakayo kua Kiumbe wake husika aliemchagua kujua ayajue, kama alivyosema katika Qur'an:

﴿عَالِمُ ٱلْغَيْبِ فَلاَ يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَداً ۞ إِلاَّ مَنِ ٱرْتَضَىٰ مِن رَّسُولٍ فَإِنَّهُ يَسْلُكُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ رَصَداً ۞ لِّيَعْلَمَ أَن قَدْ أَبْلَغُواْ رِسَالاَتِ رَبِّهِمْ وَأَحَاطَ بِمَا لَدَيْهِمْ وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَداً﴾

AAalimu alghaybi fala yu*dh*hiru AAala ghaybihi ahadan, Illa mani irtadha min rasoolin fa-innahu yasluku min bayni yadayhi wamin khalfihi rasadan, LiyaAAlama an qad ablaghoo risalati rabbihim waahata bima ladayhim waahsa kulla shay-in AAadadan *(Surat Al Jin 72:26-28)*

Tafsir: ***Ni yeye (pekee) ndie anaejua kuhusiana na Ghayb, na hivyo hamdhihirishii yeyote yule kuhusiana na Ghayb. Isipokua Mtume wake aliemchangua na hivyo humuwekea waangalizi mbele yake na nyuma yake. Ili wapate kujua kua wameleta na kuufikisha Ujumbe wa Mola wao, na ni yeye aliekizunguka kila walichonacho na huchukua hesabu juu ya kila kitu.***

Hivyo basi Al Khidhr kutokana na kua ni miongoni mwa wale ambao waliochaguliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ni wenye kufunuliwa habari za *Ghayb* kutoka kwa Mola wao basi anaweka wazi kua hakuujenga ukuta huo isipokua aliujenga kutokana na amri ya Mola wake Nabii Musa ambae pia ndie Mola wa Al Khidhr na ndie Mola wa Ulimwengu wote, kama zinavyobainisha aya pale ziliposema:

﴿وَأَمَّا ٱلْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلاَمَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِى ٱلْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُ كَنزٌ لَّهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحاً فَأَرَادَ رَبُّكَ أَن يَبْلُغَآ أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنزَهُمَا رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ وَمَا فَعَلْتُهُ عَنْ أَمْرِى﴾

Waamma aljidaru fakana lighulamayni yateemayni fee almadeenati wakana tahtahu kanzun lahuma wakana aboohuma salihan faarada rabbuka an yablugha ashuddahuma wayastakhrija kanzahuma rahmatan min rabbika wama faAAaltuhu AAan amree *(Surat Al Kahf 18:82)*

Tafsir: ***Ama kuhusiana na Ukuta basi ulikua ni wa Watoto wawili wa kiume Mayatima katika Mji na chini yake kulikua na hazina na baba yao alikua ni Mtu mwema. Hivyo alitaka Mola wako kua wabaleghe na kisha waichukue hazina yao kama Rehma kutoka kwa Mola wako, nami sikutekeleza hivyo kwa amri yangu tu.***

Hivyo Al Khidhr akamwambia Nabii Musa baada ya kumfafanulia malengo na madhumuni yaliyompelekea ufanya kama alivyofanya kwa kusema: '**Ewe Musa ulinilaumu mimi kwa**

kulitoboa Jahazi, Kumuua Mtoto na Kuusimamisha Ukuta kwa ajili ya kukimbilia malipo mbele ya Mola wangu kesho Akhera.

Hakika wewe ulinilaumu kwa kutoboa Jahazi kwa kukhofia kua watu wake watazama ndani yake na hivyo kua ni mwenye kusahau kua wakati Mama yako alipokutia kwenye Maji ya Mto Nile, wewe ulikua mtoto mchanga, dhaifu na bado *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikulinda na kukuhifadhi.'

Na ulinilaumu mimi kwa kumuua Mtoto ambae ni Kafiri bila ya sababu yeyote, na hivyo ukawa ni mwenye kusahau kua wewe mwenyewe ulimuua Mmisri bila ya sababu yeyote.

Na ulinilaumu mimi kwa kutotaka malipo nilipounyanyua Ukuta na hivyo kua ni mwenye kusahau kua hata wewe ulichota maji na kuwapa wanyama wa Shuayb kwa ajii ya Malipo ya kesho Akhera kwa ajili ya Mfalme wa siku ya Malipo.

Kisha baada ya hapo, basi Nabii Musa na Joshua wakaachana na Al Khidhr na kurudi Jangwani kwa ajili ya kukutana na watu wa Bani Israil. Ambapo katika kisa hiki ndani yake pia tunajifunza mambo yafuatayo:

1-Ni jambo muhimu sana kwa kila mwenye kutafuta Ilm kujihisi kua ana upungufu katika Ilm yake na hivyo awe tayari kutafuta njia ya kujiongezea Ilm.

2-Mwenye kutafuta Ilm anatakiwa awe mnyenyekevu kwa mwalimu wake pale inapokua Mwalimu huyo hayuko katika njia za kumuasi Mola A*llah Subhanah wa Ta'ala.*

3-Mwanafunzi anatakiwa awe na Heshima, Adabu, Ukarimu, na Upole kwa Mwalimu wake.

4-Inakubalika kwa mtu kufanya Dhambi ndogo kwa ajili ya kuepusha Dhambi kubwa.

5-Wazazi wema hata kama wameshatangulia Akhera basi hua na uwezo wa kunufaisha vizazi vyao kutokana na mema yao waliyoyafanya hapo kabla kama vile ambavyo watoto wema hua na uwezo wa kuwanufaisha wazazi wao waliokwisha tangulia Akhera kutokana na mema wanayoyafanya watoto wao katika wakati wa uhai wao.

6-Umuhimu wa kua na ukarimu na kufanya mema hata kwa wale waliokufanyia maovu, yaani ingawa inakubalika kulipiza kisasi kwa maovu bila ya kuvuka mipaka ya kisasi, lakini kusamehe na kua na ukarimu ni bora zaid.

Tumalizie kisa cha Al Khidhr na kauli ya Imam Ahmad Ibn Muhammad Ath Thalabi ambae anaendelea kutuambia kua: '**Amesema Abu Ummamah Al Bahili *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliuliza kwa kusema :** '**Jee nikupeni nyie habari ya Al Khidhr?**' Masahaba wakaitikia kwa kusema: '**Bila ya Shaka *Ya Rasul Allah!***'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema:* 'Wakati Al Khidhr alipokua anatembea katika moja kati ya masoko ya Bani Israil, basi akakutana na miongoni mwa masikini wa Bani Israil ambae alimwambia Al Khidhr kwa kusema kua: 'Allah akubariki, naomba Sadaka yako!'

Al Khidhr akajibu: 'Hakika mimi Namuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na hivyo alitakalo *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua basi litakua. Na sina cha kukupa.' Hivyo Mtu wa Bani Israil

akarudia kwa kusema: ‘Allah akubariki, naomba Sadaka yako! Hakika mimi naona uso wako umejaa Huruma na hivyo nataka Huruma iliyomo ndani ya Moyo wako.’’

Al Khidhr akajibu: ‘Hakika mimi Namuamini *Allah Subhanah wa Ta’ala*, na hivyo alitakalo *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua basi litakua. Na sina cha kukupa. Lakini kamata mkono wangu ili uniuze humu ndani sokoni’ Yule mtu wa Bani Israil akasema: ‘Itakua kama unavyotaka iwe?’ Al Khidhr akajibu: ‘Mimi ninasema ukweli, na wewe umetaka jambo kubwa sana kwani umeniulizia kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta’ala* nami nimekujibu kua chukua mkono wangu ili uniuze ndani ya soko hili.’

‘Hivyo Mtu huyo wa Bani Israil akamkamata mkono Al Khidhr akapita nae sokoni kumuuza na akafanikiwa kumuuza kwa Dirham 400. Hivyo Al Khidhr akakaa na Mmiliki wake huyo kwa siku kadhaa, lakini hata hivyo Mmiliki huyo hakuona manufaa yeyote kutokana nae. Hivyo Al Khidhr akasema kumwambia Mmiliki wake huyo kua: ‘Niajiri’.

Mmiliki huyo akasema kumwambia Al Khidhr: ‘Hakika wewe ni mtu mzima sana, nami sipendi kukuzidishia Uzito wa majukumu’ Al Khdhr akasema: ‘Hutonizidishia uzito wa Majukumu’ hivyo Mmiliki huyo akasema: ‘Basi Nyanyuka unisaidie kulisogeza hili jiwe kutoka hapa hadi pale.’ Hilo Jiwe lilikua ni jiwe kubwa ambalo haliwezi kuondolewa isipokua na watu 6 kwa mda wa siku nzima. Lakini kwa upande wa Al Khidhr alilihamisha jiwe hilo kwa mda wa saa moja, kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* alimtumia Malaika akawa ni mwenye kumsaidia Al Khidhr’

Hivyo mmiliki huyo wa Al Khidhr akafurahi sana na akasema kumwambia Al Khidhr: ‘Hongera sana’ kisha Mmiliki huyo akawa anataka kusafiri hivyo akamwambia Al Khidhr: ‘Kwa hakika mimi nakuona wewe kua ni Mja mwema mcha Mungu na Muaminifu na mwenye wasia mzuri hivyo chukua nafasi yangu katika Jamii yangu’

Al Khidhr akasema: ‘*In-shaa Allah*, lakini bora nitumie mie kwa jambo jengine’ Mmiliki akasema kumwambia Al Khidhr: ‘Hakika mimi sipendi kukubebesha Mzigo’ Al Khidhr akasema: ‘Hutokua ni mwenye kunibebesha Mzigo Mkubwa’ hivyo yule Mmiliki akasema: ‘Sawa, basi nifanyie matofali kwani nataka kujenga kasri nitakaporudi’ kisha akasafiri.

Na aliporudi kutoka safarini akakuta Al Khidhr tayari ameshajenga Kasri kama alivyotaka liwe Mmiliki wake huyo, hivyo akashangaa sana na kumuuuliza Al Khidhr: ‘Hebu niambie hivi wewe ni nani?’ Al Khidhr akajibu: ‘Mimi ni Mtumwa wako ulie ninuanua’ yule mmiliki akasema: ‘Nakuomba kwa jila la Allah ni ambie wewe ni nani.’

Al Khidhr akasema: ‘Hiki ni kiapo ambacho kimenifanya mimi niwe mtiifu. Ama kuhusiana na mimi basi mimi ni Al Khidhr, Omba omba aliniomba mimi sadaka kwa ajili ya Mola wangu kumpa yeye, lakini mimi nikawa sina cha kumpa. Hivyo nami nikamkubalia aniuze. Kwani imenifikia mimi kua yeyote yule, atakaeombwa na Mola wake na mtu huyo akawa na uwezo lakini akawa hakumtimizia haja yake yule alieomba basi atasimama katika siku ya Malipo mbele ya Mola wake huku Uso wake ukiwa hauna ngozi wala nyama bali una mifupa mitupu inayogongana’

Hivyo Mmiliki huyo wa Al Khidhr aliposikia maneno hayo akaanza kulia huku akiinama na kumbusu Al Khidhr na huku akisema: ‘**Naapa kwa Mama yangu na Baba yangu, kwa hakika mimi nimekufanyisha kazi wewe zaidi ya uwezo wako, lakini kwa sababu sikukujua hivyo nihukumu kwa Mali zangu na watu wangu, na kama utataka nikuachie huru basi nitakuachia huru’ Al**

Khidhr akasema: '**Ndio lakini mimi ningependa Mtu atakaeniwachia huru ndio awe ni mwenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala***'

Na mtu huyo alikua si mwenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala*, hivyo akasilimu na kua Muislam, kisha akampa Al Khidhr Dinar 400 na kumuachia huru. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'al*a akamshushia *Wahy* Al Khidhr na kumwambia: '**Nilikuokoa wewe kutoka Utumwani, na Kafiri akawa Muumini na nikakupa Dinar moja kwa kila Dirham ili upate kujifunza kua hakuna atakaedhurika na wala kula hasara kutokana na kunitumikia mimi'**

Hivyo baada ya Nabii Musa kuachana na Al Khidhr na kurudi kwa watu wake basi akakumbana na mkasa wa kisa kinachojulikana kama kisa cha Ngo'mbe wa Bani Israil.

AL KHDHR NI NANI

Wanasema Wanazuoni kua Al Khidhr alikua akijulikana kwa jina la Baliya Ibn Malikan Ibn Feleq Ibn Ibar Ibn Shilah Ibn Arpachshad Ibn Sham Ibn Nuh Alayhi Salam.

Ambapo kuhusiana na historia yake basi tunaona kua inaazia katika wakati wa Safari ya Isra na Miraj ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua njiani basi akasikia harufu nzuri sana na hivyo akamuuliza Malaika Jibril. : '**Ewe Jibril hivi hii harufu nzuri hivi ni ya nini?'**

Ambapo Malaika Jibril akajibu: **'Hapo awali kulikua kuna Mfalme mmoja ambae alikua ni Muadilifu sana kwa watu wake Mfalme huyu alikua na Mtoto mmoja tu wa Kiume na hakua na mtoto mwengine yeyote Hivyo Mfalme huyo akamtafutia Mtoto wake huyo Mwalimu wa kusomesha Ilm na alipopatikana basi ikawa mtoto huyo ikawa kila siku anatoka na kuenda kusoma kwa Mwalimu wake huyo, lakini kabla hajafika kwa mwalimu sake basi njiani kulikua na Nyumba ya Mzee Mmoja ambae ni Mcha Mungu Mkubwa sana na hivyo Mtoto huyo akawa pia na kawaida ya kupita ksa Mcha Mungu huyo na kumsalimia na kua na urafiki nae**

Kiasi ya kua Huyo mtoto alivutiwa zaid na huyo Mcha Mungu kukiko namna alivyovutiwa na mwalimu wake, kiasi ya kua ikafikia wakati ikawa huyu Mtoto akitoka kuenda kusoma basi ikawa hafiki kwa Mwalimu wake stahiki bali alikua akimalizia kwa Mwalimu wake huyo Mcha Mungu Na hivyo Mtoto huyo akakulia katika Mazingira ya kua na Ukaribu sana na Mcha Mungu huyo na pia na Ilm kubwa sana na tabia kama za Mcha Mungu huyo.

Kwani Ulipowadia wakati wa kuoa basi Washauri aa Mfalme wakamshauri kua bora mtoto wake huyo aowe ili kuendeleza kizazi kwa miaka inaenda na Mfalme hana Mjukuu. Lakini Mtoto huyo alipoambiwa kuhusiana na kuoa basi akakataa kuoa. Lakini hata hivyo Mfalme huyo hakuvunjika Moyo bali alimuachia mtoto wake kwa muda na kisha akamshauri tena aoe.

Na hivyo mara hii ya pili Mtoto huyo akakubali kuoa na akatafutiwa Bint aliekua bora kuliko wote kwa uzuri wa Sura, Maumbile na Tabia, Na harusi ikafanywa na Mtoto huyo akaoana na Binti huyo na wakaaa wanaishi Pamoja na mbali ya kua Mfalme alikua ni Muadilifu lakini alikua ni Mtu ambae asieamuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo Kiimani basi Mfalme alikua akiendana kinyume na mtoto wake ambae yeye kutokana na kukua kwenye Mazingira

ya Ucha Mungu wa Mwalimu wake basi alikua ni mtu mwenye kumuamini *Allah Subhanah wa Taala* kwa kisiri siri bila ya Baba yake kujua.

Na ndio maana mtoto alikua hataki kuoa kwa sababu alikua akijua kua akioa basi itabidi siri yake hio itoke nje na huenda akagombana na Baba yake. Hivyo baada ya Harusi basi kijana huyo akamwambia Mke wake kua: '**Hakika mimi nna siri kubwa sana ambayo nataka nikuambie na kama utakubaliana nami basi Mungu wangu ambae ni *Allah Subhanah aa Ta'ala* alieumba kila kitu atakuweka mbali na Maovu ya Hii Dunia na pia atakuweka mbali na Adhabu za siju ya Malipo. Lakini kama ukiitoa Siri yangu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakuadhibu wewe hapa Duniani na katika siku ya Malipo pia.'**

Hivyo Mke wake huyo akauliza kwa kusema: '**Jee ni Siri gani hio?'**

Ambapo kijana huyo akasema**: 'Hakika mimi ni Muislam (mtu mwenye kujisalimisha kwa Mola wangu) Hivyo mimi si Mtu anaefuata Dini ya Baba yangu, na kuhusiana na Wanawake basi si mwenye matamanio nao, hivyo kama utakubaliana nami katika kushikamana na Imani yangu basi nitafurahi lakini kama hutoweza basi unaweza kurudi kwa watu wako na kuendelea na maisha yako pamoja nao.'**

Na Mwanamke huyo akasema**: 'La, hakika mimi sitaki kurudi kwa watu wangu hivyl nitabakia na wewe'**

Na huyu Kijana tunaemzungumzia hapa katika hiki kisa basi ndie Al Khidhr, hivyo Al Khidhr akakaa na mke wake huyo kwa mda na hukukua na hata dalili ya kupatikana kwa mtoto.

Hivyo Washauri wa Mfalme wakamwambia Mfalme kua inaonekana kama Mke wa Mtoto wake ana tatizo kwani mda mrefu umeenda na hawajapata mtoto au Al Khidr ana tatizo. Hivyo Mfalme akasema **: 'La hilo siwezi kuliingilia'**

Washauri wakasema: '**Sawa lakini sasa tatizo ni kua wewe utakua huna mtu wa kukurithi Ufalme wako, hivyo jee itakuaje?'**

Mfalme akatafakkari na kusema kua : **'Maneno yenu ni sahih hivyo wacha nizunguzme nao kisha niwaulize tupate kujua.'**

Hivyo Mfalme akamwita Al Khidhr na kuzungumza nae na Al Khidhr nae akajibu: '**Kupata Mtoto ni mipango ya Mungu kwani yeye ndie ambae humpa amtakae na humpokonya amtakae kwa hikma zake.'**

Baada ya kujibiwa hivyo basi Mfalme akamwita mke wa Al Khidhr na kuzungumza nae ambapo nae akjibu kama alivyojibu Al Khidhr.

Hivyo Mfalme akawaacha kwanza na kisha baada ya mda akamwita Al Khidhr na kumaambia kua bora atafute mke mwengine na kua aachane na mke wa kwanza. Al Khidhr akapinga lakini mwisho ikabidi akubaliane na maamuzi hayo na hivyo akamuacha Mke huyo na akatafutiwa mke mwengine mpya ambae alikua ni mjane ambae mume wake alifariki na alikua amepata mtoto hapo kabla.

Na baada ya ndoa Al Khidhr akasema kumwambia Mke huyo kama alivyomwambia mke wa Mwanzo ambapo mke huyo ne akajibu kama alivyojibu mke wa mwanzo kua atabakia nae. Na baada ya mda kupita hali ikawa vile vile yaani hakuna dalili ya kupatikana kwa mtoto. Hivyo Mfalme akamwita

tena A Khidhr na kumuuliza kama alivyomuuliza mwanzo ambapo nae akasema kua Mtoto ni Majaaliwa ya Mungu.

Hivyo Mfalme akamwita mke na kumuuliza: '**Mbona katika ndoa yako ya kwanza umepata mtoto lakini hakuna dalili kutoka kwenye ndoa ya Mtoto wangu.'**

Ambapo mke huyo akajibu: '**Ni kwa Sababu Mtoto wako hajawahi hata kunigusa mie, na hivyo ndivyo ilivyokua kwa mke wake wa kwanza pia.'** Basi Mfalme akamwita yule mke wa mwanzo na kumhoji, ambapo nae akathibitisha ukweli wa maneno hayo.

Na baada ya kudhihirika kwa habari hizo basi Mfalme akaamua kumuita Al Khidhr kisha amuadhibu kutokana na kumfanya Baba yake kua kama mtoto mdogo. Hivyo Al Khidhr nae alipopata habari hio basi akakimbia Mji hua na kutoweka kabisa mbele ya macho ya watu wa Mji huo na baada ya habari ya kukimbia na kutoweka kwa Al Khidhr kumfikia Mfalme basi Mfalme alihuzunika sana kutokana na kuchukuliwa kaa hatua hio na Al Khidhr.

Na hii ni kwa sababu huyu alijua ndie mtoto wake pekee aliekua nae na hivyo sasa amebakia peke yake baada ya kutoweka kwake. Hivyo Mfalme akadhamiria kumtafuta mtoto wake huyo na akatayarisha Jeshi ambalo aliligawa katika vikundi vikundi kwa ajili ya kazi maalum ya kumtafuta Al Khidhr tu katika kila sehemu ya ardhi yake na baharini.

Na kwa bahati nzuri au mbaya moja kati ya Makundi hayo lililokua na Watu 10 likafanikiwa kumjuta Al Khidhr akiwa Kisiwani anakoishi peke yake. Na walipokutana nae na kumuuliza kwanini akakimbia na kuishi hapo peke yake basi Al Khidhr akawaambia kama alivyowaambia wale wake zake kua:

Hakika mimi nna siri kubwa sana ambayo kama nikikuambieni na mtanifahamu na kubakia nayo siri hio basi Mungu wangu ambae ni *Allah Subhanah aa Ta'ala* alieumba kila kitu atakuwekeni mbali na Maovu ya Hii Dunia na pia atakuweka mbali na Adhabu za siku ya Malipo. Lakini kama mkiitoa Siri yangu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakuadhibuni nyote hapa Duniani na katika siku ya Malipo pia'

Hivyo watu hao 10 wakasema**: 'Hamna tatizo tuambie hio Siri yako'**

Hivyo Mke wake huyo akauliza kwa kusema: '**Jee ni Siri Gani hio'?**

Al Khidhr akasema: '**Hakika mimi ni Muislam (mtu mwenye kujisalimisha kwa Mola wangu) Hivyo mimi si Mtu anaefuata Dini ya Baba yangu, hivyo najua kua Baba yangu amekutumeni Na nakuombeni kua msimuambie Baba yangu kua mmeniona na kukutana nami na wala msiwaambie watu wengine kwani mkisema basi ndio utakua mwisho wa Uhai wangu na nyinyi ndio mtakaobeba Jukumu la Uhai wangu.'**

Na hivyo watu hao wakakubaliana na Al Khidhr kua hawatosema chochote na kuagana nae.Lakini walipofika kwa Mfalme basi watu 9 miongoni mwa 10 hao wakasema kua wamemuona na mtu mmoja tu kati yao akasema kua hawakumuona na hivyo watu hao wakakubaliana na Al Khidhr kua hawatosema chochote na kuagana nae.

Na walipofika kwa Mfalme basi watu 9 miongoni mwa 10 hao wakasema kua wamemuona na mtu mmoja tu kati yao akasema kua la hawakumuona yaani..Miongoni mwa watu 10 basi ni Mtu mmoja tu ndie alietekeleza ahadi waliyokubaliana na Al Khidhr kua wasiseme kua wamemuona. Na

waliobakia wote wakamsaliti. Na al Khidhr aliwaaambia watu hao kua kama wakimsaliti kaa kutoa siri basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaadhibu hapa Duniani na Akhera pia.

Ama baada ya watu hao 9 kusema kua Wamemuona Al Khidhr basi wakasema pia juu ya yake aliyowaambia kua yeye si mwenye kufuata Dini ya Baba yake bali ni mwenye kufuata Dini ya Mola wa Ulimwengu wote ambae ni A*llah Subhanah wa Ta'ala.* Ambapo Jambo hili lilimmuudhi na kumtia hasira sana Mfalme na hivyo akawaamrisha watu hao 9 wakamkamate Al Khidhr kwa vyovyote vile itakavyokua na kisha waje nae.

Hivyo ikabidi watu hao 9 watoke kwa ajili ya kurudi kumfuata Al Khidhr. Na kuenda katika sehemu ya kisiwani waliyomkuta hapo awali lakini walipofika basi hawakukuta kitu kwani kisiwa kilikua kitupu, kwani Al Khidhr alijua kua watu hao watamsaliti na watarudi kumkamata hivyo akaondoka mara tu baada ya wao kuondoka.

Hivyo wakarudi kaa mfalme na walipofika na kutoa habari waliyokuja nayo kua wamemkosa na haaakumuona Al Khidhr. Basi Mfalme akaona kua Watu hao walimdanganya na kusema uongo, kwani aliesema ukweli ni yule mmoja aliesema kua hawakumuona.

Hivyo tukio hili likamyia hasira zaid Mfalme na akaamrisha watu hao 9 kuuliwa na wakauawa huku wakikumbuka kua Al Khidhr alisema kua kama watamsaliti basi wataadhibiwa hapa hapa Duniani kwanza. Kwani Mfalme akamwita yule Mke wa Pili wa Al Khidhr alievujisha Siri pia na akamwambia: **‘Hakika wewe uliniambia uliyoniambia kwa sababu ulipanga na Mtoto wangu ili apate kukimbia Hivyo adhabu yako ni kifo kwani umemsaliti Mfalme’**

Ambapo Bibi huyo nae akauliwa huku akikumbuka Maneno ya Al Khidhr kua akimsaliti basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamuadhibu hapa hapa Duniani.

Na hivyo miongoni mwa watu waliofichuliwa siri ya Al Khidhr wakabakia watu wawili ambao Mfalme alikua akiwatafuta ambao ni yule mmoja kati ya 10 ambae hakuvunja ahadi ya Al Khidhr na pia mke wa mwanzo wa Al Khidhr ambae nae hakuvunja Ahadi pia Ambao hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akiwanusuru kwani nao baada ya kusikia tu kuhusiana na adhabu ya kifo ya watu 9 na mke wa pili aa Al Khidhr basi nao wakawahi kuukimbia Mji kabla hawajachelewa.

Na katika kukimbia kwao basi wakaja wakakutana njiani wakiwa mafichoni na kutokana na kua ni wenye kumkimbia adui mmoja na kumkimbilia Allah Subhanah wa Ta'ala amabe alijaalia kua ni wenye kukutana njiani pale Mwanamke huyo alipolitaja jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kuomba kwake msaada kutoka kaa Mola wake.

Hivyo yule mwanamme akasikia sauti hio na Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na alipolelekea katika upande aliosikia sauti hio basi akamuona Mwanamke huyo na alipomhoji kuhusiana na amejuaje ju ya Allah Subhanah ya Ta'ala basi Mwanamke akasema yaliyomfika na Mwanamme nae akaelezea kisa chake pia na kwanini akakimbia. Hivyo kutokana na kua na hali moja ya ukimbizi kutoka kwenye Kiza kuelekea kwenye Nuru ya *Allah Subhabah wa Ta'ala* basi wakaamua kua waoane ili aawe pamoja katika safari yao hio.

Na katika Safari yao hio basi wakawasili katika Kijiji kimoja ambacho waliamua kuanzisha makazi yao na hivyo wakajenga Nyumba na kuishi hadi wakapata watoto watatu,

Na kwa kua katika eneo lao walikua ni Waislam peke yao basi Mume Mtu akamwambia Mke wake kua: **Mimi nataka nitakapofariki au yeyote miongoni mwetu atakapofariki basi azikwe ndani**

ya yetu hii Kwani sitakia kua Maiti zetu zijumuishwa na wasiomuamini Allah Na hivyo itakapofikia Mtu wa mwisho kwetu kifariki basi na yeye aamrishe hivyo hivyo kisha hii nyumba ivunjwe yote.'

Na baada ya miezi kadhaa yule mwanamme akafariki na akazikwa ndani ya Nyumba hio. Hili la kuzikwa ndani ya Nyumba yake lilikua ni jambo ambalo liliwashangaza watu hadi habari ikamfikia Mfalme wa eneo la Ardhi hio ambae nae alikua pia si Muislam.

Na mfalme alipopata habari hio basi akamwita mwanamke huyo na Watoto wake watatu na kuwahoji huku akiwataka wafuate Imani ya Dini yake. Lakini familia hio ikakataa. Mfalme akaamrisha kuwashwa Moto kisha likawekaa Sufuria kubwa sana la Mafuta ambayo yalichomwa hadi kuchemka na kisha akamwambia Mama huyo kua atawaingiza ndani yake mafuta hayo mmoja baada ya mmoja kama hawatoikana Imani yao hio.

Lakini hata hivyo Familia hio haikutetereka. Hivyo akachukuliwa mtoto wa kwanza na akatumbukizwa kwenye Mafuta hayo na akaangika hadi akafa na kuupata ushahidi. Kisha Mama akatakiwa aikane Imani yake. Lakini akakataa, na hivyo akachukuliwa mtoto wa pili na akaingizwa na kukaangika na kuupata Ushahidi.

Kisha Mama akapokonywa mtoto wake wa tatu ambae ni mchanga. Mama hasira zikampanda na huruma ikamzidi akataka kuwavamia walinzi wa Mfalme kuwaomba wasubiri. Lakini Mtoto huyo ambae alikua hajaanza hata kusema bado basi alisema: **Kua na Subra na Ustahmilivu ewe Mama yangu kwani sisi sote tunafikia Peponi**

Mama akashangaa na kisha akatabasam na kusema kumwambia Mfalme kua**: Mimi nitaingia na Mtoto wangu huyu pamoja, na mkishatuunguza basi nataka mifupa yetu mkaizike ndani ya Nyumba yetu, Kisha Nyumba hio Ivunjeni yote**

Hivyo Mfalme akakubalia maombi hayo na kisha Mama akaingia Sufuriani na Mtoto wake. Hivyo ndivyo Malaika Jibril alivyomwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua kwenye Safari ya Miraj na kisha akasikia Harufu nzuri na kuumuuliza ni harufu ya nini.

Na Malaika Jibril akasema kua hio ni Harufu ya Sehemu iliyokuwepo Nyumba yao ambayo wamezikiwa ndani yao.

Kwani Wanazuoni wengine wanasema kuhusiana na kisha hiki cha Al Khidr kua mda baada ya kutoweka kwa Al Khidhr kutoka katika Kisiwa alichokimbilia basi kuna kuna Wasafiri waliokua kwenye Jahazi ambao walikumbwa na Gharika na Jahazi hio ikazama. Hivyo kuna baadhi yao wakafa na baadhi wakavutwa na Maji hadi Ufukweni mwa kisiwa wasichokijua.

Na walipokuta kwenye kisiwa hicho basi mara wakamuona Mtu ambae amevaa nguo Nyeupe akiwa anasali kwenye eneo la mwambao huo wa Bahari. Na baada ya kusali basi akawageukia na kuwauliza kwa kusema: **Jee nyinyi ni kina nani?**

Watu hao wakajitambulisha na kuelezea kisa chao kisha mtu huyo nae akajitambulisha kua ni Al Khidhr. Kisha akasema**: 'Alhamd lillah kwa kua na Usalama, hivyo nami nakupeni khiari mchague kua mbakie hapa pamoja nami kwa ajili ya kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambapo nae atakujaalieni riziki yenu hapa hapa Au kama mnataka basi mnaweza kurudi katika Mji wenu. Lakini sasa kama mtarudi kwenu basi kuna sharti ambalo itabidi mlitekeleze, na sharti hilo ni kutosema chochote juu yangu.'**

Hivyo watu hao wakaona la hapo kisiwani hapakaliki kwani hakuna kitu chochote isipokua Msitu na Bahari. Na wakaamua kua bora warudi kwao na hawatosema chochote juu yake. Hivyo Al Khidhr akanyayua mikono juu akamuomba Kola wake na mara kikatokea kiwingu ambacho kilishuka hadi ufukweni hapo na kisha Al Khdhr akakiuliza kinaelekea wapi na kama kinaweza kuwachukua watu hao hadi katika ardhi yao.

Na hivyo Kiwingu hicho kikafunguka na kugawika na kisha Al Khidhr akawaambia watu hao waingie ndani yake. Kisha Kiwingu kikajifunga na kikaondoka na watu hao na kisha kikawashusha kila mmoja kati ya watu hao juu ya Nyumba zao.

Na baada ya tukio hili la Miujiza basi Baadhi yao watu hao wakashindwa kujizuia na wakaanza kuhadhithia hadi habari ikamfikia Mfalme.Hivyo watu hao wakaitwa na kuelekezea yaliyotokea na mmoja kati yao akakanusha juu ya tukio hilo.

Hivyo yule aliekanusha akafungwa Jela na kisha waliobakia wakapewa Jahazi wakamfuate Al Khidhr ambapo nao wakafunga Safari kumfuata katika kisiwa aalichoangukia mara ya mwisho lakini wakipofika basi wakakisachi kisiwa kizima bila ya kuona hata Dalili ya mtu.

Hivyo wakarudi na walipoka na kutoa habari yao mpya basi wakakamatwa na kuuliwa kwa usaliti na yule aliakana kua haaajumuona Al Khidhr basi akaachiwa, watu wa mji huo wakaendelea kuishi maisha yao wakiwa katika Dhulma hadi ikawashukia Adhabu ya Maangamizo kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia kwa Malaika Jibril.

Na hakuna alieokoka na adhabu hio isipokua yule mtu mmoja pamoja na mkewe. Hivyo kutokana na kua wako peke yao basi wakaamua kuuha Mji na kuhamia katika Mji mwengine na wakajikuta kua wamehamia katika Ardhi ya Misri kwa Fir'awn. *Allah Subhanah wa Ta'ala* akajaalia wakapata Mtoto mmoja na kisha Mke akaajiriwa na Firawn akawa ni Msusi wa Mtoto wa Firawn.

Ambapo alikua ni Mcha Mungu lakini siku moja wakati anamchana nywele Binti huyo basi limakuanguka shanuo ambapo nae akasema: **Subhanah Allah! Shanuo limeanguka kutokana na kukanushwa kwa Mungu mmoja.**

Hivyo binti akauliza**: 'Nani akiemkanusha Baba yangu?'**

Msusi akajibu : **'Aliekanushwa ni *Allah Subhanah aa Ta'ala* ambae ndie Mungu wangu na wako na wa baba yako na wa kila kitu'**

Baada ya kuskia majibu hayo Binti wa Fir'awna akafikisha ujumbe kwa baba yake na Msusi akaitwa pamoja na familia yake kukanusha aliyoyasema, lakini wakagoma na hivyo akachukuliwa mtoto wa kwanza na akatumbukizwa kwenye Mafuta hayo na akaangika hadi akafa na kuupata ushahidi. Kisha Mama akatakiwa aikane Imani yake. Lakini akakataa, na hivyo akachukuliwa mtoto wa pili na akaingizwa na kukaangika na kuupata Ushahidi.

Kisha Mama akapokonywa mtoto wake wa tatu ambae ni mchanga. Mama hasira zikampanda na huruma ikamzidi akataka kuwavamia walinzi wa Mfalme kuwaomba wasubiri. Lakini Mtoto huyo ambae alikua hajaanza hata kusema bado basi alisema: **Kua na Subra na Ustahmilivu ewe Mama yangu kwani sisi sote tunafikia Peponi**

Ama tunapozungumzia kuhusiana na Uhai na Maisha ya Al Khidhr basi hua tunazungumzia Maisha ya Kiumbe Ibn Adam ambae Wanazuoni wametofautiana juu ya kipindi cha wakati alioishi.

Kwani kuna wanaosema kua Al Khidr aliishi katika kupindi cha kabla ya kuishi Dhu Al Qarnayn ambae tutamzungumzia baadae kidogo kwenye Tafsir ya Surat Al Kahf. Ambapo Wanazuoni wanaosema hivyo akiwemo Imam Muhammad Ibn Jarir Al Tabari basi wanasema kua:

Al Khidhr na Baba yake waliishi katika kipindi Afaridin ambae alikua ni Mtoto wa Al Qaba ambae aliishi katika kipindi cha kabla ya kuishi Dhu Al Qarnayn ambae aliishi katika kipindi takriban na kipindi cha Nabii Ibrahim

Na Alikua ndie Mtawala Bir Al Yasa ambalo ni eneo lililokua na kisima alichokifukua Nabii Ibrahim baada ya kufukika kwake na Al Khidhr alikua pamoja pia na Dhu Al Qarnayn na Jeshi lake katika Safari yake ya kuizunguka Dunia

Na wakati Dhu Al Qarnayn na Jeshi lake hilo lilipowasili kwenye Mto wa Maji ya Uhai basi ilikua hakuna hata mmoja aliekua akijua juu ya Maji ya Mto huo ambapo alikua ni Al Khidhr tu ndie alieujua na ndie aliekunywa Maji hayo na hivyo kua ni mtu mwenye kuishi hadi hii leo

Na kuna wanaosema kua Dhu Al Qarnayn ambae aliishi katika kipindi cha Nabii Ibrahim ambae ndani ya jeshi lake alikuwepo Al Khidhr basi alikua ndie Afarudin mwenyewe na pia kuna wanaosema kua Al Khidhr alikua ni Mtoto wa mmoja kati ya Watu waliokua wakimuamini Nabii Ibrahim.

Lakini kwa upande kwa Imam Muhammad Ibn Is-haq basi yeye anasema kua: '**Amesema Imam Wahb Ibn Munabih kua Al Khidr alikua ni Jeremiah Ibn Hilkiah ambae alitokana na Kizazi cha Harun Ibn Amram Harun Ibn Amram alikua ni Nabii alieishi katika kupindi cha Mfalme sa Bani Israil aitwae Josiah Ibn Amon'**

Ambapo hata hivyo tunapoangalia historia basi tunaona kua Mfalme Josia Ibn Amon aliishi katika kipindi cha Nebuchardnezer Mfalme wa Baghdad. Na hivyo kuna utofauti mkubwa wa miaka baina ya Mamlaka ya Afaridin na Nebuchardnezer Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Mutawakil basi anasema kua: **Al Khidr alikua ni Mtu wa Kiajemi na alikua ni rafiki ya Nabii Ilyas na watu wawili hasa walikua wakikutana katika kila wakati wa kipindi cha Sikukuuu.'**

Ambapo amesema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Imam Amr Ibn Dinar kua: **Al Khidhr na Ilyas ndio watu pekee watakaobakia hai ardhini hadi pale Qur'an itakapofutika kisha nao watafutiwa uhai wao.**

Na anasema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mimi nilitoka pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na mara tukasikia sauti kutoka kwa baadhi ya watu fulani, ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m akaniambia 'Anas nenda kaangalie nini kinachotokea**

Hivyo mimi nikaondoka na kuelekea kwenye zogo la sauti hizo na nilipofika nikamiona Mtu akiwa anomba dua kwa kusema: 'Ya Allah! Nihesabu mimi kua ni miongoni mwa Ummah wa Muhammad! Ambao wewe umeuingiza kwenye rehma zako, ambao umesamehewa nawe, ambao umekubaliwa maombi yao, ambao Toba zao ni zenye kukubaliwa'

Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua Hivyo mimi nikageuka na kurudi Kwa Rasul Allah Salallahi alayhi wa Salam na kumwambia kile nilichokiona ambapo nae akaniambia kua

Nenda kamwambie mtu huyo kua *Rasul Allah (Salallahu Alayhi wa Salam)* anakusalimia, na kisha anakuuliza Jee wewe ndie nani?

Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua Hivyo mimi nikaenda kwa mtu huyo na kumpa ujumbe wake kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayh*i wa Salam ambapo Mtu huyo akajibu : 'Nami nifikishie salam zangu kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha mwambie kua Ndugu yako Al Khidhr anakuambia kua Umuombee kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ili nae ajumuishwe kwenye Ummah wake ambao umeingizwa kwenye Rehma, na kusamehewa na kukubaliwa maombi yao na toba zao.'

Kwa upande mwengine bais Al Khidhr alitokea pia pale baada ya kufariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua ni mwenye kujitayarisha kwa ajili ya kumkosha mwili wake basi hali ilikua kama anavyosema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu anhu kua:

Amesema Ali Jbn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Baada ya mimi kutaka kumuweka katika sehemu ya kumkoshea basi nikasikia sauti ikisema: Ali Usimkoshe kwani kwa hakika hakuna kiumbe aliekua msafi kama alivyokua yeye sasa hivi**

Hivyo nami nikageuka na kusema: Ole wako! Hivi wewe ni nani mwenye kusema hivyo wakati *Rasul Allah Aalallahu Alayhi wa Salam* ametuamrisha sisi kufanya hivi kwani ni miongoni mwa Sunna zake!

Na kisha nikasikia Sauti nyengine ikisema: 'Ali Mkoshe, kwani sauti ya kwanza ilikua ni sauti ya Shaytan ambae alikua na wivu kua *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* ataingizwa Kaburini huku akiwa Msafi na Tohara'

Nami nikasema: 'Allah akulipe kwa Mema kutokana na kunionya juu ya Ibilisi ila wewe ni nani?'

Ambapo mtu huyo akajibu: 'Mimi ni Al Khidhr nimekuja Mazikoni kwa *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam*'

Na amesema Imam Nasr Ad Din Burhan Ad Din Al Turkiy Al Hanafi kua: '**Manabii Wanne Bado wako hai, ambapo Wawili wapo Mbinguni na wawili wapo Ardhini. Wawili waliopo hai Mbinguni ni Nabii Idrisa na Nabii Isa Wawili waliopo hai Duniani ni Ilyas na Al Khidhr Ambapo Watatu kati ya Wanne hao Watakufa na mmoja ambae ni Idrisa hatokufa Kwa sababu Idrisa ameshakufa mara moja na hivyo atabakia hadi Peponi hadi katika siku ambayo itatangazwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿ لِّمَنِ ٱلۡمُلۡكُ ٱلۡيَوۡمَ لِلَّهِ ٱلۡوَٰحِدِ ٱلۡقَهَّارِ ﴾

LimaniAl Mulku Al yawma Lillahi Al Wahidi Al Qahari *(Surat Al Ghafir 40:16)*

Tafsir: ***Ufalme ni wa Nani katika siku ya leo?*** **Ni wa Allah pekee asiekua na Mpinzani kwa Kinguvu wala kiuwezo.**

Subhanah Allahi wa Bihamdi Subhanah Allahi Al Adhiim Subhana Allahi Al Wahidi Al Qahari!

Hapa inabidi tukumbushane kua Kimaumbile basi Viumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na Hikma zake basi amewajaalia Viumbe wake hao kua na Maisha ya hali za Darja zifuatazo:

1-Kuna hali ya Maisha tuliyojaaliwa kuishi mimi na wewe ambayo ni maisha ya yanahohitaji mahitajio yote ya Kiumbe Ibn Adam ikiwemo, Kula, Kunywa, Kuvuta Pumzi, Kujisaidia, Kuingiliana kimwili n.k Ambapo katika hali hii tuliyojaaliwa mimi na wewe basi hua ni hali ya kuishi maisha ya muda mfupi kutokana na kua na maumbile ya kuchoka na kuchakaa kaa miili yetu kutokana na Mazingira tunayoishi na maumbile yetu.

2-Kuna hali ya Maisha ya Waliojaaliwa Kuishi kwa muda mrefu sana tofuati na Ibn Adam wengine kama Al Khidhr na Nabii Ilyas. Ambapo hawa kutokana na Maumbile hao basi hua hawana mahitajio kama tunayoyahitajia mimi na wewe kwani mbaki ya kua wao ni Ibn Adam lakini wao hawajitajii Majitaji ya Kiibn Adam, hivyo hua hawali kama tunanyokula sisi na kwani hua hawaoni njaa hivyo hua wanakula kwa kupenda tu sio kwa kutaka.

3-Kuna hali na Maisha waliojaaliwa Ibn Adam ambao wameingia kwenye maisha ya Kimalaika ingawa wana Miili ya Ibn Adam, na hawa ndio kina Nabii Idrisa na Nabii Isa.

4-Kuna hali ya Maisha ya Wanaoishi Mashahidi waliokufa baada ya kuuawa katika Mapigano dhidi ya Maadui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo hua ni hali tofauti na hali ya Duniani na ni tofauti na hali ya Kaburini.

5-Kuna Maisha ya Kaburini ambayo haya kila mtu atayapitia na hali yake hutegemeana na Amali za kila mtu.

Na anasema Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din Ibn Arabi kwa kutuambia kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **amewabakisha Manabii wanne wakiwa hai ndani ya viwiliwili vyao, baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao ni Nabii Idrisa ambae yupo katika Mbingu ya 4, ambapo inabidi tujue kua Mbingu 7 ni sehemu ya Ulimwengu Hivyo nazo pia zitaangamia pamoja na Ulimwengu Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawaweka na kuwabakisha Nabii Ilyas na Nabii Isa ambao wote ni Mitume, na pia Al Khidhr ambae ni Nabii, ingawa Wanazuoni wametofautiana kuhusiana nae.'**

Hivyo tunapomzungumzia Al Khidhr basi ingawa Wafuasi wa Ibn Taymiyyah wanasema kua hayuko hai lakini Wanazuoni wengi sana wanasema kua yuko Al Khidr hai akiwemo Imam An Nawawi, Imam Ibn Salah.n.k

Na anasema Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ana Nawawi kua: '**Wengi miongoni mwa Wanazuoni ni wenye kukubaliana kua Al Khidhr yuko hai na anaishi miongoni mwetu. Na hili ni Jambo lenye makubaliano juu yake Miongoni mwa Watu wenye Ilm ya Tassawuf na watu wenye Ucha Mungu na wenye Maarifah juu ya Mola wao Kwani nukuu zinazohusiana na kushuhudiwa kwake, kuwepo kwake pamoja na watu, kujifunza Ilm kutoka kwake, kuhojiana nae kwa kumuukiza masuali na yeye kujibu zipo nyingi sana. Na kushuhudiwa kwake katika matukio na mazingira ya Mambo mema na ya Peponi ni mengi sana kiasi ya kua hayahesabiki na hayafichiki'** hayo ni maneno ya Imam An Nawawi katika Sharh Sahih Muslim.

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Salah Ad Din Al Kurdi Al Shahrazuhri Al Shafii maarufu kama Imam Ibn Salah basi yeye anasema kua: '**Al Khidhr yuko hai na Wanazuoni na Wacha Mungu wengi wanakubaliana juu ya hili na watu wa kawaida pia wanajua juu hilo.'**

Na kwa Upande wa Al Hafidh Imam Shams Ad zdin Muhammad Ibn Abd Rahma Al Sakhawi basi yeye amesema kua: **'Miongoni mwa Wanazuoni waliowahi kukutana na Al Khidr basi ni Imam An Nawawi'**

Na Imam Abu Fida Imad Ad Din Ismail Ibn Umar Ibn Kathir Al Qurashi Al Dimashq Al Shafii ambae ni maarufu kama Imam Ibn Kathir basi ne anasema kua: **'Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Al Khidhr yuko hai sasa hivi na kuna nukuu nyingi na Ushahidi wa kutosha na Riwaya juu yake'** *(Bidaya Al Nihaya)*

Ambapo miongoni mwa Wanazuoni wanaokubaliana juu ya kua Al Khidhr yupo hai ni pamoja na:

Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Al Hafidh Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqalani ambae anasema kua: '**Amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal katika Kitab Al Zuhd kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Ilyas na Al Khidhr hua wanakutana kila mwaka na huutumia pamoja mwezi wa Ramadhan katika ardhi ya Al Quds Jerusalem.'**

Na ndio maana miongoni mwa sehemu zilizowekwa Alama katika eneo Takatifu la Al Quds basi kuna ile ikiyokuwepo katika Upande wa Kaskazini Mashariki ya Qubat Al Saqqara ambalo ndio lile Kuba la rangi ya Dhahabu ambalo wengi hua wanadhania kua ndio Masjid Al Aqsa. Ambapo hata hivyo ile ni sehemu ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipandia ngazi ya kuelekea Mbinguni. Hivyo Masjid Al Aqsa una Kuba la Rangi nyeusi.

Hivyo Kaskazini Mashariki ya Al Saqqara kuna Mnara mdogo ambao hata hivyo uko juu. Ambapo huo hua ni mnara unaojulikana kama Quba Al Khidhr kwani ni sehemu ambayo Al Khidr alionekana mara kadhaa akiwa anasali katika eneo hilo.

Na Mujaddid Ad Din Al Faqih Imam Al Suyuti pia nae amethibitisha juu ya hayo na pia Imam At Tahawi, Imam Ibn Ata Allah Al Iskandari, na Al Allamah Al Hafidh Al Imam Al Iraqi pia n.k

Miongoni mwa Wasia wa Al Khidhr kwa Nabii Musa ni Pamoja na:

Kama Ibn Adam angekua ni mwenye kua na Subra basi kila mtu angekua ni mwenye kunufaika na mambo mengi saa yenye manufaa naye kuiko anavyotegemea.

Usijihusishe na Mambo yasiyokuhusu.

Usijishughulishe na mambo yasiyokua na maana.

Kamwe usisahau kua ndani ya mazingira yenye kutia khofu hua ni kwenye uwezekano wa kupatikana Usalama, na hivyo kamwe usivunjike Moyo haitowezekana kupata usalama pale utakapokua kwenye mazingira yanayokutia khofu.

Daima kua ni mwenye kufikiria kuhusiana na mwisho wa kila jambo lako.

Usiache kua na ukarimu hadi pale utakapokua huwezi tena kukirimu.

Usiende katika sehemu ambayo hustahiki kuwepo.

Usicheke juu ya yale ambayo hayastahiki kuchekewa.

Usimuadhirishe yule ambae ni mwenye kujuta baada ya kujuta kutokana na makosa yake.

Daima kua ni mwenye kuziona kasoro zako kwanza.

Tafuta Ilm kwa ajili ya kuifanyia kazi na wala si kwa ajili ya kuifafanua.

KISA CHA DHU AL QARNAYN

Neno Qarana kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kujumuisha kitu kimoja na chengine, Kukifunganisha kitu kimoja na chengine, Kukiunganisha Kitu kimoja na chengine.

Neno Qarana ndio lililotoa neno Qurun ambalo humaanisha Pembe Moja. Ambapo kinembo basi neno Qurun au Pembe hua linamaanisha Uwezo wa kua na Nguvu Kubwa, Darja au Mamlaka na pia humaanisha Kizazi kimoja au wakati kipindi cha Miaka 100 yaani Karne.

Neno Qarana ndio lililotoa neno Qarina ambalo hua linamaanisha Kiumbe Mwenza au anaeambatana na kiumbe mwenzake, kama vile ambavyo kila Ibn Adam hua na Qarin wake yaani Kiumbe Jini anaeambatana nae Ibn Adam husika.

Kwani neno Qarana ndio lililotoa neno Dhu Al Qarnayn ambalo hua linamaanisha Mtu Mwenye Pembe Mbili, Mtu Mwenye kuishi ndani ya Vizazi viwili miongoni mwa watu wake au mwenye kuishi ndani ya Karne mbili katika Jamii yake na pia humaanisha Mtawala wa Tawala Mbili tofauti zilizochanganywa pamoja na kua moja. Yaani kwa mfano hapa tunaweza kuchukua mfano wa Nabii Sulayman baada ya Kumuoa Malkia Bilqis na hivyo Utawala wa Nabii Sulaiman ukaujumuisha Utawala wa Bilqis ndani yake.

Wakati tupo katika Ufafanuzi wa Tafsir ya Surat Al Kahf na mwanzoni tulipoelekezea sababu za kushushwa kwake basi tulisema kua ilikua ni kutokana na Hoja za Makafiri wa Makkah walipomkabili *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumtaka athibitishe Ukweli wa Utume wake kwa kuwaelezea kuhusiana na Watu wa Pangoni, Dhu Al Qarnayn na Habari ya Roho.

Kwani Katika kujibu hoja hizo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* baada ya kuelezea kuhusiana na As-hab Al Kahf, Vijana wenye Bustani mbili na kisha kuhusiana na Al Khidr na Nabii Musa basi anaendelea kuelezea kujibu kuhusiana na hoja ya Dhu Al Qarnayn kwa kusema:

﴿وَيَسْـَٔلُونَكَ عَن ذِى ٱلْقَرْنَيْنِ ۖ قُلْ سَأَتْلُوا۟ عَلَيْكُم مِّنْهُ ذِكْرًا﴾

Wayasaluunaka aAn Dhi Al Qarnayn Qul Saatlu aAalykum minhu Dhikran *(Surat Al Kahf 18:83)*

Tafsir: ***Wanakuulizia (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) kuhusiana na Dhi Al Karnayan Basi Waambie : 'Nitakuelezeeni mimi juu Yenu Kuhusiana nae Habari yake.'***

Naam..aya zinatuonesha namna *Alla Subhanah wa Ta'ala* anavyomhakikishia Mtume wake *Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* kwa kumwambia kua Usiwe na Khofu kwani hili mnaloliulizia juu yake basi mimi nnalo jibu lake kwa urahisi kuliko mnavyofikiria nyinyi, na hivyo katika kuanza kujibu kwake hoja basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametumia neno *Saatlu* ambalo ni lenye kutokana na neno *Tala.*

Ambapo neno *Tala* hua linamaanisha Kufuata, Kutembea Nyuma ya Kitu au Mtu, Kuiga, Kufukuzia kitu ili usiwe mbali nacho kitu hicho kutokana na kua hutaki kipotee au kukikosa yaani uanataka kua na ukaribu zaidi na kitu hicho. Neno *Tala* ndio lililotoa neno *Tilawatan* ambalo hua linamaanisha kufanya mazoezi ya kusoma, kudurusu, kusoma, kurudia kukisoma kitu.

Naam..hivyo tunapochukua neno hili na namna alilivyotumika kwenye Aya basi tunaona kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Waaambie hao Watu wa Makkah wanaotaka kujua kuhusiana na *Dhu Al Qarnayn* kua *Saatluu* yaani Nitakuelezeeni hatua kwa hatua kwa karibu zaidi kiasi ya kua nanyi mtajihisi kama kwamba mmo ndani ya ya wakati aliokua akiishi Dhu Al Qarnayn na hivyo kua chini ya nyayo zake katika wakati alipokua akitembea juu ya Ardhi.'**

Subhanah Allah..sijui tunafahamaniana ama la yaani hili ni neno Moja tu *Saatluu* la kiarabu lakini maana yake kwa Lugha kiswahili ni lenye kina kirefu sana kama tunavyoona.

Na tunapoangalia zaid aya basi tunaona pia katika aya hii *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametumia neno Dhikran. Hivyo hapa inabidi tujiulize. Hivi kwanini *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ni Mwingi wa Hikma akawa ametumia neno hili katika Kujihu hoja hii?

Yaani kwanini katika sehemu nyengine alipozungumzia Visa vya Manabii akasema kwa mfano katika Surat Yusuf 12:3 alisema kua:

﴿نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ أَحْسَنَ ٱلْقَصَصِ بِمَآ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ هَٰذَا ٱلْقُرْآنَ وَإِن كُنتَ مِن قَبْلِهِ لَمِنَ ٱلْغَافِلِينَ﴾

Nahnu naqussu AAalayka ahsana alqasasi bima awhayna ilayka hadha alqur-ana wa-in kunta min qablihi lamina alghafileena *(Surat Yusuf 12:3)*

Tafsir: ***Hakika sisi tunakuhadithia wewe bora miongoni mwa visa kupitia katika Wahyi wetu kwako kwa hii Qur'an. Na kabla ya hapo wewe hukua ni mwenye kujua chochote juu yake.***

Au katika Kisa cha As-hab Al Kahf katika aya ya 13 akasema:

﴿نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِٱلْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُواْ بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى﴾

Nahnu naqussu AAalayka nabaahum bialhaqqi innahum fityatun amanoo birabbihim wazidnahum hudan *(Surat Al Kahf 18:13)*

Tafsir: ***Hakika Sisi Tunahadithia Juu yako wewe (Muhammad Salallahu Alayhi wa Sala) Habari zao Kwa Haki na kwa Kweli Hakika wao (Vijana hao) Walikua ni Vijana Shupavu, Walioamini Juu ya Mola wao Nasi Tukawazidishia wao Uongofu.***

Au katika *Surat Ta-ha* wakati *Allah Subhanah wa Taala* anakielezea kwa mara ya kwanza kisa cha Nabii Musa na kwa aya ya mwanzo kuzungumzia kuhusiana na Nabii Musa pale aliposema:

﴿ وَهَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ مُوسَىٰٓ ﴾

Wahal Ataka Hadithu Muusa*?(Surat Ta-Ha 20:9)*

Tafsir: ***Na hivi Jee imekufikia wewe (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Hadith ya Musa?***

Naam..katika aya zote hizo *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwingi wa Hikma katika kuelezea Visa vya Manabii na Watu wema basi ametumia Maneno kama Kisa, Hadith, Habari n.k

Lakini katika Kisa cha *Dhu Al Qarnayn* ameamua kutmia neno *Dhikran!*

Hivyo ili kujua Hikma iliyomo ndani yake matumizi ya nene hili kataik kisa hiki basi inabidi tuliangalie neno maana ya neno *Dhikran.* Ambapo tunaona kua neno *Dhikran* linatokana na neno *Dhakara.*

Na neno *Dhakar*a hua linamaanisha Kukumbuka, Kuzungumzia kitu ambacho ni chenye kujaa Mafunzo na Manufaisho ndani yake na hivyo si kwamba kinastahiki kukumbukwa tu kwa kuhadithiwa bali ni chenye kuhitaji kuendelea Kukumbushiwa na Kufanyiwa kazi Kutokana na Utukufu wake.

Neno *Dhakara* pia hua linamaanisha Kupandisha Darja, Kuheshimu, Kuteua kutokana na kua na sifa za Upekee. Kuusia na pia Kuonya. Ambapo *neno Dhakara* ndio lililotoa neno Dhikr ambalo humaanisha Maarufu, Mkusanyiko wa Vitu ambacho vimechaguliwa kutokana na kua na Sifa Maalum ya Uzuri wa Upekee. Na ndio maana hata Kitabu Kitukufu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* kikawa kinaitaa pia Dhikr.

Na Ndio maana Ukiihifadhi Quran na kuifanyia kazi ipasavyo katika Maisha yako basi Utapanda Darja Tu hapa Ardhini na Mbinguni kwa sababu Qur'an ni Dhikr kwa sababu Ni Chanzo cha Kumpandisha Mtu Darja mbele ya Muumba wake na Viumbe wenzake.

Ambapo Neno *Dhakara* pia hua linamaanisha **Kitu ambacho unaposikia basi unatakiwa ukizingatie na kukiweka akilini kutokana na Manufaa yake kwako, kwani ndani yake hua mna ukumbusho na maonyo ambayo unatakiwa kuyatafakari na kuyazingatia.**

Na neno *Dhakara* ndio lililotoa neno *Madhkur* ambalo humaanisha Kitu kinachostahiki Kukumbushwa Kutokana na Umuhimu Wake. Na neno *Dhakara* ndiolililotoa neno *Dhakirin* yaani Wanaume wenye akili zao na ufahamu na wasiokua na mzaha katika kusimamia majukumu yao kwani ni wenye kujua uzito wa majukumu yao. Ambapo kwa upande wa Wanawake wenye Sifa hio basi hujulikana kama *Dhakirati*

Hivyo baada ya kuona Utangulizi wa Aya hii kitafsiri na uzito wa maneno yake kilugha ambayo ni yenye kututilia mkazo kukifuatilia kisa hiki ambacho ni chenye Ukumbusho wenye Sifa stahiki za kuzingatiwa ndani yake kutokana na mafunzo yake na maonyo yake, na tunapokiangalia kisa cha Dhu Al Qarnayn basi tunaona kua ni miongoni mwa Visa ambavyo havina Hali ya kukubaliana ndani yake kuhusiana na Asili yake yeye mwenyewe na Wazazi wake.

Kwani kuna Mitizamo tofauti ambayo yote inapingana kuhusiana na yeye alikua ni nani hasa. Na kabla ya kuendelea mbele zaid basi nilikua nataka kubainishiana kwanza kua kihistoria basi kuna baadhi ya Matukio ambayo yamezungumziwa kwenye Qur'an historia zake kulingana na mafunzo yaliyomo ndani yake. Na hivyo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuainisha baadhi ya sehemu za Visa hivyo au baadhi ya matukio kutokana na kua hayana umuhimu mkubwa sana ndani yake.

Kwa mfano *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipowazungumzia Mitume wake basi ni Wachache sana miongoni mwao ambao aliwaelezea katika Qur'an kuanzia katika kipindi cha wakati wa Utoto wao na nasaba zao. Kwa mfano Manabii waliozungumziwa kuhusiana na Utoto wao ndani ya Qur'an basi ni Nabii Ibrahim, Nabii Ismail, Nabii Ishaq, Nabii Yaqub, Nabii Yusuf, Nabii Musa, Maryam Bint Imran, Nabii Yahya na Nabii Isa.

Hivyo waliobakia wote wamezungumziwa pale walipokua Watu wazima na Mitume tayari. Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amezungumzia Kuhusiana na Utoto wa Mitume hao kutokana na Umuhimu wake katika Kutuzidishia Imani na kutufunza yenye manufaa ndani yake.

Kwani baadhi ya Historia za Mitume ya *Allah Subhanah* wa ambayo haikutajwa ndani ya Qur'an basi zimefafanuliwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa mfano Muonekano wa Sura za Mitume hao, Kauli zao, Jitihada zao n.k

Ambapo pia hata *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* hakuelezea kuhusiana na Habari za Mitume wote. Bali nae alielezea juu ya yale yenye Umuhimu wa kufunza na kunufaisha tu juu ya Maisha hao. Kwa hivyo katika kuelezea Habari za Mitume wengine ambao Hawakuelezewa kwa kina historia zao ndani ya Qur'an na ndani ya Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, basi Wanazuoni wa Ilm ya Tarikh au Historia walikua wakifanyia kazi ya ziada ya kuulizia kwa Masahaba wenzao waliokua na Ilm ya Ahl Al Kitab kwa mfano Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua ni mtu aliedumu kwenye Dini 3 kabla ya kua Muislam.

Kwani Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* alikua ni Mtoto wa Kiongozi wa Watu wanaoabudu Moto na yeye alikua ndie Muwashaji wa Moto. Lakini baadae akaona kua huo ni upotofu hivyo akakimbia Mji na njiani akakutana na Padri ambae akamuingiza kwenye Ukristo na akamsomesha Biblia na akaifaham hasa. Na kisha akasikia kua kuna Mtume ametokea katika Ardhi ya Uarabuni.

Hivyo akauhama Ukristo kwa ajili ya kumkimbilia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo njiani akakamatwa na Mayahudi na kisha akafanywa kua mtumwa wa Mayahudi wa Madina na akakisoma vizuri Tawrati hadi akaijua. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipohamia Madina basi Salman Al Farsi akajikomboa na kuingia kwenye Uislam.

Kwa maana hio basi Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* alikua anajua Dini zote na hivyo Masahaba walipokua hawajui basi walikua wakimuuliza Hivi Taurat au Injil imesemaje kuhusiana na Nabii fulani au Mtume fulani na kisha yeye huwaelezea na ingawa Huo ni mfano wa Sahaba mmoja tu, lakini walikua kadhaa.

Na hivyo pia Walivyofanya Wanazuoni wa Tarikh ambapo miongoni mwao pia walikua na Ilm ya Ahl Al Kitab walioisoma Zabur Tawrat na Injil kwa Mfano Imam Wahb Ibn Munabid, Imam Kaab Al Akhbar n.k. ambapo hali hii ya kutodhihirishwa ndani ya Qur'an na Hadith kwa mambo yasiyokua na Umuhimu sana kihistoria ndio kulikowafanya Wanazuoni wafuatilie kwenye vitabu vya Ahl Al Kitab na hivyo kutofautiana juu yake.

Hivyo anasema Mujaddid Ad Din Imam Al Ghazali Al Thani Sultan Al Mutakkalimin Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Ibn Al Husayn Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua:

'Dhu Al Qaranayn alikua ni Mfalme alieishi katika wakati wa Kupindi cha Nabii Ibrahim, na inasemekana kua alikua ni Mtawala ambae ndie alietoa Hukumu iliyomuunga Mkono Nabii Ibrahim kuhusiana na Kesi ya Kisima cha Sab kilichopp katika ardhi ya Sham. Na jina lake alikua ni Tabris na pia juna wasemao kua alikua akiitwa Hardis.'

Imam Fakhr Ad Din Al Razi anaendelea kutuambia kua: '**Na kuna wasemao kua Dhu A Qarnayn alikua ni Iskandar (Alexander)ambae aliishi katika wakati aa kipindi cha Uhai wa Nabii Isa ambae alikua ni Mtu wa karibu na Mwanafalsa Aristat.'**

Imam Fakhr Ad Din Al Razi anaendelea kutuambia kua: '**Kusema kweli mtizamo wa kua Dhu Al Qarnayn anaezungumziwa na aya hizi ni Dhu Al Qarnayn wa Mwanzo ambae aliishi katika kipindi cha Nabii Ibrahim ndio Mtizamo sahihi zaid kwani Dhul Qarnayn huyu ndie ambae Ufalme wake ulikua na nguvu kubwa sana na mamlaka makubwa kiasi ya Kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* akaamua kuuzungumzia juu yake kama vilivyosema Vitabu vya historia.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Al Asraqi basi yeye anasema kua: **Dhu Al Qarnayn aliingia katika Uislam katika Ardhi ya Ibrahim, na aliwahi kufanya *Tawwaf* kuzunguka Al Kaabah pamoja na Nabii Ibrahim na Nabii Ismail. Na hii ilikua pale baada ya kua ni mwenye kufunga Safari ya Hija kwa miguu na baada ya Nabii Ibrahim kulata habari za kukaribia kwake katika Mji wa Makkah basi akampokea na kisha akamuombea Dua Na akamfundisha Ilm ya Dini ya Kiislam na kumpa Ushauri.'**

Na Dhul Al Qarnayn alipewa Farasi kwa ajili ya kupanda alipowasili kwenye Ardhi ya Nabii Ibrahim lakini akasema: Hakika Mimi sitopanda Kipando chochote wakati nikiwa kwenye Ardhi ambayo anapatikana Khalilu Allah Ibrahim'

Ambapo baada ya kusema maneno hayo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akayashusha chini Mawingu kwa ajili yake na Ardhi ikakunjwa kwa ajili yake. Na hivyo ikawa anaenda na Jeshi lake anapotaka bila ya kupanda Farasi kwani Mawingu yanashuka na kumbeba yeye na Jeshi lake na Silaha zao zote kwa pamoja na kufika atakapo kwa kukunjaa ardhi kwa ajili yake.'

Ambapo Aliulizwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Hivi Jee Dhu Al Qarnayn alikua ni Mtume au ni Mfalme?'**

Ambapo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Hakua Mtume wala Malaika bali alikua ni mja wa Allah ambae alikua akimpenda sana *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akampenda na kumshauri na akamjaalia Mawingu na Mali kua chini yake.'**

Ama kwa upande wa Imam Abu Hajjah Mujahid Ibn Jabbar Al Makhzumi Al Makki basi yeye anasema kua: '**Kuna Watu Wanne ambao waliitawala Dunia yote, ambapo wawili wao ni**

Wanaomuamini *Allah Subhanah wa Taala* na wawili wao ni Wasiomuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Wawili wanaomuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Sulayman na *Dhu Al Qarnayn*. Na wawili wasimuamini ni Namrud na Nebuchardnezzar.'

Ambapo anasema Imam Abu Yusr Al Abidin amesema kua: **'Dhu Al Qarnayn alikua ni Muislam mwenye asili ya Uarabu wa watu wa Himyar wa Yemen na aliishi katika kipindi cha Nabii Ibrahim.'**

Na Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: **'Ama kuhusiana na jina lake basi Dhu Al Qarnayn alikua akiitwa Abu Karb Shams Ibn Abr Al Himyar.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Saib Ibn Murab basi yeye amesema: **'Dhu Al Qarnayn alikua alikiitwa Afridun Ibn Dahhaq.'**

Na Imam Al Ayni anasema kua: **'Amesema Az Zubayr Ibn Bakar kua amesema Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu kua: 'Dhu Al Qarnayn alikua akiitwa kwa jina la Musab Ibn Abd Allah Ibn Qinan Ibn Mansur Ibn Abd Allah Ibn Azd Ibn Ghauth Ibn Nabt Ibn MalikIbn Zaib Ibn Kahlan Ibn Saba Ibn Qahtan.'**

Na kwa upande wa Al Hafidh Imam Abu Hasan Ibn Umar Ibn Mahd Ad Darqutni basi yeye anasema kua: '**Dhu Al Qarnayn alikua akijulikana kwa jina la Hirmis Ibn Qitn Ibn Rumi Ibn Lanti Ibn Kashaukhin Ibn Yunan Ibn Yafith Ibn Nuh Alayhi Salam.'**

Naam, hii ni mitizamo ambayo ni yenye kuonesha Uasili na jina halisi la Dhu Al Qarnayn hususan pale tunaposhikamana na mtizamo wa kua Dhu Al Qarnayn alikua ni Mtawala Muislam alieshi katika kipindi cha Nabii Ibrahim

Wakati kwa upande mwengine basi kama alivyosema Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua kuna wale wanaomnasibisha Dhu Al Qarnayn na Alexander Ibn Philips Ibn Masrim Ibn Hirmis Ibn Maitun Ibn Rumi Ibn Lanti Ibn Yunan Ibn Yafith Ibn Yunah Ibn Sharkhun Ibn Rumah Ibn Sharfah Ibn Tufil Ibn Rumi Ibn Al As Ibn Yaqz Ibn Alis Ibn Is-haq Ibn Ibrahim Alayhi Salam. Ambae huyu hakua Muislam na alikua Mrumi ambae aliishi miaka 300 kabla ya kuzaliwa kwa Nabii Isa na miongoni mwa Mawaziri wake alikua ni Mwanfalsafa maarufu aitwae Artisatalis (Aristotle)

Na ingawa alikua ni mwenye Mamlaka ya Utawala mkubwa na wenye nguvu ambao ulianzia Ugiriki hadi Iran na kutawala takriban Mwambao wote wa Mediterranian sea. Hivyo kuna utofauti baina yao watu wawili hawa, yaani Dhu Al Qarnayn na Alexandre kwani kwanza Dhu Al Qarnayn alikua Mtawala Muislam Mcha Mungu kiasi ya kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemtaja hadi kwenye Qur'an kwa uadilifu wake

Lakini Alexander alikua ni Mtawala Kafiri wa Kirumi mwenye kupigania Mamalaka yake kutokana na Matamanio ya Nafsi yake na kuwaua na kuwateka watu wasiokua na hatia katika ardhi za sehemu mbali mbali kwa ajili ya kueneza Mamlaka yake.

Na kama tulivyoona kuhusiana na maana ya neno *Dhu Al Qarnayn* ambalo hua linamaanisha Mtu Mwenye Pembe Mbili, Mtu Mwenye kuishi ndani ya Vizazi viwili miongoni mwa watu wake au mwenye kuishi ndani ya Karne mbili katika Jamii yake na pia humaanisha Mtawala wa Tawala Mbili zilizochanganywa pamoja. Hivyo basi Wanazuoni pia wametofautiana kuhusiana na asili ya Mfalme huyu Mcha Mungu kua ni mwe ye kuitwa Dhu Al Qarnayn.

Kwani kuna wasemao kua aliitwa Dhu Al Qarnayn kwa sababu alikua ni Mtawala aliekua akitawala Sehemu mbili za Mamlaka ya Ardhi ya Nchi yake na pia kuhusiana na ardhi ya Uajemi.

Na kuna wasemao kua aliitwa Dhu Al Qarnayn kwa sababu alikua amevimba katika pande mbili za uso wake.

Na kuna wanaosema kua aliitwa Dhu Al Qarnayn kwa sababu ya kua siku moja alilala na kisha akaona ndani ya Ndoto kua ameishika Miale Miwili ya Jua ambapo hii ni ndoto yenye kumaanisha kua Atatawala pande Mbili za Dunia yaani Kuanzia Mashariki hadi Magharibi.

Na kuna wanaosema kua Dhu Al Qarnayn aliitwa hivyo kwa sababu aliwaita watu wake waingie kwenye Dini ya Uislam na hivyo watu wake hao wakampiga sana katika Upande mmoja tu wa kichwa chake hadi akawa taabani. Lakini hata hivyo akaendelea kuwausia watu ambao nao wakammalizia kumpiga upande wa pili wa kichwa chake hadi akawa taabani pia.

Na kuna wanaosema kua Dhu Al Qarnayn aliitwa hivyo kwa sababu alikua ana Nywele ndefu nzuri sana ambazo alikua akizichana na kuzipasua katikati na hivyo upande mmoja hua ni wa kulia na mwengine ni wa kushoto.

Na kuna wanaosema kua Dhu Al Qarnayn aliitwa hivyo kwa sababu alikya ni mwenye kutokana na Familia mbili tukufu kutoka upande wa Baba yake na pia kutoka upande wa Mama yake.

Na kuna wasemao kua aliitsa Dhu Al Qarnayn kwa sababu aliishi kwa mda mrefu miongoni mwa watu wake kiasi ya kua aliishi na kizazi cha kwanza ambacho kukaondoka chote na kumuacha peke yake akiwa anaendelea kuishi na kizazi cha pili cha watu wake hadi Wakafariki wote na yeye kubakia hai na akafariki baadae na hivyo akwa anajulikana kama mtu alieishi ndani ya Karne mbili na vizazi vyake viwili.

Na kuna wanaosema kua aliitwa Dhu Al Qarnayn kwa sababu alikua ni Mtaalamu mkubwa wa kupigana kwa kutumia mikono yake yote miwli kwa pamoja huku akiwa ameshikilia kipando chake.

Na kuna wanaosema kua aliitwa Dhu Al Qarnayn kwa sababu alikua ni mwenye Ilm za aina mbili Ilm ya wazi na Ilm iliyofichikana.

Na kuna wanaosema kua aliitwa Dhu Al Qarnayn kwa sababu aliishi kwenye Ujahiliyah na kwenye Ucha Mungu.

Allah Subhanah wa Ta'ala anaendelea kusema kuhusiana na Dhu Al Qarnayn kua:

﴿إِنَّا مَكَّنَّا لَهُ فِي ٱلأَرْضِ وَآتَيْنَاهُ مِن كُلِّ شَيْءٍ سَبَباً ﴾

Inna Makkana lahu Fi Aal Ardhi wa Aatanahu Min Kulli Shay-in Sababan*(Surat Al Kahf 18:84)*

Tafsir: Hakika **Tulimuwekea sisi Makazi yake kwenye Ardhi Na Kisha Tukampa Kutokana na Kila kitu Sababu**

Neno Sabbabah kwa Kilugha hua linamaanisha Sababu, Kutafuta na kupata Njia ya kufanya kitu,Tokeo linalotokea baada ya kufanyika kitu, Kutafuta Maisha au Riziki, Kua ni chanzo cha Kitu Fulani, Kutumia kitu kwa ajili ya kufanikisha Kitu chengine.

Neno Sabbaba ndio lililotoa neno Asbab ambalo humaanisha Kamba ya Kufungia Kitu, Njia inayopelekea kutokea tukio fulani, Barabara. Ambapo neno Asbab humaanisha pia Mapenzi au Uhusiano wa Mapenzi kama ule Niliokua nao mimi kwenu nyie kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Bila ya shaka aya yetu hii inatuonesha kwanza kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anathibitisha kua Yeye ndie aliemjaalia na kumuweka Juu ya Ardhi. Ambapo kutokana na kauli hii basi tunaona kua baadhi ya Wanazuoni wamechukulia maneno haya kua ndio Sababu ya kuthibitisha kua Dhu Al Qarnayn alikua ni Nabii.

Ambapo kwa upande mwengine basi kuna waliotafsiri maneno haya kumaanisha kua Dhu Al Qarnayn alijaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ni mwenye kua n uwezo wa Kutembea katika kila sehemu ya juu ya Ardhini kwa uhuru bila ya upinzani. Ambapo huo ni mtizamo wa Al Qadhi Al Imam Nasir Ad Din Al Baydawi Al Shafii.

Kwani anasema Imam Ahmad Ibn Muhammad Ath Thalabi Al Shafii kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **alimwambia Dhu Al Qarnayn kwa njia ya Wahyi kua: Ewe Dhu Al Qarnayn hakika mimi nimekutuma wewe kwa ajili ya Viumbe wote wa kuanzia Mashariki ya Dunia hadi Magharibi ya Dunia Na nimekuteua kua ni Uthibitisho dhidi yao. Nakutuma kwa Watu wote waishio Ardhiji sasa hivi ambao ni wenye kua katika Mataifa 7 na ni wenye kuzungumza Lugha tofauti**.

Ambapo miongoni mwao kuna Mataifa mawili ambayo yapo pembeni mwa Dunia, Mataifa matatu yapo katikati ya Dunia ambayo ndani yake mna Ibn Adam, Majini na Juj ya Majuj

Ama kuhusiana na Mataifa mawili yaliyo pembeni mwa Dunia basi Moja Liko katika Upande Linapozama Jua ambalo linaitwa Nasik na Taifa jengine liko upande wa pili yake linaitwa Mansik ambao ni unaichomoza Jua

Na kisha kuna Mataifa mawili yaliyobakia ambayo yanaitwa Hawil liko katika Upande wa Kulia na Tawil liko katika katika Upande wa Kushoto '

Hivyo baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kumpa ujumbe huo Dhu Al Qarnayn, basi Dhu Al Qarnayn akasema kumwambia Mola wake kua: '**Ya Allah! Ama kwa hakika umenibebesha Majukumu makubwa sana ambayo ni wewe tu ndie mwenye uwezo wa kuyabeba. lla hebu niambie kuhusiana na hayo Mataifa ambayo unanituma kwa ajili yake. Hivi Jee nitakabiliana nayo kwa kutumia njia gani?**

Kwa kutumia Jeshi Gani? Na mbinu gani zitakazoniwezesha kuwashinda? Jee itanibidi niwe na Subra na Ustahmilivu wa kiasi gani? Jee nitumie Lugha gani na Kauli gani? Jee nitafahamu mimi kuhusiana na Lugha zao na Ishara zao na Vitendo vyao? Na nitasikiaje maneno yao na kuyafahamu vipi? Nitaonaje mimi Hisia zao na kuwezaje kuwashinda kwa Hoja zangu juu yao?'

'Jee hivi kweli mimi ntaweza kukabiliana nao kwa Moyo wa Ushupavu na Uadilifu na Hikma mbele yao? Jee nna Uafilifu na Ilm kiasi gani mimi kuweza kuwathibitishia wao juu yako bila ya kuwatia shaka na kutofanya ubaguzi baina yao?'

‘Ya Allah! Hivi Jee nitawezaje mimikuthibitisha Ukweli wa maneno yao watakapoamini juu yako? Jee nna uwezo gani mimi wa Ukarimu na Huruma utakaoniwezesha kuwaunganisha pamoja kwa ajili yako?’

Ewe Mola wangu! Hakika mimi sioni hata kimoja kati ya hivi nilivyovitaja ambavyo ni miongoni mwa vinavyostahiki kua navyo kwa yule mwenye kutakiwa kubeba jukumu hili. Hakika mimi sina hata kimoja kinawafanya wao kua dhaifu mbele yangu na mimi kua ni mwenye nguvu na uwezo dhidi yao mbele yao

Kwani ni wewe tu ndie mwenye uwezo juu ya kila kitu mwingi wa Rehma, Huruma na ukarimu mkubwa sana. Kwani wewe ndie ambae mwenye uwezo wa kutoibebesha Nafsi zaid ya kile inachostahiki kubebeshwa. Hakika wewe huikalifishi Nafsi na ni mwingi wa Rehma na Huruma.’

Na baada ya Dhu Al Qarnayn kutoa Hoja zake baada ya kuona uzito wa Jukumu lake analotaka kukabidhiwa na Mola wake na kudhihirisha Udhaifu wake na unyenyekevu wake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamjibu Dhu Al Qarnayn kwa kumwambia: ‘**Ewe Dhu Al Qarnayn Usiwe na Khofu wala Wasiwasi. Kwani kwa hakika mimi nitakupa wewe uwezo wa kubeba kile nitakacho kubebesha.’**

‘Kwani nitakutanulia Kifua chako na Ufaham wako na kiongeza uwezo wa Kusikia kwako na hivyo Utakua ni mwenye kufahamu na kusikia wazi kila kitu utakachokisikia. Nitautanua Ufahamu wako kiasi ya kua Utafahamu kila kitu. Nitautanua Ulimi wako na Utaweza kuzungumza kila lugha. Nitakutanulia na kukufunulia Mtizamo wa Moyo wako na Macho yako na hivyo utakua ni mwenye kuona kila kitu. Nitakuongezea Riziki yako kiasi ya kua hutokua ni mwenye kupungukiwa na kitu chochote ukihitajiacho. Nitakuongezea Nguvu juu yako na juu ya Wasaidizi wako kiasi ya kua Hutokua na khofu juu ya kitu chochote. Nitakuunga mkono kiasi ya kua hakuna atakaekuzidi Nguvu’

‘Nitaupa Nguvu Moyo wako kiasi ya kua Hutoshtuka wala kutishika na chochote. Nitaifanya Mikono yako jua ni yenye nguvu kiasi ya kua utakua na uwezo wa kuvamia kitu chochote. Na kuzipa nguvu nyayo zako kiasi ya kua hutorudi nyuma dhidi ya kitu chochote. Nitaukijaalia Kiza na Mwangaza kua chini yako kiasi ya kua Vitu hivyo vitakua ni Miongoni mwa Silaha zako. Na hivyo Mwangaza utakuongoza Mbele huku Kiza kikiaa ni chenye kukuficha na kukulina kwa nyuma yako.’

Na baada ya kuahidiwa hayo na Mola wake basi Dhu Al Qarnayn akasema: **‘Ewe Mola wangu, hakika Utiifu wangu juu ya ubebaji wa Jukumu hili juu yangu ni Wajibu kwangu.**’

Na mitizamo ya Wanazuoni katika kufafanua kuhusiana na Ucha Mungu wake na Unyenyekevu wake ambao ndio uliompelekea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kumteua na kumpa Majukumu aliyompa na kisha kuahidi kumpa Sababu au Njia za Kumpa Urahisi wa kutekeleza Majukumu yake hayo mazito kwa kama alivyosema kua: *Wataynahu min kulli Shay-in* Sababan - Na Tukampa kutokana na Kila kitu Sababu.

Ambapo ili tufahamiane vizuri kuhusiana na maneno haya basi na tuchukulie wa Mtu Mzima Mwanamme ambae anataka Kuendeleza Kizazi chake. Ambapo kimaumbile basi kwake yeye hua kamwe haiwezekani kwake peke yake kua ni mwenye kuendeleza kizazi bila ya kushirikiana na Mwanamke.

Na kama ilivyokua kwa Mtu Mzima Mwanammke kua nae hawezi kuendeleza Kizazi bila ya kushirikiana na Mwanamme.

Hivyo ili kwa kila mmoja kati ya Watu wawili hawa awe ni mwenye Kufanikisha malengo ya kuendeleza Kizazi basi ni lazima kua na njia ya kukutana na kuingiliana Kimwili kwanza kisha ndio kitapatikana Kizazi kwa Majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Hivyo kukutana kwao na kuingiliana hua moja kati sababu ya kuendeleza kizazi. Ambapo watu wawili hawa kamwe hawatoweza kukutana kimwili bila ya kuwepo sababu ya Kuonja raha inayopatikana ndani yake tendo hilo. Raha ambayo Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali anasema kua ni sawa na kuonja Raha ya Peponi Duniani.

Kwa maana hio basi Raha inayopatikana katika Muingiliano wa Kimwili baina ya Mwanamme na Mwanamke imejaaliwa kua ndio Sababu ya Sisi Ibn Adam kwanza kujua ladha ya Raha na Starehe ya Milele ya Peponi, na kisha Raha hio ndio Sababu inayotupelekea Sisi kutaka kupata kizazi.

Kwa sababu kama ingekua hakuna Raha na Utulivu ndani yake tendo hilo basi Mwanamme asingemhitaji Mwanamke na wala Mwanammke asingemhitaji Mwanamme na hivyo ingekua hakuna kuongezeka kwa watu Duniani.

Na kwa mtizamo huu basi hua tumezungumzia sababu au Asbab za kuendeleza Kizazi kwa Ibn Adam kwa ujumla. Ambapo kwa Upande wa Malengo ya Sharia za Muumba yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambazo ndio sharia za Mfumo wa Dini ya Kiislam yaani Mfumo wa Imani na njia ya Maisha ya kujisalimisha chini yake *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Basi tunaona kua njia muhimu kuliko zote na inayokubalika katika kuendeleza Kizazi basi ni Kupitia katika mfumo wa njia aliyoiweka mwenyewe *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ndio njia inayojulikana na kukubalika kihalali ambayo ni ya kuoana Kiislam.

Kwa maana hio basi Ndoa ndio sababu pekee inayokubalika na mbele ya Muumba kutumika kwa ajili ya Kuendeleza kizazi. Kwa sababu Malengo ya sharia ya ndoa hua ni kuendeleza kizazi na kusimamia haki ya Kizazi kutoka kwa Wazee na haki ya Wazee kwa Kizazi. Hivyo tukirudi kwenye mfano wa Mtu anaetaka kuendeleza kizazi kulingana na Sharia za Kiislam basi Mtu huyo hawezi kuendeleza Kizazi bila kua na sababu za kuendeleza kizazi ambazo ni Kufikia Umri wa Kuoa, Kuoa, Kuingiliana na Mke wake kisha ndio apatikane mtoto atakaehesabika kua ni mrithi na muendelezaji wa kizazi chake.

Hivyo aya zinatudhihirishia kua Dhu Al Qarnayn alijaaliwa Kila kitu na kila Njia na Kila Sababu zitakazopelekea kufanikisha Malengo Ya Jukumu aliyopewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kiurahisi kutokana na Ucha Mungu wake na Uadilifu wake.

Yaani kama tulivyoangalia mfano wetu wa Mtu anaetaka kuendeleza Kizazi chema baada yakufikia Umri wa Kuoa, na hivyo akajaaliwa kupata Mke Mcha Mungu na kisha akapewa na uwezo wa kupata Watoto ambao akawasimamia kwa Kuwatafutia Ilm ya Dini ya Kiislam na kuwasomesha hadi wakaifaham Dini yao na hivyo watoto hao wakaishi kulingana na Maamrisho ya Mola wao.

Na kama zilivyoonesha ahadi za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Dhu Al Qarnayn basi Dhu Al Qarnayn alijaaliwa Ilm, Mbinu, Uwezo, Jeshi, Zana za Kivita, n.k

Na hivyo kwanza Dhu Al Qarnayn akaanza kusimamisha Msingi wa Ngome yake kwa kuwaamrisha watu wake kujenga Msikiti kwanza. Msikiti ambao ulikua mkubwa sana na kisha akaaamrisha kuzungushiwa kwa Ukuta nje ya Msikiti huo, na hivyokua ni Msikiti ndani ya eneo la Makazi yake. Na kisha baada ya kumalizika Ujenzi huo akaamrisha kua kila mmoja alipwe mfuko wa Dhahabu kulingana na Jitihada yake katika Ujenzi huo. Na matokeo yake basi Masikini ambao ndio wengi waliosaidia ujenzi huo kua ni wenye kutajirika baada ya kumalizika ujenzi huo kutokana na jitihada zao katika ujenzi huo.

Na kisha baada ya hapo Dhu Al Qarnayn akaanda Jeshi kutokana na Watakaojitolea miongoni mwa wajenzi hao na hivyo kujikuta kua ana Wapiganaji 40000 ambao akawagawa katika makundi manne. Na kisha akakusanya Jeshi lake halisi ambalo lilikua na Wapigaji tofauti wafikao laki sita. Ambapo akaligawa Jeshi katika sehemu nne pia na kisha akalichanganya Jeshi hilo na Jeshi la Wapiganaji wa kujitolea.

Kwani baada ya Dhu Al Qarnayn kusimamisha mazingira mazuri katika ardhi yake na kisha kuandaa Jeshi lake kwa ajili kutekeleza wajibu wake kwa watu waliokua mbali zaid yake kwa ajili ya kuwafikishia ujumbe wa Mola wake. Na hivyo ikawa tayari ameshapata Sababu au Njia ya kuanza Safari zake kama alivyoamrishwa na Mola wake kuelekea kwenye maeneo ya Magharibi kwenye upande unaozama Jua. Na akafunga Safari na Jeshi lake hilo kuelekea Upande huo.

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaelezea hali ilivyokua baada ya hapo kwa kusema;

﴿ فَأَتْبَعَ سَبَباً ﴾

FaatbaAaa Sababnan*(Surat Al Kahf 18:85)*

Tafsir: **Hivyo (Dhu Al Qarnayn) akafuata Sababan**

Ambapo anasema Imam Abu Al Qushayr Al Nishapuri Al Shafii kua kuhusiana na Maneno haya kua: **‘Dhu Al Qarnayn alifunguliwa njia iliuokua Wazi kabisa juu ya Ardhi, kiasi ya kua alikua kila akipiga hatua basi mambo yalikua yanafunguka wenyewe. Na hivyo ilikua rahisi kwake kufikia malengo yake anayoyaelekea, kwani hata mipindo ya ghafla ya njia anazofuata na kupita basi kwake yeye ilikua kama ndie mwenye umiliki juu yake.’**

‘Kwani mmoja kati ya Mawalii wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapoingia ndani ya eneo la usaidizi wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* Basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* humkabidhi Mja huyo Umiliki wa eneo hilo na hivyo hua chini yake na hivyo hua ni mwenye kufanya anavyotaka.Na huweza kupata anachotaka, na kua na uwezo wa kila anachotaka kama vyakula anavyotaka, kusafiri masafa anayotaka bila kuchoka, kuwamurikia watu kwa nuru yake na hivyo wamfuatao kuweza kuona.Kuwafanikishia mahitajio yao na malengo yao wanaomfuata, kukubaliwa dua zake anapokua anamuomba Mola wake.’

Kutatua matatizo na kuwaondolea watu mitihani yao n.k Kwani hua ni wenye kuchaguliwa na Mola wao na hivyo hua ni wenye kua na uwezo wa kufanya mengi sana kwa ajili ya watu wao kaa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kuwatekelezea watu wengine mambo yao kupitia kwa Mawalii wake hao.’

Ambapo anasema Imam Ahmad ibn Muhammad Ibn Ajibah kua: **‘Mbali ya kua Waja hao hua ni wenye kupewa Mamlaka juu ya kila kitu katika kufuata njia husika. Kiasi ya kua hua ni wenye kumuona *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia katika Majina yake na Sifa zake katika kila tukio linalotokea katika kila wakati na kila sehemu. Lakini hata hivyohua kuna kikomo au mipaka ya mamlaka yao hayo**

Kwa mfano kama wakiomba kua waingizwe ndani ya Pazia la Nuru *yaAllah Subhanah wa Ta'ala* basi haitowezekana kwao. Au wakiomba kumuona *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi haitowezekana pia. Kwani wao hua katika hali kamilifu ya Mamlaka ya Darja ya Wasafiri ambao wanatakiwa kua ni wenye kufikia kwenye sehemu fulani tu na hua wameshafikishwa.’

Hivyo Dhu Al Qarnayn akawa ni mwenye sifa ya kua na hali ya kufuata Njia zinazofunguka mbele yake kulingana na Majaaliwa ya Mola wake katika kuyakumbilia Malengo aliyowekewa kama zinavyosema aya:

﴿حَتَّىٰٓ إِذَا بَلَغَ مَغۡرِبَ ٱلشَّمۡسِ وَجَدَهَا تَغۡرُبُ فِي عَيۡنٖ حَمِئَةٖ وَوَجَدَ عِندَهَا قَوۡمٗاۗ قُلۡنَا يَٰذَا ٱلۡقَرۡنَيۡنِ إِمَّآ أَن تُعَذِّبَ وَإِمَّآ أَن تَتَّخِذَ فِيهِمۡ حُسۡنٗا﴾

FaatbaAaa Sababnan Hatta itha balagha maghriba alshshamsi wajadaha taghrubu fee AAaynin hami-atin wawajada AAindaha qawman qulna ya tha alqarnayni imma an tuAAaththiba wa-imma an tattakhitha feehim husnan*(Surat Al Kahf 18:85-86)*

*Tafsir: **Na Kisha Akafuata Njia Hadi Pale alipofikia linapotua Jua Akalikuta Linatua Katika Chemchem ya Maji Ya Topetope Nyeusi Na Akakuta Karibu yake Jamii ya Watu Nasi tukasema(kwa Kumshushia Wahy) Ewe Dhu Al Qarnayn Aidha Uwaadhibu watu hao Na Ima Wachukulie Kutokana nao Kwa kuwafanyia Wema.***

Hapa tunona kua aya zinaizungumzia Safari ya Dhu Al Qarnayn kwa kutuonesha Tawsira halisi ya hali ilivyokua.

Kwani alienda hadi akafika kwenye Maghriba Shamsi ambapo neno Maghriba Linatokana na neno Gharaba ambalo ni lenye kumanisha Kutoweka, Kuzama kwa kitu ndani ya Kitu na kutooekana tena kwa kitu hicho katika sehemu hio.

Na pia humaanisha Kutua kwa Jua. Hivyo upande wa Magaharibi umeitwa Magharibi kwa sababu ndio Upande unaozama Jua katika kutua kwake ndani ya Mzunguko wake wa Kila siku kulingana na makadirio ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Neno Gharaba ndio pia lililotoa neno *Ghurab* ambalo hua linamaanisha aina ya Ndege mweusi anaejulikana ka.a Kunguru.

Na hii ni kwa sababu *Ghurab* au Kunguru ni ndege mwenye sifa ya upekee wa kua na Rangi ya *Gharabib* ambayo hua ni Rangi Nyeusi tititi ya kitu.

Kwani aya pia katika kuainisha Taswira ya safari husika basi Zinaelezea mazingira ya maeneo hayo yanayozama Jua katika Upande wa Magharibi kua na hali ya *Aaaynin Hamiatun* .

Ambapo neno **A'aynin** hua linamaanisha Chem chem ya Maji yanayobubujika na bila ya shaka neno A'aynin ambalo limetokana na neno A'ana ambalo nfio lililotoa neno Aa'inun yaani Jicho.

Na Jicho Limeitwa *Aainun* kwa sababu Jicho hua ni lenye kudhihirisha hisia za Uchungu kwa kububujikwa na Machozi.

Na pia tunaona kua aya zinaizungumzia Safari ya Dhu Al Qarnayn kwa kutuonesha Taswira halisi ya hali ilivyokua.

Kwani alienda hadi akafika kwenye Maghriba Shamsi ambapo neno Maghriba na neno Gharaba ambalo ni lenye kumanisha Kutoweka, Kuzama kwa kitu ndani ya Kitu na kutooekana tena kwa kitu hicho katika sehemu hio.

Na pia humaanisha Kutua kwa Jua. Hivyo upande wa Magaharibi umeitwa Magharibi kwa sababu ndio Upande unaozama Jua katika kutua kwake ndani ya Mzunguko wake wa Kila siku kulingana na makadirio ya Allah Subhanah wa Ta'ala.

Neno Gharaba ndio pia lililotoa neno Ghurab ambalo hua linamaanisha aina ya Ndege mweusi anaejulikana ka.a Kunguru. Na hii ni kwa sababu Ghurab au Kunguru ni ndege mwenye sifa ya upekee wa kua na Rangi ya Gharabib ambayo hua ni Rangi Nyeusi tititi ya kitu.

Kwani aya pia katika kuainisha Taswira ya safari husika basi zinaendelea kuelezea mazingira ya maeneo hayo yanayozama Jua katika Upande wa Magharibi kua na hali ya A’aainin Hamiatun.

Ambapo neno A'aynin hua linamaanisha Chem chem ya Maji yanayobubujika na bila ya shaka neno A'aynin ambalo limetokana na neno A'ana ambalo ndio lililotoa neno Aa'inun yaani Jicho.

Na Jicho Limeitwa Aainun kwa sababu Jicho hua ni lenye kudhihirisha hisia za Uchungu kwa kububujikwa na Machozi.

Na neno jengine lililotumika kwenye aya yetu hii ni neno Hamiatun ambalo ni lenye kutokana na neno Hama ambalo hua linamaanisha Kufua Kisima, Kukomba Tope kutoka ndani ya Kisima, Kusafisha Maji ya Kisima au sehemu yeye maji yaliyojaa Tope.

Neno Hama pia humaanisha Mchanganyiko wa Tope Nyeusi na Maji, ambapo anasema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu anhu kua: **‘Neno Hamiah hua pia linamaanisha Maji yenye Uvuguvugu.’** Ambapo huo pia ndio mtizamo wa Imam Hasan Al Basr.

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Jarir At Tabari basi yeye anasema kua:**Maana inayokubalika zaid ya neno Hamiah hua ni Bwawa la Tope. Lakini hata hivyo hapa hua inawezekana ikamaanisha maana zote mbili pia**

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Al Din Al Razi basi yeye anasema kua: ‘**Hamiah inayozungumziwa hapa hua ni ile hali ya Hadaa ya Macho pale unapoangalia na kuona namna Jua linavyozama ndani ya Maji Baharini. Na hii ni kutokana na kua Dunia ina maumbile ya Duara**.’

Naam..ambapo mtizamo huu wa Imam Fakhr Ad Din Al Razi ni Mfano unaotuonesha namna Wanazuoni wa Kiislam walivyokua wako mbele katika Fani za Ilm Mbali mbali ambapo Imam Fakhr Ad Din Al Razi alizaliwa mnamo mwaka 1150 CE yaani miaka 1000 iliyopita.

Ambapo wengi wetu leo hii wamesomeshwa kua alievumbua kua Dunia ni Duara ni Christopher Columbus katika safari yake ya Kuigundua America wakati Imam Fakhr Ad Din Al Razi aliefariki mnamo mwaka 604 Al Hijra alikua atayarai ameshayasema hayo na huku akiwa ni mwenye kudhihirisha na kuamini kua Dunia ni Duara.

Ama kwa upande mwengine basi tunaona kua Wanasema Wanazuoni kua: '**Neno hili likisomwa kama Hamiah basi hua linamaanisha kua ni Dimbwi au Bwawa la Tope. Lakini kama likisomwa kama Hamiya likiwa na herufi Alif bila ya kua na herufi Hamza basi hua linamaanisha Muonekano wenye Marinda marinda na mistari.'**

Ambapo anasema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu anhu* kua**; 'Ubayy Ibn Kab alinifundisha mimi kisomo cha neno hili kama alivyofundishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni Hamia hivyo kama likisomwa kama Hamiya likiwa na herufi Alif bila ya kua na herufi Hamza basi hua linamaanisha Muonekano wenye Marinda marinda na mistari.**

Ambapo anasema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu kua; Ubayy Ibn Kab alinifundisha mimi kisomo cha neno hili kama alivyofundishwa na Rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni Hamia.

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: 'Baada ya mimi kusema hivyo basi Muawwiyah akamuuliza Abd Allah Ibn Umar kwa kusema; Abd Allah Ibn Umar hivi jee wewe unakua uanisomaje aya hii?

Ambapo Abd Allah Ibn Umar akasema, hakika mimi naisoma kama ulivyoisoma wewe ewe Amir Al Muumini

Hivyo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* Akaanza kubishana na Muawwiyah na Abd Allah Ibn Umar Radhi *Allahu Anuhm*. Hadi kufikia Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* amwite Kab *Radhi Allahu Anhu* na alipofika mbele yao basi akamauuliza: **'Ewe Ka'b Hivi Jee Taurati imesema nini kuhusiana na Sehemu inayozama Jua?'**

Na Ka'b akasema: **Ama kuhusiana Lugha ya Kiarahu basi nyinyi ndio wenye kujua zaidi kwa sababu nyinyi mmesoma zaidi Kiarabu Lakini kuhusiana na kuzama kwa Jua basi Tawrat imesema kua Jua linazama kwenye Maji na tope, na nitakuelzeeni mimi kuhusiana na Jambo ambalo litakufanyeni mtafakkari zaidi**

Na katika tukio hili basi ndio tunaona kuhusiana na namna Masahaba walivyokua wakijitahjdi kufuatilia yale ambayohayakutajwa ndani ya Qur'an Na pia yakawa hayakutajwa wala kufafanuliwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m kutokana na kutokua na umuhimu mkubwa sana.

Na hivyo wao ilikua kama tulivyosema kua walikua wakiwauliza wale Waislam wenye Ilm ya *Ahl Al Kitab* kama hapa Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* alipomuuliza Kab *Radhi Allahu Anhu* hivyo katika kutaka kuwafanya watafakkat basi Kab *Radhi Allahu Anhu* akasoma Ushairi Ufuatao:

Dhu Al Qarnayn alikua Muislam Kabla yangu

Mfalme ambae Wafalme walipiga magoti mbele yake

Alifika katika sehemu za Ardhi zaKuchomoza Jua na Kuzama Jua

Akiwa ni Mwenye kutafuta Sababan kutoka kwa Mwingi wa Hikma

Na kisha akaona namna Jua linavyozama katika sehemu linapozama kwake

Katika Chemchem ya Khulub na Dhat Harmad

Hivyo Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu akauliza*: **'Ya Ka'b Hivi Khulub ndio nini?'**

Kab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Ni tope kulingana na Lugha ya Tawrat'**

Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* akauliza:**'Na Dhat Harmad ndio nini?'**

Kab *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Ni Tope Nyepesi zenye rangi nyeusi zinazonyorora'**

Hivyo Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* akamwita mwandishi wake na kumwambia kua aandike kile alichokisema Kab *Radhi Allahu Anhu.*

Ama tunapozungumzia kuhusiana na sehemu ya Magharibi inayozama Jua basi mimi na wewe hatuwezi kujua na hakuna anaeweza kujua ni sehemu gani isipokua ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee ndie anaejua kuhusiana na sehemu hio.

Hio ni kwa upande mmoja, ila kwa upande mwengine basi tunarudi kwa Wanazuoni wa Historia na Tafsiri ambao wao walijitahidi kufafanua ili wale wasiojua basi wasiwe na masuali mengi ya kujiuliza. Hivyo wengi miongoni mwa Wanazuoni wametafsiri sehemu hii ya Ardhi aliyoifikia Dhu Al Qarnayn kua ni sehemu ya Ardhi ambayo leo hii inajulikana kama ardhi ya nchi ya Morroco.

Kwani eneo la Ardhi ya Morroco kwa lugha ya Kiarabu hua linajulikana kwa Lugha ya Kiarabu pia kama Al Maghrib. Hivyo basi mimi nawe hatuwezi kutoa hukumu dhidi ya Wanazuoni kuhusiana na Mtizamo huu na hii ni kwa sababu katika kipindi waliichokua wakiishi wao basi Ardhi ilikua mwisho wake ni Morroco mbele kuna Bahari tupu.

Naam..ili tufahamiane zaidi basi tuchukulie ule mfano wa Hadith inayonukuliwa sana ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: '***Utlubul Ilma wa law fis Siin*** **yaani Tafuta Ilm hata kama ikiwa kwa kuenda kwa umbali wa China.'**

Ambapo hii ni Hadith Hasan Mashhur sana inayohimiza kuhusiana na Umuhimu wa Kutafuta kua hata kama ni China basi unatakiwa uifuate Ilm Na nataka tufahamiane kua nimesema kua hii ni Hadith Hasan Mashhur na sikusema kua ni Hadith Sahih.

Ambapo tunapozungumzia Hadith Mashhur basi hua ni Hadith ambayo inaweza ikawa Sahih, inaweza ikawa Hasan (Nzuri) na inaweza kua Dhaif.

Kwani Hadith Mashhur inaweza kua ni Hadith ambayo ingawa ni Mashuhuri lakini hua imenukuliwa na Sahaba mmoja tu ambapo hata hivyo waliomnukuu Sahaba huyo hua hawaaminiki kulingana na Vigezo vya Ilm ya Hadith..na hivyo kuifanya hadith hio ni Dhaif.

Sasa tunapoiangalia Hadith hii ambayo ni Mashhuri na inanukuliwa sana basi tunaona kua Wanaoinukuu wanasema kua Amesema Anas Ibn Malik, Abd Allah Ibn Abbas, Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Masud, Jabir Ibn Abd Allah,Abu Said Al Khudhr *Radhi Allahu Anhum.*

Lakini sasa Wanazuoni wengi sana wa Hadith wanasema kua hii ni Hadith dhaifu kwa sababu ya kua wale walioinukuu kutoka kwa Masahaba hao wana kasoro za kutoaminika.

Na tunapozungumzia kutoaminika kwenye Ilm ya Hadith basi hua mnaangaliwa mamb mengi sana ndani yake hadi mtu husika awe ni mwenye kukubalika na kuaminika,kwani kama Mtu akiwa anasahau (matn) maneno ya Hadith au amenukuu kwa nani, au amebadilisha maneno la mbele kaweka nyuma na la nyuma kaweka mbele, au mtu huyo akiwa hana Taqwa, anasema uongo, au hakuwahi kukutana na mtu anaemnukuu n.k basi mtu huyo hua hana vigezo stahiki kua hadith zake ni sahih.

Hivyo tunaporudi hadith kwenye yetu hii basi tunaona kua ingawa Wanazuoni wengi wanasema kua ni dhaifu lakini kuna Wanazuoni wasemao kua ni hasan Hadith kwa mfano kama Shaykh Al Islami Imam Jamal Ad Din Abu Al Hajjaj Yusuf Ibn Zakki Abd Rahman Ibn Yusuf Ibn Abd Al Malik Ibn Yusuf Al Kalbi Al Quda Al Mizzi ambae ni miongoni mwa Wanazuoni wanaoongoza katika fai ya ilm Rijal yaani Ilm ya walionukuu hadith na pia mtizam huo ni wa Al Hafidh Imam Shams Ad Din Ibn Muhammad Abd Rahman Al Sakhawi ambae nae ni miongoni mwa Wanazuoni walio juu katika fani ya Ilm ya Hadith na Tarikh.

Na baada ya kuiangalia hadith hio basi tunarudi kwenye sababan ya kwanini mimi nikatumia mfano wa Hadith hii. Na hii ni kwa sababu mbali ya Kua ni Hadith isiyokua na Nguvu lakini inakubalika katika kutiana ari katika Kuamrishana mema kwa sababu haina hukmu ndani yake bali ina wasia muhimu ndani yake yaani inakua ni kama Wasia wenye maneno ya Busara.

Na Sababu ya pili ambayo ni Muhimu zaid ya mimi kuitumia basi ni kua; Katika kipindi cha kabla na baada ya kuja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Waarabu walipokua wakitaja eneo la ardhi ya Siin (China) basi hawakua wakimaaanisha China, bali walikua wakimaanisha eneo la Ardhi la Kuanzia India kuelekea Mashariki yaani Bangladesh, Myanmar, Vietnam,Malaysia, n.k hadi China

Hivyo basi ilikua hata kama ikiwa mtu ameenda India basi ilikua akiulizwa alikua wapi basi ilikua ni kawaida kusema kua alikua China.

Kama vile ilivyokua kwao wao eneo la Sham ambalo kwetu sisi leo ni eneo la Syria, Jordan, Palestina na Lebanon.

Kwa maana hio basi kwao wao eneo China ndio ilikua sehem ya Ardhi iliyopo Mashariki na kupakana na Bahari ya Mashariki na Morocco ndio sehemu ya mwisho ya Ardhi katika upande wa Magharibi iliyopakana na bahari ya Magharibi.

Tunaendelea na Aya yetu inayozungumzia kuhusiana na hatua ya mwanzo aliyoichujua Dhu Al Qarnayn katika kufuata kwake Sababan kwa ajili ya kutekeleza maamrisho ya Mola wake ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na hivyo kua ni mwenye kuelekea katika maeneo ya Maghribi linapozama Jua na tunajaribu kufahamishana kwa kutumia ufahamu wetu mdogo sana kutokana na maumbile yetu Ibn Adam. Na bila ya shaka hakuna atakaeweza kujua miongoni mwetu kuhusiana na Uhalisi wa sehemu husika inayozama Jua aliyoifikia Dhu Al Qarnayn.

Ingawa kuna baadhi wanajaribu kuelezea hapa na pale kwa mitizamo Tofauti kulingana na Vithibitisho vya hoja za kiufaham ambapo hata hivyo hakuna mwenye ushahidi unaokubalika na wengine ndani ya hoja zake.

Hivyo basi Jambo la Muhimu kuliko yote ni kurudi kwenye Aya yetu huku tukuwa ni wenye kukubaliana kua Hakuna Mguu wa Ibn Adam ambao unaweza kufika katika sehemu inayozama Jua hasa.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa hikma zake basi ametuelezea hivyo kwa sababu ya Kutaka kutuonesha namna alivyokua na Utiifu Dhu Al Qarnayn katika kutekeleza Majukumu yake mbele ya Mola wake Na Hivyo alijitolea na kufunga Safari hio ndefu sana isiyokua na Mfano wake hususan tunapozungumzia kuhusiana na Usafiri wa zama hizo

Na hivyo basi haishangazi kuona kua Wanazuoni wakasema kua Alijaaliwa kuyatumia na kuyaamrisha Mawingu na kumsafirisha na Jeshi lake Hivyo Vyovyote vile itakavyokua basi Dhu Al Qarnayn aliendana kuenda katika upande wa Magharibi wa Dunia hadi akajikuta kua yuko katika sehemu ambayo alipoliangalia Ju abasi akalioona kua kama kwamba linazama kwenye Shimo lenye Tope nyeusi.

Na alipowasili Dhu Al Qarnayn katika sehemu alilolina tukio hilo la Jua Kuzama, basi mara kwa upande wa pembeni yake akaona kua Kuna Ukuta Mkubwa sana ambao ndani yake Mna Majumba Makubwa pia yaliyojengwa kwa Mawe vyuma na Shaba.

Hivyo akaachana na Kulishangaa Juu linavyozama kwenye tope na akaanza kuuangalia Mji huo kwa Mtizamo wa Makini wa Mtu mwenye kufanya uchunguziwa kituili asikose kuona hata sehemu ndogo ya kile anachokiangalia Dhu Al Qarnayn akasimama Na Jeshi Lake na kutabasamu kwani alikua anajua kua Amekutana nacho kile anachokitafuta kulingana na maamrisho ya Mola wake.

Na yuko tayari Kutimiza Malengo yake. Lakini sasa kila akiaangalia Ukuta wa Mji huo basi hakua akiona Mlango wa Kuingilia ndani ya Mji huo wala hakuna njia ya kuingia ndani yake wala ya kutokea ndani mwake wala njia inayozunguka Ukuta wa Mji huo.

Hivyo Watu wake Dhu Al Qarnayn wakausogelea Ukuta huona kujaribu kutafuta njia ya Kuingia ndani yake, lakini hawakuweza kuiona nia yeyote, nawakaamua Warushe Kamba iliyofungwa nanga ambayo itanasa katika sehemu ya Ndani ya Ukuta.

Na waliporusha mara ya kwanza na mara ya pili basi nanga ikanasa.

Akachaguliwa mmoja wapo miongoni mwao na kuambiwa kua akifika Juu basi aseme ni nini anachokiona ndani yake. Na mtu alipopanda na kufika Juu, basi hakusema Chochote bali alijitupa mwenyewe ndani yake.

Watu wa Dhu Al Qarnayn wakashangaa sana na hivyo wakamchagua wa pili na kumwambia kama walivyomwambia wa kwanza lakini nae pia alipopanda na kuangalia ndani basi hakusema bali alichupa ndani yake pia, na walipochagua mtu wa tatu na hali ikawa hivyo hivyo. Hapa sasa Dhu Al Qarnayn akawaamrisha watu watafute sehemu nyengine ya kuingilia ndani yake.

Na katika kutafuta kwao basi Upande wa pili wakaona kuna Bahari na Ukuta wa Mji huo umeingia hadi Ndani ya Bahari hio isipokua kwa mbaali akaona kuna mwambao na sehemu na Majahazi yakiwa yamevutwa juu ufukweni yote.

Akajua kua Watu wa mji huo washapata habari juu yake. Hivyo ikambidi atafute njia ya Kufika kwenye mwambao huo Hivyo wakapiga kambi na kusuburi asubuhi yake, lakini Usiku walipowasha Moto basi yakatokea Maajabu ya cheche za Moto huo kufika Kuruka na kuingia ndani ya Ukuta wa Mji huo.

Na hivyo Moto Mkubwa ukaanza kuwaka ndani yake. Kwani Moto huo uliunguza kila kitu hadi watu hao wenyewe wakaomba Msaada kwa Dhu Al Qarnayn. Dhu Al Qarnayn akapata sababu na njia ya Kuingia ndani ya Mji huo na Moto ukazimika.

Dhu Al Qarnayn alipoingia ndani yake akakuta Kuna Baadhi ya watu ambao ni Wafu lakini hata hivyo Maiti zao hazinuki. Hivyo akashangaa sana na kuwauliza watu wa Mji huo imekuaje ikawa hivyo? Watu hao wakajibu : '**Sisi tunakula Busara zetu.'**

Dhu Al Qarnayn akakaa kimya na kuandaliwa chakula na Wakuu wa Mji huo. Na katika kukaa basi zikawekwa Sahani za Dhahabu mbele yao ambazo zimefunikwa kwa mifuniko ya Dhahabu.

Na kisha kila mmoja akaanza kutoa maneno ya hekima miongoni mwao. Na ilipofika zamu ya Dhu Al Qarnayn basi akaambiwa aseme ambapo nae akawauliza: **'Kwanini mmeweka Sahani Halafu Hamli'**

Ambapo watu hao wakajibu: '**Sisi tumeshakula Maneno yetu ya Hikma tuliyosema'**

Na hapo Sahani zikafunuliwa na badala ya kujaa chakula basi zilikua zimejaa Almasi, Lulu, Dhahabu n.k. badala ya chakula ndani yake. Dhu Al Qarnayn akashangaa kwani hakutegemea kua Sahani zitabeba Hazina kiasi hicho badala ya chakula.

Na akashangaa zaidi baada ya kua ni mwenye kuamrishwa yeye kuzitia mdomoni kwa ajili ya kuzila hazina zilizomo sahanini mbele yake na mbele ya wenzake. Hivyo akasema: **'Nitakulaje wakati Hiki sio Chakula?'**

Watu hao wakajibu: **'Kwa maana hio unasema kua hizi hazina maana sio? Hebu tuambie unataka nini hasa wewe kutoka kwetu sisi?'**

Ambapo baada ya kusikia Suali hilo basi akajua kua Ukarimu aliodhania amefanyiwa na watu hao, basi haukua Ukarimu bali ulikua ni mtego wa kumuweka kati na kisha kumhukumu. Hivyo akanyanyuka na kuanza kuwausia watu hao kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kuwaambia kama zinavyosema Aya:

﴿قَالَ أَمَّا مَن ظَلَمَ فَسَوْفَ نُعَذِّبُهُ ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ رَبِّهِ فَيُعَذِّبُهُ عَذَاباً نُّكْراً ۞ وَأَمَّا مَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحاً فَلَهُ جَزَآءً ٱلْحُسْنَىٰ وَسَنَقُولُ لَهُ مِنْ أَمْرِنَا يُسْراً ۞ ثُمَّ أَتْبَعَ سَبَباً ﴾

Qala amma man *dh*alama fasawfa nuAAadhdhibuhu thumma yuraddu ila rabbihi fayuAAadhdhibuhu AAadhaban nukran; Waamma man amana waAAamila salihan falahu jazaan alhusna wasanaqoolu lahu min amrina yusran; Thumma atbaAAa sababan *(Surat Al Kahf 18:87-89)*

Tafsir: ***Akasema (Dhu Al Qarnayn kuwaambia Wale aliokua akikutana nao kua) Ama kwa yule ambae Atakefanya Dhulma Basi Tutamuadhibu Na Kisha Atarudishwa Kwa Mola wake Ambae atamuadhibu Kwa Adhabu Kali sana Na Ama kwa Yule atakaeamini Na Akafanya Mema Basi Atapata Malipo yake Yaliyo Bora Na Sisi tutazungumza Nao Kwa Urahisi kuhusiana na Jambo letu hili Na Kisha Akaendelea Kufuata Sababu nyengine.***

Ambapo Aya zunatuonesha namna Dhu Al Qarnayn alivyokua akizungumza nao watu aliotumwa kuwafikishia Ujumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo ndani yake basi tunaona kua ni mwenye kuonya kua kama Watu hao wataendelea kumshirikisa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kufanya Maovu na hivyo kua ni mwenye Kufanya Dhulma dhidi ya Nafsi yake mwenyewe basi atamuadhibu hapa hapa Duniani kabla ya kufika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambako nako atapokelewa kwa Adhabu kali zaid.

Ambapo katika kuwausia kwake basi kuna baadhi walimfaham na walimkubali na wengine Wakampinga tena sana. Hivyo Dhu Al Qarnayn akawageukia wale waliokataa Ujumbe wake, na hapo hapo Watu hao wakajkuta wamezama kwenye kiza totoro! Kiasi ya kua hawakuweza kuona mbele wala nyuma kwani kiza hicho kiliiingia mpaka ndani ya Macho yao, Pua zao, Ufahamu wao na matumbo yao, na haukuchukua mda isipokua walianza kujawa na khofu kubwa sana Na kuchanganyikiwa, hivyo Wakaanza kulia na kuomba msaada kutoka kwa Dhu Al Qarnayn.

Hivyo Dhu Al Qarnayn akawatoa kwenye Kiza watu hao na kuwaingiza kwenye Nuru na kuwaamuru wafuatane pamoja nae katika Safari yake baada ya kuondoka katika Ardhi yao.

Ambapo watu hao wakakubaliana nae, na kisha Dhu Al Qarnayn akaondoka nao huku akiiamrisha Nuruikae mbele yake na kiza kibakie nyuma yao watu hao ili wasikimbie Dhu Al Qarnayn na Jeshi lake pamoja na watu wa Magharibi linapotua Jua basi wakawa ni wenye kuelekea katika upande wa Kusini kwa ajili ya kuitafuta Ardhi ya Hawil.

Huku akiwa ni mwenye kufuata Sababan baada ya Kujisalimisha kikamilifu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Kwani Moyo wake, Ufahamu wake, Mdomo na Ulimi wake, Mikono yake, Miguu yake na kila kiungo cha mwili wake kilikua kinafanya uadilifu katika kila tendo lake lifanywalo nae.

Na baada ya kuondoka katika upande wa Magharibi basi ameelekea kwemye Upande wa Kusini katika ardhi ya Hawil, ambapo baadhi ya Wanazuoni wanasema kua Ardhi hio ya Kusini ilikua ni Ardhi ya Nchini India. Na Dhu Al Qarnayn alipowasili katika Ardhi hio Basi akatuma Mjumbe wake Ndani ya Ardhi hio kabla ya Kuingia ndaji yake.

Ambapo Mjumbe wake huyo alikua na Ujumbe ufuatao:

Hakika Mimi nna Jeshi Kubwa sana pamoja nami

Na nchi yenu imependeza kwa Mito Maziwa na Miti mingi sana

Na hivyo kama mimi nikiingia ndani ya Ardhi yenu basi nitasababisha Madhara makubwa sana Kiasi ya kua huenda Ardhi yenu nyie Itakua ni yenye kuangamia

Hivyo nakuombeni kua bora nileteeni Mjumbe wenu ili nizungumze nae

Na baada ya Mjumbe wa Dhu Al Qarnayn kufikisha ujumbe huo basi akapewa Mjumbe wa Watu wa Ardhi hio.

Na alipofika Mbele ya Dhu Al Qarnayn basi Dhu Al Qarnayn akanyanyua Uso wake kumuangalia Usoni na kisha akainamisha Uso wake chini baada ya Tukio hilo basi Mtu huyo akatia Vidole viwili puani mwake na kisha akatoka.

Kwani Watu wakaulizana kilichotokea, na hivyo Dhu Al Qarmayn akasema:**Nilipomuangalia Kuanzia juu hadi Chini halafu nikainamisha kichwa basi nilikua nikimwambia kua Hakika ya Watu Warefu sana hua na kawaida ya kutokua na Thamani Ambapo nae akatia vidole Puani kumaanisha kua: Baadhi wanaweza kua na sifa kama hizo lakini mimi sio miongoni mwao.**

Kisha Dhu Al Qarnayn akaamrisha Aitwe Mtu huyo na alipoitwa basi Dhu Al Qarnayn akamrisha awekwe kwenye moja kati ya Mahema yake na kisha akachukua chombo kama bakuli ambacho akakijaza mafuta na kisha akaamrisha apelekewe Mtu huyo bakuli hilo Na baada ya kupewa basi Mtu huyo akalirudisha Bakuli hilo huku akiwa ametia Sindano nyingi sana ndani ya Mafuta hayo.

Dhu Al Qarnayn alipopewa Bakuli hilo basi akaźitoa Sindano hizo na kisha akaweka kioo ndani yake na kuamrisha kua Bakuli lirudishwe.

Na mtu huyo alipopewa Bakuli hilo basi akakitoa kioo hicho na kisha akakipangusa na kukingarisha na kisha akakirudisha kioo hicho. Hivyo watu wa Dhu Al Qarnayn wakaanza kujiuliza: **Kitu gani kinachoendelea?**

Dhu Al Qarnayn akasema: **Nilituma Bakuli la Mafuta kumaanishakua: Mtu mwenye Ilm amewasili. Ambapo Mtu huyu alitia sindano nyingi ndani yake kumaanisha kua Wao pia Wanayo ilm Nyingi na Kubwa. Nami nikatoa Sindano na kuweka kioo ambacho kilichafuka kutokana na mafuta hayo kumaanisha kusema kua**: **Ilm yenu ni ya Bure na haitumiki kwani haina maana yeyote.**

Na yeye akakitoa kioo na kukisafisha na kukirudisha akimaanisha kusema kua: La, sio kama unavyofikiria kwani Ilm yetu sisi ni yenye Kutumika na yenye Kung'arisha Ufahamu wetu

Naam, bila ya shaka *A Used Key is Always Bright* - Ufunguo unaotumika hua Daima Unang'ara

Hivyo Dhu Al Qarnayn akawausia Watu hao na na wakakubaliana nae na kisha akaondoka na baadhi yao pia na kuwajumuisha kwenye Jeshi Lake.

Na kuanza safari ya kuelekea kwenye Maeneo ya Mansik huku akiwa ni mwenye kuliongoza Jeshi lake ambalo ukubwa wake ilikua hakuna mfano wake katika kupindi chake. Katika Safari yao hio ya kuelekea katika sehemu inayochomoza Jua ambayo ni katika maeneo ya Mashariki ya Dunia.

Ambapo alipofika katika maeneo hayo basi alikutana na watu ambao walikua si wenye kujihifadhi kwa kuvaa nguo. Kwani walikua hawana nguo hata moja na wala hawaoneani haya baina yao, kwani kuna wazee, kuna Wanaume, Wanawake, Watoto n.k Watu hao walikua hawana hata sehemu ya kujihifadhia kwani ilikua hakuna Majengo katika sehemu wanazoishi na hivyo walikua na utulivu katika wakati mchana lakini wakati wa usiku walikua hawana utulivu kwani hawana sehemu ya kujihifadhia wala kujipumzishia.

Na hivyo walikua hawana tofauti ya kimaisha baina yao na Wanyama wao. Ambapo anasema Imam Hasal Al Basr kua: '**Ardhi yao watu hao ilikua ni Ardhi ambayo haiweze kustahamili kujenga Majengo juu yake kutokana na Mchanga wake, na hivyo katika wakati wa Mchana walikua wakiishi ndani ya Maji na Jua linapozama basi hua ni wenye kutafuta chakula chao'**

Ambapo kwa upande wa Imam Abd Rahman Al Kalbi basi yeye anasema kua: '**Watu hawa walikua ni watu wa Taifala Mansik, na walikua ni watu ambao hawavai viatu wala nguo na walikua ni Vipofu wasioona kutokana na Nyoyo zao kwani walikua hawana Imani kabisa juu ya Mola wao.'**

Ambapo kwa Upande wa Amr Ibn Malik basi yeye anasema kua: '**Mimi nilienda kwenye Ardhi ya Samarkand na kisha nikawakuta Watu wanazungumzia kuhusiana na watu wanaoishi katika Sehemu inayochomoza Jua. Nami nikaulizia kuhusiana nao na kuambiwa kua itanibidi niende China nami nikaenda masafa baina yao na sehemu niliyokuwepo ni safari ya Siku moja. Hivyo nikamkodi mtu ili anipeleke na akanipeleka na nikakutana nao ambapo mtu niliefuatana nae alikua akijua Lugha yao.**

Na walimwambia kua tutayaona tutakayoyaona baada ya kuchomoza Jua, na Jua lilipochomoza nikasikia Ukelele mkali sana kiasi ya kua sikustahmili bali nikazimia. Na nilipozindukana nikajiona kua nnakandwa huku nikiwa nimepakwa mafuta, na kuwekwa katika sehemu nisiyoifaham huku watu hao walikua wakivua Samaki.'

Na anasema Imam Mujahid Ibn Jabar kuhusiana na maneno ya aya ya 88 ya Surat Al Kahf yasemayo kua:

﴿ وَأَمَّا مَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحاً فَلَهُ جَزَآءً ٱلْحُسْنَىٰ وَسَنَقُولُ لَهُ مِنْ أَمْرِنَا يُسْراً﴾

Waamma man amana waAAamila salihan falahu jazaan alhusna wasanaqoolu lahu min amrina yusran; *(Surat Al Kahf 18:88)*

Tafsir: ***Na Ama kwa Yule atakaeamini Na Akafanya Mema Basi Atapata Malipo yake Yaliyo Bora Na Sisi tutazungumza Nao Kwa Urahisi kuhusiana na Jambo letu hili.***

Kua Dhu Al Qarnayn alikua ni wenye kuwaahidi watu hao anaowaita kwa ajili ya kufuata Nji ya Maisha ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua Ama kwa wale watakaoamini na kufanya Mema basi sisi tunaahidi kua TutamfundishaIlm ya Dini ya Kiislam kulingana na Uwezo wetu tuliokua nao tena kwa Unyenyekevu. Na tutamuongoza katika njia ya Kumkaribia *Allah Subhanah wa Ta'ala* hafi kufikia kua na ukaribu zaid nae.'

Na katika kuelezea kwake basi tunaona kua Dhu Al Qarnayn anaelezea Jukumu lake hilo pamoja na watu wake la kuwaongoza watu kua sio Jambo gumu, bali ni jambo Jepesi tena sana na hi ni kwa

sababu kile wanachokifanya waokinatokana ndani ya Usafi wa Nyoyo zao na hivyo hua ni wenye kuhisi Wepesi na Raha ndani ya Nyoyo zao.

Ambapo ndani ya maneno haya basi tunaona kua Dhu Al Qarnayn anaweka wazi kua Mfumo wa Maisha ya Dini ya Kiislam sio mfumo Mgumu tofauti na wanavyofikiria wengi wasiojua. Na pia tofauti pia na wanavyoufanya wengi wasiojua Miongoni mwa Waislam, na hivyo kupelekea pia wale wasiojua Uislam kuuona kua ni mgumu sana. Wakati ni mfumo mwepesi sana wa Maisha kwa sababu ni wenye kusimamia Maslahi ya Viumbe na Mazingira yao wanauoishi hapa Duniani kwa Ujumla.

Na katika kutilia mkazo hili pia basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* alimwambia Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

﴿وَٱخۡفِضۡ جَنَاحَكَ لِمَنِ ٱتَّبَعَكَ مِنَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ﴾

Wakhfidh Janahana LimanittabaaAka mina Al Muuminina *(Surat Ash Shuara 26:215)*

Tafsir: ***Na Lishushe Bawa Lako (la Huruma) Kwa Wale Watakaokufuata Miongoni mwa Waumini***.

Ambapo hizi ni aya zinayotuonesha kua Kila Muislam anatakiwa kua na Huruma kwa Waislam wenzake na kuwraahisishia mambo hususan pale Waislam hao wanapokua ndio kwanza wameingia kwenye Dini ya Kiislam.

Na aya hii ya pili imetoa mfano hasa wa neno *Janahaka* yaani Bawa na hivyo kuainisha hali ya kua na huruma nao kam vile Kuku anavyokua na huruma na Vifaranga vyake katika kuvijali na kuvihifadhi kwa kuvifunika ndani Mabawa yake.

Hivyo aya zinaendelea kusema kuhusiana na Safari za Dhul Qarnayn kua:

﴿حَتَّىٰٓ إِذَا بَلَغَ مَطۡلِعَ ٱلشَّمۡسِ وَجَدَهَا تَطۡلُعُ عَلَىٰ قَوۡمٖ لَّمۡ نَجۡعَل لَّهُم مِّن دُونِهَا سِتۡرٗا ۞ كَذَٰلِكَ وَقَدۡ أَحَطۡنَا بِمَا لَدَيۡهِ خُبۡرٗا ۞ ثُمَّ أَتۡبَعَ سَبَبًا﴾

Hatta idha balagha matliAAa alshshamsi wajadaha tatluAAu AAala qawmin lam najAAal lahum min dooniha sitran; Kadhalika waqad ahatna bima ladayhi khubran; Thumma atbaAAa sababan. *(Surat Al Kahf 18:89-91)*

Tafsir: ***Kisha akaendelea Kufuata Sababan hadi Pale alipofikia Machomozo ya Jua akalikuta linachomoza kwa Jamii ya Watu Ambao Hatukuwajaalia Kitu cha Kujistiri dhidi yake kadhalika na hivyo ndivyo tulivyojua kuhusiana na Habari zake zote.***

Na kama tunavyoona kua Aya hizi zinautofautiana Na aya zilizotangulia, na hii ni kwa sababu aya hazikusema kuhusiana nini cha kuwafanya Watu hawa wa Mashariki. Na wala hazikusema kua Watu hawa wa Mashariki kama walikua ni Wenye Kuamini ama la. Ila zimesema kuhusiana na Mazingira

yao waliyokua wakiishi watu hao. Ambayo ni mazingira ya watu wenye kuishi katika eneo lililowazi la ardhi na wao walikua ni watu ambao hawana Majumba wanaoishi ndani yake.

Ambapo kwa upande mwengine basi kutokana na Ufahamu na ilm aliyopewa Dhu Al Qarnayn na uwezona Sababu au njia za kutekeleza Majukumu yake basi inawezekana ikawa alifanya kwa watu hawa kama yale aliyoyafanya kwa watu wengine aliowatembelea hapo kabla yaani katika maeneo mengineo. Na pia inawezekana kua ikawa Dhu Al Qaranayn hakuwafanya kitu chochote watu hawa bali aliwaacha kama walivyo na maisha yao bila ya kuwaingilia katika Mfumo wa maisha yao wanayoishi.

Na baada ya hapo *Allah Subhanah wa Taala* anathibitisha kuhusiana na Maisha ya Dhu Al Qarnayn na Safari zake hizo kwa kusema kua Bila ya Shaka Sisi ni wenye kujua Kila kitu chake Dhu Al Qarnayn kwani tulikua tumemzunguka katika kila Kitu chake. Subhanah Allah!

Tunapoyangalia maneno haya basi tunaona ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na uwezo wake wa kusimamia Kila kitu kikamilifu tangu mwanzo wake na mwisho wake bila ya kupungukiwa uwezo huo, Wala kuchoka, Wala kughafilika, Wala kukosea n.k

Ambapo kwa wasiofikiria walakutafakkari basi ndio unakuta wanajiuliza, Hivi hii Funga ya Arafah ni sawasawa na kisimamo cha Mahujaj ama vipi? Au Laylat ul Qadr inakuaje? Kama mimi niko Marekani nitafungaje wakati inakua Usiku?

Hivyo kutokana na kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kua na uwezo Juu ya kila kitu na ni mwenye kujua kila kitu basi yeye anao uwezo wa Kuifanya Dunia nzima yote ikawa na Saa moja kuanzia Mashariki hadi Magharibi. Lakini hakufanya hivyo kutokana na Hikma zake kua hawa iwe leo wale iwe kesho.

Na yeye pekee ndie mwenye mamlaka ya kupokea na Kuikubali Ibada ya Mja wake katika siku husika kulingana na Nia Husika. Hivyo kama nia yako ni kwa kufuata Sunna ya kama alivyofanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Basi fuata Sunna ya kushikamanisha Ibada zako zinazotegemea Nyakati maalum kulinga na Nyakati za sehemu uliyokuwepo. Kwani hivyo ndivyo alivyofanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ama kwa Upande mwengine basi tunapoangalia katika upande wa Tafsir ya Wanazuoni wa Ilm ya Tasawwuf kuhusiana na ayah hii basi tunaona wanasema kua: **‘Kwa mtizamo wa Juu Juu basi Dhu Al Qarnayn alikua ni mwenye kutaka kuona sehemu inayochomoza Jua Lakini kwa upande ndani wa Kiroho basi tunaona kua Dhu Al Qarnayn katika kuenda kwake katika Upande wa Mashariki basi ilikua ni kwa ajili ya Kuifikia hali ya Uchomozaji wa Jua la Kiroho. Ambapo Jua hili hua si kitu chochote isipokua hua ni Nuru ya Moyo, ambayo hua ni yenye kutandua Mapazia ya Ulimwengu wa Al Ghayb.’**

‘Hivyo nae akafuata Sababu au Njia ambayo itakayompelekea kwenye Nuru hio na akaikuta inachomoza kwenye Nyoyo za watu wenye wenye Maarifah. Ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewajaalia kua ni wenye kumurikwa na Nuru hio na hivyo hawana Sehemu ya kujifichia kutokana nayo, baada ya kuwajaalia hali ya kua ni wenye kupanda Darja watu hao.’

Kwani watu wenye Ilm hio ya Maarifah ya kumjua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni wenye Mapenzi ya hali ya juu sana kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Kiasi ya kua Hua hawawezi kutokua nae Mola wao Nyoyoni mwao na hivyo hua ni wenye kujihisi kua hawatokua na sifa

stahiki za Kuhesabiwa kua ni Waislam waliojisalimisha mbele ya Mola wao pale itakapotokea Wao kua wanakaa bila ya Kumkumbuka Mola wao. Na hivyo watu wa aina hii hua ni wenye kuogelea kwenye Bahari ya Kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kua hawana kitu ndani ya Nyoyo zao, isipokua Mola wao.

Na ukweli ni kua tunapoiangalia zaidi ayah hii basi tunaona pia imetumia Neno *Satara* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kustiri, Kufunika, Kuhifadhi, Kuweka Kitu ndani ya Pazia, Kuficha, na pia humaanisha Kua na Haya.

Ambapo anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kua:

﴿ وَقَالُواْ لِجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدتُّمْ عَلَيْنَا قَالُوٓاْ أَنطَقَنَا ٱللَّهُ ٱلَّذِى أَنطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُوَ خَلَقَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ۞ وَمَا كُنتُمْ تَسْتَتِرُونَ أَن يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلاَ أَبْصَارُكُمْ وَلاَ جُلُودُكُمْ وَلَـٰكِن ظَنَنتُمْ أَنَّ ٱللَّهَ لاَ يَعْلَمُ كَثِيراً مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴾

Waqaloo lijuloodihim lima shahidtum AAalayna qaloo antaqana Allahu alladhee antaqa kulla shay-in wahuwa khalaqakum awwala marratin wa-ilayhi turjaAAoona; Wama kuntum tastatiroona an yashhada AAalaykum samAAukum wala absarukum wala juloodukum walakin dhanantum anna Allaha la yaAAlamu katheeran mimma taAAmaloona*(Surat Fusilat 41:21-22)*

Tafsir: ***Na Watasema (Watu katika siku ya Malipo) Kuziambia Ngozi zao, 'Hivi Kwanini Mnashuhudia Dhidi yetu?'. Zitasema Ngozi: Allah ametusababishia kusema Ambae Ndie Aliekifanya Kila Kitu Kiseme, Na yeye ndie Alieukumbeni Mara ya Kwanza na Kwake Yeye ndio Mmerudishwa Na Kama msingestirika kwa kujificha dhidi yenu wenyewe. Basi Visingeshuhudia Juu yenu Masikio yenu wala Macho yenu Wala Ngozi zenu Lakini Nyinyi Mlikua Mkidhania kua kwa Hakika Allah Hajui Mengi sana miongoji mwa mnayoyafanya.***

Allahu Akbar Kabira Wa Alhamd lillah Kathira wa Subhanah Allahi Bukratan wa Asila!

La Ilaha Illa Allah Wahdahu la Sharika lah Lahu Al Mulk wa Lahu Alhamd Yuhyi wayumit wa huwa aAla Kulli shay-in Qadir, tumeanza na maana ya neno *Satara* na kisha tukaangalia Mfano wa Aya iliyotumia tena neno hilo huku ikiwa ni aya yenye kudhihirisha maana halisi ya neno hilo kulingana na Mtizamo wa Kimaumbile ya Ibn Adam na kisha pia maana ya neno Kulingana na upande wa Muumba ambae ni *Allah Subhanah aa Ta'ala.*

Ambapo tunapozungumzia kwa upande wa Muumba basi hua hakuna Kitu chochote ambacho kitaweza kua chini ya Sitran dhidi yake. Kwani kwake yeye kila kitu kiko wazi kabisa, ila kwa upande wa Viumbe wake basi yeye ni mwenye kua Nyuma ya Sitra na hivyo hua ni mwenye kuonekana kupitia kwa dalili zake tu.

Hivyo tunapomzungumzia Dhu Al Qarnayn basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaelezea kuhusiana nae kua Hakika ni mwenye kujua kila kitu juu yake kwani amemzunguka kwa Ilm yake juu yake, chini yake, ndani yake, nje yake, kabla yake, baada yake, n.k

Na hivi ndivyo inavyokua Juu ya kila kitu alichokiumba *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale tunapozungumzia Uhusiano wake juu ya Viumbe wake. Na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawa na sifa ya kua ni Mungu ambae ndie Muumba wa Kila kitu na msimamizi wa Kila kitu alichokiumba tangu mwanzo wake hadi mwisho wake. Na tunapozungumzia usimamizi i basi tunazungumzia usimamizi wa Kila kila katika kile Sekunde ya Uhai wa Kiumbe kabla ya kuwepo kwake baada ya kuwepo kwake na baada ya kutoweka kwake.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:*

«إِنَّ اللهَ عزَّ وجلَّ حَيِيٌّ سَتِيرٌ، يحب الحياءَ والسَّتر؛ فإذا اغتسل أحدُكم فليستتر»

'Inna Allaha Aaza wa Jalla Hayyi Satir yuhhibu alhayyaa wa al sitra faidha ightasil ahadakum falyastur'

Tafsir: ***Hakika Allah mwenye Nguvu na Utukufu Yuhai Na Aliefichikana Na Anapenda Staha Na Stara Hivyo Atakapokoga mmoja wenu basi na ajistiri****(Imam Abu Daud)*

Naam...Hivyo *Al Satar* pia ni miongoni mwa Majina Matukufu ya Allah Subhanah wa Ta'ala ambalo ni lenye kumaanisha Kua Yeye ni Mwenye Kustiri, Mwenye Kuhifadhi, Mwenye Kuficha, na ni mwenye Kupenda hasa Kustiri Waja wakena kuwahifadhi kutokana na kasoro zao na Udhaifu wao wa Kimaumbile.

Hivyo kwa upande mwengine basi tunaona kua Sifa Tukufu ya Al Satar ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua pia ni Sifa yenye kumaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye Utukufu wa Kukubali Kustiri au kuhifadhi Kasoro na Makosa ya Mja wake kwa ajili ya Kuja kumsamehe baadaekutokana na Mapenzi yake juu yake pale Mja huyo atakapokuja Kumuomba Msamaha Mola wake.

Ndio maana wakasema wenye kujua kua **Allah ni Mwenye Kustiri na ni mwenye Kupenda Stara, Hivyo ewe Mja nawe Stiri Siri na Aibu za Mja Mwenzako kwani Masiku ni Mzunguko Leo Yake kesho Yako. Na Kwa Mwenye Sifa ya Utukufu wa Kupenda Kustiri basi hua Hakuna Kinachoweza Kustirika bila ya Stara yake, Hakuna Kitakachokosa Stara pale atakapoamua Kukistiri na hakuna Kitakachoweza Kustirika kama akiamua Kukidhihirisha.**

Hivyo tunaporudi kwa Dhu Al Qarnayn basi tunaona kua pia nae alikua amepewa Stara kutokana na Aibu ya Kutoshindwa katika ufanikishaji wa Majukumu yake mbele ya Mola wake ambae ni Mbora wa Kustiri na mwenye kupenda Kustiri Waja wake.

Hivyo aya zinaendelea kutuelezea kuhusiana na Dhu Al Qarnayn kwa kusema kua alifuata Njia Hadi:

﴿حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ بَيْنَ السَّدَّيْنِ وَجَدَ مِن دُونِهِمَا قَوْماً لاَّ يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ قَوْلاً ﴾

Hatta idha balagha bayna alssaddayni wajada min doonihima qawman la yakadoona yafqahoona qawlan *(Surat Al Kahf 18 93)*

Tafsir: ***Hadi Alipojikuta baina ya Milima Miwili na Akakuta Baina yake Milima hio Jamii ya Watu Ambao Hata kidogo Hawawezi Kufaham Kauli***

Naam..Hivyo Aya zinasema kua katika Kufuata kwake Sababan basi Dhu Al Qarnayn alisafiri hadi akafika katika eneo ambalo lina Saddain yaani Vizingiti Viwili Vikubwa au Ukuta wa Mabwawa ya Kuzuia Maji kama yanayozalisha Umeme au Milima Miwili au Vikwazo Vinavyowekwa kwa ajili ya Kuziba Njia Ili watu wasipite katika sehemu husika n.k

Na kwa Upande aa Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kua: ' **Saddain zilizozungumziwa hapa basi ni ile sehemu ya Milimaya Mikunjo iliyoambatana pamoja iliyopo baina ya ardhi ya Armeni na Azerbaijan.'**

Ambapo huo ni Mtizamo wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* na inawezekana alisema hivyo kwa sababu kwa upande wao pia katika Wakati huo, Ilikua hawajafika katika maeneo ya India na China bado yaani Uislam ulikua haujaingia katika maeneo hayo, ambayo ndani yake mna Milima ya Himalaya.

Lakini kwa kua Uislam ulikua tayari unaingia katika Ardhi ya Armenia na Azerbaijan kutokea Syria na Uturuki na Waislam wakakutana na Milima iliyopo katika Maeneo hayo basi Ndio wakachukua Mfano huo kua huenda ikawa ni maeneo hayo.

Na ndio maana katika miongoni mwa Mitizamo ya Wanazuoni waliofuatia basi tunaona kua wao wana Mitizamo tofauti juu ya maeneo hayo. Kwani kuna wasemao kua ni maeneo ya Milima ya Khurasan, Kuna wasemao ni maeneo ya Milima ya Samarqand, kuna wasemao ni maeneo ya Ardhi ya baina ya Milima ya Himalaya n.k

Ambapo kwa upande mmoja au mwengine basi tunapoangalia maeneo hayo yote Waliyoyataja Wanazuoni basi tunaona kua ni maeneo ya Bara la Asia katika sehemu ya Katikati yaani Kusini mwa Nchi ya Urusi na China na Kaskazini ya meneo ya Mashariki ya Kati ambayo ndio maeneo yanayojumuisha Khurasan hapo zamani na kwa upande wa Samarqand basi ni maeneo ya Kaskazini mwa Afghanistan na Pakistan.

Na hii ina amaanisha kua katika Kusafiri kwake na kufuata Sababan basi Dhu Al Qarnayn alienda Magharibi, kisha akaenda Kusini na akaenda katika Maeneo ya Mashariki na kisha akapandisha Juu kuelekea katika maeneo ya Katikati ya Bara la Asia.

Na alipofika katika maeneo hayo yaliyo baina ya Milima basi akakutana na watu wasiojua Lugha na aya hii pia inatuonesha kua Dhu Al Qarnayn alipofika katika eneo husika basi alikuta sehemu ambayo Njia yake Imezibwa baina ya Milima miwili.

Na katika sehemu hio akakuta Watu ambao Ufahamu wao ni mdogo na hii pia inaonekana ni kutokana na kua Walikua hawafamu maneno ya Kauli. Yaani Hawafahamu kabisa kuzungumza kwa Kutumia Sauti ya maneno ya Lugha. Na hivyo walikua wakizungumza kwa kutumia Sauti za ajabu na Ishara za viganja vya Mikono.

Hivyo hii inamaanisha kua Dhu Al Qarnayn aliwafaham namna wanavyozungumza watu hawa kutokana na Ishara zao na ukubwa na Upana wa Ufahamu wake aliojaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Au pia inawezekana ikawa alifahamiana nao kwa kutumia Mkalimani…Wa Allahu Aalam.

Na katika kuzungumza nao basi nao wakamwambia kwa kumlalamikia Dhu Al Qarnayn kuhusiana na Juj wa Majuj. Ambapo Wanazuoni wametofautiana sana kuhusiana na asili yao pia.

Kwani anasema Imam Qatadah Al Sadusi kuhusiana nao kua: '**Juj wa Majuj wamegawika katika Makabila 21 Na Dhu Al Qarnayn aliyafungia Makabila yao 20. Ndani ya Ukuta alioujenga na hivyo Kabila moja miongoni mwa hayo 21 Limebakia nje ya Ukuta huo.'**

Na kama tunavyojua kua tunapoangalia katika kisa cha Nabii Nuh basi tunaona kua, Nabii Nuh alikua na Watoto watatu ambao ndio waliobakia baada yake na kutokana nao basi Wakazaliaa watu wote waliofuatia baada yao watoto hao walikua ni Sam, Ham na Yafet.

Ambapo inasemekana kua Sam ndio Baba wa Waarabu, Warumi na Waajemi. Ham ndie Baba wa Waafrika. Na Yafet ndie Baba wa Watu wa Kaskazini Mwa Mashariki ya Kati ambapo ndani yake ndio kuna Warusi, Waturuki, Waslavia na Juj wa Majuj.

Ambapo neno Juj wa Majuj linatokana na maneno Ujij aAla Nnar yenye kumaanisha Mwangaza na Cheche zitokazo na Moto. Na hayo ndio Maubile ya Juj wa Majuj Kitabia.

Hivyo amesema Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kuhusiana na Juj wa Majuj kua: '**Juj wa Majuj wamegawika katika Makabila 21 Na Dhu Al Qarnayn aliyafungia Makabila yao 20 ndani ya Ukuta alioujenga na hivyo Kabila moja miongoni mwa hayo 21 Limebakia nje ya Ukuta huo. Na Kabila hilo Moja lililobakia Nje ya Ukuta huo wameitwa Turkik kwa sababu ya kua ni Walioachwa Nje ya Ukuta. Kwani Neno Turkik linatokana na neno Turku la Kiarabu ambalo linamaanisha Kuachiwa.'**

Huo ni Mtizamo tu na hivyo hatusemi kua Waturuki ndio Moja kati ya Kabila hilo la watu walioachwa Nje na wala haimaanishi hivyo.

Naam..nasema hivyo kwa sababu kwanza Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi ambae tulisema katika Historia ya Maisha yake kua alikua ni Imam Kipofu lakini ni Mwenye Ufaham wa kutisha sana kwani alikua haiwezekani ukasema kitu kwake mara moja tu na kisha akakisikia ukadhani kua atakisahau..la.

Alikua hakisahau kile alichokisia kwa maisha yake yote yaani Ufahamu wake ulikua kama Maktaba ambamo unaweka Kitabu leo kisha miaka 10 baadae ukikifungua na kukiuliza ya Miaka 10 nacho kinakupa yote ya miaka hio baada ya kukisoma kwake.Kwa hivyo Imam Qatadah alikua ni Kipofu na hakuwahi kuwaona Waturuki, ila inawezekana kua aliwahi kusikia katika kusomeshwa kwake au alifaham hivyo kutokana na Upana wake wa Lugha ya Kiarabu. Na hivyo alifafanua maana ya neno kulingana na Mzizi wa Neno Husika kama ilivyo Lugha ya Kiarabu kuaKila neno lina Herufi husika ambazo hua ndio Mzizi wa Neno au Jina Husika.

Na pili ni kwa sababu Wanazuoni waliotangulia kabla yetukwa miaka 1000 iliyopita Walikua ni Salafi Al Salih kweli.

Yaani ni watu waliokuwepo kwenye Njia ya Uongofu kweli na hivyo Wanaijua Dini yao na Wanamuogopa Mola wao na hivyo Walikua ni watu wenye Tahadhari sana katika mambo ambayo yenye Shubha ndani yake. Yaani akikihisi tu kua hiki kitu kitanipatisha dhambi au kitanipunguzia Malipo ya thawabu zangu au nna shaka na wasiwasi nacho basi alikua anawachana nacho kitu hicho, hata iwe ni Dhahabu ya Kilo 100. Ataiwacha tu.

Tofauti na wengi miongoni mwa wanaojinasibisha nao leo hii kwa Usalafi, kwani wao hawana zaidi ya Unafiq, kutokana na Kujinasibisha na Sifa za Watu ambao hata kuwajua hawawajui. Na kwa sifa hawawafikii hata kwa lile Vumbi lao.

Na ni pale tunapoangalia Maisha ya Hao Salaf Salih wenyewe na kisha tutajua kwanini Imam Qatadah Al Sadusi akasema na kufikiria kwa namna alivyofikiria kuhusiana na Juj wa Majuj.

Na mfano huo si wa Imam Sufyan Ath Thawry amabe alienda kwa rafiki yake fundi Sonara na katika kukaa basi aliangusha Dinari ya Dhahabu, na alipotaka kuiokota Dinari hio basi akaona kau chini hapo kuna Dinar za Dhahabu baala ya moja, hivyo akanyanyuka bila kuokota Dinar yake kwa khofu ya kuogopa kufanya Dhulma ya kuchukua Dinar ya Dhahabu ambayo si yake. Jee Wanaojiita Salafi leo hii wanaweza kufanya Hivyo?

Naam, katika kufahamishana kuhusiana na namna Walivyojitahidi Maimamu walioishi katika Miaka 300 ya mwanzoni mwa Uislam kufafanua baadhi ya mambo yaliyoelezewa kwa juu juu ndani ya Qur'an, basi tunaona kua walijitahid kutafakkar na kutumia Ufahamu wao kulingana na mazingira yao katika wakati walioishi kwa ajili ya kutufikishia sisi mimi na wewe ili tusiwe ni wenye kubakia kizani. Na ingawa tuko katika Kisa cha Dhu Al Qarnayn lakini ili kufahamu zaid basi inabidi kuoneshana mfano wa Mithili walivyokua Waakishi waliotangulia kabla yetu ambao ndio wenye Sifa stahiki za Salaf na Walivyokua wakiyatilia maanani kwa Imani ya kweli na Taqwa maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ya *Mtume wake Salallahu Alayhi wa Salam.*

AL MASIH AL DAJJAL

Neno Masih kwa Lugha ya kiarabu hua linamaanisha Kujifuta kwa kutumia mkono au mikono, Kujipangusa, Kutembea Juu ya Ardhi kwa miguu, ambapo Neno Al Masih hua linatumika kwa Al Dajjal ambalo ni neno lenye kumaanisha Mpotovu Muongo atakaetembea Ardhini, na pia hua linatumika kwa Nabii Isa ambae ni Masih Isa Ibn Maryam kutokana na kua ni mwenye Kutembea Sana Ardhini.

Na kama ilivyokua kwa Nabii Isa kua alikua ni mwenye kua na uwezo wa kufanya Miujiza ya Kutibu watu kwa kutumia mikono yake kwa kuwagusa kua kama Dalili kwa ajili ya kuwaongoza Watu katika Njia ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* basi na Dajjal pia atakua na sifa kama hizo hapo atakapokuja, kwani atakua na miujiza kwa kutumia mikono yake, lakini kwa ajili ya kuwapotosha watu kutokana na kufuata njia ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na pia kama ilivyokua kwa Nabii Isa *Alayhi Salatu wa Salam* kua hakuwa na mke wala mtoto basi Miongoni mwa Dalili zake Dajjal pia ni kua hatokua na Mtoto wala mke.

Neno Dajjal pia limetokana na neno Dajala ambalo hua linamaanisha kuchnganya mambo au vitu kwa makusudi na hivyo kuvifanya kua vigumu kuwezekana kuvitofautisha

Ambapo wenye lugha yao hua wanatumia msemo usemao *'Dajjala al Ba'air'* yaani kumpaka Ngamia mafuta machafu kutokana na kua na maradhi ya Wadudu wanaosababisha maradhi ya Ukurutu wa kuambikiza ambayo huanzia kwa Ngamia na kisha kuwaambukiza Ibn Adam pia, hivyo Ngamia hupakwa mafuta machafu kwa ajili ya kuzuia maambukizo ya maradhi hayo.

Na amesema Imran Ibn Husein *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: 'Tangu kuzaliwa kwa Ibn Adam hadi mwisho katika wakati wa kukaribia Kiama basi hakuna Mtihani mkubwa utakaotokea kama Mtihani wa Dajjal'**

Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allau Anhu* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisimama mbele za watu na kisha akamsifu na akamtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama anavyostahiki kutukuzwa kisha akaanza kumzungumzia Masih Dajjal na akasema kua: 'Nakuonyenyi dhidi yake (Dajjal) kwani akuna Mtume ambae hakuwahi kuwaonya watu wake dhidi yake, bila ya shaka Nuh aliwaonya Watu wake juu yake, lakini mimi nitakuambieni yale ambayo hakuna Mtume aliewaambia Watu wake juu yake hapo kabla, mnatakiwa mjue kua atakua ni mwenye Jicho moja na *Allah Subhanah wa Ta'ala* si mwenye Jicho moja.''(***Imam Bukhari)*

Ama kwa upande mwengine basi Wanazuoni pia wanasema kua Masih Dajjal kwa sababu ni Mamsuh katika upande wa Jicho lake moja, yaani atakua na kasoro kwani jicho hilo halitokua ni lenye kuona, kama vile alaivyosema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Masih Dajjal atakua ni Mamsuh kwenye Jicho lake moja na atakua ni mwenye kuandikwa neno Kafir kwenye paji lake la uso.'**

Ambapo katika Hadith nyengine basi amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Masih Dajjal atakua ni Mamsuh kwenye Jicho lake moja na atakua ni mwenye kuandikwa neno Kafir baina ya Macho yake mawili, maneno ambayo kila Mumuumini atakua ni mwenye kuweza kuyasoma, iwe Muumini huyo anajua kusoma ama la.'**

Na amesema Abu Umamah Al Bahili kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituzungumzia sisi kuhusiana na Dajjal na kisha akatuonya kuhusiana nae na miongoni mwa mambo aliyoyasema juu yake ni kua: 'Kamwe hakutokua Mtihani a juu ya Ardhi tangu *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipowaumba Ibn Adam ambao utakua mkubwa kama mtihani wa Dajjal. Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuwahi kutuma Mtume yeyote yule ambae hakuwahi kuaonya watu wake kuhusiana na Dajjal. Mimi ni Mtue wa mwisho na nyinyi ndioe Ummah wa mwisho. Hivyo bila ya shaka Dajjal atatokea miongoni mwenu.'**

Na kama akitokea wakati bado mimi nikiwa niko pamoja nanyi, basim imi nitapingana nae kwa ajili ya kila Muislam, na kama akitokea wakati mimi nikiwa siko miongoni mwenu, basi kila mmoja atapingana nae kulingana na Imani yake na nafsi yake dhidi ya Dajjal na *Allah Subhanh wa Ta'ala* atamsimamia kila Muislam dhidi yake Dajjal kwa ajili yangu mie.

Dajjal atatoea katika maeneo ya Al Khallah, baina ya ardhi ya Sham na Iraq na atasababisha matatizo makubwa kulia na kushoto, hivyo enyi waja wa Allah kuweni na msimamo, nami nitamuelezea kuhusiana nae kwa namna ambayo hakuna mtume aliemuelezea kabla yangu.

Ataanza kwa kusema kua: 'Mimi ni Mtume' lakini hakuna Mtume mwengine zaidi baada yangu' na kisha atafuatia kwa kusema kua: 'Mimi ndie Mola wenu' lakini haiwezekani kwenu kumuona Mola wenu hapa Duniani hadi baada ua kifo. Dajjal ni mwenye Jicho Moja na Mola wenu si mwenye kua na Jicho moja. Dajjal atakua ni mwenye kuandikwa Kafir baina ya macho yake, na kila Muumini atakua ni mwenye kuweza kusoma neno hili iwe Muumini huyo anajua kusoma ama la.

Miongoni mwa mitihani yake ni kua atakua ni mwenye kua na Pepo na Moto, lakini Moto wake utakua ni Pepo na Pepo yake itakua ni Jahannam, hivyo yeyote yule atakaepata Mtihani kwa kujaribiwa kwa kutumia Moto wake basi na amtegemee *Allah Subhana wa Ta'ala* na awe ni mwenye kusoma aya za mwanzoni za Surat Al Kahf, na hivyo Moto huo utakua Baridi na salam kwa ajili yake kama namna ulivyokua Moto kwa ajili ya Ibrahim.

Sehemu ya Mitihani yake ni kua atamuambia mmoja kati ya Mabedui kwa kusema kua: 'Unaonaje kama mimi nikimfufua Baba yako na Mama yako kwa ajili yako, jee utashuhudia kua mimi ndio Mola wako?' na Bedui huyo atasema : 'Ndio' na kisha baada ya hapo watatokea Mashaytani wawili ambao watakua na mithili ya Baba yake na Mama yake Bedui huyo na kisha watasema kumwambia Bedui huyo kua: 'Ewe Mtoto wetu Mfuate huyu kwani kwa hakika huyu ni Mola wako.

Miongoni mwa Mitihani yake ni kua atamkamata mtu na kisha atamuua, na kisha atamkata kwa msumeno pande mbili tofauti na kisha atakua ni mwenye kusema kua: 'Mwangalieni Mja wangu huyu, kwani nitamfufua na kisha atasema kua mimi ndie Mola wake' na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamfufua Mtu huyo na mtu huyo atakua ni mwenye kuulizwa na Dajjal kwa kuambiwa: 'Jee ni nani Mola wako?'

Mtu huyo atasema: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* ndio Mola wangu na wewe ni Adui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala kwani* wewe ni Dajjal. Na kwa hakika mimi sijawahi kujua kuhusiana nawe kama nilivyojua leo hii''

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hasan Al Tanafisi basi yeye anasema kua**: 'Al Muharibi ametuambia sisi kua Ubaid Allah Ibn Walid Al Wassafi, kua amesema Atiyyah kua amesema Abu Said kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: 'Kwa hakika Mtu huyo atakua na Darja kubwa sana Peponi.'**

Na Abu Said akasema: 'Wa Allahi sisi hatukua tukimfikiria mtu mwengine yeyote ambae atakua na sifa hizo isipokua atakua ni Umar Ibn Al *Khattab Radhi Allahu Anhu*, hadi pale alipofariki'

Al Muharibi anaendelea kusema kua: 'Kisha tukarudi katika maneno ya Abu Rafi amabe anaendelea kusema kua: 'Sehemu ya Mitihani yake ni kua na uwezo wa kuziamrisha Mbingu kua zinyeshe Mvua na mvua hio itanyesha, na miongoni mwa Mitihani yake ni kua atapita katika sehemu ambayo atakutana na Ukoo wa watu ambao watakua si wenye kumuamini, na hivyo baada ya kuondoka kwake basi Mifugo yake yote itaangamia na mashamba yao.

Na miongoni mwa mitihani yake kua atapita katika sehemu ambayo watu wake watakua ni wenye kumuamini maneno yake. Na hivyo ataziamrisha Mbingu kunyesha Mvua na Mvua itanyesha, na Mazao yatanawiri na kustawi na Wanyama wao watanenepa sana kiasi ya kua watakua wanarudi kutoka malishoni wakiwa na hali tofauti ya kunenepa na hali waliyokua nayo jana yake, na chuchu zao zikiawa zimejaa maziwa tela.

Hakuna hata sehemu moja ya ardhi ambayo ataipita bila ya kua ni mwenye kuishinda na kuwazidi nguvu na uwezo watu wake isipokua katika miji ya Makkah Na Madina, kwani itakua kila akijaribu kuiingia Miji hio basi atakua ni mwenye kukutana na upinzani wa Malaika ambao tayari wametoa mapanga yao wakiwa wanamsubiri, na hivyo atasimama kwenye kilima

chenye rangi nyekundu kilichopo mwishoni mwa eneo moja lenye maji na majani yaotayo majini.'

Na kisha Mji wa Madian utatetemeka mara tatu na watu wake na hadi hautokua na mnafiq hata mmoja ndani yake miongoni mwa Wanaume na Wanawake ambao watatoka na kumfuata Dajjal na hivyo Mji huo utakua ni wenye kusafishwa kutokana na uchafu huo wa Wanafiq kama vile namna Chuma kinavyosafishwa kutokana na uchafu wake kwa Moto, na hio itakua ni siku inayojulikana kama siku ya Uokozi.'

Ambapo Umm Sharik Bint Abi Bakr akauliza: 'Ya Rasul Allah! Hivi Waarabu wote watakua wapi katika wakati huo?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: 'Katika siku hio Waarabu watakua ni kidogo sana kiidadi, na wengi wao watakua wanaishi katika maeneo ya Bayt Al Maqdis na kiongozi wao atakua ni Mcha Mungu, na hivyo kiongozi wao huyo atakapotoka katika asubuhi moja kwa ajili ya kusalisha Sala ya Alfajir, basi Isa Ibn Maryam atawashukia, na hivyo Imam wao huyo atarudi nyuma na kumwambia Isa Ibn Maryam: 'Isa Ibn Maryam sogea mbele ili upate kuwasalisha watu'**

Lakini Isa Ibn Maryam ataiweka mikono yake miwili juu ya mabega ya Imam huyo na kumwambia: 'Sogea mbele wewe usalishe kwani Iqamah imekimiwa kwa ajili yako wewe' na hivyo Imam huyo atawaongoza watu hao katika Sala hio na kisha baada ya Sala basi Isa Ibn Maryam atasema: 'Fungueni Mlango wa Bayt Al Maqdis'

Hivyo Watu watafungua Lango hilo na hivyo watakutana Dajjal akiwa na wafuasi wake 70,000 ambao ni Mayahudi, na kila mmoja miongoni mwa atakua na Panga kubwa na Joho la rangi ya Kijani. Na mara tu baada ya Dajjal kumuona Isa Ibn Maryam basi ataanza kua ni mwenye kuanza kuyeyuka kama vile Theluji inavyoyeyuka kwenye Jua. Na hivyo kuanza kutafunta njia ya kukimbilia na kukimbia lakini Isa Ibn Maryam atasema: 'Hakika mimi nina kipigo kimoja tu kwa jili yako ambacho kamwe hutoweza kukikwepa'

Na hivyo atamfukuzia na kumkamatia kwenye Lango la Ludd na kisha atamuua, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawasababishia Mayahudi kushindwa, na hivyo itakua hkanua hata kitu kimoja ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amaekiumba ambacho hakitoweza kumfichua Yahudi aliejificha Nyuma yake. Kwani Allah Subhanah wa Ta'ala atavijaalia vitu hivyo kua ni vyenye kusema, hivyo hakuna Jiwe, wala Mti wala Mnyama, isipokua Al Gharqad ambao ni Mti wao Mayahudi na hivyo hautoweza kusema, hivyo vitu vyengine vyote vitasema: 'Ewe Muislam, Ewe Mja wa Allah, hapa kuna Myahudi amejificha njoo umuue''

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Dajjal ataishi kwa mda wa miaka 40, ambapo Mwaka utakua sawa na Nusu Mwaka, Mwaka utakua kama Mwezi, na mwezi utakua kama Wiki, na siku nyenginezo itakua kama cheche za moto zitakavyotoweka. Na miongoni mwenu ataingia kwenye Milango ya Mji wa Madina asubuhi na hatolifikia geti lake jengine la upande wa pili hadi jioni yake.'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaulizwa: Ya Rasul Allah hivi jee tutasali vipi katika siku kama hizo na udogo wake?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: ‘ Mtakisia nyakati za Sala za siku hizo kama vile mtakavyokua mkikisia katika nyakati za Sala za Siku za Kawaida na kisha mtasali.’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akaendelea kusema kua: ‘Isa Ibn Maryam atakua ni Qadhi Muadilifu na Khalifa Muadilifu miongoni mwa Watu wa Ummah wangu, ataivunja Misalaba, atawaua Nguruwe, ataondoa Kodi na itakua kuna Sadaqah tu, kiasi ya kua hakuna takaechaguliwa kukusanya Zakkah ya Kondoo na Ngamia, Vinyongo na Chuki vitatoweka miongoni mwa watu na sumu ya kila aina ya Mnyama mwenye Sumu itatoweka ndani yake.**

Kiasi ya kua Mtoto awa kiume takua akimchukua Nyoka mikononi mwake na kutodhurika kutokana nae, Mtoto wa kike atakabiliana na Simba na Simba atakimbia bila ya kumdhuru na Mbwa Mwitu atakua pamoja na Kondoo kama Mbwa mwenye kuwalinda dhidi ya maadui zao. Dunia itakua ni yenye kujaa Usalama kama vile chombo kinavyojaa Maji na watu wataungana pamoja na itakua hakuna anaeabudiwa isipokua *Allah Subhanah wa Ta’ala’*

Itakua hakuna Vita na watu wa Quraysh watakua hawana Mamlaka, Ardhi itakua kama sahani ya fedha na mazao yataona juu yake kama vile yalivyokua yakiota katika wakati wa mwanzo alioishi Adam, kiasi ya kufikia kua watu watakusanyika chini ya Mzabibu na Kula kikonyo kimoja ambacho kitawatosheleza. Na watakusanyika watu mbele Gamba la Komamanga na litawatosheleza watu kadhaa kujifunika, Fahali wa Ng’ombe atauzwa kwa bei ya juu sana na Farasi atauzwa kwa Dirham chache sana.

Masahaba wakauliza: ‘Ya Rasul Allah hivi kwanini Farasi watakua Rahisi sana?’ ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akajibu: ‘Kwa sababu watakua hawatumiki kwa ajili ya kupigana vitani’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akaulizwa tena: ‘Na kwanini Ng’ombe watakua Ghali sana?’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akajibu**: ‘Kwa sababu watakua wanatumika katika kulimia ardhini, kwani kabla ya kutokea kwa Dajjal basi itatokea miaka mitatu ambayo itakua migumu sana kwa ukame, ambapo katika mwaka wa mwanzo basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* ataiamrisha Mbingu kuzuia sehemu tatu ya Mvua yake na ardhi kuzuia sehemu tatu ya mazao yake. Katika mwaka wa pili *Allah Subhanah wa Ta’ala* ataiamrisha Mbingu kuzuia sehemu mbili kati ya tatu ya mvua yake na Ardhi izuie sehemu mbili kati ya tatu za Mazao yake. Na katika mwaka wa tatu ataiamrisha Mbingu kuzuia Mvua yake yote na hivyo halitomwagika hata tone moja la maji na ardhi kuzuia mazao yake na hivyo hakuna kitakachoota hata kimoja, na hivyo Wanyama wote wenye kwato watafariki isipokua wale ambao *Allah Subhanah wa Ta’al*a hatowajaalia kua wafe’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akaulizwa: ‘Jee watau wataishi kwa kula nini katika wakati huo?’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema kua: ‘Watu wataishi kwa Tahlil, Takbir na Tahmid ambazo ndio itakua ndio yenye kuwashibisha’**

Ambapo anasema Imam Abu Abdullah Ibn Majah kua: ‘Mimi nimemsikia Abu Al Hasan Tanasifi akasema kua amesema Abd Rahman Al Muharibi kua: ‘Hadith hii inatakiwa ipelekwe kwa Mwalimu anaesomesha ili awasomeshe watoto.’*(Imam Ibn Majah)*

Na amesema Ubadah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu* kua: **‘Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua: ‘Kwa hakika mimi nimekuelezeeni mengi kuhusiana na Dajjal na nna khofu kua hamtofahamu, lakini kwa hakika Dajjal atakua ni Mtu Mfupi, mwenye Matege, Nywele zilizosokotana, na Jicho moja lisiloona ambalo halikutokeza nje wala halikuzama, na kama mkichanganyikiwa juu yake basi fahamuni kua Mola wenu hana Jicho Moja.’’***(Jamii Saghir. Imam Daud)*

Na amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam amesema kua: **‘Wakati nilipokua nikifanya Tawaf kuzugka Al Kaabah, basi niliona Mtu mmoja akiwa ni mwenye rangi ya Kiza na nywele zilizonyooka, akiwa amesimama baina ya Watu wawili hukua akiwa anatirikwa kidogo kidogo na maji, hivyo nikauliza: ‘Huyu ndio nani?’ Watu hao wakasema: ‘Huyu ndio Isa Ibn Maryam’ na kisha nikageuka upande wa pili na nikamuona mtu mwenye rangi ya kiza akiwa na mwili uliojaza, na nywele zilizosokotana akiwa na chongo katika jicho lake la kulia ambalo linaonekana kama Zabibu iliyotisika na hivyo nikauliza: ‘Huyu ndio nani?’ Nami nikaambiwa kua: ‘Huyu Ndio Dajjal’ na Mtu huyo alikua akifanana na Ibn Qatan’’** *(Imam Bukhari; Ibn Qatan alikua ni mmoja kati ya watu wa Kabila la Banu Mustalaq)’’*

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: ***‘Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alisema kua: ‘Ama kuhusiana na Dajjal basi atakua ni mwenye kuona Jicho moja, atakua na paji la uso ambalo ni pana na kifua kipana na atakua na kibyongo’*(Musnad Imam Ahmad)’***

Na ingawa kuna Hadith ambazo zinasema kua Dajjal atakua haoni katika Jicho la Kushoto na nyengine zinasema kua haoni katika Jicho la Kulia kutokana na kua na Kasoro au chongo kwenye Jicho hilo, basi anasema Qadhi Al Iyad kua: ‘**Macho yake yote mawili Dajjal yatakua ni yenye kasoro, na hii ni kwa sababu hadithi zote zilizozungumzia juu ya hili ni Sahih. Ambapo hadith ya kwanza inayosema kua Jicho lake la Kulia litakua ni Mamsuh na Limetisika na hatoweza kuona na pia kama ilivyoelezewa kwenye Hadith ya Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua Jicho la Dajjal la kushoto lityakua limefunikwa na mkunjo wa ngozi na litakua na kasoro, na kwa maana hio basi Dajjal atakua na kasoro katika Macho yake yote mawili Kushoto na Kulia.**

Na hii ni kwa sababu neno lililotumika katika hadith ni Awar ambalo hua linatumika kuelezea kitu chochote kile chenye kasoro hususan matu anapokua na makengeza, na hivyo Jicho moja hua linafanya kazin a jengine halifanyi kazi’

Na amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **‘Dajjal atakuja kwenye bwawa la Marriqanat na wengi miongoni mwa watakomfuata watakua ni Wanawake, kiasi ya kua itafikai hali ya kua Mtu ataenda Nyumbani kwake na kuwafungia Mama mkwe wake, Mama Yake, Mabinti zae, Madada zake, Mashangazi na kuwafunga kamba kwa kukhofia kua wasije wakatoka nje kwa ajili ya kumfuata Dajjal’***(Musnad Imam Ahmad)*

Na tunaporudi katika kipindi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo tunaona kua katika wakati wa Kipindi hiki cha Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, wakati alipohamia katika Mji wa Madina basi katika Mji huo kulikua na Mtoto wa Kiume ambae alikua ni Myahudi.

Mtoto huyo alikua na sifa za kipekee, kwani mbali ya kua ni mtoto lakini alikua akikuangalia tu wewe Mtu mzima basi alikua na uwezo wa kujua unachofikiria.

Hivyo baada ya kupata habari za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Mtoto huyo akaanza kumchukia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kutokana na kua na sifa yake hio basi Mtoto huyo aliekua akiitwa Safi Ibn Sayyad basi Watu wa Mji wa Madina waliposikia kuhusiana na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Dajjal basi nao hapo hapo hawakufikiria mara 2 wala 3 bali walifikiria moja kwa moja kua Saafi Ibn Sayyad ndio Dajjal mwenyewe.

Kwani baada ya kuzuka kwa Uvumi huo wa kua Katika Mji wa Madina kuna Mtoto ambae inawezekana ikawa ndio Dajjal mwenyewe na habari kuenea basi haikuchukua mda isipokua habari zikamfikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamua kutoka yeye huku akiaa ni mwenye kufuatana na Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kwa ajili ya Kuchunguza kuhusiana na uvumi huo ulioenea Mjini Madina. Hivyo baada ya kuchunguza wakasikia kua Mtoto huyo yuko sehemu fulani anacheza na wenzake katika wakati huo.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pamoja na Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* wakaelekea katika maeneo hayo, na walipofika basi Wakamuona Mtoto huyo akizungumza na kucheza na wenzake.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Umar Ibn Al Khattab *Radhi Alahu Anhu* wakanyatia katika sehemu hio anayocheza ili waweze kufika karibu yake ili wasikie anazungumzia kuhusiana na nini na wenzake hao.

Katika Kunyatia kwao, mara akatokea Mama wa Mtoto huyo, ambae alimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na hivyo akasema kwa sauti Muhammad huyo yuko mbele yako! Hivyo Saafi akanyanyua kichwa na kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha hapo hapo akakunja Uso wake huku akifumba mdomo wake.

Na anasema Abd Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Umar Ibn Al Khattab alitoka na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kwa ajili ya kumtafuta Ibn Sayyad Na wakamkuta akiwa anacheza na Watoto wenzake katika maeno ya Banu Maghalah, ambapo katika kipindi hicho Ibn Sayyad alikua anakaribia baleghe Na Ibn Sayyad hakuhisi kitu hadi pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipompiga Mgongoni mwake na kisha akamwambia Ibn Sayyad.'**

'Hivi Jee Unashuhudia kua mimi ni *Rasul Allah?'*

Ambapo Ibn Sayyad akajibu: '**Naam..Nnashuhudia kua wewe ni Mtume wa Ummah ambao haujasoma.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akamuuliza tena: **'Jee Unaamini kua Mimi ni *Rasul Allah?'***

Ambapo Ibn Sayyad akajibu: '**Hakika Mimi namuamini Allah na Mitume wake.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akaumuuliza Ibn Sayyad: **'Hivi Jee Unaona nini?'**

Ibn Sayyad akajibu: '**Baadhi ya wakati nnaona Watu wakweli wanakuja kwangu na baadhi ya wakati wananifuata watu waongo.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Inaonekana kua baadhi ya Wakati kama unakua unachanganyikiwa.'**

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: **'Hakika mimi kuna kitu sijakibainisha'**

Ibn Sayyad akajibu: '**Ni Dukh – Moshi'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Hakika wewe hutovuka zaid ya Darja yako uliwekewa uifikie**

Ambapo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Ya Rasul Allah! Jee Nimkate Kichwa chake?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Kama kweli huyu ndie Dajjal basi kamwe hutoweza kumzidi nguvu, na kama sie basi kumuua kwako hakutosaidia kitu'**

Kwani Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **'Baadae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Ubbay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* wakatoka na kuenda kwenye sehemu yenye Mitende.'**

Ambayo Ibn Sayyad alikua amekaa. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa amejificha kwenye Mitende ili asikie anachokizungumza Ibn Sayyad kabla ya Ibn Sayyad kumuona Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'

Na Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuona Ibn Sayyad akiwa amejifunika Guo huku ndani yake mnasikika maneno yasiyoeleweka. Na mara akatokea Mama yake ambae akamuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema: Ewe Saaf! Muhammad huyo!

Na hapo hapo Ibn Sayyad akashtuka.

Ambapo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu anhu* anasema kua: **Kama Mama yake Ibn Sayyad hakumshtua Ibn Sayyad basi hali ingekua wazi***(Imam Al Bukhari)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqalani kuhusiana na Hadith hii kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Alijaribu kumchunguza Ibn Sayyad, lakini hakutoa Hukmu juu yake kama alikua Dajjal ama la na hii ni kwa sababu alikua hakushushiwa Wahyi juu yake. Mbali ya kua Masahaba kadhaa walikua wakidhani kua Saaf Ibn Sayyad ndio Dajjal mwenyewe'**

Ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Munqadir kua: **'Nilimuona Jabir Ibn Abd Allah akiapa kua Ibn Sayyad ni Dajjal, nami nikawambia Unaweza kuapa?**

Ambapo nae akasema: '**Nimemsikia Mimi Umar Ibn Al Khattab Akiapa juu ya hilo mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakukubaliana nalo hilo***(Imam Al Bukhari)*

Na Mbali ya Kua Saafi alikua ni Kijana Myahudi anaemchukia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alikua akifananishwa na Dajjal kutokana na Sifa zake lakini hata hivyo baadae *Allah*

Subhanah wa Ta'ala alimtia Nuru ndani ya Moyo wake na hivyo akaingia kwenye Dini ya Kiislam. Na alioa na kupata watoto 10. Na alikua na mtihani mkubwa sana wa kuwathibitishia Masahaba kua yeye si Dajjal na wala hana uhusiano na Dajjal.

Kwani anasema Abu Said Al Khudri kua : '**Sisi tulitoka kwa ajiliya Safari ya Umra au Hajj huku Ibn Sayyad akiwa pamoja nasi. Na kisha Njiani Tukapiga Kambi, na kisha watu wakatawanyika kutoka Kambini hapo nami nikajikuta nimebakia mimi peke yangu na Ibn Sayyad. Hivyo nikakosa Utulivu na kua na khofu kubwa sana kwa sababu ya Kumuogopa Ibn Sayyad kutokana na kile kinacho zungumziwa juu yake Na mara Ibn Sayyad akachukua mizigo yake na akaja kukaa chini yangu na kuiweka mizigo yake pamoja na mizigo yangu'**

Nami Nikasema: '**Hivi kwanini wewe unaweka mizigo yako karibu yangu hujui kua hali ya hewa ni ya Joto? Hivyo kwanini usiweke Mizigo yako chini ya Mti?'**

Na hivyo Ibn Sayyad akafanya kama nilivyomwambia. Mara wakaja Kondoo mbele yetu, na Ibn Sayyad akaenda kuchukua chombo cha Maziwa na kuniletea huku akisema: '**Kunywa Ewe Abu Said'**

Nami nikasema '**Hali ya hewa ni Joto na maziwa pia ya moto.'**

Abu Said Al Khudhri anasema kua: '**Mimi nilikua najiambia ndani ya Moyo wangu kua tatizo ni kua mimi sitaki kunywa kitu chochote kutoka kwako ewe Ibn Sayyad'**

Ambapo Ibn Sayyad akasema: '**Unajua Ewe Abu Said, mimi nilikua na nia ya Kuifunga kwenye Mti na kisha nijinyonge kutokana na Wanayoyasema Watu Juu yangu**. **Ila Abu Said hebu niambie Hivi Jee kuna Mtu ambae ni mwenye kujua Ilm ya Hadith zaid yako Ansari wewe? Jee wewe si mmoja kati ya Watu wanaojua zaid Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*? Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakusema kua Dajjal atakua ni Kafiri? Wakati mimi ni Muislam? Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakusema kua Dajjal atakua hana uwezo wa Kupata Watoto, wakati mimi nnao ambao nimewaacha Madina? Hivi Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakusema kua Dajjal hatoingia katika Mji wa Madina wala Makkah? Au kua Hatoelekea katika Mji wa Madina wala Makkah?'**

Abu Said Al Khudhri anaendelea kusema kua: **'Mimi nilikua nataka Kukubali maneno yake lakini mara akasema: Wa Allahi Mimi nnajua ni nani Dajjal na najua Wapi alipo Dajjal Sasa hivi.'**

Abu Said Al Khudhry anaendelea kusema kua: '**Nami nikawambia, Na uangamie *Milele'*** *(Sahih Muslim)*

Naam..tumalizie kuhusiana na kisa cha Saaf Ibn Sayyad ambapo tunapoangalia zaid basi tunaona kua baada ya kufariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kulitokea vita pale baadhi ya Viongozi wa Miji ya Waislam walipoanza nao Kujitangazia kua nao ni Mitume na hivyo yakatokea mapigano makubwa sana katika wakati wa Mamlaka ya *Amir ul Muuminin* Abu Baqr Al Siddiq *Radhi Allahu Anhu* dhidi ya Mitume hao hao waliokua wakijitangazia Utume.

Na miongoni mwa mapigano mazito aliyoyaongoza Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* katika kipindi cha Utawala wa *Amir ul Muumin* Abu Bakr Al Sadiq *Radhi Allahu Anhu* katika vita vya Mitume hao feki basi moja wapo ilikua katika Vita dhidi ya Musallimah Al Kadhdhab ambae nae pia alikua akijiita kwa ni Mtume.

Na katika mapigano haya basi Saaf ibn Sayyad nae alikuwemo miongoni mwa wapiganaji wa Jeshi la Kiislam yeye na Familia yake yote. Na ingawa Waislam walishinda vita hivi lakini hata hivyo Waislam wengi walifariki pia ikiwemo Familia nzima ya Saaf Ibn Sayyad.

Ila Jambo la kushangaza ni kua mbali ya kua watu wote wa Familia yake Saaf Ibn Sayyad walifariki na miili yao ilionekana lakini Mwili wa Saaf ibm Sayyad haukuonekana kabisa. Yaani ilikua hakuonekana kua yuko hai na Waislam wengine wala hakuonekana akiwa ni miongoni mwa maiti hata baada ya kutafutwa mara kadhaa.
Hivyo kama ilivyokua kua kuna kutokua na uwazi na uhakika halisi tunapozungumzia kuhusiana na Dajjal, basi ndio pia ilivyokua kuna kutokua na uhakika halisi kuhusiana na Saaf Ibn Sayyad kua ndie Dajjal ama la. Na kutokana na kutokua na uhakika huo basi ndio tunaona kua Wanazuoni wametofautiana sana kuhusiana na kama kweli Saaf alikua ni Dajjal ama la.

Kwani kuna wasemao kua Saaf Ibn Sayyad ndie Dajjal mwenyewe na hii ni kulingana na vithibitisho vya Hadith.

Na kuna wasemao kua la Saaf Ibn Sayyad ni mwengine na Dajjal ni mwengine na hii ni kutokana na kutokuthibitishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama tulivyoona hapo kabla kwenye Hadith.

Ambapo kwa upande mwengine basi katika Sahih Muslim kuna Hadith ya Fatma Bint Qais *Radhi Allahu Anha* ambayo inasema kua: **‘Mimi nilisikia sauti ya Muadhini, Muadhini wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Ikisema *Alsalaatu Jaamia* (Mkusanyiko wa Sala) na hivyo nikatoka na kuelekea Msikitini na nikasalia na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku nikiwa kwenye Safu ya Wanawake iliyokua karibu na Wanaume, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomaliza Kusali, akapanda kwenye Minbar na kukaa kitako na akawa ni mwenye kutabasamu huku akisema: ‘Wacha Kila Mtu abakie katika sehemu yake aliyosalia’ na kisha akauliza: ‘Hivi Jee mnajua kwanini nimekuiteni?’**

Masahaba wakajibu: ‘Allah na Mtume wake ndie mwenye kujua zaidi’

Ambapo nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Wa Allahi, mimi sijakuiteni nyinyi kwa kukukaripieni wala kukuonyeni, bali nimekuiteni kwa sababu ya Tamim Ad Dari ambae alikua ni Mkristo na amekuja kwa ajili ya kukubali kujiunga nasi n a kua Muislam na ameniambia kitu ambacho kinakubaliana na kile nilichukua nikuambieni kuhusiana na Dajjal’

‘Ameniambia kua alikua safarini baharini Pamoja na watu 30 wa Lakhm na Judhaam, na walipigwa na Mawimbi kwa mda wa mwezi, na kisha wakajikuta wako kwenye kisiwa katika wakati wa Magharibi. Hivyo wakaingia kwenye Mashua ndogo ndogo na kufikia kisiwani hapo, na wakakutana na Mtu mkubwa sana ambae alikua amejaa nywele mwili mzima kiasi ya kua hawakuweza kutofautisha baina ya Uso wake na mgongo wake. Hivyo wakasema: ‘Ole wako, hivi wewe ndio nani?’’

Mtu huyo nae akajibu: ‘Mimi ni Jassaasah’ nao wakamuuliza: ‘Jassaasa ndio nani?’ nae akasema: ‘Enyi watu nendeni kwenye hili Jumba la Makasisi kwani kuna mtu ambae ana hamu sana ya kuonana nanyi’ ambapo Tamim anasema kua: ‘Aliposema kuhusiana na mtu basi sisi tukaingiwa na khofu, kua huyu tunaezeungumza nae asije akawa ni Shaytan’ hivyo tukakimbilia katika Jumba hilo, na ndani yake tukakutana na Mtu mkubwa sana kimaumbile ambae sisi hatujawahi kuona ukubwa kama wake hapo kabla.

Mtu huyo alikua amefungwa minyororo iliyokazwa huku mikono yake ikiwa shingoni mwake na miguu yake imefungwa kuanzia magotini na visiginoni kwa minyororo ya chuma, Nao wakasema‘Ole wako hivi wewe ni nani?’

Ambapo nae akasema: ‘Karibuni tu mtajua kua mimi ni nani, ila kwanza semeni nyinyi ni nani?’

Nao wakasema‘Sisi ni watu kutokea katika maeneo ya Uarabuni ambao tulikua safarini baharini, lakini Bahari ikachafuka na kupigwa na mawimbi na hivyo tukajikuta kwenye hii kisiwa chenu, tukachukua mashua zetu na kutua katika ufukwe wa kisiwa hikina tukakutana na Mdudu ambae hatukuweza kutofautisha baina ya Uso wake na Mgongo wake kwani alikua na Nywele nyingi sana, nasi tukamwambia: ‘Ole wako wewe hivi wewe ni nani?’ ambapo nae akasema kua yeye ni Jassaaas’, tukamuuliza Jassaaas ndio nani? Na yeye akasema: ‘Nendeni kwenye hili Jumba kuna mtu anahamu sana ya kujua kuhusiana nanyi. Hivyo sisi tukakimbilia kwako huku tukimkimbia yeye kwa sababu hatukujua Mdudu yule alikua ni Shaytan ama la.’

Yule Mtu aliefungwa akasema: ‘Hebu niambieni kuhusiana na Mitende ya Baysaan’

Nao wakasema‘Unataka kujua nini juu yake?’

Ambapo nae akasema: ‘Nakuulizeni kama Hii Mitende bado inendelea kuzaa ama la?’

Nao wakasema‘Naam Inazaa’

Nae akasema: ‘Karibuni tu itakua haizai tena Tende.’ Kisha akasema: ‘Niambieni kuhusiana na lile Ziwa la Tabarriyah’

Nao wakauliza: ‘Hivi jee unataka kujua nini juu yake?’

Nae akasema: ‘Jee mna Maji Ndani yake?’ Nao wakasema: ‘Ndio mna mjai mengi sana’

Ambapo nae akasema: ‘Karibuni tu litakauka’ kisha akasema: ‘Niambieni kuhusiana na Chemchem ya Zughar (ambayo ipo kusini mwa ardhi ya nchi ya Syria)’ Nao wakasema: ‘Unataka kujua nini juu yake?’

Ambapo nae akasema: ‘Jee kuna Maji ndani yake na watu wanapande mashamba yao kutokana na maji yake?’ Nao wakasema: ‘Naam Kuna Maji ndani yake na watu wanayatumia maji hayo kwa ajili ya mashamba yao’

Ambapo nae akasema: ‘Niambieni kuhusiana na Mtume wa Ummah usiojua kusoma, amefanya nini?’ nao wakasema: ‘Amehama kutoka katika Mji wa Makkah na amehamia katika Mji wa Madina’

Ambapo nae akauliza: ‘Hivi Jee Waarabu washaanza kupigana nae?’ Nao wakasema : ‘Naam’ nae akauliza: ‘Jee amewashugulikiaje?’

Nao wakajibu: ‘Amewashinda Waarabu katika maeneo yake na wameonesha Utiifu juu yake’ nao akauliza: ‘Hivi kwelilimetokea hilo?’ nao wakasema: ‘Naam’

Ambapo nae akasema: ‘Kama wamekubaliana nae basi hilo ni jambo bora kwao. Na hivyo sasa hivi nitakuambie kuhusiana na mimi mwenyewe. Mimi ndie Dajja na karibuni nitapewa ruhusa ya kua huru, na nitatoka na kutembea katika kila sehemu ardhini na sitoucha hata mji

mmoja isipokua nitakaa ndani yake siku 40. Isipokua katika Mji wa Makkah na Taybah (Madina) kwnai imeharamishwa kwangu mie. Na hivyo kila wakati nitakapojaribu kuingia ndani yake basi nitakabiliana na Malaika mwenye Upanga na kunizuia na kila njia ya kuingilia itakua ni yenye kua chini ya Ulinzi wa Malaika'

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaipiga Mimbar kwa fimbo yake na kisha akasema: 'Hii ni Taybah, hii ni Taybah, hii ni Taybah (Madina)' kisha akasema: 'Hivi Jee sikukwambieni mimi kuhusiana na haya hapo kabla?' Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Hakika mimi nimekipenda kisa cha Tamim kwa sababu kinakubaliana na yale niliyokua nikuambieni kuhusiana na Makkah na Madina kuhusiana nae, lakini yeye yuko kwenye Bahari ya Syria, au Bahari ya Yemen, lakini yuko Mashariki, yuko Mashariki, yuko Mashariki.' Ambapo Imam A Tirmidhi amesema katika Jamii Sahihi yake kuhusiana na Hadith hii kua ni Hadith Sahihi Gharib. Ambapo Imam Ibn Abd Al Barr amesema katika kitabu chake cha Al Istidhkar kua hii ni Hadith Sahih katika Sanad zake.

Ambapo tunapomzungumzia Tamim Ad *Dari Radhi Allahu Anhu* basi tunamzungumzia mtu ambae alikua ni Mwanazuoni wa Dini ya Kikristo wa ardhi ya Mji wa Falestina. Na alienda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mnamo mwaka wa 9 Al Hijra Pamoja na wajumbe wengine wa Kiksristo na wakawa Muislam baada ya tukio hili, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza kama wanataka kitu chochote kile ili waupende zaidi Uislam.

Hivyo Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* akazungumza na wenzake na kisha wakasema kua wanataka wawe Viongozi wa Maeneo ya Mji wa Hebron, Mertum na Halil Rahman karibu na Jerusalem. Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaambia watu hao kua Maamuzi waliyoyachukua ni yenye Miujiza ndani yake. Na hivyo hii ikawaongezea Imani ndani ya zao.

Kisha Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* na wenzake hao wakabakia Madina huku wakiendelea kujifunza Imani yao mpya ya Dini ya Kiislam chini *ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo miongoni mwa Hadith alizonukuu ni pamoja na ile isemayo kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: 'Kwa hakika Uislam utafikia katika kila sehemu yenye Usiku na Mchana,kwani *Allah Subhnah wa Ta'ala* hatoiwacha sehemu hata moja ya Hema ambayo Uislam hautofika ndani yake, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaheshimisha wale wanaotaka kuheshimika kutokana na Dini na atawadhalilisha wale wanaotaka kudhahalilishwa nayo.'**

Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* alikua akifanya biashara ya Kununua Mishumaa na mafuta ya Zaitun kutoka katika Mji wa Dimashq na kuuza katika Mji wa Madina. Ambapo siku moja Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* alimwamrisha Mfanyakazi wake achukue Mishumaa hio kisha akaiwashe Msikitini pale kitakapoingia kiza, na mfanykazi huyo akafanya hivyo.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alipoona Misikiti unang'ara kwa mwangaza wa Mishumaa basi akauliza**: 'Hivi Jee ni Nani aliefanya hivi?'** na alipoambiwa kua ni Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kumwambia Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu:* **'Hakika wewe Umeunawirisha Uislam na kuupendezesha Msikiti hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akung'arishe na wewe hapa Duniani na kesho Akhera pia'** na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: **'Hakika mimi kama ningekua na Mtoto wa Kike basi Ningekuozesha.'**

Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* aliendelea kuishi Madina Pamoja na wenzake hadi pale alipofariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku akiwa ni mwenye kuwaandikia kua wawe ni wenye kupewa Ngamia 100 waliojaza Magunia ya Tende kutokana na Kodi ya ardhi ya Khaybar.

Mji wa Jerusalem ulipotekwa chini ya Uongozi wa *Amir Ul Muuminin* Abu Bakr Al Saddiq *Radhi Allahu Anhu* na chini ya Majemedari wake wakuu wa kijeshi Khalid Ibn *Walid Radhi Allahu Anhu* na Abu Ubayda Ibn Jarrah *Radhi Allahu Anhu* basi *Amir Ul Muuminin* Abu Bakr Al Saddiq *Radhi Allahu Anhu* akatekeleza Maamrisho ya *Rasul Allah Salallahu Alyhi wa Salam* na kukabidhi Miji hio chini ya uongozi wa Familia ya Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu.* Tamim Ad Dari *Radhi Allahu Anhu* alifariki katika ardhi ya Dimashq nchini Syria.

Tunaporudi kwenye Kisa chetu cha Dajjal basi tunaona kua kuna Wanazuoni ambapo miongoni mwao akiwemo *Mujaddid Ad Din* Imam Ibn Hajjar Al Asqalani wanaosema kua Saaf Ibn Sayyad anaweza akawa ni Shaytan ambae alijitokeza katika Muonekano wa Dajjal na kisha akatoweka na kujificha hadi utakapowadia mda wa kujitokeza kwake. Na Dajjal ndio yule alieonekana na Tamim Ad Dari *Radi Allahu Anhu* na wenzake akiwa Amefungwa Minyororo.

Naam, huo tumeangalia Mfano wa kisa cha Dajjal katika kujaribu kuoneshana namna Masahaba na waliotangulia kabla yetu walivyokua makini katika kufuatilia na kushikamana na yale waliyoambiwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kiasi ya kua walikua wakikhofiana sana kutokana na kufanana tu kitabia na mtu walieonywa kuhusiana nae Mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwenyewe hakua ni mwenye kuweka wazi juu ya jambo husika.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametuhimiza kuomba Dua ndani ya Sala baada ya Attahiyat ya Mwisho kwa ajili ya mtihani wa Ad Dajjal kama inavyosema Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* kua:

‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua ndani ya Sala yake kwa kusema: ‘Allahumma inni a’udhu bika min ‘adhab al-qabri, wa a'udhu bika min fitnat il-masih il-dajjal, wa a’idhu bika min fitnat il-mahya wa fitnat il-mamat. Allahumma inni a’udhu bika min al-matham wa’l-maghram (yaani Ya Allah naomba Hifadhi yako kutokana na Adhabu ya Kaburi, Kutokana na Mtifani wa Dajjal, Kutokana na Mitihani ya Uhai na Mitihani ya kIfo na naomba hifadhi yako kutokana na Mitihani ya Dhambi na Madeni’ *(Sahih Bukhari)*

YAJUJ WA MAJUJ

Na hivyo tunaporudi katika kisa chetu cha Dhu Al Qarnayn basi tunaweza kuona wazi ni kwa sababu gani Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kuhusiana na Juj wa Majuj kua: **Juj wa Majuj wamegawika katika Makabila 21. Na Dhu Al Qarnayn aliyafungia Makabila yao 20 ndani ya Ukuta alioujenga na hivyo Kabila moja miongoni mwa Kabila moja miongoni mwa hayo 21 Limebakia nje ya Ukuta huo, Na Kabila hilo Moja lililobakia Nje ya Ukuta huo wameitwa Turkik kwa sababu ya kua ni Walioachwa Nje ya Ukuta. Kwani Neno Turkik linatokana na neno Turku la Kiarabu ambalo linamaanisha Kuachiwa.’**

Na tukasema kua huo ni Mtizamo tu na hivyo hatusemi kua Waturuki ndio Moja kati ya Kabila hilo la watu walioachwa Nje na wala haimaanishi hivyo na tukasema kua nasema hivyo kwa sababu kwanza Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi ambae tulisema katika Historia ya Maisha yake kua alikua ni Imam Kipofu lakini ni Mwenye Ufaham wa kutisha sana.

Kwa hivyo Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi alifafanua maana ya neno kulingana na Mzizi wa Neno Husika kama ilivyo Lugha ya Kiarabu kua Kila neno lina Herufi husika ambazo hua ndio Mzizi

wa Neno au Jina Husika. Nadhani itakua tumefahamiana kwa namna gani Waliotangulia walivyokua na Tahadhari katika upande wa kiimani Ucha Mungu wao.

Aya zetu zinaendelea kusema kua baada ya Dhu Al Qarnayn kuonana na watu hao wasiojua Lugha basi ilikua kama ifuatavyo:

﴿قَالُواْ يٰذَا ٱلْقَرْنَيْنِ إِنَّ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ مُفْسِدُونَ فِى ٱلأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ خَرْجاً عَلَىٰ أَن تَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ سَدّاً﴾

Qaloo ya Dha alqarnayni inna ya/jooja wama/jooja mufsidoona fee al-ardhi fahal najAAalu laka kharjan AAala an tajAAala baynana wabaynahum saddan *(Surat Al Kahf 18:94)*

Tafsir: ***Wakasema Ewe Dhu Al Qarnayn Hakika ya Majuj na Majuj Wanatufisidi Katika Ardhi Hivyo Jee Tukujaalie au Tukupe wewe Zawadi Kwa Ajili ya Kujaalia bBaina Yetu na baina yao Ukuta? .***

Na kwa upande mwengine basi tunapoiangalia Qur'an basi tunaona kua imewazungumzia viumbe hawa wanaojulikana kama Yajuj wa Majuj mara mbili tu, ambapo mara ya kwanza katika aya hii na kisha mara ya pili katika aya ya Surat Al Anbiyah ambayo ni hii ifuatayo

﴿ حَتَّىٰٓ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُم مِّن كُلِّ حَدَبٍ يَنسِلُونَ﴾

Hatta idha futihat ya/jooju wama/jooju wahum min kulli hadabin yansiloona *(SuratAl Anbiyah 21:96)*

Tafsir: ***Hadi Pale Watakapoachiwa Yajuuj wa Majuuj Ambapo Nao Na Katika Kila Kilima watatoka ndani yake kwa kasi kubwa sana***

Subhanah Allah..angalia namna aya hii inavuowazungumzia Yajuj wa Majuj kwa Namna watakavyotoka kwa kasi kubwa sana pale watakapoachiwa huru. Ambapo anasema Mujaddid Ad Din, Sultan Al Mutakalimin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: **'Inasemekana kua Katika wakati watakapotoka Katika sehemu Waliyofungiwa Yajuj wa Majuj basi Idadi yao itakua ni kulingana na Idadi ya watu wa wakati huo yaani kama wakiwa watu ni 10 basi Yajuj wa Majuj watakua ni 9.'**

Ambapo kwa mtizamo huu basi tunaona kua hawa Jamaa wakitoka basi wakivamia sehemu hakuna kitakachobakia kwa wingi wao na kasi yao. Na bila ya shaka hakuna Uthibitisho hawa Jamaa wamefungiwa wapi, kwani Jitihada za kuwatafuta na kujua ni wapi labda wakaripuliwe kwa Mabomu zimeshindikana.

Lakini kwa kua Qur'an imesema kua Watu wa Dhu Al Qarnayn wameomba wajengewe ukuta dhidi yao. Na kisha zikazungumzia namna kwa kasi watakavyotoka pale watakapoachiwa basi bila ya shaka hivi viumbe vipo na ni *Allah Subhanah wa Ta'aala* pekee ndie ajuae amewahifadhi wapi, lakini

iko siku atawaachia huru na ndio itakua ni miongoni mwa dalili za mwishoni za Dunia kama inavyosema Hadith Ambayo inapatikana katika Sahih Muslim na inasema:

'Siku Moja tulikua tumekaa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tukizungumzia kuhusiana na Siku ya Kiama Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: Kiama hakitowadia hadi pale mtakapoona Dalili 10 ambazo ni; Moshi, Dajjal, Mnyama, Kuchomoza kwa Jua kutoka Magharibi, Isa Ibn Maryam, Yajuj wa Majuj na Kubonyea mara 3 kwa Dunia, kwanza Mashariki, pili Magharibi na Tatu Mashariki ya kati na Moto utakaoanza Aden na kuwakusanya watu katika eneo la kufufuliwa.'

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atasema katika Siku ya Malipo: Adam!**

Na Adam atajibu : Ya Rabb Mimi Niko hapa chini ya Maamrisho yako na kila Kitu kizuri kiko mbele yako.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: Walete Mbele watu wa Motoni!

Na Adam atauliza kwa kusema: Ndio Wapi hao?

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: Kwa Kila miongoni mwa Watu 1000, basi wao ni watu 999.

Baada ya kusikia Maneno hayo basi Vijana watageuka na kua Wazee, na Kila Mwanamke mwenye Mimba basi ataharibu Mimba yake. Utawaona watu kama waliolewa, lakini hawakulewa, lakini hata hivyo Adhabu ya Allah ni Kali sana, na baada ya kusikia hayo basi Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakauliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah! Hivi Jee ni yupi miongoni mwetu atakua huyo mtu mmoja katika 1000 kama ikiwa katika kila watu 1000 basi watachukuliwa watu 999?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: 'Bebeni habari njema kwani kwa kila mmoja wenu basi Yajuj wa Majuj ni 999'***(Imam Bukhari)*

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Yajuj Wama Juj ni wenye kutokana na kizazi cha Adam, na kama wakiachiwa kuwafuata Ibn Adam basi watawafisidi kila kitu chao kimaisha, na hakuna hata mmoja miongoni mwao akifa isipokua atakua ni mwenye kuacha Watoto 1000 baada yake. Na kutokana nao basi kutakua na Mataifa matatu ambayo ni: Tawil, Taris na Mansak** *(Mustadrak Al Hakim)*

Ambapo amesema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Dunia imeumbwa katika sehemu 6 ambapo sehemu 5 kati yake ziko chini ya Yajuj wa Majuj.'**

Na amesema Imam Abu Amr Abd Raan Ibm Amr Al Awzai kua: **'Dunia imeumbwa katika sehemu 7, na sehemu 6 kati ya hizo basi ni zenye kua chini ya Yajuj Wamajuj.'**

Kwa upande mwengine tunapoangalia Historia ya Kiislam basi tunaona kua Imam Ibn Kathir anasema kua: **'Sultan Harun Ibn Muhammad Al Mutassim Ibn Harun Rashid aliefariki mnamo mwaka 232 Al Hijra alituma Jeshi lake likaitafute sehemu Waliyopo Yajuj Wamajuj. Hii ilikua ni safari ya miaka miwili na waliporudi basi wakasema kua Katika Upande wa meeneo ya**

Ardhi ya Kaskazini Mashariki walikuta Ukuta Mkubwa Sana wa Shaba na Chuma. Na Una Mafungio na Makufuli Makubwa sana, na hakuna alieweza kupanda Kufungua kutokana na Ukubwa wa Ukuta, Milango yake na Kufuli zake.'

Ambapo kwa upande wa Imam Sayyid Qutb basi yeye amesema kua: **'Kuna Ukuta umegunduliwa katika Makaburi ya Mji wa Tirmiz nchini Uzbekistan katika bara bara ya kuelekea Samarqand Hivyo inawezekana kua huo ndio Ukuta aliojenga Dhu Al Qarnayn'**

Hivyo inawezekana lakini hakuna mtu mwenye uhakika juu yake, hivyo sisi katika kufahamishana kuhusiana na Yajuj wa Majuj basi bado tutashikamana kuangalia kulingana na vigezo vya Hadith na mitizamo ya Wanazuoni waliotangulia kabla yetu. Kwani ingawa miongoni mwa Wanazuoni wa Karne yetu nao pia wamezungumzia kuhusiana nao kulingana na Mitizamo yao lakini, katika kuelezea kwangu basi mimi sitoangalia Mitizamo yao na hii ni kwa sababu tunapoangalia moja kati ya aya mbili zilizozungumzia kuhusiana na Viumbe hawa ambayo ni ile ya Surat Al Anbiyah isemayo:

﴿ حَتَّىٰٓ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُم مِّن كُلِّ حَدَبٍ يَنسِلُونَ﴾

Hatta idha futihat ya/jooju wama/jooju wahum min kulli hadabin yansiloona *(SuratAl Anbiyah 21:96)*

Tafsir: Hadi Pale Watakapoachiwa Yajuuj wa Majuuj Ambapo Nao Na Katika Kila Kilima watatoka ndani yake kwa kasi kubwa sana

Basi tunaona kua aya inayofuatia baada hii inasema kua:

﴿وَٱقْتَرَبَ ٱلْوَعْدُ ٱلْحَقُّ فَإِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ أَبْصَارُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ يٰوَيْلَنَا قَدْ كُنَّا فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَٰذَا بَلْ كُنَّا ظَالِمِينَ﴾

Waiqtaraba alwaAAdu alhaqqu fa-idha hiya shakhisatun absaru alladheena kafaroo ya waylana qad kunna fee ghaflatin min hadha bal kunna *dha*limeena *(SuratAl Anbiyah 21:97)*

Tafsir: ***Na Itakapokaribia Ahadi Ya Kweli (ya Siku ya Kiama) na kisha Utaona Mtizamo wa Khofu wa Macho Wa Wale waliokufuru ambao Watasema Ole wetu Kwa Hakika Tulikua kwenye Mghafiliko Juu ya Hili Na Tulikua Tuliojidhulum.***

Ambapo aya hii inazungumzia kuhusiana na hali itakavyokua katika siku ya Kiama na Kufufuliwa na kumaanisha kua Tukio hili la Yajuj wa Majuj ni tukio ambalo litatokea karibuni na mwishoni mwa Dunia.

Na sisemi kua Wanazuoni wa leo wametafsiri sivyo au mitazamo yao sio la, kwani hio ni Mitizamo yao na kusema kweli inaingia akilini kama ukiifuatilia. Lakini sasa kwangu mimi kama mimi hii hua ni kama *Conspiracy Theory* yaani Nadharia ya Kuaminisha Kitu Kisichojulikana lakini Kikaelezewa na Watu au Mtu kwa vithibitisho ambavyo ni vyenye nguvu kwa wale wenye kuvutiwa nacho Kitu hicho kutokana na kutaka kujua sana siri ya Kitu husika Kimtizamo.

Kwani nnasema hivyo kwa sababu katika Sahih Muslim kuna Hadith Sahih isemayo: **Amesema Nawwas Ibn Saman *Radhi Allahu Anhu* kua:**

Siku moja asubuhi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akizungumzia kuhusiana na Dajjal, na wakati alipokua akimuelezea basi aliainisha baadhi ya Sifa zake mbaya kimuonekano na pia akaelezea kuhusiana na baadhi ya Sifa zake ambazo zilituathiri sana kutokana na kua ni Mtihani mkubwa kwani hali itakua kama kwamba Pepo na Jahannam zitakua chini yake

Habari hii ilituhuzunisha na Kututia khofu sana kama Kwamba Dajjal amejificha chini ya Mashina ya Mitende akitusubiria. Hivyo Jioni tulipokutana tena na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi akatuona namna tulivyobadilika haki zetu kutokana na kuchanganyikiwa

Hivyo akatuuliza: 'Vipi kuna tatizo gani?'

Nasi tukajibu: 'Asubuhi Umetuambia kuhusiana na Dajjal, na katika mambo uliyotuambia basi yalikua hayana Umuhimu lakini kuna mambo ambayo ulituambia na yametuchanganya kwani ni Mtihani mkubwa sana kiasi ya kua sisi tunahisi kama kwamba Dajjal tayari ameshafika na amejificha chini ya Mitende.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: La! Sio Dajjal tu, bali kuna Mitihani myengine pia ambayo mimi nna khofu nayo juu yenu**

Na hata kama Dajjal akitokea wakati mimi niko pamoja nanyi, basi mimi mwenyewe nitakabiliana nae uso kwa uso bila ya nyinyi. Na kama akitokea wakati mimi siko pamoja nanyi basi kila mmoja wenu atakabiliana nae kulingana na Ushupavu wake, na Allah ni Msimamizi na Mlinzi wa Waumini wakati mimi nitakapokua sipo.

Na mtamjua Dajjal kutokana na kua na kua na Nywele zenye Mawimbi, Jicho moja liko juu zaidi ya Jengine, na kama ikibidi nimfananishe na Mtu kwa muonekano wake basi ni kama Abu Al Uzza Ibn Qattan(amabe alikua ni Mtu mwenye Sura Mbaya sana katika wakati wa Ujahiliyah). Na itakapotokea Mmoja wenu akakumbana nae basi na asome aya za Mwanzoni za Surat Al Kahf dhidi yake na zitamsaidia Dajjal atatokea kutoka katika sehemu ya wazi baina ya Syria na Iraq na kusababisha mtafaruku katika upande wa Kulia na Kushoto. Hivyo enyi Waja wa Allah kuweni na Msimamo dhidi yake.'

Masahaba Wakauliza kwa kusema: '*Ya Rasul Allah!* Hivi Jee atakaa kwa mda gani ardhini?'

Rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: Atakaa Kwa siku 40, lakini Siku ya kwanza itakua sawa na Mwaka mmoja, na siku ya pili kama Mwezi, na siku zilizobakia kama siku za Kawaida

Masahaba wakauliza: '*Ya Rasul Allah!* Hivi Jee atakua anatembea ardhini kwa kasi gani?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Haraka sana kama vile Mawingu yanavyosukumwa na Upepo, na kisha atawapita watu na kuwataka wafuate katika Imani yake ya Kufr**

Nao watamuitikia na kumfuata, atayakusanya Mawingu nayo yatanyesha Mvua, ataiamrisha Ardhi nayo itanawiri na kutoa Mazao, na Wanyama watakula Na Watakaporudi Malishoni wanyama hao basi Nundu zao Zitakua kubwa zaid, Chuchu zao zitajaa na kutoa Maziwa zaidi na mapaja yao yatakua yamejaa.

Kisha Dajjal atakutana na Watu wengine atawaita katika Imani yake na watu hao watamkana. Dajjal ataachana nao watu hao na kisha Watu hao watapatwa na mtihani wa Ukame na Njaa na watakua hawana kitu chochote wanachokimiliki.Kisha Dajjal atarudi katika sehemu hio na kuiamrisha Ardhi hio kwa kusema: 'Ewe Ardhi! Toa nje Hazina zako!'

Hivyo hazina ya Ardhi itatoka kama vile Nyuki wanavyomfuata Malkia wao. Kisha Dajjal atamuita mmoja kati ya Vijana shababi waliopo hapo na kisha atampiga Upanga kati kati na kumtenganisha kiwiliwili chake huku na kule kwa masafa ya Mtunga Shabaha na Upinde wake na Kisha Dajjal atamuita kijana huyo na Kiwiliwili chake kitakuja na Kuungana na atakua hai na Dajjal akasherehekea sana, Kwa Ushindi wa mafanikio yake hayo.'

Ambapo katika wakati huu *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamshusha Al Masih Isa Ibn Maryam, ambapo atashukia katika Mnara wa maeneo ya Mashariki ya Damascus. Huku akiwa amefunikwa Maguo yenye Rangi Mbili huku Mikono yake ikiwa imeegemea kwenye Mabawa ya Malaika

Na Atakapoinamisha kichwa chake chini basi matone ya Maji yatamiminika kutoka kichwani kwake. Na akinyanyua Kichwa chake basi kila tone liliopo kichwani mwake litameremeta kama Lulu halisi. Na kila asiekua Muislam basi akivuta hewa inayotokana na Pumzi zake Isa Ibn Maryam basi atakufa hapo hapo, na Pumzi yake itafikia katika Umbali wa Upeo wa Macho yake

Na kisha Isa Ibn Maryam ataanza kumtafuta Dajjal na atakutana nae karika Mlango wa Lud (Mlango wa Kuingilia Bayt ul Maqdis ambao mpaka leo unajulikana hivyo hivyo) na kisha atamuua Dajjal Na kisha baada ya hapo Isa Ibn Maryam atakutana na watu waliohifadhiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi ya Dajjal

Na Kisha Isa Ibn Maryam atawapapasa Nyuso zao (Kwa huruma baada ya kukumbwa na Mitihani na kufuzu) na kisha atawabashiria kuhusiana na Darja ya Juu ya Peponi kwa watu hao. Baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamwambia Isa Ibn Maryam kua: 'Kwa Hakika mimi nitawatuma Watu miongoni mwa waja wangu ambao hakuna mikono miwili yeyote Itakayothubutu kupigana nao. Hivyo Ewe Isa wakusanye Waja wangu (hawa walioniamini) na wachukue hadi kwenye Mlima wa Tur.'

Isa Ibn Maryam atafanya hivyo, na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaachia Yajuj WamaJuj. Ambao wataonekana wakikimbia kwa nguvu na kasi kubwa sana kutoka katika kila Upande

Ambapo Kundi la kwanza litapita katika maeneo ya Buhairah Tabariyyh. Buhairah Tabarriyah ni eneo la Bahari ya Maji Baridi au Ziwa ambalo leo linajulikana kama Bahari ya Galileo au Ziwa Tiberias au Kinneret ambalo lipo Katika ardhi inayokaliwa na Waisrail nchini Palestina.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **anasema kua:Kundi la mwanzo la Yajuj waMajuj litapita kwenye Bahati ya Buhaira Tabarriyah na Kunywa na Kula kila kilichomo ndani yake Na hivyo Kundi la Pili likipita katika eneo hilo basi litasema kua: 'Inaonekana hapa kulikua kuna Maji hapo kabla.'**

Hivyo Isa Ibn Maryam na Watu wake watakimbilia hifadhi katika Mlima Tur, Na Waumini wengine watakimbilia katika sehemu zilizokua salam kwao, watakua na akiba ya Chakula lakini mwisho wake akiba yao hio Itamalizika, na Kichwa cha Ngombe kitakua ni Bora kuliko Dinari 1000 za Dhahabu.

Na kwa upande mwengine anasema Abd Rahman Ibn Yazid *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Baada ya Yajuj wa Majuj kupita katika maeneo ya Buhaira Tabarriyah basi watapanda Mlima wa Khamar Ambao ni Mlima miongoni mwa Milima iliyopo katika Ardhi ya Bayt Al Maqdis na watasema: Hakika Tumeshawaua wale wote waliopo Juu ya Ardhi, hivyo sasa hivi wacha na tuwaue waliopo Juu Mbinguni'**

Na kisha Watatunga Shabaha kuelekea Mbinguni na kuachia Mipinde yao, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataifanya Mipinde yao hio kua ni yenye kugeuka na kuwarudia wao wenyewe na kuwamwagia Damu zao.'

Ambapo Kwa upande wa Hadith ya Nawwas Ibm Saman Radhi Allahu Anhu basi inaendelea kwa kusema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaendelea kusema kua:

Kisha Isa Ibn Maryam na Watu wake Watamgeukia *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kumuomba kua awaondelee matatizo ya Mtihani wao na Dua yao itajibiwa.

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atatuma Maradhi ya Muambukizo ya Funza anaeota Shingoni (Na kuanza kuila Shingo ya Mtu husika) na hivyo Watawaua watu wote: Miongoni mwa hao Yajuj aa Majuj.

Na kisha Isa Ibn Maryam na watu wake watashuka kutoka katika Mlima Tur na wataona kua hakuna hata sehemu moja ya Ardhi ambayo imebakia bila ya kua na Maiti ya Yajuj wa Majuj, na Ardhi itakua inanuka vibaya sana.

Kisha Isa Ibn Maryam na Watu wake watamgeukia tena Allah Subhanah wa Ta'ala
Na kumuomba kuwaondolea Mtihani huo wa Maiti hao, na watajibiwa.

Allah Subhanah wa Ta'ala atatuma Ndege wakubaa wenye Shingo kama Ngamia, ambao watabeba miili ya Maiti hao wote na kuitupa Baharini.

Na baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atatuma Mvua ambayo hakuna Nyumba ya Udongo wala Hema la mabedui liliopo Jangwani, litakoswa na Mvua hio
Hivyo Ardhi yote itasafishwa na kua safi kama kioo

Kisha Allah Subhanah wa Ta'ala ataiambia Ardhi: Otesha Mazao yako na toa wingi wa Neema zako.

Na itakua kuna neemakubwa sana kiasi ya kua Komamanga Moja litatosheleza kua chakula kwa Kikundi kizima cha Watu.

Na Gamba lake litatumika kama Paa la Kujilinda dhidi ya Jua na Maziwa ya Wanyama yatakua na Barka kubwa sana na yatawatosheleza wengi sana Kiasi ya kua Maziwa ya Ng'ombe mmoja yatawatosheleza Watu wa Kabila zima na Maziwa ya Mbuzi mmoja yatatosheleza kwa Ukoo Mzima

Baada ya kipindi cha Miaka 40 ya Neema hizi na utulivuna hifadhi basi Wakati wa Kiama utakaribia

Na ukishawadia basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atatuma Upepo maridhawa ambao utasababishia Waumini kutokua na hisia za Vifua na mabega yao na kisha Watatolewa Roho zao
Na kisha watabakia Watu ambao ni waasi, waovu na Wasioamini

Ambao watafanya Maovu na Ufisadi Ardhini na kua kama Punda, na hivyo Dhidi yao watu hawa ndio watakutanishwa na Saa ya Mwisho ya Dunia

Allah atunusuru na Uasi dhidi yake na Ufisadi ardhini na atuepushe na watu wenye sifa hizi..Amiin

Tumalizane kuhusiana na Yajuj na Majuj kwa kufahamishana kua kulingana na Vithibitisho vilivyomo kwenye aya za Qur'an na Hadithi ambavyo ndio vyanzo vikuu vya Ilm, Sharia na Hukm katika Maisha ya Kila Muislam na ndio miongoni mwa Misingi ya Imani ya Dini ya Kiislam na kuamini kwake hua ni Miongoni mwa Nguzo za Imani.

Basi hua haikubaliki kupinga Juu ya yale yaliyosemwa ndani yake vyanzo hivyo kwani Kukubaliana navyo ni Wajibu wa Kila Muislam. Na Qur'an na Hadith zimethibitisha kua kutokea kwa Yajuj wa Majuj ni miongoni mwa Dalili za Kiama, na kama tulivyoona kua Hadith na Quran hazipingani juu ya kuhusiana na kua Yajuj wa Majuj watakuja na watakuwepo na watatokea, lakini katika wakati gani basi?

Naam..katika Wakati ambao utakua ni baada ya kushuka kwa Nabii Isa Ibn Maryam *Alayhi Salam.* Na ndio maana nikasema kua tunaachana na mitizamo ya Wanazuoni wa leo hii ambao wanasema kua labda huenda wakawa Wachina au Warusi n.k

Na ndio maana hata mtizamo wa Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua ni Waturuki nikaufafanua kabisa na kusema kua huo ni Mtizamo tu na haumanaaishi kua Waturuki ndio miongoni mwao Viumbe hao.

Kwani hata Imam Al Alusi katika Tafsir yake ya Ruhi Al Maani basi tunaona kua anasema kuhusiana na wale waliokua wakiwashukia watu wa Tatataristan ambao ni Warusi wenye Asili ya Kituruki ambao ni Waislam wanaishi Kusini mwa Urusi kwenye Nchini zilizomalizia na Stan stan yaani Tatarstan, Uzbekistan, Azerbaijan, Tajikistan, Kazakhstan, Turkmenistan, Mongolia n.k

Kua ndio miongoni mwa Yajuj wa Majuj Kwa kusema kua: **‘Hili ni kosa Kubwa sana kuwafikiria watu hawa kua ndio Yajuj wamaJuj kwani kufikiria hivyo hua ni kuenda kinyume na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na hii hua ni sawa kusababisha Tafrani kama ile itakayosababishwa na hao Yajuj wa Majuj Wenyewe.’**

Kwa maana hio basi haina haja ya kutafuta kuthibitishiana kua labda ni Urusi au China au Watu wa Magharibi kua ndio Yajuj wa Majuj. Bali ni wajibu wetu kukabiliana na kitisho kikubwa zaid dhidi yetu ambacho ni Nafsi zetu, kwani hata matamanio ya Nafsi zetu yanaweza yakawa ni Dajjal kwetu pia na kutupelekea katika maangamizo yetu, kabla ya kutokea huyo Dajjal mwenyewe na hao Yajuj wa Majuj.

Kwani mimi na wewe hatujaufikia na hatutoufikia wakati huo watakapoachiwa Yajuj wa Majuj na hii ni kwa sababu hata huyo Dajjal na Mahdi hawajatokea bado, na Nabii Isa ambae nae ataishi kwa miaka 40 hajashuka bado.

Hivyo kwa sasa Jukumu letu mimi nawe ni Kutekeleza Majukumu yetu mbele ya Mola wetu, Kuelimishana kuhusiana na Dini ya Kiislam na kusimamia vizazi vyetu kwa kuvisomesha Dini ya ili kuvirahisishia uzito wa Mitihani ya Kiimani katika nyakati zao watakazoishi, kwani mbele yao kuna ugumu zaidi na mitihani yadi ya Kiimani.

﴿قَالَ مَا مَكَّنِّي فِيهِ رَبِّي خَيْرٌ فَأَعِينُونِي بِقُوَّةٍ أَجْعَلْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ رَدْماً﴾

Qala ma makkannee feehi rabbee khayrun faaAAeenoonee biquwwatin ajAAal baynakum wabaynahum radman*(Surat Al Kahf 18:95)*

Tafsir: **Akasema (Dhu Al Qarnayn) Ile sehemu aliyoniweka Mimi Mola wangu Ni Bora zaid (kuliko hivyo mnavyotaka kunizawadia kwa kukusaidieni Jambo hilo) Hivyo Nyinyi nisaidieni kwa Nguvu (Za Wafanyakazi) Nami Nitakujaalieji baina yenu Na Baina Yao Ukuta Mkubwa sana.**

Ambapo aya imetumia Neno *Kana* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha, Kua, Kuwepo, Kutokea, au Kufanyika.

Neno Kana hua linategemeana na namna lilivyotumika kwani likitumika katika hali ya kitendo kilichopita basi humaanisha Kitendo kilichokua kikiendelea kwa mda. Na pia neno *Kana* hua linatumika Kuainisha Ukweli wenye Haki na Usiopingika wala kua na shaka ndani yake.

Neno *Kana* ndio lililotoa neno Makanun ambalo humaaanisha Sehemu, Makazi, Darja au Hadhi ya Kitu. Neno *Kana* ndio pia lililotoa neno *Makanat l*enye kumaanisha Weka Sehemu yako. Na pia likatoa neno *Makanatun* lenye kumaaanisha Sehemu, Njia au hali fulani ya kitu.

Ambapo Dhu Al Qarnayn akajibu Hivyo baada ya Dhu Al Qarnayn kuombwa kua awajengee ukuta watu hao dhidi ya Yajuj wa Majuj na kisha atazawadiwa na Watu hao kutokana na kuwasaidia kwake huko kutokana na Uwezo wake basi Dhu Al Qarnayn akajibu kama zilivyosema aya.

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Muislam ndugu yake ni Muislam mwenzake, hivyo hamdhuru wala hamkabidhi Mwislamu mwenzake kwa adui yake, kwani Mwenye kumsaidia Muislam mwenzake basi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamsaidia yeye baada yake'(***Bukhari na Muslim)*

Hivyo kabla ya kuendelea kufafanua zaid basi kwanza inabidi tufahamishane kua kitu muhimu sana

Ambacho ni kua: **Aya hii ndani yake in Uthibitisho wenye Hukmu inayoonesha kua Wale watu wenye Kuwatia khofu wenzao na kutaka kuwasababisha Madhara wenzao basi hua Wanastahiki kutengenishwa na wenzao ili wasije wakawadhuru.**

Na pia ndani yake inatuwekea wazi kua Wale wenye Mamlaka na uwezo wa Kuzuia Madhara basi ni wajibu wao kuzuia Madhara hayo.

Na pia Katika baadhi ya Mambo basi hua sio lazima kuyafanya kwa kutegemea Ujira kutoka Kwa uliowafanyia kutokana na kua na neema ya uwezo Aliokujaalia kua nao Mola wako.

Bali wewe fanya tu kwa ajili ya kusaidia kutokana na kua unaweza kusaidia katika jambo hilo bila ya kupokea Malipo hata kama itapendekezaa kua utalipwa, kwani kusaidia kwako bila ya kuchukua ujira hua ni kuonesha Shukrani kwa Mola wako.

Kwa upande mwengine basi tunaona kua katika Aya iliyootangulia kabla ya hii basi Watu husika walioomba Msaada kwa Dhu Al Qarnayn walimuomba kua awajengee Saddan Yaani Kizuizi au Ukuta, Au Kizinguti.

Ambapo katika Aya hii basi ambayo ni yenye kuonesha Majibu yake Dhu Al Qarnayn basi tunaona kua kutokana na Uwezo aliojaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Dhu Al Qarnayn anaahidi kua hatowajengea *Saddan* bali anasema kua atawajengea Radman

Ambapo neno *Radman* ni neno lenye kutokana na neno *Radama* ambalo hua linamaanisha Kuziba, Kufunga na pia humaanisha Kujaza kitu katika sehemu kiasi ya kua hakutokua na Uwazi uliobakia katika sehemu husika.

Hivyo neno *Radman* Hua linamaanisha Kitu kama Ukuta ambao ni Imara zaid na mkubwa zaidi kwa mara kadhaa ukilinganisha na Sadan.

Na kufahamiana zaid basi na tuchukulie hapa mfano wa kua Dhu Al Qarnayn aliombwa ajenge Kibanda cha Kuhifadhi vitu labda kwa malipo kiasi fulani lakini yeye Dhu Al Qarnayn akaahidi kua atajenga Nyumba ya Ghorofa 10 badala yake tena Bure bila ya kuchukua malipo yeyote.

Kwani hivi ndivyo walivyokua wale kujaaliwa kua na Mali na kisha pia wakawa ni wenye kujua kua Mali hio hakuipata kutokana na Jitihada zake, bali ameipata kutokana na Rehma za Mola wake juu yake na yeye kua ni miongoni mwa wenye kuchaguliwa kua miongoni mwa walionufaika na fadhila za Mola wake juu yake. Kwani kila kiumbe hua ni chenye kua ndani ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kuishi kwake hapa Duniani.

Lakini si kila kiumbe hua chenye kujaaliwa kupata ufadhili wa kufadhiliwa na Muumba katika kuneemeshwa neema zake.

Ambapo kwa upande wa Dhu Al Qarnayn basi tunaona kua amefadhiliwa kwa kila kitu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambapo ndani ya Fadhila hizo basi alizofadhiliwa mna pia Ilm na Hikma za kujua kua Hizi ni miongoni Fadhila za Mola wangu juu yangu na hivyo ni wajibu wangu mimi kuonesha Shukrani kwa kufadhiliwa kwangu huko.

Na ndio maana baada ya kuombwa ajenge *Sadan* basi akaamua kujenga *Radman* ili kuwatatulia matatizo yao yote watu hao kwa mda wa miaka na miaka waishi bila ya kua na khofu na Yajuj wa Majuj.

Kwani katika kujielezea kwake basi Dhu Al Qarnayn katika aya hii tunaona kua anasema kua: **'Uwezo alionijaalia mimi Mola wangu kwa ajili ya kuwasaidia nyinyi ni Mkubwa na ni Bora zaidi kuliko vile mnavyotaka kunizawadia nyinyi. Hivyo nakuombeni nyinyi muwe ni wenye kunisaidia mimi kwa Vibarua wa kunisaidia kuifanya hii kazi kwani hapa inabidi nipate Watu wenye umahiri katika Ujenzi, na pia inabidi zipatikane zana na vifaa stahiki.**'

Na hivyo watu hao wakauliza: '**Hivi Jee ni Zana na Vifaa Gani hizo?'**

Hivyo Dhu Al Qarnayn akasema: '***Atuuni Zubara al Hadiid* - Nileteeni Vipande vya Chuma.'**

Na pia akasema: ***'Atuuni Qitran* - Nileteeni Shaba Imoto iliyoyayuka.'**

Ambapo neno *Zubar* limetokana na neno *Zabara* lenye kumaanisha Kukopia, Kuandika na pia humaanisha Kuchapia kama kupiga Plasta Nyumba kwa Kokoto.

Neno *Zabara* ndio lililotoa neno *Zabur* yaani Kitabu, hivyo kitabu alichopewa Nabii Daud jina lake *Zabur* ambalo kwa Kiswahili hua ni Andiko au Kitabu kitukufu kutoka kwa Allah Subhanah wa Ta'ala.

Neno *Zabara* ndio lililotoa neno *Zubrah* Ambalo humaanisha Pande Moja Kubwa sana la Chuma ambalo halijakatwa, na pia humaanisha Vipande Vingi vidogo vidogo vya Chuma ambacho kimeshakatwa.

Kwa maana hio basi hapa *Dhu Al Qarnayn* aliposema *Atuuni Zubara al Hadiid* - Nipeni Chuma basi hua inamaanisha kua apewe Pande kubwa sana la chuma ambalo likikatwa vitapatikana vipande vingi vidogo vidogo vya Chuma.

Na pia alimaanisha kua apewe Vipande Vingi vya Vyuma vilivyotokana na Chuma Kikubwa sana baada Ya kukatwa kwake.

Ambapo kwa upande wa neno *Qitran* basi ni lenye kutokana na neno *Qatara* ambalo humaanisha Kutiririka kwa kitu au Kumiminika kwa Matone ya Kitu.

Hivyo neno *Qitran* hua linamaanisha Shaba Iliyoyeyushwa na kua na Ulaini wa kuweza Kumiminika kama Uji.

Na watu hao wakamuuliza Dhu Al Qarnayn kwa kusema: **'Hivi Jee sisi tutaweza kukipata wapi Chuma cha aina hio na Shaba ya aina hio?**

Dhu Al Qarnayn akawaambia: **'Nitakuonesheni mimi ilipo migodi ya Chuma na Shaba kutokana na uwezo wa Mola wangu.'**

Watu hao wakauliza: **'Sawa, lakini jee tutawezaje kuvikata Vyuma hivyo na Shaba hio?'**

Ambapo Dhu Al Qarnayn akawatolea aina ya Madini yaitwayo Sahun ambayo ni kama Almasi lakini si Almasi. Kwani Sahun ni Madini ambayo ndio aliyotumia Nabii Sulayman *Alayhi Salam* katika kuchonga Nguzo za Bayt Al Maqdis kwa mara ya kwanza.

Kisha watu hao wakaanza kazi ya Kuchimba Vyuma na Shaba kutoka Ardhini na vilipotosheleza vitu hivyo basi Dhu Al Qarnayn akapima masafa baina ya Milima miwili iliyopo baina ya watu hao na Yajuj wa Majuj na kisha akawasha moto kwa ajili ya kuyeyusha Chuma na Shaba ili ujenzi uanze.

Naam..anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kutuelezea namna Dhu Al Qarnayn alivyojenga ukuta huo Dhidi ya Yajuj wa Majuj kua alisema:

﴿آتُونِي زُبَرَ ٱلْحَدِيدِ حَتَّىٰٓ إِذَا سَاوَىٰ بَيْنَ ٱلصَّدَفَيْنِ قَالَ ٱنفُخُواْ حَتَّىٰٓ إِذَا جَعَلَهُ نَاراً قَالَ آتُونِيٓ أُفْرِغْ عَلَيْهِ قِطْراً﴾

Atoonee zubara alhadeedi hatta idha sawa bayna alsadafayni qala onfukhoo hatta idha jaAAalahu naran qala atoonee ofrigh AAalayhi qitran*(Surat Al Kahf 18:96)*

Tafsir: ***(Dhu Al Qarnayn alisema) Nipeni Vipande vya Vyuma (Alipopewa akavipanga) Hadi Ikafikia kua sawa Baina ya Milima Miwili Akasema(Dhu Al Qarnayn kua sasa) Puliza (Moto), Hadi Akakifanya (Chuma hicho kua Chekundu kama) Moto Kisha Akasema : 'Nileteeni Niimimine Juu yake Shaba ya Moto.***

Tunapoiangalia aya hii basi tunaona namna *Allah Subhanah wa Ta'ala* anavyoelezea Namna Dhu Al Qarnayn alivyoushona Ukuta huo baina ya Milima miwili hio. Ambapo alitumia Zubara Al Hadid vipande vya Vyuma na Qitran yaani Shaba Uliyoyeyushwa.

Ambapo kwa upande mwengine basi tunapomuangalia Imam Abu Abd Allah Mubammad Ibn Ahmad Ibn Abi Bakr Al Ansari Al Qurtubi basi yeye amesema kua hi haikua shaba bali ilikua ni Fedha.Na kwa vyovyote itakavyokua iwe Shaba au Fedha na Chuma lakini tunapozungumzka kuhusiana na Utaalamu wa kuchoma na kukishona Chuma pamoja kwa njia hii basi wataalamu hua wanasema kua ni Utaalamu wa hali ya juu sana hususan katika hiki kipindi cha karne yetu ya Teknolojia.

Kwani huu hua ni ushonaji na uunganisha wa Vyuma kwa madini nyengine, Kama hii ya Shaba au Fedha hua ni wenye Umadhubuti wa hali ya juu kabisa, na hivyo hua ni vigumu sana kwa kitu kilichoshonwa kua ni chenye kuchanika au kuvunjika au kuharibika kiurahisi.

Kwani ushonaji huu hua ni tofauti na ushonaji wa kawaida ambao hua ni Ushonaji wa Chuma kwa chuma ambao hua kamwe hauwezi kuufikia kiumadhubuti ushonaji wa Dhu Al Qarnayn kama ilivyoelezwa ndani ya Qur'an.

Ambapo maneno yake yamepitia kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi aa Salam* ambae hakusoma, na wala katika Ardhi yao hawakua na Ufundi wa kushona Vyuma kama huu. Hivyo aya hii na yaliyomo ndani yake yanadhibirisha pia kua Qur'an ni Kitabu cha Muumba anaejua kila kitu na ni mwenye utaalamu wa juu ya kila kitu. Na hii ni kutokana na uthibitisho wa yaliyomo ndani yake ikiwemo Sayansi ya hali ya juu kama ilivyo ilizewa kwenye aya hii.

Na wanasema Wanazuoni kua katika kujenga kwake huko basi Dhu Al Qarnayn alichimba Ardhini kwanza hadi akafikia katika sehemu ambayo aliyakuta Maji ndani yake. Na kisha baada ya hapo akajenga Msingi wa Ukuta huo kwa kutumia mawe na Shaba iliyoyeyushwa. Na kisha akaupandisha Juu ukuta kwa Kutumia Chuma, Shaba na Mawe.

Na kisha baada ya kumalizika Ujenzi huo ambao ulikua ni baina ya Milima miwili basi ikawa kama kwamba Milima Miwili hio imeungana kuanzia shinani mwake hadi Juu Kileleni. Na hivyo Ujenzi wa Ukiuta huo ulikua kama ujenzi wa Ukuta wa Bwawa kubwa sana kiurefu kuenda juu na pia kiupana. Kwani ilikuani ukuta wa Chuma na Shaba wenye Urefu wa Mita 200 na upana wa Mita 50.

Ambapo katika kuamrisha kwake kua kupulizwe basi kunamaanisha kua yeye alikua ndio Msimamizi Mkuu Wa Ujenzi huo.

Na kwa upande mwengine basi pia kuna wasemao kua katika kujenga kwake baada ya kujenga Msingi basi Ukuta huo aliujenga kwa kupanga matabaka ya Vyuma na Mbao kuanzia chini kuelekea Juu. Kisha Ukawashwa Moto hadi Vyuma Vikawa Vyekunduu.

Kisha ikamwagiwa Shaba juu yake, na hivyo Moto ukawa Unakula Mbao huku Shaba ikiwa inajishona pamoja na Vyuma hivyo. Na baada ya kumalizika Moto huo na Ujenzi huo basi Ukuta ukawa unaonekana kama Guo lenye Rangi nne ambazo ni Nyeusi na Kijivu za Chuma na Nyekundu na Manjano za Shaba.

Hivyo Dhu Al Qarnayn aliujenga ukuta huo huku akiwa na Yaqini ya kua Ukuta huo haitovunjika hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapoamua kua Uvunjike na hivyo kua ni wenye kuwaachia huru Yajuj wa Majuj kutoka ndani yake kwani aya zikaendelea kusema kua:

﴿ فَمَا ٱسْطَاعُوٓاْ أَن يَظْهَرُوهُ وَمَا ٱسْتَطَاعُواْ لَهُ نَقْباً ﴾

Fama IstaAau an Yadhharuhu wama IstaAau lahu Naqban*(Surat Al Kahf 18:97)*

Tafsir: ***Hivyo hawawezi Kuupandia Juu yake na Wala Hawawezi kuutoboa na kupenya Ndani yake.***

Na amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu kua:* ***'Mimi nilimuuliza Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Yajuj wa Majuj Ambapo nae akasema: Wao ni Ummah wa Mataifa Kadhaa, na kilaTaifa lao kina watu 400,000, na Hakuna Hata mmoja miongoni mwao atakaekufa bila ya kuacha Watoto 1000 wa Kiume, ambapo kila mmoja wao atatoa Upanga wake.'**

Hivyo Masahaba wakasema : ***'Ya Rasul Allah! Hebu tuelezee kuhusiana nao.'***

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **Yajuj wa Majuj wako katika Makabila matatu tofauti, na kuna wenye Urefu wa Futi 20. Kuna wenye urefu na Upana sawia, na hivyo Urefu wao ni Futi 20 na upana futi 20. Na kuna aina ya 3 ambao akilala analilalia Sikio lake moja kama Shuka la kutandikia na sikio la pili kama shuka la kujifunikia.**

Wakiachiwa Hawatompita Hata Tembo, Nguruwe wala Mnyama yeyote wa Mwituni isipokua Watamla Na atakapofariki Mmoja wao Miongoni mwao basi huila maiti yake hio Ardhi yao inaanzia katika maeneo ya Syria na kumalizikia Khurasan Watakunywa Maji ya Chemchem za Mashariki na Maji ya Ziwa Tabriz.'

Subhana Allah!

Tuvute Fikra juu ya hili la kua hata Tembo Watamla na mwenzao akifa pia Wanamla. Ambapo mbali ya Nguvu na uwezo wao wote lakini hata hivyo hawatoweza kuuparamia Ukuta wa Dhu Al Qarnayn wala kuutoboa kutokana na Miujiza yake Ukuta huo.

Kwani tunapouangalia Ujenzi wake tu, basi hata wale wanaofanya kazi za Kuyayusha Vyuma Viwandani huwabidi kukaa mbali na Moto ili wasidhurike nao na pia wasidhurike na Uji wa Chuma au Shaba husika. Lakini hata hivyo kutokana na Uwezo wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi si Moto huo wala si Uji wa Chuma na Shaba vilivyoweza kuwasababishia madhara kwa Dhu Al Qarnayn na watu wake katika utekelezaji wa Jukumu lao hilo.

Na wala Yajuj wa Majuj wenyewe hawakumfanyia ufisadi Dhu Al Qarnayn katika wakati wa Ujenzi huo. Na bila ya shaka hii ni kwa sababu Dhu Al Qarnayn alikua ni mwenye kufuata Sababan kutoka kwa Mola wake.

Naam..hivyo baada ya Dhu Al Qarnayn kumaliza kuujenga Ukuta huo basi akasema kama zinavyosema Aya kua:

﴿ قَالَ هَٰذَا رَحْمَةٌ مِّن رَّبِّي فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ رَبِّي جَعَلَهُ دَكَّاءَ وَكَانَ وَعْدُ رَبِّي حَقًّا ﴾

Qala Hadha Rahmatun min Rabbii, Faidhaa jaa waAadu Rabbii Jaalahu Dakkaa Wakana WaaAdu Rabbii haqqan*(Surat Al Kahf 18:98)*

Tafsir: ***Akasema (Dhu Al Qarnayn) Hii ni Rehma Kutoka kwa Mola wangu Lakini itakapokuja Ahadi ya Mola wangu Ataujaalia Kuanguka Na Kamwe Haina shaka Ahadi Ya Mola wangu kwani ni ya Haki.***

Tunapoaiangalia aya hii basi tunaona kua inatuonesha Umuhimu wa kua ni wenye Kumshukuru *Allah Subhanah aa Ta'ala* kwa kila alichotujaalia kua nacho.

Kwani amesema Amir ul Muuminin Ali Ibn Abi Takib *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Ukarimu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni wenye kushikamana sana na Shukrani za Mja kwa Mola wake. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* hatosita Kumkirimu zaidi Mja wake hadi pale Mja huyo atakaposita kuonesha Shukrani mbele ya Mola wake.'**

Na hivyo Dhu Al Qarnayn alikua ni mwenye Kuonesha Shukrani kwa kua ni mwenye kujaaliaa kua na Uwezo wa Kutekeleza Jukumu alilopewa na Mola wake kutokana na Rehma na fadhila za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani ni kutokana na fadhila hizo kupitia kwake basi na yeye amekua ni miongoni mwa wenye kua na uwezo wa kuiokoa Jamii ya Watu hao dhidi ya Ufisadi wa Yajuj wa Majuj. Na kisha Dhu Al Qarnayn akathibitisha kua Ukuta huo utakua ni wenye kusimama Kwa uimara na Umadhubuti hadi pale atakapotaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kulingana na Makadirio yake kua Ukuta huo uvunjike na kuanguka itakapofika Ahadi yake kuanguka.

Na kuna baadhi ya Wanazuoni ambao wametafsiri kua ahadi inayozungumziwa kwenye aya hii basi ni ahadi Kuachiwa kwa Juj wa Majuj. Na hivyo kutoka ndani yake kama zilivyosema Hadith tulizoziangalia na pia ile aya ya 96 ya *Surat Al Anbiyah* ambayo tumeshaifafanua.

Ambao huu ndio mtizamo wa wengi zaid ya Wanazuoni ambao wanakubaliana kua Tukio hilo ndio itakua ni moja kati ya Dalili za Kiama.

Na kwa Upande mwengine basi kuna Wanazuoni wasemao kua Ahadi inayozungumziwa kwenye aya hii..ni ahadi ya Siku ya Malipo na hii ni kulingana na uthibitisho wa hadith ifuatayo: '**Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua; Katika Safari ya Miraj Mimi nilimkuta Ibrahim, Musa na Isa wakiwa wamekaa huku wakizungumza kuhusiana na Saa ya Kiama.**

Ambapo Ibrahim akuliziwa kuhusiana nayo hivyo nae akasema: 'Hakika Mimi sijui chochote kuhusiana nayo.' Akaulizwa na Musa nae akasema kua hajui chochote. Akaulizwa na Isa nae akasema: 'Hakuna anejua kuhusiana Saa ya Kiama utafika wakati gani.'

Lakini Mola wangu ameniambia mimi kuhusiana na matokeo yatakayo tokea kabla ya Saa ya Kiama, bila ya kuniambia itakua lini. Ameniambia mimi kua Dajjal atatokea, na kisha atanituma mimi nishuke chini Ardhini kwa ajili yake (Dajjal). Na hivyo atakaponiona mimi basi Dajjal ataanza kuyayuka kama iyayukavyo Risasi iliyochomwa moto

Na Hali itafikia kua hadi Majabali na Miti itakua ikisema: 'Enyi Waislam! Huyu Hapa Kafiri amejificha Nyuma yangu njooni mumuue.'

Hivyo Makafiri watauliawa wote, na kisha Watu watarudi kwenye Makazi ya ardhi zao. Lakini sasa, watotokea Yajuj wa Majuj kutoka katika kila sehemu ya upande wa Milima ambao itabidi wakabiliane nao. Na Yajuj wa Majuj Hawatopita katika sehemu yeyote isipokua Wataila na kunywa maji yote.

Hivyo Watu watanifuata mimi kua kunilalamikia juu yao. Nami nitamuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ambapo nae atawaangamiza wote hadi Ardhi itakua inanuka kutokana nao. Na kisha Itakuja Mvua kubwa sana na na mafuriko yatakayoipeleka Miili yao baharini, Kisha Ardhi Itatandazwa, na itakua kama kipande cha Ngozi kilichotandazwa

Na hio ndio Ahadi ya Mola wangu aliyoniahidi Katika wakati huo Ardhi itakua kama Mwanamke aliekua Mja mzito ambae ameshapitiliza mda wake wa Kujifungua na hivyo watu hawajui kua kama atajifungua asubuhi ama jioni.'*(Imam Ibn Jarir)***

***Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuambia katika aya kua:**

﴿ وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ يَمُوجُ فِى بَعْضٍ وَنُفِخَ فِى ٱلصُّورِ فَجَمَعْنَاهُمْ جَمْعاً ﴾

Watarakn<u>a</u> baAA<u>d</u>ahum yawma-i<u>dh</u>in yamooju fee baAA<u>d</u>in wanufikha fee al<u>ss</u>oori fajamaAAn<u>a</u>hum jamAA<u>a</u>n ***(****Surat Al Kahf 18:99)*

Tafsir: ***Na Tutawaachia Baadhi yao wengine (Yajuj wa Majuj) Katika Siku hio Kama Mawimbi juu ya Wengine Na Litapulizwa Baragumu Na Kisha Tutawakusanya Pamoja)***

Hapa aya bado zinaendelea kuthibitisha kua Yajuj wa Majuj ni moja kati ya Dalili kubwa za Kiama. Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Dalili za Kiama basi tunaona kua kuna Dalili ndogo ambazo ni zenye kuashiria kua Kiama kinakaribia lakini hata hivyo bado.

Yaani tuchukulie mfano Taa za Barabarani Basi hizi Dalili ndogo tuzionazo sasa kama Wanawake kua wengi, Wanawake kuvaa Ngu lakini wako Uchi n.k Hua kama Taa ya Rangi ya Manjano inayoashiria Dalili ya kukaribia kwa siku ya Kiama.

Halafu kuna aina ya pili ya Dalili za Kiama ambazo ni Dalili Kuu na Kubwa za Kiama ambazo kama ni taa za Barabarani basi Hua ni Taa Nyekundu. Yaani ni Dalili zenye kumaanisha kua Hapo hakuna mda tena kwani haijulikani Kiama kitakua asubuhi au Jioni au kesho kama alivyosema Nabii Isa *Alayhi Salam.*

Na hivyo Yajuj wa Majuj ni miongoni mwa Dalili Kuu za Kiama yaani hapo kama Hujatubu basi hutotubu tena na utaangamia. Na kama tunavyoona aya hii kua inazungumzia kuhusiana na Kuachiwa kwa Yajuj wa Majuj kama Mawimbi ya Tsunami wimbi baada ya wimbi wimbi Juu ya wimbi.

Ambapo zinamalizia kwa kusema kua Kisha Litapulizwa Baragumu na kisha tutakusanywa pamoja. Na ingawa tunapoangalia kwa upande wa baadhi ya wanazuoni akiwemo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu basi* tunaona kua wanasema kua: **'Aya hii inazungumzia kuhusiana na kuachiwa kwa Majini na Ibn Adam kabla ya saa ya Kiama.'**

Lakini Kwa upande mwengine kuna wenye mtizamo tofauti akiwemo Imam Abd Rahman Al Suddi ambao wanasema kuhusiana na aya hii kua: '**Aya inadhihirisha kua Utakapofika wakati wa Kuvunjika kwa Ukuta wa Dhu Al Qarnayn na kisha Kuachiwa kwao kua watawavamia Ibn Adam na kufanya Ufisadi na kuangamiza kila kitu, basi hautochukua mda mrefu isipokua Saa ya Kiama itawadia.'**

Hivyo baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutuambia katika aya hio isemayo kua:

﴿ وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ يَمُوجُ فِى بَعْضٍ وَنُفِخَ فِى ٱلصُّورِ فَجَمَعْنَاهُمْ جَمْعاً ﴾

Wataraknа baAAdahum yawma-idhin yamooju fee baAAdin wanufikha fee alssoori fajamaAAnahum jamAAan *(Surat Al Kahf 18:99)*

Tafsir: ***Na Tutawaachia Baadhi yao wengine (Yajuj wa Majuj) Katika Siku hio Kama Mawimbi juu ya Wengine Na Litapulizwa Baragumu Na Kisha Tutawakusanya Pamoja)***

Basi anatuambia katika aya inayofuata baada ya hio ambayo ni ya 100 ya Surat Al Kahf na ndio aya iliyotumia neno *Aa'aradha* ambapo neno *Aa'aradha* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kutokea, Kuoneshwa, Kuwasilishwa mbele za Watu, Kuhudhurisha, Kuwekwa wazi, Kufunuliwa, Kupendekezeshwa, Kulengwa au Kuoneshwa kwa dalili.

Neno *Aa'aradha* ndio lililotoa neno *Aaardhun* ambalo humaanisha Kutandazwa, Kutanuliwa. Neno *Aa'aradha* ambalo limeanzia na herufi *Aain* ni tofauti na neno *Aa'aradha* ambalo ndio lililotoa neno Ardhi lenye kumaamisha Kuzunguka, Kuburingita, Kutoa Mimea kwa wingi.

Hivyo *Allah Subhbah wa Ta'ala* anatuambia katika aya hio kuhusiana na kitakachofuata baada ya kuachiwa Yajuj wa Majuj na kutokea yatakayotokea na kuwadia Kiama kwa kusema kua:

﴿ وَعَرَضْنَا جَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ لِّلْكَافِرِينَ عَرْضاً ﴾

WaAAaradhna jahannama yawma-ithin lilkafireena AAardhan*(Surat Al Kahf 18:100)*

Tafsir: ***Na Tutaionesha Jahanama Katika Siku hio Kwa Makafiri (waliokua wakipinga) Kwa Muonekano wa wazi kabisa***

Subhana Allah! tumuombe Allah atuepushe na Ukafiri na atuepushe na Moto wa Jahanam pia..Amiin

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua**: 'Katika Siku ya Malipo Moto wa Jahannam utasogewa karibu kwa kuvutwa kwa kamba zake 70000, ambazo zitavutwa na Malaika 70000. Na hivyo basi kila aliekua akipinga juu ya Maamrisho *ya Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ataoneshwa wazi Ukali wake moto huo na Mvumo wake kabla ya hata kuingizwa ndani yake.'**

Na hali itakua ni ya kutisha sana. Na amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat Qaf aya 22 kuhusiana na Siku ya Malipo itakavyokua kua:

﴿ لَّقَدْ كُنتَ فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَٰذَا فَكَشَفْنَا عَنكَ غِطَآءَكَ فَبَصَرُكَ ٱلْيَوْمَ حَدِيدٌ ﴾

Laqad kunta fee ghaflatin min hadha fakashafna AAanka ghitaaka fabasaruka alyawma hadeedun*(Surat Qaf 50:22)*

Tafsir: ***Wataambiwa (wenye Kukufuru katika siku ya malipo kua) Hakika nyinyi Mlikua mko katika mghafiliko juu ya Jambo hili (la Kufufuliwa) Hivyo leo Tumekuondoleeni Mifuniko (ya mtizamo wa macho) yenu Na Hivyo Mtizamo wenu utakua Leo hii ni Mkali sana***

Naam hii ni miongoni mwa aya zilizotumia neno *Ghitaa*, ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kufunika, Kuziba, Kukiweka Kitu ndani ya Kiza, Kuweka Pazia Au Guo Juu ya Kitu au nje ya Kitu ili kitu hicho kisionekane na pia hua linamaanisha Ufuniko.

Neno *Ghata* ndio lililotoa neno *Ghita* ambalo hua linamaanisha Ujahiliyah au Ujinga. Ambapo aya ya pili iliyotumia neno hili basi ni ile aya yetu tunayoiangalia leo katika *Surat Al Kahf* ambayo ni aya ya 101.

Na anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake aya hio pia kuahusiana na wale waliokufuru kuhusiana na Siku ya Malipo kua:

﴿ ٱلَّذِينَ كَانَتْ أَعْيُنُهُمْ فِي غِطَآءٍ عَن ذِكْرِى وَكَانُواْ لاَ يَسْتَطِيعُونَ سَمْعاً ﴾

Alladheena kanat aAAyunuhum fee ghita-in AAan dhikree wakanoo la yastateeAAoona samAAan*(Surat Al Kahf 18:101)*

Tafsir: ***Kwa Wale ambao Yalikua Macho yao Katika Kuzibwa/Kufunikwa Kuhusiana na Ukumbusho (wa Qur'an na Maamrisho na Maonyo yangu) Na Wakawa Hawawezi Kusikiliza***

Naam..aya inasema kua kwa wale ambao Hawakuweza kua na Subra na Ustahmilivu katika kuusikiliza Ujumbe wa Qur'an mbali ya kua si Viziwi kwani Masikio wanayo na wanasikia lakini

kutokana na Kibri chao na Ujinga wao basi wamekua si wenye kuweza kusikia chochote kuhusiana na Ujumbe wa Qur'an na mtizamo wao Umefujikwa na pazia kubwa lililokua likiuficha Juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*

Na hivyo kuanzisha Uadui mkubwa sana dhidi ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Waislam kwa ujumla basi ndio watakaosogezewa karibu Moto huo na kuoneshwa namna Unavyowaka kwa Nguvu na Ukali katika siku ya Malipo.

Kwani ni kutokana na Kusikiliza, kutafakkari, kuangalia na kuona Vithibitisho vya kuwepo kwa *Allah Subhanah wa* Ta'ala ndio kunakompelekea Ibn Adam kua ni mwenye kutoka kwenye *Ghitaa* au Funiko la Ujinga unaomzunguka katika maumbile ya Nafsi yake na mazingira yake anayoishi Duniani.

Na ndio maana aya ikawa haikusema kua Kutokana na Upofu wa Macho yao au Uziwi wao bali imesema kutokana na kufungwa kwa Macho yao na kutotaka kuona na Kuzibwa kwa masikio yao kwa kutotaka kuusikia ukweli na hivyo kua ni wenye kufanya Kufuru.

KUFR - MAANA YAKE, AINA ZAKE NA HUKMU YAKE

Anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika aya inayofuatia ambayo ni aa ya 102 ya Surat Al Kahf inayowahoji watu wanaofanya Kufuru kwa kuwahoji kwa kusema:

﴿أَفَحَسِبَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَن يَتَّخِذُواْ عِبَادِى مِن دُونِيٓ أَوْلِيَآءَ إِنَّآ أَعْتَدْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ نُزُلاً﴾

Afa<u>h</u>asiba alla<u>dh</u>eena kafaroo an yattakhi<u>dh</u>oo AAib<u>a</u>dee min doonee awliy<u>a</u>a inn<u>a</u> aAAtadn<u>a</u> jahannama lilk<u>a</u>fireena nuzul<u>a</u> *(Surat Al Kahf 18:102)*

Tafsiri: ***Hivi Jee Wanajihesabu Wale Ambao Waliokufuru kua Watawachukua Waja Wangu Zaidi yangu kua na sifa ya Uungu? Ama kwa Hakika tumewatayarishia Moto wa Jahanam Kwa Waliokufuru kua Mapokezi yao (Huo Moto wa Jahannam)***

Yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anahoji katika aya hii kua: **Hivi Kweli inawezekana Kujihesabia kwa Kiumbe kumteua Kiumbe mwenzake kua Kama Mlinzi, Msimamizi au Mungu wake?**

Wakati Viumbe hao kama Malaika; Mitume kama Nabii Isa ambao wameumbwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* wanaweza kweli kua ni sawa na Mwenyewe Muumba ambae ndie Msimamizi wa Kila kitu?

Kisha baada ya kuhoji basi aya zinamalizia kwa kuthibitisha kua kutokana na kufanya kwao huko basi Watu hao wametayarishiwa Starehe ya Moto wa Jahannam kua ndio Malipo yao, na kisha ionekane kama Miungu yao hio zaid ya *Allah Subhanah wa* kama itakua na uwezo wa kuwasaidia na kuwahifadhi kutokana na mapokezi hayo ya Jahannam.

Na tunapowazungumzia Watu waliokufuru basi kuna aina tofauti za Kufr. Na hivyo ili kufahamiana vizuri zaid basi wacha tufafanue kuhusiana na maana ya neneo Kufr na aina za Kufr na Makafiri.

Ambapo neno *Kafara* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kufunika, Kuficha, Kukataa, Kutokua na Imani, Kutokua na Shukran, Kudharau, Kuchafua, Kutia Kiza Kitu na pia humaanisha Kafara au Kusamehe.

Na neno *Kafara* ndio lililotoa neno *Kafir* ambalo humanaanisha Mtu mwenye Kulima kwa Kuibadilisha Ardhi ya Juu kuiweka chini na ya chini kuiweka juu.

Na pia humaanisha Mtu anaepanda mbegu za Mimea Ardhini na kuzifukia ndani yake na pia humaanisha Mume kwani nae hupanda Mbegu zake shambani mwa Mke wake na kuziacha ndani yake.

Na pia humaanisha Mtu anaeficha neema, faida au mafanikio aliyojaliwa kua nayo na pia neno Kafir pia humaanisha Mtu asieamini kitu fulani. Kwani Anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿لاَ إِكْرَاهَ فِى ٱلدِّينِ قَد تَّبَيَّنَ ٱلرُّشْدُ مِنَ ٱلْغَىِّ فَمَنْ يَكْفُرْ بِٱلطَّاغُوتِ وَيُؤْمِن بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱسْتَمْسَكَ بِٱلْعُرْوَةِ ٱلْوُثْقَىٰ لاَ ٱنفِصَامَ لَهَا وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ﴾

La ikraha fee alddeeni qad tabayyana alrrushdu mina alghayyi faman yakfur bialttaghooti wayu/min biAllahi faqadi istamsaka bialAAurwati alwuthqa la infisama laha waAllahu sameeAAun AAaleemun*(Surat Al Baqara 2:256)*

Tafsir: ***Hakuna Kulazimishana Katika Dini Kwani Kwa hakika Umebainishwa Uongofu Kutokana na kutofautishwa na Upotovu Na Atakaekufuru Uovu wa Ushirikina na maovu mengine Na Akamuamini Allah Basi kwa Hakika atakua ni mwenye Kuegemea Egemeo Madhubuti Ambalo kamwe Halitovunjika Na Allah ni Mwingi wa Kusikia kila kitu na Kujua kila kitu.***

Naam, hii ni aya ambayo inatuonesha maana ya Kukufuru kiimani kua Kuikufuru Miungu Myengine hua ni Jambo sahih. Lakini kumkufuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua si jambo sahih kulingana na Imani ya Dini ya Kiislam.

Kwani Imani ya Dini ya Kiislam haimtaki Muislam kua ni mwenye Kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ndie Muumba pekee, lakini pia hua inamtaka Muislam kuifuru Miungu myengine yote na kisha ndio utakua kwenye Uongofu Sahih.

Na bila ya shaka Kufr ziko aina nyingi, hivyo inabidi Inabidi tuziangalie na kutanabahishana ili tupate kuzijua na kupata kuweza kuzikimbia kwa kadri tutakavyoweza. Na bila ya Shaka ingawa tunatakiwa kuzikimbia na Kuziepuka Kufr lakini hapo hapo kuna Kufr ambayo ni nzuri kama ilivyotuonesha aya kua Kufr hio ni ya Kuikufuru Taghuti yaani kuachana na Kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuachana na Maovu na kila alilotukataza.

Na tunapoiangalia Qur'an basi tunaona kua inapozungumzia Kufr basi hua inawazungumzia watu wanaoukataa na kuuificha Ukweli mbali ya kua wanaujua. Kwani inawazungumzia wale watu ambao ni wenye kuzikataa Fadhila zake juu yao kwa kupingana na Mamlaka ya uumbaji wake.

Hivyo Kufr hua ni Kutokua na Imani na Muumba yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hii hua inajulikana kama Kufr al Akbar yaani Kufr kubwa zaid. Ambapo ndani yake aina hii ya Kufr basi hua mnajumuishwa Kufr zifuatazo:

1-*Kufr Inaad* yaani Kufuru kutokana na Ukaidi – Ambayo hua kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kua:

﴿ أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيدٍ ﴾

Alqiya fee jahannama kulla kaffarin AAaneedin *(Surat Qaf 50:24)*

Tafsir: ***(Wataambiwa Malaika) Mtupeni Motoni Kila Aliekufuru kwa Kukaidi.***

Ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na aya hii kua : **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam kua: 'Kuna shingo ambayo itaibuka kutoka kwenye Moto wa Jahannam na kusema: 'Hakika katika siku ya leo Jukumu langu nililopewa ni kwa ajili ya watu watatu ambao ni Kila Mtawala Dhali, Kila aliemshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kila alieua bila ya kua na sababu ya kisharia Kuua' kisha Moto huo utawazunguka na kuwameza watu hao''**

Ambapo *Kufrul Al Aniid* hua ni hali Mtu anaeujua Ukweli na kisha akakubaliana na Ukweli huo kwa Ulimi wake lakini akakataa kuukubali na kusema kua ameukubali.

2- *Kufr Al Inkar* ambayo ni Kufr ya Kuukataa ukweli kwa Moyo na kwa Ulimi pia. Kwani neno Inakara linatokana na neno *Nakara* ambalo hua linamaanisha Kuchukia, Kukakataa kitu kwa Moyo kwa Ulimi na kwa vitendo, Kua na Ugumu kuhusiana na jambo au kitu Fulani, Kua na upinzani mkubwa sana juu ya kitu.

3-*Kufr Al Kibr* ambayo ni Kufr inayotokana na Kua na Kibr na kujiona kama ilivyokua kwa Ibilisi alipoambiwa amsujudie Adam na akakataa.

4-*Kufr Juhuud.* Yaani Kufr inayotokana Mtu anaeujua ukweli ndani ya Moyo wake lakini akaukataa kwa kutumia Ulimi wake. Ambapo ndani yake wanaingia wale ambao ni wenye kujiita kua wao ni Waislam lakini wakawa ni wenye kutosimamisha Nguzo za Kiislam. Kwa kutofunga, kutosali, kutotoa zakka.n.k Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewazungumzia watu hawa kwa kusema kua;

﴿ وَجَحَدُواْ بِهَا وَٱسْتَيْقَنَتْهَآ أَنفُسُهُمْ ظُلْماً وَعُلُوّاً فَٱنْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ ٱلْمُفْسِدِينَ ﴾

Wajahadoo biha waistayqanat-ha anfusuhum *dh*ulman waAAuluwwan faon*dh*ur kayfa kana AAaqibatu almufsideena*(Surat An Naml 27:14)***

Tafsir: ***Na wanazikataa (Dalili zetu) Ingawa wana uhakika nazo ndani ya Nafsi zao Kwa Dhulma na Kiburi Hivyo Angalia Vipi utakua mwisho wa Mafisadi.***

5-*Kufr Al Nifaaq* - Kufr ya Unafik. Yaani hali ya Mtu ambae anajidai kua ni Muislam kwa nje lakini Moyoni mwake haamini. Hawa ndio wale ambao *Allah Subhabah wa Ta'ala* amewazungumzia kwa kusema:

﴿إِنَّ ٱلْمُنَافِقِينَ فِي ٱلدَّرْكِ ٱلأَسْفَلِ مِنَ ٱلنَّارِ وَلَن تَجِدَ لَهُمْ نَصِيراً﴾

Inna almunafiqeena fee alddarki al-asfali mina alnnari walan tajida lahum *naseeran (Surat An Nisaa 4:145)*

Tafsir: ***Hakika ya Wanafiq Watakua ndani ya Kina cha chini kabisa Ndani ya Moto Na Hawatokua na wa Kuwanusuru***

6- ***Kufr Al Istihaal-*** Yaani Kufr ya kujaribu kuyahalalisha yaliyoharamishwa na kuyaharamisha yaliyohalalaishwa.

Na hii ni kwa sababu ni kufanya hivyo hua ni sawa na kuingilia kati maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kujifanya kua ni mpinzani wake.

7-*Kufr Al Kurh* ambayo ni Kufr ya Kuchukia Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambapo yeye mwenyewe amesema kua:

﴿وَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ فَتَعْساً لَّهُمْ وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ ۞ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُواْ مَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ﴾

Waalladheena kafaroo fataAAsan lahum waaddalla aAAmalahum ; Dhalika bi-annahum karihoo ma anzala Allahu faahbata aAAmalahum. *(Surat Muhammad 47:8-9)*

Tafsir: ***Na Wale Ambao Ni Wenye Kukufuru Basi Kwa ajili yao Maangamizo Na Zitadhalilika Amali zao Hio ni Kwa Sababu Kwa Hakika wao Wanachukia Kile alichokiteremsha Allah Hivyo amezifanya Amali zao kua hazina matunda***

8- ***Kufr Istihzaha.*** Ambayo ni Kufr inayotokana na kufanya Mzaha**,**

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kwenye Qur'an kua:

﴿وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ قُلْ أَبِٱللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِءُونَ ۞ لاَ تَعْتَذِرُواْ قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ إِن نَّعْفُ عَن طَآئِفَةٍ مِّنْكُمْ نُعَذِّبْ طَآئِفَةً بِأَنَّهُمْ كَانُواْ مُجْرِمِينَ﴾

Wala-in saaltahum layaqoolunna innama kunna nakhoodu wanalAAabu qul abiAllahi waayatihi warasoolihi kuntum tastahzi-oona; La taAAtadhiroo qad kafartum baAAda eemanikum in naAAfu AAan ta-ifatin minkum nuAAadhdhib ta-ifatan bi-annahum kanoo mujrimeena*(Surat At Tawbah 9:65-66)*

Tafsir: ***Na Kama Ukiwauliza Basi Watasema Hakika ya Sisi Tunazungumza na Tunatania tu Waambie Jee alikua Ni Allah Na Aya zake Na Mtume wake nyie Ndio Mlikua Mnawafanyia Mzaha? Msitoe Visingizio Kwani Mmekufuru baada ya Kuamini kwenu Kama Ikiwa tumewasamehe Baadhi yenu Basi Tutawaadhibu Wengineo miongoni mwenu Wa Sababu ni wenye Makosa.***

9-*Kufr I'raadh* hua ni Kufr inayotokana na Kuukimbia na kuuepuka Ukweli.

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameizungumzia aina hii ya Kufr katika Qur'an pale aliposema:

﴿وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ فَأَعْرَضَ عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ إِنَّا جَعَلْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَن يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْراً وَإِن تَدْعُهُمْ إِلَى ٱلْهُدَىٰ فَلَنْ يَهْتَدُوٓاْ إِذاً أَبَداً﴾

Waman adhlamu mimman dhukkira bi-ayati rabbihi faaAArada AAanha wanasiya ma qaddamat yadahu inna jaAAalna AAala quloobihim akinnatan an yafqahoohu wafee adhanihim waqran wa-in tadAAuhum ila alhuda falan yahtadoo idhan abadan*(Surat Al Kahf 18:57)*

Tafsir: ***Na Ni Nani Mwenye Kufanya Dhulma Zaid Ya Yule anaekumbushwa Juu ya Aya Za Mola wake Lakini Akazipa Mgongo Na Kusahau Yaliyotangulizwa na Mikono yake Hakika sisi Tumejaalia Juu ya Nyoyo zao Mapazia Ili Wasiifaham Na Ndani ya Masikio yao Na Hata Kama Ukiwaita (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Katika Njia ya Uongofu Basi Hawatoongoka Hata iwe vipi kwa Milele.***

10-*Kufr Al Istbdaal.* Yaani Kufr ya kujaribu Kubadilisha Hukumu na Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo ndani yake hua mna Kufr ya Kubadilisha Sharia au Hukm ya Kitu ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* tayari ameshaweka wazi Hukmu yake juu ya Jambo Husika kisha Mtu akawa ni mwenye kutoa au kutumia hukmu za Shari zilizowekwa na Watu Au Mamlaka juu ya Jambo husika na hivyo Mtu husika kua ni mwenye Kuikataa Hukmu hio ya Muumba.

Na hapa katika Hili Waislam ndio wengi sana tunapokosea. Kwani katika kesi nyingi sana za Mirathi basi unakuta watu wanakataa Hukmu ya Mirathi ya Kiislam na kutaka Mirathi ya Kiislam ikagaiwe katika Mahkama za Kiserikali na hivyo Watu wanajiita Waislam lakini hapo hapo Wanapingana na Sharia za Allah Subhanah wa Ta'ala alieweka Sharia za Dini ya Kiislam kwa malengo Maalum ya Dini yake - Hivyo hii hua ni *Kufr Ul Istibdaal* yaani Kufr ya Kubadilisha Hukmu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Maslahi ya Kidunia

Na ndani yake Kufr hii pia kuna Kufr ya Kupinga Hukmu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* Bila ya Kuikataa..yaani mtu kusema kweli hivi ndivyo inavyotakiwa kuhukumiwa jambo husika kwa Kiislam lakini mimi siwezi kufanya Hivyo.

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anahoji kuhusiana na wale wanaofanya hivyo kwa kusema:

﴿أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُواْ لَهُم مِّنَ ٱلدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَن بِهِ ٱللَّهُ وَلَوْلاَ كَلِمَةُ ٱلْفَصْلِ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ وَإِنَّ ٱلظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾

Am lahum shuraka<u>o</u> sharaAAoo lahum mina alddeeni m<u>a</u> lam ya/<u>dh</u>an bihi All<u>a</u>hu walawl<u>a</u> kalimatu alfa<u>s</u>li laqu<u>dh</u>iya baynahum wa-inna al<u>dhdha</u>limeena lahum AAa<u>dha</u>bun aleemun *(Surat Ash Shura 42:21)*

Tafsir: **Au Wana Washirika wanaowashirikisha na Allah. Waliowaanzishia Katika Dini Yale Ambayo hayakuruhusiwa Juu yake na Allah? Na kama ingekua si kauli yenye maamuzi, basi ingekua tayari jambo hilo limeshahukumiwa baina yao tayari. Na kwa hakika kwa ajili ya Madhalimu kuna adhabu inayoumiza sana.**

Na katika aya nyengine akasema:

﴿ وَلاَ تَقُولُواْ لِمَا تَصِفُ أَلْسِنَتُكُمُ ٱلْكَذِبَ هَٰذَا حَلاَلٌ وَهَٰذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُواْ عَلَىٰ ٱللَّهِ ٱلْكَذِبَ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَىٰ ٱللَّهِ ٱلْكَذِبَ لاَ يُفْلِحُونَ﴾

Wala taqooloo lima tasifu alsinatukumu alkadhiba hadha halalun wahadha haramun litaftaroo AAala Allahi alkadhiba inna alladheena yaftaroona AAala Allahi alkadhiba la yuflihoona*(Surat An Nahl 16:116)*

Tafsir: ***Na Wala Msiseme Kuhusiana na Yanayotangulizwa na Ndimi zenu Ya Uongo Kua Hiki Halali na hili Haramu Kuzusha juu ya Allah uongo Hakika ya wale Wanaozusha Juu ya Allah Uongo Kamwe hawatofanikiwa.***

Alhamd lillah tumeangalia aina 10 za Kufr ambazo hata hivyo wengi wetu mwa waislam wa leo ni wenye Kujumuika na aina kadhaa ya Kufr hizo bila ya kujijua katika maisha tunayoishi leo mimi nawe. Na namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atuepushe nazo na atusamehe katika kila aina za kasoro zetu..*Amiin*

Kwani Wanazuoni basi wamezijumuisha aina hizi 10 za Kufr katika makundi manne makuu ambayo ndani yake mna mambo ambayo Muislam akiyafanya basi hua ni mwenye kutoka katika Uislam:

1-Kukataa Sharia na Hukmu za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

2-Kufanya mambo yanayoendana Kinyume na Uislam.

3-Kuukana Uislam.

4-Kumkashif *Allah Subhanah wa Ta'ala*, Kumkashif *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, Kuukashif Uislam na Vitabu vyake.

Ambapo amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kuhusiana na watakaokufuru bila ya kutubu kua:

﴿يَسْأَلُونَكَ عَنِ ٱلشَّهْرِ ٱلْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ وَصَدٌّ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَكُفْرٌ بِهِ وَٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِندَ ٱللَّهِ وَٱلْفِتْنَةُ أَكْبَرُ مِنَ ٱلْقَتْلِ وَلاَ يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَن دِينِكُمْ إِنِ ٱسْتَطَاعُواْ وَمَن يَرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَن دِينِهِ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُوْلَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي ٱلدُّنْيَا وَٱلآخِرَةِ وَأُوْلَٰئِكَ أَصْحَابُ ٱلنَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ﴾

Yas-aloonaka AAani alshshahri alharami qitalin feehi qul qitalun feehi kabeerun wasaddun AAan sabeeli Allahi wakufrun bihi waalmasjidi alharami wa-ikhraju ahlihi minhu akbaru AAinda Allahi waalfitnatu akbaru mina alqatli wala yazaloona yuqatiloonakum hatta yaruddookum AAan deenikum ini istataAAoo waman yartadid minkum AAan deenihi fayamut wahuwa kafirun faola-ika habitat aAAmaluhum fee alddunya waal-akhirati waola-ika as-habu alnnari hum feeha khalidoona. *(Surat Al Baqara 2:217)*

Tafsir: ***Wanakuuliza kuhusiana na Kupigana katika miezi Mitukufu (Muharram, Rajab, Dhul Qaadah na Dhul Hijja). Waambie kua: 'Kupigana ndani yake ni makosa makubwa sana, lakini kuwazuia watu kutokana na njia ya Allah, Kumkufuru Allah, na kuzuia uingiaji wa Masjid Al Haram na kuwafukuza watu wake (Mji wa Makkah) na Fitna ni Kosa kubwa zaidi kuliko Kuua. Na hawatosita kukupigeni vita nyinyi hadi pale mtakapoachana na Dini yenu.' Na yeyote yule Atakaejitoa Miongoni Mwenu Katika Dini Yake na kisha Akifa Huku akiwa Kafiri Basi Zitapotea Amali zake zote Alizozifanya Duniani Na Akhera Na Hao Ndio Watu wa Motoni Watakamokaa Milele.***

Ambapo ayah hii ilishushwa kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwatuma Masahaba zake wanane *Radhi Allahu Anhum* wakiongozwa na Abd Allah Ibn *Jahsh Radhi Allahu Anhu* ambae alimpa barua na kuwaambia kua wasiifungue hadi watakapofika katika sehemu fulani, na walipowasilik wenye sehemu hio asi wakaona kua Barua hio ilikua inawaamrisha kua wakae katika maeneo ya yaina ya Makkah na Taif kwa ajili ya kuwachunguza Maadui zao. Na pia ilikua ikiwaamrisha kua kila mmoja miongoni mwao ana khiari ya kubakia katika kutekeleza amrisho la ujumbe huo au kurudi kwani jukumu hilo lilikua ni zito na lenye kuhatarisha maisha yao kila mmoja miongoni mwao, kwani watu wa Makkah walikua wakiwakamata Waislam basi wanawaua.

Lakini baada ya kuisoma barua hio basi Masahab hao wanane wakakubaliana kua hakuna hata mmoja miongoni mwa atakaerudi, bali wote watabakia pamoja na kutekeleza amrisho hilo la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Ambapo katika usiku wa mwishoni wa mwezi wa *Jumada Thani* Masahaba hao wakauvwamia msafara mdogo wa watu wa Makkah na wakamuua mtu mmoja aitwae Amr Al Hadrami na kuwateka watu wawili waliobakia na kurudi nao katika Mji wa Madina na mali walizoziteka

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoiona hali hio basi akawauliza Masahaba zake hao kwa kusema: **'Hivi Jee sikukwambieni mimi kua msipigane katika Miezi Mitukufu?'** na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakaa akitafakari cha kufanya huku akiwa hakutoa Hukmu yeyote kuhusiana na Mateka hao wawili wala kuhusiana na kuzigawa Mali walizotekwa nazo. Ambapo tukio hili liliwachanganya sana Masahaba hao wanane na kujihesabu kua wameshangamia.

Baada ya tukio hili basi watu wa Makkah wakachukua nanfasi hio na wakaanza kumshutumu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Waislam kua ni wenye kuuvunjia heshima yake na utukufu wake mmoja kati ya miongoni mwa miezi Mitukufu ambao ni mwezi wa Rajab, wakati Abd Allah Jahsh na Masahaba wenzake *Radhi Allahu Anhum* wao wakisema kua haikua Rajabu, bali ilikua ni siku ya mwisho ya mwezi wa Jumada Thani.

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akaishusha ayah hii kwa ajili ya kudhihirisha kua hata kama imetokea kumwagwa kwa Damu ya Ibn Adam katika mmoja kati ya Miezi Mitukufu lakinihata hivyo na Makafiri nao wamefanya makosa makubwa zaidi dhidi ya Waislam kwa kuwaua, kuwazuia kungia kwenye Dini ya *Allah Subanah wa Ta'ala* kuwafukuza katika mji wa Makkah na kuwazuia kufanya

ibada ya Umra na Hija, na haya ni mambo yenye kujumuisha makosa makubwa zaidi ya yale yaliyofanywa na Masahaba hao wanane.

Na bila ya shaka Makafiri hawatosita kufanya vitimbi vyao na dhulma zao hadi pale Waislamu wakatakapo achana na Uislam na kurudi katika Ukafiri, na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akatoa onyo kwa kusema kua Muislam atakaeukana Uislam basi atakua ni mwenye kupoteza amali zake zote na kama akifa katika hali hio basi atakua ni mwenye kuingia katia maagamizi ya kuunguzwa na moto wa Jahannam ambamo atakua ni mwenye kukaa ndani yake milele.

Huu ni Mtihani mwengine ambao ni mkubwa zaid hususan kwa wale wenye kufanya Maskhara katika Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Allah Atustiri na Mitihani kama hii sisi na familia zetu..Aamin

Na tunapoangalia mitizamo ya Wanazuoni katika Kuitafsiri aya hii na kuifafanua ayah hii basi tunaona kua Wanazuoni wanakubaliana kua maneno ya aya hii yasemayo kua: ***Waman yartadid minkum AAan deenihi fayamut wahuwa kafirun faola-ika habitat aAAmaluhum fee alddunya* - Na yeyote yule Atakaejitoa Miongoni Mwenu Katika Dini Yake na kisha Akifa Huku akiwa Kafiri Basi Zitapotea Amali zake zote Alizozifanya Duniani**, basi yanamaanisha kua:

1-Kufutika kwa Amali za Ibada za Mtu husika zote alizozifanya katika wakati akiwa Muislam, yaani hata kama katoa Mlima mzima wa Dhahabu kaa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha akajitoa kwenye Uislam basi hua hakutoa kitu

2-Kubatilika kwa Ndoa ya Mtu husika alieoana na Muislam au alieolewa na hubatilika hapo hapo bila kuhitajika Talaka, wala Hukmu ya Qadhi wala Mufti wala Imam wala ushauri wa Walii, Kwa maana hio watu hao wakibakia pamoja wakati Mmoja ameshaukana Uislam basi hua ni Uzinifu tu.

3-Kufutika kwa Mirathi ya Mtu husika na hivyo Mtu huyo hua ndugu wala mzee katika Dini ya Kiislam kwani amesha ukufuru na kuukana na hivyo haruhusiki Kurithishwa kutoka katika Mali za Waislam

4-Kutostahiki Kusaliwa kwa Maiti yake wala kuzikwa kwa Maiti hio katika Makaburi ya Waislam.

Ambapo kuhusiana na Kubatilika kwa ndoa baina ya Muislam na asiekua Muislam basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema tena katika aya ifuatayo :

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِذَا جَآءَكُمُ ٱلْمُؤْمِنَاتُ مُهَاجِرَاتٍ فَٱمْتَحِنُوهُنَّ ٱللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِهِنَّ فَإِنْ عَلِمْتُمُوهُنَّ مُؤْمِنَاتٍ فَلاَ تَرْجِعُوهُنَّ إِلَى ٱلْكُفَّارِ لاَ هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلاَ هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ وَآتُوهُم مَّآ أَنفَقُواْ وَلاَ جُنَاحَ عَلَيْكُمْ أَن تَنكِحُوهُنَّ إِذَآ آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ وَلاَ تُمْسِكُواْ بِعِصَمِ ٱلْكَوَافِرِ وَاسْأَلُواْ مَآ أَنفَقْتُمْ وَلْيَسْأَلُواْ مَآ أَنفَقُواْ ذَٰلِكُمْ حُكْمُ ٱللَّهِ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo idha jaakumu almu/minatu muhajiratin faimtahinoohunna Allahu aAAlamu bi-eemanihinna fa-in AAalimtumoohunna mu/minatin fala tarjiAAoohunna ila alkuffari la hunna hillun lahum wala hum yahilloona lahunna waatoohum ma anfaqoo wala

junaha AAalaykum an tankihoohunna idha ataytumoohunna ojoorahunna wala tumsikoo biAAisami alkawafiri wais-aloo ma anfaqtum walyas-aloo ma anfaqoo dhalikum hukmu Allahi yahkumu baynakum waAllahu AAaleemun hakeemun*(Surat Al Mumtahina 60:10)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini! Watakapokuja kwenu Wanawake walioamoni kama Wahamiaji, basi wachunguzeni, kwani Allah ndie mwenye kujua zaidi kuhusiana na Imani zao, namkishahakikisha kua ni Waumini wa kweli basi msiwarudishe kwa Makafiri, kwani wao si wake wa halali kwa Makafiri na wala Makafiri si Waume halali kwao. Lakini wapeni Makafiri mahari yao waliyowalipa wanawake hao. Na hakutokua na dhambi kama mkiwaoa baada ya kuwalipa mahari yao, na pia msiwafanye Wanawake wa Kikafiri kama wake zenu na waambieni (Makafiri) wakurudishieni Mahali mliyolipia na waachieni Makafiri wadai kile walicholipia. Hio ndio hukumu ya Allah aliyoihukumu baina yenu na Allah ni mwingi wa Kujua na ni mwingi wa Hikma.***

Ambapo wanasema Wanazuoni kua kuna baadhi ya Wanawake wa Mji wa Makkah walipokua wana matatizo na Waume zao basi walikua wakiwatishia Waume zao kwa kuwaambia kua watakimbilia katika Mji wa Madina kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam nah ivy Allah Subhanah wa Ta'ala* akaishusha ayah hii.

Ambapo kwa Upande wa *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kua: **'Wanawake hao walikua wakijaribiwa kuchunguzwa kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuwauliza kua jee hawakukimbilia katika Mji wa Madina kwa sababu ya Ugomvi baina yao na Waume zao**.'

'Na kama jee hawakukimbia Mji wao kwa sababu ya Mji mwengine?' au 'Hakukimbia kwa sabbu ya kua hampendi Mume wake na anampenda Mwanamme mwengine ambae yuko katika mji wa Madina?' au 'Jee amekimbilia katika Mji wa Madina kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tu au?' na kisha Mwanamke husika atakapojibu kiusahihi basi huruhusiwa kubakia katika Mji wa Madina na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwalipia na kuwaachia huru.

Na aya hii ilishushwa kutokana na kimoja kati ya vipengele vya Mkataba wa Hudaybiyyah kisemacho kua: '**Mtu yeyote wa Mji wa Makkah atakaeingia katika Uislam na kisha kukimbilia katika Mji wa Wa Madina basi Waislam wamrudishe katika Mji wa Makkah, na Muislam yeyote atakaeamua kurudi katika Ukafiri katika mji wa Makkah basi asirudishwe katika Mji wa Madina'**

Na *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* alitekelezea makubaliano hayo, pale kabla ya kushushwa kwa ayah hii lakini baada ya kushushwa aya hii basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ikambidi kukivunja kipengele hicho cha Mkataba huo, na miongoni mwa Watu wa mwanzo kuhifadhiwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya kushushwa kwa aya hii alikua ni Umm Kulthum Bint Uqba *Radhi Allahu Anha,* ambae hata Wazee wake walipomfuata na kudai arudishwe katika Mji wa Makka basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikataa kumkabidhi kwa Makafiri hao.

Na hali hii haikua kwa Wanawake wa Mji wa Makkah tu kwani hata wanawake wa Miji myengine walihifadhiwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama Ummu Habibah *Radhi Allahu Anha* ambae aliondoka na Mumuewe Abu Habibah na Mtoto wao kuelekea katika ardhi ya Uhabeshi na walipofika huko basi Abu Habibah akaingia kwenye Ukristo na hivyo Ummu Habibah Radhi Allahu Anha akabakia yeye na mtoto wake katika Uislam bila ya kutetereka na kisha baadae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuoa Ummu Habibah *Radhi Allahu Anha.*

Pia kuna watu kama Umaymah Bint Bishr Al Ansariyyah *Radhi Allahu Anha* ambae alikua ni Mwanamke wa Bani Aws wa Mji wa Madina, ambapo alipoingia katika Uislam basi ndoa yake na Mumewe ambae alikua ni Kafiri ikavunjka na akapewa hifadhi na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, lakini hakuolewa nae n.k.

Na kutokana na amrisho la Aya hii basi Hata Umar Ibn Al khattab Radhi Allahu Anhu aliamu akumuach make wake ambae alikua ni Kafiri anaeishia katika Mji wa Makkah aliekua akitoka katika ukoo wa Abu Umayyah Ibn Al Mughira na hivyo mwanamke huyo akaolewa na Muawwiyah Ibn Abu Sufyan katika mji wa Makkah wakati wote wakiwa Makafiri kabla ya kusilimu kwao. Na pia Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akamuacha mke wake mwengine wa ukoo wa Jarwal wa Khuzaah ambapo Mwanamke huyo akaolewa na Abu Jahm Ibn Huzaifah.

Na pia Talha Ibn Ubayd Allah *Radhi Allahu Anhu* akamuacha Arwa Bint Rabiah Ibn Harith Ibn Aabd Al Muttalib ambae akaolewa na Khalid Ibn Said Ibn Al Aas katika mji wa Makkah, n.k

Naam, hivyo tukirudi katika Ufafanuzi wetu wa Surat Al Kahf basi tunaona kua aya zinaendelea kuelezea kuhusiana na wale ambao ni wenye kula hasara katika amali zao kutokana na Kukufuru kwao kwa kusema:

﴿ قُلْ هَلْ نُنَبِّئُكُم بِٱلْأَخْسَرِينَ أَعْمَالاً ۞ ٱلَّذِينَ ضَلَّ سَعْيُهُمْ فِى ٱلْحَيَاةِ ٱلدُّنْيَا وَهُمْ يَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ يُحْسِنُونَ صُنْعاً ﴾

Qul hal nunabbi-okum bial-akhsareena aAAmalan; Alladheena dalla saAAyuhum fee alhayati alddunya wahum yahsaboona annahum yuhsinoona sunAAan *(Surat Al Kahf 18:103-104)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Jee nikuambieni Juu ya Wale waliokula hasara katika amali zao? Wale Ambao Wamedhalilisha jitihada zao Katika Maisha ya Kidunia Huku wakiwa Wanajihesabia Kua wao Wanapata Mema Kutokana na Amali zao***

Kwani Aya hizi mbili zinawazungumzia wale watu ambao miongoni mwao watu wanaojiona na kujihesabu kua wako njia sahih lakini hapo hapo hua ni wenye kumshirikisha Allah Subhanah wa Ta'ala.

Yaani Wanafanya mambo sio lakini wao ni wenye kujihesabu kua wanafannya mambo ndio Na hivyo Jitihada zao hua ni za Bure kwani hua hazina manufaa yeyote kwa maisha yao ha hapa Duniani na kesho Akhera pia.

Na Wanasema Wanazuoni kua ndani yake humu katika jumuisho la watu hawa waliokula hasara wanaingia pia wale watu ambao ni wenye nia njema katika kufanya amali zao lakini wakawa wanatumia njia sizo katika ufanyaji wa amali zao hizo.

Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna Watu watakuja katika Siku ya Malipo wakiwa wamenenepa na kujaza mizigo ya wingi wa Amali njema walizozifanya Duniani. Lakini matokeo yake zitakapohesabiwa Amali hizo mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hazitofikia hata uzito wa ubawa wa mbu'** Kwa maana hio basi ndani yake aya hii hawajumuishwi Makafiri tu bali pia hata wale Waislam wenye kufanya mambo yao kwa ajili ya kutaka sifa n kujionesha pia.

Kwani watajiona wamefanya mema mengi lakini yakiangaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi itakua hayana uzito kwani atasema *Allah Subhabah wa Ta'ala* kua haya hayakufanywa kwa ajili yangu bali yalifanywa kwa ajili ya kutaka umaarufu, kwa kutaka mamlaka ya kidunia n.k.

Kama zinavyo bainisha hivyo aya kuhusiana na watu wanaokufuru kua:

﴿ أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ بِآيَاتِ رَبِّهِمْ وَلِقَائِهِ فَحَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فَلاَ نُقِيمُ لَهُمْ يَوْمَ ٱلْقِيَامَةِ وَزْناً ﴾

Ola-ika alladheena kafaroo bi-ayati rabbihim waliqa-ihi fahabitat aAAmaluhum fala nuqeemu lahum yawma alqiyamati waznan *(Surat Al Kahf 18:105)*

Tafsir: ***Hao Ndio wale ambao Waliokufuru Aya za Mola wao Na Kukutana na Mola wao Hivyo Amali zao zimepotea Na wala hatutozipa (Hizo amali zao) Katika Siku ya Malipo Uzito wowote.***

Hivyo aya zinatuonesha kua katika siju ya Malipo hakitoangaliwa kwa thamani wala kwa uzito wala kwa Ukubwa kitu alichokifanya yule mtu ambae hakuamini Hapa Duniani. Kwani kila anachokichuma na kukipata na Kukitoa hapa Duniani basi hua hakifuki mipaka ya uhai wa maisha yake hapa Duniani hivyo mwishowe hua pale unapomalizika Uhai wake ndani ya Dunia hii. Na hivyo basi hata mtu awe na Ghorofa ngapi, awe na Ndege na kila aina ya vyombo vya usafiri wa fahari, Hata Awe ni mwenye kusaidia Mayatima na masikini kwa kuyoa Mamilioni kutokana na mali zake.

Lakini wakati hakua ni mwenye kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua ni mwenye kumkufuru basi vitu vyote hivyo hua havina thamani wala uzito wowote mbele ya Mizani ya Haki ya Siku ya Malipo mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo kwa upande mwengine basi tunaona kua Siju Moja Sahaba Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu* Anhu alipanda juu ya Mtende, na baada ya kupanda kwake basi watu akamuangalia wakaona namna miguu yake ilivyokua myembamba.

Hivyo wakaanza kumcheka kwa sababu ya uwembamba wa miguu yake. Ambapo wakati tukio hilo linatokea basi: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alikuwepo basi akasema: '**Hivi Nyinyi Mnaicheka Miguu ambayo uzito wa Amali zake utaushinda hata uzito wa Mlima wa Uhud katika siku ya Malipo?'**

Na hadith hii inaonesha kua baadhi ya watu watapimwa hadi uzito wao katika siku ya Malipo. Sasa ole wake mtu awe ni mwenye kula haram kwani uzito wa mwili wake hua ni wenye kumjazia Dhambi tupu. Allah atunusuru..Amiin

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Katika siku ya Malipo atatokea Mtu akiwa amejaza sana, lakini akipimwa basi hatokua na uzito wowote zaid ya Uzito wa Ubawa wa nzi'***(Sahih Muslim)*

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Wema miongoni mwa Wafuasi wangu, basi ni wale waliomo kwenye wakati wa kizazi changu, Kisha wale wanaofuatia, na kisha watakowafuatia, Na baaadae watakuja watu ambao watatoa shahada bila ya kuambiwa kua washuhudie Watu hao watakua hawaaminiki, na wasiotekeleza ahadi wala viapo na watakua na Matumbo makubwa***(Sahih Bukhari)*

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يُدۡخِلُ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ وَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ يَتَمَتَّعُونَ وَيَأۡكُلُونَ كَمَا تَأۡكُلُ ٱلۡأَنۡعَٰمُ وَٱلنَّارُ مَثۡوٗى لَّهُمۡ﴾

Inna Allaha yudkhilu alladheena amanoo waAAamiloo alssalihati jannatin tajree min tahtiha al-anharu waalladheena kafaroo yatamattaAAoona waya/kuloona kama ta/kulu al-anAAamu waalnnaru mathwan lahum *(Surat Muhammad 47:12)*

Tafsir: ***Hakika ya Allah Atawaingiza wale walioamini na Wakafanya Mema Peponi Mnamo tiririka Mito ya Maji chini yake na kwa wale ambao waliokufuru wakiwa wanajistarehesha Na Kula Kama Wanavyokula Kama Ng'ombe Na Moto ndio Utakaokua makazi yao.***

Ambapo aya hii inatuwekea wazi kua Kula ovyo hua sio miongoni mwa sifa za Muumini wa kweli. Kwani yeyote yule anaependa kula sana Ovyo basi hua na sifa ya kua na Ubakhili kwani hua anakifikiria tumbo lake tu. Na hivyo hua hajali kitu gani anaingiza ndani ya Tumbo lake kama ni cha Halali yake ama la.

Na hivyo mtu huyo hua mvivu kwani kila anaposhiba hua anasinzia na anapokosa kula hua ni mwenye kupata shida sana kwani hawezi kufikiria chochote isipokua kile alichokikosa yaani Chakula.

Na aya zinaendelea kuzungumzia kuhusiana na kila anaekataa Dalili za Kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kukataa maamrisho yake na kila anaefanya Kufr kwa kusema kua:

﴿ذَٰلِكَ جَزَآؤُهُمۡ جَهَنَّمُ بِمَا كَفَرُواْ وَٱتَّخَذُوٓاْ ءَايَاتِي وَرُسُلِي هُزُوًا﴾

Dhalika jazaohum jahannamu bima kafaroo waittakhadhoo ayatee warusulee huzuwan *(Surat Al Kahf 18:106)*

Tafsir: ***Hayo Ndio yatakayokua Malipo yao Motoni kutokana na Kukufuru kwao Na Kuzichukulia Aya zangu Na Mitume Yangu kua ni Vitu vya Mzaha***

Naam..tunapoziangalia aya hizi na kisha kutafakari basi tunaona kua ni wengi sana miongoni mwetu hua si wenye kujali sana kuhusiana na Vipi tunaishi katika kipindi cha Uhai wetu hapa Ulimwenguni. Kwani wengi wanajali na kutamani sana kua Kua na Majumba, kua na Mali, kua na Umaarufu, kua na Vyeo n.k

Ambapo hivi ni vitu vinavyompelekea mtu kua na urahisi wa Maisha yake hapa Duniani. Lakini si wengi ambao ni wenye kutafakkari na kujiuliza Hivi Jee vitu hivi vitaninufaisha vipi mimi na kunikaribisha karibu zaid na Mola wangu, jee vitapelekea kuniingiza mimi kwenye rehma za Mola wangu na kupata radha zake?.

Na hii ni kwa sababu kama Vitu hivyo havijakukaribisha karibu na Mola wako Na badala yake vikawa ni vyenye kukusukuma mbali zaid kutokana nae, basi unatakiwa ujue kua vitu hivyo mbali ya kua na thamani mbele ya Macho yako na Nafsi yako, lakini hata hivyo havina maana wala faida yeyote kwa

Mwili na Roho yako kwani ndivyo vitakavyokuja kuadhibiwa baada ya kufariki wako na katika siku ya Malipo.

Kwani utavitumia kwa mda mfupi hapa Duniani, sana sana kwa mda wa miaka 90 na sio zaidi. Wakati tunapozungumzia wakati wa Siku ya Malipo tu basi ni miaka 50,000 wachia mbali kipindi cha Kaburini na kisha Umilele wa kua ndani ya Jahanam.

Hivyo Muhimu kwa Kila Muislam ni kutojali kuhusiana na Mali, Cheo, Umaarufu, Mamlaka nk. Kwani vinaweza vikakuangamizia Akhera yako. Na amesema *Allah Subhanah wa Ta'aala* kua:

﴿ مَّثَلُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ بِرَبِّهِمْ أَعْمَالُهُمْ كَرَمَادٍ ٱشْتَدَّتْ بِهِ ٱلرِّيحُ فِى يَوْمٍ عَاصِفٍ لاَّ يَقْدِرُونَ مِمَّا كَسَبُواْ عَلَىٰ شَيْءٍ ذَٰلِكَ هُوَ ٱلضَّلاَلُ ٱلْبَعِيدُ ﴾

Mathalu alladheena kafaroo birabbihim aAAmaluhum karamadin ishtaddat bihi alrreehu fee yawmin AAasifin la yaqdiroona mimma kasaboo AAala shay-in dhalika huwa aldhdhalalu albaAAeedu*(Surat Ibrahim 14:18)*

Tafsir: ***Mfano wa wale ambao Wenye Kumkufuru Mola wao Basi Amali zao hua Kama Namna Jivu Linavyopulizwa kwa Nguvu Na Upepo Katika Siku ya Kimbunga Hawatoweza Kudhibiti chochote katika Waliyoyachuma Huo hua ni Udhalili wa Mbali sana (kutoka katika ya Uongofu)***

Kama tunavyoona kua aya zinatudhihirishia kua Mtu yeyote yule mwenye Kufanya Kufuru na basi Amali zake hua kama Jivu lililomwagwa uwanjani katika siku ya Kimbunga. Ambapo hii ni Mithali inayotutaka Tutafakari na kisha tujijibu wenyewe kua Jee Kimbunga kikipita kwenye sehemu ambayo imejaa Jivu hata lenye ukubwa wa kama mlima, jee itawezekanaje Kulidhibiti Jivu hilo ili lisipeperuke?

Baada ya maonyo hayo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawaahidi na kuwabashiria waja wake watiifu malipo yalio bora ya *Firdaws Nuzulan* katika siku ya Malipo kwa kusema kua:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّالِحَاتِ كَانَتْ لَهُمْ جَنَّاتُ ٱلْفِرْدَوْسِ نُزُلاً﴾

Inna alladheena amanoo waAAamiloo alssalihati kanat lahum jannatu alfirdawsi nuzulan *(Surat Al Kahf 18:107)*

Tafsir: ***Hakika ya wale ambao Walioamini Na Wakafanya mema Basi Kwa Hakika Kwa ajili yao kuna Bustani za Firdaus kwa Kustarehea tu.***

Neno la Kiarabu *Fardasa* hua linamaanisha Kumhisi Mtu au Kitu, Kuhisi Maumivu hadi kufikia kujipinda na Kusjudu kutokana na maumivu hayo, Kuanguka chini kwa Muanguko mkubwa sana, kama yanavyoanguka Matunda kutoka Juu ya Mti, Kutawanyika Ardhini.

Neno *Fardasa* limetoa neno *Fardasatun* ambalo humaanisha Upana Mkubwa sana wa Kitu, Wingi mkubwa sana wa vitu tofauti vilivyosambaa Ardhini

Na pia likatoa neno *Fardasan* ambalo humaanisha Kua na ukubwa na upana mkubwa sana. Neno *Fardasa* ndio lililotoa neno *Firdaws* ambalo ni lenye kumaanisha Ardhi yenye Rutba Nyingi sana isiyokua na mwisho.

Na pia humaanisha Bustani ambayo imenawiri kutokana kua ni yenye kuota kila aina ya mimea ndani yake. Na pia humaanisha sehemu ya Ardhi ya Bonde lenye Rutba nyingi sana na hivyo kuweza kuzalisha mazao mengi ya kila aina.

Kwani *Firdaws* pia hua ni Sehemu bora zaidi iliyomo ndani ya Pepo ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliyowajaalia waja wake watiifu na wenye kumpenda na yeye akawa ni mwenye kuwapenda na kuwaridhia.

Na Sehemu hio ya *Firdaws* ambapo kwa wingi hua ni Faradis basi imeitwa *Firdaws* kwa sababu ndani mna Bustani yenye kila aina ya Miti na Mimea na Vyakula na Matunda, Mito Maziwa n.k..yaani kila unachokitaka basi kimo kwa wingi sana ndani yake.

Ambapo tunapoiangalia aya hii tunaona pia imetumia neno *Nuzulan* ambalo limetokana na neno *Nazala.*

Neno *Nazala* hua linamaanisha Kushuka, Kuteremka, Kutokea, Kunawirisha au Kukaa kwenye sehemu.

Na neno *Nazala* ndio lilitoa neno *Nuzula* ambalo humaanisha Zawadi, Tunu au Kitu kinachotayarishwa kwa ajili ya Kuwastarehesha na kuwafurahisha Wageni waliowasili kwa mwenyeji wao na kua ni wenye kuthaminiwa sana na mwenyeji wao

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na *Janat Firdaws Nuzulan* kua: **'Muislam anatakiwa awe Kila siku ni mwenye kuomba kuingizwa kwenye Janat Firdaws,kwa sababu hii ndio Pepo ya Hali ya Juu Kabisa, na Juu yake ndio kuna Arshi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mito yote minne ya Peponi ina chanzo chake ndani ya Jannat Firdaws'***(Sahih Bukhari)*

Kwani amesema Ubaidah Ubn Samit Radhi Allahu Anhu kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *Janat Firdaws* ina Darja 100 ambazo zimejaandaliwa kwa ajili ya waliopigana Jihadi kwa ajili ya *Allah Subhabah wa Ta'ala* Ambapo baina ya Kila Darja basi Upana wake na Ukubwa wake hua ni sawa na Upana wa masafa ya baina ya Mbingu na Ardhi Hivyo Mnapomuomba A*llah *Subhanah wa Ta'ala* basi muombeni Firdaws kwani ndio Pepo bora na ya Juu Kabisa Kama nnavyoiona mimi kua juu yake kuna Arsh ya Rahmani Na kutoka ndani yake basi ndio Chemchem za Peponi zinatiririkia***(Sahih Muslim)*

Kwani miongoni mwa Mashahidi wa Vita vya Badr alikuwemo yule Sahaba aitwae Haritha Ibn Suraqa *Radhi Allahu Anhu.* Ambapo baada ya kumalizika vita hivyo na kujulikanaa kua yeye ni miongoni mwa waliofuzu kupata Ushahidi wa vita hivyo basi Mama yake Haritha *Radhi Allahu Anhu* alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema; '**Hivi Jee Mtoto wangu atakua katika hali gani katika siku ya Malipo?'**

Ambapo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akajibu kwa kusema: '**Ummu Haritha, Hakika ya Firdaws basi ina Jannat nyingi sana, na mtoto wako ameifikia Darja ya juu kabisa ya Jannat'***(Imam Bukhari)*

Naam..bila ya shaka kutokana na Uwezo wake *Allah Subhanah wa Ta'al*a Na utukufu wa Majina yake Matukufu na Ubora wa sifa zake Tukufu zikiwemo sifa ya Uadilifu, sifa ya Usimamizi juu ya Kila Kitu, Sifa ya Utajiri kuliko yeyote, Sifa ya Ufalme wa juu ya Kila kitu n.k

Basi bila ya shaka kila mmoja alieahidiwa Jannat Firdawsna kila mwenye kufanikiwa kuifikia kuipata Jannat Firdaws Kulingana na Darja yake basi kila mmoja atapata Jannat Firdaws yake yenye ukubwa wa masafa ya baina ya Mbingu na Ardhi kama alivyoahidi *Allah Subhanah wa Ta'ala*, kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye uwezo wa kutekeleza ahadi hio bila ya yeye kupungukiwa na kitu chochote ikiwemo Darja hizo za Pepo.

Nami Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atuingize kwenye Rehma zake ili tuwe miongoni mwa watu wa Jannat Firdaws Nuzulan..Amiin

Allah Subhanah wa Ta'ala anatuainishia hali ya Waja wake wema wanaomtii na watakaopokewa kwa Mapokezi Matukufu ya Jannat Firdaws Nuzulan kwa kusema kua hali ya watu hao itakua:

﴿ خَالِدِينَ فِيهَا لاَ يَبْغُونَ عَنْهَا حِوَلاً ﴾

Kh<u>a</u>lideena feeh<u>a</u> l<u>a</u> yabghoona AAanh<u>a</u> <u>h</u>iwal<u>a</u>n*(Surat Al Kahf 18:108)*

Tafsir: ***Watakaa Ndani yake Milele Na Wala Hawatokua na Hamu Ya Kutaka Kutolewa Ndani yake.***

Aya yetu inaelezea hali ya watu hao kua ***l<u>a</u> yabghoona AAanh<u>a</u> <u>h</u>iwal<u>a</u>n*** yaani ***Na Wala Hawatokua na Hamu Ya Kutaka Kutolewa Ndani yake.***

Ambapo neno *Hiwalan* limetokana na Neno *Hala* ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye kumaanisha Kubadilishwa, Kua baina ya Hali mbili au mambo mawili, Kukipita Kitu.

Neno Hala ndio lililotoa pia neno *Hila* ambalo humaanisha Kizingiti kikichopo baina ya pande mbili tofauti. Na pia likatoa neno Hawla ambalo humaanisha Mwaka au Mzunguko wa Wakati wa Kitu. Hivyo Hawlain hua ni wakati wa Miaka miwili.

Na Kadhalika neno *Hala* ndio lilitoa neno *Hiwala* ambalo humaanisha Kutoroka kutoka katika sehemu fulani, Kutoka nje ya Kitu au ya sehemu, Kubadilisha sehemu.

Allah atujaalie kua miongoni mwao watu hao ambao Raha ya Milele watakayokua nayo ndani yake Peponi basi hawatokua na hata hamu ya kutoka ndani yake.

Ambapo anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Jarir At Tabari kua: **‘Wamesema Masahaba *Radhi Allahu Anhum* kua: Mtu wa Kwanza kuingia Peponi atakua ni mwenye kusema kua: Inawezekana mimi nimekua ndie mtu wa Mwanzo kuingizwa Ndani yake kwa sababu hakuna mtu aliefanya Amali njema na bora kama mimi. Na mtu wa Mwisho Kuingizwa Peponi atasema Mola wangu amenijaalia mimi kuingia Mwisho Peponi kwa sababu Hakuna Mtu aliejaaliwa kupewa Pepo Nzuri kama niliyopewa Mimi.’**

Yaani hali ya Kila Jannati Firdaws Nuzula hua na Uzuri na Raha za Kipekee kiasi ya kua Kila atakaeingia ndani yake basi atajihisi kua yeye ndie aliependelewa vizuri zaidi na kwa Ubora zaid.

Naam..hii pia inatuonesha na kutusisitizia Sifa Tukufu za *Al Adil* yaani Uadilifu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, *Al Qayyum* yaani mwenye Usimamizi Kamilifu juu ya Kila kitu, *Al Ghanniyu* Mwenye Utajiri wa Kila kitu, asiehitaji Kitu na kutopungukiwa na kitu.

Hivyo Hata Waja wake wema Wawe wangapi lakini Kila Mtu atamlipa kwa Uadilifu na kwa Usimamizi Kamilifu kiasi ya kua kila mmoja ataona kua amependelewa zaid na wala *Allah Subhanah wa Ta'ala* hatopungukiwa na Kitu kutokana na Kutoa kwake huko kuwalipa Waja wake hao.

Baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuelezea Yote yaliyomo ndani ya Surat Al Kahf na kujibu hoja za Makafiri kuhusiana na Fityatun au As-hab Al Kahf, Al Khidr na Dhu Al Qarnah, Yajuj wa Majuj na yatakayowafika wale wanaompinga na watakayolipwa wale wenye kumtii basi anamalizia Sura hii Tukufu kwa kusema kua:

﴿قُل لَّوْ كَانَ ٱلْبَحْرُ مِدَاداً لِّكَلِمَاتِ رَبِّي لَنَفِدَ ٱلْبَحْرُ قَبْلَ أَن تَنفَدَ كَلِمَاتُ رَبِّي وَلَوْ جِئْنَا بِمِثْلِهِ مَدَداً﴾

Qul law kana albahru midadan likalimati rabbee lanafida albahru qabla an tanfada kalimatu rabbee walaw ji/na bimithlihi madadan*(Surat Al Kahf 18:109)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam kuwaambia Ibn Adam kua) Lau Kama Bahari ingekua Ni Wino Wa Kauli za Mola Wangu Basi kwa Hakika Ingemalizika Bahari Kabla ya Kumalizika Kauli za Mola wangu Na Hata Kama Ingeletwa(Bahari Nyengine) Mithili yake Zaidi yake.***

Hivyo zinatuwekea wazi Moja kati ya Sifa Tukufu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni Sifa ya Al Aliimun. Yaani Mwenye Kujua Juu ya Kila Kitu, kutokana na Ukubwa wa Ilm yake juu ya Kila Kitu Ambayo ni yenye Miujiza ndani yake.

Na ili kupata mfano mzuri wa kufahamu ukubwa wa Ilm ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi tukumbuke namna Al Khidr alipomwambia Nabii Musa baada ya kumuona ndege alietua na Kunywa Maji yanayopita mbele yao ambapo Al Khidr alisema kua: **Ukubwa wa Ilm ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kulingana na Ilm yetu sisi basi kwetu sisi hua ni sawa yale maji aliyoyachoukua ndege kwenye mdomo wake tu.'**

Na Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali nae akasema kua Kama Ilm ya *Allah Subhabah wa Ta'ala* itakua ni Bahari basi Ilm yetu sisi viumbe hua ni sawa na Kuchukua Sindano na kuichovywa kwenye Bahari hii na kisha Maji yatakayobakia kwenye sindano ndio Ilm yetu sisi viumbe wake. Yaani mbali ya kua na maendeleo ya hali ya Juu na kuvumbua kila kila kitu Kinachotumika sasa hivi na baada katika ulimwengu wetu basi hata hivyo bado sisi Ilm yetu mbele yake Muumba ni kama Mvuke utakaochokuliwa na Sindano baada ya kuchovywa ndani ya Maji ya Bahari.

Ama kwa waliokua hawajafahamu basi na tuchukulie mfano mwengine kwa kuangalia namna Allah Subhanah wa Ta'ala alivyotuumba sisi kutokana na Udongo. Ambapo Udongo kwetu sisi basi tumejitahid sana basi tukipewa Udongo basi tutatengeneza Tofali. Na ukweli ni kua Ibn Adam na

Ujeuri wao na kujifanya kujua kwao kote basi kila kitu chao wanachokifanya hua ni kutokana na Kufuata Mifano ya viumbe walioumbwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ukiangalia Gari zote mbele zina muonekano wa Nyuso za Wanyama mbali mbali Taa ndio Macho n.k Ukiangalia Pikipiki kama wanyama wa miguu minne miwili ya mbele na miwili ya nyuma na katikati tumbo ndio kuna injini, Ndege kama Ndege, Helicopter kama Barkoa, Meli kama samaki, Makreni ya Kubebea Mizigo kama Mdudu vunja jungu, Rocket na Torpedo kama Mchupo wa Manii, n.k

Na kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Sahil Al Tustari basi yeye anasema kuhusiana na aya hii kua: **'Qur'an Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni sehemu ya Ilm ya *Allah Subbanah wa Ta'ala,* na hivyo hata kama Mja atapewa Njia 1000 za Kuifahamu kila herufi moja ya Qur'an, basi kamwe hatoufikia hata kidogo Ukubwa wa Ilm ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'**

Na hii ni Kwa sababu pia hakuna hata moja kati ya Sifa Tukufu zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni yenye kua na sifa ya kua na mwanzo au kua na mwisho kama vile alivyokua yeye mwenyewe kwa Utukufu wake kwani hana mwanzo na wala hana mwisho na yeye ndie wa Mwanzo na ndie wa Mwisho.

Kisha Aya za Sura yetu zinamalizia kwa kusema kua:

﴿قُلْ إِنَّمَآ أَنَاْ بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَآءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحاً وَلاَ يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدَا﴾

Qul innam<u>a</u> an<u>a</u> basharun mithlukum yoo<u>ha</u> ilayya annam<u>a</u> il<u>a</u>hukum il<u>a</u>hun w<u>ah</u>idun faman k<u>a</u>na yarjoo liq<u>aa</u> rabbihi falyaAAmal AAamalan <u>sa</u>li<u>h</u>an wal<u>a</u> yushrik biAAib<u>a</u>dati rabbihi a<u>h</u>dan*(Surat Al Kahf 18:110)*

Tafsir: ***Waambie (tena ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Hakika Mimi Ni Mtu Kama Nyinyi Imeshushwa Juu yangu Kua kwa Hakika Mungu wenu Ni Mungu Mmoja Hivyo kwa Yeyote yule mwenye Kutumai Kurudi Kukutana na Mola wake Basi na Afanye Amali Njema Na Wala Asishirikishe Katika Ibada Za Mola wake Na Yeyote.***

Naam..Hii ndio aya ya Mwisho ya Surat Al Kahf ambayo ni Aya ya 110. Ambapo tunapoiangalia vizuri aya mbili hizi za mwisho Na kisha tukarudi nyuma mwanzoni mwa kitabu hiki tulipoanza kuigusa aya ya kwanza ya Sura hii na historia yake na tafsiri yake basi tunaona kua Aya ya kwanza imeanza na Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kumshukuru kaa Kumtumia Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kitabu cha Qur'an pale iliposema:

﴿ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ ٱلْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَل لَّهُ عِوَجَا﴾

Al<u>h</u>amdu lill<u>a</u>hi alla<u>dh</u>ee anzala AAal<u>a</u> AAabdihi alkit<u>a</u>ba walam yajAAal lahu AAiwaj<u>a</u>n *(Surat Al Kahf 18:1)*

Tafsir: ***Shukrani Zote Anastahiki Allah (Subahanh wa Ta'ala) Ambae Ameshusha Kwa Mja Wake Kitabu Bila Ya Kukijaalia Ndani Yake (Kitabu hicho) AAIWAJAN (Kasoro, Upotovu, Ugumu, Uchafu n.k)***

Tumefahamiana sijui ama la? Yaani tukiangalia Aya ya Kwanza ya Sura hii tuliyoianza miezi minane iliyopita na Aya ya Mwisho tunayoiangalia leo basi tunaona kua zinaendana sambamba kimaana kwa Upande wa Kufungulio na Kifungio cha Sura.

Kwani Aya ya Kwanza inathibitisha Juu ya kuwepo *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kua yeye ndie aliemtuma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Kumtumia Kitabu kisichokua na Ubaya ndani yake.

Na aya hii ya Mwisho inathibitisha kwa kumuamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aseme kua yeye ndie Mtume Mwenyewe alieshushiwa Kitabu cha Qur'an chenye kuthibitisha kua Mungu ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee. Na hivyo haitakiwi kumshirikisha Kiibada.

UTHIBITISHO WA UTUME WA RASUL ALLAH SALALLAHU ALAYHI WA SALAM

Hivyo aya ya mwisho ya Surat Al Kahf inasema:

﴿قُلْ إِنَّمَآ أَنَاْ بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَآءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحاً وَلاَ يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدَا﴾

Qul innama ana basharun mithlukum yooha ilayya annama ilahukum ilahun wahidun faman kana yarjoo liqaa rabbihi falyaAAmal AAamalan salihan wala yushrik biAAibadati rabbihi ahadan*(Surat Al Kahf 18:110)*

Tafsir: ***Waambie (tena ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Hakika Mimi Ni Mtu Kama Nyinyi Imeshushwa Juu yangu Kua kwa Hakika Mungu wenu Ni Mungu Mmoja Hivyo kwa Yeyote yule mwenye Kutumai Kurudi Kukutana na Mola wake Basi na Afanye Amali Njema Na Wala Asishirikishe Katika Ibada Za Mola wake Na Yeyote.***

Na ingawa hii ni aya ya mwisho ya Sura hii lakini hapa sio mwisho wa Ufafanuzi wa Sura hii na hii ni kwa sababu, hii aya ya mwisho tu imejumuisha mambo mengi ndani yake, hivyo jitajaribu kuyafafanua kwa kadri tutakavyojaaliwa na kwa kadri tutatakavyo weza kuzama ndani yake.

Ambapo kwa kuanzia basi tunaona kua ndani yake aya hii basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaamrishwa kua aseme kua yeye ni Basharun Mithluna pale iliposema: **Qul Innama ana Basharun Mithlukum - Waambie kua kwa Hakika mimi ni Bashara kama nyinyi.**

Hivyo ili tufahamiane vizuri zaid basi tuanze na maana ya neno hili *Bashar.* Ambapo neno *Bashar* linatokana na neno *Bashara* lenye kumaanisha Kuonesha Ngozi, Kuondoa Gamba la Nje, Kuondoa Gome la Nje la Kitu. Neno *Bashara* hua pia linamaanisha Muonekano wa Maumbile ya Nje ua Mwili, Sehemu ya Nje ya Mwili inayoonekana na kwa macho.

Nataka tufahamiane kua neno *Bashara* hua ni Tofauti na neno Insan. Kwani ingawa yote hua yanatafsirika kama Kiumbe Mtu au Ibn Adam lakini anapozungumziwa Insan basi hua inamaanisha Maumbile Kamilifu ya Ibn Adam kuanzia ndani ya Mifumo ya ufanyaji kazi ya ndani ya Mwili wake Ikiwemo Mifumo ya Hewa, Damu, Ukuaji, Mawasiliano ndani ya Mwili na nje ya mwili, Ulinzi wa Mwili, Hisia zake za kimaumbile, Ufanyaji kazi wa Viungo vya ndani ya Mwili na nje ya Mwili, n.k

Lakini inapozungumziwa kuhusiana na *Bashar* basi hua panazungumziwa Muonekano wa Maumbile ya Nje ya Mwili wa Ibn Adam na Mfumo wa Mawasiliano ya ufanyaji kazi wa Viungo vya nje ya Mwili vinavyoonekana kwa macho.

Hivyo basi sifa ya Insan hua inajumuisha Maumbile Kamilifu ya Ndani ya Ibn Adam na Mifumo yote ya Ufanyaji kazi wa ndani na nje ya mwili na muonekano wa Maumbile yake. Lakini *Bashar* hua ni Umbo la nje tu. Na hii inabainishwa na aya pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipotaka Kuumba mwili wa Nabii Adam kabla ya kumpulizia Roho yake kwa kusema:

﴿وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلآئِكَةِ إِنِّي خَالِقٌ بَشَرًا مِّن صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ﴾

Wa-idh qala rabbuka lilmala-ikati innee khaliqun basharan min salsalin min hama-in masnoonin *(Surat Al Hijr 15:28).*

Tafsir: ***Na (kumbuka) wakati Mola wako alipowaambia Malaika. Hakika mimi nitamuumba Bashar kutokana na udongo wa mfinyanzi wenye asili ya weusi.***

Na pia pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* alipompelekea Maryam Bint Imran Malaika Jibril ili kumbashiria juu ya Nabii Isa basi aya zinasema kua:

﴿وَٱذْكُرْ فِي ٱلْكِتَابِ مَرْيَمَ إِذِ ٱنتَبَذَتْ مِنْ أَهْلِهَا مَكَاناً شَرْقِياً ۞ فَٱتَّخَذَتْ مِن دُونِهِم حِجَاباً فَأَرْسَلْنَآ إِلَيْهَآ رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَراً سَوِيّاً ۞ قَالَتْ إِنِّيۤ أَعُوذُ بِٱلرَّحْمَٰنِ مِنكَ إِن كُنتَ تَقِيّاً ۞ قَالَ إِنَّمَآ أَنَاْ رَسُولُ رَبِّكِ لأَهَبَ لَكِ غُلَماً زَكِيّاً﴾

Waodhkur fee alkitabi maryama idhi intabadhat min ahliha makanan sharqiyyan; Faittakhadhat min doonihim hijaban faarsalna ilayha roohana fatamaththala laha basharan sawiyyan; Qalat innee aAAoodhu bialrrahmani minka in kunta taqiyyan; Qala innama ana rasoolu rabbiki li-ahaba laki ghulaman zakiyyan *(Surat Maryam 19:16-19)*

Tafsir: ***Na ametajwa katika kitabu, Maryam, wakati alipojitenga kutokana na familia yake katika sehemu inayoelekea upande wa Mashariki; Akaweka pazia kabla yao, kisha tukamtumia Ruhi (Malaika) wetu alietokea mbele yake katika umbo la mtu aliejaa heshima; Nae akasema: 'Hakika mimi ninajilinda kwako na kwa Mwingi wa Rehma, ikiwa unamuogopa Allah'; Nae (Malaika) akasema: 'Mimi ni mjumbe kutoka kwa Mola wako, (kukubashiria kua) utapata mtoto alie mwema'.***

Kwa Maana hio basi Malaika Jibril alimtokea Maryam Bint Imran katika Maumbile ya Muonekano wa nje wa Ibn Adam. Na hivi ndivyo pia alivyokua akiwatokea Mitume wote pale alipokua akiamrishwa aingie kwenye Umbo la Ibn Adam.

Ama katika sehemu nyengine basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anayazungumzia Maumbile ya Ibn Adam kwa kutumia neno Insan kwa mfano kwenye aya ifuatayo:

﴿ٱلَّذِيٓ أَحۡسَنَ كُلَّ شَيۡءٍ خَلَقَهُۥۖ وَبَدَأَ خَلۡقَ ٱلۡإِنسَٰنِ مِن طِينٖ﴾

Alladhi ahsana kulla shay-in khalaqahu wabadaa khalqa al-insani min teenin; *(Surat As Sajda 32:7)*

Tafsir: **Yeye ndie ambae alieumba kila alichokiumba katika umbo bora: Alianza kwa kumuumba al*'l-insāni' (mtu)* kutokana na udongo.**

Katika kumuelezea kiumbe Adam, tunaona kua pia aya hii na nyenginezo zimetumia neno ***'Insan'*** linalotokanana mzizi wa neno *'Alif-Nun-Siin'* lenye kumaanisha sifa za kua na hisia mbali mbali za ufahamu, kua na sifa ya urafiki wa kuzungumza na kusikiliza, kua na mazoea ya kuishi kijamii, sifa ya kua na ukaribu, kua na upendo, na ucheshi n.k.

Na ndio maana *Allah Subhanahu wa Ta'ala* akasema:

﴿لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِيٓ أَحۡسَنِ تَقۡوِيمٖ﴾

Laqad khalaqna al-insana fee ahsani taqweemin*(Surat Tinn 95:4)*

Tafsir: **Kwa hakika tumemuumba *Insan* katika *Taqwim* bora kabisa.**

Tukiangalia tunaona kua aya hii mbali ya kutumia neno *Insan* lakini pia imetumia neno *Taqwim*, na kusisitiza kua ni *Taqwim* bora kabisa, neno *Taqwim* linatokana na mzizi wa neno *QA-MA* ambalo kwa kiarabu lina maana ya kua katika hali ya kusimama, kua thabiti, madhubuti, kamilika, sawia bila kua na kasoro yeyote, kua na thamani, hali ya usimamizi, hali ya ulinzi, hali ya mpangilio ulokamilika, hali ya mfumo kamili, hali ya umbo lililokamilika n.k

Hivyo basi tunaweza kusema kua neno '*Bashar*' linazungumzia mfumo uliokamilika wa mwili au hali ya umbo bora la nje la *Bani Adam* na ufanyaji kazi wa viungo mbali mbali vya mwili wake kama vile ngozi, kichwa, mdomo, masikio, macho, pua, mikono, kifua, miguu n.k umbo ambalo pia viumbe wengine kama *Malaika* hulitumia, pale wanapotumwa na Mola wao kuwaletea ujumbe *Bani Adam* walioteuliwa kupokea ujumbe na Allah *Subhanah wa Ta'ala*.

Hivyo neno *'Insan'* hua linazungumzia mfumo wa umbo uliokamilika kiubora usiokua na kasoro yeyote wa umbo la *Bani Adam* unaojumuisha pamoja mfumo wa '*Bashar*' na mfumo wa viungo vya ndani ya mwili wake unaogusia roho, *Nafsi*, moyo, ubongo, akili, mfumo wa fahamu, mfumo wa damu, mfumo wa hisia n.k na pia ufanyaji kazi wa mifumo hiyo na viungo hivyo vya ndani vikishirikiana na viungo vya nje kunakompelekea kiumbe mtu kua na hisia mbali mbali za kimwili kama kuona, kusema, kusikia, kupenda, kuchukia, kutamani, kutimiza mahitaji mbali mbali ya kinafsi, kiroho, kimwili, n.k.

Ubora, ukamilifu na uzuri wa *Insan* unaelezewa zaidi katika aya zinazofuatia:-

﴿ٱلَّذِيٓ أَحۡسَنَ كُلَّ شَيۡءٍ خَلَقَهُۥۖ وَبَدَأَ خَلۡقَ ٱلۡإِنسَٰنِ مِن طِينٖ ۞ ثُمَّ جَعَلَ نَسۡلَهُۥ مِن سُلَٰلَةٖ مِّن مَّآءٖ مَّهِينٖ۞ ثُمَّ سَوَّىٰهُ وَنَفَخَ فِيهِ مِن رُّوحِهِۦۖ وَجَعَلَ لَكُمُ ٱلسَّمۡعَ وَٱلۡأَبۡصَٰرَ وَٱلۡأَفۡـِٔدَةَۚ قَلِيلٗا مَّا تَشۡكُرُونَ﴾

Alladhee ahsana kulla shay-in khalaqahu wabadaa khalqa al-insani min teenin, Thumma jaAAala naslahu min sulalatin min ma-in maheenin; Thumma sawwahu wanafakha feehi min roohihi wajaAAala lakumu alssamAAa waal-absara waal-af-idata qaleelan ma tashkuroona *(Surat As Sajda 32:7-9)*

*Tafsir: **Ni yeye aliekifanya kizuri kila kitu alichokiumba, na akaanza kumuumba Insan kutokana na udogo. Kisha akakijaalia kizazi chake kutokana mfano bora wa maji yanayo dharaulika, kisha akamtengeneza katika hali iliyokamilika, na akampulizia ndani yake sehemu ya roho yake, na akakupeni uwezo wa kusikia na kuona na kuhisi: lakini mnashukuru kidogo tu!***

Aya hizi zinamuelezea *Insan* alivyoumbwa na kukamilishwa kwake kwa kutumia kauli isemayo '*Kisha akampulizia ndani yake Ruhi yake*' ambayo inamaanisha kua Allah *Subhanahu wa Ta'ala* alimpulizia Adam ndani yake Roho yake iliyoumbwa na Allah *Subhanah wa Ta'ala.* Hivyo neno hili *Ruh* ambalo kwa Kiswahili tunasema '*Roho*' ambayo Adam amepuliziwa hua halimaanishi kua ni kama sehemu ya Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ambayo imeingizwa ndani ya Adam. La hasha! kwani kusema, kufikiri au kufahamu hivyo hupelekea kuinga katika *Kufr*.

Allahuma nsurna Aa'la al Kafirin…Aamin

Imam Fakhr Ad Din al Razi anasema katika kufafanua maana kauli hiyo kua: '**Kwa sababu *Qur'an* imeweka wazi kua Allah *Subhanahu wa Ta'ala* ni *Ahad* (mmoja), yaani umoja uzioweza kugawika katika sehemu nyengine, na tafsiri inasema kua hii '*Ruh*' imeumbwa moja, basi sifa ya kujumuishwa kwake *Ruh* hii na Allah *Subhanahu wa Ta'ala* aliposema '*Ruh*' yangu hua ni kule kunakoelezeka kwa kiarabu kama *Idhafat at Tashrif* yaani 'kupewa sifa ya kutukuzwa', inayoonesha kua *Ruh* au Roho iliyomo ndani ya mtu huyu wa kwanza na kizazi chake chote kua ni '*Tukufu, yenye Hadhi na Thamani kubwa sana*''**.

Hivyo kwanini *Allah Subhanah wa Ta'ala* akatumia neno *Basharan* katika Aya hii, na kwanini hakutumia neno Insan. Wakati amesema katika Kitabu chake kua:

﴿لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِيٓ أَحۡسَنِ تَقۡوِيمٖ﴾

Laqad khalaqna al-insana fee ahsani taqweemin*(Surat Tin 95**:4)***

Tafsir: **Kwa hakika tumemuumba *Insan* katika *Taqwim* bora kabisa.**

Ambapo katika kumuelezea kiumbe Adam, tunaona kua pia aya hii na nyenginezo zimetumia neno **'*Insan*'** linalotokanana mzizi wa neno '*Alif-Nun-Siin*' lenye kumaanisha sifa za kua na hisia mbali

mbali za ufahamu, kua na sifa ya urafiki wa kuzungumza na kusikiliza, kua na mazoea ya kuishi kijamii, sifa ya kua na ukaribu, kua na upendo, na ucheshi n.k.

Tukiangalia tunaona kua aya hii mbali ya kutumia neno *Insan* lakini pia imetumia neno *Taqwim,* na kusisitiza kua ni *Taqwim* bora kabisa, neno *Taqwim* linatokana na mzizi wa neno *QA-MA* ambalo kwa kiarabu lina maana ya kua katika hali ya kusimama, kua thabiti, madhubuti, kamilika, sawia bila kua na kasoro yeyote, kua na thamani, hali ya usimamizi, hali ya ulinzi, hali ya mpangilio ulokamilika, hali ya mfumo kamili, hali ya umbo lililokamilika n.k

Hivyo jibu lake linaturudisha tena katika ufafanuzi wa maana ya neno *Bashar* na neno *Insan.* Yaani Kimaumbile sote Ibn Adam tuna maumbile ya Muonekano wa nje wa *Bashara* unaofanana, kiasi ya kua Ukimuona tu Ibn Adam mwenzako unajua kua huyu ni Ibn Adam, tofauti ni katika Jinsia tu, ya Kiume na ya kike.

Lakini tunapozungumzia Ki I-nsan basi ingawa sote ni ibn Adam lakini tunatofautiana Kihisia, Kiiman,n.k

Isipokua kwa Mitume, kwani wao wanatofuatiana nasi kwani wao ni wabora zaid na wasafi zaid ndani ya Nyoyo zao na hivyo Wana nuru kubwa zaid ya Imani ya Allah Subhana sa Ta'ala ndani ya Nyoyo zao na hivyo Ibilisi hathubutu hata kuwajaribu kuwasogelea ndani ya Nyoyo zao.

Ambapo kwa upande wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae ni mbora wa Viumbe basi ndio kabisaa anatofauti kubwa sana ya hali ya *Insaniyah* na Kila *Basharan* yaani Ibn Adam.

Kwa Maana hio basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemuamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aseme kua yeye ni *Basharan* kama sisi kwa sababu Muonekano wake wa Nje ni kama wa Ibn Adam wengine. Lakini hata hivyo Maumbile yake ya ndani ni tofauti na ya Ibn Adam wengine kwani yeye ni mwenye Usafi na Utukufu zaid na hivyo hata mifumo ya ndani ya mwili wake ni tofauti nasi kwa mambo mengi ikiwemo Moyo wake, Kifua chake, Ufaham wake, Nafsi yake, Hisia zake Matamanio ya Nafsi.nk

Na Allah *Subhanah Wa Ta'ala* anathibitisha tena kuhusiana na Darja za Upekee wa Mitume ambao mbali ya kua na Maumbile ya Bashar lakini hua ni wenye kuchaguliwa miongoni kutokana na utofauti wao Ki Insan kama zinavyosema aya:

﴿وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَن يُكَلِّمَهُ ٱللَّهُ إِلاَّ وَحْياً أَوْ مِن وَرَآءِ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ رَسُولاً فَيُوحِيَ بِإِذْنِهِ مَا يَشَآءُ إِنَّهُ عَلِيٌّ حَكِيمٌ﴾

Wama kana libasharin an yukallimahu Allahu illa wahyan aw min wara-i hijabin aw yursila rasoolan fayoohiya bi-ithnihi ma yashao innahu AAaliyyun hakeemun *(Surah Ash-Shuraa 42:51).*

Tafsir: ***Na Haiwi kwa Bashar(Mtu) Awe ni Mwenye kuzungumzishwa na Allah Ila kwa Njia ya Wahy Au Kwa kupitia Nyuma ya pazia Au Kwa Kumtumia Mjumbe(Malaika) Ili kumshushia Wahyi Kwa Kuidhinisha Akitakacho Hakika Yeye (Allah Subhanah wa Taa'ala) Ni Mtukufu wa Juu na ni mwingi wa Hikma.***

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anadhihirisha hapa kua haiwezekani kwa Ibn Adam yeyote kuzungumzishwa na Mola aake isipokua kwa njia Tatu ambazo ni:

Nyuma ya Pazia, yaani kusikia Sauti tu kama alivyokua akisikia Nabii Musa.

Kwa Njia ya Wahy ambayo hua ni Kumuingizia Ujumbe ndani ya Ufahamu wake Mtu husika kama vile alivyooteshwa Nabii Ibrahim katika ndoto mara 3 mfululizo kua anatakiaa amchinje Nabii Ismail.

Kwa Njia ya Kumtumia Mjumbe yaani kupitia kwa Malaika Jibril kufikisha kile kinachotakiwa afikishiwe.

Na bila ya Shaka...Mtu husika anaezungumziwa ambae ni Basharan kama Basharan wengine lakini ni Insan tofauti kwani yeye hua ni Mtume.

Hivyo mbali ya kua aya hii ya 110 ya Surat Al Kahf pia inatuwekea wazi kua mbali ya kua Nabii Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* kua na maumbile ya Bashar kama watu wengine lakini yeye kwa upande wake ni tofuati na *Insan* wengine na hii ni kwa sababu yeye ni mwenye Darja ya kua ni miongoni mwa waliochaguliaa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ajili ya kubeba jukumu maalum

Ambalo ni la Kupokea Ujumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuufikisha kwa ajili ya kuwaongoza Watu katika njia iliyonyooka. Na hivyo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuwekea wazi kua Ujumbe huo anaoupokea na kuufiiisha kua sio Ujumbe wa kutunga au kuzua utokao akilini mwake bali ni Ujumbe utokao kwa Mola wake kama zisemavyo aya:

﴿قُلْ إِن ضَلَلْتُ فَإِنَّمَآ أَضِلُّ عَلَىٰ نَفْسِى وَإِنِ ٱهْتَدَيْتُ فَبِمَا يُوحِى إِلَىَّ رَبِّىٓ إِنَّهُۥ سَمِيعٌ قَرِيبٌ﴾

Qul in <u>dh</u>alaltu fa-innam<u>a</u> a<u>d</u>illu AAal<u>a</u> nafsee wa-ini ihtadaytu fabim<u>a</u> yoo<u>h</u>ee ilayya rabbee innahu sameeAAun qareebun*(Surah Sabaa 34:50)*

Tafsir: ***Waambie (ewe Muhmamad Salalahu Alayhi wa Salam kua) Kama Ikiwa Mimi nitakua nimepotea njia Basi Kwa Hakika Itakua Ni mwenye kujipoteza Njia kwa Nafsi yangu Na Kama Ikiwa nitakua nimeongoka Basi Ni kutokana na kua nimeshushiwa Wahyi na Mola wangu Kwani kwa Hakika yeye ni mwenye kusikia kila kitu na alie Karibu sana.***

Naam..hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakua ni mwenye kukaa na kujipangia kwa Ufahamu wake kuwaongoza watu kutoka upande fulani na kuwapeleka upande fulani kama wanavyofanya Wanasiasa kua sasa hivi tuwachote watu akili kwa kuwahamishia macho yao na masikio yao katika Jambo fulani ili wapate kulisahau Jambo fulani linalosumbua n.k

Au Wasanii labda pale inapokua hawajasikika basi huamua kufanya vituko tu ili wawe midomoni mwa watu na hivyo kuwapandia watu kwa juu zaid ndani ya akili zao, n.k

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* anathibitisha tena kuhusiana na Ayasemayo *Rasul Allah Salallahu Aayhi wa Salam* kua:

﴿ وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰ ۞ إِنْ هُوَ إِلاَّ وَحْيٌ يُوحَىٰ﴾

Wama Yantiqu aAa'ni Al Hawa, In Huwa Illa Wahyun Yuuha*(Surat An Najm 53:4)*

Tafsir: ***Na wala Hasemi (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Kutokana na Matamanio yake Bali hayo Ayasemayo (si chochote isipokua) Ni Wahyi Ashushiwao***

Allah Subhanah wa Ta'ala anaendelea kuthibitisha kuhusiana na kuchaguliwa kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kumfikishia Ujumbe wake kwa Watu mbali ya kua yeye mwenyewe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni mwenye kujua kuhusiana na Imani ndio nini kwa kusema:

﴿وَكَذٰلِكَ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ رُوحاً مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنتَ تَدْرِى مَا ٱلْكِتَابُ وَلاَ ٱلإِيمَانُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ نُوراً نَّهْدِى بِهِ مَن نَّشَآءُ مِنْ عِبَادِنَا وَإِنَّكَ لَتَهْدِيۤ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ۞ صِرَاطِ ٱللَّهِ ٱلَّذِى لَهُ مَا فِى ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَا فِى ٱلأَرْضِ أَلاَ إِلَى ٱللَّهِ تَصِيرُ ٱلأُمُورُ﴾

Wakatdhalika awhaynа ilayka roohan min amrinа mа kunta tadree mа alkitabu walа al-eemanu walakin jaAAalnahu nooran nahdee bihi man nashao min AAibadinа wa-innaka latahdee ilа siratin mustaqeemin; Sirati Allahi alladhee lahu mа fee alssamawati wamа fee al-ardi alа ilа Allahi taseeru al-omooru. *(Surah Ash-Shuraa : 42:52-53).*

Tafsir: ***Na Kadhalika Tumekushuhia juu yako (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Wahy na Rehma kutoka katika Amrisho letu Bila wewe Mwenyewe kujua Hata Kitabu ni nini Na Wala ni nini Imani Lakini Sisi tukakijaalia (Kitabu cha Quran kua ni) Nuru Ya Kumuongoza Kutokana nayo tumtakae Katika Waja wetu Na Kwa Hakika wewe (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Ni mwenye Kuwaongoza (Watu) Katika Njia iliyonyooka njia Ambayo Ya Yule Mwenye Umiliki wa Kila kikichomo Mbinguni Na Kila kilichomo Ardhini Na kwa Hakika Kwa Allah ndio kwenye Marudio ya Kila kitu***

Naam..hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaweka wazi kua mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakua ni mwenye kujua kua hata kitabu ni nini na Imani ndio nini lakini kutokana na kuchaguliwa kwake Kua ni kiongozi wa Watu.

Basi amejaaliwa Kitabu cha Qur'an kua ni Nuru inayomuongoza yeye na hivyo yeye kuwaongoza watu katika Njia sahih ya kumuelekea *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kua ni wenye kupata Usalama katika siku ya Malipo.

Kwani usalama huo hupatikana kutokana na Rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa wale awatakao kua waupate kutokana na kumuanini kwao na kutokana na Rehma na Huruma zake juu yao.

Ambapo kwa wale watakaopinga na kutomuamini basi hawatokua na Usalama pale watakaporudi kwa Mola wao bali watakumbana na Adhabu kali kutokana na Ghadhabu za *Allah Subhabah wa Ta'ala* juu yao.

Allah Subhanah wa Ta'ala anaendelea kuthibitisha tena kuhusiana na Umuimu wa Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika aya za mwanzoni za Surat Yasin ambapo tunapoangalia basi tunakutana na aya zisemazo:

﴿بِسْمِ اللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ يسٓ ۞ وَٱلْقُرْآنِ ٱلْحَكِيمِ ۞ إِنَّكَ لَمِنَ ٱلْمُرْسَلِينَ ۞ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ۞ تَنزِيلَ ٱلْعَزِيزِ ٱلرَّحِيمِ ۞ لِتُنذِرَ قَوْماً مَّآ أُنذِرَ آبَآؤُهُمْ فَهُمْ غَافِلُونَ﴾

Bismi Allahi Rahmani Rahim; Ya-seen; Waalqur-ani alhakeemi; Innaka lamina almursaleena; AAala siratin mustaqeemin; Tanzeela alAAazeezi alrraheemi; Litundhira qawman ma ondhira abaohum fahum ghafiloona*(Surat Yasin 36:1-6)*

*Tafsir**: Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwingi wa Huruma; Yasiin; Naapa kwa Qur'an Iliyojaa Hikma Hakika wewe (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Ni Miongoni mwa Mitume Mwenye Kua Katika Njia Iliyonyooka (Hii Qur'an) Iliyoshuhwa na Mwenye Utukufu na Wingi wa Rehma Ili (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) uwaonye Kaumu ya Watu ambao hawakuonywa Mababa zao na hivyo wakawa ni wenye Kughafilika***

Wanasema Baadhi ya Wanazuoni kuhusiana na maana ya herufi mbili za Ya na Sin zilizoachana yaani Yasiin kua hakuna anaejua Maana ya isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na pia kuna Wanazuoni wasemao kua Neno YaSiin hua ni moja kati ya Majina ya *Rasul Allah Salallahu Alahi wa Salam.* Kwani maana yake hua ni Ewe Bwana wa Bashar. Na kuna wasemao kua maana yake hua ni Mtu Mkamilifu

Ambapo baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaapa kwa Kitabu chake kitukufu cha Qur'an kwa kusema *Wa Al Qur'an Al Hakiim* – yaani Na Kwa Qur'an iliyojaa Hikma ndani yake.

Na kwa upande mwengine basi neno Hakim hua pia ni sifa yenye kumuelezea Mfikishaji au Mtekelezaji wa kitu kilichoainishwa kabla ya neno hili husika na hapa katika aya basi kile kilichoanzia kabla yake yaani Qur'an.

Na kwa maana hio basi tunaweza tukasema kua Mwenye Sifa ya kua ni Hakim wa Qur'an basi si Mwengine isipokua ni *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwani yeye ndie Mfikishaji wa Qur'an inayotoka kaa mwenye Sifa Tukufu ya Al Hakim Ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala,*

Na kisha aya zinaendelea kusema kaa kuthibitisha kua *Innaka Lamina Al Mursalina - Yaani Hakika Wewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* ni Miongoni mwa Mitume.

Na hivyo aya hii kua ni yenye kupingana na wale Waliokua wakipinga kuhusiana na Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mbali ya kua si mtu mwenye kujua kusoma wala kuandika kama ilivyoelezewa katika Surat Al Anqabut pale iliposema:

﴿وَمَا كُنتَ تَتْلُو مِن قَبْلِهِ مِن كِتَابٍ وَلاَ تَخُطُّهُ بِيَمِينِكَ إِذاً لاَّرْتَابَ ٱلْمُبْطِلُونَ﴾

Wama kunta tatloo min qablihi min kitabin wala takhuttuhu biyameenika ithan lairtaba almubtiloona*(Surat Al Anqabut 29:48)*

Tafsir: ***Mbali ya kua (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Sala.) Hukuwahi Kusoma Hapo Kabla yake Kutoka Katika Kitabu chochote kile na Wala Hukuwahi Kuandika chochote Kwa Mkono wako wa Kulia Kwani Bila ya Shaka Hao Wafuatao yaliyobatili Wangekua na shaka.***

Aya zinaweka wazi kua kama *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angekua amesoma basi bila ya shaka Makafiri wangekua na shaka nae, yaani huenda ikawa ameandika mwenyewe kwa mkono wake hii Qur'an.

Ambapo aya ya 6 ni aya yeye kuthibitisha Jukumu la Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa watu wake kwa maneno yenye kusema kua *Ma Undhira Abauhum* yaani Ambao Mababa zao hawakuonywa yanamaanisha Hali ya Upotovu waliyokua nayo watu wa kipindi cha Ujahiliyah ambayo ilikua ni hali ya upotovu wa Kurithi kutoka kwa Mababa zao.

Na hivyo kudhihirisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitumwa kwa ajili ya Kufikisha Ujumbe wa Qur'an kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kwa ajili ya kuondoa Upotovu huo wa kurithi.

Na ingawa Historia inaonesha kua Watu wa Kabila la Quraysh walikua ni wenye asili ya Nabii Ismail Ibn *Khalilu Allah Alayhi Salam* uliochanganya na Waarabu wa Yemen. Lakini hata hivyo ilikua imepita miaka mingi sana kwa karne na karne tangu kuondoka Duniani kwa Nabii Ismail Alayhi Salam. Na hivyo basi Kizazi hicho baada ya maelfu ya miaka kupita basi kikapoteza muelekeo na kutoka nje ya mafundisho ya Nabii Ibrahim.

Hivyo Nabii Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* alikuja kupitia kizazi hicho kwa ajili ya Kuwaongoza kwa kuwarudisha watu hao katika njia iliyonyooka iliyokua ikifuatwa na *Khalillu Allah* Ibrahim *Alayhi Salatu wa Salam.*

Na si hivyo tu bali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikuja pia kama Mtume wa mwisho kufikisha Ujumbe kwa Viumbe wa Duniani kutoka kwa mwenyewe Muumba yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na kwa maana hio basi jukumu la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kufikisha ujumbe huo halikuishia kwa watu wa Kabila la Quraysh tu peke yao ambao kama ilivyoeleza Aya kua walikua wameghafilika Kutokana na kurithi Imani zao kutokea kwa Mababu zao.

Bali pia Jukumu la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kufikisha ujumbe wake kwa kua ni Mtume wa mwisho basi lilikua linaanzia kwa Waarabu wa Quraysh na kisha kumalizia kumuongoza Kila mtu aliebakia Duniani baada ya Kufikishwa kwa Ujumbe huo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani aya za Qur'an zinaweka wazi kua kama *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angekua amesoma basi bila ya shaka Makafiri wangekua na shaka nae..yaani kua huenda akawa Ameaindika mwenyewe Qur'an kwa mikono yake. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'al*a baada ya kuwathibitishia

Makafiri wa Makkah kuhusiana na Kutojua Kusoma wala Kuandika kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo haiwezekani kua yeye ndie alieandika Qur'an kwa mikono yake.

Na hivyo hata kama Makafiri hao bado wanashaka kua Qur'an sio Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala basi Allah Subhanah wa Ta'ala* anatahadharisha watu hao kwa kusema:

﴿ وَلَوْلآ أَن تُصِيبَهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ فَيَقُولُواْ رَبَّنَا لَوْلآ أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولاً فَنَتَّبِعَ آيَاتِكَ وَنَكُونَ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ ❁فَلَمَّا جَآءَهُمُ ٱلْحَقُّ مِنْ عِندِنَا قَالُواْ لَوْلآ أُوتِىَ مِثْلَ مَآ أُوتِىَ مُوسَىٰ أَوَلَمْ يَكْفُرُواْ بِمَآ أُوتِىَ مُوسَىٰ مِن قَبْلُ قَالُواْ سِحْرَانِ تَظَاهَرَا وَقَالُواْ إِنَّا بِكُلٍّ كَافِرُونَ❁ قُلْ فَأْتُواْ بِكِتَابٍ مِّنْ عِندِ ٱللَّهِ هُوَ أَهْدَىٰ مِنْهُمَآ أَتَّبِعْهُ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ❁ فَإِن لَّمْ يَسْتَجِيبُواْ لَكَ فَٱعْلَمْ أَنَّمَا يَتَّبِعُونَ أَهْوَآءَهُمْ وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنِ ٱتَّبَعَ هَوَاهُ بِغَيْرِ هُدًى مِّنَ ٱللَّهِ إِنَّ ٱللَّهَ لاَ يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلظَّالِمِينَ ❁ وَلَقَدْ وَصَّلْنَا لَهُمُ ٱلْقَوْلَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴾

Walawla an tuseebahum museebatun bima qaddamat aydeehim fayaqooloo rabbana lawla arsalta ilayna rasoolan fanattabiAAa ayatika wanakoona mina almu/mineena' Falamma jaahumu alhaqqu min AAindina qaloo lawla ootiya mithla ma ootiya moosa awa lam yakfuroo bima ootiya moosa min qablu qaloo sihrani ta*dha*hara waqaloo inna bikullin kafiroona; Qul fa/too bikitabin min AAindi Allahi huwa ahda minhuma attabiAAhu in kuntum sadiqeena; Fa-in lam yastajeeboo laka faiAAlam annama yattabiAAoona ahwaahum waman adallu mimmani ittabaAAa hawahu bighayri hudan mina Allahi inna Allaha la yahdee alqawma al*dhdha*limeena; Walaqad wassalna lahumu alqawla laAAallahum yatadhakkaroona *(Surat Al Qasas 28:47-51)*

Tafsir: ***Na Kama (ingekua) hatukukutuma wewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) kwao Wao (Watu wa Makka) basi kama Ungewafika Msiba kutokana na (Madhambi) Waliyoyatanguliza kwa mikono yao wenyewe Basi wangekua ni wenye kusema Ewe Mola wetu Kwanini hukututumia Juu yetu Mtume KishaTukawa ni wenye Kufuata Aya zako na Tungekua miongoni mwa Wenye Kuamini Lakini Baada ya Ukweli (wa Ujumbe wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam) Kuwafikia Kutoka kwetu Basi Wamekua wakisema Kwanini (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Hakupewa Mithli ya Alichopewa Musa Hivi Jee Hawakua ni wenye Kukikufuru Kile Alichopewa Musa hapo Kabla (Wanasema kua Tauran na Qur'an) Ni aina mbili za Uchawi vinavyosaidiana Na Wanasema kua Hakika Sisi (Vitabu vya Taurat na Qur'an) Vyote Hatuviamini Hivyo Waambie(Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam kua) Basi Leteni Kitabu Kutoka kwa Allah Ambacho ni Bora zaidi ya Viwili hivi Ambacho Mimi nikifuate kama kweli nyinyi ni wa kweli . Lakini kama hawakukujibu basi fahamu kua wao ni weny ekufuata matamanio ya Nafsi zao, na jee ni nani aliepotoka zaidi ya yule anaefuata matamanio ya Nafsi yake? Bila ya kua na muongozo kutoka kwa Allah Subhanah wa Ta'ala. Na Allah hawaongozi watu waliokua madhalimu, na kwa hakika tumeshafikisha ujumbe (wa Qur'an) ili wao wapate kukumbuka.***

Naam..Tunaona katika aya hizi kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawohoji Makafiri wa Makkah pamoja na Mayahudi wa Madina ambao walikua ni wenye kushirikiana katika kuupiga vita Ujumbe wa *Rasul Alah Salallahu Alayahi wa Salam.*

Na hivyo kuwaambia kama hawaviamini Vitabu hivyo basi na wamletee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kitabu ambacho kitakua ni bora zaid ili akifuate kama wao kweli ni wakweli.

Kisha Allah Subhanah wa Ta'ala alikua akijibu hoja za Makafiri wa Makkah na Madina huku akiwa ni mwenye kusisitiza kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salaam* kwa vithibitisho kua yeye ndie Mtume alietumwa kwa ajili yao na kwa kila Mtu atakaefuatia baada yao Ulimwenguni kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Mtume wa Mwisho kama zisemavyo aya kua:

﴿مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّينَ وَكَانَ ٱللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيماً﴾

Ma kana Muhammadun aba ahadin min rijalikum walakin rasoola Allahi wakhatama alnnabiyyeena wakana Allahu bikulli shay-in AAaleeman*(Surat Al Ahzab 33:40)*

Tafsir: ***Na Hakua Muhammad (Salallahu Alayhi wa Salam) Muhammad Baba wa wa mtu yeyote katika watu wenu, bali yeye ni Mtume wa Allah Subhanah wa Ta'ala na ni wa Mwisho wa Manabii wetu, na kwa hakika Allah ndie mwenye kujua juu ya kila kitu.***

Hivyo hili ni thibitisho la kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Nabii wa Mwisho wa miongoni mwa *Manabii wa Allah Subhanah wa Ta'al*a na Hivyo kwa maana hio basi mbali ya kua yeye alikua akiishi na watu wa Quraysh lakini pia ni Nabii wa watu wote Ulimwenguni.

Ambapo kuna baadhi wanaweza wakajiuliza suali la kua Kama *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Mtume wa mwisho basi kwanini Hadithi zake zikabashiria kua Nabii Isa A*layhi Salatu wa Salam* atashuka katika kipindi cha wakati wa Mwisho wa Dunia?

Naam..anasema Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kuhusiana na Jawabu la Suali hili kua: '**Isa Ibn Maryam ni Nabii aliekuja katika kipindi cha kabla ya kuja kwa Nabii Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam*. Na hivyo basi kipindi chake kilimalizika baada ya kuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***

Hivyo hapo atakapokuja tena basi hatakua ni Mtume anekuja kwa ajili ya kuendeleza kipindi chake, bali anakuja kua Mfuasi wa Sharia zilizowachwa na kuwekwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'*

Ambapo kwa upande mwengine basi tunaona pia kua aya hazikusema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni *Khatam Al Rusul* Bali zimesema ni *Khatamun Nabiyyin* ambapo maneno haya maana yake ni kua kama tulivyoona hapo kabla kua Kila Rasul hua ni Nabii pia Lakini si kila Nabii hua ni Rasul, yaani Kila anaepokea Wahy Kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni Nabii ambapo miongoni mwao hao wanaopokea Wahy basi wapo pia wanaotumwa kuufikisha Wahy huo kwa Watu husika au kua ni wenye kupokea Kitabu kutoka kwa Allah Subahanh wa Ta'ala, basi hawa hua ni Manabii na Mitume pia.

Na mara kadhaa amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Utume na Unabii Umemalizika na hivyo hakutokua na Mtume wala Nabii baada yangu, na juu ya hili**

inawezekana ikawa kuna ugumu kwa watu, lakini kutakuwepo Ubashirio'. Hivyo Masahaba *Radhi Allahu Anhu*m wakauliza: 'Ubashirio wa aina gani huo ya *Rasul Allah*?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ndoto ya kweli atakayoota Muislam, hua ni sehemu ya Nubuwwat'** *(Imam At Tirmidhii)*

Na pia akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Hakika mimi nimependelewa mambo 6 dhidi ya Manabii wengine ambayo ni: Nimejaaliwa Kauli fupi zenye Maana kubwa sana; Nimejaaliwa Nusra kutokana na kuogopewa; Ngawira imehalalishwa kwangu; Ardhi imejaaliwa kwa ajili yangu kua ni Nadhifu ya Kusjudia na kujitoharishia; Nimetumaa kwa Walimwengu wote; Na Utume unamalizikia kwangu mimi**'*(Imam At Tirmidhii)*

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Watu wa Bani Israil waliongozwa na Mitume baada ya Mitume akifa mmoja basi alikua akifuatia Mtume mwengine. Lakini hata hivyo kwa upande wangu mie basi hakutokua na Nabii zaidi yangu ila watakuwepo Makhalifa waadilifu wengi***(Sahih Muslim)*

Allah Subhanah wa Ta'ala anatuelezea katika Kitabu chake kitukufu huhusiana na Ukweli wa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakutumwa kwa watu wa Kabila la Quraysh la Makkah na Mayahudi wa Madina tu bali kwa Ulimwengu Mzima na kila kiumbe kitakachofuatia baada yake na kua ni wenye kumuamini na kumfuata yeye kwa kusema kua:

﴿ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلۡأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكۡتُوبًا عِندَهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَٱلۡإِنجِيلِ يَأۡمُرُهُم بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَىٰهُمۡ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنۡهُمۡ إِصۡرَهُمۡ وَٱلۡأَغۡلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتۡ عَلَيۡهِمۡ فَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ﴾

Alla<u>dh</u>eena yattabiAAoona alrrasoola alnnabiyya al-ommiyya alla<u>dh</u>ee yajidoonahu maktooban AAindahum fee alttawr<u>a</u>ti waal-injeeli ya/muruhum bialmaAAroofi wayanh<u>a</u>hum AAani almunkari wayu<u>h</u>illu lahumu al<u>tt</u>ayyib<u>a</u>ti wayu<u>h</u>arrimu AAalayhimu alkhab<u>a</u>-itha waya<u>dh</u>aAAu AAanhum i<u>s</u>rahum waal-aghl<u>a</u>la allatee k<u>a</u>nat AAalayhim faalla<u>dh</u>eena <u>a</u>manoo bihi waAAazzaroohu wana<u>s</u>aroohu waittabaAAoo alnnoora alla<u>dh</u>ee onzila maAAahu ol<u>a</u>-ika humu almufli<u>h</u>oona*(Surah Al-A'raaf: 7:157)***

Tafsir: ***Wale Ambao Wanamfuata Mtume, Nabii (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Ambae Hajui Kusoma wala Kuandika Yule Ambae Wamemkuta Ameandikwa/Ametajwa kwa Ajili yao Katika Taurati na Injili Mwenye Kuwaamrisha Mema Na Akawakataza Maovu Aliewahalalishia Juu yao Vilivyo vizuri Na Akawaharamishia Machafu (Mtume) Ambae anawaondoshea Uzito Wao Na Mfungo wa Vifungo vya Minyororo Ambayo ilikua imewafunga wao Ama Kwa wale wanaomuamini Na Wakamheshimu Na Wakamnusuru Na Wakafuata Nuru Ambayo Wameshushiwa Juu yao Basi hao ndio Waliofuzu.***

Hivyo hii ni aya ambayo inazungumzia kuhusiana na namna alivyotajwa na kubashiriwa kuja kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani ya Zabur na katika Injil kua ni Nabii Asiejua Kusoma.

Ambapo tunapozungumzia Mtu asiejua kuandika wala kusoma basi anasema Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua: **'Kujua kusoma na kuandika ni miongoni maa mambo ambayo ni rahisi sana kuyajua ndani ya Maisha ya Ibn Adam Na ingawa *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa *Salam* alikua hana Ilm hio ya kujua kuandika na kusoma Lakini hata hivyo Kitabu alichokuja nacho cha Qur'an na Ilm iliyomo ndani yake ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliitoa kwa Ulimwengu Ni Ilm ambayo hakuna kiumbe yeyote yule aliewahi kuishi Duniani kua ni mwenye kuja nayo Ilm kama hio.'**

Na hivyo basi Huu ni Miongoni mwa Miujiza kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua hawezi kufanya jambo jepesi zaid ambalo ni kusoma na kuandika lakini hapo hapo alikua pia ni mwenye kua na uwezo wa kufanya yasiyowezekana kwa Ibn Adam wa Kawaida kama kupokea Qur'an na kuifikisha ujumbe wake kwa Ibn Adam na Majini kutokana na utukufu wake Idhini ya *Allah Subahanh wa Ta'ala.*

Kwani anasema Ataa Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* kabla ya kusilimu kwake kua: '**Hakika mimi nilikutana na Abd Allah Ibn Amr Al As na nikamuambia kua:**

Hivi Jee unaweza kuniambia mimi kuhusiana na namna alivyoelezewa *Rasul Allah (Salallahu Alayhi wa Salam)* kwenye Taurati?

Ambapo Abd Allah Ibn Amr Al As *Radhi Allahu Anhu* akasema: Naam..bila ya shaka nitakuambia, *Wa Allahi Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametajwa ndani ya Taurat kama vile alivyotajwa kwenye Qur'an, yaani..

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ إِنَّآ أَرۡسَلۡنَاكَ شَاهِداً وَمُبَشِّراً وَنَذِيراً﴾

Ya ayyuha alnnabiyyu inna arsalnaka shahidan wamubashshiran wanadheeran*(Surat Al Ahzab 35:40)*

Tafsir: ***Ewe Nabii hakika Sisi tumekutuma wewe Kama Shahidi Na Mwenye Kubashiria mema na mwenye Kuonya.***

Abd Allah Ibn Amr Al As *Radhi Allahu Anhu* akaendelea kusema kua: **Taurat inaendelea kusema kua Wewe *Rasul Allah (Salallahu Alayhi wa Salam*) kua njia ya uokozi kwa ajili ya aale wasiosoma, hakika wewe ni Mja wangu na ni Mtume wangu**

Na nimekuita wewe kwa Jina la Mutawakkkl, kwani wewe si mkali wala si mwenye Moyo mgumu na wala si mwenye kupiga makelele sokoni Kwani yeye (*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*) halipi Ubaya kwa ubaya bali ni mwenye Kusamehe na kutotilia maanani maovu anayofanyiwa.*(Sahih Muslim)*

Na kwa upande mwengine basi Anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua **:** '**Alisema mmoja kati ya Mabedui kua: 'Mimi nilienda katika Mji wa Madina siku moja katika kipindi cha Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kumuuza Ngamia wangu**

Baada ya kufanikisha jambo langu hilo basi nikajiambia ndani ya Nafsi yangu kua,Wacha nikamtembelee huyu Mtu anaesema kua yeye ni Mtume ili nipate kujua anachokisema Hivyo

nikamkuta *(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)* akiwa anaelekea katika sehemu fulani huku akiaa amefuatana na Abu Bakr na Umar

Hivyo nami nikawafuata hadi wakafika kwenye Nyumba ya mmoja kati ya Mayahudi ambae alikua akimsomea Taurat Mtoto wake wa kiume mwenye Sura nzuri ya kuvutia lakini akiwa katika hali ya kutaka kukata roho. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kumwambia Myahudi huyo kua:

Nakuomba uniambie kwa yule ambae ndie alieishusha Taurat, kua Jee nimeelezewaje ndani yake na nitafikia wapi?

Yule Myahudi akatikisa kichwa kuashiria kukataa kwake kuzungumzia juu ya jambo hilo. Ambapo yule Mtoto anaetaka kufa Basi akasema: 'Naam..Naapa mimi kwa yule ambae ameishusha Taurat kua hakika sisi tumeona kwenye Kitabu chetu cha Taurat maelezo ya muonekano wako, na sehemu utakazozifikia.

Hivyo nami nnashuhudia kua Hakuna Mungu anaestahiki Kuabudiwa ila Allah na wewe kua ni Mtume wake.'

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaambia Umar na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhum* kua: Mtenganisheni Yahudi huyu kutokana na Ndugu yenu.' Na hivyo Mtoto huyo alipofariki basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamkosha, Akamsalia na Kumzika.'

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anawahoji Makafiri kwa kuwaambia kua kama hawamini kitabu kitukufu cha Qur'an kua ni chenye kutoka kwake kupitia kwa mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* ambae hata hivyo si mtu mwenye kujua kusoma wala kuandika, kama wanavyomjua wao pia kutokana na kukaa nae kwa mda wa miaka 40 katika mji wa Makkah bila ya kumuona labda akiwa ni mwenye kuenda kusoma au kusomeshwa basi na wao wajiusanye pamja na Majni kisha waandae kitabu kama hicho na kisha wakitoe kionekanane Uthibitisho wake kama zinavyosema Aya.

﴿ وَإِن كُنتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا۟ بِسُورَةٍ مِّن مِّثْلِهِ وَٱدْعُوا۟ شُهَدَآءَكُم مِّن دُونِ ٱللَّهِ إِنْ كُنتُمْ صَٰدِقِينَ ۝ فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا۟ وَلَن تَفْعَلُوا۟ فَٱتَّقُوا۟ ٱلنَّارَ ٱلَّتِى وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلْحِجَارَةُ أُعِدَّتْ لِلْكَٰفِرِينَ ﴾

Wa-in kuntum fee raybin mimma nazzalna AAala AAabdina fa/too bisooratin min mithlihi waodAAoo shuhadaakum min dooni Allahi in kuntum sadiqeena; Fa-in lam tafAAaloo walan tafAAaloo faittaqoo alnnara allatee waqooduha alnnasu waalhijaratu oAAiddat lilkafireena*(Surat Al Baqara 2:23-24)*

*Tafsir: **Na kama nyinyi (Makafiri) mna shaka kuhusiana na (Kitabu) tulichomtumia Mja wetu(Muhamamd Salallahu Alayhi wa Salam), basi toeni Sura moja mithili yake na kisha waiteni mashahidi wenu zaidi ya Allah Subhanah wa Ta'ala kama kweli nyinyi ni wa kweli. Na kama hamkutoa, na kwa hakika hamuwezi kutoa, basi uogopeni Moto ambao Kuni zake ni Watu na Mawe uliotayarishwa kwa ajili ya Makafiri.***

Ambapo hii ni moja kati ya Aya za Qur'an ambazo ni zenye kukabiliani uso kwa uso dhidi ya shaka waliyozokua nayo Makafiri na upingaji wao dhidi ya kukubaliana na Ujumbe wa *Allah Subhanah wa Taala* na pia dhidi ya Utume wa *Rasul Allah Salallahu Aayhi wa Salam.* Na aya inaweka wazi kua

hata washikamane Viumbe wangapi basi kamwe hawatoweza kutoa hata ya moja mithili ya Sura na aya za Qur'an kama alivyosema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:

﴿قُل لَّئِنِ ٱجْتَمَعَتِ ٱلإِنْسُ وَٱلْجِنُّ عَلَىٰ أَن يَأْتُواْ بِمِثْلِ هَـٰذَا ٱلْقُرْآنِ لاَ يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيراً ﴾

Qul la-ini ijtamaAAati al-insu waaljinnu AAala an ya/too bimithli hadha alqur-ani la ya/toona bimithlihi walaw kana baAAduhum libaAAdin *dh*aheeran*(Surat Al Isra 17:88)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam): 'Lau kama Ibn Adam na Majini wakusanyike pamoja kwa ajili ya kutoa mithili ya Hii Qur'an basi hawatoweza kutoa mithili yake hata kama wakisaidiana kwa pamoja'***

Naam..*Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutoa changamoto hio kwa viumbe wake katika Bahari ya Ilm inayothibitiaha kua Qur'an ni maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kwani kama hali ikiwa kama walivyokua wakidai Watu wa Makkah kama zinavyosema aya kua;

﴿ وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِّسَانُ ٱلَّذِى يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ وَهَـٰذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ ﴾

Walaqad naAAlamu annahum yaqooloona innama yuAAallimuhu basharun lisanu alladhee yulhidoona ilayhi aAAjamiyyun wahadha lisanun AAarabiyyun mubeenun*(Surat An Naml 16:103)*

Tafsir: ***Hakika Sisi Tunajua kua Wanasema hao Ma Quraysh Hakika Wanaomfundisha(Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam kunukuu Qur'an) Ni Watu Ambao Ndimi zao Hao wanao wazungumzia ni za Kigeni (Si za Lugha ya Kiarabu) Na Hii Lugha (ya Qur'an) Ni ya Kiarabu Fasaha.***

Hivyo kutokana na kua watu wa Makkah kua na hali ya kufikia kusema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifundishwa maneno ya Qur'an na Mtu mgeni Asiejulikana kutokana na miongoni mwa watu watokao katika Mji wa Makkah, na hivyo hawakua ni wenye kumtaja jina kua labda ni fulani kwa sababu walikua wakizusha tu ili kupingana na Ujumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na hivyo basi ndio *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kama ni hivyo ndio mfikiriavyo na kusema pia basi nyinyi hamjui na hamtaki kuukubaki ukweli na hii ni kwa sababu Hata kama mkikusanyika Viumbe Ibn Adam wote na Viumbe Majini kwa pamoja pia kwa ajili ya kutoa mithili ya Hii Qur'an basi kamwe hamtoweza kutoa Mithili yake.

Allah Subhanah wa Ta'ala anasema tena kwenye Qur'an kua:

﴿ أَمْ يَقُولُونَ ٱفْتَرَاهُ قُلْ فَأْتُواْ بِعَشْرِ سُوَرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرَيَاتٍ وَٱدْعُواْ مَنِ ٱسْتَطَعْتُمْ مِّن دُونِ ٱللَّهِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ﴾

Am yaqooloona iftarahu qul fa/too biAAashri suwarin mithlihi muftarayatin waodAAoo mani istataAAtum min dooni Allahi in kuntum sadiqeena; *(Surat Hud 11:13)*

Tafsir: ***Au Wanasema: 'Yeye(Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) ameighushi (Quran), Hivyo waambie: 'Leteni basi nyinyi Sura Kumi za kughushi mithili yake, na waitena muwatakao zaidi ya Allah Subhanah wa Ta'ala (akusaidieni) kama kweli nyinyi ni wakweli.''***

Ambapo baada ya kutoa hoja hio isiyowezekana kutokana na Miujiza ya Maneno ya Qur'an basi *Allah Subhanah wa Ta'al*a anamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

﴿فَإِلَّمْ يَسْتَجِيبُواْ لَكُمْ فَٱعْلَمُوٓاْ أَنَّمَآ أُنزِلَ بِعِلْمِ ٱللَّهِ وَأَن لاَّ إِلَٰهَ إِلاَّ هُوَ فَهَلْ أَنتُمْ مُّسْلِمُونَ ﴾

Fa-illam yastajeeboo lakum faiAAlamoo annama onzila biAAilmi Allahi waan la ilaha illa huwa fahal antum muslimoona*(Surat Hud 11:14)*

Tafsir: Na Kama Hawakukujibuni (Hoja hio basi ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Basi(Waambie Makafiri kua) Jueni kua (Enyi Makafiri)Hakika hii Qur'an imeshushwa Kutokana na Ilm ya Allah Na Hakuna Mungu isipokua yeye Hivyo Jee Mtajisalimisha kwa kuingia katika Uislam(Surat Hud 11:14)

Naam tunajaribu kumalizia kufahamishana kuhusiana Uthibitisho wa Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama ilivyotajwa ndani ya Qur'an. Ambapo kwa baadhi basi yetu basi hali imekua kama kwamba kuna aya ambazo maneno yake yamekua kama kwamba ni mageni Na ya kushangaza kutokana na ukweli na uhalisia wake na hoja zilizomo ndani yake, mbali ya kua sisi ni Waislam.

Na hii inaonesha tatizo kubwa sana tulilonalo sisi Waislam ambalo ni la kusoma tu Qur'an kwa kukariri bila ya kufuatilia maana yake, Na hivyo mtu anaposomewa na kufahamishwa na kufahamu basi hua ni mwenye kubakiwa na mdomo wazi huku akijiuliza kwa kueema kua Subhanah Allah! ala? Kumbe Qur'an imesema yote haya!

Hivyo mbali ya kua Makafiri walikua hawaamini kua Qur'an ni Maneno ya *Allah Subhanah wa Taala* na hivyo walikua wakiyachukulia kua kama ni Hekaya za Kale ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alijua akihadhithiwa Asubuhi na Jioni na kisha yeye ndio huwahadithia Watu wake kama zinavyosema aya:

﴿ وَقَالُوٓاْ أَسَاطِيرُ ٱلأَوَّلِينَ ٱكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمْلَىٰ عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً ﴾

Waqaloo asateeru al-awwaleena iktatabaha fahiya tumla AAalayhi bukratan waaseelan*(Surat Al Furqan 25:5)*

Tafsir: ***Na (Makafiri) Wanasema kua ni Hikaya za Watu wa Kale Ambazo anaziandika(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kwa kuwamrisha Masahaba zake wamuandikie) Ambazo Zinaainishwa kwake Asubuhi na Jioni.***

Allah Subhanah wa Ta'ala anayasema haya kwa sababu ilikua kuna Watu hasa ambao ndio kazi yao kusema hivyo akiwemo Nadir Ibn Al Harith ambae alikua ni mfanya biashara aliesafiri katika sehemu nyingi sana na hivyo, ili kua kawaida yake kua baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusema kuhusiana na Aya alizoshushiwa basi yeye alikua akikaa na kuanza kutoa visa vya watu aa zamani wa sehemu alizotembelea kuanzia Sham hadi Uajemi na akisha maliza basi Huuliza kwa kusema: '**Hivi Jee hivi visa nnavyovitoa mimi hamuona kua ni bora na vizuri zaidi kuliko Asatir Al Awwlaiina za Muhammad?'**

Ambapo kutokana na ujinga wao basi Makafiri hao walikua Vipofu wa Macho na Ufaham kwani walikua hawaoni kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuwahi kusoma wala kuandika kwa mda wote alioishi na kukulia mbele ya macho yao katika Mji wa Makka tangu alipokua mdogo hadi kufikia umri qa miaka 40 alipopewa Utume.

Na mbali ya kua walikua wakijua kya Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam ni Mtu Mkwei, Muaminifu, Muadilifu, Hasemi Uongo, n.k.

Na hii ni kwa sababu Makafiri walikua na hali ile ya watu ambao wasiomkubali Mtu ambae ametokana nao wenye kumjua ndani nje kama zinavyosema aya:

﴿وَعَجِبُوٓاْ أَن جَآءَهُم مُّنذِرٌ مِّنْهُمْ وَقَالَ ٱلْكَافِرُونَ هَٰذَا سَاحِرٌ كَذَّابٌ﴾

WaAAajiboo an jaahum mundhirun minhum waqala alkafiroona hadha sahirun kadhdhabun *(Surat Sad 38:4)*

Tafsir: ***Na (Makafiri) Walikua Wakiona Ajabu kua Wamejiwa Muonyaji Kutoka miongoni mwao Na Walikua wakisema Makafiri Huyu ni Mchawi tu na Muongo.***

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kusema kuhusiana nao kua:

﴿ أَفَلاَ يَتَدَبَّرُونَ ٱلْقُرْآنَ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِندِ غَيْرِ ٱللَّهِ لَوَجَدُواْ فِيهِ ٱخْتِلاَفاً كَثِيراً ﴾

Afala yatadabbaroona alqur-ana walaw kana min AAindi ghayri Allahi lawajadoo feehi ikhtilafan katheeran*(Surat An Nisaa 4:82)*

Tafsir: ***Hivi Jee Hawaitafakkari kwa Umakini Quran Kwani Lau Kama ingekua Ni yenye kutoka kwa mwengine zaidi ya Allah Basi Wangekuta ndani yake (Qur'an) Khitilafu nyingi sana***

Ambapo aya hii pia ni aya inayoyusisitizia sisi Waislam pia kuisoma Qur'an si kwa ajili ya kuihifadhi na kuikariri tu bali kwa ajili ya Kutafakkari kwa makini kuizingatia na kuifanyia kazi.

Kwani anasema Shuayb kua amesema Babu yake *Radhi Allahu Anhu* kua: **Mimi na Kaka yangu tulienda kwenye Mkusanyiko ambao kamwe haubadilishiki na hata Ngamia Wekundu. Na tulipomtembelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tukakuta Masahaba wakubwa**

wamekaa Mlangoni kwake, hivyo hatukutaka kuugawa mkusanyiko wao, na tukakaa mwishoni mwishoni.

Masahaba hao walikua wakinukuu Aya za Qur'an Lakini sasa wakawa wanatofautiana kuhusiana na maana ya aya hizo na kuanza Kugombana huku sauti zao zikipanda juu sana.

Katika Hali hio akatokea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku uso wake ukiwa mwekunduu Na akachukua vumbi na kuwarushia Masahaba hao huku akisema: 'Kuweni na Utulivu enyi Watu wangu! Kwani haya ndio yaliyowaangamiza watu waliotangulia kabla yenu.'

Yaani kutokana na Kutokukubaliana juu yao na kuwanukuu sivyo Mitume wao.

Na Kunukuu sivyo baadhi ya sehemu za vitabu vyao na kuzipinganisha sehemu nyengine za vitabu vyaoHivyo Qur'an haikushushwa kwa ajili ya baadhi ya aya kuzipinganisha na aya nyenginezo.

Bali imeshushwa kwa ajili ya baadhi ya aya kuziunga mkono aya nyenginezo, Hivyo Ishini kwa kile mlichokifaham ndani ya Qur'an na kile msichokifaham basi waachieni wenye Ilm(*Sahih Muslim)*

﴿قُلْ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنِّى رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعاً ٱلَّذِى لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ لآ إِلَٰهَ إِلاَّ هُوَ يُحْيِى وَيُمِيتُ فَـَٔامِنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِ ٱلنَّبِىِّ ٱلأُمِّىِّ ٱلَّذِى يُؤْمِنُ بِٱللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ وَٱتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ﴾

Qul ya ayyuha alnnasu innee rasoolu Allahi ilaykum jameeAAan alladhee lahu mulku alssamawati waal-ardi la ilaha illa huwa yuhyee wayumeetu faaminoo biAllahi warasoolihi alnnabiyyi al-ommiyyi alladhee yu/minu biAllahi wakalimatihi waittabiAAoohu laAAallakum tahtadoona *(Surah Al-A'raaf: 7:158).*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Enyi Watu Hakika Mimi ni Mtume wa Allah Nilietumwa kwa ajili yenu nyote kwa pamoja (Allah) Ambae kwake yeye kuna umiliki Vilivyomo Mbinguni na Ardhini Hakuna Mungu isipokua Yeye Mwenye Kuwapa uhai viumbe na Kuuchukua Uhai wao hivyo Muaminini Allah Na Mtume wake (Salallahu Alayhi wa Salam) Nabii ambae hajui Kusoma wala kuandika (Nabii) Ambae ni Mwenye Kumuamini Allah Na Maneno yake (Yaliyomo ndani ya Vitabu vyake) Na Hivyo Mfuateni Ili Mpate Kuongoka.***

Ambapo tunapoiangalia aya hii basi tunaona kua imeanzia na maneno yasemauo *Ya Ayyuha Al Nassu* - yaani enyi Watu.

Na wala haikuanzia na maneno yasemayo *Ya Ayyuha Alladhiina Amanu* - yaani Enyi wale ambao Mlioamini. Kwani aya inayoanza na Enyi Mlioamini basi hua inawazungumzia Waumini wa Dini ya Kiislam.

Na aya inayoanzia na Enyi watu basi hua inawazungumzia Watu wote kwa ujumla. Na kwa maana jio basi Aya hii ina ujumbe ambao Unawahusu Ibn Adam wote kaa ujumla yaani iwe Waislam, Wakristo, Mayahudi, Mabudha, Mapagani n.k

Ambapo Ujumbe huo ni Usemao kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Mtume *wa Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie Muumba na mmiliki wa kila kitu kilichomo ndani ya Ardhi na Mbinguni.

Ujumbe ambao ni wenye kumtaka kila mtu kua Amuamini na kisha awe ni mwenye kumfuata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae nae ni mwenye kuamini Vitabu vyote *vya Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na hivyo ni mwenye Kutakiwa kufuatwa na Watu kwani kumfuata kwake humpelekea yule atakaemfuata kua ni mwenye kua kwenye Uongofu. Na hivyo bila ya shaka atakaemkana basi atakua kwenye upotovu.

Kwani kasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Wa Allahi Nnaapa mie kwa yule ambae Roho yangu imo ndani ya mikono yake kua Hakuna Yahudi wala Mkristo wa Ummah huu ambae atasikia kuhusiana nami na kisha akafariki bila ya kua ni mwenye kuniamini na kuamini kile nilichokuja nacho, isipokua atakua ni mtu wa Motoni.'**(Sahih Muslim)

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam ku*a: '**Hakika mimi nimepewa vitu vitano ambavyo hakuna Mtume aliepewa hapo kabla yake, kwanza nimepewa usaidizi wa umbali wa masafa ya safari ya mwezi mmoja, pili nimepewa majaaliwa y akua ardhi yote imefanywa kua ni safi kwa ajili yangu hivyo popote pale Mtu atakapokuwepo basi anaweza kusali juu yake unapowadia wakati wa Sala, Tatu nimejaaliwa kua Ngawira ni halali yangu, kwani ilikua ni haramu kwa watu waliotangulia kabala yangu. Nne ni kua mimi nimejaliwa kua ni mwenye kua na uwezo wa kuwaombea watu katika Siku ya Malipo. Na mwisho ni kua Mitume wote waliotumwa kabla yangu walikua wakitumwa kwa watu wao lakini mimi nimetumwa kwa Watu wote.'**

Ama kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Sahl Al Tustari basi yeye anasema kuhusiana na maneno ya aya ya mwisho ya Surat Al Kahf isemayo:

﴿قُلْ إِنَّمَآ أَنَاْ بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَآءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحاً وَلاَ يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدَا﴾

Qul innama ana basharun mithlukum yooha ilayya annama ilahukum ilahun wahidun faman kana yarjoo liqaa rabbihi falyaAAmal AAamalan salihan wala yushrik biAAibadati rabbihi ahadan*(Surat Al Kahf 18:110)*

*Tafsir: **Waambie (tena ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Hakika Mimi Ni Mtu Kama Nyinyi Imeshushwa Juu yangu Kua kwa Hakika Mungu wenu Ni Mungu Mmoja Hivyo kwa Yeyote yule mwenye Kutumai Kurudi Kukutana na Mola wake Basi na Afanye Amali Njema Na Wala Asishirikishe Katika Ibada Za Mola wake Na Yeyote.***

Kua: 'Amali njema zinazozunguziwa hapa ni ni zile ambazo hazina Riya ndani yake na kua ziko ndani ya Mipaka ya Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.'

Na kwa upande wa Muawwiyyah Ibn Abu Sufyan Radhi Allahu Anhu baasi yeye amesema kua: **'Hii ndio aya ya mwisho kuteremshiwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* (kimaana)'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Jarir basi yeye anaielezea ayah hii kwa kusema kua: **'Kuna mtu alimuliza Ubadah Ibn Samit kwa kusema kua: Hakika mimi nimeshasali sana na kufunga sana**

kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* lakini hua napendwa kusifiwa kutokana na kufanya hivyo'

Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Kwa hakika amali zako hazina thamani yeyote mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: 'Hakika mimi ni mbora zaidi ya wale nnaoshirikishwa nao, hivyo kama ikiwa kuna Amali ambayo nnashirikishwa na mwengine basi mimi humpa amali hizo zote yule nnaeshirikishwa nae.''**

Na kuna mtu *alimuuliza Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: **'Ya Rasul Allah! Hivi unasemaje kuhusiana na mtu ambae ameenda katika vita vya Jihadi kwa ajili ya *Allah Subhnah wa Ta'ala* na pia kwa ajili ya kujitafutia Umaarufu?' ambpo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: 'Hatopata Malipo yeyote.'** *(Imam Al Bayhaqi)*

Na akasema *Ibn Qays Al Khudha Radhgi Allahu Anhu* kua amesema Rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:* **'Kama ikiwa mtu atasimama kwa ajili ya kujionesha tu mbele za watu, basi hu ani mwenye kuingizwa ndani ya Ghadhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kusimama kwake huko hadi pale atakapokaa chini.'**

Na akasema pia Al Hafidh Imam Abu Yaa'ala kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaepigana vita vya Jihadi huku akiwa hana nia yeyote isipokua kupata kipande cha Kamba tu basi atakua ni mwenye kukipata kile alichokipigania.''**

Na kwa upande mwengine basi anasema Imam Muslim kua: '**Aliulizwa *Rasul Allah Sallah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kuambiwa kua: 'Ya *Rasul Allah,* hivi unasemaje kuihusiana na mtu ambae ni mwenye kufanya mema na kisha watu wakawa ni wenye kumsifu kutokana na mema hayo?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hilo hua ni Bashirio jema sana na la haraka kwa Muumini huyo.''**

Hivyo katika kipindi hiki cha miaka hii ya mwanzoni mwa Uislam mbali ya Waislam kua ni wenye kuhujumiwa lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alijaribu kutauliza na kuwafariji Waislam hao, kwani kuna sikua Masahaba walimlalamikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Saalam* kuhusiana na matezo hayo na kumwambia: '**Ya Rasul Allah Jee unaweza kutuombea kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala?'***

Ambapo na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawajibu kwa kusema: **'Miongoni mwa watu wa Walioamini wa Ummah zilizotangulia zilizotangulia walikua ni wenye kungizwa kwenye Mashimo yenye moto na kuna ambao walikua wakikamatwa na kuwekewa msumeno wa kukatia mbao juu ya vichwa vyao na kisha kukatwa pande mbili, laikini hata hivyo mateso hayo hayakuwapelekea kua ni wenye kua na hali ya kuachana na Imani yao, wengine Miili yao ilichannywa kwa Mashanuo ya Chuma na hivyo kuondolewa Ngozi zao kutokan kwenye Mifupa yao na misuli yao lakini hawakuachana na Dini yao. Wallahi Naapa mimi kua Dini hii itakua ni yenye kupata ushindi kiasi ya kua msafiri atasafirii kutoka Sanaa na Hadharamawt bila y akua na khofu ya yeyote isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na Kondoo hawatokua ni wenye kuwaogopa Mbwa Mwitu, laikini nyinyi watu hamna Subira.'**(sahih muslim)

Hivyo *Rasul Allah Salallahju Alayhi wa Salam* alipohamia katika mji wa Madina, basi Mji huo ulikua tayari una mipango ya kumtawazisha Mfalme wao ambae alikua akiitwa Abd Allah Ibn Ubyya au Ibn Salul., hivyo tukio la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhamia katika mji huyo likawa ni ;lenye kuhatarisha madaraka ya Ibn Salul.

Na siku moja wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akipitia kwenye njia za Mji wa Madina kwa ajili y akuwausia watu kuhusiana na Dini ya Kiislam basi akakutana na Ibn Salul ambae alimwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:**'Ewe Muhammad*** **hivi kwanini hukai ndani ya nyumba yako? Kwani hujui kua kama mtu atakua anataka kusikia ujumbe wako basi si atakufuata nyumbani kwako?'**

Ambapo Waislam waliposikia maneno hayo basi wakataka kumuadhibu Ibn Salul lakini hata *hivyo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam akawakataza Waislam hao kumuadhibu Ibn Salul.

Na kuna siku pia Ibn Salul alimwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua**: 'Hebu ondoka na Punda wako kwani harufu yake ni yenye kukirihisha' ambapo baada ya maneno hayo basi Waislam wa Madina wakasema kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ibn Salul anasema hivyo kwa sababu ulipowasili wewe kwenye mji wa Madina basi watu wa Madina ndio walikua Wanamalizia kuipamba Kofia ya Ufalme wako kwa Lulu za mwishoni.'**

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ وَلَا تَسْتَوِي ٱلْحَسَنَةُ وَلَا ٱلسَّيِّئَةُ ٱدْفَعْ بِٱلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا ٱلَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴾

Wala tastawee alhasanatu wala alssayyi-atu idfaAA biallatee hiya ahsanu fa-idha alladhee baynaka wabaynahu AAadawatun kaannahu waliyyun hameemun*(Surat Fusilat 41:34)*

*Tafsir**: Wala Haliwi Sawa Jambo Jema Na Jambo Ovu, Lipa (Ovu) Kwa Jema Lililo Bora Zaidi. Kwani kwa hakika kwa yule ambae kulikua na uadui baina yenu kutakua na urafiki wa karibu.***

SIKU YA KIAMA NA MIONGONI MWA DALILI KUU ZAKE.

Hivyo katika kuiangalia aya na Hadith basi tunaona kua imetaja baadhi ya miongoni mwa Dalili za Kiama ambamo ndani yake mna dalili ambazo zitatokea karibu na Kiama, kwani tunapozungumzia kuhusiana na Dalili za basi kuna Dalili za aina mbili, ambapo aina ya kwanza ni Dalili ambazo zitatokea mda mrefu kabla ya kiama na hivyo kuashiria kua tunakoelekea kua ni mwisho wa Dunia. Na aina ya pili ni zile ambazo ni dalili kuu zitakazotokea mda mfupi tu kabla ya Kiama na kuashiria kua Dunia imekwisha mda wake na hivyo wakati wowote ule saa ya Kiama itawadia.

Ambapo katika Kitabu cha Imam Muslim Ibn Hajjaj cha Sahih Muslim basi tunaona kua miongoni mwa Dalili kuu ni pamoja na:

Kumezwa kwa watu na ardhi katika upande wa Mashariki ya Dunia.
Kumezwa kwa watu na ardhi katika upande wa Magharibi ya Dunia.
Kumezwa kwa watu na ardhi katika upande wa Mashariki ya kati ya Dunia.
Kutokea kwa Moshi.
Kutokea kwa Dajjal.
Kutokea kwa Wanyama wanaotisha.

Kutokea kwa Yajuj na Majuj.
Kuchomoza kwa Jua kutoka katika upande wa Magharibi.
Kufuka kwa Moto katika maeneo ya ardhi ya Yemen.
Kushuka kwa Nabii Isa.

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَهُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضَ بِٱلْحَقِّ وَيَوْمَ يَقُولُ كُن فَيَكُونُ قَوْلُهُ ٱلْحَقُّ وَلَهُ ٱلْمُلْكُ يَوْمَ يُنفَخُ فِى ٱلصُّورِ عَالِمُ ٱلْغَيْبِ وَٱلشَّهَادَةِ وَهُوَ ٱلْحَكِيمُ ٱلْخَبِيرُ﴾

Wahuwa alladhee khalaqa alssamawati waal-ardha bialhaqqi wayawma yaqoolu kun fayakoonu qawluhu alhaqqu walahu almulku yawma yunfakhu fee alssoori AAalimu alghaybi waalshshahadati wahuwa alhakeemu alkhabeeru*(Surat Al Anaam 6:73)***

Tafsir: ***Na Yeye ndie alieumba Mbingu na Ardhi kwa haki, na katika siku hio atasema: 'Kua' na itakua. Kwani Kauli yake ni ya kweli, na Yeye ndie mwenye Mamlaka katika siku itakayopulizwa Baragumu. Yeye ndie mwenye kujua yasiyoonekana na yanayoonekana. Yeye ndie mwingi wa Hikma na ni mwenye habari juu ya kila kitu.***

Hivyo aya zinatuwekea wazi kuhusiana umiliki wa Siku ya Malipo kua ni wa Mwenyewe Muumba alieumba Mbingu na Ardhi kwa kuviambia anavyotaka kuviumba kua Viwe na vinakua na hivyo kila kitu kitakua wazi katika siku hiyo na ukweli utadhihirika hadharani na yeye ndie mwenye kujua juu ya kila kitu kinachoonekana na kisichoonekana na ni mwenye Hikma juu ya kila kitu kwanini hiki kiwe na kwanini kile kisiwe kutokana na Hikma zake na ni mwenye Habari juu ya kila kitu.

Aya pia inaendelea kutufahamisha kuhusiana na *Sur* au Baragumu, kitu ambacho kama tunavyoona katika mpangilio wa aya kua kimetajwa baada ya Mingu na Aradhi na kupulizwa kwake ambalo litapulizwa mara mbili, kwani mara ya kwanza itakua kwa ajili ya kukiangamiza kila kitu Ulimwenguni na kisha pulizo la pili litakua kwa ajili ya maumbile mapya ya kila kitu kilichoangamia kua ni chenye kua hai tena upya, na hivyo Ibn Adam na Majini watakusanywa kwenye ardhi ambayo itakua imetandazwa na kisha wataanza kuhesabiwa kuhusiana na Amali zao walizozifanya hapo kabla katika wakati wa Uhai wao walioishi Ulimwenguni.

Ambapo kuhusiana na Sur basi anasema Imam Abū Al-Qāsim Sulaymān Ibn Aḥmad Ibn Ayyūb Ibn Muṭayyir al-Lakhmial-Shāmi At Tabarani kua: **'Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kumaliza kuziumba Mbingu na Ardhi basi akaliumba Sur na kisha akamkambidhi Malaika Israfil, ambae nae akaliweka mdomoni mwake huku akiwa ni mwenye kuiangalia Arshi Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* akisubiri amri ya kulipuliza.'**

Masahaba wakauliza kwa kusema: '*Ya Rasul Allah* hivi *Sur* ndio Nini?' ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: 'Ni Tarumbeta' Masahaba wakaendelea kuuliza: 'Likoje hilo Tarumbeta?'

***Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* akasema: 'Ni Kubwa sana, kwani nnaapa mimi kwa yule ambae ndie alienituma kwa haki kua ukubwa wa mzunguko wa duara lake ni sawa upana**

wa Mbingu na Ardhi, na litapilizwa mara 3, ambapo mara ya kwanza itakua kwa ajili ya Kutia Khofu Kubwa sana, wa pili utakua kwa ajili ya kupoteza nguvu na kufariki na watatu kwa ajili ya kusimamishwa mbele ya Mola wa Ulimwengu wote.

Ambapo katika Mpulizo wa kwanza ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamuamrisha Israfil kupuliza, basi utawashuta viumbe wote wa Mbinguni na Ardhini isipokua wale tu ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* hatotaka washtuke, na atamuamrisha apulize kwa mpulizo mmoja mrefu wenye kuchukua mda bila ya kusita kwa mda mrefu.''

***Allah Subhanah wa Ta'ala* anaielezea hali hio katika Qur'an kwa kusema:**

﴿وَمَا يَنظُرُ هَٰٓؤُلَآءِ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً مَّا لَهَا مِن فَوَاقٍ﴾

Wam<u>a</u> yan<u>*dh*</u>uru h<u>a</u>ol<u>a</u>-i ill<u>a</u> s<u>a</u>yh<u>a</u>tan w<u>ah</u>idatan m<u>a</u> lah<u>a</u> min faw<u>a</u>qin*(Surat Sad 38:15)*

*Tafsir: **Na hao hawasubiri isipokua Sauti moja tu ya Mpulizo (wa Baragumu) ambao hautokua na msito wala kua na mwisho ndani yake.***

Ambapo kutokana na sauti hio pia basi hata Milima itakua ni yenye kutembea kama yanavyotembea Mawingu na kisha Ardhi itatikisika kama kibakuli kilichowekwa Juu ya Maji ya Bahari yenye mawimbi makubwa sana na yenye nguvu na kasi na hivyo kila kilichomo ndani yake kitakua ni chenye kutetemeka na kutikisika kwa mtikisiko mkubwa sana kama zinavyosema Aya ambazo zimetumia neno *Rajafa* katika kuielezea hali ya siku hio.

Neno Rajafa kwa Kiarabu hua linamaanisha Kutetemeka, Kua katika hali ya mtikisiko Mkali na wa nguvu kubwa sana, Kukosa Utulivu, Kua na Mshtuko unaotokana na Jambo lenye Kutisha sana. Hivyo aya zinasema kua:

﴿ يَوْمَ تَرْجُفُ ٱلرَّاجِفَةُ ۞ تَتْبَعُهَا ٱلرَّادِفَةُ ۞ قُلُوبٌ يَوْمَئِذٍ وَاجِفَةٌ ﴾

Yawma tarjufu alrr<u>a</u>jifatu; TatbaAAuh<u>a</u> alrr<u>a</u>difatu; Quloobun yawma-i<u>dh</u>in w<u>a</u>jifatun *(Surat An Naziat 79:6-8)*

*Tafsir: **Katika siku ya Mtikisiko mbaya sana utakapotikisa, utakaofuata na Mripuko mkubwa sana, Nyoyo katika siku hio zitakua zimejaa khofu kubwa sana.***

Yaani hii itakua ni siku ambayo watu watashuhudia yale ambayo kamwe haikuwahi kushuhudiwa na kiumbe yeyote tangu kuumbwa kwa Dunia, na hivyo Watu watashtuka na kuhamanika kutokana na taharuki waliyokumbana nayo,

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam anaendelea kusema kua: '**Watu watabiringita biringita, wenye kunyonyesha watawasahau Watoto wachanga wao, wenye Mimba wataharibu Mimba zao, Watoto wataota Mvi, Mashaytani watatoka Baharini na kuruka kukimbilia ufukweni, lakini Malaika watatokea na kuwapiga na kuwarudisha Baharini, Watu watakua hawana kwa kukimbilia isipokua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na kuna wengine watakua wanawaita wenzao,na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akaiita Siku hii kua ni siku ya Kuitana.**

Watu watakua katika hali ambayo wataona kua Ardhi inapasuka kuanzia mwanzo hadi mwisho, na watashuhudia mambo ambayo hawakuwahi kushuhudia hapo kabla na watakua na khofu kubwa sana ambayo ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu ndie anaejua hali yao hio na wataangalia juu wataona kua Mbingu zimekua kama Mafuta yaliyochemshwa,na kisha Mbingu zitapasuka na Nyota na Mwezi na Jua zitapoteza Nuru yao. Na Maiti watajua juu ya matukio hayo.'

Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* akauliza: '*Ya Rasul Allah,* Hivi jee haya maneno 'Isipokua' katika aya ifuatayo yanamaanisha nini?'

﴿وَيَوْمَ يُنفَخُ فِي ٱلصُّورِ فَفَزِعَ مَن فِي ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَن فِي ٱلأَرْضِ إِلاَّ مَن شَآءَ ٱللَّهُ وَكُلٌّ أَتَوْهُ دَاخِرِينَ﴾

Wayawma yunfakhu fee alssoori fafaziAAa man fee alssamawati waman fee al-ardhi illa man shaa Allahu wakullun atawhu dakhireena*(Surat An Naml 27:87)*

Tafsir: ***Na Katika Siku litakapopulizwa Baragumu basi watafazaika wote waliomo Mbinguni na Ardhini Isipokua wale atakaotaka Allah (kua wasiwe na khofu) na wote watakuja kwake wakiwa wanyenyekevu.***

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Ni Mashahidi ndio watakaokua hawana khofu, na waliokua hai ndio watakua na khofu kubwa sana, kwani Mashahidi wanaishi na wako Pamoja na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kulishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaepusha na khofu hio na atawaamsha wakiwa ni wenye kujisikia hali ya usalama kabisa. Kwani hio itakua ni adhabu ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaadhibu wabaya zaidi miongoni mwa viumbe wake.'**

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمنِ الرَّحِيمِ ۞ يأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱتَّقُواْ رَبَّكُمْ إِنَّ زَلْزَلَةَ ٱلسَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ۞ يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّآ أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى ٱلنَّاسَ سُكَارَىٰ وَمَا هُم بِسُكَارَىٰ وَلَكِنَّ عَذَابَ ٱللَّهِ شَدِيدٌ﴾

Bismi Allahi Rahmani Rahiim; Ya ayyuha alnnasu ittaqoo rabbakum inna zalzalata alssaAAati shay-on AAadheemun; Yawma tarawnaha tadhhalu kullu murdhiAAatin AAamma ardhaAAat watadhaAAu kullu dhati hamlin hamlaha watara alnnasa sukara wama hum bisukara walakinna AAadhaba Allahi shadeedun*(Surat Al Hajj 22:1-2)*

Tafsir: ***Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwingi wa Huruma, Enyi watu Muogopeni Mola wenu kwani kwa hakika saa ya Mtetemeko itakua ni jambo kubwa sana, itakua ni siku ambayo mtaona ndani yake kila Mwanammke anaenyonyesha akiwa ni mwenye kumsahau mtoto wake***

mchanga na kila mja mzito atapukutisha alichokibeba (ndani ya tumbo lake) na utawaona watu wakiwa kama wamelewa, lakini hawakulewa, bali Adhabu ya Allah ni kali sana.

Hivyo watu watakua katika hali hio ya adhabu kwa kadiri atakavyo *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na itakua mda mrefu, na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamuamrisha Israfil kupuliza Baragumu kwa mpulizo wa kuanguka na kuzimia, na akipuliza kwa mpulizo huo basi kila mmoja ataanguka isipokuwa wale ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawajaalia wasianguke, wakati kila mmoja akiwa ameanguka na kupoteza fahamu na kua wabaridi basi Malaika wa Mauti ataenda kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kusema: 'Ewe Mola wangu, kila mmoja Mbinguni na Ardhi ni mwenye kufariki isipokua wale uliotaka kua wasife'

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atauliza ingawa ni mwenye kujua kwa kusema kua: 'Hivyo nani na nani wamebakia?'

Malakat al Mawt atajibu: 'Wale waliobaki ni wewe mwenyewe Mwenye kubakia Hai Milele na Kamwe Kutofariki, Malaika wabebao Arshi yako Tukufu, Mimi, Jibril na Mikail' ambapo baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Wacha Jibril, Mikail na Israfil wafe' na hapo Arshi Tukufu itasema: 'Ewe Mola wangu Jee Jibril na Mikail lazima wafe?'

***Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Kimya! Hakika mimi nimeandika kua kila aliechini ya Arshi yangu atakufa'**

Hivyo Malaika Jibril na Malaika Mikail watakufa, na kisha Malakat Al Mawt ataenda mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na atasema: 'Ewe Mola wangu, Jibril, Mikail na Israfil wameshafariki '

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atauliza tena ingawa ni mwenye kujua kwa kusema kua: 'Hivyo nani na nani wamebakia?'

Malakat al Mawt atajibu: 'Wale waliobaki ni wewe mwenyewe Mwenye kubakia Hai Milele na Kamwe Kutofariki, Malaika wabebao Arshi yako Tukufu na Mimi' hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Wacha na wabebaji wa Arashi nao wafe'

Malaika wabebaji Arshi na watafariki, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atauliza tena ingawa ni mwenye kujua kwa kusema kua: 'Hivyo nani na nani wamebakia?'

***Malakat al Mawt* atajibu: 'Wale waliobaki ni wewe mwenyewe Mwenye kubakia Hai Milele na Kamwe Kutofariki na Mimi.'**

***Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Wewe pia ni Viumbe miongoni mwa viumbe wangu, na nilikuumba kwa ajili ya kazi ambayo umeishuhudia, hivyo nawe pia Kufa.' Na Malakut Al Mawt atakufa na hivyo kua hakuna aliebakia isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala Al Wahidi, Al Hayy Al Qayyum, Al Fardun, Al Aziz, Al Qahar, Lam Yalid wa lam Yulad, Al Awwal Al Akhir,* atazikunja Mbingu na Ardhi kama yanavyokunjwa maandiko na kisha atasema: 'Mimi ndie Mfalme, ndie mwenye Kuweza kudhibiti kila kitu, ndie mwenye Kuweza kudhibiti kila kitu, ndie mwenye Kuweza kudhibiti kila kitu.'**

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atauliza mara 3: 'Hivi Jee Ufalme ni wa nani leo hii? Hivi Jee Ufalme ni wa nani leo hii? Hivi Jee Ufalme ni wa nani leo hii?' na hakuna atakejibu, kwa

sababu kila kiumbe kimefariki na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema kwa kuhoji kama zinavyosema aya:

﴿يَوْمَ هُم بَارِزُونَ لاَ يَخْفَىٰ عَلَى ٱللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ لِّمَنِ ٱلْمُلْكُ ٱلْيَوْمَ لِلَّهِ ٱلْوَاحِدِ ٱلْقَهَّارِ﴾

Yawma hum barizoona la yakhfa AAala Allahi minhum shay-on limani almulku alyawma lillahi alwahidi alqahhari*(Surat Ghafir 40:16)*
Tafsir: ***Katika siku ambayo wote watatoka nje, na hakuna kitakachofichikana kutokana nae Allah(Subhanah wa Ta'ala). Jee Ufalme ni wa Nani Leo hii? Ni wa Allah pekee mwenye kudhibiti kila kitu.***

Ambapo neno Barizuna linamaanisha Baraza au sehemu ambayo watu wanakaa na kuonana na kuonekana wazi pia, ambapo Waarabu hua ni wenye kusema kua Braza Fulanun yaani Namuona Fulani ametokezea.

Na hivyo aya kua ni zenye kumaanisha kua katika siku hio hakuna kitakachofichikana Ambapo anasema Abd Allah Ibn Masoud *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na aya hii kua ni yenye kuzungumzia kuhusiana na Siku ya Kufufuliwa ambapo Ardhi itakua kama Sahani Mpya ya Fedha ambayo haijafanyiwa Dhambi yeyote juu yake,na Watu watakusanywa pamoja Juu yake Kisha itanadia Sauti ya mwenye kunadia kwa kusema:

Hivi Jee Ufalme ni wa Nani leo hii?

Na Majini na Ibn Adam Waumini na Makafiri watasema: Ni wa Allah Al Wahidi Al Qahhar

Ambapo Waumini watajibu huku wakiwa ni wenye kujisikia Raha ndani ya Roho zao wakati wale waliokua hawakuamini basi Watajibu huku wakiwa wamejawa na Hali ya kua na Uchungu wa Kudhihirishiwa Ukweli wa Haki

Na kama ilivyosema katika aya nyengine ya Surat Ibrahim kua:

﴿يَوْمَ تُبَدَّلُ ٱلأَرْضُ غَيْرَ ٱلأَرْضِ وَٱلسَّمَاوَاتُ وَبَرَزُواْ لِلَّهِ ٱلْوَاحِدِ الْقَهَّارِ﴾

Yawma tubaddalu al-ardhu ghayra al-ardhi waalssamawatu wabarazoo lillahi alwahidi alqahhari*(Surat Ibrahim 14:48)*

Tafsir: ***Katika siku ambayo Ardhi itabadilishwa na kua Ardhi nyengine na Mbingu pia na Viumbe wote watakapotokea mbele ya Allah (Subhanah wa Ta'ala) Al Wahidi Al Qahhar.***

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataitandaza Ardhi na kuinyoosha na kua tambarare na iliyonyooka sawia bila ya kua na Milima wala mabonde kama zinavyoelezea aya:

﴿لاَّ تَرَىٰ فِيهَا عِوَجاً وَلاَ أَمْتاً﴾

La tara feha AAiwajan wala amtan*(Surat Ta-Ha 20:107)*

Tafsir: ***Na hutoona ndani yake muinuko wala mbonyeo.***

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **anaendelea kutuambia kua; Baada ya kufariki Viumbe wote hapo basi** ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atajaalia kutokea kwa Mtikisiko mkubwa sana katika Ardhi ambao utawasababishia Viumbe waliofariki kutikisika na kutokea Ardhini, ambapo waliokua juu ya Ardhi watakua juu ya Ardhi na waliozikwa watakua ndani ya Ardhi Na kisha Atatuma Maji kutoka chini ya Arshi yake Tukufu, na baada ya hapo itafuatia Mvua kubwa sana ambayo itanyesha Ardhini kwa mda wa siku 40.Kiasi ya kua Maji yake yatajaa na kufikia urefu wa yadi 12, na kufunika kila kitu.**

Kisha A*llah Subhanah wa Ta'ala* ataiamrisha Miili ya Viumbe kuota kama inavyoota Mimea hadi kufikia ukamilifu wa Viumbe husika Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala a*taamrisha kwa kusema: "Wacha Malaika Wabebao Arshi Wawe Hai" Na Malaika hao watakua hai na kisha ataamrisha Israfil Awe hai nae atakua hai. Na kisha Atamuamrisha Israfil Kuliweka Baragumu mdomoni mwake na atafanya hivyo.

Kisha Atamuamrisha Malaika Jibril na Mikail kua hai, nao watakua hai na Kisha ataamrisha Kuletwa kwa Roho zote mbele yake, ambapo nazo zitakuja mbele yake huku Roho za Waumini zikiwa zinang'ara na za Makafiri zikiwa zimejaa kiza.

Kisha A*llah Subhanah wa Ta'ala* atazichukua Roho zote hizo na kuzisukumiza kwenye Baragumu ndani yake.

Na kisha A*llah Subhanah wa Ta'ala* atamuamrisha Israfil kua apulize Baragumu hilo Israfil atapuliza Baragumu na hivyo Roho za Viumbe zitatoka kaa nguvu ndani yake na kuruka kama warukavyo Nyuki ambao wameenea kote Ardhini na Mbinguni

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Kwa Uwezo Wangu na Mamlaka yangu nataka Kila Roho iingie kwenye Kiwiliwili chake.'

Na hapo Roho hizo zitaingia ndani ya Miili ya Watu kwa kupitia Puani na kuenea mwilini kama vile Sumu inavyoenea ndani ya mwili wa mtu alietafunwa na Mdudu mwenye Sumu.

Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Baada ya Hapo Ardhi Itapasuka kwa ajili ya kukutemeni na mimi ndie nitakua wa mwanzo kutemwa kutokana nayo miongoni mwenu. Nanyi Mtatoka huku Mkikimbilia kwa haraka sana kuelekea mbele ya Mola wenu.'

Subhana Allah! Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atunusuru na Uzito wa Mitihani ya Juu ya Ardhi, ya Ndani ya Ardhi na ya siku hio ya Kupasuka kwa Ardhi...Aamiin

Tukio hili la kufuliwa kwa kutoka ndani ya ardhi kutokana na mtetemeko wake wa mwisho limezungumziwa ndani ya Qur'an pale aya ziliposema baada ya:

﴿بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ﴾

Bismi Allahi Alrrahmani AlRrahiimi.

﴿ إِذَا زُلْزِلَتِ ٱلْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ۞ وَأَخْرَجَتِ ٱلْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ﴾

Idha zulzilati al-ardhu zilzalaha, Waakhrajati al-ardu athqalaha*(Surat Al Zilzala 99:1-3)*

Tafsir: ***Itakapotetemeka Ardhi kwa Mtetemeko wake(wa Mwisho) Na Itakapotoa Ardhi Mizigo iliyomo ndani yake.***

Naam..hizi ni miongoni mwa Aya ambazo xinaelezea kuhusiana na tukio ambalo ni la Mtetemeko wa mwisho miongoni mwa Mitetemeko ya Ardhi., ambao ni Mtetemeko wa Kufufuliwa kwa kila Mtu baada ya Kufariki kwake kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Baada ya Hapo Ardhi Itapasuka kwa ajili ya kukutemeni na mimi ndie nitakua wa mwanzo kutemwa kutokana nayo miongoni mwenu. Nanyi Mtatoka huku Mkikimbilia kwa haraka sana kuelekea mbele ya Mola wenu.'**

Ambapo hili pia ni tukio lililoelezewa tena na *Surat Al Inshiqaq* pale iliposema baada ya Bismi Allahi Alrrahmani AlRrahiimi.

﴿ بِسْمِ اللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنشَقَّتْ ۞ وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ۞ وَإِذَا ٱلْأَرْضُ مُدَّتْ ۞ وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ ۞ وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴾

Idha alssamao inshaqqat, Waadhinat lirabbiha wahuqqat, Wa-idha al-ardhu muddat, Waalqat ma feeha watakhallat, Waadhinat lirabbiha wahuqqat *(Surat Al Inshiqaq 84:1-5)*

Tafsir: ***Pale Mbingu Zitakapogawanyika na Kufunguka Na zitakaposikiliza na Kumtii Mola wake kwani ni Lazima(Kwake) Kufanya hivyo Na Pale Ardhi Itakapotandazwa Na Itakapotupa nje (Ardhi) Vile vilivyomo ndani yake na kisha ikawa Tupu Na Itakaposikiliza na kufanya hivyo kwa Kumtii Mola wake, Na Ni Lazima (Kwake) kufanya hivyo.***

Subhanah Allah! Yaa Allah...Rabbana Ighfirlana wa Arhamna wa ArdhaAana..ya Rabbi!

Na ingawa aya hizi zimetumia neno *Adhinat* ambalo ni lenye kutokana na neno *Adhina* lenye kumaanisha Kupewa Idhini, Kupewa Ruhusa, Kukubalika kutokana na Maneno yake au Kusikilizika, Kutangazia.

Ambapo neno *Adhina* ndio lililotoa neno *Udhunun* yaani Masikio. Na pia likatoa neno *Adhana* yaani Tangazo au Wito wa Kitu au wa Sala.

Lakini kwa upande mwengine basi tunapoziangalia aya mbili hizi za Surat Al Inshiqaq zilizotumia neno hili Adhinat, Pale zilipozungumzia Matukio ya Mbingu na Ardhi kwa kila moja kua na hali ya *Wa Adhinat Lirabbiha wa Huqqat.*

Basi tunaona kua Sultan Al Balagha Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari, Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi, Imam Al Qurtubi na kadhalika basi wanasema kua: **'Neno *Adhinat Li Rabbiha* halimaanishi Kua ni Kutokana na Idhini ya Mola wake. Bali yanamaanisha Kutokana na Utiifu wa Vitu hivyo juu ya Mola wao. Yaani Mbingu na Ardhi zitafanya**

yatakayofanywa navyo kwa sababu ya Utiifu wao juu ya Mola wao kwani utiifu huo ni Wajibu wao.'

Na kuhusiana na Kutema kwake hivyo Ardhi basi ingawa Hadithi zinasema kua Ardhi Itawatema Watu wote waliomo ndani yake tangu mwanzo wa Dunia hadi mwisho wake, tena wakiwa katika hali kama walivyokua nayo hapo kabla walipokua wakiishi Duniani.

Lakini kwa upande mwengine basi baadhi ya Wanazuoni wanasema kua: '**Baada ya Kutemwa kwa Watu na Ardhi, basi Ardhi itatema kila aina ya Madini ya Thamani yaliyomo ndani yake, kuanzia Dhahabu, Almasi, Fedha, Platinum, Titanium n.k**

Na hivyo Ibn Adam wataziona Mali hizo na Kugundua kua Mali zote hizo hazikua chochote isipokua ni kwa Kumsababishia kupata Adhabu kutoka ksa Mola wake kwani Ameua, Amedhulumu, Ameiba n.k kwa ajili ya Mali hizo ambazo hazina maana yeyote katika siku hio.'

Katika kuelezea tukio la siku hio la Mtetemeko wa Ardhi ambao utapelekea kufufuliwa kwa Banu Adam ambao walikua wako Makaburini mwao kwa mda mrefu na hivyo kua kama Waliojisahau kua Watafufuliwa na kuhukukiwa, basi Watu Watashtuka kutokana na mtetemeko huo utakaowatupa nje ya tumbo la Ardhi na hivyo watauliza kama zinavyosema Aya:

﴿ وَقَالَ ٱلۡإِنسَانُ مَا لَهَا ﴾

Waqala Al Insanu Malaha. *(Surat Az Zalzala 99:3)*

Tafsir: ***Na Watasema Watu: Ina Nini hii Ardhi leo hii?***

Na katika kuelezea tukio la siku hio la kufufuliwa kwa Banu Adam na Majini *basi Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua:

﴿ خُشَّعاً أَبۡصَارُهُمۡ يَخۡرُجُونَ مِنَ ٱلۡأَجۡدَاثِ كَأَنَّهُمۡ جَرَادٞ مُّنتَشِرٞ ۝ مُّهۡطِعِينَ إِلَى ٱلدَّاعِۖ يَقُولُ ٱلۡكَافِرُونَ هَٰذَا يَوۡمٌ عَسِرٞ ۝ ﴾

KhushshaAAan absaruhum yakhrujoona mina al-ajdathi kaannahum jaradun muntashirun, MuhtiAAeena ila alddaAAi yaqoolu alkafiroona hadha yawmun AAasirun *(SuratAl Qamar 54:08)*

Tafsir: ***Huku wakiwa na Unyenyekevu ndani ya Mtizamo ya Macho yao Watatoka Ndani ya Makaburi yao Kama Nzige waliokua Wametawanywa kwenye Eneo kubwa sana Wakikimbilia kwa haraka kwa Muitaji Watasema Makafiri Hii Leo ni Siku Nzito Sana.***

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m anaendelea kutuambia kua: **'Katika Siku hio Watu watakua Bila ya Viatu na Watakua Uchi, na Hakuna alietahiriwa na Watasimamishwa kisimamo ambacho ukubwa wake ni Miaka 70 Ambapo ndani ya Kipindi hicho itakua hakuna atakaewatizama wala atakaehukumu baina yenu.**

Hivyo Mtalia hali hadi Machozi yenu yatakatika, na kisha mtaanza kulia machozi ya Damu huku mkitokwa na Majasho ambayo yatamwagika na kukufikieni hadi kwenye Pua zenu, na kwenye ndewe za Masikio yenu na mtakua mkiulizana kwa kusema 'Hivi Jee ni Nani atakaetuombea mbele ya Mola wetu hii leo ili tupate kuhukumiwa makosa yetu?'

Na kisha mtasema : 'Hakuna anaestahiki kutuombea isipokua Baba yetu Adam, kwani yeye ameumbwa kwa mikono ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha akampulizia Roho yake na pia amezungumza nae moja kwa moja. Watu wataenda kwa Nabii Adam na kumuomba Awaombee ili wahukumiwe, lakini nae atakataa na kusema : 'La Mimi Sistahiki kukuombeeni.'

Watu wataondoka kwa Adam na kumfuata Kila Mtume mmoja baada ya Mmoja Lakini kila Mtume wanaomfuata awaombee atakua ni mwenye kuwakatalia.

*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam a*naendelea kusema kua: **Mwisho watakuja Watu Watakuja Mbele yangu na kuniomba nikawaombee kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala***

Nami nitaenda mbele ya Arshi Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kusjudu Nami nitabakia katika hali hio ya Kusjudu hadi pale Atakapotokea Malaika na Kunishika Mabega yangu na Kuninyanyua. Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Ya Muhammad!'

Nami nitajibu : 'Naam ya Rabbi!'

***Allah Subhanah wa Ta'ala* ataniuliza ijapokua ni mwenye kujua kwa kusema: 'Unataka Nini? Nami nitasema : Ewe Mola wangu, Hakika wewe uliniahidi Kua Utanijaalia kua ni mwenye kua na uwezo wa Kuwaombea Viumbe wako, Hivyo na kuomba kwa Ruhusa yako, anza kuwahukumu Viumbe wako.'**

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Nimekubalia maombezi yako juu ya Viumbe wangu Ewe Muhammad, Hivyo nitaaanza kuhukumu baina yenu.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi aa Salam* anaendelea kutuambia kua: 'Hivyo Mimi nitarudi katika nafasi yangu miongoni mwa Viumbe wenzagu na kisha tutasikia sauti ya Kushtusha sana ambayo itatuingiza sote katika hali ya Khofu kubwa sana.**

Na Kisha baada ya Hapo tutashangazwa na Mshuko wa Viumbe wa Mbingu iliyopo karibu na Ardhini ambao Idadi yake itakua Maradufu ya Idadi ya Watu wote na Majini Wote waliokuwepo kwenye mkusanyiko huo. Subhanah Allah!

Naam...bila ya shaka Tunapozungumzia wingi wa Viumbe Malaika basi idadi yake haitajiki, yaani hapa nataka tutafakari kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anasema kua : **'Watashuka Malaika wa Mbigu ya Mwisho iliyokaribu na Ardhi tu,ambao idadi yake ni mara dufu yaani mara mbili ya Idadi ya Ibn Adam na Majini wote Tangu kuanza kuumbwa kwa ulimwengu hadi mwisho wake'**

Hivyo Hio Idadi sio mchezo, na hapa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amezungumzia Malaika wanaoishi kwenye Mbigu moja tu iliyokaribu na Ardhini, ambapo inatubidi tukumbuke kua Mbingu ziko Saba. Kwani Malaika wote hao kazi ya ni Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'al*a na Kumtukuza, hivyo na hii inatuoneshea wazi kua Ibada zetu mimi na wewe hazimpunguzii wala hazimzidishii kitu *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo yeye hana haja nazo.

Ila kufanya kwetu Ibada hizo hua kunatunufaisha katika kuonesha Utiifu mbele ya Muumba na kutafutia sisi wafanyaji Ibada hizo njia ya kuupata Ukaribu wa A*llah Subhanah wa Ta'ala*, kupata ridhaa zake na kuingizwa ndani ya Rehma zake na kuupata Unafuu katika siku hii ya Kufufuliwa tunayoizungumzia.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anatueleezea kwa kusema. **'Hivyo Mimi nitarudi katika nafasi yangu miongoni mwa Viumbe wenzagu na kisha tutasikia sauti ya Kushtusha sana ambayo itatuaingiza sote katika hali ya Khofu kubwa sana'**

Na Kisha baada ya Hapo tutashangazwa na Mshuko wa Viumbe wa Mbingu iliyopo karibu na Ardhini ambao Idadi yake itakua Maradufu ya Idadi ya Watu wote na Majini Wote waliokuwepo kwenye mkusanyiko huo Malaika hao watakapofika Karibu na Ardhi basi Ardhi Itakua ni yenye kujaa Mwangaza kutokana na Nuru ya Malaika Hao

Na Watakapokua wanajipanga Safu basi wataulizwa: 'Hivi Jee Mmekuja pamoja na Mola wenu?'

Ambapo Malaika hao nao watajibu kwa kusema: 'La lakini atakuja'

Na Kisha watashuka Malaika wa Mbingu ya Pili kutoka Ardhini kuelekea Juu Ambao nao Idadi yake itakua mara dufu ya Idadi ya Malaika wa Mbingu ya Kwanza walioshuka hapo kabla

Na watakapofika Karibu ya Ardhi basi Ardhi Itajaa mwangaza kutokana na Nuru yao

Ambapo wakati wanajipanga Safu basi wataulizwa: 'Jee Mmekuja na Mola wenu?'

Nao watajibu: 'La, Lakini atakuja'

Na kisha watashuka Malaika wa Mbingu ya Tatu Ambao wingi wake ni mara dufu ya Idadi ya Malaika ya Mbingu ya Pili, nao Wataing'arisha Ardhi na baada ya kujipanga basi wataulizwa kama walivyoulizwa Malaika waliotangulia na Watajibu kama walivyojibu Malaika waliotangulia

Hali itaendelea kama hivyo kwa kushuka Malaika wa Mbingu zote Saba Mbingu moja baada ya nyengine Na Kisha baada ya kumalizika basi Watafuata Malaika wabebao Arshi Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambao wako wanne

Malaika hao Miguu yao inasimamia chini kabisa kwenye Ardhi ya Saba, na Mbingu na Dunia zitakua Pembeni yao kutokana na Ukubwa wa Maumbile yao

Na watakua wameibeba Arshi T*ukufu ya Allah Subhanah wa Ta'ala* baina ya Mabega yao Na watakua wakifanya Tasbih kwa sauti inayosikika kila mahali kwa maneno yasemayo:

سبحان ذي العرش والجبروت، سبحان ذي الملك والملكوت، سبحان الحي الذي لا يموت، سبحان الذي يميت الخلائق ولا يموت، سُبُّوح قدوس قدوس قدوس، سبحان ربنا الأعلى، رب الملائكة والروح، سبحان ربنا الأعلى، الذي يميت الخلائق ولا يموت،

Subhanah Dhi Arshi Wa Al Jabaruti Subhanah Dhi Al Mulki wa Al Malakuti Subhanah Al Hayyi Ladhii la Yamut Subhanah Al Ladhii Yumiit Al Khalaik Wala Yamut Subuh Quddus Quddus Quddus Subhanah Rabbi Al Aala Rabbu Al Malakuti wa Al Ruh Subhanah Rabbana Al Aala Al Ladhii YumitAl Khalaiq wala Yamut.

Tafsir: **Utukufu ni wake Mwenye Umiliki wa Arshi Tukufu na mwenye Uwezo Juu ya Kila Kitu Utukufu ni wake mwenye Umiliki wa Kila Kitu na Ufalme Juu ya Kila kitu - Ametakasika Yule Ambae Yuko Hai na Kamwe Hatufariki Utukufu ni wake yule ambae ni Mwenye Kuvifisha Viumbe na wala yeye si mwenye kufa Utukufu wake Mtakatifu Mtakatifu Mtakatifu Utukufu ni wake Mola wetu Aliejuu kwa Utakatifu Mola wa Malaika na Roho Utukufu ni wake Mola wetu Utukufu ni wake Mwenye Kuwafisha Viumbe Lakini yeye si mwenye kufa.**

Na kisha baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataiweka Arshi yake juu ya Ardhi yake pale atakapo kuiweka Na Kisha ataanza kuzungumza na Viumbe wake Na Kisha ataanza kuzungumza na Viumbe wake Kwa kusema kua:

‘Enyi Viumbe Ibn Adam na Majini, Hakika mimi nimekua nikikaa kimya tangu hapo nilipokuumbeni nyinyi hadi hii leo, nikiwa ni mwenye kusikiliza maneno yenu na kuangalia Matendo yenu Hivyo leo hii Nyinyi Mtakaa kimya na mtakua ni wenye kua na umakini name.

Ni Matendo yenu na Vitabu vya Amali zenu ndivyo vitakavyosomwa mbele yenu Hivyo Yeyote yule atakaekua ni mwenye kua na Mema basi na amshukuru Mola wake Na yeyote yule atakaekua ni Mwenye kua na Maovu basi hana wa Kumlaumu isipokua Nafsi yake mwenyewe.’

Na baada ya hapo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha Moto wa Jahannam usogezwe karibu, na ukisha sogezwa basi ndani yake itatoka Shingo kubwa sana ya Moto huo na Itakayonukuu maneno ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa kusema:

﴿ أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يٰبَنِيٓ آدَمَ أَن لاَّ تَعْبُدُواْ ٱلشَّيطَانَ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ۞ وَأَنِ ٱعْبُدُونِى هَـٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ۞ وَلَقَدْ أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلاًّ كَثِيراً أَفَلَمْ تَكُونُواْ تَعْقِلُونَ ۞ هَـٰذِهِ جَهَنَّمُ ٱلَّتِى كُنتُمْ تُوعَدُونَ ۞ ٱصْلَوْهَا ٱلْيَوْمَ بِمَا كُنتُمْ تَكْفُرُونَ﴾

Alam aAAhad ilaykum ya banee adama an la taAAbudoo alshshaytana innahu lakum AAaduwwun mubeenun; Waani oAAbudoonee hadha siratun mustaqeemun; Walaqad adhalla minkum jibillan katheeran afalam takoonoo taAAqiloona; Hadhihi jahannamu allatee kuntum tooAAadoona; Islawha alyawma bima kuntum takfuroona*(Surat Yasin 36:60-64)*

*Tafsir: **H**ivi* **Jee sikukuamrisheni Mimi Enyi Bani Adam kua Msimuabudu Shaytan Kwani Kwa Hakika yeye Kwenu ni Adui aliekua Wazi? Na Mniabudu Mimi Pekee Kwani hii ndio Njia Iliyonyooka 'Na Kwa hakika Amekudhalilisheni (kwa kukupotosheni) Miongoni mwenu kwa Wingi sana Hivi Jee Hamkuwahi kua na Akili Nyinyi? Hivyo Hii ndio Jahannam Ambayo Mlikua mmeahidiwa. Hivyo Wiveni Ndani yake leo hii kutokana na yale Mliyokua Mkipingana nayo**

Subhanah Allah!...Allahuma Aajirna Minna Nnar..Aamiin

Maneno haya ya Aya 5 za Surat Yasin. Sura ambayo mara kwa Mara tunaisoma lakini ni wachache wenye kujua maana ya maneno wanayoyasoma ambayo ni yenye ujumbe mzito sana ambayo yanatudhihirishia kua Shaytan au Ibilisi hakupewa Uwezo wa Nguvu za kimwili katika kumlazimisha Ibn Adam kufanya Maovu na hivyo kuelekea katika njia ya Upotovu.

Bali amepewa Uwezo wa Kumshauri Ibn Adam, Kumtia Ari, Kumshawishi kwa kupitia njia ya Kumtia wasiwasi kwenye Vifua na Ufahamu wa Ibn Adam. Na hapo hapo Ibn Adam amepewa Uwezo wa Kuthibiti Moyo wake na Ufahamu wake kwa kutumia Akili yake na pia akaoneshwa njia ya Kumuelekea Mola wake katika kila kitu chake kupitia katika Miongozo ya Mitume wa Mola wake na ujumbe wa Uongofu uliomo ndani ya Vitabu vyake alivyowashushia Mitume wake.

Na si hivyo tu, bali Ibn Adam Khiari pia Amejaaliwa Khiari ya kua na Maamuzi huria ya Aidha kufuata Mola wake kwa Kumtii na kua ni mwenye kumkufuru Ibilsi au kumuasi Allah Subhanah wa Ta'ala na hivyo kua ni mwenye kufuata Maamrisho ya Ibilisi na kua ni sawa na Mwenye kukuabudu Ibilisi kama zinavyosema Aya.

Ambazo pia ndani yake zimeweka wazi kua Ibilisi huyo ni Adui Mkubwa aliekua wazi kwa Ibn Adam. Haya yatakua maneno ambayo yatawafanya Bani Adam waliokua wamemuasi Mola wao na kua ni wafuasi wa Ibilisi kua ni wenye hali ya Majuto Makubwa sana.

Ambayo hata hivyo Majuto hayo hayatowanufaisha kitu, kwani hali inakua ni sawa na Mtu alikimbilia Kufunga Mlango wa Banda la Farasi, wakati Farasi wote ameshakimbia kutoka ndani ya Banda lake hilo.

Na hivyo kua ni Mwenye kubakiwa na Banda bila ya kua na Farasi hata mmoja ndani yake na uwezo wa Kununua tena Farasi hana! Hivyo Nasi Wakati wetu wa kufanya Mema ndio huu kwani tukishakua hatupo basi na wakati wetu hua haupo kwani wakati wetu huhesabika kutokana na kuwepo kwetu.

Kwani siku hio itakua ni siku nzito kwa kila Mtu, na kila kila mtu atakua anahijati uombezi ambao hata hivyo hautomfaa kila mtu, kwani ni wale tu watakaoridhiwa na Mola wao kutokana na Matendo yao mema hapa Duaniani ndio wtakaopata Uombezi huo kama anavyotuwekea wazi *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale alipohoji *k*uhusiana na uombezi huo kwa kusema katika sehemu nyengine ndani ya Kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَكَمْ مِّن مَّلَكٍ فِى ٱلسَّمَاوَاتِ لاَ تُغْنِى شَفَاعَتُهُمْ شَيْئاً إِلاَّ مِن بَعْدِ أَن يَأْذَنَ ٱللَّهُ لِمَن يَشَآءُ وَيَرْضَىٰ﴾

Wakam min malakin fee alssam<u>a</u>w<u>a</u>ti l<u>a</u> tughnee shaf<u>a</u>AAatuhum shay-an ill<u>a</u> min baAAdi an ya/<u>dh</u>ana All<u>a</u>hu liman yash<u>a</u>o wayar<u>dha</u>*(Surat An Najm 53:26)*

Tafsir: **Na wangapi miongoni mwa Malaika walio Mbinguni (huwaombea watu) ambapo hauwanufaishi chochote uombezi wao isipokua kwa Idhini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa wale awatakao na awaridhiao.**

Allah Subhanah wa Ta'ala anaendelea kuelezea hali itakvyokua katika siku hio kwa kusema:

﴿وَتَرَىٰ كُلَّ أُمَّةٍ جَاثِيَةً كُلُّ أُمَّةٍ تُدْعَىٰ إِلَىٰ كِتَابِهَا ٱلْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

Watara kulla ommatin jathiyatan kullu ommatin tudAAa ila kitabiha alyawma tujzawna ma kuntum taAAmaloona*(SuratAl Jathiya 45:28)*

*Tafsir: **Na Utaona Kila Umma wa Watu Ukiwa Umepiga Magoti Kila Ummah Utaitwa Kwa Kitahu chake (Cha Amali zao) Siku hio Mtalipwa kutokana na Yale mliyokua Mkiyafanya.***

Naam, hio ni aya ya Surat Al Jathiya ambayo inaelezea tukio la watu kubakia katika hali ya kupiga magoti mara baada ya kufufuliwa bila kuhojiwa chochote hadi pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam at*akaposjudu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika *Maqamat Mahmuda* na kuomba kua bora watu Wahukumiwe.

Neno Jatha kwa Lugha ya Kiaraju hua ni lenye kumaanisha Kuchutama, Kukaa katika hali ya mkao wa Magoti kua ni yenye kugusa chini ulipokaa, Kukaa kitako huku miguu ikiwa imesimamia Vidole, Kukaa kitako mbele ya Mtu huku Magoti yenu yakiwa yamegusana.

Na ingawa kama tulivyoona kua neno Jathiyat maana yake ni Kuchutama au kupiga magoti, kama alivyosema ImamAd Dahhaq Ibn Muzahim, lakini kwa upande mwengine basi tunaona kua anasema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Maana ya Neno Jathiyatan hua ni Kukusanya pamoja Na ukweli ni kwamba Waarabu wa Quraysh walikua wakutumia neno Jathiya kumaanisha Kukusanya pamoja na kuweka katika kua chini ya hali ya Unyenyekevu.'**

Kwa maana hio basi Neno Jathiyah hua linaingia kotekote kimaana kama walivyotafsiri Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu anhu* na Imam Ad Dahhaq Ibn Muzahim kwani katika Siku hio basi Watu watakua wamekusanyika pamoja wakiwa wamekaa kwa Unyenyekevu kwa Makundi kulingana na Ummah walioishi nao.

Kwani neno Jathiya limetumika tena katika Aya za Surat Maryam pale zilipoelezea tena tukio la baada ya kufufuliwa kwa kuanzia kwenye aya ya 66 hadi 72 kwa kusema:

﴿ وَيَقُولُ ٱلْإِنسَانُ أَإِذَا مَا مِتُّ لَسَوْفَ أُخْرَجُ حَيّاً ﴾

Wayaqoolu al-insanu a-idha ma mittu lasawfa okhraju hayyan, *(Surat Maryam 19:66)*

*Tafsir: **Na Hivi Anasema Mtu Hivi Baada ya Kufa Mimi Nitafufuliwa Kua Hai Tena?***

Ambapo aya hii inaelezea ni maneno ya wale Wasioamini, Hivyo baada ya hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anajibu kwa kusema hoja kwa kusema:

﴿ أَوَلاَ يَذْكُرُ إِلإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِن قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْئاً ۞ فَوَرَبِّكَ لَنَحْشُرَنَّهُمْ وَٱلشَّيَاطِينَ ثُمَّ لَنُحْضِرَنَّهُمْ حَوْلَ جَهَنَّمَ جِثِيّاً ﴾

Awa la yadhkuru al-insanu anna khalaqnahu min qablu walam yaku shay-an, Fawarabbika lanahshurannahum waalshshayateena thumma lanuhdirannahum hawla jahannama jithiyyan *(Surat Maryam 19:67-68)*

Tafsir: ***Hivi Hakumbuki Mtu Kua Sisi Tulimuumba Hapo Kabla Wakati akiwa si Chochote si Lolote? Hivyo Kwa Hakika kwa Mola wako Tutakusanyeni (na Kukuunganisheni Viungo na Miili yenu) Na (Majini na) Mashaytani pia nao Na Kisha Tutawahudhurisha Ndani ya Moto wakiwa wamepiga Magoti.***

Subhnaha Allah...Ya Allah tunusuru na Jahannam..Amiin

Aya zinatuonesha kua baada ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuombwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua apitishe Hukumu kwa Viumbe wake ambao tayari wameshakaa kwenye Uwanja wa Kufufuliwa kwa mda wa Miaka 70 ya Akhera na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akakubali kupitisha hukmu yake kwa Kila Kiumbe chake basi hatoanza kuwashughulikia Ibn Adam wala Majini kwanza. Bali ataanza na Viumbe Wanyama hadi pale atakapomalizana nao katika kupitisha hukmu ya kiuadilifu kwa Wanyama hao, kiasi ya kua katika kuhukumiwa huoo basi hata Mbuzi mwenye Pembe ataulizwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwanini akampiga pembe Mbuzi mwenzake ambae yeye hakujaaliwa kua na Pembe?

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawahoji wanyama wote hadi Kufikia hali ya kua hakuna hata mnyama mmoja kua ni mwenye kubakiwa na kinyongo na mnyama mwenzake. Ambapo baada ya kupitishwa kwa Hukmu baina ya Wanyama wote hao basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema kuwaambia Wanyama hao kua: **'Kuweni Jivu!'**

Na hapohapo Wanyama hao watakua Majivu, na kisha baada ya hapo sasa ndio kazi itaanza Kwa viumbe Ibn Adam na Majini kuanza ambapo baada ya Ibn Adam na Majini kuona namna walivyohukumiwa Wanyama basiiuna watu watasema, Yalaiti na Mimi bora ningekua Mbuzi,na kuna watakaosema kua Yalaiti bora mimi ningekua Jivu.

Kwani anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu cha Qur'an katika kutukumbusha hali itakavyokua kua:

﴿ إِنَّآ أَنذَرْنَاكُمْ عَذَاباً قَرِيباً يَوْمَ يَنظُرُ ٱلْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ وَيَقُولُ ٱلْكَافِرُ يٰلَيْتَنِي كُنتُ تُرَاباً ﴾

Inna andharnakum AAathaban qareeban yawma yan*th*uru almaro ma qaddamat yadahu wayaqoolu alkafiru ya laytanee kuntu turaban *(Surat An Naba 78:40)*

Tafsir: ***Hakika Sisi Tumekuonyeni kuhusiana na Adhabu Yenye kukaribia Katika Siku ambayo ataona Mtu Amali zilizotangulizwa Na Mikono yake Na Watasema Makafiri (Wale wanaopinga) Ya Laiti Bora Mimi ningekua Jivu.***

Naam..haya ni maneno ambayo yanatudhihirishia namna hali itakavyokua, katika siku ya Malipo ya Adhabu kulingana na makosa tuliyoyafanya bila ya kuomba msamaha baada yake na hii ni siku ya

Adhabu kwa waliofanya makosa ya maasi kisha hawakutubu ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua Ni Qariban..yaani iliyokaribu sana.

Ambapo ingawa katika kuzungumzia kwetu kuhusiana na Dalili kuu za Kiama basi tulisema kua kwa kizazi chetu basi siku hizo ziko mbali sana kaa sisi na Wajukuuu zetu tutakua tumeshafariki. Lakini hii ni kwa kipimo cha kuwepo kwetu hapa Duniani yaani hatutofikia wakati huo.

Ila sasa tatizo ni kua katika kuishi kwetu hapa Duniani hata tuishi kwa umri wa miaka 1000 kama alivyoishi Nabii Nuh, Basi mda huo utakua mdogo sana na usiokua na masafa marefu baina yake, kwani hata Nabii Nuh alipoulizwa vipi anajihisi ameishi mda gani Duniani basi alijibu kua alijihisi kama kwamba mtu alieingia Nyumbani kwake kwa Mpito wa kupitia Mlango wa mbele na kisha moja kwa moja akatokea kwa Mlango wa Nyuma bila ya kusimama hata ukumbini kwake.

Na pia kama tulivyoona katika Tafsiri ya kisa cha Fityatun yaani Vijana Shujaa wa as-hab Al Kahf waliolala kwa miaka 309 na walipoamka walisema kua wamelela kwa Masaa tu.

Hivyo ndivyo hali itakavyokua kwa upande wetu baada ya kufariki, kwani nasi hata kama tutakaa Makaburini kwa miaka 10000 basi tukifufuliwa itakua kama tulikufa kwa mda wa Masaa tu na tukafufuliwa. Na huo ndio Ukaribu wa siku ya Malipo kwa kila Mtu.

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuelezea hali itakavyokua kwa kila Muasi ambae atakua na sifa ya kua ni Adui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika siku hio inayokaribia kwa kusema:

﴿وَيَوْمَ يُحْشَرُ أَعْدَآءُ ٱللَّهِ إِلَى ٱلنَّارِ فَهُمْ يُوزَعُونَ ۞حَتَّىٰٓ إِذَا مَا جَآءُوهَا شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَأَبْصَارُهُمْ وَجُلُودُهُم بِمَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ ۞وَقَالُواْ لِجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدتُّمْ عَلَيْنَا قَالُوٓاْ أَنطَقَنَا ٱللَّهُ ٱلَّذِى أَنطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُوَ خَلَقَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ۞ وَمَا كُنتُمْ تَسْتَتِرُونَ أَن يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلاَ أَبْصَارُكُمْ وَلاَ جُلُودُكُمْ وَلَـٰكِن ظَنَنتُمْ أَنَّ ٱللَّهَ لاَ يَعْلَمُ كَثِيراً مِّمَّا تَعْمَلُونَ﴾

Wayawma yu<u>h</u>sharu aAAda<u>o</u> Alla<u>h</u>i ila alnna<u>r</u>i fahum yoozaAAoona. <u>H</u>atta <u>i</u>dha ma jaooha shahida AAalayhim samAAuhum waabsaruhum wajulooduhum bima kanoo yaAAmaloona. Waqaloo lijuloodihim lima shahidtum AAalayna qaloo antaqana Allahu allathee antaqa kulla shay-in wahuwa khalaqakum awwala marratin wa-ilayhi turjaAAoona, Wama kuntum tastatiroona an yashhada AAalaykum samAAukum wala absarukum wala juloodukum walakin *dh*anantum anna Allaha la yaAAlamu katheeran mimma taAAmaloona*(*Surat Fusilat 41:19-23)*

Tafsir: ***Na Katika Siku Ambayo Maadui wa Allah Watakusanywa kwa ajili ya Moto Na Hivyo Watakusanyika (Na kuhojiwa kuanzia Waasi wa Tangu Mwazo wa Dunia hadi mwisho wa Dunia) Hadi Pale watakapoufikia (Moto Huo) Basi Watatolewa Watatolewa Ushahidi Na Kusikia kwao (Kwa Masikio) Na Kuona kwao (Kwa Mtizamo wa Macho) Na Kwa Ngozi zao Kutokana na Yale waliyokua wakiyafanya - Na Watasema Watu hao Kuziambia Ngozi za Miili yao Hivi Kwa Nini Mnatoa Ushahidi Dhidi yetu? (Ambapo) Zitasema (Ngozi hizo) Ametufanya Tuzungumze sisi Allah Kama vile ambavyo alivyovifanya Vitu vyote vizungumze Na Yeye ndie aliekuumbeni Mara Ya kwanza Na Kwake yeye Mmerudishwa Na Kamwe nyinyi hamkua ni wenye kuweza Kujificha***

(kutokana nasi) Ili Msishuhudiwe Na Masikio yenu Wala Macho yenu Na Wala na Ngozi zenu Bali Mlikua Mkidhani Kua kwa Hakika Allah Hajui Mengi sana Katika yale mliyokua Mkiyafanya

Hivyo mbali ya kua Kiungo ngozi ni Kiungo kinachopendezesha Miili yenu na hivyo kuhifadhi viungo na mifumo ya Ufanyaji kazi za ndani ya miili yetu isionekane inavyofanya kazi.

Yaani kwa mfano unapokula basi Usione namna Chakula kinavyopita Kwenye Njia yake na kuchujwa hadi kua makapi na kufikia hali ya kua ni Uchafu Unaonuka na unaotakiwa kutolewa nje, kwani kama uchafu huo utaonekana na kutoka mbele za Watu basi Tutakimbiana na hakutokalika. Basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameijalia Ngozi kua ni Stara ya Aibu za Ndani ya Miili yetu na pambo la Miili yetu, na Kiungo cha hisia chenye kazi ya Kuhisi hisia mbali mbali ikiwemo ya maumivu kwa ajili ya kututaarifu kua na hadhari dhidi ya hatari za kimazingira katika maisha yetu zinazoweka Kuidhuru Miili yetu na hata kusababishia Kifo. Kuwasilisha hisia za mahusiano baina yetu na pia baina ya viumbe wengine kama misisimko ya mapenzi, Khofu maliwazo n.k.

Kudhibiti hali ya Joto ya mwili inapokua imezidi na inapokua imepungua n.k Lakini pia Ngozi zetu zimejaaliwa kua ni viangalizi vinavyotushuhudia matendo yetu katika kila sekunde ya Uhai wetu hapa Dunianina hivyo basi katika siku ya Malipo Ngozi hizi zitatoa ushahidi juu ya kila kitu chetu cha kheri na cha uovu, na hali ya uhalisia ni kua hata ukijichuna ngozi yako basi viungo vyengine vyote vy amwili ni venye kukushushudia pia na vitato ushahidi kama zinavyosema aya.

Kwani anasema pia *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat An Nur kua:

﴿ يَوْمَ تَشْهَدُ عَلَيْهِمْ أَلْسِنَتُهُمْ وَأَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ ﴾

Yawma tashhadu AAalayhim alsinatuhum waaydeehim waarjuluhum bim<u>a</u> k<u>a</u>noo yaAAmaloona *(Surat Nur 24:24)*

Tafsir: ***Siku Ambayo Watatolewa ushuhuda na Ndimi zao Na Mikono yao Na Miguu yao Juu ya Yale waliyokua Wakiyafanya.***

Na kama alivyosema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika *Surat Yasin* kua

﴿ ٱلْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰٓ أَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَآ أَيْدِيهِمْ وَتَشْهَدُ أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُواْ يَكْسِبُونَ﴾

Alyawma nakhtimu AAal<u>a</u> afw<u>a</u>hihim watukallimun<u>a</u> aydeehim watashhadu arjuluhum bim<u>a</u> k<u>a</u>noo yaksiboona*(Surat Yasin 36:65)*

Tafsir: ***Leo Hii Tutaifunga Midomo yao Na Watakua wakizungumza Kwa Mikono Yao Na Watatolewa Ushahidi na Miguu yao Juu ya yale Waliyokua wakiyafanya.***

Hivyo aya zote hizi zinaonesha kua katika siku hio basi kuna wakati wa kuhojiwa kua Midomo wala Ndimi haitokua na uwezo wa Kujibu yale yanayoulizwa, bali vitakua viungo vyengine vya mwili ndio vitakavyojibu, kama mikono, Miguu, Masikio, Macho, Ngozi ya mwili mzima n.k

Kama alivyosema Abu Hurayrah *Radhi Allahu anhu* kua: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Katika Siku ya Malipo kila Mnafiq atakua ni mwenye kusema: Ewe Mola wangu, hakika mimi nilikua ni mwenye kukuamini wewe, na Mitume wako na Vitabu vyako, na nilikua nikisali, nikifunga na kutoa Sadaka.' Ambapo katika hali kama hii basi Mnafiq huyo atakua ni mwenye kuendelea kujisifu zaidi na zaidi : Na kisha baada hapo Allah *Subhanah wa Ta'ala* atasema: 'Tutayaona yote hayo kutokana na Mashahidi watakaposhuhudia' Ambapo Mnafiq huyo atashtuka na kushangaa na kujiuliza, ni Mashahidi gani hao tena?**

Na kisha Mdomo wake Utazibwa na baada ya hapo Mapaja yake, Nyama zake na Mifupa yake itaamrishwa kuzungumza Na hapo sasa Viungo vyote hivyo vitaanza kutoa Ushahidi juu ya yale yaliyokua yakifanywa na Mwili wake Na hili litafanywa ili Ibn Adam asije akatoa Hoja ya Malalamiko dhidi ya *Allah Subhana wa Ta'ala* *(Sahih Muslim)*

Subhanah Allah!

Kwani tunakumbushana tena juu ya kujiangalia Nafsi zetu na kujihesabu kabla ya kufika siku ya kuhesabiwa kisha viungo vyetu kimoja baada ya kimoja vikatoa Ushahidi Ambapo baada ya Maombi hayo ambayo yatakubaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Ibn Adam na Majini wataanza Kuhukumiwa, kama zinavyosema Aya na Hadith kua Midomo yetu haitosema bali viungo vya Mwili ndio vitakavyosema na kutoa Ushahidi wa yale yote tuliyoyatenda.

Na hii haimaanishi kua Midomo haitosema kabisa, la, kwani itaruhusiwa kusema lakini pale baada ya viungo vya Mwili kutoa Ushahidi dhidi ya Kiumbe husika na hivyo basi midomo na ndimi zake zitakua ni zenye kuvihoji viungo vya mwili kua kwanini Vinashuhudia dhidi ya Mwili wa Mtu husika kama zilivyosema aya kua:

﴿ لِمَ شَهِدتُّمْ عَلَيْنَا ﴾

lima shahidtum AAalayn<u>a</u> *(Surat Fusilat 41:22)*

Tafsir: ***Hivi kwanini Mnatoa Ushahidi dhidi yetu?***

Na Midomo itasema hivyo kwa sababu ni yenye kujua kua kushuhudia huko kwa viungo hivyo ni kwenye kupelekea katika kuingia kwenye maangamizi ya adhabu kali ya moto wa Jahanam ambao hautouunguza Mdomo peke yake tu bali utavinguza viungo vyote vya mwili wa Ibn Adam Husika, Hivyo hatuna wajibu mwengine zaidi mimi nawe isipokua kabla ya kuwadia kwa siku hio basi tumuombe Allah atusamehe Madhambi yetu ya siri na ya dhahiri na pia atuepushe na adhabu ya Moto..Amiin

Kwani baada ya Midomo kusema hivyo basi Viungo hivyo vitajibu kwa kusema kama inavyomalizia aya hio kwa kusema kua;

﴿ وَيَوْمَ يُحْشَرُ أَعْدَآءُ ٱللَّهِ إِلَى ٱلنَّارِ فَهُمْ يُوزَعُونَ ۞حَتَّىٰٓ إِذَا مَا جَآءُوهَا شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَأَبْصَارُهُمْ وَجُلُودُهُم بِمَا كَانُواْ يَعْمَلُونَ ۞وَقَالُواْ لِجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدتُّمْ عَلَيْنَا قَالُوٓاْ أَنطَقَنَا ٱللَّهُ ٱلَّذِى أَنطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُوَ خَلَقَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ۞ وَمَا كُنتُمْ تَسْتَتِرُونَ أَن يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلاَ أَبْصَارُكُمْ وَلاَ جُلُودُكُمْ وَلَـٰكِن ظَنَنتُمْ أَنَّ ٱللَّهَ لاَ يَعْلَمُ كَثِيراً مِّمَّا تَعْمَلُونَ﴾

Wayawma yuhsharu aAAdao Allahi ila alnnari fahum yoozaAAoona. Hatta idha ma jaooha shahida AAalayhim samAAuhum waabsaruhum wajulooduhum bima kanoo yaAAmaloona. Waqaloo lijuloodihim lima shahidtum AAalayna qaloo antaqana Allahu allathee antaqa kulla shay-in wahuwa khalaqakum awwala marratin wa-ilayhi turjaAAoona, Wama kuntum tastatiroona an yashhada AAalaykum samAAukum wala absarukum wala juloodukum walakin *dh*anantum anna Allaha la yaAAlamu katheeran mimma taAAmaloona*(Surat Fusilat 41:19-23)**

Tafsir: ***Na Katika Siku Ambayo Maadui wa Allah Watakusanywa kwa ajili ya Moto Na Hivyo Watakusanyika (Na kuhojiwa kuanzia Waasi wa Tangu Mwazo wa Dunia hadi mwisho wa Dunia) Hadi Pale watakapoufikia (Moto Huo) Basi Watatolewa Watatolewa Ushahidi Na Kusikia kwao (Kwa Masikio) Na Kuona kwao (Kwa Mtizamo wa Macho) Na Kwa Ngozi zao Kutokana na Yale waliyokua wakiyafanya - Na Watasema Watu hao Kuziambia Ngozi za Miili yao Hivi Kwa Nini Mnatoa Ushahidi Dhidi yetu? (Ambapo) Zitasema (Ngozi hizo) Ametufanya Tuzungumze sisi Allah Kama vile ambavyo alivyovifanya Vitu vyote vizungumze Na Yeye ndie aliekuumbeni Mara Ya kwanza Na Kwake yeye Mmerudishwa Na Kamwe nyinyi hamkua ni wenye kuweza Kujificha (kutokana nasi) Ili Msishuhudiwe Na Masikio yenu Wala Macho yenu Na Wala na Ngozi zenu Bali Mlikua Mkidhani Kua kwa Hakika Allah Hajui Mengi sana Katika yale mliyokua Mkiyafanya***

Yaani katika siku hio basi viungo vyengine vya Mwili vitasutana na Mdomo na Ulimi, na kuhoji kwa kusema: **Hivi Wewe Mdomo na Ulimi wako mnatafakkari lakini au mnasema tu? Hivi kwanini mnatulaumu sisi kwa kusema wakati leo hii haiwezekani kwetu kupingana na Maamrisho ya Muumba, hivyo haishangazi kuona kua tunazungumza na kushuhudia dhidi ya Mwili huu kwa sababu yeye ndie alieuumba na ndie aliekiwezesha kila kitu kiwe ni chenye kusema kama unavyosema Wewe na Ulimi wako.'**

Na anasema Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* kua**: 'Siku Moja tulikua tumekaa *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na mara akaanza kucheka kimya kimya.'**

Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza Masahaba zake kwa kusema: **'Hivi Mnajua kwanini nimecheka?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakajibu: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake Salallahu Alayhi sa Salam ni wenye kujua Zaidi.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Mimi nnacheka kile ambacho Mja atakisema kumwambia Mola wake katika siku ya Malipo kwa kuuliza: Ewe Mola wangu, hivi wewe hukuniahidi mimi kua kamwe hutonidhulumu?'**

Na *Allah Subhanah aa Ta'ala* atajibu kwa kusema: '**Naam..kweli mimi nilikuahidi hivyo'**

Hivyo Ibn Adam atasema: '**Kama ni hivyo basi kwa hakika mimi sikubali kuletewa Shahidi isipokua shahidi huyo atokane na mimi mwenyewe.'**

Na hapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atasema: **'Bila ya shaka leo hii hakuna shahidi mwengine dhidi yenu isipokua Nafsi zenu kwani zitatoshelezea kutoa ushahidi dhidi yenu. Na Kiraman Katibin (Malaika wanaoandika kila Amali za Ibn Adam) wataosheleza kushuhudia dhidi yenu. Na kisha Midomo ya Ibn Adam itafungwa na viungo vitaambiwa Zungumza!'**

Na hapo viungo vyote vitaanza kutoa ushahidi kwa kuelezea kila kitu kikichofanywa ndani ya maisha ya mtu husika. Na baada ya Viungo kutoa Ushahidi juu ya kila kitu, basi mdomo utafumbuliwa. Ambapo nao utasema kuviambia viungo vyengine vya mwili kua: Hakika Nyinyi Viungo vya mwili leo hii mmeangamia, kwani mimi nilikua napapatua kwa ajili ya kukuokoeni nyinyi na Moto*(Mishakat Masabih)*

Ama baada ya Viungo vya mwili kulaumisa kwa kutoa Ushahidi dhidi ya Mwili basi Aya zinaendelea kutuambia kua Viungo hivyo vitauambia Mdomo na Ulimi kua:

﴿وَقَالُواْ لِجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدتُّمْ عَلَيْنَا قَالُوٓاْ أَنطَقَنَا ٱللَّهُ ٱلَّذِى أَنطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُوَ خَلَقَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ۞ وَمَا كُنتُمْ تَسْتَتِرُونَ أَن يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلاَ أَبْصَارُكُمْ وَلاَ جُلُودُكُمْ وَلَٰكِن ظَنَنتُمْ أَنَّ ٱللَّهَ لاَ يَعْلَمُ كَثِيراً مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴾

Waqaloo lijuloodihim lima shahidtum AAalayna qaloo antaqana Allahu allathee antaqa kulla shay-in wahuwa khalaqakum awwala marratin wa-ilayhi turjaAAoona, Wama kuntum tastatiroona an yashhada AAalaykum samAAukum wala absarukum wala juloodukum walakin *dh*anantum anna Allaha la yaAAlamu katheeran mimma taAAmaloona*(Surat Fusilat 41:21-23)*

Tafsir: ***Na Watasema Watu hao Kuziambia Ngozi za Miili yao Hivi Kwa Nini Mnatoa Ushahidi Dhidi yetu? (Ambapo) Zitasema (Ngozi hizo) Ametufanya Tuzungumze sisi Allah Kama vile ambavyo alivyovifanya Vitu vyote vizungumze Na Yeye ndie aliekuumbeni Mara Ya kwanza Na Kwake yeye Mmerudishwa Na Kamwe nyinyi hamkua ni wenye kuweza Kujificha (kutokana nasi) Ili Msishuhudiwe Na Masikio yenu Wala Macho yenu Na Wala na Ngozi zenu Bali Mlikua Mkidhani Kua kwa Hakika Allah Hajui Mengi sana Katika yale mliyokua Mkiyafanya***

Yaani Viungo hivyo vitakua vikithibitisha kua, kama vile *Allah Subhanah wa Ta'ala* alivyokua na Uwezo sa Kukuumbieni Roho zenu mara ya kwanza kabla ya kuziingiza kwenye Miili yenu baada ya kutoka kwenye sehemu za Siri za Wazee wenu kutoka katika hali ya tone la Manii na kuanza kua

pande la Damu na kisha kugeuka nyama na kisha kutiaa Mifupa ndani kwa ndani na mifupa hio kuoteshwa Nyama juu yake.

Na kisha mkawa watu ndani ya Matumbo ya Mama zenu mkazaliwa mkaishi na kisha mkafa na kufufuliwa upya mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* kamwe hatoshindwa kutufanya sisi viungo vya Miili yenu kua nk wenye kuzungumza leo hii katika siku ya Malipo kama vile alivyouwezesha Mdomo na Ulimi kuzungumza katika wakati wa Uhai sa kidunia.

Na ama kwa upande wa wasioamini basi hua si wenye kufikiria kua viungo vyao vitatoa ushahidi dhidi yao kaa kuzungumza katika siku ya Malipo.

Na hivyo hua hawakubali kua hali itakua hivyo yaani haiwezekani kujificha dhidi ya Madhambi hata kutokana na Viungo vyako na hivyo inawezekana haga kujificha dhidi ya *Allah Subhabah wa Ta'ala* na hivyo hii Hua ni Kukufuru kwani hua ni sawa na kumfananisha Muumba yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ni sawa na Viumbe wake na hivyo hajui kitu kuhusiana na Viumbe wake.

Ambapo anasema Imam Al Bukhari kua: **‘Siku moja Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu anhu* alikua amekaa nyuma ya Guo linalofunika Ukuta wa Al Kaabah Na mara wakatokea watu wa Quraysh wakiwa na mmoja kati ya watu wa Banu Thaqaf Watu hao walikua Wanene na Ufaham wao ulikua mdogo,na hakuweza kusikia vizuri wanachokizungumzia ila mara mmoja wao akawauliza wenzake kwa kusema : ‘Hivi mnafikiria nyinyi kua *Allah Subhanah wa Ta’ala* anasikia mnayoyasema?’**

Ambapo mmoja akajibu: ‘Anakusikia kama ukizungumza kwa sauti kubwa lakini kama kimya kimya hawezj kukusikia.’

Na kisha mmoja wapo miongoni mwao akasema: ‘Ah..Kama anaweza kusikia ukisema kwa sauti basi hata kimya kimya pia atakua anakusikia kila kitu’

Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya tukio hili na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha maneno ya Aya ya 23 ya Surat Fusilat ambayo ni yenye kusema:

﴿وَمَا كُنتُمْ تَسْتَتِرُونَ أَن يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلاَ أَبْصَارُكُمْ وَلاَ جُلُودُكُمْ وَلَكِن ظَنَنتُمْ أَنَّ ٱللَّهَ لاَ يَعْلَمُ كَثِيراً مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴾

Wam<u>a</u> kuntum tastatiroona an yashhada AAalaykum samAAukum wal<u>a</u> abs<u>a</u>rukum wal<u>a</u> juloodukum wal<u>a</u>kin *<u>dh</u>*anantum anna All<u>a</u>ha l<u>a</u> yaAAlamu katheeran mimm<u>a</u> taAAmaloona*(*Surat Fusilat 41: 23)*

Tafsir: ***Kamwe nyinyi hamkua ni wenye kuweza Kujificha (kutokana nasi) Ili Msishuhudiwe Na Masikio yenu Wala Macho yenu Na Wala na Ngozi zenu Bali Mlikua Mkidhani Kua kwa Hakika Allah Hajui Mengi sana Katika yale mliyokua Mkiyafanya.***

Naam..hivyo kila mwenye kudhania kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* haoni wala hasikii na hivyo akafanya kama anavyotaka kufanya basi atakua ni mwenye kula Hasara katika siku ya Malipo.

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye uwezo juu ya kila kitu na ni mwenye kujua juu ya kila kitu na hivyo ni mwenye kuweza kua kama anavyofikiriwa kua na mja husika kama alivyosema kwenye hadith al Quds kua: '**Hakika mimi niko kama anavyonifikiria nilivyo Mja wangu, kwani hua pamoja nae pale atakaponikumbuka, akinikumbuka peke yake nami uumkumbuka peke yangu na akinikumbuka kwenye kundi la watu basi nami nitamkumbuka kwenye kundi bora zaid**

Na akinikaribia kwa masafa ya Nyanda moja basi mimi humkaribia yeye kwa masafa ya Mkono mmoja, na akinikaribia mimi kwa masafa ya mkono mmoja, basi mimi humkaribia kwa masafa ya mikono miwili,na akinikaribia kwa mwenda wa kutembea basi mimi nitamfuata kwa mwendo wa kumkimbilia'(*Sahih Bukhari)*

Yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kututaka viumbe wake kua ni wenye Mtizamo mzuri juu yake yaani tumuamini kikamilifu. Kiasi ya kua kama unamuomba Basi uwe na yakini ya kumuamini yeye na pia ya wewe mwenyewe kujiamini kua anakusikia anakuona na atakujibu na kukutekelezea shida yako, au ukimuomba msamaha basi bila ya shaka atakusamehe, au ukifanya mema basi atakulipa kulingana na nia yako, n.k

Yaani tusivunjike Moyo na Rehma zake juu yetu kwani tukiwa tunaamini vyenginevyo kwa mfano kwa kufanya Mema huku tukiwa tunaamini kua hatoyakubali basi kamwe hatutonufaika na mema hayo kutokana na kuvunjika, Moyo na kutokana na rehma zake kwani yeye mwenyewe amesema kua:

﴿قُلْ يٰعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ أَسْرَفُواْ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ لاَ تَقْنَطُواْ مِن رَّحْمَةِ ٱللَّهِ إِنَّ ٱللَّهَ يَغْفِرُ ٱلذُّنُوبَ جَمِيعاً إِنَّهُ هُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ﴾

Qul ya AAibadiya alladheena asrafoo AAala anfusihim la taqnatoo min rahmati Allahi inna Allaha yaghfiru aldhdhunooba jameeAAan innahu huwa alghafooru alrraheemu*(Surat Az Zumar 39:53)*

Tafsir: ***Sema: Enyi Waja wangu Ambao Mmzifanyia Israfu Nafsi zenu Msivunjike Moyo na Rehma za Allah kwani kwa Hakika Allah (Subhanah wa Ta'ala) ni mwenye kusamehe Dhambi zote, kwa hakika yeye ni Mwingi wa kusmaehe na ni mwingi wa Huruma.***

Naam..hivyo basi Aya inatuwekea wazi kua hatutakiwi kua na dhana Mbaya pale tunapomfikiria *Allah Subhanah wa Ta'ala* hata kama ikiwa tumefanya makosa, basiturudi kwake na atatupokea Hivyo kuvunjika Moyo na rehma zake basi hua ni kua na Sifa ya Unafiq na kutomuamini na hivyo hali itakua kama zinavyosema aya;

﴿وَيُعَذِّبَ ٱلْمُنَافِقِينَ وَٱلْمُنَافِقَاتِ وَٱلْمُشْرِكِينَ وَٱلْمُشْرِكَاتِ ٱلظَّآنِّينَ بِٱللَّهِ ظَنَّ ٱلسَّوْءِ عَلَيْهِمْ دَآئِرَةُ ٱلسَّوْءِ وَغَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِمْ وَلَعَنَهُمْ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ وَسَآءَتْ مَصِيراً﴾

WayuAAadhdhiba almunafiqeena waalmunafiqati waalmushrikeena waalmushrikati al*dhdha*nneena biAllahi *th*anna alssaw-i AAalayhim da-iratu alssaw-i waghadiba Allahu AAalayhim walaAAanahum waaAAadda lahum jahannama wasaat maseeran*(*SuratAl Fat-h 48:6)*

Tafsir: **Na Atawaadhibu Wanafik wa Kiume na Wanafik wa kike Na Washirikina wa Kiume na Washirikina wa Kike Wanaomdhania *Allah Subahanh wa Ta'ala* Dhana Ovu Ni Juu yao Maovu ya Dhana hizo na Ghadhabu za Allah ni Juu yao Na Wanalaaniwa na Allah Na Anaahidi kwa ajili yao Moto wa Jahannam, ambao ni makazi mabaya sana kufikia**

Na ndio maana akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Asitokee Mmoja wenu akawa ni mwenye Kufariki huku akiwa ni mwenye kuvunjika Moyo juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*'***(Musnad Imam Ahmad)***

Na akasema kuhusiana na hadithi hii Al Hafidh Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammad Al Khattabi Al Busti Al Shafii kua: **'Inapendekezwa kwa Kila Muumini anaekaribia kufa kua ni mwenye Kufikiria Wema juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na pia katika wakati Mtu anapokua anaumwa, anapokua katika Mitihani na katika kila wakati**.'

Na amesema pia Imam Abu Yaala kua Amesema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Watu wawili watatolewa kutoka kwenye Moto wa Jahannam na kisha wataletwa mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* Na kisha itaamrishwa kua watu hao warudishwe tena kwenye Moto huo Ambapo Wakati watu hao watakapokua wanarudishwa basi mmoja wao atagoma na kugeuka nyuma huku akisema: **'Ewe Mola wangu, Hakika mimi sikua nikikufikiria hivi wewe, kwani mimi nilikua nakufikiria kua Umenitoa kwenye Moto na hutonirufisha tena kutokana na kua umenisamehe.'**

Allah Subhanah wa Ta'ala atamwambia Mtu huyo**: 'Basi hatutokurudisha tena ndani yake.'**

Kwani amesema pia Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Mubarak kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Baada ya kumalizika kutolewa hukumu *na Allah Subhanah wa Ta'ala* katika siku ya Malipo, basi watabakia wawili, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha kua watu hao waingizwe Motoni Na hivyo mmoja kati yao atasindikizwa huku akiwa anaangalia nyuma, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha kwa kusema: Hebu mrudisheni mbele yangu huyo anaeangalia nyuma.'**

Hivyo Mtu huyo atarudishwa mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo ataulizwa: **'Kwanini ulikua ukiangalia nyuma?'**

Mtu huyo atajibu kwa kusema: **'Ewe Mola wangu, hakika mimi nilikua nikidhania kua wewe Utaniingiza Peponi.'**

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha Mtu huyo aingizwe Peponi.

Na kisha Mtu huyo akishaingizwa Peponi basi atasema: Hizi ndio Fadhila za Mola wangu, humu nna uhakikakua hata kama nikiambiaa niwahudumie watu wote wa Peponi kwa Chakula.

Basi kufanya kwangu huko hakutonipunguzia mimi kitu chochote kutokana na nilivyokua navyo ndani ya Pepo hii.

Ambapo anasema yule alieinukuu hadithi hizi kua: Kila wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akizizungumzia Hadithi hizi basi Sura yake ilikua iking'ara kaa Nuru.

Ambapo anasema Al Muhakkik Al Faqih, Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii Al Makki kua: **Walionukuu hadith hizi katika Sanad ya Ahmad Ibn Hanbal wote ni thiqah na waaminifu, ijapokua kuna baadhi wana udhaifu kidogo.**

Na akasema Imam Hasan Al Basr kua: **'Kuna baadhi ya watu walikua ni wenye kua na Dhana nzuri juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala. Lakini* hata hivyo wakawa hawafanyi Mema, na wakaondoka Duniani huku wakiwa hawana Jema hata moja kwenye Amali zao.**

Na miongoni mwao alikua akisema kua : Hakika mimi nilikua ni mwenye kua na Dhana njema juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Lakini maneno yake hayo si ya kweli kwani kama angekua na Dhana nzuri juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi angekua ni mwenye kufanya mema.'

Hivyo kuna umuhimu sana wa Kua na Dhana Njema na kuzidisha kufanya Mema Kwani Kufanya Mema na kua na Mtizamo Mzuri juu *ya Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni kua na Msimamo juu ya Rehma, Huruma na Mapenzi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yetu ambae hua ni mwenye kufanya kila akifanyacho kutokana na Hikma zake.

Ambapo amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwenye Kitabu chake kitukufu kuhusiana na wale wenye Msimamo Thabit Juu yake kua:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَامُواْ تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ ٱلْمَلاَئِكَةُ أَلاَّ تَخَافُواْ وَلاَ تَحْزَنُواْ وَأَبْشِرُواْ بِٱلْجَنَّةِ ٱلَّتِى كُنتُمْ تُوعَدُونَ﴾

Inna alla<u>dh</u>eena q<u>a</u>loo rabbun<u>a</u> All<u>a</u>hu thumma istaq<u>a</u>moo tatanazzalu AAalayhimu almal<u>a</u>-ikatu all<u>a</u> takh<u>a</u>foo wal<u>a</u> ta<u>h</u>zanoo waabshiroo bialjannati allatee kuntum tooAAadoona. *(Surat Fusilat 41:30)*

Tafsir: **Hakika ya Wale Wasemao Mola wetu ni Allah Na Kisha Wakawa na Msimamo (Katika Imani ya Dini ya Kiislamu na Kutekeleza Majukumu yao Kidini) - Basi Watashukiwa juu yao Na Malaika (Ambao watakua wakiwaambia Waumini hao wenye Msimamo kua) Msiwe na Khofu wala Huzuni Bali Pokeeni Bashirio la Pepo Ambayo Mliahidiwa.**

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin, Imam Al Mushaqikkin Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Al Husayn Al Taymi Al Bakri Al Tabaristan Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kuhusiana na maneno ya aya hii kua: **Tukio hili linalozungumziwa kwenye Aya hii litatokea mara tatu:**

Kwanza litatokea katika Wakati wa Kifo

Pili litatokea pale Mtu huyo atakapoingizwa Kaburini

Tatu litatokea katika siku ya Kufufuliwa.

Ambapo anasema Imam Abd Rahmani Al Sudi na Imam Mujahhid Ibn Sulayman kua**: Ama kuhusiana na Khofu iliyozungumziwa hapa basi ni Khofu juu ya yale yatakayofuata Na kuhusiana na Huzuni basi ni Juu ya yale yaliyopita Na hii ni kwa sababu Hisia za Khofu na Huzuni ndio Hisia ambazo zinawachanya sana Ibn Adam, yaaani Khofu juu ya Yale yatakayofuata hapo baadae ambayo hatuyajui kua yatakuaje mazuri au mabaya.**

Na Huzuni hua ni kuhusiana matukio yaliyokwisha pita tayari na hivyo kua ni yenye kujaa Majuto ndani yake.'

Ambapo Hisia ya Khofu hua ndio hisia yenye Nguvu zaidi ya Hisia ya Huzuni kwani yaliyopita ndio yameshapita na tumeshayajua ila yanayokuja ndio balaa kwani hatuyajui yatakuaje na ndio maana tunahimizana kufanya mema zaid.

Na ndio maaana pia mara zote *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapozungumzia Hisia mbili hizi katika Qur'an basi huanza na Khofu kisha humalizia na Huzuni.

Naam..*Allah Subhanah wa Ta'ala anaendelea* kuelezea Hali itakavyokua katika Siku ya Malipo baada ya watu wote Kujikuta ndani ya Kiza cha Ghafla na kuamriwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua Waelekee Motoni,ambapo hali itakua kama zisemavyo aya:

﴿يَوْمَ تَرَى ٱلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَىٰ نُورُهُم بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِم بُشْرَاكُمُ ٱلْيَوْمَ جَنَّاتٌ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ذَٰلِكَ هُوَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ﴾

Yawma tara almu/mineena waalmu/minati yasAAa nooruhum bayna aydeehim wabi-aymanihim bushrakumu alyawma jannatun tajree min tahtiha al-anharu khalideena feeha dhalika huwa alfawzu *alAAatheemu (SuratAl Hadid 57:12)*

Tafsir: ***Siku hio Utaona Waumini wa Kiume na Waumini wa Kike Wakitanguliwa Mbele na Nuru zao Na Katika Upande wa Mikono yao ya Kulia (Wakiambiwa) Pokeeni Habari Njema Pepo Ni kwa Ajili Yenu leo hii Zenye Mito inayotirirka Maji Ndani yake Ingieni Mbakie Ndani yake Huko Ndio Kufuzu kuliko Bora zaidi.***

Aya zinazungumzia hali watakayokua nayo wale waliokua ni wenye Msimamo Imam katika Kumuamini Mola wao na hivyo kutokua na shaka juu yake kutokana na Yaqini waliyokua nayo juu ya Mola wao na yale aliyoyaahidi kwa kila Mwenye Kumtii kwa kufuata Maamrisho yake na kuachana na Makatazo yake, na wakawa ni wenye Kurudi kwa Mola wao kuomba Msamaha kila wanapomkosea. Na kutokana na kua ni wenye Kumuomba msamaha Mola wao kwani ni wenye kujua yeye ni Mwingi wa Usamehevu na mwenye Huruma na kumuomba msamaha mara kwa mara basi Watakua na wepesi katika Mizani ya Mizigo yao.

Na ndio maana baadhi ya Wanazuoni wakaielezea hii Nuru itakayoambatana nao Watu hao Mbele yao na katika Mikono ya Kulia kua ni kutokana na kua ni wenye Kupokea Vitabu vya amali zao kwa Mikono ya Kulia, Na hivyo Watu hao watakua ni wenye Nuru tofauti na wale wasiokua ni wenye Kuamini.

Na kutokana na Wasioamini na Wanafik kutokua na Nuru basi itakua vigumu kwao kuona Wanakoelekea Watu hao, na hawatokua na la kufanya ila Kuwafuata Nyuma watu hao wenye Nuru kutokana na Amali zao.

Lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataweka Ukuta baina ya Waumini na baina ya Makafiri na Wanafik. Kwani Mafikio yao wao ni tofauti yaani ni Motoni na wala si Peponi, hivyo wanatakiwa kutenganishwa. Na hivyo watu hao waliopo gizani watajikuta wamegonga Ukuta huku wakiwa nje ya Ukuta huo na wanatayarishiwa Adhabu kali sana na hivyo hali itakua kama zinavyosema aya kua:

﴿يَوْمَ يَقُولُ ٱلْمُنَافِقُونَ وَٱلْمُنَافِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُواْ ٱنظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِن نُّورِكُمْ قِيلَ ٱرْجِعُواْ وَرَآءَكُمْ فَٱلْتَمِسُواْ نُوراً فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَّهُ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ ٱلرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِن قِبَلِهِ ٱلْعَذَابُ﴾

Yawma yaqoolu almun<u>a</u>fiqoona waalmun<u>a</u>fiq<u>a</u>tu lilla<u>th</u>eena <u>a</u>manoo on<u>*dh*</u>uroon<u>a</u> naqtabis min noorikum qeela irjiAAoo war<u>a</u>akum failtamisoo nooran fa<u>d</u>uriba baynahum bisoorin lahu b<u>a</u>bun b<u>a</u>tinuhu feehi alrra<u>h</u>matu wa<u>*dh*</u>a<u>h</u>iruhu min qibalihi alAAa<u>dh</u>abu. *(Surat Al Hadid 57:13)*

Tafsir: ***Siku Hio Watasema Wanafiq wa Kiume na Wanafiq wa Kike Kuwaambia Wale Walioamini Tusubirini Ili Mtuazime Nuru zenu Wataambiwa Rudini Nyuma yenu mlikotoka Katafuteni Nuru zenu Na Hivyo Watawekewa Baina yao Ukuta wenye Mlango Ambapo Ndani yake Mtakua na Rahma Na Nje yake Itakua Adhabu.***

Na tunapomuangalia Imam Ad Dahhaq Ibn Muzahim basi yeye anasema kuhusiana na aya hii kua: **‘Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: Wakati watu watakapokua wamesimama kwenye Uwanja wa Kufufuliwa basi Ghafla moja kutakua na kiza kikubwa sana. Na kisha baada ya hapo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atajalia kutokea kwa Muale wa Nuru Na hivyo Waumini watakua ni wenye kuuona Muangaza wa Nuru hio, na kuanza kuusogelea Mwangaza huo ambao ndio utakua ni muongozo pekee wa kuwaongozea Watu kuelekea Peponi.**

Na wakati Waumini wanaelekea katika sehemu unapoangaza muangaza wa Nuru hio, basi na Wanafiq nao wataaanza kuona Nuru hio na hivyo nao watawafuata Waumini hao Lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Taala* ataufanya Muangaza huo utoweke mbele ya Wanafiq hao. Na baada ya kuona kua Mwangaza huo umetoweka basi Wanafiq hao ndio watasema kuwaambia Waumini kua: 'Tusubirini ili mtiazime Nuru yenu kwani kwa hakika sisi tulikua pamoja nanyi Duniani.'

Na hapo Waumini watawajibu Wanafiq hao kwa kusema: Kama ni hivyo basi Rudini Mlipokua na mtaiona Nuru yenu huko mlikotoka*(Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo kwa upande wa Abu Umammah *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kuhusiana na aya hii kua: **'Utafikia wakati katika Siku ya Malipo wakati watu wapo kwenye Uwanja wa Malipo kua kila kitu kua ni chenye kufunikwa na kiza kikubwa sana Kiasi ya kua Watu wote Walioamini na wasioamini hawataweza kuziona hata sehemu za upande wa ndani wa viganja vya mikono yao.**

Hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapoamua kutokea kwa Nuru kwa ajili ya kila Muumini wa mwanzo tangu kuumbwa kwa Dunia hafi mwisho wa Dunia kulingana na Amali zao kwa kila mmoja miongoni mwao.'

Kwani maana hio basi maneno ya Abu Umamah *Radhi Allahu Anhu* yanamaanisha kua Kila ukiwa na Amali njema nyingi zaid basi ndio unavyokua na Muangaza mkubwa zaidi wa Nuru hio na kujiongezea uwezo wa kujaaliaa kuingia Peponi, na kila ukiwa na amali kidogo basi ndivyo unavyoizidisha. Kufifia kwa Nuru hio na hivyo unazidi kujiongezea hatari ya kupotea njia na kutumbukia Motoni.

Ambapo amesema Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Miongoni mwa Waumini katika siku hio Watakua Wanamurikiwa na Nuru kama umbali wa Masafa ya kuanzia kutoka katika Mji wa Madina hadi Mji wa Aden Yemen na Zaidi. Na kuna baadhi ambao Nuru yao haitozidi zaidi ya ukubwa wa sehemu wanayoweka Nyayo zao***(Imam Ibn Jarir At Tabari)*

﴿يُنَادُونَهُمْ أَلَمْ نَكُن مَّعَكُمْ قَالُواْ بَلَىٰ وَلَٰكِنَّكُمْ فَتَنتُمْ أَنفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ وَٱرْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ ٱلْأَمَانِيُّ حَتَّىٰ جَآءَ أَمْرُ ٱللَّهِ وَغَرَّكُم بِٱللَّهِ ٱلْغَرُورُ﴾

Kwa upande wa *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin, Imam Al Mushaqikkin* Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Al Husayn Al Taymi Al Bakri Al Tabaristan Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii anasema kua: **'Ingawa Wingi wa Amali njema za Mtu utakua ni wenye athari juu ya wingi wa Nuru ya Mtu husika, lakini pia ukweli ni kua tunapoangalia Kwa makini basi tunaona kua Nuru ya Ilm basi ndio Nuru ya Uhakika katika kuona juu ya Uhakika wa Kitu, basi hii pia hua inamaanisha kua Wingi na Sifa ya Ubora wa Nuru ya Siku hio ya Malipo itakua ni sawia na Wingi na Ubora wa Nuru ya Ilm ambayo Mtu aliipata wakati alipokua akiishi hapa Duniani. Na kwa maana hio basi Waislam kuna umuhimu zaid wa Kutafuta Ilm ili tuwe ni wenye kujua namna ya kuboresha Amali zetu, kwani Amali njema bila ya Ilm hua ni Batil.'**

Ambapo kwa upande wa Sahaba Mwanazuoni Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kua: **'Maneno yasemayo kua Nuru zao zitawatangulia basi yanamaanisha kua Waumini watakua ni wenye kupewa Nuru kulingana na Amali njema zao na hivyo watakua ni wenye kupita kwenye Sirat kiasi ya kua baadhi yao watakua na wingi wa Nuru kama Mlima, Wengine Nuru yao itakua kama Mtende ukubwa wake, na watakaokua na Nuru kidogo kabisa basi itakua kama wale wenye Nuru kwenye Vidole gumba tu, Nuru ambayo inawaka na kuzimika.'**

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Hakika mimi nitakua ndie wa mwanzo kuruhusiwa kusjudu, katika siku ya Malipo na ndie wa Mwanzo kuruhusiwa kunyanyua Uso wangu. Na nitakaponyanyua Uso wangu basi nitaweza kuona mbele yangu, nyuma yangu, kulia kwangu na kushoto kwangu, na kuweza kuwajua Wafuasi wangu na kuaatofautisha na watu wa Ummah nyengine.'**

Masahaba wakauliza: 'Ya Rasul Allah Hivi Jee utawezaje kuwatofautisha watu wa Ummah wako na watu wa Ummah nyenginezo?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **Hakika mimi nitawajua watu wa Ummah wangu kutokana kua ni wenye kua na Alama zitokanazo na Udhu wao Kwani Alama hizo hawatokua nazo wstu wa Ummah nyenginezo, na nitawajua kutokana na kua watakua ni wenye kupewa Vitabu vyao kwa mikono yao ya Kulia,na nitawajua kutokana na Alama kwenye Mapaji ya Nyuso zao Na nitawajua kutokana na Nuru zao, zitakazokuA zinamurika mbele ya Miili ya**o.*(Mustadrak Al Hakim)*

Ambapo bila ya shaka Nuru inayozungumziwa hapa ni Nuru ya Imani ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo hua inatokea ndani ya Moyo wa Mja husika kama alivyosema Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi.

Na anasema *Jarrah Allah Sultan Al Balagha* Imam Abh Qasim Al Zamakhshari kuhusiana na Mlango huo kua: '**Mlango huo utakua ni Mmoja kati ya Milango ya kuingilia ndani ya Milango Saba ya Peponi, na hivyo kua ndio Mlango Mkuu wa kuingia katika upande wenye Pepo na hivyo Ukijumuishwa na Mlango huu basi Milango hio itakua ni Minane..W Allahu Aaalam.**

Ambapo kwa Upande wa Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi basi yeye anasema kua: **Kutokana na Ukweli wa kua Pepo itakua ndio sehemu ya Juu kabisa ya Vitu vitakavyokuwepo, na Moto utakua ndio sehemu ya chini kabisa ya Vitu vitakavyokuwepo, basi hapa tunaweza kuhitimisha kua kutokana na aya hii basi Ukubwa wa Masafa ya baina ya sehemu hizi mbili hautokua na ukaribu kama ilivyoelezewa hapa**

Kwani kama tulivyoona katika hii kua Watu walioko ndani ya Ukuta huo watakua ni wenye hali ya kuingia Peponi na watu watakaokuwepo nje yake watakua na hali ya kutauarishiwa Adhabu kali sana kutokana na kua ni wrenye kuingia Motoni basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kwa kutuambia kua

﴿يُنَادُونَهُمْ أَلَمْ نَكُن مَّعَكُمْ قَالُواْ بَلَىٰ وَلَٰكِنَّكُمْ فَتَنتُمْ أَنفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ وَٱرْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ ٱلْأَمَانِيُّ حَتَّىٰ جَآءَ أَمْرُ ٱللَّهِ وَغَرَّكُم بِٱللَّهِ ٱلْغَرُورُ﴾

Yunadoonahum alam nakun maAAakum qaloo bala walakinnakum fatantum anfusakum watarabbastum wairtabtum wagharratkumu al-amaniyyu hatta jaa amru Allahi wagharrakum biAllahi *algharooru* *(SuratAl Hadid 57:14)*

Tafsir: ***Watu hao (Watakaokua wanatayarishiwa Adhabu) watawanadia (Waumini walioko upande wa pili wa Ukuta huo kwa kusema) :Hivi Jee sisi Hatukua pamoja Nanyi? Waumini watajibu kwa kusema Ndio! Ila Sasa, Lakini Nyie mmezifitinisha Nafsi zenu Kwa kuzipa mitihani ya kuendekeza Matamanio ya kidunia Na Mlikua Mnashaka Na (Imani ya Dini ya Kiislam) Na Mmehadaika na Starehe zenye Utulivu wa Mpito Hadi Pale ilipowadia Amri ya Allah Na mwenye Hadaa zaid (Ibilisi) akakuhadaeni juu ya Allah.***

Naam..hivyo Wasioamini watawaomba Walioamini kua wawasaidie kwani wamegonga Ukuta kizani kwani bila ya Nuru yao walioamini basi hawawezi kuelekea katika upande wowote

Lakini sasa Waumini hao watawaambia Wasioamini kua, Hilo ni kosa lenu, kwani Mliendekeza Matamanio ya Nafsi zenu na Starehe za Kidunia ambazo ndizo zimekupelekeeni kua na hali mliyokua nayo leo hii Kutokana na Hadaa za Ibilisi

Ambapo anasema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alikaa,*** **kisha akachora umbo la pembe nne na kisha akachora mstari utokao katikati ya Umbo hilo hadi nje yake, na kisha kuanzia kwenye mstari huo akachora mistari myengine pembeni yake Kisha akasema: Huyu ndio Ibn Adam na haya ndio mambo yanayomzunguka kila upande. Huu mstari wa kati ndio Ibn Adam na Mistari myengineyo inayotokana nao ni miongoni mwa mambo ambayo anakabiliana nayo ambapo akifanikiwa kuyakwepa mengine basi hua yanampata na kukumbana nayo Na Mstari wa Nje hua ni Matumaini yake.**

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alichora Mstari nje ya Kiboksi na kusema Kua ndio Matumaini ya Ibn Adam, kumaanisha kua Usitumaini kufanya Toba kesho kwani hujui kama utakua nje yake au ndani yake hio kesho.'

Kwa kuendelea kufafanua zaidi basi na tuangalie neno Warada ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kuwepo katika Sehemu husika katika Mda Husika.Kuwasili katika sehemu husika,, kukaribia sehemu husika, Kuingia katika sehemu husika na pia humaanisha Kuwasili katika sehemu ya kunywea Maji.

Neno Warada ndio lililotoa neno Wardatun ambalo hua linamaanisha Ua la Wardi, Ua lenye Kuchanua, na pia humaanisha Kuficha. Na pia neno Warada limetoa neno Warid ambalo humaanisha Mshipa mkuu wa Damu.

Hivyo bila ya shaka nimefafanua maana ya neno Warada si kwa sababu ya kua nataka tuzungumzie kuhusiana na habari ya Maua ya Mawardi, au Udi wa Mawardi labda kimapenzi au Kimujarabati...La!

Bali nimeanza na neno hilo kwa sababu *Warada* ndio lililotumia katika aya ambayo ni yenye kuzungumzia kuhusiana na hali itakavyokua katika Siku ya Malipo. Kwani anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat Maryam kua:

﴿ وَإِن مِّنكُمْ إِلاَّ وَارِدُهَا كَانَ عَلَىٰ رَبِّكَ حَتْماً مَّقْضِيّاً ۞ ثُمَّ نُنَجِّي ٱلَّذِينَ ٱتَّقَواْ وَّنَذَرُ ٱلظَّالِمِينَ فِيهَا جِثِيّاً ﴾

Wa-in minkum illa wariduha kana AAala rabbika hatman maqdhiyyan, Thumma nunajjee alladheena ittaqaw wanatharu aldhdhalimeena feeha jithiyyan. *(Surat Maryam 19:71-72)*

Tafsir: ***Na Hakuna Miongoni mwenu Isipokua Atakuwepo na Kupita Juu yake (Moto) Kwani Hii ni Kutokna na Mola wako Ni Hatima Aliyoifanya kua Lazima Ifanyike Kisha Tutawaokoa wale Ambao ni Wenye Taqwa (Wenye Kumtii na Kumuogopa Mola wao) Na Tutawaacha Wale Waliofanya Maovu Ndani yake(Motoni) wakiwa wamepiga magoti.***

Naam...anasema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na aya hizi kua: Neno Warid maana yake hua ni Kuingia, na hivyo aya inamaanisha kua kila Mtu ataingia Motoni na kisha Waumini Watatolewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*

Ambapo huu ni mtizamo wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* pia.

Na hii ni kwa sababu pia amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kuhusiana na Masahaba wa Badr kua**: 'Nna matumaini kua wale Waliopigana Vita vya Badr na Waliokua kwenye Makubaliano ya Hudaybia kua hawatoguswa na Moto'**

Ambapo Ummu Ul Muuminin Hafsa Bint Umar *Radhi Allahu Anha akauliza* kwa kusema: **Ya Rasul Allah! Hivi jee hakusema *Allah Subbanah wa Taala* kua Hakuna hata mmoja Miongoni mwenu isipokua Atapita Juu yake?**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Soma aya inayofuatia baada ya hio inayoema :Kisha tutawaokoa wale wenye Taqwa**(*Sahih Muslim)*

Na tumeona kua Aya zimezungumzia kuhusiana na kutenganishwa baina ya Waumini na Wasiokua Waumini kwa kuwawekea Ukuta baina yao na kisha kutudhihirisha kua Wasiomini watakua moja kwa moja wanasubiri Adhabu yao ambayo itafuatia hapo hapo walipo na hii ni kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* hahitaji kuwahesabia Amali zao wale walimkufuru kwani walichokichuma kwao Duniani ndio chao na Akhera hawana lao isipokua Moto.

Ama kwa upande wa Walioamini na kisha Wakawa wako upande wa Pili wa Ukuta husika basi wao watakua katika hali ya kupitishwa kwenye Sirat au Daraja ambalo linapita Juu ya Moto wa Jahannam.

Na juu yake hua kuna vituo vyake ambavyo ndio kila mtu atakua akijibu yale atakayoulizwa juu yake kabla ya Kuangukia Motoni au kuelekea Moja kwa moja Peponi. Kwani amesema Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* kua: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na mpito wa juu ya Sirat kua: Watu wataanza kuvuka Juu ya Moto kupitia kwenye Sirat, ambapo kuna Waislam watakaovuka bila ya kuathirika wala kudhurika, na kuna baadhi watajeruhiwa na Moto huo Kuna watakaouepuka na kuna kuna utakaiwazuia Moto huo, na pia kuna Watakaoangukia na kukusanyika ndani yake**

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapomaliza kuwahesabia Watu amali zao, basi baadhi ya Waumini watagundua kua kuna baadhi ya Waislam waliokua miongoni mwao wakisali, wakitoa Zakah, wakifunga pamoja nao, wakienda katika Ibada ya Hija pamoja nao na kupigana Jihadi pamoja no Duniani kua hawako pamoja nao Hivyo Waumini hao watasema kumwambia *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

Ewe Mola wetu! Kuna baadhi ya Waja wako tuliokua nao Duniani walikua wakisali kama sisi, wakitoa Zaka kama sisi, wakifunga kama sisi, wakifanya ibada ya Hija kama sisi wakipigana Jihadi pamoja nasi, mbona hatuwaoni kua pamoja nasi hapa?

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha kwa kusema: Nendeni kwenye Moto na mkiwaona wamo ndani yake basi Watoeni Hivyo Watu hao watafuatawa kwenye Moto ambapo watakutikana kua kuna baadhi wameshaliwa na Moto kulingana na Madhambi yao

Kwani kuna baadhi watakua wameungua visigino vyote, kuna watakaoungua hadi kwenye ugoko wa miguu, kuna watakaoungua hadi magotini, kuna watakaoungua hadi kifuani na hadi shingoni, lakini moto hautofika Nyusoni mwao Hivyo Watu hao watatolewa kwenye Moto na kutumbukizwa kwenye Maji ya Uhai

Masahaba wakauliza: Maji ya Uhai ndio nini ya Rasul Allah?

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: Ni Maji yaliyotumiwa na Watu wa Peponi**

Na hivyo watu hao wataanza kua wazima kama namna unavyokua mmea kwenye maji yanayopita mafuriko Kisha Mitume wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* wataanza kuwaombea Watu wote waliokua na Ikhlasi katika kushuhudia kua hakuna Mungu anaestahiki kuabudiwa kwa haki ila *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na hivyo Watu hao watatolewa ndani ya Moto

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atapitisha Rehma zake kwa amtakae ili atoke ndani ya Moto huo, hivyo kila aliekua na chembe ya Imani ndani ya Moyo wake atatolewa ndani yake *(Imam Ibn Jarir At Tabari)*

Anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Muhammad Ibn Abh Bakr Al Ansari Al Qurtubi kua: **Khalid Ibn Madan amesema kua Watu wa Peponi watakapoingia Peponi basi watakua ni wenye kuulizana: Hivi Jee Mola wetu hakutuambia kua Kwa Hakika Kila Mtu Atauingia Moto?**

Ambapo nao watajibiwa kaa kuambiwa kua: Tayari Mmeshapita ndani yake lakini Moto huo Ulikua Jivu*(Imam Ibn Abi Shaybah)*

Na amesema Imam Al Hakim Al Tirmidhi kua: **Amesema Ibn Sumayyah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Katika Siku ya Malipo Kutakua na Mlango ambao hakuna mtu ambae hatouingia Moto iwe Mtu mwema ama muovu, Lakini Moto Huo utakua Baridi kwa Waumini kama vile ukivyokua kwa Ibrahim.'**

Ambapo kwa upande wa Al Muhakkik Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii Al Makki amesema kua: Walionukuu Hadithi hii ni watu wanaoaminika

Na huo pia ndio Mtizamo wa Al Hafidh Shams Ad Din Adh Dhahabi na Imam Ahmad Ibn Hanbal ambao wamesema kua Hii ni Hadith Sahih

Na Wanasema Wanazuoni pia kua: **'Katika Siku ya Malipo basi Watu watavuka kwenye Daraja la Sirat ambalo litakua lipo juu ya Moto wa Jahanam. Na kila atakaepita Juu yake basi atapita kulingana na wingi wa Amali njema zake, na wengi sana wataanguka Ndani yake Ambapo baadae watu hao walioanguka watajaaliwa kupata uombezi kutoka kwa Waumini, Mitume na Malaika pia Ambao watawaombea hadi waliofanya Dhambi kubwa, na hivyo watawatoa watu walioungua katika kila sehemu za Miili yao isipokua katika sehemu za Mapaji ya uso ambapo ni sehemu ya Kusujudia Na watawatoa watu waliokua na Imani hadi kufikia ukubwa duara la Dinari moja.**

Na kisha watawatoa watu wengine wenye Imani ndogo zaidi hadi kufikia wale wenye Imani ndooogo kabisa Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwenyewe kwa Rehma zake atawatoa hata wale ambao hawakushuhudia na hawakufanya hata jema. Na hivyo baada ya hapo basi ndani ya Moto huo watabakia wale ambao wanastahiki kubakia ndani yake Milele*(Imam Ibn Kathir)***

Hapa inabidi Waislam tukumbushane kua kila siku tunaposali hua ni wenye kuisoma Surat Al Fatiha zaid ya mara 17 kwa siku. Ambapo ndani yake mna Dua isemayo kua:

﴿ ٱهْدِنَا ٱلصِّرَاطَ ٱلْمُسْتَقِيمَ ﴾

Ihdina Al Ssirata Al Mustaqii*ma**(Surat Al Fatiha 1:6)*

Tafsir: **Tuongoze katika Njia Iliyonyooka.**

Na tunapoiangalia Dua ya aya hii basi tunaona kua ina maneno matatu tu Ambayo ni: *I*hdin*a Al Sirat Al Mustaqiima* mna maana ya neno Sirat tumeshaiangalia hapo Jana na tukasema kua ni Njia au Daraja. Ambayo ni Njia iliyonyooka, Njia Fupi au ya Mkato, Njia Inayoelekea Sehemu Maalum, Njia Pana na Yenye kuonesha wazi Mwisho wa njia hio.

Neno *Al Mustaqiima* liko wazi kwani tushawahi kulitafsiri mara kadhaa ila kwa kukumbushana tu basi maana yake ni Iliyonyooka.

Hivyo tumebakiwa na neno *Ihdina* ambalo Humaanisha Tuongoze, Tueleekeze au Tuoneshe njia. Na Ingawa neno *Ihdina* limetokana na neno Hada na pia na neno Hidayat ambayo yote humaanisha Kuongoza njia kwa Upole na Ukarimu.

Lakini neno *Huda* hua ni lenye umaalum wa kumaanisha Muongozo anaoupata Mtu ambao hu ani wenye kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na Neno *Hidayat* pia kwa upande mwengine hua linamaanisha Kuongozwa katika Njia ya Peponi Katika Siku ya Malipo.

Kwani tunapojumuisha maana ya neno Sirata na Maana ya Dua hii ya Surat Al Fatiha isemayo: *Ihdina Al Ssirata Al Mustaqiima.*

Basi hua tunamaanisha kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kutuongoza katika Njia ya Muongozo wake uliojaa Upole, Ukarimu hapa Duniani na pia atuongoze tuwe ni wenye kuingia Peponi Katika Siku ya Malipo kutokana na Kukubaliwa kwa amali zetu njema na kuridhiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuingizwa ndani ya Rehma zake.

Hivyo anasema Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Aliulizwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: ' Jee ni nini hio Sirat?'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* akajibu: Sirat Ni Daraja ambalo ni lenye Kuteleza na kua na miba pembeni yake, ambapo baadhi ya Waumini watapita kwenye Daraja hilo kwa kasi kubwa sana kama kufumba na kufumbua na wengine watapita kwa kasi ya Radi, wengine watapita kwa kasi ya Upepo au ya Farasi na wengine watakua salama na watadhurika kidogo lakini watakua salama baada ya kuchunika kwao na kuna wengne watakua Moytoni. Mtu wa Mwisho kuvuka atavuka Daraja kwa kuburuzwa**.(Imam Al Bukhari)

Na ndio maana wa Imam Ali Ibn Daqqaq ambae muda baada ya kufariki kwake basi Mwanafunzi wake alimuota akiwa anavuka Sirat ambayo ni pana hasa. Hivyo Mwanafunzi huyo akamuuliza Imam Ibn Daqqaq: **'Vipi mbona sisi tunajua kua Sirat Ni Nyembamba kam aUnywele na ina ncha ya Upanga?'**

Imam Ibn Daqqaq akajibu kwa kusema kua: **'Hamjakosea, Kwani hua inategemea na mpitaji, kama mtu alikua hana Imani katika Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Hua Nyembamba na kama alikua Makini na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua Pana.'**

Na kwa upande mwengine basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema katika Qur'an kua:

﴿ وَٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّالِحَاتِ لاَ نُكَلِّفُ نَفْساً إِلاَّ وُسْعَهَا أُوْلَئِكَ أَصْحَابُ ٱلْجَنَّةِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ۞وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِم مِّنْ غِلٍّ تَجْرِى مِن تَحْتِهِمُ ٱلأَنْهَارُ وَقَالُواْ ٱلْحَمْدُ للَّهِ ٱلَّذِى هَدَانَا لِهَـٰذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِىَ لَوْلاۤ أَنْ هَدَانَا ٱللَّهُ لَقَدْ جَآءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِٱلْحَقِّ وَنُودُوۤاْ أَن تِلْكُمُ ٱلْجَنَّةُ أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ۞وَنَادَىٰ أَصْحَابُ ٱلْجَنَّةِ أَصْحَابَ ٱلنَّارِ أَن قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقّاً فَهَلْ وَجَدتُّم مَّا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقّاً قَالُواْ نَعَمْ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌ بَيْنَهُمْ أَن لَّعْنَةُ ٱللَّهِ عَلَى ٱلظَّالِمِينَ۞ ٱلَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجاً وَهُمْ بِٱلآخِرَةِ كَافِرُونَ ۞ وَبَيْنَهُمَا حِجَابٌ وَعَلَى ٱلأَعْرَافِ رِجَالٌ يَعْرِفُونَ كُلاًّ بِسِيمَاهُمْ وَنَادَوْاْ أَصْحَابَ ٱلْجَنَّةِ أَن سَلاَمٌ عَلَيْكُمْ لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ ۞ وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَآءَ أَصْحَابِ ٱلنَّارِ قَالُواْ رَبَّنَا لاَ تَجْعَلْنَا مَعَ ٱلْقَوْمِ ٱلظَّالِمِينَ۞ وَنَادَىٰ أَصْحَابُ ٱلأَعْرَافِ رِجَالاٍ يَعْرِفُونَهُمْ بِسِيمَاهُمْ قَالُواْ مَآ أَغْنَىٰ عَنكُمْ جَمْعُكُمْ وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ ﴾

Waalladheena amanoo waAAamiloo alssalihati la nukallifu nafsan illa wusAAaha ola-ika as-habu aljannati hum feeha khalidoona; WanazaAAna ma fee sudoorihim min ghillin tajree min tahtihimu al-anharu waqaloo alhamdu lillahi alladhee hadana lihadha wama kunna linahtadiya lawla an hadana Allahu laqad jaat rusulu rabbina bialhaqqi wanoodoo an tilkumu aljannatu oorithtumooha bima kuntum taAAmaloona; Wanada as-habu aljannati as-haba alnnari an qad wajadna ma waAAadana rabbuna haqqan fahal wajadtum ma waAAada rabbukum haqqan qaloo naAAam faadhdhana mu-adhdhinun baynahum an laAAnatu Allahi AAala al*dhdha*limeena *(Surat Al Aaraf 7:42-43)*

Tafsir: ***Ama Kwa Wale walioamini Na Kisha Wafanya Mema Basi Hatuikalifishi Nafsi (kwa kuibebesha) zaidi ya Kile isichokiweza Hao Ndio Watu wa Peponi Ndani Yake Wataka Milele Tutawaondolea Yale Yaliyomo Ndani ya Vifua Vyao Kila Chuki na Vinyongo (Watakaa) Kwenye (Sehemu) zinazotiririka Maji ya Mito Chini yake Na Watasema Shukrani zote anastahiki Allah ambae ndie alietuongoza Katika Haya Kwani Tusingeongoka Kama Sio kutokana na kuongozwa na Allah Kwa Hakika Mitume wa Mola wetu walikuja Na Ujumbe wa Haki na Itanadiwa kwao (watu hao kwa kuambiwa) Hii ndio Pepo Ambayo Mmeirithi kutokana na yale Mliyokua Mkiyafanya.***

Naam..hizi ni aya za Surat Al Aaraf ambazo zinaelezea hali itakavyokua kwa wale Waumini watakaoingia Peponi. Kua hawatokua na hali ya Chuki wala Kinyongo ndani ya vifua vyao baina yao.

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Al Sudddi kua: '**Waumini watakapoingia Peponi basi watakutana na Mti ambao utakua upo pembeni ya Mlango wa Pepo Ambapo Mti huo utakua unatiririsha Maji ya chem chem za aina mbili pembeni yake na hivyo Watakunywa kutoka katika Chem chem moja ya kwanza ambayo itawashibisha na kuwasafisha pia vifua vyao na hivyo chuki na kinyongo vitaondoka ndani ya Vifua vyao. Na kisha wataingia kwenye Chem chem ya pili ambayo watakoga ndani yake na hivyo wakitoka ndani yake basi hawatokua wachafu tena.'**

Ama kwa Upande wa Imam Bukhari basi yeye ana hadith isemayo kua: '**Wakati Waumini watakapookoka kutokana na Moto wa Jahannam, basi watazuiwa kwenye Daraja la Sirat ambalo lipo baina ya Pepo na Moto Na kisha watamalizana hesabu zao kuhusiana na Chuki na Vinyongo vyao walivyokua navyo baina yao hapa Duniani, Na hivyo pale watakapomalizana na kua wasafi tu basi ndio wataruhusiwa kuingia Peponi.'**

Ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Jariri At Tabari kua: '**Amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Watu Wema watakapowasili kwenye Milango ya Peponi basi watakua Mti ambao pembeni yake kuna chem chem mbili zinazotiririka Maji Na hivyo wataingia na kukoga ndani ya Chemchem moja wapo na watajikuta kua ni wenye Kugubikwa na Baraka Ambapo baada ya hapo basi Nywele zao hazitosokotana tena, na wala Nyuso zao hazitoingia vumbi. Na kisha watakunywa kutoka katika Chem chem nyengineo ambayo itawasafisha kutokana na Uchafu uliomo ndani ya Miili yao. Na kisha Milango ya Pepo itafunguliwa kwa ajili yao na watakua ni wenye kuambiwa kua:**

﴿وَسِيقَ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوْاْ رَبَّهُمْ إِلَى ٱلْجَنَّةِ زُمَراً حَتَّىٰ إِذَا جَآءُوهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلاَمٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَٱدْخُلُوهَا خَالِدِينَ﴾

Waseeqa alladheena ittaqaw rabbahum ila aljannati zumaran hatta idha jaooha wafutihat abwabuha waqala lahum khazanatuha salamun AAalaykum tibtum faodkhulooha khalideena. *(Surat Az Zumar 39:73)*

*Tafsir***: Na wale ambao watakaotekeleza Majukumu yao kwa Mola wao, basi wataongozwa Peponi kwa makundi hadi waifikie, na Milango yake itafunguliwa kwa ajili yao na Walinzi wake watasema Salama iwe Juu yenu Mmefuzu! Hivyo Ingieni na Mkae ndani yake Milele**

Na jambo la kwanza litakua ni kupokelewa na kusalimiwa na Watoto Ambao watawazunguka kwa furaha kama vile ambavyo watoto wanavyowafurahikia wale waliorudi nyumbani baada ya safari ya mda mrefu Watoto hao watakimbilia kwa Hur Al Ayn wa Watu hao wa Peponi na kuwabashiria habari ya kuingia Peponi kwa watu hao, huku wakiwataja majina yao kikamilifu kuanzia kwao wao hadi kwa mababu zao Na Hur Al Ayn watawauliza watoto hao: 'Kweli? Hivi mmewaona kwa macho yenu?'

Na hivyo Hur Al Ayn hao watakua na Furaha kubwa sana na kukimbilia kwenye Milango yao Kwa ajili ya kuwasuburi na kuwapokea watu hao wa Peponi. Na watakapoingia ndani ya Majumba yao basi wataona kua yamejengwa kwa kila aina ya Mapambo ya Thamani, kuanzia Kwenye Lulu na Marjani na kila aina ya Madini na kila aina ya rangi

Kutakua na Masofa yaliyoshiba na kupanda juu, Vikombe vya vinywaji tofauti Mapazia na Mazulia mazuri yaliyotandazwa kila mahali. Watu hao watakumbatiana na Hur Al Ayn wao kwa furaha na kisha watakaa kwenye Masofa hayo na kupumzika kwa raha kabisa Na kisha baada ya hapo ndio watasema kama zilivyosema aya:

﴿وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِم مِّنْ غِلٍّ تَجْرِي مِن تَحْتِهِمُ ٱلْأَنْهَارُ وَقَالُواْ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِي هَدَانَا لِهَٰذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلآ أَنْ هَدَانَا ٱللَّهُ لَقَدْ جَآءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِٱلْحَقِّ وَنُودُوٓاْ أَن تِلْكُمُ ٱلْجَنَّةُ أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

WanazaAAna ma fee sudoorihim min ghillin tajree min tahtihimu al-anharu waqaloo alhamdu lillahi alladhee hadana lihadha wama kunna linahtadiya lawla an hadana Allahu laqad jaat rusulu rabbina bialhaqqi wanoodoo an tilkumu aljannatu oorithtumooha bima kuntum taAAmaloona *(Surat Al Aaraf 7:43)*

*Tafsir****: Tutawaondolea Yale Yaliyomo Ndani ya Vifua Vyao Kila Chuki na Vinyongo (Watakaa) Kwenye (Sehemu) zinazotiririka Maji ya Mito Chini yake Na Watasema Shukrani zote anastahiki Allah ambae ndie alietuongoza Katika Haya Kwani Tusingeongoka Kama Sio kutokana na kuongozwa na Allah Kwa Hakika Mitume wa Mola wetu walikuja Na Ujumbe wa Haki na Itanadiwa kwao (watu hao kwa kuambiwa) Hii ndio Pepo Ambayo Mmeirithi kutokana na yale Mliyokua Mkiyafanya.***

Kwani hapa tumetaja Hur Al Ayn ambao ni viumbe wazuri sana wa Peponi wa Kike na wa Kiume, hivyo Muumin wa Kiume atapata Mke Hur Al Ayn na Muumini wa Kike atapata Mume Hur Al Ayn Kwani anasema Imam Muslim kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Watu wa Peponi watakapoingia Pepoji basi Atanadia mwenye kunadaia kwa kusema kua: Kuweni**

ni wenye Afya njema, na kamwe msiwe ni wenye kuumwa. Kuweni ni wenye Kuishi na kamwe msiwe ni wenye Kufariki. Kuweni na Mamumbile ya Ujana na kamee msiwe wazee: Kuweni ndani ya Rehma za Mola wenu na kamwe msiwe ni wenye kuvunjika Moyo.'

Kwani tunazungumzia kuhusiana Habari za Peponi ambamo haiwezekani kuingia ndani yake bila ya kupata Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Kwani siku moja alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Hakuna hata mtu mmoja atakaeingia Peponi kutokana ba Amali njema zake'**

Hivyo Masahaba wakauliza: 'Hata wewe ya *Rasul Allah*?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: 'Naam..Hata mimi, hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakaponiingiza ndani ya Rehma zake'(Sahih Bukhari)*

Ambapo hapa inabidi tufahamiane kua kufanya kwetu mema na kudumu na ibada ipasavyo basi ndio njia pekee itakayompelekea mtu kuingizwa ndani ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika hadith nyengine kua: **'Hakuna Muislam atakaefariki isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* humuingiza Kafiri Motoni badala yake.'***(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Al Suddi kua**: 'Hakutokua na Mtu hata mmoja Motoni ambae hatokua ni mwenye kuoneshwa Sehemu yake Peponi ambayo angeipata kama angekua ni mwenye kufanya Mema, Na kisha sehemu yake hioitachukuliwa na kupewa Miongoni mwa Walioamini, na huu ndio Urithi uliozungumziwa katika aya pale iliposema**

﴿تِلْكُمُ ٱلْجَنَّةُ أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

Tilkumu aljannatu oorithtumooha bima kuntum taAAmaloona *(Surat Al Aaraf 7:43)*

*Tafsir**: Hii ndio Pepo Ambayo Mmeirithi kutokana na yale Mliyokua Mkiyafanya.***

Naam..kisha aya zinaendelea kusema kua:

﴿وَنَادَىٰٓ أَصْحَابُ ٱلْجَنَّةِ أَصْحَابَ ٱلنَّارِ أَن قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدتُّم مَّا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا قَالُوا۟ نَعَمْ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌۢ بَيْنَهُمْ أَن لَّعْنَةُ ٱللَّهِ عَلَى ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

Wanada as-haabu aljannati as-haba alnnari an qad wajadna ma waAAadana rabbuna haqqan fahal wajadtum ma waAAada rabbukum haqqan qaloo naAAam faadhdhana mu-adhdhinun baynahum an laAAnatu Allahi AAala al*dhdha*limeena(*Surat (Al Araf 7:44))*

*Tafsir: Na **Watanadia Watu wa Peponi Kwa watu wa Motoni Hakika Sisi Tumekuta Yale aliyotuahidi Mola wetu njia ya kweli na ya Uhakika Hivyo Jee Mmekuta nyinyi Yale Mliyoahidiwa na Mola wenu kua ya Kweli na Uhakika? Watasema (Watu wa Motoni kuwajibu Watu wa Peponi) ndio kisha Ataatangazia mwenye Kutangazia baina yao Laana za Allah - Ziko Juu ya Waliofanya Dhulma(Makafiri).***

Kwa upande mwengine tunapoangalia historia basi tunaona kua baada ya Vita vya Badr, Waislam. Waliwachukua Maiti wa Makafiri wa Makkah na kisha wakachimba shimo na wakawatia ndani yake shimo hilo kwa ajili ya kuwafukia. Ambapo baada ya Kuwatumbukiza Maiti hao basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanadia kwa kuwataja kwa majina Maiti watatu wa Makafiri hao kama inavyoelezewa hadith ifuatayo:

أَنَّ رَسولَ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ، تَرَكَ قَتْلَى بَدْرٍ ثَلَاثًا، ثُمَّ أَتَاهُمْ فَقَامَ عليهم فَنَادَاهُمْ، فَقالَ: يا أَبَا جَهْلِ بنَ هِشَامٍ يا أُمَيَّةَ بنَ خَلَفٍ يا عُتْبَةَ بنَ رَبِيعَةَ يا شيبَةَ بنَ رَبِيعَةَ أَليسَ قدْ وَجَدْتُمْ ما وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا؟ فإنِّي قدْ وَجَدْتُ ما وَعَدَنِي رَبِّي حَقًّا فَسَمِعَ عُمَرُ قَوْلَ النبيِّ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ، فَقالَ: يا رَسولَ اللهِ، كيفَ يَسْمَعُوا وَأنَّى يُجِيبُوا وَقَدْ جَيَّفُوا؟ قالَ: وَالَّذِي نَفْسِي بيَدِهِ ما أَنْتُمْ بأَسْمَعَ لِما أَقُولُ منهمْ، وَلَكِنَّهُمْ لا يَقْدِرُونَ أَنْ يُجِيبُوا ثُمَّ أَمَرَ بهِمْ فَسُحِبُوا، فَأُلْقُوا في قَلِيبِ بَدْرٍ

‘Ya Abi Jahal Ibn Hisham, Ya Ummayah Ibn Khalf, Ya Utba Ibn Rabiah na Ya Shaybah Ibn Rabiah! Jee Mmekuta Nyinyi? Yale Mliyoahidiwa na Mola wenu kua ya Kweli na Uhakika? Kwani Kwa Hakika Mimi Nimekuta Yale aliyojiahidi Mola wangu kua Ni ya Kweli

Ambapo Umar Ibn Ak Khattab *Radhi Allahu Anhu* alipoyasikia Maneno hayo ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kwa Maiti hao basi akamuuliza Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kaa kusema:

Ya Rasul Allah! Hivi Jee watakusikiaje na Watakujibu vipi Watu hawa wakati tayari wameshakua Maiti?

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu kaa kusema: Wa Allahi nnaapa mimi kwa yule ambae Uhai wangu umo ndani ya Mikono yake kua, Watu hawa wanasikia vizuri zaidi ya mnavyosikia nyinyi yale nnayowaambia, ila sasa hawawezi kunijibu*(Imam Al Bukhari)*

Ambapo kwa upande wa Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi basi anasema kuhusiana na maneno haya kua: **‘*Allah Subhanah wa Ta'ala* aliwajaalia Watu hawa kua ni wenye kuyasikia maneno hayo na Wenye kua na hali ya kujuta sana.’**

Kwani watu hawa walikua ni maadui wakubwa sana wa Uislam na Daima Majuto hua ni Mjukuu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema kua:

﴿ ٱلَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجاً وَهُمْ بِٱلآخِرَةِ كَافِرُونَ ﴾

Alla<u>dh</u>eena ya<u>s</u>uddoona AAan sabeeli All<u>a</u>hi wayabghoonah<u>a</u> AAiwajan wahum bial-<u>a</u>khirati k<u>a</u>firoona*(Surat Al Araf 7:45)*

Tafsir: ***Hao ndio wale Wanaozuia Njia ya Kumuelekea Allah Na Wakafanya Kuipindisha Na Hivyo pia Kua ni Makafiri Akhera.***

Naam..hizi ni aya za Surat Al Aaraf ambapo neno A'arafa hua linamaanisha Kujua, Kufaham, Kua na Habari juu ya Mtu jambo au kitu fulani.

Na mara nyingi watu hua wanatafsiri neno hili pale unapowadia mwezi 9 Dhul Al Hija unapotokezea mzozo wa Funga ya Arafah na kuanza kuulizana kama Aarafah hua ni Sehemu, Kisimamo au Siku, ambapo huu ni mzozo usiokwisha kwa wajinga na wasiojua na hivyo kutaka kuwapotosha wasiojua zaidi. Na bila ya shaka kama tulivyoona katika aya yetu ya 45 ya Surat Al Aaraf ambayo imesema:

﴿ ٱلَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجاً وَهُمْ بِٱلآخِرَةِ كَافِرُونَ ﴾

Alladheena yasuddoona AAan sabeeli Allahi wayabghoonaha AAiwajan wahum bial-akhirati kafiroona*(Surat Al Araf 7:45)*

Tafsir: ***Hao ndio wale Wanaozuia Njia ya Kumuelekea Allah Na Wakafanya Kuipindisha Na Hivyo pia Kua ni Makafiri Akhera.***

Kwani Funga ya Arafa inakua katika mwezi 9 wa Dhul Hijja kulingana na sehemu aliyokuwepo Muislam iwe Tanzania, Zanzibar, Misri, Saudi Arabia, India, Newzealand, Mexico, Canada, Chile nk (*Na katika Skuli ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni bora zaid [Awla; lakini si Sunna Mu'akkada] pia kufunga katika siku ya mwezi 8 kama funga ya Arafa, ili kua na hadhari zaid [Ahwat], katika hali ambayo huenda Arafa itatokea mwanzo kuliko muandamo wa sehemu uliyokuwepo [Fath al-Mu'in: I'anat, 2:265]*), hivyo bila ya kujali jina lake basi funga ya Arafah hu ani mwezi 9 Dhu Al Hijjah, popote pale utakapo kuwepo, hata kama ikiwa ni siku tofauti na siku halisi ya Arafa ya Mahujaji, tusema siku moja baadae.'

Hivyo haina haja ya watu kupotoshana kwani kama mtu hajui basi bora akae kimya au awaulize wenye kujua kama alivyoamrishwa kua:

﴿.. فَٱسْأَلُواْ أَهْلَ ٱلذِّكْرِ إِن كُنْتُم لاَ تَعْلَمُونَ﴾

Fais-aloo ahla aldhdhikri in kuntum la taAAlamoona. (*Surat An Nahl 16:43*).

*Tafsir: '**Ulizeni wenye kujua ikiwa nyinyi hamjui**'.*

Katika kuielezea aya hii, basi Al Khatib Al Baghdad anamalizia kwa kusema kua : '**Amr Ibn Qays, alisema kua *Ahl ul Dhikr* katika aya hii inamaanisha watu wenye *I'lm* yaani, Ulamaa'.**

Vile vile anasema Imam Al Suyuti kuhusiana na aya hii kua, '**Ayah hii inawahimiza wale wasiokua na ufahamu wa *I'lm* ya dini kufanya *Taqlid* kwa *Mujtahid*. Kwani ukiiangali aya hiyo utaona kua imetumia neno *Ahl Dhikr* ambalo maana yake ni watu wenye *I'lm*, na Maimamu wa *Madhhab* ni miongoni mwa *Ahlu Dhikr***'

Na tunaporudi kwenye maana ya neno *Aarafa* basi tunaona kua hua linatofautiana kimaana na neno *Alima.*

Kwa sababu neno *Aarafa* hua linatumika kuelezea juu ya kujua kitu fulani maalum. Na neno *Alima* hua linatumika kuelezea kujua vitu kwa Ujumla. Na hivyo neno *A'arafa* kinyume chake hua *Ankara*

yaani Kukana juu ya Kitu Fulani. Na neno *Alima* kinyume chake hua ni Jahila yaani kua Na hali ya Ujinga wa mambo au vitu.

Neno *Aarafa* ndio lilitoa neno Urfun ambalo humaanisha Nufaa, Julikana, Adilifu.

Neno *A'arafa* ndio lililotoa neno *Al Aaraf* ambalo ndio neno lilitomika kua kama Jina la Sura ambayo baadhi ya aya zake ndio tunazitafsiri kutokana na kua zenye kuzungumzia kuhusiana na mada yetu inayozungumzia juu ya Hali itakavyokua katika Siku ya Malipo baada ya kufufuliwa.

Ambapo jina la Sura hii ya Al Aaraf hua linamaanisha Sehemu Iliyopo Juu kabisa ya Kitu, sehemu ya Juu kidarja na kiheshima, Sehemu ya upekee kiubora, Sehemu inayotofautiana na nyengine kiubora baina sehemu mbili.

Na ndio maana Ufahamu wa Akili ya Ibn Adam ukawa unaitwa Maarifah kutokana na kua ndio sehemu yenye ubora wa hali ya juu kabisa ya Ufahamu kimaumbile.

Na bila ya shaka tunapozungumzia kuhusiana na Maarifah basi kuna Ufahamu wa aina mbili, Kuna Ufahamu wa Akili ya Moyo na kuna Ufahamu wa Akili ya Ubongo.

Ingawa kuna baadhi watasema kua wanaume hua wana ufahamu wa aina ya tatu baina ya miguu yake ambao ukianza kufanya kazi na kuchachamaa basi ufahamu mwengine wake wote hua haufanyi kazi...hio ni habari nyengine na sitaki kubishana na wengine kwa hivyo tunaachana nayo.

Lakini ukweli ni kua Maarifah ya Ufaham wa Ibn Adam wote hua ni katika Moyo na Ubongo. Na bila ya shaka Maarifah ya Ufahamu wa Moyo ndio maarifah yenye nguvu kabisa kwani Maarifah ya Moyo ndio yanayodhibiti Viungo vyote vya mwili wa Ibn Adam ikiwemo Marifah ya Ufahamu wa Ubongo.

Kiasi ya kua kama mtu atakua na Matatizo ya Moyo kisha akapandikizwa Moyo wa mtu mwengine basi Tabia za Mtu huyo aliepandikizwa zote hubadilika na kua na Tabia za mtu alitolewa Moyo wake.

Yaani kama Aliefariki akatolewa Moyo alikua Muislam na kisha Moyo huo ukapandikizwa kwa mwengine alie hai ambae ni Mkristo, basi aliepandikizwa Moyo atasilimu.

Na kama alitolewa Moyo alikua anampenda fulani aliekua anaishi Marekani labda basi na aliepandikizwa Moyo atampenda mtu huyo na hata kumuota hata kama akiwa hajawahi kuonana nae mtu huyo kutokana na kua yeye anaishi Afrika labda.n.k

Kwani kila wakati pale inapokua aya zinazungumzia kuhusiana na Ufahamu wa Akili basi hua zinazungumzia Maarifah ya Ufahamu wa Moyo na ndio maana aya zikizungumzia kuhusiana na kutafakkari na kuhoji juu ya kua na Ufaham au kutumia akili basi hua hazinasibishi neno Ufaham na Kichwa bali hua zinanasibisha na Kifua na Moyo, kwa mfano:

﴿وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيراً مِّنَ ٱلْجِنِّ وَٱلإِنْسِ لَهُمْ قُلُوبٌ لاَّ يَفْقَهُونَ بِهَا وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لاَّ يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ آذَانٌ لاَّ يَسْمَعُونَ بِهَآ أُوْلَئِكَ كَٱلأَنْعَامِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ أُوْلَئِكَ هُمُ ٱلْغَافِلُونَ﴾

Walaqad dhara/na lijahannama katheeran mina aljinni waal-insi lahum quloobun la yafqahoona biha walahum aAAyunun la yubsiroona biha walahum adhanun la yasmaAAoona biha ola-ika kaal-anAAami bal hum adallu ola-ika humu alghafiloona(*Surat Al Aaraf 7:179)***

Tafsir: ***na kwa Hakika tumewaumbe kwa ajili ya Moto wengi sana miongoni mwa Majini na Ibn Adam, kwani wana Nyoyo lakini hawafamu (Ukweli halisi kuhusiana na Allah Subhanah wa Ta'ala) kutokana nazo, wana macho lakini hawaoni Ukweli halisi kuhusiana na Allah Subhanah wa Ta'ala) kutokana nayo, na wana Masikio lakini hawasikii Ukweli halisi kuhusiana na Allah Subhanah wa Ta'ala). Wako kama Ngo'mbe, na zaidi kwa upotovu kwani hao ndio waliokumbwa na mghafiliko (kuhusiana na Allah Subhanah wa Ta'ala)***

Ambapo neno Aarafa ndio lililotoa neno *Maaruf* ambalo humaaanisha Wema, Uzuri, Manufaa, Yanayofaa, Haki, Uadilifu na pia Tabia za Jamii ya watu husika, na neno Maaruf hua ni kinyume cha neno *Munkar.*

Na hivyo neno Maarifah pia hua linamaanisha Ufahamu wa kuweza kutofautisha Jema na Ovu na mara nyingi hua linatumika kuainisha watu waliokua juu kitabia kidarja na kiufahamu kama Mitume.

Naam..baada ya kuona maana ya neni Al Aaraf basi moja kwa moja tunaingia kwenye Aya ya 46 ya Surat Al Aaraf ambayo ndio iliyobeba Neno hilo na hivyo kua ndio Aya iliyotoa jina la Sura hii pale ilipoendelea kuelezea kuhusiana na hali itakavyokua katika siku ya Malipo kwa kusema kua:

﴿وَبَيْنَهُمَا حِجَابٌ وَعَلَى ٱلْأَعْرَافِ رِجَالٌ يَعْرِفُونَ كُلاًّ بِسِيمَاهُمْ وَنَادَوْاْ أَصْحَابَ ٱلْجَنَّةِ أَن سَلاَمٌ عَلَيْكُمْ لَمْ يَدْخُلُوهَا وَهُمْ يَطْمَعُونَ﴾

Wabaynahuma hijabun waAAala al-aAArafi rijalun yaAArifoona kullan biseemahum wanadaw as-haba aljannati an salamun AAalaykum lam yadkhulooha wahum yatmaAAoona *(Surat Al Aaraf 7:46)*

Tafsir: ***Na Baina Yao (Watu wa Peponi ni watu wa Motoni) (Kutakua na) Pazia, Kizuizi Na Juu ya Al Aaraf(Darja ya Juu) (Kutakua kuna) Watu (Ambao Mema yao na Maovu yao yatakua sawia kiuzito) Ambao Watakaojuana baada ya kuonana watu wote (Wa Peponi na wa Motoni) Kutokana na Alama zao Na Hivyo Watawanadia Watu wa Peponi Kwa Kusema Salaam Alaykum Ambapo Katika Wakati huo watakua hata hawajaiingia Pepo Lakini wakiwa na Matumaini ya Uhakika wa Kuingia ndani yake.***

Na anasema Imam Mujahid Ibn Sulayman kua: '**Neno Hijab lililotumika hapa kwenye aya hii linamaanisha Kua kutakua na Ukuta utakaotenganisha baina ya Pepo na Moto.'**

Ambapo kwa upande wa Bahr Al Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kuhusiana na neno Al Aaraf kua: '**Al Aaraf ni Jengo au Kitu chochote kile ambacho Kimepanda Juu au kimenyanyuka Juu zaid: Na ndio Maana Hata Upanga wa Jogoo hua unaitwa Urf kwa sababu Umesimama na kua juu ya Kichwa cha Jogoo, na hivyo hapa aya inamaanisha kua kutakua na Ukuta mrefu kwenda Juu zaidi na Mpana zaidi utakaokua baina ya Pepo na Moto.'**

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Al Din Shaykh Ul Islami Mujtahid Imam Abu Fadhl Abd Rahman Ibn Abu Bakr Ibn Muhammad Jalal Ad Din Al Suyuti basi yeye anasema kua: **'Al Aaraf iliyozungumziwa hapa basi inamaanisha kua ni sehemu ya Mwishoni mwa Al Sirat'**

Na tunaporudi tena kwa *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anaendelea kuifafanua aya hii kwa kusema kua: **'Katika eneo hili kutakua na watu wenye Uzito sawia wa amali njema na amali mbovu Na hivyo watakua ni wenye jua na sifa ya kuingia Motoni na pia kuingia Peponi,na hivyo watakua hawajua wataingizwa wapi na watakaa kwenye Al Aaraf kwa mda mrefu lakini mwishowe wataingizwa Peponi kwa Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Na huu ni mtizamo pia wa Hudhayfah Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu*, Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi, Imam Ad Dahhaq Ibn Muzahim n.k

Na hivyo Watu hao watakua wanawaona Watu wa Peponi na wa Motoni kutokana na Alama za Nyusoni mwao.

Kwani watu wa Peponi watakua wanang'ara nyuso zao na watu wa Motoni watakua na Nyuzo zilizojaa kiza na macho ya rangi ya buluu.

Na ingawa Watu hawa wa Al Aaraf watakua hawajaingia Peponi, kutokana na uzito wa Dhambi zao na hawajaingizwa Peponi kutokana na wepesi wa Thawabu kutozizidi dhambi zao lakini watakua ni wenye Matumaini makubwa kua wataingia Peponi kutokana na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Naam..hivyo watu watakaokua kwenye Al Aaraf watawaamkia watu wa Peponi baada ya kuwaona kwa kuwaambia *As Salaam Alaykum!*

Ambapo watakua wakiwasalimia na kuyasema haya huku wakiwa na hamu kubwa sana inayoonesha kutaka kua pamoja nao watu hao kutokana na kua na utulivu na usalama na kuepukana na Moto.

Na baada ya kuwasalimia watu hao mtizamo wa macho ya Watu hao wa Al Aaraf utaangukia kwa watu wa Motoni na hali itakua kama zinavyosema aya kua:

﴿ وَإِذَا صُرِفَتْ أَبْصَارُهُمْ تِلْقَآءَ أَصْحَابِ ٱلنَّارِ قَالُواْ رَبَّنَا لاَ تَجْعَلْنَا مَعَ ٱلْقَوْمِ ٱلظَّالِمِينَ﴾

Wa-idha surifat absaruhum tilqaa as-habi alnnari qaloo rabbana la tajAAalna maAAa alqawmi al*dhdha*limeena*(Surat Al Araf 7:47)*

Tafsir: ***Na Kisha Watakapogeuzia Mtizamo Wa Macho yao Watawaona hao hapo watu wa Motoni Watasema (Watu wa Al Aaraf) Ewe Mola wetu Usitujaalie kua Pamoja na Watu Waliofanya Dhulma***

Allahuma Amiin

Yaani Watu wa Al Aaraf watawaona watu wa Motoni na Viongozi wao wa Ukafiri, ambapo miongoni mwao wakiwemo wale ambao walikua wakiwadharau na kuwanyanyasa Waumini na kutumia kila njia ili Watu wasiufuate Uislam.

Na hivyo watamuomba *Allah Subhabah wa Ta'ala* asiwajaalie nao kua miongoni mwao, kwani hawajijui katika hali waliyokua nayo watakua ni wenye kuelekea wapi ingawa ni wenye kua na matumaini ya kua wataingia Peponi kutokana na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo katika kuomba kwao huko kutakua ni sehemu ya kuomba kupata Rehma hizo za *Allah Subhabah wa Ta'ala* ambazo wanazihitaji sana katika wakati huo.

Kwani baada ya kuomba kuepushwa nao watu hao wa Motoni basi Watu hao wa Al Aaraf watawanadia Watu hao wa Motoni kwa kusema kama anavyoelezea *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ وَنَادَىٰٓ أَصۡحَٰبُ ٱلۡأَعۡرَافِ رِجَالٗا يَعۡرِفُونَهُم بِسِيمَاهُمۡ قَالُواْ مَآ أَغۡنَىٰ عَنكُمۡ جَمۡعُكُمۡ وَمَا كُنتُمۡ تَسۡتَكۡبِرُونَ ﴾

Wanada as-habu al-aAArafi rijalan yaAArifoonahum biseemahum qaloo ma aghna AAankum jamAAukum wama kuntum tastakbiroona. *(Surat Al Aaraf 7:48)*

Tafsir: ***Na Watanadia watu wa Al Aaraf Kwa Watu wanaowajua (Katika watu hao wa Motoni) Kutokana na Alama zao Kuwaambia Jee umekunufaisheni nini nyinyi Wingi wa Idadi yenu na Mjumuiko wa Mali zenu? Na Kua na Kibri kwenu?***

Hapa tunaona kua aya imetumia neno Jam/aakum ambalo nimelitafsiri kama wingi wa kiidadi ya watu na pia kimali na hii ni kwa sababu neno Jam hua pia linamaanisha wingi wa Mali na Utajiri.

Na kwa kua Kawaida tangu wakati wa kipindi cha Mitume wote hadi hii leo Wasioamini kua ni wengi zaidi ya wenye kuamini basi Mjumuiko wao ni mkubwa zaidi kiidadi na kimali pia na kumaanisha wingi wa hali zote hizo kitafsiri pia.

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuambia katika aya ya 49 ya Surat Al Aaraf kua:

﴿ أَهَٰٓؤُلَآءِ ٱلَّذِينَ أَقۡسَمۡتُمۡ لَا يَنَالُهُمُ ٱللَّهُ بِرَحۡمَةٍۚ ٱدۡخُلُواْ ٱلۡجَنَّةَ لَا خَوۡفٌ عَلَيۡكُمۡ وَلَآ أَنتُمۡ تَحۡزَنُونَ ﴾

Ahaola-i allatheena aqsamtum la yanaluhumu Allahu birahmatin odkhuloo aljannata la khawfun AAalaykum wala antum tahzanoona (*Surat Al Aaraf 7:49)*

Tafsir: ***Hivi Jee Hawa (Wayu wa Al Aaraf) ndio Wale ambao Mliokua Mkiapa Kua Hawatoingizwa na Allah Ndani ya Rehma zake? Hivyo Ingieni Peponi Wala hamtokua na Khofu juu yenu Na Wala Hamtokua na Huzuni***

Naam..anasema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na aya hii kua: ‘***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **atawaambia Wale watu waliokua na Kibri hapa Duniani na kuukataa ukweli ambao katika wakati huo watakua ndani ya Moto na hivyo wataulizwa kuhusiana na Watu wa Al Aaraf kua: Hivi Jee hawa si ndio wale ambao Nyinyi Mlikua mkiapa kuhusiana nao kua hawatopata Rehma za Mola wao?**

Na kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawaambia Watu hao wa Al Aaraf kua: Ingieni Peponi na wala hamtokua na Khofu wala Huzuni ndani yake.’

Ambapo hii Inaonesha kua wale Waumini wanaoonekana kua hawana kazi pale wanapokua wanamuabudu Mola wao hapa Duniani na Kumtii na kudhihakiwa kua ni Wajinga basi katika siku ya Malipo ndio watakaokua na Darja mbele ya Mola wao na kuingizwa Peponi.

Allah atujaalie nasi kua miongoni mwao watu hao..Aamiin. Kwani watu hao ndio watakaokua ndani ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo aya zinaendelea kusema kua:

﴿ وَنَادَىٰٓ أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِ أَصۡحَٰبَ ٱلۡجَنَّةِ أَنۡ أَفِيضُواْ عَلَيۡنَا مِنَ ٱلۡمَآءِ أَوۡ مِمَّا رَزَقَكُمُ ٱللَّهُ قَالُوٓاْ إِنَّ ٱللَّهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى ٱلۡكَٰفِرِينَ ﴾

Wanada as-habu alnari as-haba aljannati an afeedoo AAalayna mina alma-i aw mimma razaqakumu Allahu qaloo inna Allaha harramahuma AAala alkafireena *(Surat Al Aaraf 7:50)*

Tafsir: Na Watanadi Watu wa Motoni Kuwaambia Watu wa Peponi Hebu Tumwagieni Baadhi ya Maji Aliyokuruzukuni Allah (Watu wa Peponi kuwajihu watu hao wa Motoni kua) Hakika ya Allah Ameyaharamisha (Maji na kila kitu cha Peponi) Kwa Makafiri

Hivyo aya hizi zinatuonesha kua baina ya Watu wa Peponi, Watu wa Al Aaraf na Watu wa Motoni kua wataonana na kuzungumza na kuombana misaada lakini sasa hali haitokua kama ilivyo sasa hapa Duniani kwani siku hio kutakua na uadilifu wa hali ya Juu na ahadi zitatekelezwa. Hivyo Aya zinatuonesha kua Watu wa Peponi watazungumza na watu wa Al Aaraf na pia Watu wa Al Aaraf watazungumza na watu wa Motoni.

Na kisha Watu wa Motoni wataomba msaada kwa Watu wa Al Aaraf baada ya watu hao wa Al Aaraf kuingizwa Peponi kwa kuwaambia wawamwagie Maji waliyojaaliwa kua nayo Peponi ili yawapunguzie Ukali wa Adhabu waliyokua nayo ndani ya Moto.

Ila sasa *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kuwaelezea tena hawa watakaoomba Maji kutokana na Kiu na Joto la Motoni na kisha kukataliwa kupewa Maji hauo kutokana na kuharamishiwa Maji hayo kutokana na kua ni Makafiri walioukataa Ukweli wa Ujumbe wa Dini ya Kiislam waliofikishwa na *Allah Subhabah wa Ta'ala* kupitia kwa Mitume wake kwa kusema:

﴿ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ دِينَهُمۡ لَهۡوٗا وَلَعِبٗا وَغَرَّتۡهُمُ ٱلۡحَيَوٰةُ ٱلدُّنۡيَا فَٱلۡيَوۡمَ نَنسَىٰهُمۡ كَمَا نَسُواْ لِقَآءَ يَوۡمِهِمۡ هَٰذَا وَمَا كَانُواْ بِـَٔايَٰتِنَا يَجۡحَدُونَ﴾

Alladheena ittakhadhoo deenahum lahwan walaAAiban wagharrat-humu alhayatu alddunya faalyawma nansahum kama nasoo liqaa yawmihim hadha wama kanoo bi-ayatina yajhadoona*(Surat Al Aaraf 7:51)*

Tafsir: ***Hao Ndio wale ambao Walioichukulia Dini yao -Kua Ni Mchezo wa Upuuzi Na Wakadanganyika Na Maisha ya Kidunia Na Hivyo Leo Tutawasahau Kama Wao Walivyokua wamesahau Makutano ya Siku hii (ya leo ya Malipo) Na kama vile Walivyokua pia juu ya Dalili zetu ni wenye kuzikataa***

Yaani Watu hao walikua ni wenye kuendekeza Matamanio ya Kidunia na kuyakumbatia Mapambo ya Dunia huku wakiwa ni wenye Kusahau na kudharau kuhusiana na Akhera yao. Mbali ya kua walikua ni wenye kuoneshwa Vithibitisho.

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakua ni mwenye kuwadaharau na kutowajali na kutowaingiza ndani ya Rehma zake mbali ya kua ni wenye kujuta na kuomba watolewe kwenye Adhabu hio ya Moto ambao watakaa ndani yake Milele.

Allah atunusuru na Adhabu ya Moto..kwani hakuna hata mmoja anaeweza kuistahmilia ukali wake..Aamiin

Na hivyo watakaa ndani ya Moto huo kwa milele kwa sababu ya kutoamini na kupotoka kwao kama zilivyosema aya kua:

﴿ وَلَقَدْ جِئْنَاهُمْ بِكِتَابٍ فَصَّلْنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴾

Walaqad ji/nahum bikitabin fassalnahu AAala AAilmin hudan warahmatan liqawmin yu/minoona *(Surat Al Aaraf 7:52)*

Tafsir: ***Na Kwa Hakika Tumewaletea (Vithibitisho hivyo) Katika Kitabu Tulichofafanua Ambacho ni Chanzo cha Ilm, Uongofu Na Kilichojaa Rehma - Kwa Watu Wenye Kuamini***

Hapo awali tulisema kua Neno Sirat kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Njia iliyonyooka na yenye upana wa kupitika bila ya wasiwasi wowote. Na pia humaanisha Njia ambayo imenyooka sawasawa katika kila upande na kila sehemu.

Na tunapowaangalia wenye Lugha yao kuhusiana na pale wanapozungumzia kuhusiana na njia Ambayo inaweza kua na Sifa ya Sirat basi hubidi kua na vigezo vitano vifuatavyo:

1-Njia Iliyonyooka Sawia katika kila kitu.

2-Njia ambayo ni yenye Kuelekea katika sehemu Maalum iliyokusudiwa kufikiwa.

3-Njia ambayo si ya mzunguko bali ni ya Mkato.

4-Njia ambayo si ya uchochoro yaani ni Pana na inayopitika kwa wapita njia.

5-Njia ambayo ni yenye kufahamika na mpita njia husika kua ndio itakaoyomfikisha katika sehemu husika.

Naam..amesema Abu Said Al Khudri Radhi Allahu Anhu kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Wakati Waumini watakapopita juu ya Moto wa Jahannam (kwa kupitia kwenye Sirat) basi watasimamishwa kwenye Qantarah ya kuingia Peponi, ambapo hapo watasimamishwa na kisha watalipiziana kwa namna walivyokoseana baina yao hadi watakaposafika na kisha wataruhusiwa kuingia Peponi. Na nnaapa mimi kwa yule ambae Roho yangu imo ndani ya Mikono yake kua Waumini hao wataijua njia ya kuelekea kwenye Majumba yao Peponi kuliko vile wanavyozijua njia za kuelekea kwenye Majumba yao hapa Duniani***(Imam Bukhari)*

Kwani ingawa tumeanza kufafanua Maana ya Al Sirat lakini lengo ni kuifafanua hadith hii ambayo tunaona kua imetumia neno Al Qantara. Ambapo neno Al Qantara hua linamaanisha Daraja Dogo au Fupi.

Na kutokana na Hadith hii basi kuna Wanazuoni wanaosema kua Al Sirat na Al Qantara ni kitu kimoja kwani Al Qantara ni sehemu ambayo ipo kwenye Al Sirat.

Na kuna wanaosema kua Al Sirat na Al Qantara ni vitu viwili tofauti. Ambapo kwa wale wanaosema kua Al Qantara ni sehemu ya Al Sirat basi wanasema kua Al Qantara ni sehemu iliyopo mwishoni mwa Al Sirat ambayo Waumini watasimamishwa ili kumalizana waliyodhulumiana kabla ya Kuingizwa Peponi.

Na wale wanaosema kua Al Qantara na Al Sirat ni vitu tofauti basi wao wanasema kua kila mtu atapita kwenye Sirat, yaani Waumini, Wasioamini na Wanafiq pia lakini ni Waumini tu ndio watakaopita kwenye Al Qantara.

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameytoa mfano wa namna Watu wa Peponi watakavyo malizana katika eneo la Al Qantara kabla ya kuingizwa Peponi kupitia katika hadith iliyoelezewa na Imam Al Hakim ambayo inasema: **'Kuna watu wawili kuyoka katika Ummah huu ambao wataletwa mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, ambapo mmoja wao atashtaki kwa kusema:**

Ya Rabb huyu Fulani Ibn Fulani alinidhulumu mimi hivyo mimi nataka anilipe kutoka katika amali njema zake

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamwambia mtu huyo kua: Jee unaliona hili Kasri kubwa la Peponi?
Na hivyo Mtu huyo ataliangalia Kasri hilo la Peponi, na Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamwambia mtu huyo kua:

Hivyo Kasri hili litakua lako, lakini kama utamsamehe ndugu yako huyu

Na hivyo Mtu huyo atamsamehe ndugu yake huyo

Hivyo Enyi Waumini Muogopeni *Allah Subhabah wa Ta'ala* na Jirekebisheni na pataneni kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* atawapatanisha Waumini katika siku ya Malipo *(Mustadrak Al Hakim)*

Na anasema Abd Rahman Ibn Samura *Radhi Allahu Anhu* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoka nje na kutufuata sisi huku akiwa ni mwenye kutuambia kua:**

Kwa hakika Jana Usiku niliona Mambo ya Ajabu sana, kwani nilimuona Mtu miongoni mwa Watu wa Ummah Wangu akiwa amekamatwa na kuzuiliwa na Malaika Na Mara Ukatokea Udhu wake na kumuokoa Dhiidi ya Malaika hao.

Nikamuona Mtu Miongoni mwa Watu wa Ummah wangu akiwa amezungukwa na Mashaytani na mara zikatokea Dhikr Allah zake na zikamuokoa dhidi ya Mashaytani hao.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa Watu wa Ummah wangu akiwa amebanwa na Kiu kubwa saba, na mara ikatokea Funga yake ya Ramadhani na kumpa Kinywaji.

Na nimemuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu akiwa yuko katikati ya kiza kikubwa sana mbele yake, nyuma yake, kulia kwake, kushoto kwake, juu yake na chini yake na mara ikatokea Hija yake na kumuokoa na Kiza hicho.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu akiwa anataka kuchukuliwa Roho yaje na Malakat ul Mawt na mara wema wake kwa Wazee wake ukatokezea na kumzuia Malakat ul Mawt.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu ambae Waumini walikua hawazungumzi nae na mara ukatokea uunganishaji wake kwa jamaa zake na kuwaambia Waumini hao kua: Kwa hakika huyu ni mwenye kuunga Udugu hivyo Zungumzeni nae hivyo Mtu huyo akawa pamoja na watu hao.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu ambae alikua kila akisogea kwenye Mikusanyiko ya watu basi watu bao humfukuza.

Na Mara Likatokea Josho lake la kujitoharisha (na Janaba, Hedhi na Nifasi) na kumshika mkono kisha likamuweka pamoja na mikusanyiko ya watu hao

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu akiwa ameyazinga Macho yake kutokana na Ukali wa Moto wa Jahanam, na mara zikatokea Sadaka zake na Kumpatia Mtu huyo kivuli kutokana na Ukali wa Moto huo.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu ambae Malaika wa Adhabu wanataka kumkamata lakini mara Kuamrisha kwake mema na kukataza maovu kukatokea na kumuokoa dhidi ya Malaika hao.

Na nikamuona mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu akiwa anatumbukia ndani ya Moto wa Jahannam lakini mara Machozi yake aliyolia kwa ajili ya Mola wake yakatokea na kumuokoa na kutokana na Moto huo.

Na nikamuona mtu miongoni mwa Watu wa Ummah wangu ambae kitabu cha Amali zake kiliangukia kwenye mkono wake wa Kushoto lakini mara Khofu yake juu ya Mola wake ikatokea na kukidaka na kukiweka kitabu hicho kwenye mkono wake wa Kulia.

Na nikamuona mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu akiwa anayumbishwa na Upepo kama unavyoyumbishwa Mtende na mara zikatokea Dhana zake njema Juu ya Allah Subhanah wa Ta'ala na Kumtuliza kutokana Myumbisho huo.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu akiwa anatambaa juu ya Sirat juu ya Jahanam, huku mara akiwa anataka kudondoka na kuninginia lakini mara Sala zake katika kunisalia mimi zikatokea na kumpa mkono na kumsimamisha na kumvusha salama katika Sirat.

Na nikamuona Mtu miongoni mwa watu wa Ummah wangu amefungiwa Mlango wa Pepo ili asiingie ndani yake lakini mara ikatokea Shahada yake na kumfungulia mlango na kumuingiza Peponi*(Imam At Tabaran)*

Naam..hii ni Hadith inayoelezea kama alivyoona katika Ndoto *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam namna* hali itakavyokua katika Siku ya Malipo.

Kua kuna baadhi ya Watu wataoonekana kua na Makosa lakini wataokoka kutokana na makosa hayo kutokana na Amali njema zao ikiwemo Dhikhr Allah, Udhu, Sadaka, Hija, Machozi n.k na hivyo kuingia Peponi badala yake.

Ambapo miongoni mwa yaliyotajwa ndani yake hadith hio yatatokea katika Al Sirat au katika *Al Qantarah.*

Ambayo juu yake mwishoni kutakua na hio sehemu ambayo kila mmoja wetu ataulizwa Masuali na baada ya kutoa majibu yanayoridhisha basi ndio itapatikana ruhusa ya kuingia ndani ya Mlango wa Jannat Al Firdaus.

Kwani Masuali hayo yatakua ni yenye kuhusiana na Mambo 7 ambayo kila mmoja wetu anatakiwa ajitayarishe nayo kua na Majibu yake kabla hajaifikia siku hio.

Ambapo Suali la kwanza litakua ni kuhusiana na Imani, yaani kuhusiana na Nguzo za Imani za Kumuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Malaika wake,Vitabu vyake, Mitume wake, Siku ya Malipo na Qadar.
Suali la pili litakua kuhusiana na Ibada ya Sala na namna tulivyozisimamia ambapo kwa wenye kusali basi watamalizia Kuvuka Sirat kwa Nuru ya Sala zao.

Suali la tatu litakua ni kuhusiana na Zakkah na Sadaqah, ambapo kwa wenye kutoa basi watamalizia kuvuka Sirat kwa Upepo maridhawa.

Suali la Nne litakua kuhusiana na Funga ya Ramadhan ambapo kwa kila anaefunga basi Atajibiwa Suali hili na funga yake na kuombewa na Funga yake.

Suali la Tano litakua kuhusiana na Ibada ya Hija, ambapo kila aliekua na uwezo atatakiwa ajibu kuhusiana na Ibada hii na namna alivyoitekeleza.

Suali la Sita litakua kuhusiana na Udhu wa Sala na Josho la Janaba, Hedhi na Nifasi kwa ajili ya matayarisho Ufanyaji wa Ibada huku tukiwa katika haki ya Unadhifu.

Suali la Saba ni kuhusiana na Haki baina ya Viumbe, baina ya Wazee na Watoto, Baina ya Waislam kwa Waislam, Baina ya Mke na Mume, Baina ya Ndugu na Kaka, Baina ya Mtu na Jirani, baina ya Mtawala na watu wake n.k ambapo hapa sasa kwa kila aliemdhulumu mwenzake basi atakua anaandamana na kiwingu chenye kiza kikubwa sana nyuma yake.

Na baada ya kujibu Masuali hayo Saba kiusahih basi ndio Waumini wataruhusiwa kuingia ndani ya Jannat Al Firdaus.

Ambapo amesema Buraydah *Radhi Allahu Anhu* kua: **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Watu wa Peponi watakua ni wenye Kujipanga kwenye Safu 120. Ambapo Safu 80 miongoni mwao zitakua zinamilikiwa na Watu wa Ummah wangu, na 40 zilizobakia zitakua za Ummah nyenginezo** *(Sunan Al Tirmidhii)*

Allah atujaalie nasi kua miongoni mwa hao watakaokua katika hizo Safu 80 za ummah wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam..Amiin.*

Ila sasa inabidi tujue kua kuna umuhimu wa Kurudi mbele ya Mola wetu huku tukiwa Matajiri waliojaza Amali njema bila ya kua ni wenye kufilisika. Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:‘ **Baada ya Kuwauliza Masahaa zake kwa kusema: Hivi Jee mnajua ni nani Mtu aliefilisika miongoni mwenu?’**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakajibu, La!

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: ‘**Mtu aliefilisika Miongoni Mwenu sio yule ambae aliekua hana Pesa au hana Mali yeyote anayoimiliki. Bali aliefilisika Miongoni mwa Watu wa Ummah wangu atakua ni yule mtu ambae atakuja katika siku ya Malipo huku akiwa amesheni Amali njema ikiwemo za Sala, Funga, na za Sadaka**

Lakini hata hivyo atajikuta kua ni miongoni mwa waliofilisika katika siku hio ya Malipo kutokana na kua ni mwenye kuzitoa Amali hizo Kwa Sababu alikua ni mwenye kuwatukana Waislam wenzake, alikua ni mwenye kudhulumu Waislam wenzake, Alikua akiwafanyia Ufisadi Waislam wenzake, Alikua akimwaga Damu za Waislam wenzake na kuwapiga wenzake

Hivyo Amali zake zote hizo njema ikawa amezitoa kwa ajili ya kuwalipia fidia wale wenzake aliowadhulumu Hadi kufikia Amali zake kupungua na kutoweza Kulipia Fidia wenzake hao, na hivyo itambidi kubeba Dhambi za wenzake hao badala yake na kisha mtu huyo atakua ni mwenye kuingizwa ndani ya Moto wa Jahannam.(Sahih Muslim)

Subhabah Allah! Huu utakua ni mtihani mkubwa sana ambao matokeo yake itakua ni maadhirisho na majuto yatakayomkuta Muislam katika siku ya Malipo kwenye Al Qantara.

Allah atustiri na watu hao..Aamiin.

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Hibban basi yeye ana ile hadith isemayo kua: ‘**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Watu wengi hawatojua kua tayari wameshapita kwenye Sirat na hivyo watawauliza Malaika: ‘Hivi Jee likowa pia Daraja la Sirat? Na uko wapi Moto wa Jahannam’ ambapo nao wataambiwa kua: ‘Hakika nyinyi tayari mmeshalivuka Daraja la Sirat ambalo lilikua juu ya Jahannam na hamkuweza kuliona wala kuhisi Moto wake kwa sababu ya Nuru zenu’’***(Jamii Al Saghir)*

na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: **‘Kuna watu katika Ummah wangu wataigia Peponi moja kwa moja mara tu baada ya kufufuliwa kutoka Makaburini mwao.’**

Na hivyo Malaika watawauliza watu hao kwa kusema: ‘Hivi Jee nyinyi mmehesabiwa amali zenu?’

Nao watajibu: ‘**La sisi hata hatukuulizwa kuhusiana na amali zetu.**’

Malaika watasema kuwaambia watu hao: ‘Jee mlilivuka Sirat?’

Watu hao watasema: ‘**La sisi hata hatukuliona hilo Sirat.’**

Malaika watawauliza kwa kusema: ‘Na jee Mliuona Moto’

Watu hao watasema: ‘La hata hatujauona Moto huo pia’

Hivyo Malaika watawauliza watu hao: 'Hivi Jee mlikua mkifanya Jambo gani jema ambalo limekupelekeeni kuingia moja kwa moja Peponi bila y hata kuhesabiwa na kuvuka Sirat?'

Watu hao watasema: 'Hakika sisi tulikua na sifa mbili ambazo zimetupeleeka kuzipata rehma hizi. Ambapo kwanza tulikua tukimuonea haya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kiasi ya kua hatukua ni wenye kufanya dhambi pale tulipokua mbele ya watu wala tulipokua peke yetu, na pia tulikua tukiridhika na riziki ndogo tuliyojaaliwa na Mola wetu'

Malaika watawaambia watu hao: 'Naa..Rehma hizi ndio malipo yenu mnayostahiki.*(Imam Ibn Hibban)'*

Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anahoji kuhusiana na wasioamini kwa kusema kua:

﴿هَلْ يَنظُرُونَ إِلاَّ أَن تَأْتِيَهُمُ ٱلْمَلآئِكَةُ أَوْ يَأْتِىَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِىَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ يَوْمَ يَأْتِى بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لاَ يَنفَعُ نَفْساً إِيمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِن قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِيۤ إِيمَانِهَا خَيْراً قُلِ ٱنتَظِرُوۤاْ إِنَّا مُنتَظِرُونَ﴾

Hal yan*dh*uroona illa an ta/tiyahumu almala-ikatu aw ya/tiya rabbuka aw ya/tiya baAAdu ayati rabbika yawma ya/tee baAAdu ayati rabbika la yanfaAAu nafsan eemanuha lam takun amanat min qablu aw kasabat fee eemaniha khayran quli inta*dh*iroo inna munta*dh*iroona *(Surat Al Anaam 6:158)*

Tafsir: ***Hivi jee wanasubiri nini zaidi ya kua Malaika wawashukie au labda Mola wako aje, au labda Dalili za Mola wako ziwadie? Katika siku ambayo baadhi ya Dalili za Mola wako zitakapotokea basi hakutomfaa mtu kuamini kwake kama hakua ni mwenye kuamini hapo kabla, au hakuchuma mema katika wakati wa Imani yake. Sema: 'Subirini, kwani sisi (pia) ni miongoni mwa wenye kusubiri.'***

Naam..tunarudi kwenye kumalizia Dalili kuu za Kiama kabisa ambazo hatukuziangalia zote, na Dalili hizi haziko kwa mpangilio maalum kwani zimetajwa kwenye Hadith tofauti, nasi katika kufafanua kwetu basi tayari tumeshazungumzia kuhusiana na Yajuj wa Majuj, Dajjal na pia kuhusiana na *Nabii Isa Alayhi Salatu wa Salam.*

Hivyo na tuanze na kuchomoza kwa Jua kutoka katika Upande wa Magharibi ya Dunia ambapo Amesema Abu Dhar Al Ghifari *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Hivi Jee mnajua Jua hua linaenda wapi?**

Masahaba wakasema: Allah na Mtume wake ni wenye kujua zaidi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Kwa Hakika Jua hua linatembea taratibu hafi kufikia katika sehemu yake ya kupumzikia ambayo ni Chini ya Arshi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*

Na kisha husjudu na kubakia hapo hadi pale linapoambiwa Nyanyuka na kisha nenda katika sehemu uliyokuwepo hapo kabla. Hivyo Nalo hunyanyuka na kuelekea katika sehemu hio na kuchomoza tena na kuendelea kutembea Taratibu hadi kufikia kwenye sehemu yake ya

kupumzikia na kusjudu na kubakia katika hali hio hadi litakapoambiwa kua Nyanyuka, na litafanya tena hivyo. Na litaendelea kufanya hivyo bila ya watu kuhisi hadi pale litakapofikia katika sehemu yake ya kupumzikia chini ya Arshi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha likaambiwa Nyanyuka na nenda kachomozee katika sehemu uliyotulia, hivyo nalo litachomoza katika Upande lililotulia (yaani upande wa Magharibi)

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hivi Jee mnajua wakati gani itatokea hivyo? Itatokea katika wakati ambao Imani ya Mtu haitomnufaisha yule ambae hakuamini hapo kabla**(Sahih Muslim)

Na kulingana na mtizamo wa Wanazuoni kua maneno ya Hadith hii ndio maana ya maneno ya aya yasemayo

﴿ وَٱلشَّمْسُ تَجْرِى لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ ٱلْعَزِيزِ ٱلْعَلِيمِ﴾

Waalshshamsu tajree limustaqarrin laha dhalika taqdeeru alAAazeezi alAAaleemi *(Surat Yasin 36: 38):*

Tafsir: ***Na Jua linatembea katika mzunguko wake, na hayo ndio Makadirio ya Mwenye wingi wa Uwezo na mwenye kujuakila kitu.***

Ambapo kwa upande mwengine basi anasema Abd Allah Ibn Abi Awf *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mimi nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: Kwa Hakika Watu watakutwa na Usiku ambao ni sawa na Usiku mitatu, na utakapokuja basi wale wenye kufanya Ibada za Usiku wataugundua Mtu atasimama kufanya Ibada na kusoma kisomo chake na kisha ataenda kulala.'**

Kisha ataamka kwa mara ya pili na atafanya kisomo chake na kurudi kulala tena Na kisha ataamka tena kwa mara ya 3 na atafanya kisomo kisha atalala tena Ambapo wakati hali hio inaendelea basi watu wataanza kupiga kelele na kuitana na kuuliza, kua kimetokea nini?

Na kisha watakimbilia Miskitini kwa khofu na watapigwa na mshangao pale watakapoona kua Jua linachomoza kutoka katika upande wa Magharibi Na kisha likishafika katikati basi litageuka na kurudi tena upande wa Magharibi na kuzama Hapo ndipo Imani ya mtu haitomfaa kama ikiwa hakuamini hapo kabla yake.'

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Kiama kitawadia katika wakati ambao itakua watu wawili wamekunjua Kitamba lakini kamwe hawatoweza kuuziana wala kukikunja tena. Kiama kitatokea katika wakati ambao Mfugaji atakaa kitako na kumkama Ngamia wake jike maziwa na kisha kuondoka na maziwa yake lakini hatowahi kuyanywa maziwa hayo. Kiaka kitatokea waka Mfugaji atakua ametayarisha kuwapa Maji Wanyama wake na kuwatilia kwenye seheu ya kunuywea lakini hatoweza kuwapa Maji Wanyama wake hao. Kiaka kitatokea katika wakati amba Mtu atachukua tonge ya chakula na kuitia mdomoni lakini hatoweza kuichakua wala kuimea tonge hio'**

Kwani amesema Abu Huraira *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Kiama hakitowadia hadi pale Jua litakapochomoza kutoka katika upande wa Magharibi**

Na watu watakapoliona katika hali hio basi kula mmoja aliepo juu ya mgongo wa Ardhi atakua ni mwenye kua na Imani, lakini sasa wakati umewadia na hivyo hakutomsaidia kitu mtu mwenye kuamini kama hakua ni mwenye kuamini hapo kabla.(Imam Bukhari)

Kwani Malengo ya Misingi ya Imani ya Dini ya Kiislam hua ni kumfanya Mtu kuamini uhalisia wa Ukimwengu wa Al Ghayb na mambo yasiyojulikana yaliyosikika kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo kama mtu hakuamini hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapodhihirisha mambo hayo basi bila ya shaka Kuamini kwake mtu husika hakutomsaidia kitu. **Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapodhihirisha kutokea kwa tukio hilo la Jua kua ni lenye kuchomoza kutoka katika sehemu linalotulia yaani Upande wa Magharibi wa Dunia, basi kila Ibn Adam atachanganyikiwa na kujiuliza kitu gani kinatokea na kisha baada ya kutafakkari basi ndio watu watapata jawabu kua hio ni kutokana na uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ambae ndie Muumba.**

***Allah Subhanah wa Ta'ala* hunyoosha Mkono wake katika wakati wa Usiku ili Waliofanya Madhambi katika wakati wa Asubuhi wapate kutubu Na hunyoosha Mkono wake katika wakati wa Asubuhi ili Waliofanya Madhambi katika wakati wa Usiku wapate kutubu Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataendelea kufanya hivyo hadi pale Jua litakapochomoza kutoka katika upande wa Magharib**i(Sahih Muslim)

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ***Allah Subhanah wa Ta'ala* ameweka Mlango wa Toba katika Upande wa Magharibi Ambapo Upana wake ni sawa na masafa ya safari ya miaka 70 Na Mlango huo hautofungwa hadi pale Jua litakapochomoza kutoka katika Upande wa Magharibi**

Ambapo anasema *Mujaddid Ad Din Al* Hafidh Imam Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Hadithi zinazongumzia kuhusiana na Kufungwa kwa Mlango wa Toba baada ya kuchomoza Jua kutoka katika upande wa Magharibi zinaungana mkono na kupeana nguvu katika kuthibitisha kua baada ya Jua kuchomoza kutoka Magharibi basi Mlango huo utafungwa na hautofunguliwa** tena' *(Fat-h Al Barri)*

Hivyo miongoni mwa Dalili Kuu za Kiama ambapo ndani yake tumeona kua mmetajwa kua ni Kutokea Wanyama Wanaotisha. Ambapo amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَإِذَا وَقَعَ ٱلْقَوْلُ عَلَيْهِم أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَآبَّةً مِّنَ ٱلأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ ٱلنَّاسَ كَانُوا بِآيَاتِنَا لاَ يُوقِنُونَ﴾

Wa-i<u>dha</u> waqaAAa alqawlu AAalayhim akhrajn<u>a</u> lahum d<u>a</u>bbatan mina al-ar<u>dh</u>i tukallimuhum anna alnn<u>a</u>sa k<u>a</u>noo bi-<u>ay</u>atin<u>a</u> l<u>a</u> yooqinoona *(Surat An Naml 27:82)*

Tafsir: ***Na litakapowadia na kutekelezwa Neno Juu yao Basi Tutawatolea Wao Wanyama Watishao Kutoka Ardhini Wazungumze nao kwa Sababu Watu Wamekua Hawaamini Aya zetu.***

Kwani amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **Hakika mimi nimeihifadhi hadhith niliyoisikia kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Ambayo kamwe siwezi kuisahau, kwani nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua Alama Moja Kuu ya Kiama ambayo itakuja itakua ni Kuchomoza kwa Jua upande wa Magharibi Na kutokea kwa Wanyama wanaotisha kwa Watu, na sijui Lipi litatokea mwanzo baina ya Mawili haya isipokua yatafuatana moja baada ya jengine.***(Sahih Muslim)*

Na Anasema Al Hafidh Al Faqih Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Abd Allah Al Hakim Al Nishapuri kuhusiana na Hadith hii kua: '**Kuchomoza kwa Jua kutaanza kutokea mwanzo kabla ya kutokea kwa Wanyama watishao, yaani Wanyama hao Watatokea baada ya Kuchomoza kwa Jua hilo siku hio hio au baadae kidogo.'**

Ama kwa upande aa Mujaddid Ad Din Al Hafidh Imam Abh Fadhl Shihab Ad Din Al Asqalani basi yeye anasema baada ya kumnukuu Imam Al Hakim Al Nishapuri kua: '**Hikma iliyomo ndani ya Kutokea kwa Wanyama hao Wakali baada ya kuchomoza Jua kutoka katika Upande wa Magharibi Ni kutokana na kua Mlango wa Toba utakua umeshafungwa Baada ya kuchomoza Huko kwa Jua kutoka Magharibi. Na hivyo Wanyama hao watatokea kwa ajili ya Kuwatofuatisha Wale watu waliokua wakiamini kabla ya tukio la Kuchomoza kwa Jua na wale waliokua hawakuamini kabla ya tukio hilo la Jua**'*(Fath Al Barri)*

Na Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Maumbile ya Wanyama hao watakaotokea baada ya kuchomoza kwa Jua katika Upande wa Magharibi. Kwani wako wasemao kua Wanyama watakaokuja watakua wanafanana na yule alietajwa kwenye Hadith ya Dajjal ya Fatma Bint Qais *Radhi Allahu Anha* isemayo kua **'Mimi nilisikia sauti ya Muadhini, Muadhini wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Ikisema *Alsalaatu Jaamia* (Mkusanyiko wa Sala) na hivyo nikatoka na kuelekea Msikitini na nikasalia na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku nikiwa kwenye Safu ya Wanawake iliyokua karibu na Wanaume, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomaliza Kusali, akapanda kwenye Minbar na kukaa kitako na akawa ni mwenye kutabasamu huku akisema: 'Wacha Kila Mtu abakie katika sehemu yake aliyosalia' na kisha akauliza: 'Hivi Jee mnajua kwanini nimekuiteni?'**

Masahaba wakajibu: 'Allah na Mtume wake ndie mwenye kujua zaidi'

Ambapo nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Wa Allahi, mimi sijakuiteni nyinyi kwa kukukaripieni wala kukuonyeni, bali nimekuiteni kwa sababu ya Tamim Ad Dari ambae alikua ni Mkristo na amekuja kwa ajili ya kukubali kujiunga nasi n a kua Muislam na ameniambia kitu ambacho kinakubaliana na kile nilichukua nikuambieni kuhusiana na Dajjal'

'Ameniambia kua alikua safarini baharini Pamoja na watu 30 wa Lakhm na Judhaam, na walipigwa na Mawimbi kwa mda wa mwezi, na kisha wakajikuta wako kwenye kisiwa katika wakati wa Magharibi. Hivyo wakaingia kwenye Mashua ndogo ndogo na kufikia kisiwani hapo, na wakakutana na Mtu mkubwa sana ambae alikua amejaa nywele mwili mzima kiasi ya kua hawakuweza kutofautisha baina ya Uso wake na mgongo wake. Hivyo wakasema: 'Ole wako, hivi wewe ndio nani?''

Mtu huyo nae akajibu: 'Mimi ni Jassaasah' nao wakamuuliza: 'Jassaasa ndio nani?' nae akasema: 'Enyi watu nendeni kwenye hili Jumba la Makasisi kwani kuna mtu ambae ana hamu sana ya kuonana nanyi' ambapo Tamim anasema kua: 'Aliposema kuhusiana na mtu basi sisi tukaingiwa na khofu, kua huyu tunaezeungumza nae asije akawa ni Shaytan' hivyo

tukakimbilia katika Jumba hilo, na ndani yake tukakutana na Mtu mkubwa sana kimaumbile ambae sisi hatujawahi kuona ukubwa kama wake hapo kabla.

Mtu huyo alikua amefungwa minyororo iliyokazwa huku mikono yake ikiwa shingoni mwake na miguu yake imefungwa kuanzia magotini na visiginoni kwa minyororo ya chuma, Nao wakasema'Ole wako hivi wewe ni nani?'

Ambapo nae akasema: 'Karibuni tu mtajua kua mimi ni nani, ila kwanza semeni nyinyi ni nani?'

Nao wakasema'Sisi ni watu kutokea katika maeneo ya Uarabuni ambao tulikua safarini baharini, lakini Bahari ikachafuka na kupigwa na mawimbi na hivyo tukajikuta kwenye hii kisiwa chenu, tukachukua mashua zetu na kutua katika ufukwe wa kisiwa hikina tukakutana na Mdudu ambae hatukuweza kutofautisha baina ya Uso wake na Mgongo wake kwani alikua na Nywele nyingi sana, nasi tukamwambia: 'Ole wako wewe hivi wewe ni nani?' ambapo nae akasema kua yeye ni Jassaaas', tukamuuliza Jassaaas ndio nani? Na yeye akasema: 'Nendeni kwenye hili Jumba kuna mtu anahamu sana ya kujua kuhusiana nanyi. Hivyo sisi tukakimbilia kwako huku tukimkimbia yeye kwa sababu hatukujua Mdudu yule alikua ni Shaytan ama la.'

Yule Mtu aliefungwa akasema: 'Hebu niambieni kuhusiana na Mitende ya Baysaan'

Nao wakasema'Unataka kujua nini juu yake?'

Ambapo nae akasema: 'Nakuulizeni kama Hii Mitende bado inendelea kuzaa ama la?'

Nao wakasema'Naam Inazaa'

Nae akasema: 'Karibuni tu itakua haizai tena Tende.' Kisha akasema: 'Niambieni kuhusiana na lile Ziwa la Tabarriyah'

Nao wakauliza: 'Hivi jee unataka kujua nini juu yake?'

Nae akasema: 'Jee mna Maji Ndani yake?' Nao wakasema: 'Ndio mna mjai mengi sana'

Ambapo nae akasema: 'Karibuni tu litakauka' kisha akasema: 'Niambieni kuhusiana na Chemchem ya Zughar (ambayo ipo kusini mwa ardhi ya nchi ya Syria)' Nao wakasema: 'Unataka kujua nini juu yake?'

Ambapo nae akasema: 'Jee kuna Maji ndani yake na watu wanapande mashamba yao kutokana na maji yake?' Nao wakasema: 'Naam Kuna Maji ndani yake na watu wanayatumia maji hayo kwa ajili ya mashamba yao'

Ambapo nae akasema: 'Niambieni kuhusiana na Mtume wa Ummah usiojua kusoma, amefanya nini?' nao wakasema: 'Amehama kutoka katika Mji wa Makkah na amehamia katika Mji wa Madina'

Ambapo nae akauliza: 'Hivi Jee Waarabu washaanza kupigana nae?' Nao wakasema : 'Naam' nae akauliza: 'Jee amewashugulikiaje?'

Nao wakajibu: 'Amewashinda Waarabu katika maeneo yake na wameonesha Utiifu juu yake' nao akauliza: 'Hivi kweli limetokea hilo?' nao wakasema: 'Naam'

Ambapo nae akasema: ‘Kama wamekubaliana nae basi hilo ni jambo bora kwao. Na hivyo sasa hivi nitakuambie kuhusiana na mimi mwenyewe. Mimi ndie Dajja na karibuni nitapewa ruhusa ya kua huru, na nitatoka na kutembea katika kila sehemu ardhini na sitoucha hata mji mmoja isipokua nitakaa ndani yake siku 40. Isipokua katika Mji wa Makkah na Taybah (Madina) kwnai imeharamishwa kwangu mie. Na hivyo kila wakati nitakapojaribu kuingia ndani yake basi nitakabiliana na Malaika mwenye Upanga na kunizuia na kila njia ya kuingilia itakua ni yenye kua chini ya Ulinzi wa Malaika’

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaipiga Mimbar kwa fimbo yake na kisha akasema: ‘Hii ni Taybah, hii ni Taybah, hii ni Taybah (Madina)’ kisha akasema: ‘Hivi Jee sikukwambieni mimi kuhusiana na haya hapo kabla?’ Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: ‘Hakika mimi nimekipenda kisa cha Tamim kwa sababu kinakubaliana na yale niliyokua nikuambieni kuhusiana na Makkah na Madina kuhusiana nae, lakini yeye yuko kwenye Bahari ya Syria, au Bahari ya Yemen, lakini yuko Mashariki, yuko Mashariki, yuko Mashariki.’ Ambapo Imam Al Tirmidhi amesema katika Jamii Sahihi yake kuhusiana na Hadith hii kua ni Hadith Sahihi Gharib. Ambapo Imam Ibn Abd Al Barr amesema katika kitabu chake cha *Al Istidhkar* kua hii ni Hadith Sahih katika Sanad zake.

Na kuna wasemao kua Watakua wanafanana na Ndama wa Ngamia wa Watu wa Nabii Saleh ambapo huu ndio Mtizamo wa Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr Al Ansari Al Qurtubi

Na kuna wasemao kua ni Wanyama wenye maumbile ya tofauti yaani kama alivyosema Imam Abu Zubayr kua: ‘**Wanyama haowana vichwa kama vya Nyati, Macho ya Nguruwe, Masikio ya Tembo Pembe kama za Gazelle, Shingo kama ya Mbuni ‹Kifua kama cha Simba, Rangi ya Mabaka kama Chui, Mkia kama wa Kondoo, Miguu kama ya Ngamia na hatua yake moja hua ni Dhiraa 12** *(Tadhkirah)*

Na kuna wasemao kua Wanyama hao watakua kama Nyoka.

Na ndio maana akasema Imam Abu Amr Uthman Ibn Sad Al Mukri Ad Dani kua: ‘**Kuna Nukuu nyingi sana zinazowazungumzia Wanyama hao na Maumbile yao, Ukubwa wao n.k Ambapo Nukuu zote hizo nyingi ni zenye Kauli za kuanzia kwa Masahaba au Matabiina ambazo hujulikana pia kama Mawquf. Na kuna Nukuu zinazosemwa kua ni kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yaani Marfuu, lakini hata hivyo nyingi sana miongoni mwao si Hadith sahih Ambapo miongoni mwa Marfuu Hadith basi ni zenye kusema kua Kutatokea Viumbe Wanyama wengine ambao ni tofauti na hakuna Mnyama mwengine wala Ibn Adam atakaekua na uwezo wa Kuwaepuka Wanyama hao wanaotisha Na Watakua wanawapiga Mihuri watu katika Mapaji ya Nyuso zao kua huyu ni Muumini na huyu ni Kafir’** *(Sunan Al Waridha Fil Fitan)*

Ambapo Wanyama hao wenye kutisha watakua na Fimbo ya Nabii Musa yenye Muhuri wa Pete ya Nabii Sulayman na hivyo Huwapiga Muhuri Ibn Adam kwenye Mapaji yao ya uso kuonesha kua huyu ni Muumini na Uso wake mtu huyo utakua unang'ara. Na kwa asieamini basi akipigwa Muhuri huo basi Uso wake hua mweusi hapo hapo Na hivyo Watu wote watakua ni wenye kutofautishwa na Wanyama hao baina ya Waumini na Makafir*(Musnad Imam Ahmad)*

Na Wanyama hao watakua wanasema: ‘**Ibn Adam Hawakuamini juu ya kile walichoteremshiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala*’**

Ambapo kwa Upande wa Imam Said Ibn Jubayr basi yeye anasema kua: '**Maneno *Tukallimuhum* yaliyotumika katika aya hii:**

﴿وَإِذَا وَقَعَ ٱلْقَوْلُ عَلَيْهِم أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَآبَّةً مِّنَ ٱلأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ ٱلنَّاسَ كَانُوا بِآيَاتِنَا لاَ يُوقِنُونَ﴾

Wa-idha waqaAAa alqawlu AAalayhim akhrajna lahum dabbatan mina al-ardhi tukallimuhum anna alnnasa kanoo bi-ayatina la yooqinoona *(Surat An Naml 27:82)*

Tafsir: ***Na litakapowadia na kutekelezwa Neno Juu yao Basi Tutawatolea Wao Wanyama Watishao Kutoka Ardhini Wazungumze nao kwa Sababu Watu Wamekua Hawaamini Aya zetu.***

Nie yenye kumaanisha kua Wanyama hao Watawajeruhi Watu hao.'

Na kwa maana hio basi aya hii inatuthibitishia kua Wanyama hao au Wadudu hao watatokea kweli. Na Wataibuka kwa kutokea Chini ya Ardhi yaani hata kama uko ndani ya Nyumba yako Basi anakuibukia humo humo.

Subhanah Allah!

Hii itakua hali ya Tafrani kubwa sana kwa sababu ardhini itakua hakuna kwa kujifichia wala kwa kujikinga nao kwani wanatokea ndani yake. Na aya pia inatuthibitisha kua Wanyama hao Watakabiliana na Watu kwa kuwasuta kwa maneno na kwa kuwajeruhi.

Na hivyo Hii inamaanisha kua watakua ni wenye kuadhibu. Na Wanazuoni Wanasema kua Wanyama hao watatokea Mara 3 Kutokea Jangwani na Kujificha kisha Watatokea tena kutoka Vijijini na kisha watatokea katika Masjid Al Haram…Allah atunusuru na mitihani hii..Amiin

Tukiendela kuangalia kuhusiana na miongoni mwa Dalili Kuu za Siku ya Kiama basi ni Moto mkubwa sana kwani amesema Hudhaifah Ibn Usaid *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mwishoni mwa Dunia kutatokea Moto Mkubwa sana kutokea katika maeneo ya Ardhi ya Yemen na Utawapelekea watu kukusanyika katika maeneo ya Mkusanyiko wa Kiama'***(Sahih Muslim)***

Hivyo Kutokea kwa Moto mkubwa sana katika maeneo ya Yemen na hivyo kuwapelekea watu kuukimbia na matokeo yake Watu kujikuta kua wamekusanyika katika Sehemu wanayotakiwa kukusanyika kwa ajili ya Tukio la Kiama kama zinavyoelezea Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo amesema pia Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Katika Siku ya Kiama basi Watu watakusanywa na kua katika hali 3 zifuatazo:**

1-Sehemu ya kwanza na ya wale Watu ambao ni wenye kua na matumaini ya Kuingia Peponi na huku wakiwa na khofu na Adhabu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

2-Sehemu ya Pili ni ya wale watu ambao watakusanyaa huku wakiwa wamepandishwa Juu ya Vipando Wakiwa wawilli juu ya Ngami, au watatu watatu juu ya Ngamia na hadi kufikia watu 10 juu ya Ngamia

3-Sehemu ya Tatu itakua ni ile ya Watu waliobakia ambao wao watalazimishwa kukusanyika kutokana na Moto ambao utawakumba wakati wakiwa wamelala mchana na hivyo Moto huo utawaamsha na kuendelea kukumbana nao hadi utakapoingia Usiku na hadi Asubuhi yake*(Sahih Bukhari)*

Ambapo hii ni hadithi tambayo inamaanisha kua Moto huo utakua ni sehemu au Sababu au njia ya kuwakusanya pamoja watu kama vile ambavyo walivyokua wakifanya Wawindaji wa zamani ambao walikua wakiwasha Moto upande mmoja wa msitu kisha wao hukaa upande wa pili na hivyo Wanyama wanaowindwa hua Ni wenye kuukimbia Moto na kuwakimbilia maadui zao yaani wale watu wanaowawinda, au kama Wavuvi wanaotumia Nyavu ambao hutandanza nyavu kwanza na kisha huizunguka Nyavu hio na kuanza kuisukuma na kuivuta kuelekea ufukweni ili wawakaa te Samaki walioingia ndani ya Nayvu hio na hivyo samaki wote hua ni wenye kukimbilia ufukweni kutokana na kujaribu kuikimbia Nyavu hio isiwanase.

Kwa maana hio basi Ibn Adam katika wakati huo nao watakua na hio, ya Samaki kuikimbia nyavu kukimbilia Ufukweni na kukusanywa na kukamatwa au Wanyama ya kuukimbia Moto unaowaripukia nyuma yao na kukimbilia kusikokua na moto yaani mbele yao na hivyo Moto huo kuwaongozea Watu kule wanakotakiwa kukusanyikia. Kiasi ya kua Moto huo utawakimbilia na wao wataukimbia, kwa masiku hadi watakapowasili katika Ardhi ya Syria ambapo ndipo wanapotakiwa kukusanyiwa.

Na amesema Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema kua: Watu Watakusanywa katika siku ya Kiama katika Makundi Matatu, Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* o itakua kuna wale watakaokua na chakula na mavazi, na watakua Vipando. Kuna watakao kua wanatembea na wanaokimbia, na kuna watakao kua wanabururwa na Malaika kwa Nyuso zao.'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: '**Ama hawa watu wa aina mbili tunawajua ila ni wapi hao watakaokua wanatembea na kukimbia?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: **'Watu hao watakua na Vipando lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* atavijaalia vipando hivyo kupatwa na Maradhi na hivyo hawatoweza kuvipanda, kiasi ya kua kuna watu watakua na mabustani na watataka kuyabadilisha ili wapate kipando japo cha Ngamia Mzee na dhaifu lakini hawatompata hata Ngamia huyo.** *(Musnad Imam Ahmad)*

Ama kuhusiana na kumezwa kwa Watu katika sehemu tatu tofauti za Ardhi basi ukweli ni kua Hadith hazikuelezea Matukio hayo yatayokea katika maeneo gani ya Ardhi na itakua vipi kwani zimezungumzia kuhusiana na sehemu moja tu ambayo ni ya Mashariki ya Kati pale baadhi ya Hadith ambazo zinazungumzia juu ya matukio hayo katika Hali zifuatazo:

Anasema Imam Nafii Mawla Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: Kuna Mtu alikuja kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* na kisha akasema:

Ya Ibn Umar fulani na fulani wanakusalimia.

Ambapo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: Hakika mimi nimesikia Juu yake kua ameanzisha Uvumi katika Uislam, na hivyo kama kweli ameanzosha Uvumi katika Dini basi usimjibu Salam yangu, kwani mimi nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*

aksema kua: Kutakuja Watu Katika Ummah wangu ambao watageuzwa na kua Wanyama, Watamezwa na Ardhi na Watanyeshewa na Mvua ya Mawe.'*(Imam Ibn Majah)*

Na amesema Anas Ibn Malik R*adhi Allahu Anh*u kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ewe Anas! hakika Watu watajenga Miji Mikubwa na Mmoja wao utaitwa Al Busayrah, hivyo utakapopita katika Mji huo basi kua makini na Mwambao wake, Mashamba yake ya Chumvi, Masoko yake na Milango ya Viongozi wake.

Kwani unatakiwa upite nje ya Mipaka yake mji huo, kwani ndani yake mtatokea Maporomoko ya Ardhi, na Utaangukiwa na Mawe kutoka Mbinguni, na Watu wake watalala usiku na kuamka asubuhi yake huku wakiwa wamegeuzwa Nguruwe na Kima.' *(ImamAbu Daud)*

Na akasema tena Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Itatokea wakati Mtu atakua ni mwenye kutembea huku akiburuza chini nguo yake kwa Kujiona Na kisha atamezwa na Ardhi na ataendelea Kuzama Ardhini hadi katika Siku ya Malipo.'***(Imam Bukhari)*

Na akasema pia Abu Umammah *Radhi Allahu Anh*u kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

Baadhi ya Watu aa Umma wangu watakua ni wenye kukaa Usiku Wakila na Kunywa na Kustarehe, na itakapofika asubuhi basi watu hao watakua wamegeuzwakua Nguruwe na Watamezwa na Ardhi wao pamoja na Watu wao na Majumba yao Ambapo Asubuhi yake watu watasema kua Ukoo wa Fulani na Fulani Ulimezwa na Ardhi Jana Usiku na Nyumba ya Fulani na Fulani imemezwa na Ardhi Jana Usiku

Na Mawe yatawashukia Watu hao na Utatokea Upepo Mkubwa ambao utawapeperusha kama walivyopeperushwa waliotangulia kabla yao kwa sababu ya Ulevi wao, Kula Riba kwao, Kuvaa mavazi ya Hariri kwao, Kuweka Wanawake wanoimba kwao na Kuvunjiana Udugu kwao.*(Mustadrak Al Hakim)*

Na amesema Umm Salamah *Radhi Allahu Anha* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

Kutatokea Mvutano baada ya Kufariki Kiongozi wa Kiislam, na kisha Mtu moja kutoka katika Mji wa Madina atatoka na kukimbilia Madina

Na Baadhi ya Watu wa Makkah watatoka na kumtoa Mtu huyo kutoka kwenye Mji wa Makkah bila ya yeye kutaka, na kisha Watakubaliana nae baina ya Hajar Al Aswad na Maqaam Ibrahim Na kisha litatoka Jeshi kutoka katika Ardhi ya Sham kwa ajili ya kumkamata yeye ambalo litamezwa na Ardhi litakapofika katika maeneo ya Al Baydha Baina ya Mji wa Makkah na Madina

Na watu watakapoona hivyo basi wale Wacha Mungu wa Sham na Iraq watakuja na Kuungana nae Mkono*(Sahih Ibn Hibban)*

Na tunapoendelea kuangalia Dalili Kuu ya Siku ya Kiama basi tunaona kua moja wapo ni ile ambayo inajulikana kama ni Dalili ya Moshi, ambapo kwa upande wa Qur'an basi tunaona kua Surat Ad Dukhan Imezungumzia kuhusiana na Moshi ambao utakua ni Adhabu kwa wanaopinga Ujumbe wa

Kiislam na Dalili na hoja zilizoelezewa ndani ya Qur'an kuhusiana na kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitakatifu kua:

﴿ فَٱرْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِى ٱلسَّمَآءُ بِدُخَانٍ مُّبِينٍ ۞ يَغْشَى ٱلنَّاسَ هَٰذَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ۞ رَّبَّنَا ٱكْشِفْ عَنَّا ٱلْعَذَابَ إِنَّا مُؤْمِنُونَ ﴾

Fairtaqib yawma ta/tee alssamao bidukhanin mubeeni, Yaghsha alnnasa hatha AAathabun aleemun; Rabbana ikshif AAanna alAAathaba inna mu/minoona *(Surat Ad Dukhan 44: 10-12)*

Tafsir: ***Hivyo Subiri Siku Ambayo Zitatoa Mbingu Moshi Mkubwa Sana Uliowazi Utakaowafunika watu Hii Ni Adhabu Kali Sana (Watasema Watu hao) Ewe Mola wetu Tuepushe Sisi Na Adhabu hii Kwani kwa Hakika Sisi Tumeshaamini.***

Na hivyo mwisho wake basi watu hao watatashushiwa Moshi kutoka Mbinguni ambao utakua katika hali ya Adhabu kwani Harafu yake na uzito wake unachuna hadi Tundu za Pua, Koo na Mapafu pia, na ukikuingia Machoni hua kuliko inavyowasha Pilipili.

Kwani kwa upande mwengine basi anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Jarir At Tabari Al Shafii kuhusiana na aya hizi za Surat Ad Dukhan kua: '**Kuna baadhi ya Wanazuoni ni wenye kusema Moshi uliozungumziwa na Aya hii ni ule uliokua Moshi wa Njaa na Ugumu wa Maisha ukiowakumba Watu wa Quraysh pale Walipoombewa Dua Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya Kuukanusha Ujumbe wake juu yao.**

Ambapo nao wakanyanyua nyuso zao na hawakuweza kuona kitu chochote isipokua Kitu mithili ya Moshi, kutokana na hali ya Ugumu wa Maisha waliyokua nayo katika wakati huo.'

Ambapo huu pia ndio mtizamo wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu.*

Kwani anasema Imam Masruq Ibn Ajda kua**: 'Sisi tulikua tumekaa na Abd Allah Ibn Masud, pale alipokuja Mtu mmoja na kumwambia Ewe Abu Abd Rahman! Kuna Mtoaji Visa kwenye Mlango wa Kindah ambae anatoa visa vyake na kusema kua Itakapotokea Dalili Kuu ya Moshi, basi utachukua Roho za Makafiri na kuwaaacha Waumini wakiwa na hali ya kua kama wenye Kuona Baridi.'**

Ambapo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akanyanyuka kwa hasira na akasema**: 'Enyi Watu Muogopeni Allah, Hivyo kama Kuna mtu mwenye kuujua ukweli wa Kitu basi na auseme na asiejua basi na Asema Allah ni mwenye kujua zaidi Kwani Ni Kua na Ilm Kubwa sana pale Mtu anaposema kua Hajui na Allah Anajua zaidi.'**

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemwambia Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

﴿ قُلْ مَآ أَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُتَكَلِّفِينَ ﴾

Qul ma as-alukum AAalayhi min ajrin wama ana mina almutakallifeena *(Surat Sad 38:86)*

*Tafsir**: Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam kua) Sikuombeni Nyinyi Malipo Na Wala Mimi Si Mwenye Kuzusha Mambo yasiyokuwepo.***

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipowaona Watu Wanampa mgongo basi alisema: 'Ya Allah! miaka 7 Kama miaka 7 ya Yusuf.'

Na hivyo ikaja miaka 7 ya Njaa iliyowapelekea watu wa Quraysh kula kila wakipatacho hadi Ngozi za Wanyama na Nyamafu kwa sababu ya Njaa, kiasi ya kua ilikua Wakiangalia Juu basi hawaoni kitu isipokua kama Moshi. *(Mutawaffak Allayhi)*

Naam..hivyo mbali ya kua Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* amesema hivyo kuhusiana na Watu wa Quraysh kua walikua ni kama wenye kuona Moshi walipokua wakiangalia Juu kutokana na Njaa kama ilivyosemwa katika Hadith hio lakini pia katika Hadith nyengine basi amesema pia Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua:

Kuna Matukio ya Moshi wa Aina Mbili, ambapo Tukio moja kati yao Limeshatokea na Tukio la pili halijatokea, kwani Moshi huo utakua ni wenye kufunika eneo lote la baina ya Mbingu na Ardhi, lakini Makafiri wataingiwa na Moshi huo hadi kwenye Masikio yao na kwa Waumini hawatohisi chochote isipokua kama kukereketwa Kooni tu basi(*Al Tadhkirah)*

Hivyo ukweli ni kua Kutokea kwa Moshi litakua ni Tukio ambalo litatokea katika Kipindi cha Mwisho wa Dunia kutakakothibitishwa na Moshi huo. Kwani miongoni mwa wanakubaliaa na mtizamo huu ni pamoja *na Bab Al Ilm Amir Ul Muuminin* Ali Ibn Abi *Talib Radhi Allahu Anhu*, *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* n.k.

Na bila ya shaka Masahaba na Tabiina na Tabii Tabiina walikua ni wenye kua na khofu sana juu ya tukio hili la Kutokea kwa Moshi kama vile ambavyo sisi tunavyotakiwa kua na Khofu nao pia.

Kwani anasema Imam Abd Allah Ibm Abi Mulaykah kua: '**Asubuhi ya Siku moja Mimi nilienda kwa Abd Allah Ibn Abbas (*Radhi Allahu Anhu*) na akaniambia kua: 'Wa Allahi mimi sikulala Jana Usiku kucha hadi asubuhi hii ya Leo.'**

Ambapo Imam Ibn Mulaykah akamuuliza: '**Kwanini Hukulala?'**

Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Nimesikia Watu wakisema kua Sayari Moja Imetokea na kupita kwa kasi hivyo nami nikawa nna khofu ya Kuanza kutokea kwa tukio la Moshi,na hivyo sikuweza kulala hadi asubuhi kwa kufikiria Moshi huo na Kuwadia siku ya Kiama***(Imam Ibn Jarir At Tabari)*

Na Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameusia kwa kusema pia kua '**Harakisheni Kufanya Mema kabla hazijatokea Dalili Sita zifuatazo:**

Kuchomoza Kwa Jua kutokea Katika Upande Unalozama

Moshi

Dajjal

Wanyama wanaotisha

Kifo chake mmoja wenu Miongoni mwenu

Siku ya Malipo *(Imam At Tirmidhi)*

Naam..hivyo ingawa mimi nawe tunaona kua hatutozifikia Dalili za Jua, Moshi, Dajjal na Wanyama watishao, lakini bado hakuna miongoni mwetu atakaekiepuka Kifo na Siku ya Malipo.

Tafakkar!

Alhamd Lillahi Rabbi Al Alamiin

MARUDIO YA VITABU VILIVYOTUMIKA KATIKA KITABU HIKI:

AL BURHANI FII ULUM UL QUR'AN – *Shaykh Islami* Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi Al Shafii.
AR RUH AL MAÁNI FI TAFSIR AL QURAN AL ADHIM WA SABAA AL MATHANI - *Imam* Abu Al Thana Shihab Din Sayyid Mahmud Ibn Abd Allah Al Husayn Al Alusi Al Baghdadi Al Hanafi.
ARAIS FI MAJALIS FI QASAS AL ANBIYAH – Imam Abu Is-haq Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Al Thalabi Al Shafii.
BAYAN AL FARQ BAYN AL SADR WA AL QALB WA AL FUAD WA AL LUBB - Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ali Ibn Hasan Ibn Bashir Al Hakim Al Tirmidhi Al Shafii.
JAMI'I LI AHKAM AL QUR'AN - TAFSIR AL QURTUBI - Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr Al Ansari Al Qurtubi.
KASHF AL ASRAR WA UDDAT AL ABRAR – Imam Rashid Al Din Al Maybudi.
KITAB JAWAHIR AL QUR'AN - *Hujjat ul Islami Mujaddid ad Din* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii.
MISHKAT UL MASABIH – *Shaykh Waliuddin* Abu Abdullah Al Khatib Al Tibrizi Al Hanafi.
MUFRADAT FI GHARIB AL QURAN - *Allamah* Abu Qasim Ibn Husein Ibn Mufadal Ibn Muhammad Raghib Al Isfahani.
QISAS AL ANBIYAAH- *Allamah* Nasiruddin Burhan Ad Din Al Rabghuzi.
TAFSIR AL KABIR – MAFATIH AL GHAYB – *Sultan al Mutakallimin Mujaddid ud Din* Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Ibn Al Husayn Al Taymi Al Bakri Al Tabaristan Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii.
TAFSIR AL KASHSHAF AN TAHQIQ AL TANZIL - *Sultan Al Balagha Jarrah Allah* Imam Abu Al Qasim Mahmud Ibn Umar Ibn Ahmad Al Zamakhshari Al Hanafi Al Mutazila.
TAFSIR AL QURÁN AL ADHIM – Imam Abu Muhammad Sahl Ibn Abdallah Al Tustari Al Shafii.
TARIKH AL RUSUL W AL MULUK– Imam Abu Jafar Muhammad Ibn Jarir at Tabari Al Shafii.

MARUDIO YA MITANDAO ILIVYOTUMIKA KATIKA KITABU HIKI

www.dar-alifta.org
www.eshaykh.com
www.islamqa.org
www.muftiwp.gov.my
www.seekersguidance.com